

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

# TAFSIR IBN KATHIR

**Juzuu ya Nne**  
**Al-Anfâl mpaka Yunus**

Kimetafsiriwa na:  
**Kamati ya Wataalamu**

**IBN HAZM MEDIA CENTER**  
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم  
للإمام ابن كثير

# TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.

Chapa ya Kwanza 2021.

**Msimamizi Mkuu wa Mradi:**  
Yassir Salim Awadh Masoud

**Kimetafsiriwa na:**  
Kamati ya Wataalamu

**Kimehaririwa na:**  
Wanazuoni wa Kiislamu

**Usanifu Kurasa:**  
Ally Said Abdallah  
Ibn Hazm Media Center  
P.O. Box 22197,  
Dar es Salaam  
Tanzania.

**Kimechapwa:**  
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

**Haki Zote Zimehifadhiwa.**

## Yaliyomo:

|   |    |
|---|----|
| <b>Tafsiri ya <i>Suratul Anfaal</i></b> .....                             | 1  |
| Tafsiri ya Neno <i>Al-Anfaal</i> .....                                    | 2  |
| Sababu ya Kuteremshwa Aya 8:1.....  | 2  |
| Sababu Nyingine ya Kuteremshwa Aya 8.1.....                               | 3  |
| Sifa za Waumini wa Kweli.....   | 5  |
| Imani Huongezeka Isomwapo Qur'an.....                                     | 7  |
| Kubainisha Maana ya <i>Tawakkul</i> .....                                 | 7  |
| Kubainisha Matendo ya Waumini wa Kweli.....                               | 8  |
| Kubainisha Ukweli wa Imani.....   | 8  |
| Matunda ya Imani Iliyokamilika.....                                       | 9  |
| Kumfuata Mtume ﷺ ni Sababu ya Kupatikana Kheri.....                       | 10 |
| Waislamu Kuomba Msaada wa Allah تعالی ..... 15                            | 15 |
| Waislamu Kuzidiwa Nguvu na Usingizi.....                                  | 21 |
| Kunyeshwa kwa Mvua Usiku wa Badri.....                                    | 23 |
| Allah تعالی Kuwaamuru Malaika Wazitie Udhhibiti.....                      | 24 |
| Makatazo ya Kukimbia Vitani na Adhabu Yake.....                           | 27 |
| Allah تعالی Kuwaua Makafiri katika Badri na Kuwarushia Mchanga.....       | 30 |
| Kuwajibu Washirikina Wanaoomba Hukumu.....                                | 33 |
| Amri ya Kumtii Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ.....                           | 36 |
| Amri ya Kumuitikia na Kumtii Allah تعالی na Mtume ﷺ.....                  | 38 |
| Allah تعالی Huingia Kati Baina ya Mtu na Moyo Wake.....                   | 39 |
| Kutahadharishwa na <i>Fitnah</i> Yenye Kuenea.....                        | 41 |
| Kuwakumbusha Waislamu Juu ya Hali yao ya Udhalili na Unyonge.....         | 46 |
| Sababu za Kuteremshwa Aya Hii na Makatazo Dhidi ya Khiyana .....          | 48 |
| Maelezo Kuhusu Njama za Watu wa Makkah za Kutaka Kumuuu.....              | 52 |
| Madai ya Makuraishi kuwa Wanaweza Kuleta Mfano wa Qur'an.....             | 55 |
| Washirikina Wanaomba Hukumu na Wanataka Adhabu....                        | 56 |
| Kusalimika kwa Washirikina na Adhabu .....                                | 58 |
| Washirikina Wanastahiki Adhabu ya Allah تعالی Baada ya Ufedhuli Wao....   | 61 |
| Makafiri Kutoa Mali Zao kwa Ajili ya Kuzuia Dini ya Allah تعالی.....      | 65 |
| Kuwashajiisha Makafiri Wafanye Toba na Kuwaonya.....                      | 68 |
| Amri ya Kupigana kwa Ajili ya Kuumaliza Ushirikina na Ukafiri.....        | 69 |
| Hukumu ya <i>Ngawira</i> au <i>Ghanima</i> na <i>Fai</i> .....            | 74 |
| Baadhi ya Maelezo Juu ya Vita vya Badr.....                               | 80 |
| Allah تعالی Kulifanya Kila Kundi Kuwa Dogo Machoni mwa Kundi Jingine..... | 84 |
| Mafunzo ya Adabu za Kivita.....   | 87 |
| Amri ya Kuwa Imara Wakati wa Kukabiliana na Adui.....                     | 88 |

|   |     |
|---|-----|
| Hali Waliyotoka nayo Washirikina Kuelekea Badri.....                  | 90  |
| Shetani Hulipamba Ovu Lionekeane Jema na Kuwahadaa Kwake.....         | 91  |
| Msimamo wa Wanafiki Siku ya Badri.....                                | 93  |
| Kipigo cha Malaika kwa Makafiri Wakati wa Kuwatoa Roho Zao.....       | 95  |
| Amri ya Kuwapiga Vikali Makafiri na Wanaovunja Mikataba.....          | 100 |
| Amri ya Kuuvunja Mkataba ili Wawe Sawa.....                           | 101 |
| Amri ya Kufanya Maandalizi Kadri Iwezekanavyo .....                   | 103 |
| Amri ya Kufanya Suluhu kama Adui Ataomba Hivyo.....                   | 109 |
| Ukumbusho kwa Waumini juu ya Neema ya Kuziunganisha Nyoyo.....        | 110 |
| Uhamasishaji juu ya Kupigana na Adui.....                             | 112 |
| Ahadi kwa Mateka juu ya Kupata Mazuri Kuliko Walivyovipoteza.....     | 119 |
| <i>Muhajirina</i> na <i>Ansar</i> ni Marafiki Wao kwa Wao.....        | 123 |
| Si Wajibu Kumpa Ulinzi Aliyeamini bila Kufanya Hijra.....             | 125 |
| Makafiri ni Marafiki Wao kwa Wao.....                                 | 127 |
| Sifa za Waumini wa Kweli.....   | 128 |
| Haki ya Kurithi ni ya Ndugu wa Karibu.....                            | 129 |
| <b>Tafsiri ya <i>Suratu Tawbah</i></b> .....                          | 131 |
| Tangazo Kwamba Washirikina Wamevunja Mkataba.....                     | 132 |
| Mikataba ya Amani Iliyokuwepo Itaendelea Mpaka Muda Wake.....         | 136 |
| Hii Ndiyo Aya Inayoruhusu Kupigana kwa Upanga (Silaha).....           | 137 |
| Mshirikina Akiomba Amani Akubaliwe.....                               | 139 |
| Kusisitiza Kujiweka Kando ( <i>Baraa</i> ) Dhidi ya Washirikina.....  | 142 |
| Viongozi wa Kikafiri Hawaheshimu Viapo Vyao.....                      | 145 |
| Uhimizaji wa Kupigana na Makafiri na Ubainifu wa Baadhi ya Faida..... | 148 |
| Miongoni mwa Hikima za Jihadi ni Kuwajaribu Waislamu.....             | 150 |
| Washirikina Si Waimarishaji Misikiti ya Allah <b>تعالى</b> .....      | 152 |
| Waumini wa Kiislamu Ndio Waimarishaji wa Misikiti.....                | 152 |
| Kuwapa Maji Mahujaji na Kuimarisha Msikiti Mtukufu.....               | 156 |
| Amri ya Kukataza Kuwafanya Vipenzi na Marafiki Washirikina.....       | 159 |
| Matokeo ya Ushindi ni kwa Msaada wa Allah <b>تعالى</b> .....          | 162 |
| Tukio la Vita vya Hunayn.....   | 162 |
| Kuzuliwa kwa Washirikina Kuingia <i>Masjid Al-Haram</i> .....         | 168 |
| Amri ya Kuwapiga Vita Watu wa Kitabu .....                            | 170 |
| Ulipaji wa Jizya ni Alama ya Ukafiri na Udhalili .....                | 171 |
| Shirki na Ukafiri wa Mayahudi na Wakristo.....                        | 171 |
| Hila za Watu wa Kitabu za Kuizima Nuru ya Uislamu.....                | 177 |
| Dini ya Uislamu Itazishinda Dini Zingine Zote.....                    | 178 |
| Onyo Dhidi ya Wanazuoni Waovu na Wafuasi wa Ibada Potofu.....         | 180 |
| Adhabu kwa Wanaolimbikiza Dhahabu na Fedha.....                       | 181 |

|   |     |
|---|-----|
| Mwaka Una Miezi Kumi na Miwili.....   | 185 |
| Miezi Mitukufu.....   | 188 |
| Kupigana Katika Miezi Mitukufu.....   | 191 |
| Makemeo Dhidi ya Kutumia Rai katika Sheria.....                             | 193 |
| Lawama na Onyo kwa Wanaojitia Uzito kwenda kwenye Jihad.....                | 196 |
| Allah <b>تعالى</b> ni Mwenye Kumnusuru Nabii Wake <b>ﷺ</b> .....            | 199 |
| Ulazima wa Kwenda Katika Jihad kwa Hali Yoyote.....                         | 202 |
| Safari ya Wanafiki Kutojiunga Katika Jihadi na Kubainisha Vitimbi Vyao..... | 206 |
| Lawama kwa Mtume <b>ﷺ</b> kwa Kuwapa Idhini ya Kubaki.....                  | 207 |
| Kufichua Hali za Wanafiki.....  | 210 |
| Allah <b>تعالى</b> Anamhadharisha Mtume <b>ﷺ</b> juu ya Wanafiki.....       | 213 |
| Kubainisha Woga na Khofu ya Wanafiki.....                                   | 222 |
| Usengenyi wa Wanafiki na Tamaa Yao Kuhusu Ugawaji wa Sadaqah.....           | 223 |
| Ubainifu wa Ugawaji wa Zaka.....  | 226 |
| Mafukara.....   | 227 |
| Masikini.....   | 227 |
| Wafanyakazi wa <i>Baitu Zaka</i> .....                                      | 228 |
| Wenye Kuzoeshwa Nyoyo Zao ' <i>Al-Muallafatu Quluubuhum</i> '.....          | 228 |
| Wenye Kuandikiana na Mabwana Wao Kujikomboa " <i>Riqaab</i> "......         | 229 |
| Fadhila za Kuwapa Uhuru Watumwa.....  | 230 |
| ' <i>Al-Gharimun</i> ' Waliozidiwa na Madeni.....                           | 230 |
| Waliotoka katika Njia ya Allah <b>تعالى</b> .....                           | 231 |
| <i>Ibnus-Sabil</i> Msafiri .....  | 231 |
| Miongoni mwa Alama za Wanafiki ni Kumuudhi Mtume <b>ﷺ</b> .....             | 233 |
| Katika Alama za Wanafiki ni Kujaribu Kuwahadaa Watu kwa Viapo.....          | 234 |
| Katika Alama za Wanafiki ni Kuogopa Siri Zao Kudhihirika.....               | 236 |
| Katika Alama za Wanafiki ni Kutoa Nyudhuru kwa Batili Walizofanya.....      | 237 |
| Baadhi ya Sifa Nyingine za Wanafiki.....                                    | 239 |
| Nasaha kwa Wanafiki Wachukue Mazingatio Kutoka kwa Waliopita .....          | 243 |
| Sifa Njema za Waumini wa Kweli.....   | 245 |
| Habari Njema kwa Waumini ya Kupata Neema za Kudumu Milele.....              | 247 |
| Amri ya Kufanya Jihadi Dhidi ya Makafiri na Wanafiki.....                   | 251 |
| Sababu za Kushushwa kwa Aya 9:74.....                                       | 251 |
| Njama za Wanafiki Kutaka Kumuua Mtume <b>ﷺ</b> .....                        | 253 |
| Katika Alama za Wanafiki ni Kukusanya Mali.....                             | 257 |
| Katika Alama za Wanafiki ni Kuwabeua Wanaotoa.....                          | 258 |
| Makatazo Juu ya Kuwaombea Msamaha Wanafiki.....                             | 261 |
| Furaha ya Wanafiki kwa Kubaki Nyuma Wakati wa Vita vya Tabuk.....           | 263 |
| Wanafiki Hawaruhusiwi Kutoka na Waumini Katika Jihadi.....                  | 266 |

|  |            |
|--|------------|
| Makatazo Juu ya Kusalia Jeneza za Wanafiki.....  | 267        |
| Shutuma kwa Wanaokataa Kushiriki Jihadi.....   | 270        |
| Nyudhuru Halali za Kisheria Zinazoruhusu Kutokushiriki Jihadi.....                       | 274        |
| Ubainifu wa Vitimbi vya Wanafiki.....  | 278        |
| Mabedui Wamezidi katika Ukafiri na Unafiki.....  | 280        |
| Fadhila za Muhajiruna, Answar na Waliowafuata kwa Wema.....                              | 283        |
| Wanafiki Mabedui wa Madinah.....   | 285        |
| Waumini ambao Hawakujiunga na Jihadi kwa Sababu ya Uvivu.....                            | 287        |
| Amri ya Kukusanya Zaka na Kubainisha Faida Zake.....                                     | 289        |
| Onyo kwa Waasi.....  | 291        |
| Kucheleweshwa Uamuzi kwa Masahaba Watatu .....   | 293        |
| Msikiti Uliojengwa kwa Lengo la Kuwagawa Watu, .....                                     | 296        |
| Fadhila za Msikiti wa Qubaa na Hukumu ya Kusali Ndani Yake.....                          | 298        |
| Tofauti kati ya Misikiti Miwili hiyo, <i>Masjidut Taqwaa</i> na <i>Masjid Quba</i> ..... | 301        |
| Allah تعالی Amezidhamini Roho na Mali za Wanaopigana Jihadi .....                        | 302        |
| Makatazo Juu ya Kuwaombea Dua Washirikina.....   | 307        |
| Allah تعالی Hawaadhibu Wafanyao Maasi.....   | 310        |
| Vita vya Tabuk.....  | 312        |
| Kisa cha Masahaba Watatu Ambao Shauri Lao Lilisubiri Wahyi.....                          | 315        |
| Amri Juu ya Kusema Ukweli.....   | 322        |
| Malipo ya Kutoka Kwenda Kupigana Jihadi.....   | 324        |
| Amri ya Jihadi dhidi ya Makafiri.....  | 330        |
| Imani ya Waumini Huongezeka na Hupungua.....   | 334        |
| Kutahiniwa kwa Wanafiki.....   | 335        |
| Kuletwa Mtume ﷺ ni Neema Kubwa Kutoka kwa Allah تعالی.....                               | 338        |
| <b>Tafsiri ya <i>Suratu Yunus</i>.....</b>   | <b>343</b> |
| Mtume ﷺ ni Mwanadamu.....  | 344        |
| Allah تعالی Ndiye Muumbaji Ulimwengu,.....   | 346        |
| Kila Kitu Kitarejea kwa Allah تعالی.....   | 348        |
| Kila Kitu ni Shahidi wa Qudura ya Allah تعالی.....                                       | 350        |
| Makazi ya Wanaoikanusha Siku ya Kiyama ni Motoni.....                                    | 353        |
| Malipo Mema ni kwa Watu wa Imani na Amali Njema.....                                     | 354        |
| Allah تعالی Hazijibu Dua za Shari Kama Anavyozijibu za Kheri.....                        | 357        |
| Mwanadamu Humkumbuka Allah تعالی Wakati wa Shida.....                                    | 358        |
| Mazingatio Yanayopatikana Katika Hilaki za Umma Zilizotangulia.....                      | 360        |
| Ubainifu wa Ukaidi wa Wakuu wa Makuraishi.....   | 363        |
| Uthibitisho wa Ukweli wa Qur'an.....   | 363        |
| Wanachokiamini Washirikina Juu ya Miungu Yao.....  | 367        |
| Ushirikina ni Jambo Geni.....  | 368        |

|   |     |
|---|-----|
| Washirikina Wataka Muujiza.....   | 369 |
| Kubadilika kwa Mwanadamu Akishapata Rehema Baada ya Madhara.....        | 373 |
| Mfano wa Maisha ya Duniani.....   | 377 |
| Kuhamasishwa Kwenye Neema za Milele.....                                | 379 |
| Malipo ya Waja Wema.....  | 382 |
| Malipo ya Waovu.....  | 384 |
| Waungu wa Washirikina Watawakana Wafuasi Wao Siku ya Kiama.....         | 387 |
| Washirikina Wanaitambua Tawhidi ya Allah تعالی Kwamba Yeye ni Mola..... | 390 |
| Qur'an Kweli ni Maneno ya Allah تعالی na Kubainisha Muujiza Wake.....   | 397 |
| Amri ya Kujitenga Dhidi ya Washirikina.....                             | 403 |
| Hisia Juu ya Ufupi wa Maisha ya Kidunia Katika Siku ya Kufufuliwa.....  | 405 |
| Wahalifu Watalipizwa Kisasi, Ima Humu Duniani Ama Huko Akhera.....      | 407 |
| Juu ya Waikanushao Siku ya Kiyama Ambao Hutaka Iharakishwe.....         | 409 |
| Kiyama ni Kweli.....  | 413 |
| Qur'an ni Mawaidha, Ponyo, Rehema na Mwongozo.....                      | 414 |
| Allah تعالی Pekee Ndiye Mwenye Mamlaka ya Kuhalalisha Kitu .....        | 416 |
| Kitu Chochote, Kikubwa na Kidogo Kimo Katika Elimu ya Allah تعالی.....  | 418 |
| Kuwatambuwa Mawalii wa Allah تعالی.....                                 | 420 |
| Ndoto ya Kweli ni Utaratibu wa Uzuri wa Bishara (Habari).....           | 421 |
| Nguvu Zote, Uweza na Utukufu Wote ni wa Allah تعالی .....               | 425 |
| Allah تعالی Yu Mbali na Jambo la Kujifanyia Mke au Mtoto.....           | 426 |
| Kisa cha Nuh عليه السلام Pamoja na Kaumu Yake.....                      | 429 |
| Uislamu ni Dini ya Manabii Wote.....                                    | 431 |
| Lengo la Uovu na Mwisho wa Madhalimu (Khatma Yao).....                  | 434 |
| Kisa cha Nabii Musa عليه السلام na Firauni.....                         | 435 |
| Baina ya Nabii Musa عليه السلام na Wachawi.....                         | 439 |
| Vijana Wachache tu Katika Kaumu ya Firauni.....                         | 440 |
| Musa عليه السلام Aliwatumainisha Kaumu Yake Wamtegemee Allah تعالی..... | 442 |
| Waliamriwa Wasali Majumbani Mwao.....                                   | 444 |
| Dua ya Nabii Musa عليه السلام Dhidi ya Firauni na Wakuu Wake.....       | 445 |
| Wana wa Israel Waliokolewa na Watu wa Firauni Wakagharikishwa.....      | 449 |
| Kuwekwa kwa Wana wa Israel Katika Ardhi.....                            | 453 |
| Vitabu Vilivyotangulia Vinathibitisha Ujio wa Qur'an.....               | 456 |
| Imani Wakati wa Adhabu Haikufaa kwa Yeyote Isipokuwa.....               | 458 |
| Sio Katika Hekima ya Allah تعالی Kuwalazimisha Watu katika Imani.....   | 460 |
| Amri ya Kutafakari Juu ya Kuumbwa kwa Mbingu na Ardhi.....              | 463 |
| Amri ya Kumuabudu Allah تعالی Peke Yake na Kutawakali Kwake.....        | 466 |

## Tafsiri ya Suratul Anfaal

### Sura ya 8

#### Iliteremshwa Madinah

#### سُورَةُ الْأَنْفَالِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَنْفَالِ قُلِ الْأَنْفَالُ لِلَّهِ وَالرَّسُولِ ط فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَصْلِحُوا ذَاتَ بَيْنِكُمْ ط وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١﴾ إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّت قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢﴾ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا هُمْ دَرَجَاتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٤﴾ كَمَا أَخْرَجَكَ رَبُّكَ مِنْ بَيْتِكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ فَرِيقًا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ لَكَرِهُونَ ﴿٥﴾ يُجَادِلُونَكَ فِي الْحَقِّ بَعْدَ مَا تَبَيَّنَ كَأَنَّمَا يُسَاقُونَ إِلَى الْمَوْتِ وَهُمْ يَنْظُرُونَ ﴿٦﴾ وَإِذْ يَعِدُكُمُ اللَّهُ إِحْدَى الطَّائِفَتَيْنِ أَنَّهَا لَكُمْ وَتَوَدُّونَ أَنَّ غَيْرَ ذَاتِ الشَّوْكَةِ تَكُونُ لَكُمْ وَيُرِيدُ اللَّهُ أَن يُحِقَّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَيَقْطَعَ دَابِرَ الْكَافِرِينَ ﴿٧﴾ لِيُحِقَّ الْحَقَّ وَيُبْطِلَ الْبَاطِلَ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴿٨﴾

Ina Aya sabini na tano, maneno elfu moja mia sita thelathini na moja elfu. Ina herufi elfu tano mia mbili tisini na nne. *Allah Anajua zaidi.*

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu**

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَنْفَالِ قُلِ الْأَنْفَالُ لِلَّهِ وَالرَّسُولِ ط فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَصْلِحُوا ذَاتَ بَيْنِكُمْ ط وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١﴾

1. “Wanakuuliza juu ya ugawaji wa Ngawira. Sema: Ngawira ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume. Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni Waumini”.



### Tafsiri ya Neno *Al-Anfaal*

Bukhari alisema: Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: "*Al-Anfaal* ni ngawira." Pia ilisimuliwa kuwa; Sa'id bin Jubayr alisema, "Nilimuuliza Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuhusu "*Surat Al-Anfaal*". Akasema, "Iliteremshwa kuhusu (vita vya) Badr"<sup>1</sup>. Ama haya maoni ya Ibn 'Abbas رضي الله عنهما ndivyo pia yalivyosimuliwa na 'Ali bin Abu Twalhah, kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "*Al-Anfaal* ni ngawira. Na ilikuwa kwa ajili ya Mtume ﷺ tu, mtu mwingine hakuwa na chochote humo"<sup>2</sup>. Kadhalika, alisema hivyo Mujahid, 'Ikrimah, 'Atwaa, Adh-Dhahhak, Qatadah, 'Atwaa Al-Khuraasani, Muqatil bin Hayyan, 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam na wengine, kuwa maana yake ni ngawira<sup>3</sup>. Na ilisemwa: *An-Nafil* (umoja wa neno *Anfaal*), maana yake ni fungu la ngawira ambalo jemadari huwapa wapiganaji walioiteka au mfano wake, baada ya mgao wa ngawira wa awali. Pia ilisemwa: Ni khumusi moja (moja ya tano) iliyosalia baada ya kugawanywa khumusi nne. Pia ilisemwa: Ni *Al-Fay-a*, nayo ni mali inachukuliwa kwa makafiri bila mapigano, na inaweza kuwa mnyama au mtumwa au kijakazi au mali yoyote inayoponyoka kutoka kwao na kuingia kwa Waislamu. Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Ali bin Salih bin Hay alisema: "Ilinifikia khabari katika Kauli Yake Allah تعالى;

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَنْفَالِ

"***Wanakuuliza juu ya Ngawira***". Akasema: Ni vikosi vya Jeshi maalumu vilivyotumwa sehemu fulani "*Ni As-Saraaya*", na maana yake ni kile anachokigawanya jemadari kwa baadhi ya askari kama ziada juu ya mgao wao wa pamoja na wanajeshi waliosalia".

### Sababu ya Kuteremshwa Aya 8:1

Imamu Ahmad alinukuu kwamba Sa'id ibn Malik رضي الله عنه alisema: "Niliuliza, "Ewe Mtume! Allah تعالى Amenipa faraji leo dhidi ya Washirikina, kwa hiyo nipatie upanga". Mtume ﷺ akasema,

«إِنَّ هَذَا السَّيْفَ لَا لَكَ وَلَا لِي، ضَعُّهُ»

"*Upanga huu sio wako wala sio wangu, uweke*". Alisema: "Basi nikauweka, nikarejea na nikajisemea, "Huenda Mtume ﷺ akampa upanga huu mtu ambaye hakupigana (kwa bidii) kama mimi". Akasema tena, "Mara nikamuona mtu

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:156.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:378.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:361/362.

akiniita kutokea nyuma yangu. Nikasema, Allah تعالى Ameteremsha Aya kunihusu mimi?" Mtume ﷺ akasema,

«كُنْتُ سَأَلْتُكَ السَّيْفَ وَلَيْسَ هُوَ لِي، وَإِنَّهُ قَدْ وَهَبَ لِي، فَهُوَ لَكَ»

*"Uliniomba nikupe upanga, ambao haukuwa wangu. Hata hivyo, nimeshapewa (na Allah تعالى), basi sasa ni wako (ninakupa)".*

Allah تعالى Akateremsha Aya hii,

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَنْفَالِ قُلِ الْأَنْفَالُ لِلَّهِ وَالرَّسُولِ

***"Wanakuuliza juu ya ugawaji wa Ngawira. Sema: Ngawira ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume"***<sup>1</sup>.

Wameinukuu Abu Dawud, At-Tirmidhi na An-Nasai. At-Tirmidhi alisema, "Ni Hasan Sahih"<sup>2</sup>.

### **Sababu Nyingine ya Kuteremshwa Aya 8.1**

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Abu Umamah alisema: "Nilimuuliza 'Ubadah juu ya *Anfaal* akajibu: "Iliteremshwa kuhusu sisi tulioshiriki vita vya Badr. Iliteremshwa tulipokhitilafiana juu ya *An-Nafil* na tukakosa adabu. Allah تعالى Akaichukua *Anfaal* kutoka kwetu na Akamkabidhi Mtume ﷺ ili aigawe baina ya Waislam kwa usawa"<sup>3</sup>. Imamu Ahmad alinukuu pia kutoka kwa Umamah kutoka kwa 'Ubaadah bin As-samit رضي الله عنه, kuwa alisema: "Tulitoka na Mtume ﷺ na tulishiriki pamoja naye vita vya Badr. Majeshi ya pande mbili yakakabiliana. Allah تعالى Akamshinda adui. Kundi moja la Waumini likawakimbiza adui kwa mashambulizi na kuwaua. Kundi jingine la maaskari likawa linakusanya ngawira. Kundi jingine likamzingira Mtume ﷺ ili asije adui akamshambulia kwa ghafla. Usiku ulipoingia na watu wote wakarejea kambini kwao, wale waliokusanya ngawira walisema, "Sisi tumeikusanya, hapana yeyote mwingine atakayepata mgao". Waliomkimbiza adui wakasema, "Nyinyi hamna haki kutushinda. Sisi tumemzuia adui dhidi ya hiyo ngawira na tukamkimbiza". Wakasema wale waliomzingira Mtume ﷺ: "Nyinyi hamna haki zaidi yetu. Sisi tulimzingira kwa kumlinda Mtume ﷺ, tukihofia adui asije akamshambulia kwa ghafla. Kwa hivyo tumeshughulika naye".

<sup>1</sup> Ahmad 1:178.

<sup>2</sup> Abu Dawud 3:177, Tuhfat Al-Ahwadh 8:466, An-Nasai katika Al-Kubra 348.

<sup>3</sup> Ahmad 5:322.

Basi ikateremshwa,

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَنْفَالِ قُلِ الْأَنْفَالُ لِلَّهِ وَالرَّسُولِ فَأَتَقُوا اللَّهَ وَأَصْلِحُوا ذَاتَ بَيْنِكُمْ

**“Wanakuuliza juu ya ugawaji wa Ngawira. Sema: Ngawira ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume. Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu”.**

Basi, Mtume ﷺ akaigawanya sawa baina ya Waislamu<sup>1</sup>.

«وَكَانَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ إِذَا أَغَارَ فِي أَرْضِ الْعَدُوِّ نَقَلَ الرَّبِيعَ، فَإِذَا أَتَبَلَ وَكَلَّ النَّاسِ رَاجِعًا نَقَلَ الثُّلُثَ»

**“Na Mjumbe wa Allah alipokuwa akishambulia ardhi ya adui kwa ghafla, aliigawa robo tu ya ngawira zote. Na kama kulikuwepo na mapigano aliwagawia theluthi moja watu waliorejea (kutoka vitani)”.**

Mtume ﷺ alikuwa hapendi Ngawira na alikuwa akiwashajihisha wapiganaji shujaa wawape baadhi ya hisa zao wapiganaji dhaifu huku akisema: *“Ili iwarudishie nguvu Waumini juu ya udhaifu wao”*. Ameinukuu At-Tirmidhi na Ibn Majah kama hivyo. Na At-Tirmidhi akasema: *“Ni Hasan”*<sup>2</sup>.

Kauli ya Allah تعالى، فَأَتَقُوا اللَّهَ وَأَصْلِحُوا ذَاتَ بَيْنِكُمْ

**“Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu”.**

Maana yake: Mcheni Allah تعالى katika mambo yenu, na muyasuluhishe yaliyo baina yenu, wala msidhulumiane, wala msikhasimiane wala msigombane. Basi, uongofu na elimu aliyokupeni Allah تعالى ni bora kuliko hayo mnayokhasimiana kwayo.

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ

**“Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake”.**

Maana: Katika kukugawieni kwa namna Allah تعالى Alivyoagiza, kwani yeye kwa hakika huigawa kama Alivyoamriwa na Allah تعالى kwa uadilifu na insafu. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, *“Hii ni amri kutoka kwa Allah تعالى na Mtume ﷺ kwa Waumini, kwamba wamche Allah na wayasuluhishe yaliyo baina yao.”*<sup>3</sup>

<sup>1</sup> Ahmad 5:323.

<sup>2</sup> Tuhfat Al-Ahwadhi 8:468 na Ibn Majah 2:951.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:384.

Kadhaliika Mujahid alisema hivyo<sup>1</sup>. As-Suddi alisema:

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَصْلِحُوا ذَاتَ بَيْنِكُمْ

***“Basi Mcheni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu.”***

“Msitukanane”<sup>2</sup>.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٢٠﴾ الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٢١﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا هُمْ دَرَجَتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٢٢﴾

**2. “Hakika Waumini ni wale ambao Anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanaposomewa Ayah Zake huwazidishia Imani, na wakamtegemea Mola Wao Mlezi”.**

**3. “Hao ambao wanadumisha Sala na wanatoa katika yale Tunayowaruzuku”.**

**4. “Hao ndio Waumini wa kweli. Wao wana vyeo, na msamaha, na riziki bora, kutoka kwa Mola wao Mlezi”.**

### Sifa za Waumini wa Kweli

‘Ali bin Abi Twalha alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ

***“Hakika si venginevyo Waumini ni wale ambao Anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu”.***

Akasema, “Wanafiki hawaingiwi na chochote nyoyoni mwao kutokana na kutajwa Allah تعالى katika kutekeleza Aliyoamrisha, wala hawaamini chochote katika Ayah za Allah تعالى, wala hawatawakali kwa Allah تعالى, wala hawasali wanapoghibu (wanapokuwa peke yao), wala hawatoi Zaka za mali zao. Allah تعالى Alisema hao si Waumini. Kisha Allah تعالى Akaeleza sifa za Waumini,

<sup>1</sup> At-Tabari 13:384.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:384.

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ

**“Hakika si vinginevyo Waumini ni wale ambao Anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu”.**

Na kwa ajili hiyo wakatekeleza mambo waliyoamrisha,

وَإِذَا تَلَّيْتْ عَلَيْهِمْ ءَايَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا

**“...na wanaposomewa Aya Zake huwazidishia Imani”.** Kwa maana: Huwazidishia kusadiki kwao.

وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿٦٠﴾

**“...na wakamtegemea Mola Wao Mlezi”.** Anasema, hawamtegemei asiyekuwa Yeye<sup>1</sup>. Mujahid alisema,

وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ ﴿٦١﴾

**“...nyoyo zao hujaa khofu”** Kwa maana: “Hutishika na kuogopa”<sup>2</sup>. Basi akatekeleza maamrisha na akayaacha makatazo Yake. Sawa na Kauli ya Allah,

وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَجِيحَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ وَمَنْ يَغْفِرُ

الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ وَلَمْ يُصِرُّوا عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٦٢﴾

**“Na ambao pindi wafanyapo uchafu au wakijidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha kwa dhambi zao – ni nani anayefuta dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? – na wala hawaendelei na waliyoyafanya na hali wanajua”.** (3:135) Na Kauli Yake تعالى،

وَأَمَّا مَنْ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِ وَنَهَىٰ النَّفْسَ عَنِ الْهَوَىٰ ﴿٦٣﴾ فَإِنَّ الْجَنَّةَ هِيَ الْمَأْوَىٰ ﴿٦٤﴾

**“Na ama yule anayeogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akaizuia nafsi yake na matamanio. Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makazi yake!”.** (79:40-41)

Kwa ajili hii, Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisema, “Nilimsikia As-Suddi akiizungumzia Kauli ya Allah تعالى،

<sup>1</sup> At-Tabari 13:386.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:386

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ

**“Hakika Waumini ni wale ambao Anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu”.**

Kwamba ni mtu anayekusudia kudhulumu, au alisema: Ni yule anayezimia kufanya maasi, akiambiwa, “Mche Allah تعالى”, basi moyo wake unajaa khofu”.

### Imani Huongezeka Isomwapo Qur’an

Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿١٢٤﴾

**“...na wanapo somewa Ayah Zake huwazidishia Imani, na wakamtegemea Mola Wao Mlezi”.**

Sawa na Kauli Yake nyingine,

وَإِذَا مَا أَنْزَلْنَا سُورَةً فَمِنْهُمْ مَّنْ يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ هِدَايَةً إِيمَانًا ۚ فَأَمَّا الَّذِينَ

ءَامَنُوا فزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿١٢٥﴾

**“Na inapoteremshwa Surah wapo miongoni mwao wasema: Ni nani miongoni mwenu surah hii imemzidishia imani? Ama wale walio amini inawazidishia Imani, nao wanafurahi”.** (9:124)

Bukhari na Maimamu wengine wameitolea ushahidi Ayah hii (8:2) na nyingine zinazoshabihiana nayo, kwamba imani huongezeka na huzidiana katika nyoyo za watu kama yalivyo maoni ya wanazuoni wengi wa Kiislamu. Bali kwa ujumla, wamesema hivyo Maimamu wengi, kama vile Ash-Shafi رحمه الله تعالى, Ahmad bin Hanbal رحمه الله تعالى na Abu ‘Ubayd. Kama tulivyobainisha kwa kirefu katika maelezo ya mwanzo katika sherehe ya Bukhari. Shukran na Sifa zote ni za Allah تعالى.

### Kubainisha Maana ya *Tawakkul*.

Allah تعالى Anasema,

وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ ﴿١٢٦﴾

**“...na wakamtegemea Mola Wao Mlezi”.** Maana: Hawamtarajii asiyekuwa Yeye wala hawamkusudii mwingine, isipokuwa Yeye, wala hawakimbilii, isipokuwa katika Himaya Yake, wala hawahitaji kitu, isipokuwa kutoka Kwake,

wala hawatumaini isipokuwa Kwake. Wanajua kwamba Akitakacho huwa, na Asichokitaka hakiwi, na Yeye Ndiye Mwenye Uamuzi katika Milki Yake, ni Mpweke wala Hana mshirika, hapana wa kuipinga Hukumu Yake, na Yeye ni Mwepesi wa Kuhesabu. Kwa ajili hii, Sa'id bin Jubayr alisema, "Kumtegemea Allah تعالی ndio msingi wa Imani".

### Kubainisha Matendo ya Waumini wa Kweli.

Kauli ya Allah تعالی,

الَّذِينَ يُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنْفِقُونَ ﴿٢٠﴾

***"Hao ambao wanadumisha Sala na wanatoa katika yale Tunayowaruzuku".***

Allah تعالی Anaelezea matendo yao, baada ya kutaja itikadi yao, na, matendo yanayokusudiwa hapa ni yale yanayokusanya namna mbalimbali za kheri. Nazo ni kusimamisha Sala, na hiyo ni haki ya Allah تعالی. Qatadah alisema, "Kusimamisha Sala ni kuchunga nyakati zake, udhu, rukuu na sijda zake"<sup>1</sup>. Muqatil bin Hayyan alisema, "Kusimamisha Sala ni kuchunga nyakati zake, na kuufanya vyema udhu wake, kutimiza rukuu na sijda zake, kusoma Qur'an ndani yake na kutoa shahada na kumsalia Mtume ﷺ. Huku ndiko kusimamisha Sala"<sup>2</sup>. Na kuhusu kutoa sehemu ya Alivyowaruzuku Allah تعالی, kunakusanya wajibu wa kutoa Zakah na haki nyingine za wajibu zilizopendekezwa ambazo hutolewa kwa ajili ya waja. Viumbe wote ni wenye haja kwa Allah تعالی, basi mwenye kupendwa zaidi na Allah تعالی ni, wenye kuwanufaisha viumbe Wake.

### Kubainisha Ukweli wa Imani

Kauli ya Allah تعالی,

أُولَئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا

***"Hao ndio Waumini wa kweli".*** Kwa maana: Wenye kuwa na sifa hizi, ndio Waumini wenye Imani ya kweli.

<sup>1</sup> Ibn Hatim 1:37.

<sup>2</sup> Ibn Hatim1:37. Isnadi yake ni dhaifu.

**Matunda ya Imani Iliyokamilika.**

Kauli ya Allah تعالى، هُمْ دَرَجَاتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ

**“Wao wana vyeo, kwa Mola wao Mlezi”**, Kwa maana: Wana daraja na hadhi mbalimbali katika pepo sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى.

هُمْ دَرَجَاتٌ عِنْدَ اللَّهِ وَاللَّهُ بِصِيرٍ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿١٦٦﴾

**“Hao wana vyeo mbalimbali kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona yote wayatendayo”**. (3:163)

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَمَغْفِرَةٌ

**“..na msamaha.”** Maana: Atawasamehe madhambi yao na Kuwalipa kwa mema yao. Hadithi iliyonukuliwa katika sahihi mbili kwamba Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ أَهْلَ عَلَيْنَ لَيَرَاهُمْ مَنْ أَسْفَلَ مِنْهُمْ كَمَا تَرَوْنَ الْكُذَّابَ الْغَائِرَ فِي أَفْقٍ

“*Hakika Wakazi wa ‘Illiyin (Peponi) wataonwa na wale wa chini yao, kama muonavyo sayari ipitayo katika anga mojawapo miongoni mwa anga za mbinguni*”.

Wakauliza: “Ewe Mtume! Daraja hizo ni za Mitume ﷺ, wasiokuwa wao hawatazipata”. Akajibu:

«بَلَىٰ وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لِرِجَالٍ آمَنُوا بِاللَّهِ وَصَدَّقُوا الْمُرْسَلِينَ»

“*Ndiyo. Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Hayo ni kwa ajili ya waliomuamini Allah na kuwasadikisha Mitume*”<sup>1</sup>.

Katika Hadithi nyingine ambayo Imamu Ahmad na Maulamaa wa Sunan wameinukuu ni aliyosimulia ‘Atwiyyah kwamba Abu Sa’id رضي الله عنه alisema,

«إِنَّ أَهْلَ الْجَنَّةِ لَيَرَاءُونَ أَهْلَ الدَّرَجَاتِ الْعُلَىٰ كَمَا تَرَاءُونَ الْكُذَّابَ الْغَائِرَ فِي أَفْقِ

السَّمَاءِ وَإِنَّ أَبَا بَكْرٍ وَعُمَرُ مِنْهُمْ وَأَنْعَمًا»

“*Kwa hakika! Watu wa peponi watawaona wale wenzao wa daraja za juu, kama muonavyo sayari inayopita katika anga miongoni mwa*

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 6:368, Muslim 4:2177.



anga za mbingu, na kwamba Abubakr na 'Umar ni miongoni mwao (hao wa daraja za juu zaidi), na wameneemeka mno"<sup>1</sup>.

كَمَا أَخْرَجَكَ رَبُّكَ مِنْ بَيْتِكَ بِالْحَقِّ وَإِنَّ فَرِيقًا مِنَ الْمُؤْمِنِينَ لَكَرِهُونَ ﴿٥﴾ مُجْدِلُونَكَ  
 فِي الْحَقِّ بَعْدَ مَا تَبَيَّنَ كَأَنَّمَا يُسَاقُونَ إِلَى الْمَوْتِ وَهُمْ يَنْظُرُونَ ﴿٦﴾ وَإِذْ يَعِدُكُمُ اللَّهُ  
 إِحْدَى الطَّائِفَتَيْنِ أَنَّهَا لَكُمْ وَتَوَدُّونَ أَنَّ غَيْرَ ذَاتِ الشَّوْكَةِ تَكُونُ لَكُمْ وَيُرِيدُ اللَّهُ  
 أَنْ يُحِقَّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَيَقْطَعَ دَابِرَ الْكَافِرِينَ ﴿٧﴾ لِيُحِقَّ الْحَقَّ وَيُبْطِلَ الْبَاطِلَ وَلَوْ كَرِهَ  
 الْمُجْرِمُونَ ﴿٨﴾

5. ***"Kama Mola wako Mlezi alivyokutoa nyumbani kwako kwa Haki, na hakika kundi moja la Waumini linachukia kutoka kwako".***

6. ***"Wanajadiliana nawe kwa jambo la Haki baada ya kwisha bainika, kama kwamba wanasukumwa kwenye mauti nao wanaona".***

7. ***"Na kumbukeni pale Mwenyezi Mungu Alipokuahidini kuwa moja katika makundi mawili ni lenu. Nanyi mkipenda lisilo na nguvu ndio liwe lenu; na Mwenyezi Mungu Anapenda Ahakikishe Haki kwa Maneno Yake, na Aikate mizizi ya makafiri".***

8. ***"Ili Ahakikishe Haki na Auvunje upotovu na upotevu hata kama wakichukia wakosefu".***

**Kumfuata Mtume ﷺ ni Sababu ya Kupatikana Kheri kwa Waumini**

Kauli ya Allah تعالى،

كَمَا أَخْرَجَكَ رَبُّكَ

***"Kama Mola wako Mlezi Alivyokutoa"***: Baadhi yao walisema: "Imeshabihishwa na maslahi kwa waumini kule kumcha kwao Mola wao na kusuluhisha kwao yaliyo baina yao na twaa yao kwa Allah تعالى na Mtume ﷺ. Maana yake ni kwamba, Allah تعالى Amesema: Kama mlivyokhitilafiana juu ya ngawira na mkagombana, Allah تعالى Akakuondoleeni kutoka kwenu, na Akajaalia katika

<sup>1</sup> Ahmad 3:27, Abu Dawud 4:287, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:142 na Ibn Majah 1:37.

fungu lake na la Mtume ﷺ akalikasimu kwa uadilifu na usawa. Huku kukawa ndiko kutengemaa kuliko timilifu kwa ajili yenu. Kadhalika, mlipokataa kutoka kuwaendea maadui kwa ajili ya kupigana na jeshi lenye silaha, ambao walitoka kwa ajili ya kuitetea dini yao na kuulinda msafara wao. Hatima yenu ilikuwa ni kuchukia kupigana. Allah تعالى Akaviwezesha vita kwenu vitokee na Akakukusanyeni nyinyi na maadui wenu pasi na kupanga mapambano. Tukio hili ni funzo na uongofu, nusura na ushindi. Kama Alivyosema Allah تعالى pahala pengine,

كُيِّبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

***“Mmefaradhishiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu Anajua na nyinyi hamjui.” (2:216)***

As-Suddi alisema,

وَإِنَّ فَرِيقًا مِّنَ الْمُؤْمِنِينَ لَكَرِهُوا

***“..na hakika kundi moja la Waumini linachukia”.*** Wanachukia Matakwa ya washrikina.

يُجَادِلُونَكَ فِي الْحَقِّ بَعْدَ مَا تَبَيَّنَ

***“Wanajadiliana nawe kwa jambo la Haki baada ya kuisha bainika.”***

Baadhi yao walisema (katika maoni yao): “Wanakuuliza juu ya ngawira katika hali ya kujadiliana kama walivyojadiliana nawe siku ya Badr. Walisema: “Sisi umetutoa kwa minajili ya kuuvamia msafara, wala hukutujulisha juu ya kupigana ili tujiandae kwa ajili hiyo.”

وَيُرِيدُ اللَّهُ أَن يُحِقَّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ

***“...na Mwenyezi Mungu Anapenda Athibitisha Haki kwa Maneno Yake”.***

Kwa maana: “Allah تعالى Anataka Kukukutanisheni katika mapigano na kundi lenye silaha na mpigane ili Allah تعالى Akupeni ushindi na Kukunusuruni dhidi yao, na Aidhihirisha Dini Yake na Kuunyanyua Uislamu, ili uzishinde dini nyingine zote. Na Yeye Ndiye Mjuzi wa matokeo ya mambo yote. Yeye Ndiye

Anayekupangieni mpango mzuri, ijapokuwa, waja hupenda kinyume cha hivyo kwa jinsi ilivyowadhihirikia.” Kama Kauli nyingine ya Allah تعالى inavyosema,

كُنِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كَرْهٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَن تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ  
 أَن تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ

***“Mmefaradhishiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu.” (2:216)***

Muhammad bin Is-haq, Allah تعالى Amrehemu, alisema kuwa: Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: Mtume ﷺ aliposikia kuwa Abu Sufyan alikuwa akirudi Makkah na msafara wenye mali za Makureshi kutokea Shamu, aliwahimiza Waislamu kwenda kuwazuia, na akasema:

«هَذِهِ عِيرٌ قَرَيْشٍ فِيهَا أَمْوَالُهُمْ، فَأَخْرَجُوا إِلَيْهَا لَعَلَّ اللَّهَ أَن يَنْفَلَكَمُوهَا»

*“Huu ni msafara wa makuraishi ukiwa na mali zao, basi tokeni muuendee, huenda Allah Akaufanya kuwa ngawira kwenu.”*

Watu wakaanza kuhamasishana, baadhi yao wakawa wepesi na wengine wakawa wazito, hayo ni kwa sababu walidhani kuwa Mtume ﷺ atapigana vita. Abu Sufyan alikwishapata khabari pindi alipokaribia Al-Hijaz kwa njia ya upelelezi na kwa kuwauliza wasafiri kutokana na kukhofia mali za watu (msafara). Mpaka akapata khabari kutoka kwa baadhi ya wasafiri kuwa Muhammad ﷺ amekwisha wahamasisha Masahaba wake kwa ajili ya msafara wao. Akawa na tahadhari kwa hilo na akamuajiri Dhwaṁdhwaṁ bin ‘Amri Al-Ghifari. Akamtuma kwa watu wa Makkah na akamuamuru kuwaendea Makuraishi na kuwataka watoke ili kuzilinda mali zao, na awapashe khabari kuwa Muhammad ﷺ amekwisha wahamasisha Masahaba wake wauzuie msafara. Dhwaṁdhwaṁ bin ‘Amri akatoka upesi kwenda Makka. Wakati huo Mtume ﷺ akatoka na Masahaba wake, mpaka akafika katika bonde lililoitwa Dhafirani. Alipokuwa katika baadhi ya maeneo ya bonde hilo, alipiga kambi hapo na ikawafikia khabari ya kuja kwa Makuraishi kuulinda msafara wao. Mtume ﷺ akawataka Masahaba ushauri, na akawapa khabari za Makuraishi. Akasimama Sayyidina Abubakr رضي الله عنه na akasema maneno mazuri, kisha Sayyidina Umar رضي الله عنه naye akasimama akasema maneno mazuri, kisha akasimama Mikdadi bin Umar رضي الله عنه akasema : “Ewe Mtume! Nenda kama

Alivyokuamuru Allah تعالى. Wallahi! Sisi tuko pamoja nawe. Hatutakuambia kama Wana wa Israil walivyomuambia Musa عليه السلام,

فَأَذْهَبَ أَنْتَ وَرَبُّكَ فَقَتِلَا إِنَّا هُنَا قَاعِدُونَ ﴿٥٤﴾

**“...nenda wewe na Mola wako Mlezi mkapigane. Sisi tutakaa hapa hapa”. (5:24)**

Bali tunasema: ‘Nenda wewe na Mola wako, mkapigane, sisi tuko pamoja nanyi, tukiwa wapiganaji. Naapa kwa Ambaye Alikutuma kwa Ukweli! Ikiwa utatupeleka katika *Birkul-Ghamad* (mji uliopo Al-Habashah) tungelipigana pamoja nawe mpaka uuingie.” Mtume ﷺ akasema maneno mazuri juu ya Miqdad akamuomba kheri. Kisha, Mtume ﷺ akasema tena,

«أَشِيرُوا عَلَيَّ أَيُّهَا النَّاسُ»

*“Nipeni ushauri wenu, Enyi watu!”*

Alitaka kusikia kauli kutoka kwa Ansar. Kwa sababu wao ndio walikuwa wengi na pia ni kwamba, pindi walipompa ahadi ya kumtii na kumfuata huko Al-‘Aqabah, walisema, “Ewe Mtume ﷺ! Kwa hakika, sisi hatutafungika na baina yako mpaka utakapofika katika ardhi yetu. Utakapofika kwetu, basi utakuwa katika hifadhi yetu, tutakuhami kama tunavyofanya kwa watoto na wake zetu.” Mtume ﷺ alikuwa akihofia Ansar wangeweza kudhani kwamba walikuwa na jukumu la kumlinda dhidi ya maadui zake waliotaka kumshambulia pindi anapokuwa Madinah tu, na kwamba haikuwa katika ardhi yao. Baada ya Mtume ﷺ kusema hayo, Sa’d bin Mu’adh رضي الله عنه alimuambia, Mtume ﷺ: “Wallahi! Ni Kama kwamba unatukusudia sisi, ewe Mtume ﷺ?” Mtume ﷺ akasema, “Ndiyo, umesema kweli”. Sa’d رضي الله عنه akasema, “Tumeshakuamini, kukusadiki na tumeshuhudia kwamba uliyokuja nayo ni ya kweli na tumekupa ahadi na maagano mengi juu ya hilo na juu ya usikivu na utii. Basi, nenda ewe Mtume ﷺ! katika yale uliyoamrisha na Allah تعالى. Naapa kwa Ambaye Aliyekutuma kwa haki! Ukiamua kukatisha bahari (ya Shamu) hii, tutakufuata ndani yake na hakuna hata mmoja miongoni mwetu wa kubakia. Wala hatuchukii kwamba tutakutana na adui kesho. Kweli Allah تعالى Atakuonesha kutokana nasi jambo la kulituliza jicho lako. Basi twende pamoja nawe kwa baraka za Allah تعالى.” Mtume ﷺ alifurahishwa na kauli ya Sa’d رضي الله عنه na hilo likampa nguvu. Kisha akasema,

«سِيرُوا عَلَى بَرَكَاتِ اللَّهِ وَأَبْسِرُوا فَإِنَّ اللَّهَ قَدْ وَعَدَنِي إِحْدَى الطَّائِفَتَيْنِ وَاللَّهُ لَكَائِي الْآنَ  
أَنْظُرُ إِلَى مَصَارِعِ الْقَوْمِ»

*“Nendeni kwa Baraka za Allah, na furahini, kwani Allah Amenipa ahadi ya ushindi wa moja kati ya mawili (kuchukua ngawira za msafara au kulishinda jeshi la Makuraishi). Wallahi! Hivi sasa ni kama vile ninayaona maeneo ya mauti ya watu hao (Makuraishi)”<sup>1</sup>.*

Al-‘Awfi alisimulia mfano huu kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما<sup>2</sup>. Kadhalika, alisema hivyo, As-Suddi, Qatadah, ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam na wengine katika *Salaf*. Tumeelezea kauli zao kwa muhtasari unaotosheleza katika riwaya ya Muhamad bin Is-haq رحمه الله تعالى.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 13:399.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:403.

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُمْ بِالْفِ  
 مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُرَدِّينَ ﴿٩﴾ وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَى  
 وَلِتَطْمَئِنَّ بِهِ قُلُوبُكُمْ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ  
 اللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾ إِذْ يُغَشِّيكُمُ النُّعَاسَ أَمَنَةً مِنْهُ  
 وَيُنزِلُ عَلَيْكُمْ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً لِّيُطَهِّرَكُم بِهِ وَيُذْهِبَ  
 عَنْكُمْ رِجْزَ الشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَى قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ  
 الْأَقْدَامَ ﴿١١﴾ إِذْ يُوحِي رَبُّكَ إِلَى الْمَلَائِكَةِ أَنِّي مَعَكُمْ  
 فَثَبِّتُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا سَأَلْتَنِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا  
 الرَّعْبَ فَأَضْرِبُوا فَوْقَ الْأَعْنَاقِ وَأَضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ  
 ﴿١٢﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَمَنْ يُشَاقِقِ اللَّهَ  
 وَرَسُولَهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٣﴾ ذَلِكَ  
 فَذُوقُوا وَأَنَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابَ النَّارِ ﴿١٤﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ  
 ءَامَنُوا إِذَا لَقِيْتُهُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا زَحَفًا فَلَا تُولُوهُمْ الْأَدْبَارَ  
 ﴿١٥﴾ وَمَنْ يُؤَلِّمِهِمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ أَوْ  
 مُتَحَرِّفًا إِلَىٰ فِئَةٍ فَقَدْ بَاءَ بِغَضَبٍ مِنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ  
 جَهَنَّمُ وَيُسَّ أَنْصِرُ ﴿١٦﴾

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ  
 لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُمْ بِالْفِ  
 الْمَلَائِكَةِ مُرَدِّينَ ﴿٩﴾ وَمَا جَعَلَهُ  
 اللَّهُ إِلَّا بُشْرَى وَلِتَطْمَئِنَّ بِهِ قُلُوبُكُمْ  
 وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ  
 اللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾

9. "Kumbukeni mlipokuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, Naye Akaku jibuni kuwa: Kwa yakini Nitakusaidieni kwa Malaika elfu wanaofuatana mfululizo."

10. "Na Mwenyezi Mungu Hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu na ili nyoyo zenu zituwe. Na haipatikani ushindi ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, na Mwenye Hikima".

Waislam Kuomba Msaada wa Allah تعالى na Allah تعالى Kuwajibu Maombi Yao kwa Kuteremsha Malaika.

Bukhari alisema katika Kitabu cha Mambo ya Vita (katika Sahih yake) chini ya, "Mlango unaoelezea Kauli ya Allah تعالى:

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ

"Kumbukeni mlipokuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, Naye Akakujibuni". Mpaka kwenye Kauli Yake:

فَأَبَىٰ اللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٥﴾

**“Hakika Allah ni Mkali Anapotesa”.**

Kisha alinukuu kwamba Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema: “Nilishuhudia jambo alilofanya Al-Miqdad bin Al-Aswad رضي الله عنه nililipenda mno kuliko kitu chochote, kuwa ningekuwa nimelitenda mimi. Yeye alikuja kwa Mtume ﷺ wakati huo alikuwa akimuomba Allah تعالى dhidi ya Washirikina. Akisema, “Sisi hatusemi kama walivyosema kaumu ya Musa عليه السلام: ‘Nenda wewe na Mola wako mkapigane.’ Bali sisi tutapigana kutokea kumeni na kushotoni kwako, na kwa mbele na kwa nyuma yako”. Nikauona wajihi wa Mtume ﷺ ukiangaza na kufurahishwa na kauli yake.”<sup>1</sup> Kisha alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, kwamba katika siku ya Badr, Mtume ﷺ alisema:

«اللَّهُمَّ! أَنْشُدْكَ عَهْدَكَ وَوَعْدَكَ، اللَّهُمَّ! إِنْ شِئْتَ لَمْ نُعْبَدْ،

*“Ewe Allah! Nakuomba kwa Ahadi Yako na Agano Lako. Ewe Allah! Ukitaka (na Ukasababisha kushindwa kwetu) basi hautaabudiwa”.*

Abubakr رضي الله عنه akamshika mkono wake na kusema, “Inatosha”. Mtume ﷺ akatoka huku akisema:

سَيُزِمُ الْجَمْعُ وَيُؤَلُّونَ الدُّبُرُ ﴿١٦﴾

**“Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma.”**

An-Nasai naye pia alinukuu Hadithi hii<sup>2</sup>.

بِأَلْفٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُرَدِّفِينَ ﴿١٧﴾

**“...kwa Malaika elfu wanaofuatana mfululizo”.**

Maana yake: Wao kwa wao wanafuatana mfululizo. Kama alivyosema Harun bin Hubayrah kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, kuwa: “Murdifin” Ina maana, “wenye kufuatana”<sup>3</sup>. ‘Ali bin Abu Twalhah alisimulia kwamba Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Allah تعالى Alimsaidia Nabii Wake pamoja na Waumini kwa Malaika elfu moja. Mia tano kati yao ni chini ya uongozi wa Jibril عليه السلام,

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 7:335.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 7:335 na An-Nasai katika Al-Kubra 6:477.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:412.

kadhhalika Mikail عليه السلام aliongeza Malaika mia tano”<sup>1</sup>. Alisimulia Imam Abu Ja’far Ibn Jariri رحمه الله تعالى na Muslim kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa ‘Umar رضي الله عنه alisema:<sup>2</sup> “Wakati mtu mmoja katika Waislamu alipokuwa anaharakia kumuwahi mshirikina aliyekuwa mbele yake, alisikia sauti ya kipigo cha mkwaju juu yake pamoja na sauti ya mpanda farasi akisema, “Songa mbele, ewe Hayzum!” Tahamaki, alipomuangalia yule mshirikina wa mbele yake, alimkuta akiwa amebwagwa chali. Akamuangalia na kumuona akiwa pua yake imejeruhiwa na uso wake ukiwa umechanika, kama mtu aliyepata kipigo cha mjeledi. Na uso mzima umegeuka na kuwa wa rangi ya kijani”. Mtu huyo, wa Kiansari akaja na kumueleza hilo Mtume ﷺ naye akasema:

«صَدَقْتُ، ذَلِكَ مِنْ مَدَدِ السَّمَاءِ الثَّالِثَةِ»

*“Umesema kweli! Hiyo ilitokana na nguvu ya msaada kutokea mbingu ya tatu”.*

Siku hiyo, Waislamu waliwaua Washirikina sabini na kuwateka wengine sabini<sup>3</sup>. Bukhari alisema: Katika “Mlango wa kushiriki kwa Malaika katika vita vya Badr.’ Kisha akanukuu Hadithi ya Rifa’ah bin Rafi’ Az-Zuraqi رضي الله عنه, ambaye alikuwa miongoni mwa walioshiriki Badr. Alisema kuwa Jibril عليه السلام alikuja kwa Mtume ﷺ na akasema, “Mnadhani watu wa Badri wana nafasi gani kwenu?” Mtume ﷺ akasema,

«مِنْ أَفْضَلِ الْمُسْلِمِينَ»

*“Wao ni miongoni mwa Waislamu bora”.*

Au alitoa kauli kama hiyo. Kadhhalika Malaika walioshiriki Badri<sup>4</sup>. Bukhari peke yake aliinukuu, At-Tabarani alinukuu katika kitabu chake *Al-Mu’jam Al-Kabiir* lakini kutoka Hadith ya Rafi bin Khadij رضي الله عنه, hili ni kosa, na sahihi ni aliyoyanukuu Bukhari kuwa upokezi ni kutoka kwa Rifa’ah. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi. Katika Sahihi mbili, kuna Hadith kuwa Mtume ﷺ alimuambia ‘Umar رضي الله عنه, baada ya kumshauri juu ya kumuua Hatib bin Abi Balta’ah رضي الله عنه,

«إِنَّهُ قَدْ شَهِدَ بَدْرًا وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ اللَّهَ قَدِ اطَّلَعَ عَلَى أَهْلِ بَدْرٍ فَقَالَ: اَعْمَلُوا مَا  
يَشْتُمُ فَقَدْ عَفَرْتُ، لَكُمْ»

<sup>1</sup> At-Tabari 13:423.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:409 na Muslim 3:1383.

<sup>3</sup> Muslim 3:1384.

<sup>4</sup> Fat’hul Al-Bari 7:362.



*“Hakika yeye (Hatib) alishiriki Badr. Unajuaje? Huenda Allah Aliwatazama watu wa Badr na akasema, “Fanyeni mtakacho kwani Nimekusameheni”<sup>1</sup>.*

وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ

**“Na Mwenyezi Mungu Hakufanya haya ila kuwa ni bishara”.**

Kwa maana: Allah تعالى Hakujaalia upelekaji wa Malaika na Kukululisheni Kwake juu ya kushuka kwao, isipokuwa iwe ni bishara,

وَلِتَطْمَئِنَّ بِهِمْ قُلُوبُكُمْ

**“...na ili nyoyo zenu zitulie”.**

Hakika Allah تعالى ni Mwenye Uweza wa Kukunusuruni dhidi ya maadui zenu pasi na hao malaika na kwa ajili hii, Alisema:

وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ

**“Na haupatikani ushindi ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu”.**

Sawa na Alivyosema,

فَإِذَا لَقِيتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَخْنَتُمْهُمْ فَشُدُّوا الْوَتَانَ فِإِمَّا مَثًّا بَعْدُ  
وَإِمَّا فِدَاءً حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا ۗ ذَٰلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَانتَصَرَ مِنْهُمْ وَلَٰكِن لِّيَبْتَلُوا  
بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ ۗ وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَنْ يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٤٧﴾ سَمَّيْتَهُمْ وَيُضِلُّح  
بَاهُمْ ﴿٤٨﴾ وَيُدْخِلُهُمْ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ﴿٤٩﴾

**“Basi mnapowakuta waliokufuru katika vita wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe. Ndio hivyo. Na lau Angelitaka Mwenyezi Mungu Angeliwashinda Mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu Akutieni mitihani nyinyi kwa nyinyi. Na walio uliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu Hatazipoteza amali zao. Atawaongoza na Awatengenezee hali yao. Na Atawaingiza katika Pepo Aliyowajulisha”. (47:4-6) Aidha Amesema Allah تعالى;**

<sup>1</sup>Fat’hul Al Bari 7:355 na Muslim 4:1941.

وَتِلْكَ الْأَيَّامُ نَدَاوَلُهَا بَيْنَ النَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَيَتَّخِذَ مِنْكُمْ شُهَدَاءَ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿١٤﴾  
 وَلِيَمَّخَصَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَيَمَّحَقَ الْكٰفِرِينَ ﴿١٥﴾

***“Na siku za namna hii Tunawaleta watu kwa zamu, ili Mwenyezi Mungu Awapambanue walioamini na Awateue miongoni mwenu Mashahidi. Na Mwenyezi Mungu Hawapendi madhalimu. Na pia ili Mwenyezi Mungu Awasafishe walioamini na Awafutilie mbali makafiri”. (3:140-141)***

Hizi ni hikima za Allah تعالى Alizoziweka kwa ajili ya Jihadi dhidi ya makafiri kwenye mikono ya Waumini. Allah تعالى Alikuwa Akiziangamiza ummah zilizotangulia ambazo ziliwakadhibisha Manabii wao, kwa kutumia majanga mbalimbali ambayo yalizienea hizo ummah zilizokanusha. Kama Alivyowaangamiza kaumu ya Nuhu عليه السلام kwa gharika, Ad kwa upepo; Thamud kwa ukelele; kaumu ya Lut عليه السلام kwa zilizala, kupinduliwa ardhi na mawe ya udongo wa Motoni, na kaumu ya Shu’ayb عليه السلام kwa Siku ya Kivuli. Baada ya Allah تعالى Kumtuma Musa عليه السلام na Kumuangamiza adui wake, Firauni na kaumu yake, kwa kuzama baharini, kisha Alimteremshia Taurati na Aliweka Sharia ya kupigana dhidi ya makafiri na hukumu ikiendelea katika Sharia nyingine zilizobaki baada yake. Kama Kauli nyingine ya Allah تعالى Inavyosema:

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونَِ الْأُولَىٰ بِصَٰئِرٍ لِّلنَّاسِ

***“Na hakika bila ya shaka Tulimpa Musa Kitabu baada ya kwisha ziangamiza kaumu za mwanzo, ili kiwafumbue macho watu (muongozo).” (28:43)***

Waumini kuwaua makafiri kuna fedheha kubwa kwao za kuzifariji nyoyo za Waumini. Kama Allah تعالى Alivyosema juu ya Waumini wa Ummah huu,

قَتَلُوهُمْ يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَتُخْزِهِمْ وَيَنْصُرُهُمْ عَلَيْهِمْ ۗ وَإِذْ صُدُّوا قَوْمٍ

مُؤْمِنِينَ ﴿١٤﴾

***“Piganeni nao, Mwenyezi Mungu Awaadhibu kwa mikono yenu, na Awadhaliishe na Akunusuruni muwashinde, na Avipoze vifua vya kaumu ya Waumini.” (9:14)*** Kwa maana: Wafurahi.

Kwa minajili hii, jambo la kuwaua vigogo wakuu wa Kikuraishi kwa mikono ya maadui zao ambao waliwaangalia kwa macho ya dharau, lilikuwa la fedheha zaidi kwao na faraja katika vifua vya waumini. Abu Jahal, kwa mfano, aliuawa katika vita hii, na hili lilikuwa jambo la fedheha kubwa mno kuliko kufia kitandani kwake, au kutokana na radi, upepo au mfano wa hayo. Ni sawa na alivyofariki Abu Lahab, alaaniwe na Allah تعالى, kwa ugonjwa mbaya *Al-adsat* (uliomsababisha anuke vibaya) kwa namna ambayo nduguye yeyote hakumkaribia, na akaoshwa kwa maji ya kumwagiwa kwa mbali, wakautupia mawe mwili wake mpaka yakamfunika. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema,

إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ

**“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu”.** Kwa maana: Yeye Ndiye Mwenye Nguvu na Mtume Wake, kisha wanaowaamini hapa duniani na Akhera. Kama Kauli nyingine ya Allah تعالى Inavyosema:

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهُدُ ﴿٥١﴾

**“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi”.**

(40:51), Allah تعالى Anasema baadae:

حَكِيمٌ ﴿٥٢﴾

**“...na Mwenye Hekima”.** Kutokana na sharia Aliyoiweka ya kupigana na makafiri, pamoja na kuwa Yeye Ana uwezo wa Kuwaangamiza na Kuwahilikisha kwa Utashi na Nguvu Zake.

إِذْ يُغَشِّيكُمُ النُّعَاسَ أَمَنَةً مِّنْهُ وَيُنزِلُ عَلَيْكُمْ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً لِّيُطَهِّرَكُم بِهِ وَيُذْهِبَ عَنْكُمْ

رِجْسَ الشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَى قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ الْأَقْدَامَ ﴿٥٣﴾ إِذْ يُوحِي رَبُّكَ إِلَى الْمَلَأَةِ

أَنِّي مَعَكُمْ فَثَبَّتُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا سَأَلْتَنِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ فَأَضْرِبُوا فَوْقَ

الْأَعْنَاقِ وَأَضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ ﴿٥٤﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۗ وَمَنْ يُشَاقِقِ

اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۖ إِنِ يَأْتِ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٥﴾ ذَلِكَ فَذُوقُوهُ وَأَنَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابَ

النَّارِ ﴿٥٦﴾

11. *“Kumbukeni Alipokuleteeni usinginzi uwe ni uaminisho kutoka Kwake, na Akakuteremshieni maji kutoka mawinguni ili Kukusafisheni kwayo na Kukuondoleeni uchafu wa Shetani na Kuzipa nguvu nyoyo zenu, na Kuitia uimara miguu yenu”.*

12. *“Kumbuka pindi Mola wako Mlezi Alipowafunulia Malaika: Hakika ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu walioamini. Nitatia woga katika nyoyo za waliokufuru. Basi wapigeni juu ya shingo zao na wapigeni kila ncha za vidole”.*

13. *“Hayo ni kwa sababu wamemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake basi Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu”.*

14. *“Hii ni adhabu ya Mwenyezi Mungu! Basi ionjeni! Na bila ya shaka makafiri wana adhabu ya Moto”.*

### Waislamu Kuzidiwa Nguvu na Usingizi.

Allah تعالى Anawakumbusha Waislamu kwa neema Aliyowapa kwa Kuwapelekea Amani ya usingizi ukiwa ni usalama kwao kutokana na khofu iliyowapata, kwa sababu ya wingi wa idadi ya maadui, ilhali wao wakiwa wachache. Kadhalika hivyo ndivyo Allah تعالى Alivyowafanyia siku ya Uhud. Kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya nyingine,

ثُمَّ أَنْزَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ بَعْدِ الْغَمِّ أَمْنَةً نُبُوءًا يُغْشَىٰ طَائِفَةٌ مِّنْكُمْ وَطَائِفَةٌ قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنفُسُهُمْ

***“Kisha baada ya dhiki Alikuteremshieni utulivu – usingizi ambao ulifunika kundi moja kati yenu. Na kundi jengine nafsi zao ziliwashughulisha.”(3:154)***

Abu Twalhah رضي الله عنه alisema, “Nilikuwa miongoni mwa waliopatwa na usingizi katika siku ya Uhud, na upanga uliniponyoka mara nyingi toka Mkononi. Ulikuwa unaanguka, nami nauchukua, unaanguka tena, nami nauchukua tena. Masahaba nao niliwaona vichwa vikiwaanguka wakiwa katika lindo la nyuma”. Al-Hafidh Abu Ya'laa alisimulia kutoka kwa 'Ali رضي الله عنه kwamba alisema: “Hatukuwa na mpanda farasi mwingine zaidi ya Miqdad, na kuna kipindi niliona

kwamba hakuna aliyesalia katika sisi ila alikuwa amelala, isipokuwa Mtume ﷺ ambaye alikuwa akisali chini ya mti na akilia.”<sup>1</sup>. Naye ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema, “Kusinzia vitani ni usalama kutoka kwa Allah تعالى, lakini kusinzia ndani ya Sala kunasababishwa na Shetani”<sup>2</sup>. Qatadah alisema: “Kusinzia kunakuwa katika kichwa na kulala kunakuwa moyoni.”<sup>3</sup>

Mimi nasema usingizi uliwapata katika siku ya Uhud, na tukio hili ni mashuhuri sana. Ama Ayah hii tukufu (8:11) inazungumzia juu ya kisa cha Badr, na inaonesha kuhusu kutokea jambo hilo, kana kwamba hilo ni lenye kuwatokea Waumini kila wakati wa dhiki ili nyoyo zao ziwe na amani na utulivu juu ya kupata nusura ya Allah تعالى. Haya ni kutokana na Fadhila za Allah تعالى, Rehema Zake na Neema Zake juu yao. Na kama Allah تعالى Alivyosema:

فَإِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٥٦﴾ إِنَّ مَعَ الْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٥٧﴾

**“Basi kwa hakika pamoja na uzito upo wepesi. Hakika pamoja na uzito upo wepesi”. (94:5-6)**

Kwa ajili hii ilinukuliwa katika Sahihi mbili kwamba Mtume ﷺ ilipokuwa siku ya Badr alikuja katika kiriri cha kupumzikia akiwa pamoja na Abubakr Al-Siddiq رضي الله عنه wakiwa wanaomba dua. Usingizi ukampata Mtume ﷺ kisha akaamka akiwa anatabasamu, na akasema:

«أُبَشِّرُ يَا أَبَا بَكْرٍ هَذَا جِبْرِيلُ عَلَى نَتَائِبِهِ النَّعْمُ»

**“Ni khabari njema, Ewe Abubakr. Huyu hapa Jibril عليه السلام akiwa na vumbi mgongoni mwake”.**

Kisha akatoka katika mlango wa kiriri chake huku akisoma Kauli ya Allah تعالى,

سَيُزِمُّ الْجَمْعُ وَيُولُونَ الدُّبُرَ ﴿٥٤﴾

**“Wingi wao huu utashindwa, na wao watasukumwa nyuma”.**  
(54:45)<sup>3</sup>

<sup>1</sup> Musnad Abu Ya ‘ala 1:242.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:419.

<sup>3</sup> Ibn Abu Hatim 5:1664.

## Kunyeshwa kwa Mvua Usiku wa Badri.

Kauli ya Allah تعالى،

وَيُنزِلُ عَلَيْكُمْ مِّنَ السَّمَاءِ مَاءً

**“...na Akakuteremshieni maji kutoka mawinguni”.**

‘Ali bin Abi Twalhah alinukuu kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kwamba alisema: “Mtume ﷺ alipofika Badr alipiga kambi huku Washirikina wakiwa baina yao na maji (kisima) na eneo lenye mchanga. Waislamu wakajisikia udhaifu sana na shetani akawatia ghadhabu kwa kuwatia wasiwasi; na aliwanong’oneza: “Mnadai kwamba nyinyi ni mawalii wa Allah تعالى، na kwamba Mtume ﷺ yuko pamoja nanyi, lakini washirikina wameshayadhibiti maji, huku nyinyi mkiwa mnasali kwa ajili ya Allah تعالى mkiwa na janaba?” Allah تعالى Akawateremshia mvua nyingi, Waislamu walikunywa na kujitwahaisha, na Allah تعالى Akawaondolea uchafu wa Shetani, na Akaufanya udongo ukamatane na kuwa mgumu baada ya kunyeshewa na mvua. Waislamu wakatembea na wanyama wao juu yake kuwaendea makafiri. Allah تعالى Akamsaidia Mtume ﷺ na Waislamu kwa kuteremsha Malaika Efu Moja. Jibril عليه السلام aliongoza Malaika mia tano, kadhalika Mikail عليه السلام aliongoza Malaika mia tano<sup>1</sup>.

Masimulizi mazuri zaidi katika tukio hili ni yale aliyoyasimulia Muhammad ibn Is-haq bin Yasaar, mwandishi wa Habari za vita *Al-Maghazi*, Allah تعالى Amrehemu, kwamba: Yazid bin Ruman aliniezea kuwa alipokea kutoka kwa ‘Urwah bin Az-Zubayr رضي الله عنه، kuwa: “Allah تعالى Alipeleka mvua kutoka angani, na kulifanya bonde kuwa lenye kupitika vyema, basi Mtume ﷺ na Masahaba wake wakapata ardhi iliyo ngumu kwa ajili yao, upande wa makafiri hawakupata mahali pa kupita”<sup>2</sup>. Mujahid alisema, “Allah تعالى Aliteremsha mvua kabla ya usingizi ambayo iliyatuliza mavumbi na kuifanya ardhi kuwa ngumu, wakajisikia vyema na miguu yao kuwa thabiti”<sup>3</sup>. Kauli ya Allah تعالى،

لِيُطَهِّرَكُمْ بِهِ

**“... ili akusafisheni kwayo”.** Akusafisheni, kutokana na hadathi ndogo au kubwa, nayo ni twahara ya nje,

<sup>1</sup> At-Tabari 13:423.

<sup>2</sup> Al-Waqid katika Al-Maghazi 1:54.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:425.

وَيُذْهِبَ عَنْكُمُ رِجْزَ الشَّيْطَانِ

**“... Na Akuondoleeni uchafu wa Shetani”.**

Kwa maana: Kutokana na wasiwasi au fikra mbaya. Hiyo ni twahara ya ndani. Sawa na Kauli ya Allah تعالى kuhusu watu wa Peponi,

عَلَيْهِمْ ثِيَابٌ سُنْدُسٌ خُضْرٌ وَإِسْتَبْرَقٌ وَحُلُوعًا أُسَاوِرَ مِنْ فِضَّةٍ

**“Juu yao zipo nguo za Hariri laini za kijani kibichi, na Hariri nzito ya atilasi. Na watavikwa vikuku vya fedha...” (76:21)**

Hili ni pambo kwa nje,

وَسَقَنَّهُمْ رِئُومَ شَرَابًا طَهُورًا

**“...na Mola wao Mlezi Atawanyweshwa kinywaji safi kabisa”. (76:21)**

Kwa maana: Chenye kuwatwarisha dhidi ya hasira, husuda na chuki. Hilo ni pambo la batini na twahara yake,

وَلَيَرْبِطَ عَلَى قُلُوبِكُمْ

**“...na Azipe nguvu nyoyo zenu”.** Kwa maana: Kwa subira na kushajiisha kumpiga adui. Huu ni ujasiri wa ndani,

وَيُثَبِّتَ بِهِ الْأَقْدَامَ

**“... na kuitia uimara miguu yenu”.** Huo ni ushujaa wa nje.

**Allah تعالى Kuwaamuru Malaika Wazitie Uthabiti Nyoyo za Waislam na Wapigane ili Kuwasaidia Wao**

Kauli ya Allah تعالى,

إِذْ يُوحَىٰ رُبُّكَ إِلَى الْمَلَائِكَةِ أَنِّي مَعَكُمْ فَتَثْبُتُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا

**“Mola wako Mlezi Alipowafunulia Malaika: Hakika mimi ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu walioamini”.**

Hii ni neema iliyojificha ambayo Allah تعالى Aliwadhihirishia ili wamshukuru kwayo. Allah تعالى, ni Mkuu, Mtukuka, na Msifiwa kwa Sifa njema, Aliwashushia Wahyi Malaika Wake Aliowateremsha kwa ajili ya kumnusuru Nabii Wake, Dini na kundi lake, Waumini. Aliwapa Wahyi kwamba wawathibitisha wale walioamini. Kauli ya Allah تعالى,

سَأَلِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا أَلرُّعْبَ

**“Nitatia woga katika nyoyo za waliokufuru”.** Inamaanisha, enyi Malaika! Wasaidieni Waumini na muwape nguvu juu ya maadui wao kutokana na Amri Yangu kwenu. Nami Nitaupeleka uoga, udhalili na unyonge kwa waliokhalifu Amri Yangu na kumkadhibisha Mtume Wangu,

فَأَضْرِبُوا فَوْقَ الْأَعْنَاقِ وَأَضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ

**“Basi wapigeni juu ya shingo zao na wapigeni kila ncha za vidole”.**

Kwa maana: Wapigeni katika mapaji ya nyuso zao na kuyachana chana, muwakate maungo, mikono na miguu yao. Kauli Yake,

فَوْقَ الْأَعْنَاقِ

**“...juu ya shingo”.** Ilisemwa kwamba maana yake, wapigeni vichwani kuwachana au shingo, kwa mujibu wa Adh-Dhahhak na ‘Atwiyyah Al-‘Awfi. Maana hii inathibitishwa na Kauli ya Allah تعالى,

فَإِذَا لَقِيتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبِ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَخْنَتُمْهُمْ فَشُدُّوا الْوَتَاقَ

**“Basi mnapowakuta vitani waliokufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu”.** (47:4)

Ar-Rabi bin Anas alisema, “Katika siku ya Badr, watu walikuwa wakiwajua waliouawa na Malaika ambapo miongoni mwao walipigwa vichwani na vidoleni, kana kwamba walichomwa na moto na kuwaunguza. Kauli ya Allah تعالى,

وَأَضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ

**“...na wapigeni kila ncha za vidole”.**

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema, inamaanisha: “Enyi Waumini! Wapigeni maadui wenu katika kila kidole cha mkono na mguu.” Neno *Banan* ni wingi wa ‘*Bananah*<sup>1</sup>. Al-‘Awfi alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alivizungumzia vita vya Badr, mpaka akasema, Abu Jahl alisema, “Msiwaue (Waislamu), lakini muwateke, ili muwafahamisha walichokifanya katika kukebehi dini yenu na kumuacha Al-Lata na Al’Uzza.” Allah تعالى Akawateremshia Wahyi Malaika,

<sup>1</sup> At-Tabari 13:431.



أَيُّ مَعَكُمْ فَتَّبَتُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا سَأَلْتِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ فَأَضْرِبُوا فَوْقَ  
الْأَعْنَاقِ وَأَضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ ﴿٧﴾

***“Hakika Mimi ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu walioamini. Nami Nitatia woga katika nyoyo za waliokufuru. Basi wapigeni juu ya shingo na wapigeni kila ncha za vidole”.***

Akauawa Abu Jahl – Allah تعالى Amlaani – miongoni mwa watu sitini na tisa. ‘Uqbah bin Abu Mu’ait alitekwa na kuuawa. Hivyo idadi ya waliouawa ikafikia sabini. Kwa ajili hii Allah تعالى Alisema,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ

***“Hayo ni kwa sababu wamemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake”.***

Kwa maana: Walikhalifu na wakawaasi, wakaacha Sharia na kumuamini. Neno hilo limechukuliwa kutoka katika neno *Shaq* ambalo maana yake ni kuchana kitu na kukifanya sehemu mbili.

وَمَنْ يُشَاقِقِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنِ ٱلَّهِ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿٨﴾

***“Na Mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake basi Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu”.***

Kwa maana: Atawapata na Kuwashinda wenye Kumkhalifu, hakuna kitu kinachomfutu, wala hakuna kinachoweza kusimama dhidi ya Ghadhabu Zake. Hapana Mola wa haki kuabudiwa ghairi Yake, wala hakuna Mola Mlezi isipokuwa Yeye.

ذَٰلِكُمْ فَذُوقُوهُ وَأَنَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿٩﴾

***“Hiyo ni adhabu! Basi ionjeni! Na bila ya shaka makafiri wana adhabu ya Moto”.***

Maneno haya Wanaambiwa makafiri, yaani, ionjeni adhabu hii na hilaki duniani, na mtambue kwamba makafiri wana adhabu ya Moto huko Akhera.

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيتُمْ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا زَحَفًا فَلَا تُولُوهُمُ ٱلْأَدْبَارَ ﴿١٠﴾ وَمَنْ يُؤَلِّهِمْ  
يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ أَوْ مُتَحَيِّرًا إِلَىٰ فِقْعٍ فَعَدَّ بَاءً بِغَضَبٍ مِّنَ ٱللَّهِ وَمَأْوَاهُ  
جَهَنَّمُ وَبئسَ ٱلْمَصِيرُ ﴿١١﴾

**15. “Enyi Mlioamini! Mkikutana na waliokufuru vitani msiwageuzie mgongo (msikimbie)”.**

**16. “Na atakayewageuzia mgongo wake siku hiyo – isipokuwa kwa mbinu za vita au kuungana na kikosi – basi atakuwa amestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na pahala pake ni Jahannamu, na huo ni mwisho muovu”.**

### **Makatazo ya Kukimbia Vitani na Adhabu Yake.**

Allah تعالى Anasema, huku Akionya dhidi ya kukimbia vitani, Anawakhofisha kwa Moto hao wafanyao hivyo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيْتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا زَحَفًا

**“Enyi Mlioamini! Mkikutana na waliokufuru vitani”** Kwa maana: Mkiwakaribia na kuwasogelea karibu,

فَلَا تُؤَلُّوهُمْ الْآدْبَارَ

**“...msiwageuzie mgongo”.** Kwa maana: Mkakimbia na kuwaacha wenzenu.

وَمَنْ يُؤَلِّهِمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا لِّقِتَالٍ

**“Na atakayewageuzia mgongo wake siku hiyo – isipokuwa kwa mbinu za vita...”.**

Kwa maana: Mtu kumkimbia adui kama mbinu ili kumuonesha kwamba amemuogopa, hivyo anamfuata na yeye anatumia fursa hiyo kumuua. Hilo halina ubaya. Haya ni maelezo ya Sa’id bin Jubayr na As-Suddi<sup>1</sup>. Adh-Dhahhak alisema: “Ni mtu kuwatangulia Waislamu wenzake kwa ajili ya kuwachunguza maadui na kuwavamia.”

أَوْ مُتَحَرِّفًا إِلَىٰ فِتْنَةٍ

**“...au kuungana na kikosi ...”.** Kwa maana: Kukimbia hapa na kwenda katika kikosi kingine cha Waislamu kwa ajili ya kuwasaidia na wao wamsaidie, basi hilo linajuzu kwake, hata kama ni katika kikosi kisha akakimbia kwenda kwa kamanda<sup>2</sup> au kwa Imamu mkuu, yote yanaingia katika ruhusa hii.

<sup>1</sup> At-Tabari 13:436-437.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:436.

'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alizungumzia suala la Abu 'Ubayd alipokuwa akipigana darajani na kuuawa katika ardhi ya wafursi kutokana na kukithiri kwa Wanajeshi wa upande wa Majusi. 'Umar رضي الله عنه alisema: "Kama angelikimbilia kwangu, kingemuongezea kikosi kingine". Hivi ndivyo alivyosimulia Muhammad bin Sirin kutoka kwa 'Umar رضي الله عنه. Na katika masimulizi ya 'Uthman An-Nahdi, kutoka kwa 'Umar رضي الله عنه, alisema kwamba: Abu 'Ubayd alipopigana, 'Umar رضي الله عنه alisema: "Enyi watu! Mimi ni kikosi chenu". Mujahid alisema: "Umar رضي الله عنه alisema: "Mimi ni kikosi kwa ajili ya kila Muislamu." Abdul Malik bin 'Umar رضي الله عنه alisema kutoka kwa 'Umar رضي الله عنه: "Enyi watu! Aya hii isikufanyeni mhadaike, kwani ilikuwa ni kwa ajili ya Badr tu, nami ni kikosi kwa ajili ya kila Muislamu." Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisema, baba yangu alitusimulia kuwa, Hasan bin 'Abdullah Al-Misri alitueleza kuwa, Khalad bin Sulayman Al-Hadhrami alituambia kuwa Nafi' alitueleza kuwa yeye alimuuliza Ibn 'Umar رضي الله عنهما: "Sisi ni watu ambao hatuko madhubuti wakati wa kumpiga adui yetu, wala hatujui kikosi chetu ni kipi, ni Imamu wetu au askari wetu?" Akasema, "Kikosi ni Mtume ﷺ." Nikasema, Allah تعالى Alisema:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا زَحَفًا

**"Enyi Mlio amini! Mkikutana na walio kufuru vitani...".**

Akasema, 'kwa hakika, Aya hii iliteremshwa katika siku ya Badr si kabla wala baada yake.' Adh-Dhahhak alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى,

أَوْ مُتَحَيِّرًا إِلَىٰ فِقَةٍ

**"...au kuungana na kikosi."** "Al-Mutahayyiz" ni anayemkimbilia Mtume ﷺ na Masahaba wake رضي الله عنهم<sup>1</sup>. Ama kukimbia ambako si kwa sababu hizi, basi ni haramu, na ni mojawapo ya madhambi makubwa kwa mujibu wa aliyoyanukuu Bukhari na Muslim katika *Sahih* Mbili, kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema,

«اجْتَنِبُوا السَّبْعَ الْمُؤْبَقَاتِ»

**"Jiepusheni dhidi ya mambo saba yaangamizayo".**

Pakaulizwa, "Ewe Mtume! Ni yapi hayo?" Akasema:

<sup>1</sup> At-Tabari 13:437.

«الشُّرْكَ بِاللهِ وَالسُّحْرُ وَقَتْلُ النَّفْسِ الَّتِي حَرَّمَ اللهُ إِلَّا بِالْحَقِّ وَأَكْلُ الرِّبَا وَأَكْلُ مَالِ  
الْيَتِيمِ وَالتَّوَلَّى يَوْمَ الرُّحْبِ وَقَذْفُ الْمُحْصَنَاتِ الْغَائِلَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ»

*“Kumshirikisha Allah تعالى uchawi, kuua nafsi Aliyoiharamisha Allah تعالى, isipokuwa kwa haki, ulaji riba, ulaji mali za yatima, kukimbia katika uwanja wa mapambano na kuwazushia tuhuma za zinaa wanawake Waumini, watenda mema, ambao hawana hatia, na hawana fikra ya kufanya uovu.”<sup>2</sup>*

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

فَقَدْ بَاءَ

**“Basi atakuwa amestahiki.”** Kwa maana: Amerejea.

بِغَضَبٍ مِنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ

**“...ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na pahala pake”.**

Kwa maana: Makazi na mwisho wake katika Siku ya Marejeo yake.

جَهَنَّمَ وَيُنْسِطُ إِلَى النَّصِيرِ ﴿٨﴾

**“...ni Jahannamu, na huo ni mwisho muovu”.**

\* \* \*

<sup>2</sup>Fat’hul Al-Bari 5:462 na Muslim 1:92.

فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ<sup>٤</sup> وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ  
 وَلَٰكِنَّ اللَّهَ رَمَىٰ<sup>٥</sup> وَلِيُبْلِيَ الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَاءً حَسَنًا<sup>٦</sup>  
 إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٧﴾ ذَلِكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ مُوهِنُ  
 كَيْدِ الْكَافِرِينَ ﴿٨﴾ إِنْ تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ  
<sup>٩</sup> وَإِنْ تَنْتَهُوا فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ<sup>١٠</sup> وَإِنْ تَعُودُوا نَعُدْ وَلَنْ تُغْنِيَ  
 عَنْكُمْ فِتْنَتُكُمْ شَيْئًا وَلَوْ كَثُرَتْ وَأَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١١﴾  
 يَتَأَيُّمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا تَوَلَّوْا عُنُقَهُ  
 وَأَنْتُمْ تَسْمَعُونَ ﴿١٢﴾ وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ قَالُوا سَمِعْنَا  
 وَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ ﴿١٣﴾ \* إِنْ شَرَّ الدَّوَابِّ عِنْدَ اللَّهِ الضُّمُّ  
 الْبَكْمُ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٤﴾ وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا  
 لَأَسْمَعَهُمْ<sup>١٥</sup> وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوْا وَهُمْ مُعْرِضُونَ ﴿١٦﴾  
 يَتَأَيُّمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ  
 لِمَا نَحْيِيكُمْ<sup>١٧</sup> وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَنْحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ  
 وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ نُحْشِرُونَ ﴿١٨﴾ وَأَتَّقُوا فِتْنَةً لَا  
 تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً<sup>١٩</sup> وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ  
 شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢٠﴾

فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ<sup>٤</sup>  
 وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ  
 رَمَىٰ<sup>٥</sup> وَلِيُبْلِيَ الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَاءً  
 حَسَنًا<sup>٦</sup> إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٧﴾  
 ذَلِكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ مُوهِنُ كَيْدِ  
 الْكَافِرِينَ ﴿٨﴾

17. "Hamkuwaua nyinyi lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Aliye waua. Na wewe hukutupa mchanga, wala-kini Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyetupa, ili Awajaribu Waumini majaribio mema yatokayo Kwake. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Msikivu na Mjuzi".

18. "Ndio hivyo! Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kudhoofisha vitimbi vya makafiri".

Allah تعالى Kuwaua Makafiri katika Badri na Kuwarushia Mchanga.

Allah تعالى Anabainisha kuwa Yeye Ndiye Muumba wa matendo ya waja, na kwamba Yeye Ndiye wa Kusifiwa kwa kheri zote walizozifanya, kwa sababu Yeye Ndiye Aliyewawafikisha kufanya hayo na Akawaauni.

Kwa ajili hiyo Alisema,

فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ

**“Hamkuwaua nyinyi lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyewaua”.**

Kwa maana: Si kwa mbinu wala nguvu zenu kwamba mliwaua maadui zenu, huku wao wakiwa wengi, nanyi mkiwa wachache. Bali, Yeye Ndiye Aliyekupeni ushindi dhidi yao.

Kama Alivyosema:

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ

**“Na hakika Alikunusuruni Mwenyezi Mungu katika vita vya Badri nanyi mlikuwa wanyonge”. (3:123)**

Na Amesema تعالى:

لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ  
عَنكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُم مُّدْبِرِينَ ﴿١٢٣﴾

**“Hakika Mwenyezi Mungu Amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunayni ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu. Na ardhi ikawa dhiki kwenu pamoja na upana wake. Kisha mkageuka mkarudi nyuma”. (9:25)**

Allah تعالى Anajulisha hapa kuwa nusura haitokani na wingi, wa idadi au kwa kukusanya silaha na ngao, bali nusura hutoka Kwake.

Kama katika Kauli Yake nyingine,

كَمْ مِنْ فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةً بِإِذْنِ اللَّهِ وَاللَّهُ مَعَ الصَّٰدِقِينَ ﴿٢٤٩﴾

**“Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wenye kusubiri”. (2:249)**

Kisha Allah تعالى Alimuambia pia Nabii Wake juu ya fumba moja la mchanga ambalo alilitupa katika nyuso za makafiri siku ya Badr, alipotoka katika kiriri, baada ya dua yake, kunyenyekea kwa haja yake kwa Allah تعالى. alipowarushia mchanga huo na akasema:

«شَاهَتِ الرُّجُوه»

“Zimehiliki nyuso” Halafu, akawaamuru Masahaba wake waanze kupigana mapigano makali kwa kuunga mkono dua hiyo, na wakafanya hivyo. Allah تعالی Aliufikisha ule mchanga machoni mwa Washirikina. Hakusalia yeyote katika wao, bali alipatwa na kiasi cha mchanga kilichomfanya aishughulikie hali yake badala ya kupigana. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema,

وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَيْكَ بِاللهِ رَمِيٌّ

“**Na wewe hukutupa, lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Aliye tupa**”<sup>1</sup>. Maana: Yeye Ndiye Aliyeufikisha kwao huo mchanga na Kuwafanya washughulishwe nao na si wewe (ewe Muhammad!). Muhammad bin Is-haq alisema: “Alinieleza Muhammad bin Ja’far bin Az-Zubayr bin ‘Urwah bin Az-Zubayr katika Kauli ya Allah تعالی,

وَلَيْتِي الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَاءٌ حَسَنًا

“**.. ili Awajaribu Waumini majaribio mema yatokayo Kwake**”. Maana: “Ili Awajulishe Waumini neema Zake zilizo juu yao, kwa Kuwapa ushindi dhidi yao pamoja na kukithiri idadi ya adui na wao kuwa wachache. Ili kwa hilo, waijue haki ya Allah تعالی, na kwa hilo pia, wamshukuru Allah تعالی kwa neema Zake.”<sup>2</sup> Na hivyo pia ndivyo alivyoifasiri Ibn Jariri رحمه الله تعالی. Na katika Hadithi,

«وَكُلُّ بَلَاءٍ حَسَنٍ أَبْلَانَا»

“Kila jaribio jema Allah تعالی Alilotujaribu kwalo”.

Na Kauli Yake,

إِنَّ اللهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

“**Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Msikivu na Mjuzi**”.

Maana: Ndiye Msikivu wa dua zinazoombwa dhidi yao, na Mjuzi juu ya Anayestahiki nusura na ushindi. Kauli ya Allah تعالی:

ذَلِكُمْ وَأَنَّ اللهَ مُوهِنٌ كَيْدِ الْكَافِرِينَ

“**Ndio hivyo! Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kudhoofisha vitimbi vya makafiri**”.

<sup>1</sup> At-Tabari 13:444.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:448.

Hii ni bishara nyingine, pamoja na nusura waliyoipata. Allah تعالی Aliwajulisha kwamba Ataviondosha vitimbi vya makafiri siku za usoni, kuwa Atawashushia hadhi wao, na kila kilicho chao kitaangamia na kuharibika. Sifa njema na shukrani ni kwa Allah تعالی.

إِن تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ وَإِن تَنْتَهُوا فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَإِن تَعُودُوا نَعُدْ وَلَنْ تُغْنِيَ  
عَنْكُمْ فِتْنَتَكُمْ شَيْئًا وَلَوْ كَثُرَتْ وَأَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٩﴾

**19. "Kama mnataka hukumu basi hukumu imekwisha kujieni. Na mkiacha itakuwa ndio kheri kwenu. Na mkarejea Sisi pia Tutarejea. Na jeshi lenu halitakufaeni kitu, hata likiwa kubwa. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na Waumini".**

### Kuwajibu Washirikina Wanaoomba Hukumu.

Allah تعالی Anawaambia makafiri,

إِن تَسْتَفْتِحُوا

**"Kama mnataka hukumu..."** Kwa maana: Nyinyi makafiri mnamuomba Allah تعالی nusura, hukumu na uamuzi baina yenu na maadui wenu Waumini, basi mliyoyaomba tayari yamekwisha kujieni. Kama alivyosema Muhammad bin Is-haq na wengine, kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa 'Abdullah bin Tha'labah bin Su'ayr kwamba Abu Jahal alisema siku ya Badr: "Ewe Allah! Ni yupi katika sisi (wapiganaji na Waislamu) aliyevunja undugu, na akatuletea kisichojulikana, basi muangamize leo". Hiyo ilikuwa ni kutaka hukumu kutoka kwa Allah تعالی, ikateremshwa Aya,

إِن تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ

**"Kama mnataka hukumu basi hukumu imekwishakujieni".** Mpaka mwisho wa Aya<sup>1</sup>.

Imamu Ahmad alimnukuu 'Abdullah bin Tha'labah kwamba: "Abu Jahali alisema pindi alipokutana na kaumu (ya Waislamu), "Ewe Allah! Yeyote katika sisi (wapagani na Waislamu) aliyevunja undugu, na akatuletea kisichojulikana,

<sup>1</sup> At-Tabari 13:453.



basi muangamize leo.” Kwa maneno haya alikuwa akitaka hukumu<sup>1</sup>. Naye An-Nasai alinukuu katika Kitabu cha Tafsiri (katika *Sunan* yake). Kadhalika Al-Hakim alinukuu katika *Al-Mustadrak* yake, na akasema, “Hadithi hii ni *Sahih* kwa vigezo vya Masheikh wawili, lakini wao hawakuinukuu.”<sup>2</sup> Pia ilisimuliwa kama hivyo kutoka kwa Ibn ‘Abbas, Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah, Yazid bin Ruman na wengine رضي الله عنهم. As-Suddi alisema, “Washirikina walipotoka Makkah kwenda Badr walishikilia pazia la Al-Ka’bah na wakamuomba Allah تعالی Awape ushindi, walisema: “Ewe Allah! Wape ushindi upande ulio na haki kati ya majeshi mawili, na upe ushindi upande ulio mtukufu kati ya makundi haya mawili.” Allah تعالی Akasema,

إِنْ تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمْ الْفَتْحُ

**“Kama mnataka hukumu basi hukumu imekwisha kujieni”. (8:32)**

Na kama vile Allah تعالی Anasema, “Nimeikubali dua yenu, na Muhammad ﷺ amepata nusura.” Naye, ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema hiyo ni Kauli ya Allah تعالی Akipasha khabari zao,

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِنَّكَ كَارِبٌ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ

**“Na waliposema: Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako...” (8:32)**

Kauli ya Allah تعالی,

وَإِنْ تَنْتَهُوا

**“Na mkiacha...”** Yale mliyonayo, miongoni mwa kumkufuru Allah تعالی na kumkadhibisha Mtume ﷺ wake.

فَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ

**“...itakuwa ndio kheri kwenu.”** Duniani na Akhera. Kauli ya Allah تعالی,

وَإِنْ تَعُودُوا نَعُدَّ

**“Na mkirejea Sisi pia Tutarejea.”** Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

<sup>1</sup> Ahmad 5:431.

<sup>2</sup> An-Nasai katika Al-Kubra 6:350 na Al-Hakim 2:328.

وَإِنْ عُدْتُمْ عُدْنَا

**“Na mkirudia na Sisi Tutarudia”. (17:8)**

Maana yake ni kuwa kama mtayarudia yale mliyokuwa nayo katika ukafiri na upotevu, Tutawarejesheeni tukio kama hili.

وَلَنْ تُغْنِيَ عَنْكُمْ فِئَتُكُمْ شَيْئًا وَلَوْ كَثُرَتْ

**“Na jeshi lenu halitakufaeni kitu, hata likiwa kubwa.”**

Kwa maana: Hata kama mtayakusanya majeshi mtakavyoweza, basi mjue kwamba yule atakayekuwa pamoja Naye (Allah تعالی) hana wa kumshinda.

وَأَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ

**“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na Waumini.”**

Nao Waumini ndio kundi la Mtume ﷺ nao ndio upande wa Mjumbe mteule.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا تَوَلَّوْا عَنَّهُ وَأَنْتُمْ تَسْمَعُونَ ﴿١٧﴾ وَلَا  
تَكُونُوا كَالَّذِينَ قَالُوا سَمِعْنَا وَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ ﴿١٨﴾ \* إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِنْدَ اللَّهِ الصُّمُّ  
الْبُكْمُ الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٩﴾ وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَأَسْمَعَهُمْ ۗ وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوْا  
وَهُمْ مُعْرِضُونَ ﴿٢٠﴾

**20. “Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msijiepushe naye, nanyi mnasikia.”**

**21. “Wala msiwe kama wale wanaosema: Tumesikia na kumbe Hawasikii.”**

**22. “Hakika vinyama viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni vile Viziwi na bubu visiotumia akili zao.”**

**23. “Na Mwenyezi Mungu Angelijua wema wowote kwao Ange wasikilizisha, na lau Angewasikilizisha wangeligeuka wakapuuza.”**

**Amri ya Kumtii Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ.**

Allah تعالى Anawaamuru waja wake wamtii Yeye na Mtume ﷺ, na Anawakemea dhidi ya kumkhalifu na kujishabihisha na makafiri wanaomkataa. Kwa hiyo, Allah تعالى Alisema,

وَلَا تَوَلَّوْا عَنْهُ

**“..Na wala msijiepushe”.** Kwa maana: Msiache kumtii na kufuata amri zake, na kuyazingatia maonyo yake.

وَأَنْتُمْ تَسْمَعُونَ ﴿١٧﴾

**“..Hali ya kuwa, nanyi mnasikia”.** Kwa maana: Baada ya nyinyi kuyajua anayokuitieni.

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ قَالُوا سَمِعْنَا وَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ ﴿١٨﴾

**“Na wala msiwe kama wale wanaosema: Tumesikia na kumbe Hawasikii”.**

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema: “Hao ni wanafiki, kwani wao huonesha dhahiri kwamba wamesikia na wameitikia, kumbe hawako hivyo”<sup>1</sup>. Kisha Allah تعالى Alieleza hawa ndio viumbe waovu zaidi katika wanadamu. Allah تعالى Akasema,

﴿١٩﴾ إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِنْدَ اللَّهِ الصُّمُّ

**“Hakika viumbe viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni vile Viziwi...”.**

Yaani, dhidi ya kuisikia haki.

الْبُكْمُ

**“Bubu”.** Ni mabubu wasioweza kuelewa, Allah تعالى Alisema:

الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٢٠﴾

**“...visiotumia akili zao”.** Hao ndio viumbe waovu zaidi, kwani wanyama wote wasiokuwa wao ni wenye kumtii Allah تعالى kwa yale Aliyowaumbia kwayo, na hao waliumbwa kwa ajili ya ibada, wakakataa. Kwa ajili hii, Aliwashabihisha na wanyama katika Kauli Yake,

وَمَثَلُ الَّذِينَ كَفَرُوا كَمَثَلِ الَّذِي يَنْعِقُ بِمَا لَا يَسْمَعُ إِلَّا دُعَاءً وَنِدَاءً صُمٌّ بُكْمٌ عُمْىُ

فَهُمْ لَا يَعْقِلُونَ ﴿٢١﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 13:458.

**“Na mfano wa waliokufuru ni kama wa anayempigia kelele asiye sikia ila wito na sauti tu – viziwi, mabubu, vipofu, kwa hivyo hawaelewi”. (2:171)** Na katika Aya nyingine Alisema;

أُولَئِكَ كَالَّذِينَ نَادَىٰ رَبَّهُمْ أَوْ لَوْ أَنَّ كَانُوا يَسْمَعُونَ ﴿١٧١﴾

**“Hao ni kama wanyama bali wao wamepotea zaidi hao ndiyo wenye kughafilika”. (7:179)**

Ilisemwa kwamba: Makusudio ya hao waliotajwa ni kikundi cha Makuraishi kutoka kabila la Banu ‘Ad-Dar. Hayo ni kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, Mujahid na Ibn Jariri رحمه الله تعالى<sup>1</sup>. Muhammad bin Is-haq alisema: “Wanaokusudiwa hapa ni wanafiki”. Mimi nasema: “Hakuna tofauti kati ya wanafiki na makafiri hapa, kwa sababu kila mmoja amekoseshwa ufahamu sahihi na makusudio ya amali njema.” Kisha Allah تعالى Alieleza kwamba wao hawana ufahamu wa makusudio sahihi hata kama wana namna ya uelewa. Allah تعالى Alisema,

وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَّأَسْمَعَهُمْ

**“Na Mwenyezi Mungu Angelijua wema wowote kwao Ange wasikilizisha”.**

Angeliwasaidia wangeweza kufahamu lakini hakukuwa na kheri kwao, hivyo, Hakuwafahamisha kwa sababu, Yeye Anajua kwamba,

وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ

**“...na lau Angewasikilizisha”.** Kwa maana: Kuwafahamisha,

لَتَوَلَّوْا

**“...wangeligeuka”.** Dhidi ya hilo kwa makusudi na ujeuri, hata baada ya wao kufahamu,

وَهُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿١٧٢﴾

**“...wakapuza”.** Hayo.

يَتَأَيُّمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا تَحْيِيكُمْ ۗ وَعَلِمُوا أَنَّ اللَّهَ

يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ ۗ وَأَنذَرَتْ إِلَيْهِ تُحْشِرُونَ ﴿١٧٣﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 13:460.

**24. Enyi mlioamini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume Anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na Jueni kuwa Mwenyezi Mungu Huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika Kwake Yeye tu mtakusanywa”.**

**Amri ya Kumuitikia na Kumtii Allah تعالى na Mtume ﷺ.**

Bukhari alisema maana ya,

أَسْتَجِيبُوا لِلَّهِ

**“Muitikieni”.** Ni kujibu kwa kukubali.

لِمَا تُحْيِيكُمْ

**“...jambo la kukupeni uzima wa milele”.**

Linalokufanyeni kuwa wema. Kisha, Bukhari alisimulia juu ya Sa'id bin Al-Mu'alla رضي الله عنه kwamba alisema: “Nilikuwa katika Sala, Mtume ﷺ akapita karibu yangu. Akaniita, nami sikwenda, mpaka nikakamilisha Sala. Nikamuendea akasema:

«مَا مَنَعَكَ أَنْ تَأْتِيَنِي؟ أَنْتُمْ يَقُولُ اللَّهُ

“Kitu gani kilikuzuia usinijie? Kwani Allah تعالى Hakusema, Kisha akasoma,

يَأْتِيَهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ<sup>ط</sup>

**“Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele.”** Kisha akasema,

«لَا أَعْلَمُكَ أَكْبَرُ سُوْرَةِ فِي الْقُرْآنِ قَبْلَ أَنْ أُخْرَجَ»

**“Nitakufundisha Sura kuu katika Qur'an kabla sijatoka”.**

Alipokaribia kuondoka, nikamkumbusha. Mu'adh رضي الله عنه pia alisema, kuwa Hafs bin 'Asim alimsikia Abu Sa'id akisema kwamba alimsikia Sahaba mmoja wa Mtume juu ya hili. Mtume ﷺ akasema:

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾

**“Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote”. (1:1-6)**

### «هِيَ السَّعَةُ الْمَتَانِي»

“Aya hizi ni Aya saba zenye kurudiwa mara kwa mara”<sup>1</sup>.

Alinukuu Muhammad bin Is-haq رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى kutoka kwa Muhammad bin Ja'far bin Az-Zubayr رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى kutoka kwa 'Urwah bin Az-Zubayr رَضِيَ اللهُ عَنْهُ kuwa alisema juu ya Aya,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ

**“Enyi mlioamini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume Anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele.**

Maana: “Jibuni muitwapo kwa ajili ya vita ambavyo Allah تَعَالَى Anakutunzeni kutokana na matokeo ya vita hivyo baada ya udhalili na Anakupeni nguvu baada ya unyonge, na Anakuingeni dhidi ya adui aliyekukandamizeni<sup>2</sup>.”

**Allah تَعَالَى Huingia Kati Baina ya Mtu na Moyo Wake.**

Allah تَعَالَى Amesema,

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ

**“Na Jueni kuwa Mwenyezi Mungu Huingia kati ya mtu na moyo wake”.**

Ibn 'Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا alisema, “Allah تَعَالَى Humzuia Muumini na Kumuepusha na ukafiri, na kafiri Humuepusha na Imani”<sup>3</sup>. Al-Hakim alinukuu katika Kitabu cha *Al-Mustadrak* na alisema, “Ni hadithi *Sahih* lakini hawakuinukuu Bukhari na Muslim.”<sup>4</sup> Kadhalika alisema hivyo hivyo, Mujahid, Sa'id, 'Ikrimah, Adh-Dhahhak, Abu Swalih, 'Atwiyyah, Muqatil, Hayyan na As-Suddi<sup>5</sup>. Katika masimulizi mengine ya Mujahid juu ya Kauli ya Allah تَعَالَى,

يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ

**“...huingia kati ya mtu na moyo wake”.**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:158.

<sup>2</sup> Ibn Hisham 2:324.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:468.

<sup>4</sup> Al-Hakim 2:328.

<sup>5</sup> At-Tabari 13:470-471.

Kwa maana: "Mpaka amuache akiwa hautambui". As-Suddi alisema, "Huzuia kati ya mwanadamu na moyo wake, kiasi kwamba hawezi kuamini wala kukufuru, isipokuwa kwa idhini Yake Yeye. Kuna hadithi kadhaa kutoka kwa Mtume ﷺ ambazo zinasibiana na Aya hii. Imamu Malik alimnukuu Anas bin Malik رضي الله عنه akisema: "Mtume ﷺ alikuwa akikithirisha kusema:

«يَا مُقَلَّبَ الْقُلُوبِ! نَبَتْ قَلْبِي عَلَى دِينِكَ»

*"Ewe Mola Ambaye Huzigeuza nyoyo. Uthibitisha moyo wangu katika Dini Yako".*

Nikauliza, "Sisi tunakuamini wewe na ulichokuja nacho, je una khofu juu yetu?" Akajibu:

«نَعَمْ، إِنَّ الْقُلُوبَ بَيْنَ إِصْبَعَيْنِ مِنْ أَصَابِعِ اللَّهِ تَعَالَى يُقَلِّبُهَا»

*"Ndiyo, Nyoyo ziko baina ya Vidole viwili katika Vidole vya Allah تعالى. Yeye Huzigeuza (Atakavyo)"<sup>1</sup>.*

Hivi ndivyo alivyoinukuu At-Tirmidhi katika Kitabu cha Qadari katika Jami' yake (Sunan) na akasema, ni Hasan<sup>2</sup>. Imamu Ahmad alinukuu tena kutoka kwa An-Nawwas bin Sam'an Al-Kilaabi رضي الله عنه, alisema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَا مِنْ قَلْبٍ إِلَّا وَهُوَ بَيْنَ أَصْبَعَيْنِ مِنْ أَصَابِعِ الرَّحْمَنِ رَبِّ الْعَالَمِينَ إِذَا شَاءَ أَنْ يُقِيمَهُ أَقَامَهُ وَإِذَا شَاءَ أَنْ يُرِيغَهُ أَرَاغَهُ»

*"Hapana moyo wowote bali uko baina ya Vidole Viwili miongoni mwa vidole vya Ar-Rahman, Mola wa viumbe wote. Akitaka Kuunyoosha Anaunyoosha na Akitaka Kuupotosha Huupotosha".*

Na alikuwa akisema pia,

«يَا مُقَلَّبَ الْقُلُوبِ! نَبَتْ قَلْبِي عَلَى دِينِكَ»

*"Ewe Mola Ambaye Huzigeuza nyoyo. Ufanye moyo wangu uwe imara katika dini Yako".*

Alisema pia,

<sup>1</sup> Ahmad 3:112.

<sup>2</sup> Tuhfat Al-Ahwadhi 6:369, 350.

«وَالْيَزَانُ بِيَدِ الرَّحْمَنِ يُخَفِّضُهُ وَيَرْفَعُهُ»

*“Na Mizani iko Mikononi mwa Ar-Rahman, Huishusha na Kuinyanyua”<sup>1</sup>.*

Hivi ndivyo alivyopokea pia An-Nasai na Ibn Majah<sup>2</sup>.

وَاتَّقُوا فِتْنَةً لَا تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢٥﴾

**25. “Na jikingeni na Fitna ambayo haitowasibu waliodhulumu peke yao kati yenu. Na Jueni kuwa Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu”.**

**Kutahadharishwa na Fitnah Yenye Kuenea.**

Allah تعالی Anawaonya waja wake waumini juu ya majaribio na mtihani ambao unawaenea waovu na wasiokuwa waovu. Kwa hivyo, mtihani unaposhuka huwa hauwahusu wafanyao maasi na madhambi peke yao, bali unawaenea wabaya na wema ikiwa waovu hawatakatizwa na kuzuiliwa. Sawa na alivyonukuu Imam Ahmad kwamba Mutwarrif alisema, “Tulimuambia Az-Zubayr رضي الله عنه: “Ewe Abu ‘Abdullah! Ni nini kilichokuleteni (Je ni vita vya Al-Jamal)?” Mmemtelekeza Khalifa ambaye ameuawa (‘Uthman bin Affan رضي الله عنه), kisha mmekuja mkitaka kulipiza kisasi cha damu yake?” Az-Zubayr رضي الله عنه akasema, “Sisi tulisoma zama za uhai wa Mtume ﷺ, Abubakr, ‘Umar na ‘Uthman رضي الله عنهما Kauli ya Allah تعالی,

وَاتَّقُوا فِتْنَةً لَا تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً

**“Na jikingeni na Fitna ambayo haitowasibu waliodhumu peke yao kati yenu”.**

Hatukuwa tukidhani kwamba Aya hii ilituhusu sisi pia, mpaka ilipotufikia kama ilivyotokea<sup>3</sup>. Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنه alisema: Aya hii,

<sup>1</sup> Ahmad 4:182.

<sup>2</sup> An-Nasai katika Al-Kubra 4:414 na Ibn Majah 1:72.

<sup>3</sup> Ahmad 1:165.



وَاتَّقُوا فِتْنَةً لَا تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً

**“Na jikingeni na Fitna ambayo haitowasibu waliodhulumu peke yao kati yenu”.**

Inawahusu hasa Masahaba wa Mtume ﷺ<sup>1</sup>. Katika masimulizi yake mengine kutoka kwa ‘Abbas رضي الله عنه, katika kuitafsiri Aya hii, alisema: “Allah تعالى Aliwaamuru Waumini wasiyakubali maovu yashamiri mbele ya macho yao, ili Allah تعالى Asiwajumuishe wote katika Kuwaadhibu”<sup>2</sup>.

Tafsiri hii ni nzuri sana, na kwa minajili hii, Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَاتَّقُوا فِتْنَةً لَا تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْكُمْ خَاصَّةً

**“Na jikingeni na Fitna ambayo haitowasibu waliodhulumiwa peke yao kati yenu”.**

Kwamba, “Nayo pia ni kwa ajili yenu”<sup>3</sup>. Hivyo ndivyo pia alivyosema Adh-Dhahhak na Yazid bin Abu Habib na wengine. Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa, “Hapana yeyote miongoni mwenu, isipokuwa ana *Fitnah*, kwani Allah تعالى Anasema,

إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ وَاللَّهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿١٥﴾

**“Hakika mali zenu na watoto wenu ni fitnah. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa”. (64:15)**

Kwa hiyo, yeyote aombaye kinga, basi amuombe Allah تعالى Amkinge dhidi ya *Fitnah* zenye kupoteza. Aliinukuu Ibn Jariri رحمه الله تعالى<sup>1</sup>. Na kauli ya tahadhari hii inawajumuisha Masahaba na ghairi yao ni kweli, hata kama mazungumzo yaliwahusu wao. Hadithi zilizopokelewa juu ya tahadhari dhidi ya *Fitnah* kwa ujumla ni dalili inayoweka wazi jambo hilo na kuna kitabu mahsusi kinachofafanua jambo hilo *In sha Allah*. Kama walivyofanya Maimamu walioandika mengi juu ya hili. Na katika mapokezi mahsusi hapa ni yale ya

<sup>1</sup> At-Tabari 13:474.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:474.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:475.

<sup>4</sup> At-Tabari 13:475.

Imam Ahmad kutoka kwa Hudhaifa Al-Yaman رضى الله عنه kwamba Mtume ﷺ amesema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَتَأْمُرَنَّ بِالْمَغْرُوفِ وَلَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ أَوْ لَيُوشِكَنَّ اللَّهُ أَنْ يَبْعَثَ عَلَيْكُمْ عِقَابًا مِنْ عِنْدِهِ نُمْ لَتَدْعُهُ فَلَا يَسْتَجِيبُ لَكُمْ»

*“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Mtaamuru mema na kukataza maovu, au Allah تعالى Ataleta adhabu juu yenu kutoka Kwake, kisha mtamuomba Yeye, lakini hatakujibuni.”<sup>1</sup>*

Imamu Ahmad, alinukuu kutoka kwa Abu Ar-Riqad, kuwa alisema: “Nilitoka na bwana mkubwa wangu na nikaelekea kwa Hudhaifah رضى الله عنه na kumkuta akisema: “Ilikuwa mtu akizungumza neno moja zama za Mtume ﷺ basi huwa ni Mnafiki. Lakini mimi (siku hizi) hulisia mtu akilitamka kiasi cha mara nne katika kikao kimoja tu. Kwa hakika, mtaamrisha mema na kukataza maovu na mtahimizana katika kheri, vinginevyo, Allah تعالى Atakuenezeeni nyote adhabu, ama Atawaweka waovu wenu kuwa watawala wenu, kisha wabora wenu wataomba dua, lakini hawatakubaliwa.”<sup>2</sup>

### Hadithi Nyingine.

Imamu Ahmad alinukuu tena kutoka kwa An-Nu'man bin Bashir رضى الله عنه kuwa Mtume ﷺ alitoa khutuba, akiashiria masikioni mwake kwa vidole viwili, akisema,

«مَثَلُ الْقَائِمِ عَلَى حُدُودِ اللَّهِ وَالْوَاقِعِ فِيهَا وَالْمُدَاهِنِ فِيهَا كَمَثَلِ قَوْمٍ رَكِبُوا سَفِينَةً فَأَصَابَ بَعْضُهُمْ أَسْفَلُهَا وَأَوْعَرَهَا وَشَرَّهَا وَأَصَابَ بَعْضُهُمْ أَعْلَاهَا فَكَانَ الَّذِينَ فِي أَسْفَلِهَا إِذَا اسْتَقَمُوا الْمَاءَ مَرُّوا عَلَى مَنْ فَوْقَهُمْ فَأَذَوْهُمْ فَقَالُوا: لَوْ خَرَقْنَا فِي نَصِيبِنَا خَرْقًا فَاسْتَقَمْنَا مِنْهُ وَلَمْ نُؤْذِ مَنْ فَوْقَنَا: فَإِنْ تَرَكَوهُمْ وَأَمَرَهُمْ هَلَكُوا جَمِيعًا وَإِنْ أَخَذُوا عَلَى أَيْدِيهِمْ نَجَوْا جَمِيعًا»

*“Mfano wa mwenye kushikamana na mipaka ya Allah تعالى kulinganisha na mwenye kuikiuka na mwenye kukaa tu huku ikikiukwa, ni kama watu waliopanda Safina. Baadhi yao wakawa*

<sup>1</sup> Ahmad 5:388.

<sup>2</sup> Ahmad 5:390.

sehemu ya chini ambayo iko hovy na mbaya zaidi. Baadhi yao wakawa sehemu ya juu. Wale wa chini walipohitaji maji iliwabidi wapande juu, hilo likawapa usumbufu, na wakasema, “Lau tungelifanya tundu huku kwetu ili tuyapate, na tusiwasumbue wale wa juu yetu”, kwa hivyo, kama wangelibaacha waendeleo na jambo lao, wangelihiliki wote, na kama wangeliwazuia, wangelinusurika wote”<sup>1</sup>.

Ameinukuu Imam Bukhari peke yake katika Kitabu cha Ushirika na Ushahidi<sup>2</sup>. At-Tirmidhi aliinukuu katika mlango wa *Fitan* kwa njia nyingine ya usimulizi<sup>3</sup>. Isiyokuwa moja.

### Hadithi Nyingine.

Imamu Ahmad alimnukuu Umm Salamah رضي الله عنها, Mke wa Mtume ﷺ kuwa alisema, nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«إِذَا ظَهَرَتِ الْمَعَاصِي فِي أُمَّتِي عَمَّهُمُ اللَّهُ بِعَذَابٍ مِنْ عِنْدِهِ»

“Maasi yatakapodhihiri katika ummah wangu, basi Allah تعالى Atawaenezea adhabu kutoka Kwake.”

Nikasema: “Ewe Mtume! Je hakutakuwa baina yao na watu wema?” Akasema,

«بَلَى»

“Amba!” watakuwepo

Akasema: “Hao watafanya nini?” Akasema,

«يُصِيبُهُمْ مَا أَصَابَ النَّاسَ ثُمَّ يَصِيرُونَ إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٍ»

“Yatawasibu yanayowasibu watu lakini katika mwisho wao watapatiwa maghufira na Radhi za Allah!”<sup>4</sup>

<sup>1</sup> Ahmad 4:269.

<sup>2</sup> *Fat’hul Al-Bari* 5:157, 345.

<sup>3</sup> *Tuhfat Al-Ahwadhi* 6:394.

<sup>4</sup> Ahmad 6:304.

**Hadithi Nyingine.**

Imamu Ahmad alinukuu pia, kutoka kwa Jariri رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, kwamba Mtume ﷺ alisema,

«مَا مِنْ قَوْمٍ يُعْمَلُ فِيهِمْ بِالْمَعَاصِي هُمْ أَغْرُ وَأَكْثَرُ مِمَّنْ يَعْمَلُونَ ثُمَّ لَمْ يُغَيِّرُوهُ إِلَّا عَمَّهُمُ اللهُ بِعِقَابٍ»

*“Hapana kaumu hufanywa maasi baina yao na wana uwezo wa kuyazuia na ni wengi zaidi ya wafanyao kisha hawakuyazuia, ila Allah تَعَالَى Atawaenezea mateso.”<sup>1</sup>*

Aliikusanya Ibn Majah<sup>2</sup>.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ahmad 3:364.

<sup>2</sup> Ahmad 4:366 na Ibn Majah 2:1329.

وَأَذْكُرُوا إِذْ أَنتُمْ قَلِيلٌ مُسْتَضْعَفُونَ فِي الْأَرْضِ  
تَخَافُونَ أَنْ يَتَخَطَّفَكُمُ النَّاسُ فَفَاونَكُمْ وَأَيَّدَكُمْ بِنَصْرِهِ  
وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٢٦﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ  
ءَامَنُوا لَا تَخُونُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ وَتَخُونُوا أَمْنَتِكُمْ وَأَنْتُمْ  
تَعْلَمُونَ ﴿٢٧﴾ وَعَلِمُوا أَنَّ مَا أَمْوَالِكُمْ وَأَوْلَادِكُمْ فَتِنَةٌ  
وَأَنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا  
إِنْ تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَلْ لَكُمْ فُرْقَانًا وَيُكَفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ  
وَيَغْفِرْ لَكُمْ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾ وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ  
الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُبْتَئُواكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يَخْرُجُوكَ وَيَمْكُرُونَ  
وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٣٠﴾ وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ  
ءَايَاتُنَا قَالُوا قَدْ سَمِعْنَا لَوْ نَشَاءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هَذَا إِنْ  
هَذَا إِلَّا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٣١﴾ وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِنْ كَانَتْ  
هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ  
السَّمَاءِ أَوْ آتِنَا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٢﴾ وَمَا كَانَ اللَّهُ  
لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ ؕ وَمَا كَانَ اللَّهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ  
يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٣٣﴾

وَأَذْكُرُوا إِذْ أَنتُمْ قَلِيلٌ مُسْتَضْعَفُونَ  
فِي الْأَرْضِ تَخَافُونَ أَنْ يَتَخَطَّفَكُمُ  
النَّاسُ فَفَاونَكُمْ وَأَيَّدَكُمْ بِنَصْرِهِ  
وَرَزَقَكُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ لَعَلَّكُمْ  
تَشْكُرُونَ ﴿٢٦﴾

26. "Na kumbukeni mlipo kuwa wachache, mkionekana wanyonge katika nchi, mnaogopa watu wasikunyakueni, Naye Akakupeni pahala pazuri pa kukaa, na Akakutieni nguvu kwa Nusura Yake, na Akakupeni riziki nzuri ili mpate kushukuru."

Kuwakumbusha Waislamu Juu ya Hali yao ya Udhaili na Unyonge Waliyokuwa nayo na Hatimaye kuwa na Nguvu na Ushindi.

Allah تعالى Anawazindua waja Wake Waumini, neema na ihsani Yake kwao, walipo

kuwa wachache, Akawakithirisha; walikuwa wanyonge na waoga, Akawajalia nguvu na Akawapa ushindi; na walipokuwa wenye ufukara na dhiki, Akawaruzuku yaliyo mazuri, Akawataka washukuru, nao wakamtii na wakafuata amri Zake zote. Hii ndiyo ilikuwa hali ya Waislamu walipokuwa Makkah, wakiwa wachache, wanyonge, wenye kuteswa, wakiwa na khofu ya kutekwa na watu wa miji mingine ya Washirikina, Majusi na Warumi. Wote hao ni adui zao.

Khofu hiyo ni kwa sababu ya uchache wao na ukosefu wa nguvu. Hali hiyo iliendelea kuwakumba mpaka Allah تعالی Alipowapa idhini ya kuhamia Madinah, Akawapa makazi huko, wakapokewa na watu wa huko, wakawapa makazi, wakiwasaidia katika vita vya Badr na vingine, wakawapatia mali zao na wakajitolea nafsi zao katika kumtii Allah تعالی na Mjumbe wake. Qatadah bin Di'amah As-Sadusi alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالی:

وَأَذْكُرُوا إِذْ أَنتُمْ قَلِيلٌ مُسْتَضْعَفُونَ فِي الْأَرْضِ

***“Na kumbukeni mlipokuwa wachache, mkionekana wanyonge katika nchi.”***

Alisema: “Waarabu walikuwa dhalili wenye maisha magumu sana, wenye matumbo yenye njaa sana, wakosefu wa nguo na wapotevu dhahiri zaidi kuliko watu wengine. Aliyeishi miongoni mwao alikuwa katika umasikini na alipokufa mmoja wao, alipelekwa katika moto. Wao waliliwa na wenzao, yaani maadui, lakini wao hawakuweza kumla adui yao. Wallahi! Hatulijui kabila lolote katika watu walioishi duniani kwa wakati huo waliokuwa na nafasi mbaya zaidi kuliko wao, mpaka Allah تعالی Alipouleta Uislamu, Akaumakinisha duniani na Akawakunjulia riziki na Kuwafanya wakuu wa Kuwaongoza watu. Ni kwa kupitia Uislamu ndio Allah تعالی Amekupatieni mnayoyaona, basi mshukuruni Allah تعالی juu ya neema Zake, kwani Mola wenu ni Mwenye Fadhila, Anapenda Kushukuriwa, na watu wenye kushukuru ndio wenye kuzidishiwa fadhila za Allah.”<sup>1</sup>

يَتَأَيُّمُوا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَخُونُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ وَتَخُونُوا أَمْنَتِكُمْ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٧﴾ وَأَعْلَمُوا

أَنْتُمْ أَمْوَالِكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فَفِتْنَةٌ وَأَنْ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾

***27. “Enyi mlioamini! Msimfanyie khiana Mwenyezi Mungu na Mtume, wala msikhini amana zenu, nanyi mnajua.”***

***28. “Na Jueni ya kwamba mali zenu na wana wenu ni Fitna (mtihani) na kwamba kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa.”***

<sup>1</sup> At-Tabari 13:478.

### Sababu za Kuteremshwa Aya Hii na Makatazo Dhidi ya Khiana.

Katika *Sahih* Mbili kuna kisa cha Hatib bin Abu Balta'ah رضي الله عنه kuwa aliwaandikia Makuraishi katika mwaka wa *fat-h* (ushindi wa Makkah) akiwajulisha makusudio ya Mtume ﷺ kuwaendea wao. Allah تعالى Akaifichua siri hiyo kwa Mtume ﷺ. Naye akampeleka mjumbe kuirudisha barua, akaletwa Hatib na akakiri kosa hilo alilolifanya. 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه akasimama na kusema: "Ewe Mtume! Hivi huniachii nimkate shingo yake? Kwani yeye amemfanyia usaliti Allah تعالى, Mtume ﷺ na Waumini." Naye Mtume ﷺ akasema:

«دَعَا فَإِنَّهُ قَدْ شَهِدَ بَدْرًا، وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ اللَّهَ أَطَّلَعَ عَلَى أَهْلِ بَدْرِ فَقَالَ: اغْمَلُوا مَا  
بِشَيْئِكُمْ فَقَدْ عَفَرْتُ لَكُمْ»

*"Mwache! Yeye alishiriki katika Badr. Unajuaje? Huenda Allah تعالى Akawatazama watu wa Badr, na akasema, "Fanyeni mkitakacho kwani Nimeshakupeni maghufira."*

Mimi nasema: Aya Inaonekana maana yake ni ya ujumla, ingawa iliteremshwa kwa sababu makhsusi<sup>1</sup>. Kwa hivyo kinachozingatiwa ni tamko la jumla, na si sababu makhsusi (ya kuteremshwa kwa mujibu wa maulamaa wengi). Khiana inajumuisha madhambi madogo na makubwa, yanayomlazimu mtu yeye mwenyewe au anayowafanyia wengine. 'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Aya,

وَتَحْوُنُوا أَمْسِنَتِكُمْ

**"...wala msikhini amana zenu".**

*"Amanah ni amali ambazo Allah تعالى Aliwapa waja kama amana, maana; mambo ya Faradhi. Allah تعالى Anasema:*

لَا تَحْوُنُوا

**"Msimfanyie khiana".**

<sup>1</sup> Alikuwa akisema hivi kwa sababu alivitaja visa viwili visivyokuwa sahihi katika mnasaba huo. Zaidi ya hivyo, katika suala la Hatib, Aya hii iliyoshushwa ilikuwa *Al-Mumtahinah* (60:1) kama ilivyonukuliwa na Al-Hakim na wengine.

Maana: Msizitengue na kuzivunja (hayo ya Faradhi)<sup>1</sup>. 'Abdur-Rahman bin Zayd alisema: "Allah تعالى Amekukatazeni kumfanyia khiana Yeye na Mtume Wake, kama wafanyavyo wanafiki."<sup>2</sup> Kauli ya Allah تعالى،

وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا آمَوَلِكُمْ وَأَوْلَدُكُمْ فَتِنَةٌ

**"Na Jueni ya kwamba mali zenu na wana wenu ni Fitna (mtihani)."**

Maana yake: Jaribio na mtihani wake kwenu. Amekupeni haya ili Ajue kwamba mtamshukuru na kumtii katika hayo au mtakuwa wenye shughuli nyingi na kuzithamini zaidi, badala Yake. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّمَا آمَوَلِكُمْ وَأَوْلَدُكُمْ فَتِنَةٌ وَاللَّهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ

**"Hakika mali yenu na watoto wenu ni jaribio. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa." (64:15)**

وَتَبْلُوكُمْ بِالْأَثَرِ وَالْخَيْرِ فَتِنَةٌ

**"...na Tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri." (21:35)**

Na Amesema pia،

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تُلْهِكُمْ أَمْوَالِكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ ؕ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ

فَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ

**"Enyi mlio amini! Yasikusahaulisheni mali yenu wala watoto wenu, kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Na wenye kufanya hayo ndio waliokhasirika". (63:9)** Na Amesema Allah تعالى،

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ مِنْ أَزْوَاجِكُمْ وَأَوْلَادِكُمْ عَدُوًّا لَكُمْ فَاحْذَرُوهُمْ

**"Enyi mlioamini! Hakika miongoni mwa wake zenu na watoto wenu wamo maadui zenu. Basi tahadharini nao..."**

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ

**"...na kwamba kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa".**

<sup>1</sup> At-Tabari 13:485.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:483.



Maana: Thawabu Zake, Fadhila Zake na Pepo Zake ni bora kwenu kuliko mali na watoto, kwani anaweza kupatikana adui miongoni mwao, na wengi wao hawakutoshelezi kwa lolote. Allah تعالی Peke Yake Ndiye Mtawala, Mmiliki wa dunia na Akhera, Kwake Yeye kuna thawabu nyingi Siku ya Kiyama. Katika *Sahih* kuna Hadithi ya Mtume ﷺ alisema.

ثَلَاثٌ مَنْ كُنَّ فِيهِ، وَجَدَ بَيْنَ حَلَاوَةِ الْإِيمَانِ: مَنْ كَانَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِمَّا سِوَاهُمَا، وَمَنْ كَانَ يُحِبُّ الْمَرْءَ لَا يُحِبُّهُ إِلَّا اللَّهُ، وَمَنْ كَانَ أَنْ يُلْقَى فِي النَّارِ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِنْ أَنْ يَرْجِعَ إِلَى الْكُفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْقَذَهُ اللَّهُ مِنْهُ

*"Kuna sifa tatu ambazo iwapo mmoja wapo atakuwa nazo, atakuwa ameonja utamu wa Imani. Mwenye kuwapenda Allah تعالی na Mtume ﷺ zaidi ya kitu chochote, mwenye kumpenda mtu mwingine, si kwa jambo jingine isipokuwa kwa ajili ya Allah تعالی na mtu ambaye anahitari kutumbukizwa kwenye moto, kuliko kurejea katika kufuru, baada ya Allah تعالی Kumnusuru dhidi yake."*<sup>1</sup>

Kwa hivyo kipaumbele chake ni kumpenda Mtume ﷺ kuliko watoto wake, mali yake na nafsi yake<sup>2</sup>. Sawa na ilivyothibiti katika Sahihi kuwa Mtume ﷺ alisema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! لَا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّىٰ أكونَ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِنْ نَفْسِهِ وَأَهْلِهِ وَمَالِهِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ»

*"Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Hapana yeyote miongoni mwenu ambaye atakuwa ni Muumini wa kweli isipokuwa mpaka niwe ni mpendwa zaidi kwake kuliko nafsi yake, familia yake, mali yake, na watu wote"*<sup>3</sup>.

يَنَائِبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَل لَكُمْ فُرْقَانًا وَيُكَفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾

**29. "Enyi mlioamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu Atakupeni kipambanuo, na Atakufutieni makosa yenu, na Atakusameheni, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kubwa".**

<sup>1</sup> Muslim 1:66.

<sup>2</sup> Muslim 1:67.

<sup>3</sup> Fat'hul Al-Bari 1:75.

Alisema Ibn 'Abbas, As-Suddi, Mujahid, 'Ikrimah, Adh-Dhahhak, Qatadah na Muqatil bin Hayyan na wengine رضي الله عنهم kuwa maana ya neno,

فُرْقَانًا

**"Furqanan"**, Kwa maana: "Njia ya kutolea ufumbuzi". Mujahid aliongeza: Ufumbuzi huo ni wa hapa "Duniani na Akhera"<sup>1</sup> Na katika masimulizi ya Ibn 'Abbas رضي الله عنهما juu ya Aya, **"Furqanan"** alisema maana yake ni "kuokoka", na katika masimulizi yake mengine alisema maana yake ni "nusura". Muhammad bin Is-haq alisema, **"Furqan"** yaani kitenganishi baina ya haki na batili. Tafsiri hii ya Ibn Is-haq ni ya ujumla zaidi kuliko zilizotangulia na inazijumuisha maana nyingine zote, kwani wenye taqwa kwa Allah تعالى kivitendo, kwa kuzitekeleza Amri Zake na kuyaacha Anayoyakataza, watakuwa wamefikishwa kupambanua baina ya haki na batili. Hivyo itakuwa ndiyo sababu ya kunusurika na kuokoka kwao na kubabaika kwao na mambo ya kidunia, na kuwa na furaha katika Siku ya Kiyama na kufutwa kwa madhambi yao, na kughufiriwa, na kusitiriwa dhidi ya watu, na hiyo husababisha kupata thawabu nyingi za Allah تعالى. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وءَامِنُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتِكُمْ كِفْلَيْنِ مِن رَّحْمَتِهِ وَيَجْعَل

لَكُمْ نُورًا تَمْشُونَ بِهِ وَيَغْفِرَ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٨﴾

**"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na muaminini Mtume wake, Atakupeni sehemu mbili katika Rehema Yake, na Atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo. Na Atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."**  
(57:28)

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ ۚ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ ۗ وَاللَّهُ

خَيْرُ الْمَكْرِينِ ﴿٣٠﴾

**30. "Na kumbuka walipokupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuue, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu Akapanga Yake. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa mipango".**

<sup>1</sup> At-Tabari 13:489-490.

## Maelezo Kuhusu Njama za Watu wa Makkah za Kutaka Kumuua Mtume ﷺ, au Kumhamisha au Kumfukuza Kutoka Makkah.

Alisema, Ibn 'Abbas, Mujahid na Qatadah رضي الله عنهم,

لِيُنْبِتُواكَ

“**Wakufunge**” Ina maana, “wakuweke kizuizini”<sup>1</sup>. As-Suddi alisema, “*Ithbat* ni kuwekwa kizuizini na kutiwa mahabusu.”<sup>2</sup>

Imamu Muhammad bin Is-haq bin Yasaar رحمه الله تعالى, mwandishi wa mambo ya vita, *Maghazi*, alimnukuu 'Abdullah bin Abu Najih, kutoka kwa Mujahid kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, katika masimulizi mengine kuwa alisema: Alinisimulia Al-Kalbi kutoka kwa Baadhan, Mwacha huru wa Umm Hani kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: “Wakuu wa kila kabila la Kikuraish walijumuika katika *Daru-Nadwah* (jumba lao la mikutano), akawatokea Iblis katika sura ya Mzee, kutokea Najd. Walipomuona walimuuliza, “Wewe ni nani?” Akajibu: “Ni mzee kutoka Najid.” Nimesikia kwamba nyinyi mmekutana, nikataka kuhudhuria. Maoni na nasaha zangu hazitakukatisheni tamaa.” Wakasema, “Imekubalika, ingia”. Akaingia pamoja nao, na akasema: “Hebu angalieni jambo la mtu huyu. Wallahi! Limekaribia, jambo lake kuwa na nguvu zaidi ya la kwenu.” Msemaji mmoja katika wao akasema: “Muwekeni kifungoni kisha mumuache humo mpaka afariki, kama walivyofanyiwa washairi wa kabla yake, kama vile Zuhayr na An-Nabighah! Kwa hakika, yeye ni sawa na mmoja wao.” Adui wa Allah تعالى, Mzee wa Najd akapiga kelele na kusema, “Wallahi! Hii si rai nzuri. Wallahi! Mola wake Atamtoa kifungoni kwenda kwa Masahaba wake ambao wataleta matatizo ya kutaka kumuokoa na wao kufanikiwa na kumchukua kutoka Mikononi mwenu. Kisha watamhami dhidi yenu na hamtakuwa na amani kwani watakutoeni katika ardhi yenu.” Wakasema, “Mzee amesema kweli, angalieni rai nyingine isiyokuwa hii.” Akasema msemaji mwingine miongoni mwao, “Mtoeni kutoka katika ardhi yenu ili mpumzike naye, kwani akishaondoka, hayatakudhuruni atakayoyafanya au mahali anapokwenda pindi udhia wake ukighibu kwenu, nanyi mkapumzika. Kwa hivyo jambo lake litakuwa kwa watu wengine.” Mzee wa Najdi akasema: “Wallahi! Haya si maoni mazuri kwenu. Hivi hamjaona utamu wa kauli yake na ufasaha, wa mazungumzo yake na namna yanavyozivuta nyoyo? Wallahi! Ikiwa mtafanya

<sup>1</sup> At-Tabari 13:491.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:492.

hivyo, kisha ikiwadhihirikia Waarabu, watamkusanyikia, kisha watakujieni na kukutoeni kutoka katika ardhi yenu na kuwaua wakuu wenu.” Wakasema, “Wallahi! Amesema kweli.” Basi angalieni rai isiyokuwa hii.

Abu Jahal, laana ya Allah تعالى imshukie, akasema: “Wallahi! Nitakushaurini rai ambayo hamjaiona kabla ya leo.” Yaani; hapana aliyeipendekeza. Wakasema, “Ni ipi hiyo?” Akasema, “Mumchukue kijana mmoja mmoja mwenye nguvu, mwenye umri wa kati, kutoka kila kabila. Kisha, kila kijana kati yao, apewe upanga mkali, kisha wampige nao pigo la mtu mmoja (yaani wote kwa pamoja). Wakishamuuu, basi damu yake itakuwa imemwagwa na makabila yote. Nami sidhani Banu Hashim watakaokuwa hai wanaweza kuwa na nguvu za kupigana na Makuraish wote. Kwa hiyo, wakishaona hivyo, itawabidi wakubali kulipwa fidia. Nasi tutapumzika na hivyo kuondosha udhia wake”. Mzee wa Najdi akasema, “Wallahi! Hii ndio rai. Sioni rai iliyo bora ghairi ya kauli aliyoisema huyu kijana.” Wakaondoka wakiwa na azimio hilo, na makubaliano juu ya hilo.

Jibril عليه السلام akamjia Nabii na kumuamuru kuwa usiku ule asilale katika kitanda chake alichozoea kukilalia na akampa khabari za njama za Makuraish. Siku hiyo, Mtume ﷺ hakulala nyumbani kwake, na Allah تعالى Akampa idhini ya kuhama. Baada ya kuwasili Madinah, Allah تعالى Akamteremshia Surat Al-Anfaal, kwa kumtaja neema Zake na mitihani Yake kwake Mtume ﷺ,

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ ۚ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ ۗ وَاللَّهُ

خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٥٠﴾

***“Na walipokupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuue, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu Akapanga Yake. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa mipango”.***

Akateremsha juu ya kauli yao: “Tunamtarajia kupatilizwa na dahari kama walivyohiliki washairi waliokuwepo kabla yake.”

أَمْ يَقُولُونَ شَاعِرٌ نَّتَرَبَّصُ بِهِمْ رَبِّبَ الْمُتَنُونَ ﴿٥١﴾

***“Au wanasema: Huyu ni mtunga mashairi, tunamtarajia kupatilizwa na dahari.” (52:30)***

Siku hiyo waliyotoa azimio lao ilikuwa ikiitwa *Yawmuz-Zahma* (Siku ya Mkutano) kwa sababu ya kujumuika kwao kwenye rai yao hiyo.”<sup>1</sup>

As-Suddi naye alikisimulia kisa hiki. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema kutoka kwa Muhammad bin Ja'far bin Az-Zubayr رحمه الله تعالى, kutoka kwa 'Urwah bin Az-Zubayr عنه رضي الله عنه alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى:

وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٢٦﴾

**“Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu Akapanga Yake.  
Na Mwenyezi Mungu ndiye Mbora wa mipango”.**

Maana yake: “Nikawafanyia Mipango Yangu Mimi ya uhakika, na Nikakuokoa (ewe Muhammad ﷺ), dhidi yao<sup>2</sup>.”

وَإِذَا تَتَلَىٰ عَلَيْهِمْ ءَايَاتُنَا قَالُوا قَدْ سَمِعْنَا لَوْ نَشَاءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هَذَا إِنْ هَذَا إِلَّا  
أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٢٧﴾ وَإِذْ قَالُوا اٰللّٰهُمَّ اِنْ كَانِ هٰذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَاَمْطِرْ عَلَيْنَا  
حِجَابًا مِّنَ السَّمَاءِ اَوْ اَتِّنَا بِعَذَابٍ اَلِيمٍ ﴿٢٨﴾ وَمَا كَانَ اَللّٰهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَاَنْتَ فِيهِمْ  
وَمَا كَانَ اَللّٰهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٢٩﴾

**31. “Na wanaposomewa Aya Zetu, wao husema: Hakika tumesikia.  
Na lau tungelipenda tungesema kama haya. Haya si chochote ila  
hadithi za watu wa kale tu.”**

**32. “Na waliposema: Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli  
itokayo kwako basi tulettee mvua ya mawe kutoka mbinguni, au  
tulettee adhabu yoyote iliyo chungu.”**

**33. “Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa Kuwaadhibu nawe umo  
pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa Kuwaadhibu na hali ya  
kuwa wanaomba msamaha.”**

<sup>1</sup> Ibn Hisham 1:480-482.

<sup>2</sup> Ibn Hisham 2:325.

### Madai ya Makuraishi kuwa Wanaweza Kuleta Mfano wa Qur'an.

Allah تعالی Anakhabarisha juu ya kufuru ya Makuraishi, uchupaji wa mipaka, ufedhuli, ukaidi na madai yao batili wayatoayo wakati wanapozisikia Ayah za Allah تعالی zinaposomwa kwao, husema:

سَمِعْنَا لَوْ نَشَاءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هَذَا

**“Hakika tumesikia. Na lau tungelipenda tunganese kama haya”.** Hizi ni kauli zitokazo kwao, ambazo hawawezi kuzitekeleza kwani walipewa changamoto mara nyingi kuwa walete Surah moja mithili ya Qur'an, na wakakosa njia ya kulifanya hilo. Ama kwa kauli yao hii wanadanganya nafsi zao na waliowafuata katika upotevu wao. Ilisemwa kwamba msema wa hayo alikuwa An-Nadhr bin Al-Harith, Allah تعالی Amlaani. Hayo ni kwa mujibu wa Sa'id bin Jubayr, Ibn Jurayj na wengineo. An-Nadhr, Alaaniwe na Allah تعالی, alikwenda katika nchi ya Fursiy, akajifundisha khabari za wafalme wao kina Rostum na Isfandiyar. Aliporudi alikuta Mtume ﷺ alikwishaletwa na Allah تعالی na alipokuwa akiwasomea watu Qur'an na Mtume ﷺ anapowahubiria watu katika majilisi, An-Nadhr naye huja na kuanza kuwahadithia khabari za hao wafalme na kisha husema: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu! Ni nani mwenye visa vizuri vya kusimulia, ni mimi au Muhammad?” Allah تعالی Alipowawezesha Waislamu kumteka An-Nadhr katika siku ya Badr, Mtume ﷺ aliamuru akatwe shingo akishuhudia na hilo likafanyika. Allah تعالی Ndiye Mwenye Haki ya Kushukuriwa. Na maana ya neno:

أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٥٦﴾

**“...asaatirul-awalina...”**, Asaatiru ni wingi wa neno *Ustuwrah*, na maana yake ni vitabu vyao kwa maana kuwa, Mtume ﷺ aliiba maandishi katika vitabu vyao na kujifunza na kuwasomea watu. Huu ni uongo wa wazi, kama Allah تعالی Alivyopasha khabari zao katika Aya ifuatayo,

وَقَالُوا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ۖ أَكْتَتَبَهَا فَهِيَ تُمَلَّى عَلَيْهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا ﴿٥٦﴾ قُلْ أَنْزَلَهُ الَّذِي

يَعْلَمُ الْسِرِّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ إِنَّهُ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٥٧﴾

**“Na wakasema: Hivi ni visa vya watu wa kale alivyoviandikisha, anavyosomewa asubuhi na jioni. Sema: Ameyateremsha haya ni yule ambaye Ajuaye siri za katika mbingu na ardhi. Hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.” (25:5-6)**

Maana yake: Kwa mwenye kutubu, Allah تعالی Atampokea na Atamsamehe.

Washirikina Wanaomba Hukumu na Wanataka Adhabu ya Allah تعالى.

Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِن كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابَةً مِنَ السَّمَاءِ  
أَوْ آتِنَا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢٦﴾

**“Na waliposema: Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako basi tulettee mvua ya mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyo chungu”.**

Haya ni kwa sababu ya kukithiri kwa ujahili wao na kuzidi kukadhibisha kwao, ukaidi wao na uchupaji mipaka. Ilikuwa ni bora kwao wangaliomba: “Ewe Allah تعالى! Ikiwa hii ndiyo haki itokayo Kwako, basi Utuongoze kwenye haki hiyo na Utuwafikishe kuifuata.” Lakini badala yake walijiomba hukumu yao wenyewe na wakaomba waharakishiwe kupewa adhabu, na kuwatangulizia mateso. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَسْتََعْجَلُونَكَ بِالْعَذَابِ ۚ وَلَوْلَا أَجَلٌ مُّسَمًّى لَّجَاءَهُمُ الْعَذَابُ وَلَيَأْتِيَنَّهُمْ بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٢٧﴾

**“Na wanakuhimiza waletewe adhabu kwa haraka. Na lau kwamba hapana wakati maalumu uliowekwa, basi adhabu ingeliwajia na ingeliwatokea kwa ghafla, na hali wao hawana khabari”. (29:53)**  
Na pia Kauli Yake,

وَقَالُوا رَبَّنَا عَجِّلْ لَنَا قِطْعَانًا قَبْلَ يَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٢٨﴾

**“Na wao husema: Mola wetu Mlezi! Tulettee upesi sehemu yetu ya adhabu kabla ya Siku ya Hisabu”. (38:16)** Na Kauli yake,

سَأَلَ سَائِلٌ بِعَذَابٍ وَاقِعٍ ﴿٢٩﴾ لِّلْكَافِرِينَ لَيْسَ لَهُ دَافِعٌ ﴿٣٠﴾ مِنَ اللَّهِ ذِي  
الْمَعَارِجِ ﴿٣١﴾

**“Muulizaji aliuliza juu ya adhabu itokayotokea. Kwa makafiri – ambayo hapana awezaye kuizua – Kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Mbingu za daraja”. (7:1-3)**

Kadhaliika, majahili katika ummah zilizotangulia walisema maneno kama hayo, kama Shu'ayb عليه السلام alivyoambiwa na kaumu yake;

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿٢٦﴾

***“Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao ukweli”. (26:187)***

Na Washirikina wa Kikuraishi nao walisema:

اللَّهُمَّ إِن كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِن عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَارَةً مِّنَ السَّمَاءِ أَوْ آتِنَا

بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢٧﴾

***“Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo Kwako basi tulettee mvua ya mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyochungu”.***

Shu'bah alisema kutoka kwa 'Abdul-Hamid mwandishi wa “Ziyaad” kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema: Abu Jahl bin Hisham ndiye aliyetamka maneno haya kuwa,

اللَّهُمَّ إِن كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِن عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَارَةً مِّنَ السَّمَاءِ أَوْ آتِنَا

بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢٧﴾

***“Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako basi tulettee mvua ya mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyo chungu”.***

Ikateremshwa,

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ ؕ وَمَا كَانَ اللَّهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٢٨﴾

***“Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa Kuwaadhibu nawe umo pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa Kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha”.***

Ameinukuu Bukhari<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:160.



**Kusalimika kwa Washirikina na Adhabu ni kwa Sababu ya Kuwepo kwa Mtume ﷺ na Kuomba kwao Msamaha.**

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ وَمَا كَانَ اللَّهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٣٣﴾

***“Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa Kuwaadhibu nawe umo pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa Kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha”.***

Ibn Abu Hatim رضي الله عنهما alisimulia kuwa Ibn ‘Abbas رحمه الله تعالى alisema, Washirikina walikuwa wakiitufu Ka’aba huku wakisema, “Tumekuitika ewe Allah تعالى! Tumekuitika, ewe usiye na mshirika”. Mtume ﷺ naye akawa anasema:

﴿قَدَّ، قَدَّ﴾

*“Ni hakika, Ni hakika!”*

Lakini walikuwa wakiendelea kusema: “Tumekuitika ewe Allah! Tumekuitika, ewe usiye na mshirika, isipokuwa mshiriki aliye pamoja Nawe. Wewe Unammiliki yeye na kila anachomiliki”. Pia walikuwa wakisema, “(Tunakuomba) Msamaha wako! (Tunakuomba) Maghfira yako!” Allah تعالى Akateremsha:

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ

***“Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa Kuwaadhibu nawe umo pamoja nao”.***

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Walikuwa na kinga mbili za kuwepo kwa Mtume ﷺ na uombaji wa maghufira. Mtume ﷺ akaondoka, ikabakia uombaji wa msamaha”<sup>1</sup>. At-Tirmidhi alimnukuu Abu Musa رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema,

﴿أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَيَّ آمَاتَيْنِ لِأُمَّتِي﴾

*“Allah تعالى Aliniteremshia hifadhi mbili za amani kwa ajili ya umma wangu”.* Kisha akasoma,

<sup>1</sup> At-Tabari 13:511.

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ وَمَا كَانَ اللَّهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٢٦﴾

**“Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa Kuwaadhibu nawe umo pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa Kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha”.**

«فَإِذَا مَضَىٰ تَرَكْتُ فِيهِمْ الْأَسْتِغْفَارَ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

*“Nitakapofariki, nitawaachia jambo la uombaji wa maghufira mpaka Siku ya Kiyama”<sup>1</sup>.*

Hili linathibitishwa na yaliyonukuliwa na Imamu Ahmad katika *Musnad* wake na Al-Hakim katika *Al-Mustadrak* wake, kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ الشَّيْطَانَ قَالَ: وَعِزَّتِكَ يَا رَبُّ! لَا أَبْرُحُ أُغْوِي عِبَادَكَ مَا دَامَتْ أَرْوَاحُهُمْ فِي أَجْسَادِهِمْ. فَقَالَ الرَّبُّ: وَعِزَّتِي وَجَلَالِي! لَا أَزَالُ أُغْفِرُ لَهُمْ مَا اسْتَعْفَرُونِي»

*“Shetani alisema, “Naapa kwa Nguvu Zako, ewe Mola! Nitaendelea kuwahadaa waja Wako, maadamu roho zao ziko katika viwiliwili vyao!. Mola Akasema, “Naapa kwa Nguvu na Utukufu Wangu! Nitaendelea Kuwaghufiria maadamu wananiomba msamaha”<sup>2</sup>.*

Kisha Al-Hakim alisema: “Hadithi hii ina Isnadi Sahihi, lakini (Bukhari na Muslim) hawakuinukuu”<sup>3</sup>.

\* \* \*

<sup>1</sup> Tuhfatu Al-Ahwadhi 8:472.

<sup>2</sup> Ahmad 3:29.

<sup>3</sup> Al-Hakim 4:261.

وَمَا لَهُمْ إِلَّا يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ وَهُمْ يَصُدُّونَ عَنِ الْمَسْجِدِ  
 الْحَرَامِ وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ<sup>٤</sup> إِنْ أَوْلِيَاؤُهُ إِلَّا الْمُتَّفِقُونَ  
 وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٤﴾ وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِنْدَ  
 الْبَيْتِ إِلَّا مُكَاءً وَتَصَدِيَةً<sup>٥</sup> فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ  
 تَكْفُرُونَ ﴿٣٥﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ  
 لِيَصُدُّوا عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ<sup>٦</sup> فَسَيُنْفِقُونَهَا ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ  
 حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ<sup>٧</sup> وَالَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ مُخْشَرُونَ  
 ﴿٣٦﴾ لِيَمِيزَ اللَّهُ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ وَيَجْعَلَ الْخَبِيثَ  
 بَعْضُهُ عَلَىٰ بَعْضٍ فَيَرْكُمَهُ جَمِيعًا فَيَجْعَلُهُ فِي جَهَنَّمَ<sup>٨</sup>  
 أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٣٧﴾ قُلْ لِلَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ  
 يَنْتَهُوا يُغْفَرْ لَهُمْ مَا قَدْ سَلَفَ وَإِنْ يَعُودُوا فَقَدْ مَضَتْ  
 سُنَّتُ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٨﴾ وَقَتَلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ  
 وَيَكُونَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِللَّهِ<sup>٩</sup> فَإِنْ أَنْتَهُوا فَإِنَّ اللَّهَ بِمَا  
 يَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٣٩﴾ وَإِنْ تَوَلَّوْا فَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَوْلَانَكُمْ  
 إِنَّ اللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٤٠﴾

وَمَا لَهُمْ إِلَّا يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ وَهُمْ  
 يَصُدُّونَ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ  
 وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ<sup>٤</sup> إِنْ أَوْلِيَاؤُهُ إِلَّا  
 الْمُتَّفِقُونَ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا  
 يَعْلَمُونَ ﴿٣٤﴾ وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِنْدَ  
 الْبَيْتِ إِلَّا مُكَاءً وَتَصَدِيَةً<sup>٥</sup> فَذُوقُوا  
 الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٥﴾

34. "Lakini wana jambo gani hata Mwenyezi Mungu Asiwaadhibu, na hali ya kuwa wanawazuilia watu Msikiti Mtakatifu? Wala wao hawakuwa ndio walenzi wake, bali walenzi wake hawakuwa ispokuwa wachamungu tu. Lakini wengi katika wao hawajui".

35. "Na haikuwa ibada yao kwenye hiyo Nyumba (Al Ka'bah) ila ni kupiga miluzi na

makofi. Basi onjeni adhabu kwa vile mliyokuwa mkikufuru".

**Washirikina Wanastahiki Adhabu ya Allah تعالى Baada ya Ufedhuli Wao.**

Allah تعالى Anaeleza kuwa Washirikina wanastahiki Kuadhibiwa, lakini Yeye Hakufanya hivyo, kwa sababu ya heshima ya Mtume ﷺ akiishi pamoja nao. Kwa minajili hiyo, alipoondoka kwao, Allah تعالى Aliwapelekea adhabu Yake katika siku ya Badr. Wakuu wao wakauawa na wengine wakatekwa. Allah تعالى Akawapa uongozi wa kufanya maghufira ya dhambi ya shirki na ufisadi. Lau si baadhi ya Waislamu waliodho ofishwa, waliokuwa wakiishi nao Makkah ambao walikuwa wakifanya maghufira, Washirikina wangepatwa na adhabu isiozuiwa. Lakini Allah تعالى Aliwaondolea kwa sababu hiyo. Sawa na Kauli ya Allah تعالى katika siku ya Hundaybiyah:

هُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَأَنتُمْ مَعَكُوا أَن يَبْلُغَ مِجْلَدٌ  
وَلَوْلَا رِجَالٌ مُّؤْمِنُونَ وَنِسَاءٌ مُّؤْمِنَاتٌ لَّمَّ تَعَلَّمُوهُمْ أَن تَطَّوَّهُمْ فَنِتَّصِبْكُمْ مِنْهُمْ مَعَرَّةٌ  
بِغَيْرِ عِلْمٍ ۖ لِيُدْخِلَ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ مَن يَشَاءُ ۗ لَوْ تَزَيَّلُوا لَعَذَّبْنَا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ  
عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٤٥﴾

**“Hao ndio waliokufuru na wakakuzieni msiingie Msikiti Mtakatifu, na wakawazuilia wanyama kufika mahala pao. Na lau si wanaume Waumini na wanawake Waumini msiowajua mkawasaga na mkaingia makosani kutokana nao bila ya kujua. Mwenyezi Mungu (Amefanya haya) ili Amuingize Amtakaye katika Rehema Yake. Lau wangelitengana bila ya shaka Tungeliwaadhibu waliokufuru kwa adhabu chungu”. (48:25)**

Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا لَهُمْ آلَا يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ وَهُمْ يَصُدُّونَ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ ۗ إِنْ  
أَوْلِيَاؤُهُمْ إِلَّا الْمُنَافِقُونَ وَلَٰكِن أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٦﴾

**“Lakini wana jambo gani hata Mwenyezi Mungu Asiwaadhibu, na hali ya kuwa wanawazuilia watu Msikiti Mtakatifu? Wala wao hawakuwa ndio walinzi wake, bali walinzi wake hawakuwa isipokuwa wachamungu tu. Lakini wengi katika wao hawajui”.**

Maana: kwa vipi Allah تعالى Asiwaadhibu ilhali wao wanazuia watu wasije Masjid Al-Haram. Maana, msikiti ambao uko Makkah, kwa kuwazuia wanaostahiki, ambao ni Waislamu wasisali ndani yake wala wasitufu.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ ۖ إِنَّ أَوْلِيَاءَهُ إِلَّا الْمُتَّقُونَ

**“Wala wao hawakuwa ndio walinzi wake, bali walinzi wake hawakuwa isipokuwa wachamungu tu”.**

Aya ina maana ya, wao si wanaoustahiki Al-Masjid Al-Haram, kwani wenye haki nao ni Mtume ﷺ na Masahaba wake.

Sawa na Kauli ya Allah تعالى,

مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ بِالْكَفْرِ ۚ أُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَلُهُمْ فِي النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ ﴿١٧﴾ إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ  
الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الزَّكَاةَ وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ ۚ فَعَسَىٰ أُولَٰئِكَ أَنْ يَكُونُوا مِنَ  
الْمُهْتَدِينَ ﴿١٨﴾

**“Haiwi kuwa makafiri ndio waimarisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudishia wenyewe ukafiri. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika, na katika Moto watadumu. Hakika wanaoimarisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanao muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na wakashika Sala, na wakatoa Zakah na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu. Basi huenda hao wakawa katika waongofu”.** (9:17-18) Na,

وَصَدَّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفِّرْ بِهِ ۖ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجِ أَهْلِهِ مِنْهُ أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ

**“Lakini kuzuilia watu wasiende katika njia ya Mwenyezi Mungu na kumkanusha Yeye, na kuzuilia watu wasiende kwenye Msikiti Mtakatifu na kuwatoa watu wake humo, ni makubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu...”.** (2:217)

Al-Hakim alinukuu ndani ya kitabu chake *Al-Mustadrak* kutoka kwa Rifa'ah kwamba alisema: "Mtume ﷺ aliwakusanya Makuraish, akasema: "Je, baina yenu yupo asiyekuwa miongoni mwenu?" Wakasema, "Kati yetu kuna mtoto wa dada, kuna aliyeungana na sisi na kuna bwana mkubwa wetu". Mtume ﷺ Akasema, "Aliyeungana nasi ni katika sisi, mtoto wa dada yetu ni katika sisi na bwana mkubwa wetu ni katika sisi. Kwa hakika! Marafiki zangu ni wacha-Mungu". Kisha akasema, "Hadithi hii ni Sahih lakini hawakuinukuu Bukhari na Muslim"<sup>1</sup>. 'Urwah, As-Suddi na Muhammad bin Is-haq walisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ أَوْلِيَاءَهُمْ إِلَّا الْمُتَّقُونَ

**"...bali walinzi wake hawakuwa isipokuwa wachamungu tu".**

Kwamba: "Hao ni Muhammad ﷺ na Masahaba wake رضي الله عنهم". Mujahid alisema: "Hao ni *Mujahiduna* (katika njia ya Allah تعالى), wowote wawavyo, na popote walipo". Kisha Allah تعالى Alitaja waliyokuwa wakitegemea na kufanya Washirikina, katika *Al-Masjid Al-Haram*,

وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِنْدَ الْبَيْتِ إِلَّا مُكَاءً وَتَصَدِيَةً

**"Na haikuwa ibada yao kwenye hiyo Nyumba (Al Ka'bah) ila ni kupiga miluzi na makofi".**

Abdullah bin 'Amr, Ibn 'Abbas, Mujahid, 'Ikrimah, Sa'id bin Jubayr, Abu Raja Al-Utwaridiy, Muhammad bin Ka'b Al-Kuradhi, Hujr bin 'Anbasi, Nubaytw bin Shuaritw, Qatadah na 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam رضي الله عنهم walisema: "Ni miluzi"<sup>2</sup>. Mujahid aliongeza, "Na walikuwa wakiingiza vidole vyao vinywani mwao"<sup>3</sup>. Sa'id bin Jubayr na Ibn 'Abbas walizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِنْدَ الْبَيْتِ إِلَّا مُكَاءً وَتَصَدِيَةً

**"Na haikuwa ibada yao kwenye hiyo Nyumba (Al Ka'bah) ila ni kupiga miluzi na makofi".**

<sup>1</sup> Al-Hakim 2:328.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:522,526.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:525.

Kwamba, “Makuraishi walikuwa wakiitufu Ka’bah wakiwa uchi, wakipiga miluzi na kupiga makofi. Neno *Mu’ka-a* lina maana ya kupiga mbinja, na neno *At-Tasdiyah* ni kupiga makofi. Hivi ndivyo pia alivyosimulia ‘Ali bin Abu Twalhah na Al-Awfi kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما. Kadhalika ndivyo, alivyosimulia kutoka kwa Ibn Umar, Mujahid, Muhammad bin Ka’b, Abu Salamah bin ‘Abbas na Ibn ‘Abza. Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِنْدَ الْبَيْتِ إِلَّا مُكَاءً وَتَصَدِيَةً

**“Na haikuwa ibada yao kwenye hiyo Nyumba (Al Ka’bah) ila ni kupiga miluzi na makofi”.**

Kwamba, “*Al-Muka-a* ni kupiga mbinja, na *At-Tasdiyah* ni kupiga makofi”. Naye Sa’id bin Jubayr na ‘Abdur-Rahman bin Zayd walisema kuwa,

وَتَصَدِيَةً

“...*wa t-Tasdiyah*” Maana yake: “Walizuia watu njia ya Allah تعالى<sup>1</sup>. Kauli ya Allah تعالى,

فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٦﴾

**“Basi onjeni adhabu kwa vile mlivyokuwa mkikufuru”.**

Alisema Adh-Dhahaak, Ibn Jurayj na Ibn Is-haq: “Adhabu iliyowapata ni vifo na kutekwa kulikowasibu katika siku ya Badr”<sup>2</sup>.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ لِيَصُدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ۖ فَسَيُنْفِقُونَهَا ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ مُخْشَرُونَ ﴿٣٦﴾ لِيَمِيزَ اللَّهُ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ وَيَجْعَلَ الْخَبِيثَ بَعْضُهُ عَلَىٰ بَعْضٍ فَيَرْكُمَهُ جَمِيعًا فَيَجْعَلُهُ فِي جَهَنَّمَ ۗ أُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٣٧﴾

**36. “Hakika waliokufuru hutoa mali yao ili kuzuilia njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watazitoa mali zao, kisha yatakuwa juu**

<sup>1</sup> At-Tabari 13:527.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:528.

***yao majuto, na kisha watashindwa. Na wale waliokufuru watakusanywa kwenye Jahannam”.***

***37. “Ili Mwenyezi Mungu Apate kuwapambanua walio waovu na walio wema, na Kuwaweka waovu juu ya waovu wengine, na Kuwarundika wote pamoja, na Kuwatupa katika Jahannam. Hao ndio waliokhasirika”.***

### **Makafiri Kutoa Mali Zao kwa Ajili ya Kuzuia Dini ya Allah ﷻ ni Majuto Juu Yao**

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, Az-Zuhri, Muhammad bin Yahya bin Hibban, ‘Asim bin ‘Umar bin Qatadah na Huswain bin Abdur-Rahman bin ‘Amri bin Sa’id bin Mu’adh walisema, “Makuraishi walipata kipigo katika Badr, jeshi lao likarejea Makkah, na akarejea Abu Sufyan na msafara wake pamoja nao. Ndipo wakati ambapo ‘Abdullah bin Abu Rabi’ah, ‘Ikrimah bin Abu Jahl, Swafan bin Umayyah na baadhi ya watu wa Kikuraish, ambao baba zao, watoto wao na Ndugu zao waliouawa katika Badr walikwenda kwa Abu Sufyan bin Harb. Wakamuambia yeye, pamoja na Makuraishi waliokuwa naye katika msafara ule wa kibiashara, “Enyi kundi la Makuraishi! Muhammad amekupeni huzuni, na amewaua wabora wenu, basi tupeni msaada wa mali ili tumpige vita, huenda tukalipiza kisasi cha waliouawa miongoni mwetu”. Wakakubali kufanya hivyo. Basi, kwa mujibu wa Ibn Abbas رضي الله عنهما, Allah تعالى Akateremsha Aya hii,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ

***“Hakika waliokufuru hutoa mali yao...”***. Mpaka katika Kauli Yake,

هُمُ الْخٰسِرُونَ ﴿٦٧﴾

***“Hao ndio waliokhasirika”***. Na hivyo ndivyo alivyosimulia Mujahid Sa’id bin Jubayr, Al-Hakam bin ‘Uyaynah, Qatadah, As-Suddi na Ibn Abza, kwamba iliteremshwa Aya hii ya kumpiga Mtume ﷺ<sup>2</sup>. Adh-Dhahhak alisema: “Iliteremshwa Aya hii kuhusu Washirikina katika Badr”<sup>3</sup>. Kwa vyovyote itakavyokadiriwa, Ayah hiyo ni ya ujumla, hata kama ilikuwepo sababu mahsusi ya kuteremshwa kwake. Allah تعالى Amekwishaeleza kwamba makafiri hutoa

<sup>1</sup> At-Tabari 13:527.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:527.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:527.



mali zao ili wazuie kufuatwa kwa njia ya kweli. Basi watafanya hayo na mali zao kupotea, kisha majuto yatakuwa juu yao, kwa kutopata kwao ushindi, kwani makusudio yao yalikuwa ni kuizima nuru ya Allah تعالى na kutaka kulifanya neno lao kulishinda Neno la kweli, ilhali, Allah تعالى ni Mwenye Kuitimiza nuru Yake, hata kama makafiri watachukia. Na Atainusuru Dini Yake, Atalitangaza Neno Lake na Ataifanya Dini Yake ishinde Dini nyingine zote. Huu ndio udhalili wao duniani, na Akhera wana adhabu ya Moto. Atakayeishi zaidi miongoni mwao, basi ataona kwa macho yake na kusikia kwa masikio yake mambo yatakayomtia huzuni, na atakayeua au kufariki kati yao, basi ataelekea katika fedheha ya milele na adhabu ya kuendelea kwa mfululizo, bila kukoma. Kwa ajili hii Allah تعالى Alisema,

فَسَيُنْفِقُونَهَا ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ<sup>١</sup> وَالَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ

مُحْشَرُونَ ﴿٣٤﴾

**“Basi watazitoa mali zao, kisha yatakuwa juu yao majuto, na kisha watashindwa. Na wale waliokufuru watakusanywa kwenye Jahannam”. Allah تعالى Anasema,**

لِيَمِيزَ اللَّهُ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ

**“...Ili Mwenyezi Mungu Apate Kuwapambanua walio waovu na walio wema...”.**

Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli hii ya Allah تعالى, kuwa ina maana ya, “Atawapambanua watu wema na watu waovu”<sup>1</sup>. Na ili Awapambanue Wanaomtii kwa Kuwapiga maadui zake, makafiri, au wale wanaomuasi juu ya hilo kwa kujizuia kufanya hivyo. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ<sup>٢</sup> وَمَا كَانَ اللَّهُ

لِيُطْلِعَكُمْ عَلَى الْغَيْبِ

**“Haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwaacha Waumini katika hali mliyo mpaka Apambanue wabaya na wema. Wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kukujulisheni mambo ya ghaibu...” (3:179)**

<sup>1</sup> At-Tabari 13:534.

Na Kauli Yake,

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُدْخَلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾

**“Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu Hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana Jihadi, na Hajawapambanua waliosubiri? ”. (3:142)**

Kwa hivyo, Aya (8:37) inamaanisha: “Tulikufanyieni mtihani wa makafiri kwa kukupigeni na Tukawawezesha kutumia mali yao na kuitoa katika jambo hilo”.

لِيَجْزِيَ اللَّهُ الَّذِينَ مِنَ الطَّيِّبِ وَيَجْعَلَ الْخَبِيثَ بَعْضُهُ عَلَىٰ بَعْضٍ قَتْرُكُمْ

**“...Ili Mwenyezi Mungu Apate kuwa pambanua walio waovu na walio wema na Kuwaweka waovu juu ya waovu wengine, na Kuwarundika...”.**

Kwa maana: Kuwakusanya.

فَيَجْعَلُهُمْ فِي جَهَنَّمَ أُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٤٣﴾

**“...na Kuwatupa katika Jahannam. Hao ndio waliokhasirika”.**

Kwa maana: Hao ndio wenye khasara duniani na Akhera.

قُلْ لِلَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ يَنْتَهُوا يُغْفَرْ لَهُمْ مَا قَدْ سَلَفَ وَإِنْ يَعُودُوا فَقَدْ مَضَتْ سُنَّتُ

الْأُولَئِينَ ﴿١٤٤﴾ وَقَتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ كُلَّهُ لِلَّهِ فَإِنِ

أَنْتَهُوا فَإِزْبَ اللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١٤٥﴾ وَإِن تَوَلَّوْا فَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَوْلَانَكُمْ نِعَمَ

الْمَوْلَىٰ وَنِعَمَ النَّصِيرِ ﴿١٤٦﴾

**38. “Waambie wale waliokufuru: Wakikoma watasamehewa yaliyokwisha pita. Na wakiyarudia basi imekwishapita mifano ya watu wa zamani”.**

**39. “Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu Anayaona wanayoyatenda”.**

**40. “Na kama wakigeuka basi Jueni kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye Mola Mwema na Msaidizi Mwema”.**

## Kuwashajiisha Makafiri Wafanye Toba na Kuwaonya Dhidi ya Kuendelea na Ukafiri Wao.

Allah تعالیٰ Anamuambia Nabii Wake, Muhammad ﷺ,

قُلْ لِلَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ يَنْتَهُوا

**“Waambie wale waliokufuru: Wakikoma...”** Kwa maana: Kwa kuacha kufuru waliyonayo, ukinzani na ukaidi na kisha wakaingia katika Uislamu, kwa kufanya twaa na kuleta toba,

يُغْفَرَ لَهُمْ مَا قَدْ سَلَفَ

**“...watasamehewa yaliyokwisha pita”.** Watasamehewa kwa kufuru yao, madhambi na makosa yao. Sawa na Hadithi ya Abu Waa-il iliyonukuliwa katika *Sahih* kwamba Ibn Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ أَحْسَنَ فِي الْإِسْلَامِ لَمْ يُؤَاخِذْ بِمَا عَمِلَ فِي الْجَاهِلِيَّةِ، وَمَنْ أَسَاءَ فِي الْإِسْلَامِ أُخِذَ بِالْأَوَّلِ وَالْآخِرِ»

*“Mwenye kuwa mwema ndani ya Uislamu, hataadhibiwa kwa aliyo yatenda wakati wa ujahili. Na mwenye kuwa muovu ndani ya Uislamu, ataadhibiwa kwa ya hapo awali na yajayo”<sup>1</sup>.*

Katika *Sahih* kuna Hadithi nyingine, kwamba Mtume ﷺ alisema,

«الْإِسْلَامُ يَجُوبُ مَا قَبْلَهُ وَالتَّوْبَةُ تَجُوبُ مَا كَانَ قَبْلَهَا»

*“Kuingia katika Uislamu kunayafuta ya kabla yake na toba nayo huyafuta ya kabla yake”<sup>2</sup>.*

Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَإِنْ يَعُودُوا

**“Na wakiyarudia”.** Kwa maana: Wakiendelea na yale ambayo wao wamo ndani yake.

فَقَدْ مَضَتْ سُنَّتُ الْأَوَّلِينَ ﴿٣٨﴾

**“...basi imekwishapita mifano ya watu wa zamani”. (8:38)**

Maana yake: Imekwishapita mifano Yetu kwa wale watu wa zamani, kwamba wao walikuwa wanapokadhibisha na wakiendelea na ukaidi wao, basi Sisi Huwaharakishia adhabu na mateso.

<sup>1</sup> *Fat’hul Al-Bari* 12:227.

<sup>2</sup> Muslim 121 na Ahmad 4:205.

## Amri ya Kupigana kwa Ajili ya Kuumaliza Ushirikina na Ukafiri

Allah تعالى Anasema,

وَقَتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةً وَيَكُونَ الدِّينُ كُلَّهُ لِلَّهِ

**“Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna na mateso, na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu...”**

Bukhari alinukuu kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما kuwa mtu mmoja alikuja na kusema, “Ewe Abu ‘Abdur-Rahman! Kwanini huyafanyi Aliyoyataja Allah?”

وَإِنْ طَائِفَتَانِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ اقْتَتَلُوا

**“...Na ikiwa makundi mawili katika Waumini yanapigana...” (49:9)**

Basi ni nini kinachokuzuia kupigana wakati Allah تعالى Alishataja katika Kitabu Chake? Makundi mawili yanapopigana?, Akasema Ibn Umar رضي الله عنهما, “Ewe mwanawe Ndugu yangu! Kuacha kwangu kupigana kisha nikaabishwa kwa kusomewa Aya hiyo ni bora kwangu kuliko kupigana kisha nikaabishwa kwa kusomewa Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُتَعَمِدًا

**“Na mwenye kumuua Muumini kwa kukusudia...” (4:93)**

Mpaka mwisho wa Aya, Alisema, Allah تعالى Anasema,

وَقَتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةً

**“Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna...”**

Ibn Umar رضي الله عنهما akasema, “Tulishafanya hivyo wakati wa uhai wa Mtume ﷺ, wakati Uislamu ulipokuwa dhaifu, na mtu aliweza kupatiwa mtihani katika Dini yake, ama makafiri walimuua ama walimfunga. Mpaka Uislamu ukaenea, kukawa hakuna *Fitnah* tena”. Mtu yule Alipoona kwamba Ibn ‘Umar رضي الله عنهما haafikiani naye, alimuuliza, “Ni nini kauli yako juu ya Ali na ‘Uthman.” Ibn Umar رضي الله عنهما akasema: “Ama Uthman رضي الله عنه alikwisha samehewa na Allah تعالى, lakini nyinyi mkachukizwa na hilo, na ama Ali رضي الله عنه ni mwana wa ami wa Mtume ﷺ na mkwe wake”, na akaashiria kwa mkono wake huku akisema, “Na yule mnayemuona pale ni binti yake”<sup>1</sup>. Sa’id bin Jubayr alisema,

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:160.

Ibn 'Umar رضي الله عنهما alitujia na kusema, "Mnaonaje kuhusu kupigana wakati wa *Fitnah*?" Akauliza tena, "Na mnaijua *Fitnah* ni nini? Mtume Muhammad ﷺ alikuwa akiwapiga Washirikina, na kuingia katika maeneo yao ilikuwa ni *Fitnah* (mtihani katika Dini). Hakukuwepo mapigano kama yenu ya kugombania ukubwa"<sup>1</sup>. Masimulizi yote haya yalinukuliwa na Bukhari. Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema juu ya Aya,

وَقَتِلُوهُمْ حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةً

**"Na piganeni nao mpaka isiwepo fitna"**. Maana yake ni: "Usiwepo ushirikina"<sup>2</sup>. Kadhalika wamesema hivyo, Abu Al-'Aliyyah, Mujahid, Al-Hasan, Qatadah, Ar-Rabi' bin Anas, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan na Zayd bin Aslam. Muhammad bin Is-haq alisema, "Ilinifikia khabari kutoka kwa Az-Zuhri, kutoka kwa 'Urwah bin Az-Zubayr رضي الله عنه Maulamaa wetu wengine kuwa Aya,

حَتَّى لَا تَكُونَ فِتْنَةً

**"...mpaka isiwepo fitna"**. Tafsiri yake ni mpaka Muislamu asifanyiwe *Fitnah* dhidi ya Dini yake<sup>3</sup>. Allah تعالى Amesema,

وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

**"...na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu"**. Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Aya hii kwa kusema, "Tawhid ifanywe kwa Ikhlasu kwa ajili ya Allah تعالى" Alisema Al-Hasan, Qatadah na Ibn Jurayj kuhusu Aya,

وَيَكُونَ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

**"...na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu"**.

Ili itamkwe *Laa ilaaha illallah*<sup>4</sup>. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema Tawhid iwe ni kwa ikhlasi ya Allah تعالى, kusiwe na ushirikina ndani yake na kuwepo kuwaacha miola ghairi Yake"<sup>5</sup>. 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema,

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:160.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:538.

<sup>3</sup> Ibn Abu Hatim 5:1701.

<sup>4</sup> At-Tabari 13:538-539.

<sup>5</sup> Ibn Hishaam 2:327.

وَيَكُونُ الدِّينُ كُلُّهُ لِلَّهِ

**“...na Dini yote iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu”.**

“Na ukafiri hauwezi kuishi pamoja na Dini yenu”<sup>1</sup>. Ushahidi wa hili, ni Hadithi iliyothibiti katika *Sahih Mbili* kwamba Mtume ﷺ alisema,

«أَمِرْتُ أَنْ أَقَاتِلَ النَّاسَ، حَتَّى يَقُولُوا: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، فَإِذَا قَالُوا مَا عَصَمُوا مِنِّي دِمَاءَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ، إِلَّا بِحَقِّهَا، وَحَسَابُهُمْ عَلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

*“Nimeamrisha nipigane dhidi ya watu, mpaka waseme, “Hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالی”. Wakishayasema hayo, watakuwa wameihifadhi damu na mali zao dhidi yangu, isipokuwa kwa haki zake (Sharia ya Kiislamu). Na hesabu yao ni juu ya Allah تعالی.”*<sup>2</sup>

Pia, katika *Sahih Mbili*, kuna Hadithi ya Abu Musa Al-Ash’ari رضي الله عنه kuwa, Mtume ﷺ aliulizwa juu ya mtu aliyepigana kwa sababu ya kusifiwa kuwa ni shujaa, au kwa ajili ya ukabila au kwa ria, ni nani kati yao aliye katika njia ya Allah?” Akasema,

«مَنْ قَاتَلَ لِتَكُونَ كَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا فَمُو فِي سَبِيلِ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

*“Mwenye kupigana ili Neno la Allah تعالی liwe juu, atakuwa yuko katika njia ya Allah تعالی”*<sup>3</sup>.

Allah تعالی Amesema,

فَإِنِ أَنْتَهُوَ

**“Lakini wakiacha.”**

Kwa maana: Kuwapigeni kwa kuulinda ukafiri wao basi acheni kuwapiga hata kama hamujui undani wao.

<sup>1</sup> At-Tabari 13:539.

<sup>2</sup> *Fat’hul Al-Bari* 1:95 na Muslim 1:53.

<sup>3</sup> Al-Bukhari 123, 2810, 3126 na 7458.

فَارَبَّ اللَّهِ بِمَا يَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٣٤﴾

**“..basi hakika Mwenyezi Mungu Anayaona wanayoyatenda.”**

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣٥﴾

**“Lakini wakitubu, wakashika Sala, na wakatoa Zakah, basi waachilieni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”. (9:5)**

Na katika Aya nyingine،

فَأِحْوَأْنُكُمْ فِي الدِّينِ

**“...basi ni Ndugu zenu katika Dini...”. (9:11)**

Na Amesema،

وَقَتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ الدِّينُ لِلَّهِ فَإِنْ أَبَتْهُوَ فَلَا عُدْوَانَ إِلَّا عَلَى الظَّالِمِينَ ﴿١٩٣﴾

**“Na Piganeni nao mpaka pasiwepo fitina, na Dini iwe ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha basi usiweko uadui ila kwa wenye kudhulumu”. (2:193)**

Katika Sahih imenukuliwa Mtume ﷺ alimuambia Usama رضي الله عنه، pindi alipomuendea mtu na upanga wake. Mtu huyu akasema, *Laa ilaaha illallah*, Usama رضي الله عنه akampiga na kumuua. Taarifa hiyo ikatolewa kwa Mtume ﷺ naye akamuambia Usamah رضي الله عنه،

«أَفْتَلَنَّهُ بَعْدَ مَا قَالِ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ؟ وَكَيْفَ تَصْنَعُ بِلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ؟»

**“Ulimuua baada ya yeye kusema, “Laa ilaaha illallah (Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى)”? Utaifanya nini Laa ilaaha illallah Siku ya Kiyama?”**

Akasema, “Ewe Mtume! Aliyasema hayo kwa kujikinga tu”. Akasema Mtume

ﷺ:

«هَلَّا شَقَقْتُ عَنْ قَلْبِهِ؟»

**“Je, Uliupasua moyo wake?”**

Akaendelea kumkariria,

«مَنْ لَكَ بِلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ؟»

*“Utaifanya nini Laa ilaaha illallah Siku ya Kiyama?”*

Usamah رضي الله عنه alisema, “Mpaka nikatamani kwamba ningelikuwa sijasilimu ila siku hiyo”<sup>1</sup>

وَإِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَوْلَانَكُمْ نِعَمَ الْمَوْتَىٰ وَنِعَمَ النَّصِيرِ ﴿٣٤﴾

***“Na kama wakigeuka basi Jueni kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye Mola wenu, ni Mola Mwema na Msaidizi Mwema”.***

Kwa maana: Wakiendelea na kukhalifu kwao na kukupigeni vita, basi mtambue kwamba Allah تعالى ni Mlinzi wenu na Bwana wenu, wa Kukusaidieni dhidi ya maadui wenu. Naam, kwa hakika Yeye ni Mlinzi na Msaidizi Bora.

\* \* \*

<sup>1</sup>Muslim 1:96.



\* وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّن شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ  
 وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَآبِئِ السَّبِيلِ إِن  
 كُنْتُمْ ءَامَنْتُمْ بِاللَّهِ وَمَا أُنزَلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ  
 اتَّخَذَ الْجَمْعَانِ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤١﴾ إِذْ  
 أَنْتُمْ بِالْعُدْوَةِ الدُّنْيَا وَهُمْ بِالْعُدْوَةِ الْقُصْوَىٰ وَالرَّكْبُ  
 أَسْفَلَ مِنْكُمْ ۗ وَلَوْ تَوَاعَدْتُمْ لِاخْتَلَفْتُمْ فِي الْمِيعَادِ  
 وَلَكِنَّ لَيَقْضَىٰ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا لِيَهْلِكَ مَن  
 هَلَكَ عَن بَيِّنَةٍ وَيَحْيَىٰ مَن حَىٰ عَن بَيِّنَةٍ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ  
 لَسَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٤٢﴾ إِذْ يُرِيكُهُمُ اللَّهُ فِي مَنَايِكَ قَلِيلًا ۖ وَلَوْ  
 أَرَادْتَهُمْ كَثِيرًا لَّفَشَلْتُمْ وَلَتَنزَعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَلَكِنَّ  
 اللَّهَ سَلَّمَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٤٣﴾ وَإِذْ يُرِيكُمُوهُمْ  
 إِذْ اتَّقَيْتُمْ فِي أَعْيُنِكُمْ قَلِيلًا وَيُقَلِّلُكُمْ فِي أَعْيُنِهِمْ  
 لِيَقْضَىٰ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ  
 الْأُمُورُ ﴿٤٤﴾

\* وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّن شَيْءٍ  
 فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي  
 الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينِ وَآبِئِ  
 السَّبِيلِ إِن كُنْتُمْ ءَامَنْتُمْ بِاللَّهِ وَمَا  
 أُنزَلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ  
 اتَّخَذَ الْجَمْعَانِ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ  
 شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤١﴾

41. "Na Jueni ya Kwamba  
 ngawira mnayoipata, basi  
 khums (sehemu moja  
 katika tano) ni kwa ajili ya  
 Mwenyezi Mungu na  
 Mtume, na jamaa, na  
 mayatima, na masikini, na  
 wasafiri, ikiwa nyinyi  
 mmemuamini Mwenyezi  
 Mungu na Tuliyoa-  
 teremsha kwa mja Wetu  
 siku ya kipambanuo, siku

yalipo kutana majeshi mawili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu".

### Hukumu ya Ngawira au "Ghanima na Fai.

Allah تعالى Anabainisha ufafanuzi wa Aliyoyaruhusu, hususan kwa ajili ya ummah huu mtukufu kinyume na ummah nyingine zote zilizotangulia kuhusu kuhalalishwa kwa Ngawira "Ghanima". Ngawira au Ghanima ni mali iliyochukuliwa kutoka kwa makafiri, kwa njia za kivita. Faini mali zilizochukuliwa kutoka kwa makafiri bila mapigano, kama vile mali ambazo zinapatikana kwa njia ya kusuluhishana kwa amani, au wanaokufa na kuziacha mali bila kuwepo

warithi, *Jizyah* (kodi ya nchi), *Kharaaj* (kodi ya mali) na mfano wa hivyo. Kauli ya Allah تعالى،

﴿ وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّن شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسُهُ ﴾

**“Na Jueni ya kwamba ngawira mnayoipata, basi khums (sehemu moja katika tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu...”**

Ni katika kutilia mkazo juu ya *Khums* kwa kila kichache na kingi hata sindano ya uzi. Allah تعالى Alisema,

﴿ وَمَن يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ثُمَّ تُوَفَّى كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦١﴾ ﴾

**“Na atakayefanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyo yafanyia khiyana, kisha kila mtu atalipwa kwa aliyo yachuma, kwa ukamilifu, wala hawatadhumiwa”. (3:161) Na Kauli ya Allah,**

﴿ وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّن شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسُهُ وَلِلرَّسُولِ ﴾

**“...basi khums (sehemu moja katika tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume”.**

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, Mtume ﷺ alipowatuma askari na wakapata ngawira, aliigawa katika mafungu matano na kuichukua *khums* ambayo aliigawa tena katika mafungu matano, kisha alisoma,

﴿ وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِّن شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسُهُ ﴾

**“Na Jueni ya Kwamba ngawira mnayoipata, basi khums (sehemu moja katika tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ...”.**

Alisema, na Kauli ya Allah تعالى،

﴿ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسُهُ ﴾

**“...basi khums (sehemu moja katika tano) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu”.**

Ufunguzi wa Maneno ya Allah تعالى،

﴿ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ﴾

**“Viliomo mbinguni na viliomo duniani ni vya Mwenyezi Mungu”. (2:284)**

“Hivyo Akajaalia fungu la Allah تعالى na la Mtume ﷺ kuwa ni moja”<sup>1</sup>. Na hivi ndivyo alivyosema Ibrahim An-Nakha’, Al-Hasan bin Muhammad Ibn Al-Hanafiyyah, Al-Hasan Al-Basri, Ash-Sha’bi, ‘Ata bin Abu Rabaah, ‘Abdullah bin Buraydah, Qatadah, Mughirah na wengine, ‘kwamba fungu la Allah تعالى na Mtume Wake ni moja”<sup>2</sup>. Haya yanapewa nguvu na Hadithi iliyonukuliwa na Imamu Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bayhaqi, kwa isnadi *Sahih*, kutoka kwa ‘Abdullah bin Shaiq kuwa mtu mmoja (kutoka Balqan) alisema, “Nilimjia Nabii na kumkuta akiwa katika Jangwa la *Wadi Al-Qura* akimkagua farasi”. Nikamuuliza, “Ewe Mtume ﷺ! Unasemaje kuhusu ghanima?” Naye akanijibu,

«لِلَّهِ خُمُسُهَا وَأَرْبَعَةُ أَخْمَاسِهَا لِلْجَيْشِ»

“Fungu la Allah تعالى ni khums moja, na khums nne ni za jeshi”.

Nikamuuliza, “Hapana yeyote aliye na haki nayo zaidi ya mwingine?” akanijibu,

«لَا، وَلَا السَّهْمُ تَسْتَخْرِجُهُ مِنْ جَنِّبِكَ لَيْسَ أَنْتَ أَحَقُّ بِهِ مِنْ أَخِيكَ الْمُسْلِمِ»

“Hapana, hata kama ni mshale unaoutoa kutokea mbavuni mwako, huna haki zaidi ya nduguyo Muislamu”<sup>3</sup>.

Imamu Ahmad alimnukuu Miqdan bin Ma’dikarib Al-Kindi kwamba alikaa pamoja na ‘Ubadah bin As-Swamit, Abu Ad-Darda’a na Al-Harith bin Mu’awiyah Al-Kindi رضي الله عنهم, wakakumbushana Hadithi ya Mtume ﷺ. Abu Ad-Dardai رضي الله عنه alimuambia ‘Ubadah رضي الله عنه, “Ewe ‘Ubadah! Nini maana ya maneno ya Mtume ﷺ katika vita kadha wa kadha kuhusu jambo la sehemu ya moja ya tano “*Akhmas*” (wingi wa neno *khums*)?” ‘Ubadah رضي الله عنه alisema kumuambia, “Mtume ﷺ aliwasalisha katika vita hali wakiwepo ngamia waliopatikana kwa njia ya ngawira. Alipotoa salamu (kumaliza Sala) alisimama na akashika manyoya ya ngozi ya ngamia (ikiwa bado na manyoya), kwa vidole vyake, na akasema:

«إِنَّ هَذِهِ مِنْ غَنَائِمِكُمْ وَإِنَّهُ لَيْسَ لِي فِيهَا إِلَّا نَصِيبِي مَعَكُمْ إِلَّا الْخُمْسُ، وَالْخُمْسُ مَرْدُودٌ عَلَيْكُمْ، فَأَذُوا الْخَيْطَ وَالْمَخِيطَ، وَأَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ وَأَضْفَرَ، وَلَا تَغْلُوا فَإِنَّ الْعُلُولَ نَارٌ وَعَارٌ عَلَى أَصْحَابِهِ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَجَاهِدُوا النَّاسَ فِي اللَّهِ الْقَرِيبِ»

<sup>1</sup> At-Tabari 13:549.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:450, 548.

<sup>3</sup> Al-Bayhaqi 6:324.

وَالْبَعِيدَ، وَلَا تَبَالُوا فِي اللَّهِ لَوْمَةً لَّائِمَةً، وَأَقِيمُوا حُدُودَ اللَّهِ فِي الْحَضَرِ وَالسَّفَرِ،  
وَجَاهِدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ، فَإِنَّ الْجِهَادَ بَابٌ مِنْ أَبْوَابِ الْجَنَّةِ عَظِيمٌ، يُنَجِّي بِهِ اللَّهُ مِنَ  
النَّهْمِ وَالْغَمِّ

*“Kwa hakika, haya manyoya ni miongoni mwa ghanima zenu. Nami sina fungu katika hao isipokuwa sehemu ya moja ya tano “khumusi”. Hata hiyo khumusi itarudishwa kwenu (kuonesha ihsani za Mtume ﷺ). Kwa hivyo, isalimisheni hata nguo na uzi, na kilicho kikubwa au kidogo zaidi yake (kutoka katika ngawira). Wala Msifanye ulaghai, kwani ulaghai ni moto na fedheha kwa watu hao duniani na Akhera. Fanyeni Jihadi dhidi ya watu hao na wa mbali. Wala msijali lawama za wenye kulaumu, maadamu mko katika njia ya Allah تعالى. Isimamieni Sharia ya Allah تعالى, mjini na safarini. Na mfanye Jihadi katika njia ya Allah تعالى kwani Jihadi ni lango kubwa la kuingia Jannah. Kupitia hiyo, Allah تعالى Huokoa kutoka katika huzuni na majonzi”<sup>1</sup>.*

Hadithi hii ni *Hasan*, na ni Adhimu, lakini sikuiona katika vitabu sita kwa njia hii. Lakini aliinukuu Imamu Ahmad pia, Abu Dawud na An-Nasai, kutokana na Hadithi ya ‘Amir bin Shua’bi, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake, ‘Abdullah bin ‘Amri رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ juu ya kisa cha *Khums* na kukatazwa ulaghai<sup>2</sup>. Pia alinukuu Abu Dawud na An-Nasai<sup>3</sup> kutoka kwa ‘Amri bin ‘Anbasa. Mtume ﷺ alikuwa na kitu katika ghanima alichokuwa akikichagua kwa ajili yake mwenyewe; ama atachagua mtumishi wa kiume au wa kike, farasi, upanga au kama hivyo. Kama alivyotarifu Muhammad bin Sirin, ‘Amir Ash-Sha’bi na Maulamaa wengi wameafikiana nao. Alinukuu Imamu Ahmad na At-Tirmidhi ambaye alisema kuwa ni hadithi *Hasan* kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما: Kwamba Mtume ﷺ aliuchagua upanga ulioitwa *Dhul-Fiqaar* katika siku ya Badr. Nao ndio ambao aliuona katika ndoto ya siku ya Uhud<sup>4</sup>. ‘Aishah رضي الله عنها alisema: ‘Swafiyyah رضي الله عنها alikuwa miongoni mwa wanawake waliotekwa.’ Abu Dawud alinukuu katika *Sunan* yake<sup>5</sup>. Ama kuhusu fungu la jamaa wa karibu wa Mtume ﷺ hilo hutolewa kwa Banu Hashim na Banu Al-Muttwalib, kwa sababu Banu Al-Muttalib waliwasaidia Banu Hashim tokea

<sup>1</sup> Ahmad 5:316. Isnadi yake ni dhaifu.

<sup>2</sup> Ahmad 2:184 na Abu Dawud 2694. (Tz.3:161).

<sup>3</sup> Abu Dawud 2755.

<sup>4</sup> Ahmad 1:271 na At-Tirmidhi 1561.

<sup>5</sup> Abu Dawud 2994.

zama za Ujahili na mwanzoni mwa Uislamu. Zaidi ya hayo, walishiriki katika vikwazo walivyowekewa Banu Hashim katika *Shiib* Abi Twalib (Bonde la Abi Twalib) kwa kuwa na uchungu na Mtume ﷺ na pia kumhami (pindi Makuraishi walipomuekea vikwazo kwa miaka mitatu). Waliokuwa Waislamu (kutoka kwa Banu Al-Muttwalib) waliyafanya haya kwa kumtii Allah تعالى na Mtume ﷺ, na waliokuwa makafiri katika wao walifanya hilo, kwa ajili ya kulisaidia kabila lao na kumtii Abu Twalib, Ami wa Mtume ﷺ. Allah تعالى Anasema,

وَأَلَيْتَنِي

**“...na mayatima...”.** Kwa maana: Mayatima wa Waislamu,

وَالْمَسْكِينِ

**“...na masikini...”.** Ni wahitaji ambao hawapati cha kuziba au kuondoa umasikini wao.

وَأَتَّبِعِ السَّبِيلِ

**“...na wasafiri...”** Huyo ni msafiri au mtu anayetaka kusafiri katika masafa ambayo Sala hufupishwa, na hana cha kukitumia katika safari yake hiyo. Tafsiri yake itaelezwa katika Aya ya masuala ya watu wanaostahiki kupewa Zaka (9:60), katika *Surat Baraa-a, In sha Allah*. Kutegemea na kutawakali kwetu ni Kwake Allah تعالى. Na Kauli ya Allah تعالى,

إِنْ كُنْتُمْ ءَامِنْتُمْ بِاللَّهِ وَمَا أُنزَلْنَا عَلَىٰ عَبْدِنَا

**“...ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu na Tuliyo yateremsha kwa mja Wetu...”.**

Kwa maana: Ifuateni Sharia Tuliyo kuwekeeni kuhusu sehemu ya 1/5 “*Khums*” katika ghanima, ikiwa mnamuamini Allah تعالى na Siku ya Mwisho. Pia muyafuate Aliyoyateremsha Allah تعالى kwa Mtume Wake ﷺ. Kwa ajili hii, ilinukuliwa katika *Sahihi Mbili*, Hadithi ya ‘Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنهما kuhusu ujumbe wa ‘Abdul-Qais kuwa Mtume ﷺ aliwaambia,

«وَأَمْرُكُمْ بِأَرْبَعٍ، وَأَنْتَهَاكُمْ عَنْ أَرْبَعٍ. أَمْرُكُمْ بِالْإِيمَانِ بِاللَّهِ ثُمَّ قَالَ: هَلْ تَدْرُونَ مَا  
الْإِيمَانُ بِاللَّهِ؟ شَهَادَةٌ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ، وَإِقَامُ الصَّلَاةِ  
وَإِيْتَاءُ الزُّكَاةِ، وَأَنْ تُؤَدُّوا الْخُمْسَ مِنَ الْمَغْنَمِ»

**“Ninakuamrisheni mambo manne, na ninakukatazeni mambo**

manne. Nakuamrisheni kumuamini Allah تعالى. “Je mnajua imani ya Allah تعالى ni nini?” Ni Kutoa Shahada kwamba hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى na kwamba Muhammad ﷺ ni Mtume, kusimamisha Sala, kutoa Zaka na kuzisalimisha khums kutoka katika ghanima”<sup>1</sup>.

Ilinukuliwa Hadithi hiyo kwa urefu wake.

Kwa hivyo, Mtume ﷺ aliorodhesha jambo la kutekeleza katika moja ya tano “Khums” kuwa ni katika Imani. Na Bukhari ameweka mlango maalumu juu ya Imani katika Sahihiyake, akasema, “Mlango: Kutoa Khums ni Sehemu ya Imani”. Kisha akasimulia Hadithi hii ya Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما. Kauli ya Allah تعالى,

يَوْمَ الْفُرْقَانِ يَوْمَ اتَّخَذَ الْجَمْعَانِ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٤١﴾

**“...siku ya kipambanuo, siku yalipokutana majeshi mawili. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu”**

Allah تعالى Anakumbusha neema na ihsani Yake kwa viumbe Wake, kwa kupambanua Kwake baina ya haki na batili siku ya Badr, na inaitwa *Al-Furqan*, kwa sababu Allah تعالى Aliinyanyua juu kalima ya Imani juu ya neno la batili na Akaipa ushindi Dini Yake na Akamnusuru Nabii Wake na kundi lake. Alisema ‘Ali bin Abu Twalhah, Al-‘Awfi kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa: “Yawmul-Furqan (Siku ya Upambanuzi) ni siku ya Badr, ambapo Allah تعالى Alionesha dhahiri tofauti baina ya Haki na Batili”<sup>2</sup>. Al-Hakim aliinukuu. Hivyo, na ndivyo alivyosema Mujahid, Miqsam, ‘Ubaydullah bin ‘Ubaidillah, Adh-Dhahhak, Qatadah, Muqatil bin Al-Hayyan na wengine kuwa ni siku ya Badr<sup>3</sup>.

إِذْ أَنْتُمْ بِالْعُدْوَةِ الدُّنْيَا وَهُمْ بِالْعُدْوَةِ الْقُصْوَىٰ وَالرَّكْبُ أَسْفَلَ مِنْكُمْ ؕ وَلَوْ تَوَاعَدْتُمْ لَا خْتَلَفْتُمْ فِي الْمِيعَادِ ۗ وَلَٰكِن لِّيَقْضِيَ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا لِّيَهْلِكَ مَنْ هَلَكَ عَنْ بَيِّنَةٍ وَيَحْيَىٰ مَنْ حَيَّ عَنْ بَيِّنَةٍ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَسَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٤٢﴾

**42. “Kumbukeni pale mlipokuwa nyinyi kwenye ng’ambo ya karibu ya bonde, na wao wakawa ng’ambo ya mbali na msafara ulipo kuwa chini yenu. Na ingelikuwa mmeagana mngelikhitilafiana**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 1:157 na Muslim 1:46.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:561.

<sup>3</sup> At-Tabari 13:561, 563.

***katika miadi. Lakini (mkakutana) ili Mwenyezi Mungu Atimize jambo lililokuwa lazima litendeke, kwa sababu aangamie wa kuangamia kwa dalili zilizo dhahiri, na asalimike wa kusalimika kwa dalili zilizo dhahiri. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua”.***

**Baadhi ya Maelezo Juu ya Vita vya Badr.**

Allah تعالیٰ Anaizungumzia *Yawm Al-Furqan* (Siku ya Badr),

إِذْ أَنْتُمْ بِالْعُدْوَةِ الدُّنْيَا

***“Kumbukeni pale mlipokuwa nyinyi kwenye ng’ambo ya karibu ya bonde”.***

Kwa maana: Pale mlipokuwa mkiweka kambi karibu kabisa na sehemu ya kuteremkia bonde linaloelekea Madinah.

وَهُمْ

***“...na wao”.*** Kwa maana: Washirikina wakiwa wameweka kambi.

بِالْعُدْوَةِ الْقُصْوَى

***“...ng’ambo ya mbali”.*** Kwa maana: Mbali na Madinah, katika upande wa kuelekea Makkah.

وَالرَّكْبِ

***“...na msafara...”.*** Kwa maana: Katika msafara wa biashara alimokuwemo Abu Sufyan.

أَسْفَلَ مِنْكُمْ

***“...chini yenu...”.*** Maana yake: Karibu kabisa na ukingo wa bahari.

وَلَوْ تَوَاعَدْتُمْ

***“...Na ingelikuwa mmeagana...”.***

Nyinyi na Washirikina kukutana mahali fulani,

لَا خْتَلَفْتُمْ فِي الْمِيعَادِ

***“...mngelikhitilafiana katika miadi...”.***

Muhammad bin Is-haqi رحمه الله تعالى alisema: “Yahya bin ‘Ibadi bin ‘Abdullah bin Az-Zubayr alinieleza kutoka kwa baba yake kuhusu Ayah hii kuwa, “Kama

mngelikuwa na miadi baina yenu na wao na ikakufikieni khabari ya wingi wa idadi yao na uchache wenu, msingelikutana nao,

وَلَيْكِن لِّيَقْضِيَ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا

**“...ili Mwenyezi Mungu Atimize jambo lililokuwa lazima litendeke...”.**

Maana yake: Ili Allah تعالی Atimize jambo Alilolihukumu katika Qadar Yake kuhusu Kuutukuza Uislamu na Waislamu, na Kuudhalilisha ushirikina na Washirikina, bila ya nyinyi kujua. Akayafanya hayo Atakavyo kwa Upole Wake<sup>1</sup>. Na katika Hadithi ya Ka'b bin Malik رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alitoka pamoja na Waislamu, wakiukusudia msafara wa Makuraishi, mpaka Allah Akawakutanisha wao na adui zao pasi na kuwekeana miadi”<sup>2</sup>. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, Yazid bin Ruman alinisinulia kutoka kwa 'Urwah bin Az-Zubayr رضي الله عنه kuwa alisema, Mtume ﷺ alipokaribia Badr Alimtura 'Ali bin Abu Twalib, Sa'd bin Abu Waqqas na Az-Zubayr bin Al-'Awwam رضي الله عنهم kutoka katika Masahaba wake kwenda kupeleleza khabari kwa ajili yake. Wakawakamata Vijana wawili, mtumishi wa Banu Sa'id bin Al-'As na mwingine wa Banu Al-Hajjaj. Wakaja nao kwa Mtume ﷺ wakamkuta akiwa anasali. Masahaba wa Mtume ﷺ wakaanza kuwauliza, “Nyinyi mnatoka kwa nani?” Wakasema, “Sisi tunafanya kazi ya kuwapatia maji ya kunywa”. Masahaba walichukizwa na khabari yao, kwani waliwachukulia kwamba wako chini ya Abu Sufyan. Wakawapiga vikali, wakasema, “Tuko chini ya Abu Sufyan”. Nao wakawaacha. Mtume ﷺ alirukuu, kisha akasujudu sijida mbili na akatoa salamu na akasema.

«إِذَا صَدَقَاتُكُمْ صَرَيبَتُمْوهُمْ، وَإِذَا كَذَبَاتُكُمْ تَرَكَتُمْوهُمْ، صَدَقًا وَاللَّهِ! إِنَّهُمَا لِقُرَيْشٍ،  
أَخْبِرَانِي عَنْ قُرَيْشٍ»

*“Wanapokuambieni ukweli mnawapiga, na wakikuongopeeni mnawaacha? Wamesema ukweli, Wallah! Wao wanatoka kwa Makuraishi (Akawaambia Vijana hao): Nijulisheni kuhusu makuraishi”.*

Wakasema; “Wao wako nyuma ya kilima hiki cha mchanga mnachokiona, katika sehemu ya mbali bondeni”. Mtume ﷺ akawauliza,

<sup>1</sup> Ibn Hisham 2:328.

<sup>2</sup> At-Tabari 13:566.



«كَمْ الْقَوْمُ؟»

“Wako wangapi?”

Wakasema: “Wengi”.

«مَا عُدْتُهُمْ؟»

“Idadi yao ngapi:

Wakasema, “Hatujui”

«كَمْ يَنْخَرُونَ كُلَّ يَوْمٍ؟»

“Wao huchinja ngamia wangapi kila siku?”

Wakasema, “Tisa au kumi” Mtume ﷺ akasema,

«الْقَوْمُ مَا بَيْنَ الشَّعْبَانَةِ إِلَى الْأَنْفِ»

“Watu hao wako baina ya mia tisa na elfu”.

Halafu akawauliza,

«فَمَنْ فِيهِمْ مِنْ أَشْرَافِ قُرَيْشٍ؟»

“Mkuu gani wa Kikuraishi aliye miongoni mwa jeshi?”

Wakasema, ‘Utbah bin Rabi’ah, Shaybah bin Rabi’ah, Abu Al-Bakhtari bin Hisham, Hakim bin Hizam, Nawfal bin Khuwaylid, Al-Harith bin ‘Amir bin Nawfal, Tuaymah bin ‘Adi bin Nawfal, An-Nadhr bin Al-Harith, Zam’ah bin Al-Aswad, Abu Jahl bin Hisham, Umayyah bin Khalaf, Nabih na Munabbih ambao ni wana wa Al-Hajjaj, Suhayl bin ‘Amr na ‘Umar bin ‘Abd Wadd”. Mtume ﷺ aliwakabili Masahaba akawaambia,

«هَذِهِ مَكَّةُ فَذَ أَلْقَتْ إِيَّكُمْ أَفْلَادَ كَيْدِمَا»

“Hii ni Makkah, imekuleteeni Wanawe wa tunu kubwa (wakuu wake).”<sup>1</sup>

Allah تعالی Anasema,

لِيَهْلِكَ مَنْ هَلَكَ عَنْ بَيِّنَةٍ وَيَحْيَىٰ مَنْ حَيَّ عَنْ بَيِّنَةٍ

“...kwa sababu aangamie wa kuangamia kwa dalili zilizo dhahiri, na asalimike wa kusalimika kwa dalili zilizo dhahiri”.

<sup>1</sup> Ibn Hisham 2:268.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, “Ili wenye kukufuru, wafanye hivyo baada ya kupata dalili kutokana na kushuhudia Ishara na mazingatio, na mwenye kuamini, aamini kutokana na hayo kadhalika”<sup>1</sup>. Hii ni tafsiri nzuri. Ufafanuzi wake ni kwamba: Allah تعالى Anasema kuwa Amekukutanisheni na maadui wenu katika mahali pamoja, pasi na miadi, ili Akupeni ushindi na Alinyanyue neno la haki juu ya batili, ili jambo liwe dhahiri, na hoja (dalili) iwe yenye kukata (kila la batili) na ushahidi wazi wazi. Wala kusalie yeyote mwenye hoja wala shaka. Wakati huo, atahiliki wa kuangamia, yaani aendelee kubaki katika ukafiri anayetaka kufanya hivyo, huku akiwa na dalili juu ya jambo lake, akijua fika kwamba yeye amepotoka kutokana na ushahidi dhidi yake.

وَيَحْيَىٰ مِّنْ حَىٰ

“...*na asalimike wa kusalimika*...”. Maana yake: Aamini anayetaka kuamini.

عَنْ بَيِّنَةٍ

“...*kwa dalili zilizodhahiri*”. Maana: Kwa hoja na ushahidi. Imani ndio uhai wa nyoyo. Allah تعالى Alisema,

أَوْ مَن كَانَ مِيْتًا فَأَحْيَيْنَاهُ وَجَعَلْنَا لَهُ نُورًا يَمْشِي بِهِ فِي النَّاسِ

**“Je, aliyekuwa maiti kisha Tukamhuisha, na Tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu”. (6:122)**

Mama Aisha رضي الله عنها alikizungumzia kisa cha uzushi (*ifki*), “Basi akahiliki kwa ajili ya jambo langu, aliyehiliki”. Maana yake: Aliyesema juu yake mambo ya uzushi<sup>2</sup>. Kauli ya Allah تعالى,

وَإِنَّ اللَّهَ لَسَمِيعٌ عَلِيمٌ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua”.**

Kwa maana: Kuzisikia dua zenu Kwake, unyenyekevu wenu na kutaka kwenu msaada.

عَلِيمٌ

“*Mwenye Kujua*”. Kwa maana: Kukujieni nyinyi na kwamba nyinyi mnastahiki nusura juu ya maadui wenu makafiri mafedhuli.

<sup>1</sup> At-Tabari 13:568.

<sup>2</sup> Ahmad 6:195.

إِذْ يُرِيكُمُ اللَّهُ فِي مَنَايِكٍ قَلِيلًا ۖ وَلَوْ أَرَنَكُمُ كَثِيرًا لَفَشِلْتُمْ وَتَلْتَزَعْتُمْ فِي الْأَمْرِ  
 وَلَكِنَّ اللَّهَ سَلَّمَ ۗ إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٤٣﴾ وَإِذْ يُرِيكُمُوهُمْ إِذِ الْتَقَيْتُمْ فِي  
 أَعْيُنِكُمْ قَلِيلًا وَيُقَلِّلُكُمْ فِي أَعْيُنِهِمْ لِيَقْضَى اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا ۗ وَإِلَى اللَّهِ  
 تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٤٤﴾

43. "Kumbuka alipokuonesha usingizini mwako kwamba wao ni wachache – na lau angelikuonesha kuwa ni wengi, mngeliingiwa na woga, na mngelizozana katika jambo hilo. Lakini Mwenyezi Mungu Kakulindeni. Hakika Yeye ni Mwenye Kuyajua yalio vifuani."

44. "Na kumbukeni mlipokutana Akakuonesheni machoni mwenu kuwa wao ni wachache, na Akakufanyeni nyinyi ni wachache machoni mwao, ili Mwenyezi Mungu Atimize jambo lililokuwa liwe. Na mambo yote hurejeshwa kwa Mwenyezi Mungu."

Allah تعالی Kulifanya Kila Kundi Kuwa Dogo Machoni mwa Kundi Jingine.

Mujahid alisema, "Allah تعالی Alimuonesha Mtume ﷺ kuwa maadui ni wachache na Akawajulisha hilo Masahaba wake, nao likawapa nguvu"<sup>1</sup>. Ndivyo hivyo walivyosema Is-haq رحمه الله تعالی na wengine. Kauli ya Allah تعالی;

وَلَوْ أَرَنَكُمُ كَثِيرًا لَفَشِلْتُمْ

"...na lau Angelikuonesha kuwa ni wengi, mngeliingiwa na woga..."

Mngeliwaogopa, na mngelikhitilafiana baina yenu,

وَلَكِنَّ اللَّهَ سَلَّمَ

"Lakini Mwenyezi Mungu Kakulindeni..."

Maana: Kutokana na hilo, kwa kule Kukuonesheni kuwa ni wachache.

إِنَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿٤٣﴾

"Hakika Yeye ni Mwenye Kuyajua yalio vifuani". (8:43)

<sup>1</sup> At-Tabari 13:570.

Kwa maana: Yanayofichwa na dhamira na nafsi ya ndani kabisa.

يَعْلَمُ حَاطِبَةَ الْأَعْيُنِ وَمَا تُخْفِي الصُّدُورُ ﴿٤١﴾

**“(Mwenyezi Mungu) Anajua khiyana ya macho na yanayo fichwa na vifua”. (40:19)**

Kauli ya Allah تعالى،

وَإِذْ يُرِيكُمُوهُمْ إِذِ الْتَقَيْتُمْ فِي أَعْيُنِكُمْ قَلِيلًا

**“Kumbuka Alipokuonesha usingizini mwako kwamba wao ni wachache”.**

Hii nayo ni miongoni mwa huruma ya Allah تعالى kwao, kwa Kuwaonesha kwamba wao ni wachache kwa kuonekana, basi hilo likawapa ujasiri na kuwa na shauku ya kukabiliana nao. Abu Is-haq As-Sabiy alipokea kutoka kwa Abu ‘Ubaydah, kutoka kwa ‘Abdullah bin Mas‘ud رضي الله عنهم، kuwa, “Walifanywa waonekane wachache machoni mwetu katika siku ya Badr, mpaka nikamuambia mtu aliyekuwa pembeni mwangu, “Unawaona wako sabini?” Akasema, “Hapana, bali wako mia moja”. Mpaka tulipomkamata mmoja wao, tukamuuliza. Akasema, “Tulikuwa elfu moja”<sup>1</sup>. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir تعالى waliinukuu. Kauli ya Allah تعالى،

وَيُقَلِّبُكُمْ فِي أَعْيُنِهِمْ

**“...na Akakufanyeni nyinyi ni wachache machoni mwao...”.**

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alimnukuu ‘Ikrimah, kuwa:

وَإِذْ يُرِيكُمُوهُمْ إِذِ الْتَقَيْتُمْ

**“Na mlipokutana Akakuonesheni”.**

Kwamba, waliwahimiza wao kwa wao<sup>2</sup>. Isnadi yake ni *Sahih*. Muhammad bin Is-haq alisema: Yahya bin Ubad bin Az-Zubayr alinisimulia kutoka kwa baba yake juu ya Kauli ya Allah تعالى،

<sup>1</sup> At-Tabari 13:572. Isnadi yake ni dhaifu, kwani Ubaidah hakupokea kutoka kwa Abdillah bin Masoud.

<sup>2</sup> Ibn Abu Hatim 5:1710.

لِيَقْضِيَ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا

**“...ili Mwenyezi Mungu Atimize jambo liliokuwa liwe”.**

Maana: “Ili Allah تعالی Aingize vita baina yao ili Alipize kisasi dhidi ya Alioamua walipizwe kisasi (Washirikina) na Kuwaneemesha Aliotaka Kuwaneemesha katika walio mawalii Wake”<sup>1</sup>. Maana yake hapa, ni kwamba, Allah تعالی Alilihimiza kila kundi dhidi ya jingine, na Akalifanya dogo machoni mwao ili wawe na shauku ya kukutana. Hili liliokuwa wakati wa kuelekeana uso kwa uso. Mapigano yalipoanza na Allah تعالی Akawasaidia Waumini kwa Malaika elfu moja kwa mfuatano, makafiri wakawaona Waumini hali ya kuwa mara mbili yao. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی,

قَدْ كَانَ لَكُمْ آيَةٌ فِي فِئَتَيْنِ الَّذِينَ كَفَرُوا فَمَقَّ يَوْمَ يَأْتِيكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا يُوقِنُونَ أَنَّكُمْ آلُ قُرَيْشٍ وَالْقُرَىٰ أُذُنًا لِّأُولَئِكَ لَمَّا كَفَرُوا فَوَقَّ اللَّهُ فِتْنَتَهُمْ فَلْيَتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا

مَثَلِهِمْ رَأَىٰ أَلْعَيْنَ ۗ وَاللَّهُ يُؤَيِّدُ بِنَصَرِهِ مَن يَشَاءُ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّأُولِي

الْأَبْصَارِ ﴿١٣﴾

**“Hakika ilikuwa ni Ishara kwenu katika yale majeshi mawili yalipopambana. Jeshi moja likipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu na jingine kafiri likiwaona zaidi kuliko wao mara mbili, kwa kuona kwa macho. Na Mwenyezi Mungu Humuunga mkono Amtakaye kwa Nusura Yake. Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa wenye macho”. (3:13)**

Maana ya Aya mbili hizi zinajumuishwa, kwani kila moja ya hizo ni hakika na kweli. Sifa Njema na Shukrani zinamstahikia Allah تعالی.

\* \* \*

<sup>1</sup> Ibn Hisham 2:328 na Ibn Hatim 5:1710.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيتُمْ فِئَةً فَاثْبُتُوا وَاذْكُرُوا اللَّهَ  
 كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٤٥﴾ وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا  
 تَتَزَعَّوْا فَتَفْشَلُوا وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ ۖ وَأَصْبِرُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ مَعَ  
 الصَّابِرِينَ ﴿٤٦﴾ وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ خَرَجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ  
 بَطْرًا وَرِئَاءَ النَّاسِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا  
 يَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿٤٧﴾ وَإِذْ زَيْنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ  
 وَقَالَ لَا غَالِبَ لَكُمْ أَيَّوْمَ مِنَ النَّاسِ وَإِنِّي جَارٌ  
 لَكُمْ ۖ فَلَمَّا تَرَآتِ الْفَيْتَانِ نَكَصَ عَلَى عَقِبَيْهِ وَقَالَ إِنِّي  
 بَرِيءٌ مِّنْكُمْ إِنِّي أَرَىٰ مَا لَا تَرَوْنَ إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ ۗ وَاللَّهُ  
 شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٤٨﴾ إِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي  
 قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ غَرَّ هَتُولَاءِ دِينَهُمْ ۗ وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ  
 فَإِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٩﴾ وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ يَتَوَقَّى الَّذِينَ  
 كَفَرُوا آلَ مَلَيْكَةَ يَضْرِبُونَ وُجُوهَهُمْ وَأَدْبَارَهُمْ وَذُوقُوا  
 عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٥٠﴾ ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيكُمْ  
 وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلْمٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٥١﴾ كَذَّابٌ ءَالٍ فِرْعَوْنِ  
 ۖ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۗ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ  
 بِذُنُوبِهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٢﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيتُمْ فِئَةً  
 فَاثْبُتُوا وَاذْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ  
 تُفْلِحُونَ ﴿٤٥﴾ وَأَطِيعُوا اللَّهَ  
 وَرَسُولَهُ وَلَا تَتَزَعَّوْا فَتَفْشَلُوا  
 وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ ۖ وَأَصْبِرُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ مَعَ  
 الصَّابِرِينَ ﴿٤٦﴾

45. "Enyi mlioamini! Mki-kutana na jeshi, basi kueni imara, na mkumbukeni Mwenyezi Mungu sana ili mpate kufanikiwa".

46. Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala msizozane mkaingiwa woga, na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wanaosubiri".

**Mafunzo ya Adabu za Kivita.**

Haya ni mafunzo, Allah تعالى Anawapa waja Wake Waumini kuhusu adabu za

kupambana na adui na mbinu za kuonesha ushujaa wakati wa kumkabili adui. Allah تعالى Alisema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيتُمْ فِئَةً فَاثْبُتُوا

"Enyi mlioamini! Mkikutana na jeshi, basi kueni imara...".

Imethibiti katika Sahihi Mbili kutoka kwa 'Abdullah bin Abu Awfa رضي الله عنه, kuwa Mtume ﷺ katika baadhi ya siku alizokabiliana na adui, alingojea mpaka jua liliposhuka, alisimama kati yao, akasema:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ لَا تَتَمَنَّوْا لِقَاءَ الْعَدُوِّ، وَاسْأَلُوا اللَّهَ الْعَاقِبَةَ فَإِذَا لَقَيْتُمُوهُمْ فَاصْبِرُوا  
وَاعْلَمُوا أَنَّ الْجَنَّةَ تَحْتَ ظِلَالِ الشُّوفِ»

*“Enyi watu! Msitamani kukutana na adui, na muombeni Allah afya, na mtakapokabiliana na adui, basi muwe na subira, na mjue kwamba Jannah (pepo) iko chini ya vivuli vya mapanga”.*

Kisha akasimama na kusema:

«اللَّهُمَّ مُنْزِلَ الْكِتَابِ، وَمُجْرِي السَّحَابِ، وَهَازِمَ الْأَخْرَابِ، اهْزِمْنَاهُمْ وَأَنْصِرْنَا  
عَلَيْهِمْ»

*“Ewe Allah تعالى! Mteremsha Kitabu, Mwendeshaji wa mawingu, Mwenye Kuyashinda makundi. Washinde na Utunusuru juu yao”<sup>1</sup>.*

Naye, Ka'b Al-Ahbar alisema: “Hapana kitu Akipendacho sana Allah تعالى kuliko kisomo cha Qur'an na Dhikri, ndio Akawaamuru watu Sala na jihadi, je hamuoni kuwa Yeye Aameamrisha dhikri wakati wa kupigana? Pale Aliposema:

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا لَقِيتُمْ فِئَةً فَاغْلِبُوا وَادْكُرُوا اللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ.

*“Enyi mlioamini! Mkikutana na jeshi, basi kueni imara na mkumbukeni Mwenyezi Mungu sana ili mpate kufanikiwa.”<sup>2</sup>*

### **Amri ya Kuwa Imara Wakati wa Kukabiliana na Adui.**

Pia Allah تعالى Aameamuru kuwa imara wakati wa kumkabili adui na kuwa na subira katika kupigana nao. Kwa hivyo, wapiganaji wasitoroke wala kuwakwepa maadui, wala kuwa waoga, na wamdhukuru Allah تعالى katika hali hiyo, na wasimsahau. Bali wamuombe msaada na watawakali Kwake Yeye na wamuombe Awape ushindi dhidi ya maadui wao. Pia wamtii Allah تعالى na

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 6:140 na Muslim 3:1362.

<sup>2</sup> Ibn Abii Hatim (9132) na 5:1711 Sanadi yake ni dhaifu. Tz “Tahriru At-Tah'dhibu”

Mtume ﷺ katika hali yao hiyo, basi kile ambacho Allah تعالى Amewaamuru, wakitekeleza na Alichowakataza wajiepushe nacho. Pia wasibishane kwa yaliyo baina yao ambayo yanaweza kuwafanya wakhitilafiane na kuwa sababu ya kutelekezana na kushindwa kwao.

وَتَذَهَبَ رَيْحُكُمْ

“...zikapotea nguvu zenu...”. Maana yake: Ni nguvu zenu nyingi na hali ya kusonga mbele vitapotea.

وَأَصْبِرُوا إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٤٥﴾

**“Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wanaosubiri”.**

Kuhusu ushujaa na utekelezaji wa amri za Allah تعالى na Mtume ﷺ na kuyafuata maelekezo Yake, Masahaba walifikia daraja ya juu sana ambayo hawajaifikia umma zote za kabla yao. Wala haitatokea kwa walio baada yao. Kwa baraka za Mtume ﷺ na utii wao kwa kila alichokiamuru, walifanikiwa kufungua nyoyo na mataifa mengi Mashariki ya dunia na Magharibi, katika kipindi kidogo, licha ya uchache wao mbele ya majeshi ya mataifa, kama vile, Warumi, Waajemi, Waturuki, As-Swaqaalibah, Waberber na Wahabeshi. Pamoja na Wasudani, Wakhofti na mataifa mengine ya wanadamu. Waliwashinda wote hawa, na Neno la Allah تعالى likanyanyuliwa juu zaidi, na Dini ya Allah تعالى Uislamu ikawa juu ya dini nyingine. Dola ya Kiislamu ikaenea Mashariki ya Dunia mpaka Magharibi yake, kwa uchache mafanikio hayo hayakuchukua hata miaka thelathini. Tunamuomba Allah تعالى Awaridhie wote, na Atufufue pamoja nao, kwani Yeye ni Mkarimu, Mwenye Fadhila.

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ خَرَجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بَطْرًا وَرِثَاءَ النَّاسِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

وَاللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿٤٦﴾ وَإِذْ زَيْنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ وَقَالَ لَا غَالِبَ لَكُمْ

الْيَوْمَ مِنَ النَّاسِ وَإِنَّ جَارَ لَكُمْ<sup>ط</sup> فَلَمَّا تَرَأَتِ الْفِئْتَانِ نَكَصَ عَلَى عَقْبَيْهِ وَقَالَ إِنَّي

بَرِيءٌ مِّنْكُمْ إِنَّي أَرَى مَا لَا تَرَوْنَ إِنِّي أَخَافُ اللَّهَ وَاللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٤٧﴾ إِذْ

يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ غَرَّ هَتُّوْلَاءِ دِينُهُمْ<sup>ط</sup> وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ

فَإِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٨﴾



47. *“Na wala msiwe kama wale waliotoka majumbani mwao kwa fakhari na kujionesha kwa watu, na wakawazuilia watu njia ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Ameyazunguka yote wanayoyafanya”.*

48. *“Na kumbuka pale Shetani alipowapambia vitendo vyao, na akawaambia: Hapana watu wa kukushindeni leo hii, na hali mimi ni Mlinzi wenu. Yalipoonana majeshi mawili, akarudi nyuma na akasema: Mimi si pamoja nanyi. Mimi naona msiyoyaona. Mimi namuogopa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu”.*

49. *“Na waliposema wanafiki, na wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao: Watu hawa dini yao imewadanganya. Na mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu Ametukuka, na Mwenye Hekima”.*

### Hali Waliyotokanayo Washirikina Kuelekea Badri.

Baada ya kuwaamuru Waumini kuwa na ikhilasi wanapopigana katika njia Yake na kukithirisha kumdhukuru, Allah تعالى Anawakataza kujishabihisha na Washirikina wanapotoka majumbani mwao,

بَطْرًا

*“...kwa fakhari...”*. Kwa maana: Wao wanatoka kwa nia ya kuondoa haki.

وَرِثَاءَ النَّاسِ

*“...na kujionesha kwa watu”*. Nako ni kujifakharisha na kiburi juu yao. Kama alivyosema Abu Jahl, alipoambiwa: “Msafara umeshanusurika, basi rejeeni”. Akasema: “Hapana Wallahi! Hatutarejea, mpaka tuyafikie maji ya Badr, tuchinje ngamia, tunywe pombe na watuimbie waimbaji wa kike. Tukifanya hivyo, siku zote, Waarabu watazungumzia uwezo wetu, kwa siku hiyo, na katika jamii ya Waarabu maisha yote”. Hayo yote yakawawia kinyume, kwani walipoyafikia maji ya Badr walifikwa na mauti. Walitupwa katika kisima cha Badr, wakiwa wafu, dhalili, waliofedheheka na waovu wenye kustahiki adhabu yenye kuendelea milele. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

وَاللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿٤٧﴾

***“Na Mwenyezi Mungu Ameyazunguka yote wanayoyafanya”.***

Kwa maana: Ni Mwenye Kuyajua zaidi yale yaliyowaleta, na kwa ajili hiyo Aliwapa adhabu mbaya<sup>1</sup>. Walisema Ibn ‘Abbas, Mujahid, Qatadah, Adh-Dhahhak na As-Suddi kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ خَرَجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بَطْرًا وَرِثَاءَ النَّاسِ

***“Wala msiwe kama wale waliotoka majumbani mwao kwa fakhari na kujionesha kwa watu”.***

Wakasema: “Hao ni Washirikina waliopigana dhidi ya Mtume ﷺ katika siku ya Badr”<sup>2</sup>. Naye Muhammad bin Ka'b alisema: “Makuraishi walipotoka Makkah kwenda Badr, walileta waimbaji wa kike na ngoma.” Allah تعالى Akateremsha,

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ خَرَجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ بَطْرًا وَرِثَاءَ النَّاسِ وَيَصُدُّونَ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ

وَاللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿٤٧﴾

***“Na wala msiwe kama wale waliotoka majumbani mwao kwa fakhari na kujionesha kwa watu, na wakawazuilia watu njia ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Ameyazunguka yote wanayo yafanya”.***

**Shetani Hulipamba Ovu Lionekane Jema na Kuwahadaa Kwake Washirikina.**

وَإِذْ زَيْنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَلَهُمْ وَقَالَ لَا غَالِبَ لَكُمْ الْيَوْمَ مِنَ النَّاسِ وَإِنِّي جَارٌ لَكُمْ

***“Na kumbukeni pale Shetani alipowapambia vitendo vyao, na akawaambia: Hapana watu wa kukushindeni leo hii, na hali mimi ni mlinzi wenu”.***

<sup>1</sup> Ibn Hisham 2:329.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:8-9.

Aliwafanyia yaonekane mema kwao (Laana ya Allah تعالى imfikie) yale yaliyowaleta na waliyoyakusudia na akawapa tamaa kwamba hakuna mtu wa kuwashindeni leo<sup>1</sup>. Pia aliwaondolea uoga juu ya uwezekano wa maadui wao, kabila la Banu Bakr kushambulia nyumba zao watakapoondoka (huko Makka) na akasema:

وَأِنِّي جَارٌ لَّكُمْ

*“Mimi ni mlinzi wenu”*

Shetani Alijitokeza kwao katika sura ya Suraqa bin Malik bin Jushum, mkuu wa Banu Mujiad, kama Allah تعالى Alivyomuelezea shetani huyo,

يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا

***“Anawaahidi na anawatia tamaa. Na shetani hawaahidi ila udanganyifu”.*** (4:120)

Ibn Jurayri alisema: Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alizungumzia Ayah hii, “Ilipofika siku ya Badr, Ibilisi akiwa na bendera na jeshi lake alikwenda pamoja na Washirikina, na akanong’ona nyoyoni mwao, “Hapana wa kukushindeni, nami ni mlinzi wenu.” Lakini walipokutana, na Ibilisi akaona msaada wa Malaika, kutoka kwa Allah تعالى,

نَكَصَ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ

*“...akarudi nyuma...”*

Kwa maana: Akarejea nyuma kukimbia, na akasema:

إِنِّي أَرَىٰ مَا لَا تَرَوْنَ

***“Hakika mimi naona msiyoyaona”<sup>2</sup>.***

‘Ali bin Abu Twalhah alipokea kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema: “Ibilisi alikuja katika sura ya Suraqah bin Malik bin Ju’shum huku akiwa na bendera siku ya vita vya Badri, katika hali hiyo alikuja Badr pamoja na jeshi la mashetani. Shetani akawaambia washirikina,

<sup>1</sup> At-Tabari 14:14.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:9.

لَا غَالِبَ لَكُمْ الْيَوْمَ مِنَ النَّاسِ وَإِنَّ جَارَ لَكُمْ

*“Leo hakuna watu wa kukusaidieni, nami ni mlinzi wenu...”.*

Watu waliposimama safu (kukabiliana kijeshi), Mtume ﷺ alichukua mchanga akautupa katika nyuso za Washirikina, mashetani wakageuka na kukimbia. Jibril عليه السلام akamkabili Ibilisi, naye alipomuona huku mkono wake ukiwa umeshikana na mkono wa mmoja wa Washirikina, aliutoa mkono wake, kisha akageuka na kukimbia pamoja na askari wake. Mtu yule akasema: “Ewe Suraqah! Unadai kwamba wewe ni mlinzi wetu?” Akasema:

أَرَى مَا لَا تَرَوْنَ إِنِّي أَخَافُ اللَّهََ وَاللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥١﴾

*“Mimi naona msiyoyaona. Mimi namuogopa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu”.*

Hayo ni pale alipowaona Malaika<sup>1</sup>.

### Msimamo wa Wanafiki Siku ya Badri.

Kauli ya Allah تعالى،

إِذْ يَقُولُ الْمُنَافِقُونَ وَالَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ غَرَّ هَتُّوْلَاءِ دِينُهُمْ

*“Na waliposema wanafiki, na wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao: Watu hawa dini yao imewadanganya...”.*

‘Ali bin Abi Twalhah alisema: kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuhusu Ayah hii kuwa, ‘Kaumu hizo zilipokaribiana, Allah تعالى Aliwafanya wachache Waislamu machoni mwa Washirikina, na Akawafanya hivyo washirikiana machoni mwa Waislamu. Washirikina wakasema:

غَرَّ هَتُّوْلَاءِ دِينُهُمْ

*“...Watu hawa dini yao imewadanganya...”.*

<sup>1</sup> At-Tabari 14:7.

Hayo walijasema kwa sababu ya kuonekana kwa Waislamu wachache machoni mwao, wakawa wanaamini bila kuwa na shaka kwamba wangeliwashinda Waislamu. Allah تعالى Alisema:

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٥﴾

**“Na mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu Ametukuka, na Mwenye Hekima”<sup>1</sup>.**

Qatadah alisema: “Waliona kundi la Waumini waliokuja kutetea Dini ya Allah تعالى. Tulielezwa kwamba adui wa Allah تعالى, Abu Jahal, alipomuona Muhammad ﷺ na Masahaba wake, alisema kwa ukali na ufedhuli, “Wallah! Hawatamuabudu Allah تعالى baada ya leo hii”<sup>2</sup>. ‘Amir Ash-Sha’bi alisema: “Baadhi ya watu wa Makkah waliniuia kuingia katika Uislamu, wakatoka pamoja na Washirikina katika siku ya Badr, walipouona uchache wa Waislamu walisema:

غَرَّهتُوا لآءِ دِينُهُمْ

**“...Watu hawa Dini yao imewadanganya...”<sup>3</sup>.**

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ

**“Na mwenye kumtegemea Mwenyezi Mungu...”**. Maana yake: Anategemea rehema na neema za Allah تعالى.

فَإِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ

**“...basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu...”**

Kwa maana: Hawaangamii wale wamtegemeao, kwani Allah تعالى ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kinga na Mwenye Mamlaka makubwa,

حَكِيمٌ ﴿٤٦﴾

**“...Mwenye Hekima.”** Katika Matendo Yake, kwani Haweki vitu ila mahali pake, hivyo Humnusuru mwenye haki ya kunusuriwa na Kumdhalilisha mwenye kustahiki kufanywa hivyo.

<sup>1</sup> Ad-Dur Al-Manthur 4:78.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:14.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:13.

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ يَتَوَقَّى الَّذِينَ كَفَرُوا الْمَلَائِكَةَ يَصْرِيحُونَ وَجُوهَهُمْ وَأَدْبَرَھُمْ وَذُوقُوا  
عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٥٠﴾ ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَمٍ لِّلْعَالَمِينَ ﴿٥١﴾

**50. "Na laiti ungeliona Malaika wanapowafisha wale waliokufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao, na kuwaambia: lonjeni adhabu ya Moto!"**

**51. "Hayo ni kwa sababu ya yale yaliyokwishatangulizwa na mikono yenu, na hakika Mwenyezi Mungu si Mwenye Kuwadhulumu waja."**

### Kipigo cha Malaika kwa Makafiri Wakati wa Kuwatoa Roho Zao.

Allah تعالیٰ Anasema: Ungewaona Malaika, ewe Muhammad ﷺ, Malaika wanapotoa roho zao, ungeona jambo kubwa la kutisha, na baya sana. Pindi,

يَصْرِيحُونَ وَجُوهَهُمْ وَأَدْبَرَھُمْ

**"...wakiwapiga nyuso zao na migongo yao..."**Huku wakiwaambia,

وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٥٠﴾

**"...lonjeni adhabu ya Moto!"**Ibn Jurayj amesema kuwa Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَأَدْبَرَھُمْ

**"...na migongo yao..."**Upande wao wa nyuma, kama ilivyotokea siku ya Badr. Ibn Jurayj alisimulia pia kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما: "Washirikina walipowakabili Waislamu, waliwapiga nyuso zao kwa mapanga na walipogeuka kukimbia Malaika waliwapiga migongoni mwao"<sup>1</sup>. Ingawa sababu ya kushuka kwa Ayah hizi ni kuelezea tukio la Badr, lakini inahusu katika jambo la kila kafiri, na kwa ajili hiyo, Allah تعالیٰ Hakuikhusisha Aya na watu wa Badr, bali Alisema:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ يَتَوَقَّى الَّذِينَ كَفَرُوا الْمَلَائِكَةَ يَصْرِيحُونَ وَجُوهَهُمْ وَأَدْبَرَھُمْ

**"Na laiti ungeliona Malaika wanapowafisha wale waliokufuru wakiwapiga nyuso zao na migongo yao".**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:16.

Na katika *Surat Al-Qital* (au *Muhammad*, Sura ya 47) kuna Aya kama hiyo, na katika *Surat Al-An'am*, Allah تعالى Anasema,

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلَائِكَةُ بَاسِطُوا أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنفُسَكُمُ

**“Na lau ungeliswa madhalimu wanavyokuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyooshea mikono wakiwaambia: Zitoeni roho zenu!”.** (6:93)

Kwa maana: Wamewanyooshea mikono yao kuwapiga kwa amri ya Mola wao, nafsi zao zinapokuwa ngumu na kukataa kutoka katika viwiliwili, hivyo, hutolewa kwa nguvu. Hayo ni baada ya kujuzwa adhabu na ghadhabu ya Allah تعالى. Kama ilivyopokewa katika Hadithi ya Al-Baraa, kuwa Malaika wa mauti akija kwa kafiri humjia kwa sura ya kutisha, husema, “Toka ewe nafsi chafu! uende kwenye upepo mkali wa moto, maji yachemkayo na kivuli cha moshi mweusi.” Kisha roho yake inaacha mwili wake, na Malaika wataitoa mwilini kama sindano inavyotoka katika pamba iliyorowa. Na itatoka pamoja na mishipa ya damu na fahamu.”<sup>1</sup> Kwa hili, Allah تعالى Amejuzua kuwa Malaika watawaambia, **“Onjeni adhabu ya Moto!”.**

ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمْتِ أَيْدِيكُمْ

**“Hayo ni kwa sababu ya yale yaliyokwisha tangulizwa na mikono yenu...”.**

Maana yake: Malipo haya ni kwa sababu ya matendo maovu mliyoyafanya katika maisha yenu ya duniani. Allah تعالى Amekulipeni malipo haya.

وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَمٍ لِلْعَبِيدِ ﴿٩٤﴾

**“...na hakika Mwenyezi Mungu si Mwenye Kuwadhulumu waja”.**

Maana: Hadhulumu kiumbe Wake yeyote, bali Yeye ni Mpangaji wa kila kitu kwa Kukiweka mahali pake, Muadilifu, Hamdhulumu yeyote, Ametakasika na Kutukuka, na Ameepukana na kila hila, Mkwasi, Msifiwa. Kwa hili, ilikuja Hadith *Sahih* ameipokea Muslim, kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه kutoka kwa Mtume

﴿٩٤﴾ إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَقُولُ: يَا عِبَادِي إِنِّي حَرَمْتُ الظُّلْمَ عَلَىٰ نَفْسِي وَجَعَلْتُهُ بَيْنَكُمْ مُحَرَّمًا فَلَا تَظَالَمُوا، يَا عِبَادِي إِنَّمَا هِيَ أَعْمَالُكُمْ أُحْصِيهَا لَكُمْ فَمَنْ وَجَدَ خَيْرًا فَلْيَحْمَدِ اللَّهَ وَمَنْ وَجَدَ غَيْرَ ذَلِكَ فَلَا يَلُومَنَّ إِلَّا نَفْسَهُ،

<sup>1</sup> Ahmad 4:287-288.

“Allah Anasema, “Enyi waja wangu, Mimi nimeharamisha dhuluma katika nafsi Yangu na Nika iharamisha kwenu, basi msidhulumiane. Enyi waja wangu! Amali zenu Ninazihifadhi. Mwenye kukuta kheri, amshukuru Allah, Mwenye kukuta ghairi ya hivyo, asilaumu ila nafsi yake”<sup>1</sup>.

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema,

كَذَّابٍ ءَالٍ فِرْعَوْنَ ۖ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِذُنُوبِهِمْ ۗ إِنَّ  
اللَّهَ قَوِيٌّ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٢﴾

**52. “Kama ada ya watu wa Firauni na waliokuwa kabla yao – walizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu. Basi Mwenyezi Mungu Aliwashika kwa sababu ya madhambi yao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mkali wa Kuadhibu”.**

Allah تعالى Anasema, kitendo cha Washirikina wakadhibishaji kwa uliyotumwa kwayo, ni kama kitendo cha wakadhibishaji kabla yao. Nasi Tulifanya ada na sunna yetu kwa wakadhibishaji mfano wao katika jamaa wa Firauni na ummah za wakanushaji Mitume kabla yao, waliokataa Aya za Allah تعالى,

فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ بِذُنُوبِهِمْ

**“Basi Mwenyezi Mungu Aliwashika kwa sababu ya madhambi yao”.**

Maana: Aliwahilikisha kwa sababu ya dhambi zao na Aliwashika mshiko wa Mwenye Nguvu Muweza.

إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٢﴾

**“Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mkali wa Kuadhibu”.**

Maana yake: Hapana yeyote wa Kumshinda, wala Kumponyoka kwa kukimbia.

\* \* \*

<sup>1</sup> Muslim 4:1994.



ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ لَمْ يَكُ مُغَيِّرًا نِعْمَةً عَلَىٰ قَوْمٍ  
 حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ ۗ وَأَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٥٣﴾  
 كَذَّابِ ۖ آلِ فِرْعَوْنَ ۖ وَالَّذِينَ مِنَ قَبْلِهِمْ ۚ كَذَّبُوا  
 بِآيَاتِ رَبِّهِمْ فَأَهْلَكْنَاهُمْ بِذُنُوبِهِمْ وَأَغْرَقْنَا آلَ فِرْعَوْنَ ۚ  
 وَكُلًّا كَانُوا ظَالِمِينَ ﴿٥٤﴾ إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِنْدَ اللَّهِ  
 الَّذِينَ كَفَرُوا فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٥﴾ الَّذِينَ عَاهَدتَّ مِنْهُمْ  
 ثُمَّ يَنْقُضُونَ عَهْدَهُمْ فِي كُلِّ مَرْقٍ وَهُمْ لَا يَتَّقُونَ  
 ﴿٥٦﴾ فَإِذَا تَثَقَّفْتُمْ فِي الْحَرْبِ فَشَرِّدْ بِهِمْ مَنْ خَلَفَهُمْ  
 لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٥٧﴾ وَإِنَّمَا تَخَافُونَ مِنْ قَوْمٍ خِيَانَةً  
 فَانذِرْ إِلَيْهِمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ ۚ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِبِينَ ﴿٥٨﴾  
 وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَبَقُوا ۚ إِنَّهُمْ لَا يُعْجِزُونَ ﴿٥٩﴾  
 وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ  
 تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَءَاخِرِينَ مِنْ دُونِهِمْ  
 لَا تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ ۚ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي  
 سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿٦٠﴾

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ لَمْ يَكُ مُغَيِّرًا نِعْمَةً  
 أَنْعَمَهَا عَلَىٰ قَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا  
 بِأَنْفُسِهِمْ ۗ وَأَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ  
 ﴿٥٣﴾ كَذَّابِ ۖ آلِ فِرْعَوْنَ ۖ  
 وَالَّذِينَ مِنَ قَبْلِهِمْ ۚ كَذَّبُوا  
 بِآيَاتِ رَبِّهِمْ فَأَهْلَكْنَاهُمْ بِذُنُوبِهِمْ وَأَغْرَقْنَا  
 آلَ فِرْعَوْنَ ۚ وَكُلًّا كَانُوا  
 ظَالِمِينَ ﴿٥٤﴾

53. "Hayo ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Habadilishi kabisa neema Alizowaneemesha watu, mpaka wao wabadilishe yaliyomo ndani ya nafsi zao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kujua".

54. "Kama ada ya watu wa Firauni na waliokuwa kabla yao – walizikataa Ishara za

**Mola wao Mlezi, basi Tukawateketeza kwa madhambi yao. Na Tukawazamisha watu wa Firauni. Na wote walikuwa wenye kudhulumu".**

Allah تعالى Anaeleza juu ya Kutimiza Uadilifu Wake na kutopendelea katika Hukumu Zake, kwani Yeye Habadili neema aliyomneemesha mmoja wao, ila kwa sababu ya madhambi aliyoyatenda.

Ni kama Kauli Yake nyingine,

إِنَّ اللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنْفُسِهِمْ ۗ وَإِذَا أَرَادَ اللَّهُ بِقَوْمٍ سُوءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُ ۗ  
وَمَا لَهُمْ مِّنْ دُونِهِ مِّنْ وَّالٍ ﴿٥٣﴾

***“Hakika Mwenyezi Mungu Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo nafsini mwao. Na Mwenyezi Mungu Anapo watakia watu adhabu hakuna cha kuzuia wala hawana Mlinzi yeyote badala Yake.” (13:11)***

Kauli ya Allah تعالى،

كَذَّابٍ ءَالَ فِرْعَوْنَ

***“Kama ada ya watu wa Firauni”.***

Maana yake: Kama Alivyowafanyia watu wa Firauni na walio mfano wao, walipozikadhibisha Aya Zake, Aliwahilikisha kwa sababu ya madhambi yao na Akawanyang’anya neema Alizowapa miongoni mwa mabustani, chemchem, mazao, hazina na makazi mazuri na neema nyingine walizozifurahia. Wala Allah تعالى Hakuwadhulumu katika hilo, bali wao wenyewe ndio waliodhulumu.

إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِنْدَ اللَّهِ الَّذِينَ كَفَرُوا فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٤﴾ الَّذِينَ عَاهَدتَّ مِنْهُمْ ثُمَّ  
يَنْقُضُونَ عَهْدَهُمْ فِي كُلِّ مَرْجٍ وَهُمْ لَا يَتَّقُونَ ﴿٥٥﴾ فَإِذَا تَقَفَّيْتُمْ فِي الْحَرْبِ  
فَشَرَّدَ بِهِمْ مَن حَلَفْتُمْ لَعَلَّهُمْ يَدْكُرُونَ ﴿٥٦﴾

***55. “Hakika vinyama vilio viovu kabisa mbele ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaokufuru, basi hao hawaamini”.***

***56. “Wale ambao miongoni mwao umepatana nao ahadi, kisha wanavunja ahadi yao kila mara, wala hawamchi Mungu”.***

***57. “Basi ukiwakuta vitani wakimbize walio nyuma yao ili wapate kukumbuka”.***

### Amri ya Kuwapiga Vikali Makafiri na Wanaovunja Mikataba.

Allah تعالی Alijulisha kwamba kiumbe muovu zaidi kuliko wote wanaotembea juu ya uso wa dunia ni wale wanaokufuru, ambao hawaingiwi na Imani, ambao kila wanapotoa ahadi huzivunja au wanapokokotezea kwa kula yamini kuhusu Imani huvunja ahadi zao.

وَهُمْ لَا يَتَّقُونَ ﴿٥٤﴾

**“...wala hawamchi Mungu”.**

Maana yake: Hawamuogopi Allah تعالی juu ya dhambi yoyote wanayoifanya.

فَأِمَّا تَثْقَفَنَّهُمْ فِي الْحَرْبِ

**“Basi ukiwakuta vitani...”.**

Maana: Iwapo utawapiga na kuwashinda katika vita.

فَشَرَّدَ بِهِم مِّنْ خَلْفَهُمْ

**“...wakimbize walio nyuma yao...”.**

Maana yake: Wape adhabu. Hayo ni kwa mujibu wa upokezi wa Ibn ‘Abbas, Al-Hasan, Adh-Dhahhak, As-Suddi, Ataa Al-Khuraasani na Ibn ‘Uyayna رضي الله عنهم<sup>1</sup>. Walisema maana yake, wape adhabu ngumu na mateso yenye kuua. Ili Waarabu na wengine wasiokuwa wao waogope, na wapate mazingatio kutokana nao,

لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٥٥﴾

**“...ili wapate kukumbuka”.**

As-Suddi alisema, “Ili wawe na hadhari kwamba wakivunja mikataba na wao watafanyiwa kama hao.”<sup>2</sup>

وَإِمَّا نَحْنُ بِمِنْ قَوْمٍ خِيَانَةٌ فَانْبِذْ إِلَيْهِمْ عَلَى سَوَاءٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِبِينَ ﴿٥٦﴾

**58. “Na ukichelea khiana kwa watu fulani basi watupilie ahadi yao kwa usawa. Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi makhaini”.**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:23-24.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:24.

**Amri ya Kuuvunja Mkataba ili Wawe Sawa.**

Allah تعالیٰ Anamuambia Mtume ﷺ,

وَلِمَا تَخَافُونَ مِنْ قَوْمٍ

**“Na ukichelea khiana kwa watu fulani”.**

Uliwekeana nao mkataba.

خِيَانَةً

**“...khiana”.**

Maana: Kuvunjwa makubaliano baina yako na wao katika mkataba.

فَأَنْذِرْ لَهُمْ

**“...basi watupilie ahadi yao”.**

Maana yake: Mkataba wao utupilie mbali.

عَلَىٰ سَوَاءٍ

**“...kwa usawa”.**

Maana yake: Wajulishe kwamba wewe umevunja mkataba wao, ili ijulikane kuna hali ya vita baina yako na wao. Hapo wewe utakuwa sawa nao katika hilo la kutojilazimisha na utelekezaji wa mkataba.

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْخَائِبِينَ ﴿٥٤﴾

**“Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi makhaini”.**

Maana yake: Hata kama ni kwa upande wa makafiri, Allah تعالیٰ Hawapendi pia. Imamu Ahmad alimnukuu Sulaym bin ‘Amir kwamba alisema: “Mu’awiyah alikuwa akipita (na jeshi) katika ardhi ya Roma na kulikuwepo baina yao na wao kipindi cha mkataba. Akataka kuwasogelea, ili muda utakapomalizika awapige vita. Kukatokea mzee amempanda mnyama akasema: “Allahu Akbar (Allah تعالیٰ ni Mkubwa), “Allahu Akbar (Allah ni Mkubwa)! Tekelezeni, wala msisaliti, hakika Mtume ﷺ alisema:

«وَمَنْ كَانَ بَيْنَهُ وَبَيْنَ قَوْمٍ عَهْدٌ فَلَا يَحُلُّنَّ عُقْدَةً وَلَا يَشُدُّهَا حَتَّىٰ يَنْقُضِي أَمَدَهَا، أَوْ يَبْنُدَ إِلَيْهِمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ»

*“Mwenye kuweka mkataba baina yake na kaumu yeyote, basi asiifungue sehemu yoyote ya mkataba huo, wala asiizidisha kuitilia nguvu, mpaka umalizike muda wake au auvunje mkataba, ili pande zote ziwe sawa”.*

Hayo yakamfikia Mu’awiyah, akarejea. Tahamaki walimkuta mzee huyo alikuwa ‘Amr bin ‘Abasah”<sup>1</sup>.

Hadithi hii ameipokea Abu Dawud, At-Tayalisi, At-Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Hibban katika *Sahih* yake. At-Tirmidhi alisema, “Ni *Hasan Sahih*”<sup>2</sup>.

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا سَبِقُوا إِيَّاهُمْ لَا يُعْجِزُونَ ﴿٥٩﴾ وَأَعِدُوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ  
وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ تُرْهِبُونَ بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ وَءَاخِرِينَ مِنْ دُونِهِمْ لَا  
تَعْلَمُونَهُمُ اللَّهُ يَعْلَمُهُمْ ۗ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا  
تُظْلَمُونَ ﴿٦٠﴾

**59. “Na wala wasidhanie wale waliokufuru kwamba wao wametangulia mbele. La, wao hawatashinda”.**

**60. “Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi waliofungwa tayari – tayari, ili kuwatishia maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu na wengineo ambao hamuwajui, lakini Mwenyezi Mungu Anawajua. Na chochote mtakachokitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu mtarudishiwa, na wala nyinyi hamtadhulumiwa”.**

<sup>1</sup> Ahmad 4:111.

<sup>2</sup> Abu Dawud At-Tayalis 157, Abu Dawud 3:190, Tuhfatul Ahwadhi 5:203, Annasai 5:223 na Ibn Hibban 7:182.

## Amri ya Kufanya Maandalizi Kadri Iwezekanavyo Mpaka Watishike Maadui wa Allah, Zipate Khofu Nyoyo Zao.

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ, wala usidhani ewe Muhammad ﷺ kwamba,

الَّذِينَ كَفَرُوا سَبَقُوا

**“...wale waliokufuru kwamba wao wametangulia mbele...”.**

Maana yake: Wametangulia na kwamba Sisi Hatukuwaweza, bali wao wako chini ya uwezo Wetu na kutolewa roho kwa Utashi Wetu, wala Hawatushindi Sisi.

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ أَنْ يَسْبِقُونَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ ﴿٢٩﴾

**“Au wanadhani wanaotenda maovu kwamba watatushinda? Hukumu mbaya hiyo wanayo hukumu”. (29:4)**

Maana yake: Wanadhani. Na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا مُعْجِزِينَ فِي الْأَرْضِ وَمَا أَوْلَاهُمْ أَتَأْتُونَ الْمَصِيرُ ﴿٥٧﴾

**“Msiwadhanie waliokufuru kwamba watashinda katika nchi. Na makazi yao ni Motoni, na hakika ni maovu kweli marejeo yao”. (24:57)**

Na Kauli Yake Allah تعالى,

لَا يَغْرِبُكَ تَقَلُّبُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي الْبِلَادِ ﴿١٩٦﴾ مَتَّعٌ قَلِيلٌ ثُمَّ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٩٧﴾

**“Kabisa kusikudanganye kubakia kutangatanga kwa waliokufuru katika nchi. Hiyo ni starehe ndogo. Kisha makazi yao yatakuwa Jahannam. Na ni mahali pabaya mno pa kupumzikia”. (3:196-197)**

Kisha, Allah تعالى Aliamuru maandalizi ya zana za kivita ili kupigana nao kadiri iwezekanavyo kulingana na uwezekano wa nguvu na uwezo.

Allah تعالى Alisema:

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ

**“Basi waandalieni kama muwezavyo...”**

Kwa maana: Kadri mnavyomudu.

مِن قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ

**“...nguvu na kwa farasi waliofungwa tayari – tayari...”**

Imamu Ahmad alimnukuu ‘Uqbah bin ‘Amir رضي الله عنه akisema: Nilimsikia Mtume ﷺ akiwa katika mimbari akisema,

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ

**“...Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo...”**

«أَلَا إِنَّ الْقُوَّةَ الرَّمْيَ أَلَا إِنَّ الْقُوَّةَ الرَّمْيَ»

*“Hakika, Nguvu ni kulenga shabaha! Nguvu ni kulenga shabaha”<sup>1</sup>.*

Ameinukuu Muslim.<sup>2</sup>

Imamu Malik alimnukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alisema;

«الْخَيْلُ لثَلَاثَةِ، لِرَجُلٍ أَجْرٌ، وَلِرَجُلٍ سِنْرٌ، وَعَلَى رَجُلٍ وَزْرٌ، فَأَمَّا الَّذِي لَهُ أَجْرٌ، فَرَجُلٌ رَبَطَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَأَطَالَ لَهَا فِي مَرْجٍ أَوْ رَوْضَةٍ، فَمَا أَصَابَتْ فِي طِيلِهَا ذَلِكَ مِنَ الْمَرْجِ أَوْ الرُّوضَةِ، كَانَتْ لَهُ حَسَنَاتٍ وَلَوْ أَنَّهَا قَطَعَتْ طِيلَهَا، فَاسْتَنْتَ شَرْفًا أَوْ شَرْفَيْنِ كَانَتْ آثَارُهَا وَأَزْوَانُهَا حَسَنَاتٍ لَهُ، وَلَوْ أَنَّهَا مَرَّتْ بِنَهْرٍ فَشَرِبَتْ مِنْهُ وَلَمْ يَرِدْ أَنْ يَسْفِي بِهِ، كَانَ ذَلِكَ حَسَنَاتٍ لَهُ، فَهِيَ لِذَلِكَ الرَّجُلِ أَجْرٌ، وَرَجُلٌ رَبَطَهَا تَنْبِيًا وَتَعَفُّفًا، وَلَمْ يَنْسَ حَقَّ اللَّهِ فِي رِقَابِهَا وَلَا ظُهُورِهَا فَهِيَ لَهُ سِنْرٌ، وَرَجُلٌ رَبَطَهَا فَخْرًا وَرِيَاءً وَنَوَاءً، فَهِيَ عَلَى ذَلِكَ وَزْرٌ»

*“Farasi ni kwa ajili ya mambo matatu; kwa ajili ya mtu kulipwa, kwa ajili ya mtu kupata sitara, na kwa ajili ya mtu kupata dhambi, Ama aliye na malipo, ni mtu aliyefuga katika njia ya Allah, akamdumisha katika malisho au Bustani kile watakachokutana nacho katika kufungwa kwake kamba. Basi huwa ni mema yake. Na kama watakata kamba zao na nyayo zao zitaandikwa amali njema zake, Kama watapita katika mto wakanywa bila kusudio lake, hiyo itakuwa ni amali njema kwake. Basi farasi wa aina hii ni wa kumpatia malipo mtu huyo. Na mwengine ni mtu aliyewafuga kwa kujitosheleza na*

<sup>1</sup> Ahmad 4:156.

<sup>2</sup> Muslim 3:1522.

*kujizuilia kuomba, na hakusahau haki ya Allah تعالى kuhusiana na shingo na migongo yao, basi hao ni stara kwake. Na mtu mwingine ni yule aliyewafuga kwa ufakhari, ria na kujifanyisha, basi huyo atapata madhambi juu ya hilo.”*

Mtume ﷺ aliulizwa juu ya punda, akasema:

«مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَيَّ فِيهَا شَيْئًا إِلَّا هَدَيْهِ الْجَمِيعَةَ الْفَادَةَ»

*“Allah تعالى Hajaniteremshia chochote kuhusu huyo, isipokuwa punda hukumu yake inaingia katika Aya hii”. Kisha akasoma,*

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧٧﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٧٨﴾

***“Basi anayetenda chembe ya wema, atauona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona!” (99:7-8)<sup>1</sup>***

Aliinukuu Bukhari, na hilo ni tamko lake yeye na Muslim<sup>2</sup>.

Imamu Ahmad alimnukuu ‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه, alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْخَيْلُ ثَلَاثَةٌ: فَفَرَسٌ لِلرَّحْمَنِ، وَفَرَسٌ لِلشَّيْطَانِ، وَفَرَسٌ لِلْإِنْسَانِ، فَأَمَّا فَرَسُ الرَّحْمَنِ فَالَّذِي يُرْبَطُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، فَعَلَّمَهُ وَرَوَّعَهُ وَبَوَّأَهُ - وَذَكَرَ مَا شَاءَ اللَّهُ - وَأَمَّا فَرَسُ الشَّيْطَانِ، فَالَّذِي يُقَامَرُ أَوْ يُرَاهَنُ عَلَيْهَا، وَأَمَّا فَرَسُ الْإِنْسَانِ، فَالْفَرَسُ يَرْبِطُهَا الْإِنْسَانُ يَلْتَمِسُ بَطْنَهَا، فَيَبِي لَهْ سِتْرٌ مِنَ الْفَقْرِ»

*“Farasi ni namna tatu: Farasi kwa ajili ya Ar-Rahman, farasi kwa ajili ya shetani, na farasi kwa ajili ya mwanadamu. Ama farasi kwa ajili ya Allah تعالى ni anayefugwa katika njia ya Allah, na ni hivyo hivyo chakula chake, choo na mkojo wake – akataja vitu vingi. Ama farasi wa shetani ni yule anayetumiwa katika kamari au rehani. Farasi wa mwanadamu ni yule ambaye mwanadamu humfuga kwa ajili ya manufaa yake. Huyo ni stara kwake dhidi ya ufakiri”<sup>3</sup>.*

Katika Sahih Bukhari, kuna nukuu kuwa ‘Urwah bin Abu Al-Ja’d Al-Bariqi رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

<sup>1</sup> Al-Muwatta 2:414.

<sup>2</sup> Al-Bukhari 6:66 na Muslim 987.

<sup>3</sup> Ahmad 1:395.



«الْخَيْلُ مَعْقُودٌ فِي نَوَاصِيهَا الْخَيْرُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، الْأَجْرُ وَالْمَنْعَمُ»

“Farasi amefungwa katika utosi wake kheri mpaka Siku ya Kiyama, nayo ni malipo na ghanima.”<sup>1</sup>

Kauli ya Allah تعالى،

تُرْهِبُونَ

“...*ili kuwatishia*...”. Maana yake: Kuwatia khofu,

بِهِ عَدُوَّ اللَّهِ وَعَدُوَّكُمْ

“...*maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu*...”.

Maana yake: Katika makafiri.

وَأَخْرَجْنَا مِنْ دُونِهِمْ

“...*na wengineo*...”. Mujahid alisema, maana yake hapa wanakusudiwa Banu Quraidhah<sup>2</sup>. As-Suddi alisema: Ni Wafursi<sup>3</sup>.

Muqatil bin Hayyan na ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam walisema: “Maana yake ni wanafiki”<sup>4</sup>. Hilo linaungwa mkono na Kauli ya Allah تعالى،

وَمِمَّنْ حَوْلَكُم مِّنَ الْأَعْرَابِ مُنْفِقُونَ<sup>ط</sup> وَمِنَ أَهْلِ الْمَدِينَةِ<sup>ط</sup> مَرَدُوا عَلَى النِّفَاقِ لَا

تَعْلَمُهُمْ<sup>ط</sup> حَتَّى نَعْلَمَهُمْ<sup>ط</sup>

“*Na katika mabedui walio jirani zenu wamo wanafiki; na katika wenyeji wa Madina pia wapo waliobobea katika unafiki. Wewe huwajui. Sisi Tunawajua*...”. (9:101)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يُوَفَّ إِلَيْكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تُظْلَمُونَ ﴿١٠١﴾

“*Na mkatoa chochote katika njia ya Mwenyezi Mungu mtarudishiwa, na wala nyinyi hamtadhulumiwa.*”

<sup>1</sup> Fat’hul-Al-Bari 6:66.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:36.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:36.

<sup>4</sup> Ahmad 1:90.

Maana yake: Kadiri mtakavyotoa katika Jihadi, basi hicho kitalipwa kwenu kwa utimilifu na ukamilifu. Sawa na Kauli ya Allah تعالى iliyotangulia,

مَثَلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثَلِ حَبَّةٍ أَنْبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلٍ فِي كُلِّ سُنبُلَةٍ  
مِائَةٌ حَبَّةٌ وَاللَّهُ يُضْعِفُ لِمَنْ يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٥٦﴾

***“Mfano wa wanaotumia mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyo chipuza mashuke saba. Katika kila shuke zimo punje mia. Na Mwenyezi Mungu Humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mwenye Kujua”. (2:261)***

\* \* \*

\* وَإِنْ جَنَحُوا لِلسَّلَامِ فَاجْتَنَحْهَا وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ هُوَ  
 السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦١﴾ وَإِنْ يُرِيدُوا أَنْ يَخَذَعُوكَ فَإِنَّ  
 حَسْبَكَ اللَّهُ هُوَ الَّذِي آتَاكَ بِنَصْرِهِ وَبِالْمُؤْمِنِينَ  
 ﴿٦٢﴾ وَأَلْفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ لَوْ أَنْفَقْتَ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا  
 مَا أَلْفَتْ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ أَلْفَ بَيْنَهُمْ إِنَّهُ  
 عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٣﴾ يَأَيُّهَا النَّبِيُّ حَسْبَكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ  
 مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٤﴾ يَأَيُّهَا النَّبِيُّ حَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ  
 عَلَى الْقِتَالِ إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ عَشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُوا  
 مِائَتِينَ إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ يَغْلِبُوا أَلْفًا مِنَ الَّذِينَ  
 كَفَرُوا بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٦٥﴾ أَلَسَنَ خَفَفَ اللَّهُ  
 عَنْكُمْ وَعَلِمَ أَنَّ فِيكُمْ ضَعْفًا فَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ  
 صَابِرَةٌ يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ أَلْفٌ يَغْلِبُوا أَلْفَيْنِ  
 بِإِذْنِ اللَّهِ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٦٦﴾ مَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَنْ  
 يَكُونَ لَهُ أَسْرَى حَتَّى يُفْجِرَ فِي الْأَرْضِ تَرِيدُوتَ  
 عَرَضَ الدُّنْيَا وَاللَّهُ يُرِيدُ الْآخِرَةَ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٧﴾  
 لَوْلَا كِتَابٌ مِنَ اللَّهِ سَبَقَ لَمَسَّكُمْ فِيمَا أَخَذْتُمْ عَذَابٌ  
 عَظِيمٌ ﴿٦٨﴾ فَكُلُوا مِمَّا غَنِمْتُمْ حَلَالًا طَيِّبًا وَاتَّقُوا اللَّهَ

إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٦٩﴾

\* وَإِنْ جَنَحُوا لِلسَّلَامِ فَاجْتَنَحْهَا  
 وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ  
 الْعَلِيمُ ﴿٦١﴾ وَإِنْ يُرِيدُوا أَنْ  
 يَخَذَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ اللَّهُ هُوَ  
 الَّذِي آتَاكَ بِنَصْرِهِ  
 وَبِالْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾ وَأَلْفَ بَيْنَ  
 قُلُوبِهِمْ لَوْ أَنْفَقْتَ مَا فِي الْأَرْضِ  
 جَمِيعًا مَا أَلْفَتْ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ  
 وَلَكِنَّ اللَّهَ أَلْفَ بَيْنَهُمْ إِنَّهُ عَزِيزٌ  
 حَكِيمٌ ﴿٦٣﴾

61. "Na wakielekea amani nawe pia elekea, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kujua".

62. "Na wakitaka kuku-khadaa basi Mwenyezi Mungu Atakutosheleza. Kwani Yeye Ndiye Aliyekuunga mkono kwa nusura Yake kwa Waumini".

63. "Na Akaziunga nyoyo zao. Na lau wewe ungelitoa vyote vilivyomo duniani usingeliweza kuzifunga

nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyewaunganisha. Hakika Yeye Ndiye Mtukufu Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima".

**Amri ya Kufanya Suluhu Kama Adui Ataomba Hivyo.**

Allah تعالى Anasema, ikiwa utakhofia khiyana kwa watu hao basi utupilie mbali mkataba wao wa amani ili muwe sawa katika kuacha kuutekeleza. Ikiwa wataendelea kukupiga vita na kuvunja mkataba basi pigana nao.

﴿ وَإِنْ جَنَحُوا ﴾

**“Na wakielekea...”.**

Kwa maana yake: Wakionesha ishara ya,

لِلسَّلَامِ

**“...amani...”.**

Wakataka Amani, Suluhu na Mikataba.

فَأَجْنَحْ هَا

**“...nawe pia elekea...”.**

Maana yake: Onesha ishara, na uwakubalie hilo. Hili ni pale Washirikina walipotaka suluhu, katika mwaka wa Al-Hudaybiyah, na kuacha vita baina yao na Mtume ﷺ kwa miaka tisa. Aliwajibu hilo, pamoja na masharti mengine waliyoyaweka katika mkataba. ‘Abdullah bin Al-Imam Ahmad alinukuu kuwa ‘Ali bin Abu Talib رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّهُ سَيَكُونُ بَعْدِي اخْتِلَافٌ أَوْ أَمْرٌ فَإِنْ اسْتَطَعْتَ أَنْ يَكُونَ السَّلْمَ فَافْعَلْ»

*“Kutakuwepo na khitilafu au jambo baada yangu, ukiweza kuliondoa kwa njia ya amani, basi fanya hivyo.”<sup>1</sup>*

وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ

**“...na mtegemee Mwenyezi Mungu...”**

Fanya nao suluhu na tawakali kwa Allah تعالى, kwani Yeye Anakutosha, Atakunusuru, hata kama wana lengo la kukuhadaa katika kufanya kwao suluhu, ili waweze kukusanya nguvu na kujiandaa upya.

<sup>1</sup> Ahmad 1:90.

فَارِبْ حَسْبِكَ اللَّهُ

**“...basi Mwenyezi Mungu Atakutosheleza.”** Kwa maana: Yeye Peke Yake Atakidhi haja zako zote.

**Ukumbusho kwa Waumini juu ya Neema ya Kuziunganisha Nyoyo Zao.**

Kisha Allah تعالى Akataja neema Zake kwa Mtume ﷺ kwa Kumpa nguvu kwa Kuwapa waumini ambao ni Muhajirina na Ansar. Alisema,

هُوَ الَّذِي أَيْدَكَ بِنَصْرِهِ وَيَا الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦١﴾ وَأَلْفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ

**“Yeye Ndiye Aliyekuunga mkono kwa Nusura Yake na kwa Waumini. Na Akaziunga nyoyo zao...”**

Kwa maana: Kuwakusanya Kwake katika kukuamini wewe, kukutii, kukusaidia na kukuunga mkono,

لَوْ أَنْفَقْتَ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مَا أَلْفَتَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ

**“...Na lau wewe ungelitoa vyote vilivyomo duniani usingeliweza kuzifunga nyoyo zao...”**

Maana: Kutokana na uadui na chuki baina yao, kwani Ansar walikuwa na vita vingi baina yao katika zama za ujahili, baina ya makabila ya Awsi na Khazraji na kulikuwa na mambo mengi yaliyochochea kuleta shari baina yao. Mpaka Allah تعالى Alipoyaondoa hayo kwa Kuwaletea nuru ya Imani. Kama Alivyosema:

وَأَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلْفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا

وَكُنْتُمْ عَلَى شَفَا حُفْرَةٍ مِنَ النَّارِ فَأَنْقَذَكُمْ مِنْهَا كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ

تَهْتَدُونَ ﴿٦٢﴾

**“Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyokuwa nyinyi kwa nyinyi maadui Naye Akaziunganisha nyoyo zenu: kwa neema Yake mkawa Ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, Naye Akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu Anakubainishieni Ishara Zake ili mpate kuongoka”. (3:103)**

Katika Sahihi Mbili Bukhari na Muslim wamenukuu kwamba, Mtume ﷺ pindi alipowahutubia Ansar, kuhusu suala la ngawira za Hunayn, aliwaambia:

«يَا مَعْزَرَ الْأَنْصَارِ أَلَمْ أَجِدْكُمْ ضَلَالًا فَهَدَاكُمْ اللَّهُ بِِي، وَعَالَةً فَأَغْنَاكُمْ اللَّهُ بِِي،  
وَكُنْتُمْ مُتَفَرِّقِينَ فَأَلَّفَكُمُ اللَّهُ بِِي»

*"Enyi kundi la Ansar! Je sikuwakuteni mkiwa mmepeotea, basi Allah تعالى Akakuongoeni kupitia kwangu, na mkiwa masikini, Allah تعالى Akakutajirisheni kupitia kwangu na mlikuwa mliofarakana, Allah تعالى Akakuunganisheni kupitia kwangu?"*

Kila aliposema jambo, walisema, "Allah تعالى na Mtume ﷺ ndio wenye fadhila nyingi"<sup>1</sup>. Kwa ajili hii Allah تعالى Alisema:

اللَّهُ أَلْفَ بَيْنَهُمْ إِنَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٤﴾

***"...Jakini Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyewaunganisha. Hakika Yeye Ndiye Mtukufu Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima".***

يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ حَسْبُكَ اللَّهُ وَمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٥﴾ يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ حَرَضِ  
الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ ۚ إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ عَشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُوا مِائَتِينَ ۚ وَإِنْ يَكُنْ  
مِنْكُمْ مِائَةٌ يَغْلِبُوا أَلْفًا مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٦٦﴾ أَلْقَنَ  
خَفَفَ اللَّهُ عَنْكُمْ وَعَلِمَ أَنَّ فِيكُمْ ضَعْفًا ۚ فَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ صَابِرَةٌ يَغْلِبُوا مِائَتِينَ ۚ  
وَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ أَلْفٌ يَغْلِبُوا أَلْفِينَ بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ مَعَ الصَّابِرِينَ ﴿٦٧﴾

**64. "Ewe Nabii! Mwenyezi Mungu Anakutosheleza wewe na Waumini waliokufuata".**

**65. "Ewe Nabii! Wahimize Waumini waende vitani. Wakiwapo kati yenu ishirini wanaosubiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo kati yenu mia watawashinda elfu moja katika waliokufuru. Kwa sababu wao ni watu wasiofahamu".**

**66. "Sasa Mwenyezi Mungu Amekupunguzieni, na Anajua kuwa upo udhaifu kwenu. Kwa hivyo wakiwa wapo watu mia moja kati yenu wenye kusubiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo elfu moja watawashinda elfu mbili kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wenye kusubiri".**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 7:644 na Muslimu 2:738.

## Uhamasishaji juu ya Kupigana na Adui, na Bishara kwamba Waislamu Wachache Wanaweza Kuwashinda Makafiri Wengi

Allah تعالى Anamuhimiza Nabii Wake na Waumini juu ya kupigana, kupambana dhidi ya adui na kuendesha vita vya *Mubaaraza* (ana kwa ana). Pia Anawajuza khabari, kwamba Yeye Anatosha, Atawasaidia, Atawapa nguvu dhidi ya adui, hata kama maadui wao watakuwa wengi kwa idadi, na silaha nyingi za kisiasa, na hata kama idadi ya Waislamu itakuwa chache. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema:

يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ حَرَضِ الْمُؤْمِنِينَ عَلَى الْقِتَالِ

**“Ewe Nabii! Wahimize Waumini waende vitani...”** Maana yake: Wahimize au washajiishe juu ya hilo. Kwa ajili hiyo, Mtume ﷺ alikuwa akihimiza kupigana pale anapokabiliana na adui. Kama alivyowaambia Masahaba wake katika vita vya Badr, wakati alipokabiliana na Washirikina waliokuwa na idadi kubwa ya majeshi na silaha nyingi.

«قَوْمُوا إِلَىٰ جَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ»

*“Simameni muipiganie pepo ambayo, upana wake ni kama mbingu na ardhi”.*

‘Umayri bin Al-Hammam رضي الله عنه akauliza, “Upana wake ni kama mbingu na ardhi?” Mtume ﷺ akamjibu:

«نَعَمْ»

*“Ndiyo”.* Akasema, “Vizuri sana! Vizuri sana!” Mtume ﷺ akasema:

«مَا يَحْمِلُكَ عَلَىٰ قَوْلِكَ: بَخٍ بَخٍ»

*“Nini kinachokufanya useme, “Vizuri sana! Vizuri sana!?”.* Akasema, “Natumaini kwamba nitakuwa miongoni mwa wakazi wake”. Mtume ﷺ akasema,

«فَإِنَّكَ مِنْ أَهْلِهَا»

*“Wewe ni katika watu wake”.* Mtu huyo (‘Umayr) akasonga mbele katika mapambano na akavunja ala ya upanga wake, akatoa tende kadhaa na kuanza kuzila. Kisha akatupa zilizosalia mkononi mwake, akasema: “Ikiwa nitaishi mpaka nimalize tende hizi, huo utakuwa uhai mrefu,” Kisha akaingia mapambanoni, akapigana mpaka akauawa.<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Muslim 3:1511.

Kisha, Allah تعالى Akawapa bishara Waumini na kuwaamuru, kuwa:

إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ عِشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ ۚ وَإِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ مِائَةٌ يَغْلِبُوا أَلْفًا مِّنَ الَّذِينَ كَفَرُوا

**“Wakiwapo kati yenu ishiriniwanaosubiri watawashinda mia mbili. Na wakiwapo kati yenu mia watawashinda elfu moja katika walio kufuru”.**

Kila Muislamu mmoja kwa Washirikina kumi. Baadaye, Allah عزوجل Akafuta hukumu ya Ayah hii na kubakia bishara. ‘Abdullah bin Al-Mubarak alisema, Jarir bin Hazim alitueleza, Az-Zubayr bin Al-Khirrit kutoka kwa ‘Ikrimah kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Iliposhuka,

إِنْ يَكُنْ مِنْكُمْ عِشْرُونَ صَابِرُونَ يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ

**“...Wakiwapo kati yenu ishirini wanaosubiri watawashinda mia mbili...”**. Hilo likawa zito kwa Waumini, mpaka Allah تعالى Akawalazimisha kwamba Muislamu yeyote asiwakimbie Washirikina kumi. Kisha takhfifu ikaja, Allah تعالى Akasema:

الَّذِينَ خَفَّفَ اللَّهُ عَنْكُمْ

**“...Sasa Mwenyezi Mungu Amekupunguzieni...”** Inaendelea mpaka katika Kauli Yake,

يَغْلِبُوا مِائَتَيْنِ

**“...watawashinda mia mbili...”**. Kwamba, “Allah تعالى Aliwapunguzia idadi na kuipunguza subira iliyohitajika, kwa kiasi cha hesabu waliyopunguziwa”<sup>1</sup>. Al-Bukhari alinukuu sawa na hivyo kutoka katika Hadithi ya Ibn Al-Mubarak.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, kwamba Aya hii iliposhuka, jambo hilo likawa zito kwa Waislamu na wakauona uzito watu ishirini kupigana na watu mia mbili, na watu mia moja kwa elfu moja. Allah تعالى Akawafanyia takhfifu hukumu hiyo na Akaifuta kwa Ayah nyingine,

الَّذِينَ خَفَّفَ اللَّهُ عَنْكُمْ وَعَلِمَ أَنَّ فِيكُمْ ضَعْفًا

**“Sasa Mwenyezi Mungu Amekupunguzieni, na Anajua kuwa upo udhaifu kwenu”.**

<sup>1</sup> Abu Dawud 3:105.



Hivyo, "Itakapokuwa Waislamu idadi yao ni nusu ya adui yao, hawakuruhusiwa kuwakimbia, na iwapo watakuwa pungufu zaidi ya hivyo, si wajibu juu yao kupigana na adui yao na wakaruhusiwa kuwakwepa na kuwaepuka."<sup>1</sup>

مَا كَانَ لِنَبِيِّ أَنْ يَكُونَ لَهُدَّ أَسْرَىٰ حَتَّىٰ يُخْرَجَ فِي الْأَرْضِ تَرْيَدُونَ عَرَضَ الدُّنْيَا  
وَاللَّهُ يُرِيدُ الْآخِرَةَ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٦٧﴾ لَوْلَا كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ لَمَسَّكُمْ فِيمَا  
أَخَذْتُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٦٨﴾ فَكُلُوا مِمَّا عَنِمْتُمْ حَلَالًا طَيِّبًا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ  
رَّحِيمٌ ﴿٦٩﴾

**67. "Haimfalii Nabii yeyote kuwa na mateka mpaka awe ameshinda katika nchi. Mnataka vitu vya dunia, na Mwenyezi Mungu Anataka Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye Nguvu Mwenye Hekima".**

**68. "Lau isingelikuwa hukumu iliyokwishatangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu ingelikupateni adhabu kubwa kwa vile mlivyochukua".**

**69. "Basi kuleni katika mlivyoteka, ni halali na vizuri, na Mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu".**

Imamu Ahmad alimnukuu Anas رضي الله عنه kuwa alisema: Mtume ﷺ aliwataka ushauri watu kuhusu mateka wa vita vya Badr, akasema:

«إِنَّ اللَّهَ قَدْ أَمَنَكُم مِّنْهُمْ»

"Allah Amekujaalieni muwashinde".

'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه akasimama na kusema, "Ewe Mtume! Zikate shingo zao". Mtume ﷺ akampa kisogo. Kisha Mtume ﷺ akarejea kusema:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّ اللَّهَ قَدْ أَمَنَكُم مِّنْهُمْ وَإِنَّمَا هُمْ إِخْوَانُكُمْ بِالْأَمْسِ»

"Enyi watu! Allah تعالی Amekujaalieni muwashinde, na wao ni jana tu walikuwa Ndugu zenu".

<sup>1</sup> Al-Bukhari 4652-4653.

'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه akasimama na kusema, "Ewe Mtume! Zikate shingo zao". Mtume ﷺ akampa kisogo. Kisha Mtume ﷺ akarejea tena kuwaambia watu maneno yale yale. Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه alisimama, akasema: "Ewe Mtume! Tuna rai kwamba uwaachilie kwa kupokea fidia kwa ajili yao". Huzuni iliyodhihiri usoni mwa Mtume ﷺ ikaondoka. Akawasamehe na kupokea fidia zao. Allah تعالى Akateremsha,

لَوْلَا كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ لَمَسَّكُمْ فِيمَا أَخَذْتُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٦١﴾

***"Lau isingelikuwa hukumu iliyokwishatangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu ingelikupateni adhabu kubwa kwa vile mlivyo chukua."***<sup>1</sup>

'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

لَوْلَا كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ

***"Lau isingelikuwa hukumu iliyokwishatangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu."***

Maana: Katika sheria mama iliyotumika huko nyuma yakuwa imeandikwa kwamba Ngawira "ghanima" na mateka ni mambo yaliyo halali kwenu,

لَمَسَّكُمْ فِيمَا أَخَذْتُمْ

***"...ingelikupateni kwa vile mlivyochukua..."***. Kutokana na mateka,

عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿٦٢﴾

***"...adhabu kubwa"***. Allah تعالى Alisema,

فَكُلُوا مِمَّا غَنِمْتُمْ حَلَالًا طَيِّبًا

***"Basi kuleni katika mlivyoteka, ni halali na vizuri..."***

Pia hivyo ndivyo Al-'Awfi alivyosimulia aya hii kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما. Kauli kama hiyo ilisimuliwa kutoka kwa Abu Hurayrah, Ibn Mas'ud, Sa'id bin Jubayr, 'Ata, Al-Hasan Al-Basri, Qatadah na Al-A'mash رضي الله عنهم<sup>3</sup>. Wote wakisema kwamba makusudio ya,

<sup>1</sup> Ahmad 3:243.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:65.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:65-69.

لَوْلَا كِتَابٌ مِّنَ اللَّهِ سَبَقَ

**“...Lau isingelikuwa hukumu iliyokwihatangulia kutoka kwa Mwenyezi Mungu...”**

Kwa ummah huu kuhalalishwa Ngawira. Kauli hii inaungwa mkono na Hadithi iliyopokelewa katika Sahih Mbili kuwa Jubayr bin ‘Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أُعْطِيتُ حَنْمًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ قَبْلِي: نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ، وَجُعِلَتْ لِي الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهْرًا، وَأَجِلَّتْ لِي الْغَنَائِمُ وَلَمْ تُحَلَّ لِأَحَدٍ قَبْلِي، وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ، وَكَانَ النَّبِيُّ يُعْتَقُ إِلَى قَوْمِهِ، وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

*“Nimepewa mambo matano, hakupewa Nabii yeyote kabla yangu. Nimenusuriwa kwa kumtishia adui kwa masafa ya mwenendo wa mwezi mmoja, na ardhi imefanywa kwangu kuwa mahali pa kusali na kitoharisho. Nimehalalishiwa ghanima, na hakuhalalishiwa yeyote kabla yangu. Nimepewa jambo la kuombea shufaa. Na ilikuwa Nabii akipelekwa kwa kaumu yake tu mimi nimetumwa kwa watu wote”<sup>1</sup>.*

Al-A'mash amepokea kutoka kwa Abu Swalih kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema: Mtume ﷺ alisema:

«لَمْ تَحِلَّ الْغَنَائِمُ لِسُودِ الرُّؤُوسِ غَيْرَنَا»

*“Ghanima hazikuruhusiwa kwa mwanadamu yeyote, isipokuwa sisi”.*

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema,

فَكُلُوا مِمَّا غَنِمْتُمْ حَلَالًا طَيِّبًا

**“Basi kuleni katika mlivyoteka, ni halali na vizuri...”<sup>2</sup>**

Waislamu walichukua fidia kwa mateka. Imamu Abu Dawud alinukuu katika Sunan yake kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema; Mtume ﷺ alihukumu fidia kwa mateka makafiri baada ya vita vya Badr Dirham mia nne<sup>3</sup>. jopo la

<sup>1</sup> Fat'h Al-Bari 1:519 na Muslim 1:370.

<sup>2</sup> An-Nasai katika Al-Kubra 6:352.

<sup>3</sup> Abu Dawud 3:139.

wanazuoni wa Kiislamu wamesema kuwa suala la mateka wa kivita ni uamuzi wa Imamu. Akitaka atawaua kama ilivyokuwa kwa Banu Quraidhwah, na akitaka atachukua fidia kama walivyofanyiwa mateka wa Badr, au kubadilishana na mateka Waislamu, kama Mtume ﷺ alivyofanya kwa mwanamke mateka na bintiye, walipokamatwa na Salamah bin Al-Akwi' aliwarudisha kubadilishana na Waislamu waliotekwa na Washirikina. Na Imamu akitaka anaweza kuwafanya watumwa mateka hao.



يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ قُل لِّمَن فِي أَيْدِيكُمْ  
 مِنَ الْأَسْرَىٰ إِن يَعْلَمَ اللَّهُ فِي قُلُوبِكُمْ خَيْرًا يُؤْتِكُمْ خَيْرًا مِّمَّا أُخِذَ مِنْكُمْ وَيَغْفِرَ  
 لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧٠﴾ وَإِن يُرِيدُوا خِيَانَتَكَ فَقَدْ  
 خَانُوا اللَّهَ مِن قَبْلُ فَأَمْكَنَ مِنْهُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾  
 إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي  
 سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ ءَاوَأُوا وَنَصَرُوا أُولَٰئِكَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ  
 بَعْضٍ ۗ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يُهَاجِرُوا مَا لَكُم مِّن لَّدُنِّيهِمْ مِّن  
 شَيْءٍ حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا ۗ وَإِنِ اسْتَنْصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمْ  
 النَّصْرُ إِلَّا عَلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُم مِّيثَاقٌ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ  
 بَصِيرٌ ﴿٧٢﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۗ إِلَّا تَفْعَلُوهُ  
 تَكُن فِتْنَةً فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ ﴿٧٣﴾ وَالَّذِينَ  
 ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ ءَاوَأُوا  
 وَنَصَرُوا أُولَٰئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا ۗ هُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ  
 كَرِيمٌ ﴿٧٤﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مِن بَعْدِ وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا  
 مَعَكُمْ فَأُولَٰئِكَ مِنكُمْ ۗ وَأُولَٰئِكَ الْأَرْحَامُ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ  
 فِي كِتَابِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٧٥﴾

يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ قُل لِّمَن فِي أَيْدِيكُمْ  
 مِنَ الْأَسْرَىٰ إِن يَعْلَمَ اللَّهُ فِي  
 قُلُوبِكُمْ خَيْرًا يُؤْتِكُمْ خَيْرًا مِّمَّا أُخِذَ  
 مِنْكُمْ وَيَغْفِرَ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ  
 رَّحِيمٌ ﴿٧٠﴾ وَإِن يُرِيدُوا خِيَانَتَكَ  
 فَقَدْ خَانُوا اللَّهَ مِن قَبْلُ فَأَمْكَنَ مِنْهُمْ  
 ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

70. "Ewa Nabii! Waambie mateka waliomo Mikononi mwenu: Kama Mwenyezi Mungu Akiona kheri yoyote kwenu Atakupeni bora kuliko vilivyochukuliwa kwenu, na Atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu."

71. "Ikiwa wanataka kuku-fanyia khiana, wao wali-kwishamfanyia khiana Mwenyezi Mungu kabla na Yeye Akakuwezesha Kuwa-shinda. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima."

## Ahadi kwa Mateka juu ya Kupata Mazuri Kuliko Walivyovipoteza Kama Watabadili Mwenendo.

Muhammad bin Is-haq رضي الله عنهما alisema kuwa Abdullah bin 'Abbas رضي الله عنهما alisema katika siku ya (Vita vya) Badr:

«إِنِّي قَدْ عَرَفْتُ أَنَّ أَنَا مِنْ بَنِي هَاشِمٍ وَغَيْرِهِمْ قَدْ أُخْرِجُوا كَرَمًا لَا حَاجَةَ لَهُمْ  
بِقَاتِلِنَا فَمَنْ لَقِيَ مِنْكُمْ أَحَدًا مِنْهُمْ - أَنِي مِنْ بَنِي هَاشِمٍ - فَلَا يَقْتُلُهُ، وَمَنْ لَقِيَ أَبَا  
الْبُخْتَرِيِّ بْنِ هِشَامٍ مُنْتَكِرًا»

*“Hakika Mimi najua kuwa kuna watu katika Banu Hashim na wengine wametolewa kwa nguvu (kuungana na jeshi la Washirikina), hawana haja ya kupigana nasi. Kwa hivyo miongoni mwenu atakayekutana na mmoja wao – yaani katika Banu Hashim – asimuue. Na atakayekutana na Abu Al-Bukhtari naye asimuue na atakayekutana na Abbas bin Abdi-Muttalib asimuue kwani naye amelazimishwa”.*

Abu Hudhayfah bin Ut'bah alisema, “Tuwaue baba zetu, watoto, ndugu na watu wa kabila letu (katika Qurayshi), na kumuacha Al-Abbas? Naapa kwa Allah تعالى! Nikikutana naye, nitamuua kwa upanga. Habari hii ilipomfikia Mtume ﷺ alimuambia bin Al-Khattab رضي الله عنه,

«يَا أَبَا حَفْصٍ!»

“Ewe Abu Hafs!”

«أَيْضَرَبُ وَجْهَ عَمِّ رَسُولِ اللَّهِ بِالسَّيْفِ!»

*“Je ni halali uso wa ami yake Mjumbe wa Allah kupigwa upanga?”*

Umar رضي الله عنه kasema: “Wallahi! Ilikuwa ndiyo siku ya kwanza Mtume ﷺ kuniita kwa kutumia lakabu yangu (yaani: Baba fulani), ‘Umar رضي الله عنه akasema, “Ewe Mtume ﷺ! Nipe idhini nimkate shingo yake, hakika yeye (Abu Hudhaifa), Wallah! Amekuwa Mnafiki.” Abu Hudhaifa رضي الله عنه akawa anasema baada ya hayo: “Wallah! Sina amani tena baada ya neno nililolisema, na nitaendelea kuwa na khofu isipokuwa Allah تعالى Akinifutia hayo kwa njia ya kufa shahidi.” Na ndivyo ilivyokuwa, alikufa shahidi katika vita vya Al-

<sup>1</sup> Ibn Sa'īd 4:10. Pia Taz. “Dalaail An-Nubuwa cha Al-Bayhaqi 3:140.

Yamamah<sup>1</sup>. Pia alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, jioni ya siku ya vita vya Badr na huku mateka wakiwa wamefungwa pingu, Mtume ﷺ alipitisha sehemu ya mwanzo ya usiku akiwa macho. Masahaba wake wakamuambia: “Ewe Mtume! Mbona hulali?” Na wakati huo, Al-'Abbas alikuwa ametekwa na mtu mmoja katika Ansar. Mtume ﷺ akasema,

«سَمِعْتُ أُنَيْنَ عَمِّي التَّبَّاسِ فِي وَثَاقِهِ

*“Nimesikia kilio cha maumivu cha ami yangu, Al-'Abbas kutokana na kufungwa kwake”.*

Basi wakamuachia, akanyamaza. Mtume ﷺ akalala<sup>1</sup>. Na katika Sahih Al-Bukhari, Hadithi ya Musa bin 'Uqbah, alisema Ibn Shihab alinisimulia kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa watu katika Ansar walimuomba idhini Mtume ﷺ wakasema: “Ewe Mtume! Tutamuachia huru mpwa wetu Al-'Abbas bila ya fidia”. Akasema:

«لَا وَاللَّهِ لَا تَذَرُونَنِي مِنْهُ دِرْهَمًا»

*“Hapana. Wallahi! Msiache hata Dirham moja kutokana naye”<sup>2</sup>.*

Yunus bin Bukair alisema kutoka kwa Muhammad bin Is-haq kutoka kwa Yazid bin Ruman kutoka kwa 'Urwah kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa watu kadha walimuambia, 'Makuraishi walipeleka kwa Mtume ﷺ ombi kwa ajili ya kuwakomboa mateka wao na kila kaumu ikawakomboa kwa kutoa fidia waliyoridhiana. Al-'Abbas akasema: “Ewe Mtume! nimeshasilimu”. Mtume ﷺ akasema,

«اللَّهُ أَعْلَمُ بِإِسْلَامِكَ فَإِنْ يَكُنْ كَمَا تَقُولُ فَإِنَّ اللَّهَ يُجْزِيكَ وَأَمَّا ظَاهِرُكَ فَقَدْ كَانَ عَلَيْنَا فَاقْتَدِ نَفْسَكَ وَابْنِي أَخِيكَ نَوْفَلَ بْنَ الْحَارِثِ بْنِ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ وَعَقِيلَ بْنَ أَبِي طَالِبِ بْنِ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ ، وَحَلِيفَتَكَ عُتْبَةَ بْنَ عَمْرٍو أَخِي بَنِي الْحَارِثِ بْنِ فِهْرِ»

*“Allah تعالى Anajua zaidi juu ya kusilimu kwako. Ikiwa ni sawa na usemayo, basi Allah تعالى Atakulipa. Ama muonekano wako wa nje ulikuwa ni dhidi yetu. Kwa hivyo, jikomoe nafsi yako na wana wawili wa nduguzo, Nawfal bin Al-Harith bin 'Abdul-Muttwalib na 'Aqil bin Abu Twalib bin 'Abdul-Muttwalib, na pia rafiki yako, 'Utbah bin 'Amri na ndugu wa Banu Al-Harith bin Fihri”.*

<sup>1</sup> Ibn Sa'id 4:13. Pia Dalaail An-Nubuwa cha Al-Baihaq 3/141 Isnadi yake ni Sahihi.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 7:373.

Al-Abbas رضي الله عنه akasema, "Mimi sina mali ewe Mtume!"

دَفَائِنَ الْمَالِ الَّذِي دَفَنْتَهُ أَنْتَ وَأُمُّ الْقَضَلِ فَقُلْتَ لَهَا: إِنْ أَصَبْتُ فِي سَفَرِي هَذَا،  
فَهَذَا الْمَالُ الَّذِي دَفَنْتَهُ لِي فِي الْفَضْلِ وَعَبْدِ اللَّهِ وَنُتْمِ؟

*"Iko wapi mali uliyoizika wewe na Ummu Al-Fadhli, nawe ukamuambia, "Nikiuawa katika safari yangu hii (vita hivi). Basi mali hii niliyoizika ni kwa ajili ya Banu Al-Fadhli, 'Abdullah na Qutham."*

Akasema: "Wallah! Ewe Mtume ninajua kwamba wewe ni Mtume! Hili ni jambo ambalo hapana aliyelijua ghairi yangu mimi na Umm Al-Fadhli. Kwa hivyo, Ewe Mtume! Hesabu kiasi cha (uzito wa) *Uwqiyah* ishirini mlizochukua katika mali yangu." Mtume ﷺ akasema:

«لَا ذَاكَ شَيْءٌ أَعْطَانَا اللَّهُ تَعَالَى مِنْكَ»

*"Hapana. Hiyo (ni mali ambayo) Allah تعالى Ametupa (kama ngawira kutoka kwako)."*

Kwa hivyo 'Abbas akajikomboa mwenyewe, pamoja na wana wawili wa kaka zake, na rafiki yake. Allah تعالى Akateremsha Ayah kuhusu jambo lake,

يَأْتِيهَا النَّبِيُّ قُلٌ لِّمَنْ فِي أَيْدِيكُمْ مِنْ الْأَشْرَىٰ إِنْ يَعْلَمِ اللَّهُ فِي قُلُوبِكُمْ خَيْرًا يُؤْتِكُمْ خَيْرًا  
مِّمَّا أُخِذَ مِنْكُمْ وَيَغْفِرَ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٧٥﴾

***"Ewa Nabii! Waambie mateka waliomo Mikononi mwenu: Kama Mwenyezi Mungu Akiona kheri yoyote kwenu Atakupeni bora kuliko vilivyochukuliwa kwenu, na Atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu".***

Al-'Abbas رضي الله عنه akasema: "Basi badala ya *Uwqiyah* ishirini, Allah تعالى Akanipa baada ya kusilimu watumishi ishirini kila mmoja akiwa na mali nyingi, pamoja na kupewa maghufira ya Allah تعالى<sup>1</sup>."

Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bayhaqi رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa: "Mtume ﷺ aliletewa mali kutoka Bahrain, akasema:

<sup>1</sup> Al-Qurtubi 8:52.



«انْتَرَوْهُ فِي مَسْجِدِي»

“*Igaweni Msikitini kwangu*”. Ilikuwa ni mali nyingi sana iliyowahi kuletwa kwa Mtume ﷺ. Akatoka kwenda kusali, wala hakuingalia. Baada ya kukamilisha Sala, alikaa karibu na mali hiyo, na akawa kila anayekuja anampa. Akaja ‘Abbas رضي الله عنه akasema: “Ewe Mtume! Nipatie na mimi, kwani mimi nilijikomboa nafsi yangu na jamaa zangu”. Mtume ﷺ akamuambia, “**Chukua**”. Akaifunga na nguo yake, akajaribu kuibeba lakini akashindwa. Akasema: “Waamuru baadhi yao wanisaidie kuinyanyua” Akasema: “**Hapana**”. Akasema: “Basi nisaidie wewe kuinyanyua.” Mtume ﷺ akakataa. Kisha Al-Abbas رضي الله عنه aliipunguza baadhi na akaibeba begani na kuondoka. Mtume ﷺ hakuacha kumuangalia akistaajabia pupa yake, mpaka akaghibu, Mtume ﷺ hakusimama katika kuigawa mpaka dirham ya mwisho ilipoondoka<sup>1</sup>. Bukhari alinukuu katika sehemu kadha za Sahihi yake kwa isnadi iliyofupishwa, (katika namna ya kuonesha kuthibitishwa kwake)<sup>2</sup>. Na Kauli ya Allah تعالى،

وَإِنْ يُرِيدُوا خِيَانَتَكَ فَقَدْ خَانُوا اللَّهَ مِنْ قَبْلُ

“...*Ikiwa wanataka kukufanyia khiana, wao walikwishamfanyia khiana Mwenyezi Mungu kabla yake...*”. Maana yake;

وَإِنْ يُرِيدُوا خِيَانَتَكَ

“...*Ikiwa wanataka kukufanyia khiana...*”.

Kutokana na kauli walizo kudhihirishia.

فَقَدْ خَانُوا اللَّهَ مِنْ قَبْلُ

“...*Hakika wao walikwishamfanyia khiana Mwenyezi Mungu kabla yake...*”.

Kwa maana yake: Kabla ya vita vya Badr, kwa kumkufuru Yeye.

فَأَمْكَنَ مِنْهُمْ

“*Akakuwezesha kuwashinda*”. Kwa maana: Kwa kuwakamata mateka katika vita hivyo.

<sup>1</sup> Al-Bayhaqi 6:356.

<sup>2</sup> Al-Bukhari 421, 3049, 3165.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٧٠﴾

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hekima”.**

Maana: Ni Mwenye Kuyajua Ayafanyayo na Mwenye Hekima kwa Anayoyaamua.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ ءَاوَأُو  
وَنَصَرُوا أَوْلِيَّكَ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۗ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يُهَاجِرُوا مَا لَكُمْ مِّنْ وَلِيَّتِهِم مِّن  
شَيْءٍ حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا ۗ وَإِنِ اسْتَنْصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمْ النَّصْرُ إِلَّا عَلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ  
وَبَيْنَهُمْ مِّيثَاقٌ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٧١﴾

**72. “Hakika wale walioamini na wakahama na wakapigania njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, na wale waliotoa mahala pa kukaa, na wakamnusuru, hao ni marafiki na walenzi wao kwa wao. Na wale walioamini lakini hawakuhama, nyinyi hamna wajibu wa ulinzi kwao hata kidogo mpaka wahame. Lakini wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipo kuwa juu ya watu ambao yapo mapatano baina yenu na wao. Na Mwenyezi Mungu Anayaona mnayoyatenda”.**

**Muhajirina na Ansar ni Marafiki Wao kwa Wao.**

Allah تعالی Alitaja aina mbalimbali za Waumini na Akawagawa baina ya Muhajirina ambao walitoka na kuacha nyumba na mali zao, wakaja kumnusuru Allah تعالی na Mtume ﷺ na kuisimamisha Dini Yake, na wakajitolea mali na nafsi zao kwa ajili ya hilo. Na jingine ni kundi la Ansar, nao ni Waislamu wa Madinah ambao waliwapatia Ndugu zao, Muhajirina makazi majumbani mwao na wakawasaidia kwa mali zao, na wakamnusuru Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ kwa kushirikiana nao katika mapigano. Basi hao,

بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ

**“Hao ni marafiki na walenzi wao kwa wao”.** Maana yake: Kila mmoja katika wao ana haki kwa mwenzake zaidi ya mtu mwingine yeyote. Kwa ajili hii Mtume ﷺ alianzisha undugu kati ya Muhajirina na Ansar. Wakawa wanarithiana kwa

undugu huo, wakautanguliza mbele huo kuliko undugu wa kinasaba kwa kuleta hukumu ya mirathi. Mpaka Allah تعالى Alipoifuta hukumu hiyo kwa ajili ya warithi. Hilo lilithibiti ndani ya *Sahihi* Al-Bukhari kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما. Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Jarir رحمه الله تعالى, naye ni Ibn 'Abdullah Al-Balaji alisema: Mtume ﷺ alisema:

«الْمُهَاجِرُونَ وَالْأَنْصَارُ أَوْلِيَاءُ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ، وَالطُّلَقَاءُ مِنْ قُرَيْشٍ، وَالْمُعْتَقَاءُ مِنْ ثَقِيفٍ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

*"Muhajirina na Ansar ni Marafiki wao kwa wao, huku Tulaqaa wa kikuraishi (waachwa huru baada ya fat-h Makkah) na 'Utaqaa kutoka Thaqif (waachwa huru baada ya vita vya Hunayn) ni marafiki wao kwa wao mpaka Siku ya Kiyama."*<sup>1</sup>

Ahmad pekee alinukuu Hadithi hii. Allah تعالى na Mjumbe ﷺ waliwasifu Muhajirina na Ansar, katika Aya nyingi katika Kitabu Chake, Allah تعالى Alisema:

وَالسَّبِقُونَ الْأَوْلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

*"Na wale waliotangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na waliowafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu Ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na Amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake". (9:100) Na*

لَقَدْ تَابَ اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ الْعُسْرَةِ

*"Mwenyezi Mungu Amekwishapokea toba ya Nabii na Wahajiri na Ansari waliomfuata katika saa ya dhiki". (9:117) Na*

لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ هُمُ الصَّادِقُونَ ﴿١١٧﴾ وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالْإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْتُونَ عَلَى أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقِ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١١٨﴾

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 12:30.

***“Wapewe mafakiri Wahajiri waliotolewa majumbani mwao na mali zao kwa ajili ya kutafuta fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi Zake, na wanamsaidia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hao ndio wa kweli. Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda waliohamia kwao, wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyopewa (Wahajiri), bali wanawapendelea kuliko nafsi zao, ingawa wao wenyewe ni wahitaji na wenye kuepushwa na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu.” (59:8-9)***

Ni kizuri zaidi kilichosemwa katika Aya,

وَلَا يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِّمَّا أُوتُوا

***“Wala hawaoni choyo katika vifua vyao kwa walivyopewa (Wahajiri)...” (59:9)***

Kwa maana: Hawana husuda juu ya fadhila ambazo Allah تعالى Amewapatia kwa kufanya kwao Hijra. Dhahiri ya Aya ni kuwatanguliza Muhajirina kabla ya Ansar. Jambo hili linakubaliwa na Ulamaa, hawakhitilafiani katika hilo.

### **Si Wajibu Kumpa Ulinzi Aliyeamini bila Kufanya Hijra**

Kauli ya Allah تعالى,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَلَمْ يُهَاجِرُوا مَا لَكُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا

***“Na wale walioamini lakini hawakuhama, nyinyi hamna wajibu wa ulinzi kwao hata kidogo mpaka wahame...” (8:72)***

Hamzah alisoma neno *Walaayah* kwa Irabu ya kasra: *Wilaayah*, huku waliosalia walisoma kwa Irabu ya *fat’ha*, yaani *Walaayah* (ulinzi). Na hayo matamshi mawili yana maana moja, sawa na neno *Ad-Dilaalah* na *Ad-Dalaalah*,

مِن شَيْءٍ حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا

***“...hata kidogo mpaka wahame...”***Hii ni aina ya tatu ya Waumini, nao ni wale walioamini, lakini hawakufanya Hijra, bali walibaki katika miji yao. Hao hawatagaiwa fungu la Ngawira “*ghanima*” wala khumsi yake, isipokuwa kama wakishiriki katika vita. Kama alivyonukuu Imamu Ahmad kutoka kwa Buraydah

bin Al-Haswib Al-Aslami, alisema: Mtume ﷺ alikuwa anapomtuma Jemedari na kikosi kidogo au jeshi, alimuusia kumcha Allah تعالى khususan juu ya nafsi yake, na kuwafanyia wema Waislamu anaoshirikiana nao, na akasema:

«اغزوا باسمِ الله في سبيلِ الله، فاتلوا من كَفَرِ بالله، إِذَا لَقِيتَ عَدُوَّكَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ فَادْعُهُمْ إِلَى إِحْدَى ثَلَاثِ خِصَالٍ - أَوْ خِلَالٍ - فَأَيُّهُنَّ مَا أَجَابُوكَ إِلَيْهَا فَاقْبَلْ مِنْهُمْ، وَكُفَّ عَنْهُمْ. اذْعُهُمْ إِلَى الْإِسْلَامِ، فَإِنْ أَجَابُوكَ فَاقْبَلْ مِنْهُمْ وَكُفَّ عَنْهُمْ. ثُمَّ اذْعُهُمْ إِلَى التَّحَوُّلِ مِنْ دَارِهِمْ إِلَى دَارِ الْمُهَاجِرِينَ، وَأَعْلِمُهُمْ إِنْ فَعَلُوا ذَلِكَ أَنَّ لَهُمْ مَا لِلْمُهَاجِرِينَ، وَأَنَّ عَلَيْهِمْ مَا عَلَى الْمُهَاجِرِينَ، فَإِنْ أَبَوْا وَاخْتَارُوا دَارَهُمْ، فَأَعْلِمُهُمْ أَنَّهُمْ يَكُونُونَ كَأَعْرَابِ الْمُسْلِمِينَ، يَجْرِي عَلَيْهِمْ حُكْمُ اللَّهِ الَّذِي يَجْرِي عَلَى الْمُؤْمِنِينَ، وَلَا يَكُونُ لَهُمْ فِي الْفَيْءِ وَالْغَنِيمَةِ نَصِيبٌ، إِلَّا أَنْ يُجَاهِدُوا مَعَ الْمُسْلِمِينَ، فَإِنْ هُمْ أَبَوْا، فَادْعُهُمْ إِلَى إِعْطَاءِ الْجُزْئِ. فَإِنْ أَجَابُوا فَاقْبَلْ مِنْهُمْ وَكُفَّ عَنْهُمْ، فَإِنْ أَبَوْا فَاسْتَعِينِ بِاللَّهِ ثُمَّ فَاتِلْهُمْ»

*“Piganeni kwa Jina la Allah تعالى katika njia ya Allah تعالى. Mpigeni anayemkufuru Allah تعالى, ukikutana na adui yako miongoni mwa Washirikina, basi mlinganie katika moja ya mambo matatu. Lolote watakalokujibu, wakubalie na uwaachilie. Kisha uwalinganie wahame kutoka maeneo yao na waje katika maeneo ya Muhajirina. Na uwajulishe kwamba, ikiwa watafanya hivyo, watakuwa na haki na majukumu kama ya Muhajirina. Wakikataa na kukhitari kukaa katika maeneo yao, basi wajulishe watakuwa sawa na mabedui ambao ni Waislamu. Hukumu ya Allah تعالى itapita kwao sawa na inavyopita kwa Waumini wengine. Wala hawatakuwa na haki ya kupata ghanima au Faida (ngawira). Wakikataa, basi walinganie juu ya kulipa Jizia (kodi). Wakijibu, wakubalie na uwaachilie. Wakikataa, Muombe Allah تعالى msaada, kisha pigana nao”<sup>1</sup>. Muslim alinukuu Hadith hii<sup>2</sup>.*

Kauli ya Allah تعالى,

وَإِنْ أَسْتَنْصَرُوكُمْ فِي الدِّينِ فَعَلَيْكُمْ النَّصْرُ

**“Na kama wakiomba msaada kwenu katika Dini, basi ni juu yenu kuwasaidia...”**

<sup>1</sup> Ahmad 5:352.

<sup>2</sup> Muslim 3:1357.

Allah تعالیٰ Anasema, mabedui hawa ambao hawakuhama kwa ajili ya kupigania Dini yao, wakikuombeni msaada juu ya kumpiga adui, wasaidieni, kwani wao ni ndugu zenu katika Dini, isipokuwa wakikuombeni msaada dhidi ya makafiri ambao “...**yapo mapatano baina yenu na wao**”. Maana, mna mkataba wa amani kwa muda maalumu. Kwa hivyo, msiusaliti mkataba wenu wala msivunje ahadi mlizowekeana nao. Hii imesimuliwa kupitia kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما<sup>1</sup>.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ إِلَّا تَفْعَلُوهُ تَكُن فِتْنَةً فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ ﴿٧٣﴾

**73. “Na wale waliokufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipofanya hivi itakuwako fitna katika nchi na ufisadi mkubwa”.**

**Makafiri ni Marafiki Wao kwa Wao, Wala Hakuna Urafiki Baina Yao na Waislamu.**

Baada ya Allah تعالیٰ kutaja kuwa Waumini ni marafiki wao kwa wao, alikataa urafiki baina ya Waislamu na makafiri. Sawa na alivyonukuu Al-Hakim katika kitabu chake, *Al-Mustadrak* kutoka kwa Usama رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«لَا يَتَوَارَتُ أَهْلُ مِلَّتَيْنِ، وَلَا يَرِثُ مُسْلِمٌ كَافِرًا، وَلَا كَافِرٌ مُسْلِمًا»

“Watu wa dini mbili hawarithiani, wala Muislamu hamrithi kafiri, wala kafiri hamrithi Muislamu”.

Kisha akasoma,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ إِلَّا تَفْعَلُوهُ تَكُن فِتْنَةً فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ ﴿٧٣﴾

**“...Na wale waliokufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipo fanya hivi itakuwako fitna katika nchi na ufisadi mkubwa”.**

Kisha, Al-Hakim alisema: “Ina isnadi sahih, lakini hawakuinukuu”<sup>2</sup>. Mimi nasema, Hadithi hii imo ndani ya *Sahih* Mbili kwa kusimuliwa na Usamah bin Zayd رضي الله عنه. Alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا يَرِثُ الْمُسْلِمُ الْكَافِرَ وَلَا الْكَافِرُ الْمُسْلِمَ»

“Muislamu hamrithi kafiri, wala kafiri hamrithi Muislamu”<sup>3</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:83.

<sup>2</sup> Al-Hakim 2:240.

<sup>3</sup> *Fat’hul Al-Bari* 12:51 na Muslim 3:1233.

Na maana ya Kauli ya Allah تعالى،

إِلَّا تَفْعَلُوهُ تَكُنْ فِتْنَةٌ فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ ﴿٧٤﴾

**“...Msipofanya hivi itakuwako fitna katika nchi na ufisadi mkubwa”.**

Kwa maana: Msipojitenga na Washirikina na mkawafanya Waislamu kuwa marafiki, basi *Fitnah* itatokea kati ya watu. Nayo ni kutokea kwa mkanganyiko na mchanganyiko mkubwa wa Muumini kuchanganyika na kafiri, na kusababisha kuenea kwa ufisadi mkubwa baina ya watu.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ ءَاوَأُوا وَنَصَرُوا أُولَئِكَ هُمُ  
 الْمُؤْمِنُونَ حَقًّا هُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٧٥﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْ بَعْدِ وَهَاجَرُوا  
 وَجَاهَدُوا مَعَكُمْ فَأُولَئِكَ مِنْكُمْ وَأُولُوا الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ إِنَّ  
 اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٧٦﴾

**74. “Na walioamini na wakahama na wakapigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, na waliotoa mahala pa kukaa na wakawanusuru, hao ndio Waumini wa kweli. Watapata msamaha wa Mwenyezi Mungu na Kuruzukiwa kwema”.**

**75. “Na watakaoamini baadaye na wakahajiri, na wakapigana Jihadi pamoja nanyi, basi hao ni katika nyinyi. Na jamaa wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe zaidi katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua kila kitu”.**

### Sifa za Waumini wa Kweli.

Baada ya Allah تعالى kutaja hali ya Waumini duniani Alieleza hali watakayokuwa nayo huko Akhera. Kwa hivyo, Akawapa khabari za imani ya kweli kama ilivyotangulia mwanzoni mwa Surah, na kwamba Allah تعالى Atawalipa kwa Kuwapa maghufira na Kuwafutia madhambi yao, watakayokuwa nayo. Pia Atawapatia riziki tukufu, iliyo nzuri, nyingi, safi na ya kudumu milele, haikatiki wala kumalizika, wala si ya kuchosha kwa sababu ya uzuri na wingi wake na

itakuwa ya sampuli mbalimbali. Kisha Allah تعالى Akataja wafuasi wao duniani katika Imani waliokuwa na amali njema, nao watakuwa pamoja nao huko Akhera. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

وَالسَّابِقُونَ الْأُولُونَ

**“Na wale waliotangulia, wa kwanza”.** (9:100) Na Kauli Yake,

وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ

**“Na waliokuja baada yao...”.** (59:10)

Na katika Hadithi iliyopokewa na Bukhari na Muslim ambayo pia ni *Mutawaatir* katika njia zake kadhaa za usimulizi, kwamba Mtume ﷺ alisema,

«الْمَرْءُ مَعَ مَنْ أَحَبَّ»

*“Mtu huwa pamoja na ampendaye.”*<sup>1</sup>

Na katika Hadithi nyingine,

«مَنْ أَحَبَّ قَوْمًا فَهُوَ مِنْهُمْ»

*“Mwenye kuwapenda watu, basi yeye ni katika mmoja wao.”*

Na katika masimulizi mengine:

«خَيْرٌ مَعَهُمْ»

*“Atafufuliwa pamoja nao (katika Siku ya Kiyama).”*

**Haki ya Kurithi ni ya Ndugu wa Karibu.**

Ama kauli ya Allah تعالى,

وَأُولُوا الْأَرْحَامِ بَعْضُهُمْ أَوْلَىٰ بِبَعْضٍ فِي كِتَابِ اللَّهِ

**“Na jamaa wa nasaba wanastahikiana wenyewe kwa wenyewe zaidi katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu...”.**

Maana yake: Katika hukumu ya Allah تعالى, na wala Kauli hii ya Allah تعالى.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 10:573.



وَأُولُوا الْأَرْحَامِ

**“Na jamaa wa nasaba...”**

Haiwakusudii ndugu maalumu walioelezwa na wanazuoni wa Elimu ya mirathi, ambao hawana fungu mahsusi katika kurithi kwao wala sio *Asaba* (wanaorithi kinachobaki). Bali kurithi kwao mpaka waunganishwe na mtu mwengine anayerithi, kama vile mama mdogo (*khalati*) na mjomba (*khalī*) na shangazi na watoto wa mabinti na watoto wa madada na mfano wao, kama ambavyo wanadhani baadhi yao, na wanatolea hoja kwa Aya (hiyo) na wanaamini hivyo kabisa katika masuala haya. Bali ukweli ni kwamba Aya hii inawahusu ndugu zote wa karibu. Kama Alivyoeleza Ibn ‘Abbas, Mujahid, Ikrimah, Hassan, Qatadah na wengine <sup>1</sup>رضي الله عنهم. Kwamba Aya hii imefuta urithi kwa njia ya kiapo na undugu wa hiari, kwani walikuwa wanarithishana hapo mwanzo kwa njia hizi mbili; kwa kuzingatia hayo, basi Aya hii inawajumuisha ndugu wote wa nasaba ya kuzaliwa. Kwa jina maalumu. Na wanazuoni wasiowarithisha, wanatoa hoja kwa dalili nyingi, yenye nguvu zaidi katika dalili hizo ni Hadithi ya Mtume ﷺ,

«إِنَّ اللَّهَ قَدْ أَعْطَى كُلَّ ذِي حَقٍّ حَقَّهُ فَلَا وَصِيَّةَ لِبَوَارِثٍ»

*“Hakika Allah تعالی Amempa haki kila mwenye kuistahiki, kwa hivyo hakuna wasia kwa mwenye kurithi”.*

Walisema: “Kama angekuwa ni mwenye haki basi angekuwa na fungu lake lililotajwa katika Kitabu cha Allah تعالی, na kwa kuwa haikuwa hivyo, basi hawezi kuwa na haki ya kuwa mrithi”. Allah تعالی Ndiye Mjuzi zaidi.

Mwisho wa *Surat Al-Anfaal*. Sifa zote njema na shukrani ni za Allah تعالی. Kwake Yeye tunatawakali, Anatutosha, Naye ni Mbora wa Kutegemewa.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 14:90

## Tafsiri ya Suratu Tawbah

## Sura ya 9

## Iliteremshwa Madinah

## سُورَةُ التَّوْبَةِ

بَرَاءَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١﴾  
 فَسِيحُوا فِي الْأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ  
 غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ <sup>٢</sup> وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ  
 الْمُخْزِي لِلْكَافِرِينَ ﴿٢﴾  
 إِلَى النَّاسِ يَوْمَ الْحَجِّ الْأَكْبَرِ أَنَّ اللَّهَ بَرِيءٌ مِّنَ  
 الْمُشْرِكِينَ وَرَسُولُهُ <sup>٣</sup> فَإِن تُبْتِغُوا فَهَوْاْ خَيْرٌ لَّكُمْ  
 وَإِن تَوَلَّيْتُمْ فَأَعْلَمُوا أَنَّكُمْ  
 غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ <sup>٤</sup> وَبَشِّرِ الَّذِينَ كَفَرُوا بِعَذَابِ  
 الْيَمِّ <sup>٥</sup> إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ثُمَّ لَمْ  
 يَنْقُصُوكُمْ شَيْئًا  
 وَلَمْ يُظَاهِرُوا عَلَيْكُمْ أَحَدًا فَأَتِمُوا إِلَيْهِمْ  
 عَهْدَهُمْ إِلَىٰ مُدَّتِهِمْ <sup>٦</sup>  
 إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٣﴾ فَإِذَا أَسْلَخَ  
 الْأَشْهُرَ الْحُرْمَ فَاقْتُلُوا  
 الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ وَخُذُوهُمْ  
 وَأَحْصُرُوهُمْ وَأَقْعُدُوا لَهُمْ  
 كُلَّ مَرْصِدٍ <sup>٧</sup> فَإِن تَابُوا وَأَقَامُوا  
 الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ  
 إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٤﴾  
 وَإِن أَحَدٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ اسْتَجَارَكَ فَأَجِرْهُ  
 حَتَّىٰ يَسْمَعَ  
 كَلِمَةَ اللَّهِ ثُمَّ أبلغه ما منه <sup>٨</sup> ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ  
 لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥﴾

بَرَاءَةٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَى الَّذِينَ  
 عَاهَدْتُمْ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١﴾ فَسِيحُوا  
 فِي الْأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ وَاعْلَمُوا أَنَّكُمْ  
 غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ <sup>٢</sup> وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ  
 الْمُخْزِي لِلْكَافِرِينَ ﴿٢﴾

**1. Huku ni kujitoa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kwenye jukumu la maagano na mlioahidiana nao katika Washirikina.**

**2. Basi tembeeni katika nchi miezi minne, na Jueni kwamba nyinyi hamuwezi kumshinda Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu Ndiye Anayewahizi (wadhalilisha) makafiri.**

**Kwa Nini Bismillah Haiku andikwa Mwanzoni mwa Surah Hii?**

Sura hii tukufu ni katika Uteremsho wa mwisho kwa Mtume ﷺ, sawa na alivyoandika Bukhari kutoka kwa Baraa amesema: Aya ya mwisho kushushwa ni:

يَسْتَفْتُونَكَ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِي الْكَلْبَةِ

**“Wanakuomba hukumu, sema: Mwenyezi Mungu Atakupeni hukumu juu ya mkiwa”. (4:176)**

Ambapo Sura ya mwisho kuteremshwa ni *Bara-ah*<sup>1</sup>. Haina *Bismillah* mwanzoni mwake kwa sababu Masahaba hawakuiandika mwanzoni mwake, ndani ya *Msahafu kiongozi* (Msahafu kamili) walioutayarisha, bali pia katika mpangilio huu, walimfuata Amiri wa Waumini, ‘Uthman bin ‘Affan رضي الله عنه. Sehemu ya mwanzoni mwa Surah hii iliteremshwa kwa Mtume ﷺ baada ya kurejea kutoka katika vita vya Tabuk, na akakusudia Hijja. Kisha akakumbuka kuwa Washirikina nao watahudhuria katika msimu huu kama ada yao na kwamba watatufu Al-Ka’ba wakiwa uchi. Hakupenda kuchanganyikana nao, akamtuma Abubakr رضي الله عنه kuwa Amiri wa Hijja katika mwaka huo, ili awaongoze watu katika ibada zao na kuwajulisha Washirikina kwamba baada ya mwaka huo wasihiji tena. Pia awatangazie watu:

بِرَاءةٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ

**“Huku ni kujitoa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.”**

Baada ya Abubakr رضي الله عنه kuondoka, Mtume ﷺ alimuongeza nyuma Ally bin Abu Talib رضي الله عنه ili awe ndiye wa kufikishia Washirikina khabari kutoka kwa Mtume ﷺ kwa sababu alikuwa binamu yake kama itakavyo bainishwa.

### Tangazo Kwamba Washirikina Wamevunja Mkataba

Kauli ya Allah تعالى،

بِرَاءةٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ

**“Huku ni kujitoa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake”.**

Yaani, huku ni kujibarii kwa Allah تعالى na Mjumbe Wake،

إِلَى الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩﴾ فَسِيحُوا فِي الْأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ

**“...kwenye jukumu la maagano na mlioahidiana nao katika Washirikina. Basi tembeeni katika nchi miezi minne”. (9:1-2)**

Aya hii ni kwa wenye mikataba ya wazi isiwekewa wakati, au kwa wenye mikataba yenye muda wa chini ya miezi minne. Watakamilishiwa miezi minne

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:167. Surah hii ni mashuhuri kwa jina la *Bara-ah*.

na si zaidi. Ama waliokuwa na mikataba yenye muda maalumu, kuisha kwake ni baada ya kufika muda huo, bila ya kujali urefu wake. Kama Kauli ya Allah تعالى Alivyosema:

فَأْتِمُوا إِلَيْهِمْ عَهْدَهُمْ إِلَىٰ مُدَّتِهِمْ

**“...basi hao watimizieni ahadi yao mpaka muda wao”. (9:4)**

Pia kutokana na Hadithi inayolizungumzia jambo hili isemayo, “Mwenye mkataba baina yake na Mtume ﷺ, basi ataendelea mpaka muda wake ukamilike”. Na ilisimuliwa na Al-Kalbi, Muhammad bin Ka’b Al-Quradhi na wengine<sup>1</sup>.

Na Abu Ma’shar Al-Madani alisema alituhadithia Muhammad bin Ka’b Al-Quradhi na wengine kuwa: “Mtume ﷺ alimtuma Abubakr رضي الله عنه akiwa Amiri katika msimu wa Hijja katika mwaka wa tisa, na akamtuma ‘Ali bin Abu Talib رضي الله عنه pamoja na Ayah thelathini au arobaini kutoka katika *Suratul Bara-a*. Akawasomea watu. Washirikina walipewa miezi minne ambapo wanakuwa huru kwenda mahali popote katika nchi. Akawasomea Ayah hizo siku ya ‘Arafa. Aliwapa siku ishirini (zilizosalia) za mwezi wa *Dhul-Hijjah*, mwezi mzima wa *Muharram*, *Swafar*, *Rabi’ul Awwal* na siku kumi za *Rabi’ul Akhir*. Aliwasomea katika kambi zao na kuwaambia: “Baada ya mwaka huu, Mshirikina yeyote hataruhusiwa kuhiji wala kufanya *Tawaf* huku akiwa uchi”<sup>2</sup>. Na kwa ajili hiyo Allah تعالى Alisema,

وَأَذَانٌ مِّنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ إِلَىٰ النَّاسِ يَوْمَ الْحَجِّ الْأَكْبَرِ أَنَّ اللَّهَ بَرِيءٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ  
وَرَسُولُهُ فَإِنْ تُبْتُمْ فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَإِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَأَعْلَمُوا أَنَّكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي اللَّهِ وَبَشِّرِ  
الَّذِينَ كَفَرُوا بِعَذَابِ الْيَمِّ

**3. Na ni tangazo kutokana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kwa wote siku ya Hijja kubwa kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hawana jukumu lolote kwa Washirikina. Basi mkitubu itakuwa kheri kwenu, na mkigeuka basi Jueni kuwa nyinyi hamumshindi Mwenyezi Mungu. Na wabashirie makafiri kuwa watapata adhabu chungu.**

<sup>1</sup> Tabari 14:100-102.

<sup>2</sup> Tabari 6:304. Isnadi yake si sahihi. Bukhari aliandika Hadithi sawa na hiyo ikiwa na maneno tofauti. Angalia namba 4363.

Allah تعالى Anasema: Na ni ilani,

مِنْ أَلَلِّهِ وَرَسُولِهِ

**“...kutokana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake”.** Na ni Utangulizi wa onyo kwa watu,

يَوْمَ الْحَجِّ الْأَكْبَرِ

**“...siku ya Hijja kubwa”.** Hiyo ni siku ya kuchinja ambayo ni yenye fadhila kubwa zaidi miongoni mwa siku za ibada ambapo huwa na mkusanyiko mkubwa.

أَنَّ أَلَلِّهِ بَرِيءٌ مِّنَ الْمُشْرِكِينَ وَرَسُولُهُ

**“...kwamba Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hawana jukumu lolote kwa Washirikina”.**

Maana: Pia amejitweka mbali dhidi yao. Halafu Akawalingania kuleta toba.

فَإِن تُبَتُّوْا

**“Basi mkitubu.”** Na kuacha ushirikina na upotevu.

فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَإِن تَوَلَّيْتُمْ

**“...itakuwa kheri kwenu, na mkigeuka”.** Kwa kuendelea na hayo mliyo nayo.

فَاعَلَمُوا أَنكُمْ غَيْرُ مُعْجِزِي أَلَلِّهِ

**“...basi Jueni kuwa nyinyi hamumshindi Mwenyezi Mungu”.**

Bali, Yeye ni Muweza juu yenu, na nyinyi mko katika mfumbato wake, na chini ya Kuteza Kwake nguvu na Kutaka Kwake.

وَبَشِّرِ الَّذِينَ كَفَرُوا بِعَذَابِ أَلِيمٍ

**“Na wabashirie makafiri kuwa watapata adhabu chungu”.**

Kwa kulipwa, fedheha na majanga duniani na adhabu ya minyororo na pingu Akhera. Bukhari, Allah تعالى Amrehemu, alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Abubakr رضي الله عنه alinituma pamoja na Wajumbe wengine katika siku ya Kuchinja, aliwaagiza kutangaza huko Mina kwamba, “Baada ya mwaka huu, Mshirikina hatoruhusiwa kuhiji, na hakuna atakayeruhusiwa kutufu akiwa uchi”. Humayd رضي الله عنه alisema: “Kisha, Mtume ﷺ baada ya kuondoka Abubakr رضي الله عنه alimtumia Ali Abu Talib رضي الله عنه na akamuambia atangaze

kujitoa *Bara-ah*." Abu Hurayra رضي الله عنه alisema: Ali رضي الله عنه alitangaza kujitoa *Bara-ah* pamoja nasi tukiwa Mina katika siku ya Kuchinja, na kwamba, "Mshirikina hataruhusiwa kuhiji akiwa uchi baada ya mwaka huo"<sup>1</sup>. Bukhari alinukuu tena, kwamba Abu Hurayra رضي الله عنه alisema: "Abubakr رضي الله عنه alinituma kwenda Mina pamoja na watangazaji kwamba nitangaze, "Baada ya mwaka huu, Mshirikina yeyote hataruhusiwa kuhiji, wala kufanya tawafu katika Kaaba huku akiwa yu uchi". Pia kutangaza kuwa siku ya Hijja kuu *Alhajjul-Akbar*, ni siku ya Kuchinja. Iliitwa kwa jina hili (*Akbar*) kwa sababu ya watu kusema ni Haji *Asghar*, yaani Hijja ndogo. Abubakr رضي الله عنه aliwatangazia watu katika mwaka huo, na katika mwaka uliofuatia wa *Hijjatul Wada*. (Hijja ya Kuaga), aliyohiji Mtume ﷺ hakukuwa na Mshirikina aliyefanya Hijjah."<sup>2</sup> Masimulizi haya ni kwa mujibu wa alivyonukuu Bukhari katika Kitabu cha Jihadi.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Abu Ja'far Muhammad bin 'Ali bin Al-Husayn bin Ali ambaye alisema, "Pindi sura *Bara-ah* iliposhushwa kwa Mtume ﷺ, huku akiwa ameshamtuma Abubakr رضي الله عنه kuwaongoza watu katika Hijja, aliambiwa: "Ewe Mtume! Ungetuma (ujumbe huu) kwa Abubakr رضي الله عنه". Akasema,

«لَا يُؤَدِّي عَنِّي إِلَّا رَجُلٌ مِنْ أَهْلِ بَيْتِي»

"Haitasadikika kuwa imetoka kwangu ikiwa haitapitia kwa mmoja wapo katika familia yangu".

Halafu akamuita 'Ali رضي الله عنه na kumambia:

«اخْرُجْ بِهَذِهِ الْقِصَّةِ مِنْ صَدْرِ بَرَاءةٍ وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ يَوْمَ النَّخْرِ إِذَا اجْتَمَعُوا بَيْنِي، أَنَّهُ لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ كَافِرًا، وَلَا يَخُجُّ بَعْدَ الْعَامِ مُشْرِكًا، وَلَا يَطُوفُ بِالْبَيْتِ عُرْبَانًا، وَمَنْ كَانَ لَهُ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ ﷺ عَهْدٌ فَهُوَ لَهُ إِلَىٰ مُدَّتِهِ»

"Chukua khabari hii kuanzia mwanzoni mwa *Bara-ah* na uwatangazie watu katika siku ya Kuchinja watakapokuwa wanajumuika Minaa, kwamba, hapana kafiri atakayeingia peponi, wala hapana Mshirikina atakayeruhusiwa kufanya Hijja baada ya mwaka huu, na haitaruhusiwa mtu kutufu Ka'ba akiwa uchi, na mwenye mkataba na Mtume ﷺ utaendelea kuwepo mpaka wakati wake utakapomalizika".

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:168.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 8:168.

'Ali رضي الله عنه akatoka huku akiwa amempanda Ngamia wa Mtume ﷺ aitwaye 'Al-Adhbaa hadi akamdiriki Abubakr رضي الله عنه njiani. Baada ya Abubakr رضي الله عنه kumuona alimuuliza, "Umekuja kama Amiri au mfuasi?" Akajibu, Mfuasi". Wakaendelea wote na safari. Katika mwaka huo, Abubakr رضي الله عنه aliongoza Hijja, huku Waarabu wakiwa na Desturi yao ya Hijja ile ile ya zama za ujahili. Mpaka Akawadia siku ya kuchinja, Ali bin Abu Talib رضي الله عنه alisimama na kuwatangazia watu kuhusu aliyoamrisha na Mtume ﷺ kwa kusema, "Enyi watu! Kafiri hataingia peponi, wala Mshirikina hataruhusiwa kufanya Hijja baada ya mwaka huu wala kufanya Tawafu katika Nyumba hali akiwa uchi, na mwenye mkataba na Mtume ﷺ, basi utaisha pindi muda wake utakapofika". Baada ya mwaka huo hakukuwa na Mshirikina aliyehiji wala kufanya Tawafu katika Kaaba akiwa uchi. Halafu Abubakr na 'Ali رضي الله عنهما wakarejea kwa Mtume ﷺ. Kwa hivyo, hili lilikuwa tangazo la kujibari kwa Allah تعالى dhidi ya Washirikina ambao walikuwa na ahadi ya mwaka mmoja na wale waliokuwa na muda wa kuendelea mpaka kumalizika kwa wakati wake"<sup>1</sup>.

إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ثُمَّ لَمْ يَنْقُصُوكُمْ شَيْئًا وَلَمْ يُظَاهِرُوا عَلَيْكُمْ أَحَدًا  
فَاتَّبِعُوا إِلَهُكُمْ عَاهِدَهُمْ إِلَىٰ مُدَّتِهِمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿١٠٧﴾

**4. Isipokuwa Washirikina ambao mliahidiana nao kisha wasikupunguzieni chochote, wala hawakumsaidia yeyote dhidi yenu, basi hao watimizieni ahadi yao mpaka muda wao. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wacha-Mungu.**

**Mikataba ya Amani Iliyokuwepo Itaendelea Mpaka Muda Wake Kumalizika.**

Azimio hili halihusu mikataba iliyokuwa na muda maalumu bali linahusu mikataba yote ambayo haina ukomo maalumu. Mwisho wake ni miezi minne Katika muda huo wa miezi minne, waliruhusiwa na kuwa huru kwenda popote walipopataka katika ardhi kwa ajili ya kutafuta kimbilio la kujinusuru. Isipokuwa waliokuwa na mkataba uliowekewa muda, basi kuisha kwake ni kufika kwa wakati waliowekeana. Hadithi kadhaa juu ya hayo zimeshatangulia kuelezwa

<sup>1</sup> At-Tabari 14:107. Masimulizi haya si *Sahihi* kwa sababu ni *Mursal*. Kauli ya Mtume imeungwa mkono na masimulizi ya Anas, yalinyonukuliwa na At-Tirmidhi, chini ya Tafsir ya Surah hiyo. Masimulizi yaliyosalia yaliungwa mkono na wengine. Wanazuoni wanaeleza kuwa familia ya Muhammad ﷺ imetajwa kwa kumaanisha kuwa uwakilishi wa namna hiyo ulihitajika wakati wa kuibadili mkataba.

ya kuwa yeyote aliyekuwa na Mkataba pamoja na Mtume ﷺ hadi pale utakapoisha. Kwa hivyo, kila aliyekuwa na mkataba na Mtume ﷺ, basi hilo lilikuwa hivyo mpaka muda wake ulipofika kwa masharti kwamba mwenye mkataba asiuvunje, wala asimsaidie adui yeyote dhidi ya Waislamu. Hivi ndivyo ilivyokuwa, aliyekuwa na mkataba alitakiwa aendelee nao mpaka kumalizika kwake, kwa ajili hii, Allah تعالى Alihamasisha utekelezaji wa hayo, Alisema:

إِنَّ اللَّهَ سَخِبُ الْمُتَّقِينَ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wacha-Mungu.”** Maana yake: Wanatekeleza mikataba yao.

فَإِذَا أَنْسَلَخَ الْأَشْهُرَ الْحَرَّمَ فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ وَخُذُوهُمْ وَأَحْصُرُوهُمْ  
وَأَقْعُدُوا لَهُمْ كُلَّ مَرْصِدٍ ۚ فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ  
إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٥﴾

**5. Na ikiisha miezi mitukufu basi Waueni Washirikina popote muwakutapo, na washikeni na wazungukeni, na wavizieni katika kila njia. Lakini wakitubu, wakashika Sala na wakatoa Zaka, basi waachilieni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.**

### Hii Ndiyo Aya Inayoruhusu Kupigana kwa Upanga (Silaha)

Mujahid, Amri bin Shu'ayb, Muhammad bin Is-haq, Qatadah, As-Suddi na 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam walisema kuwa makusudio yake ni kupita kwa kipindi cha miezi minne iliyotajwa katika Aya iliyotangulia.<sup>1</sup>

فَسِيحُوا فِي الْأَرْضِ أَرْبَعَةَ أَشْهُرٍ

**“...basi tembeeni katika ardhi miezi minne”. (9:2)**

Halafu Akasema,

فَإِذَا أَنْسَلَخَ الْأَشْهُرَ الْحَرَّمَ

**“Na ikiisha miezi mitukufu”** Maana yake: Baada ya kupita miezi minne ambapo Tumekukatazeni kuwapiga na Tukawapa Washirikina muda, baada ya hapo popote muwakutapo wapigeni na muwau. Na Kauli ya Allah تعالى:

<sup>1</sup> At-Tabari 14:136-137.



فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ

**“...basi Waueni Washirikina popote muwakutapo.”**Maana yake popote ardhini. Aya hii imetaja sehemu zote kwa ujumla lakini ni mashuhuri kuwa eneo takatifu la *Haram* haliruhusiwi kupigana. Ni kutokana na Kauli Yake katika Aya nyingine.

وَلَا تُقَاتِلُوهُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ حَتَّى يُقَاتِلُوكُمْ فِيهِ ۖ فَإِنْ قَاتَلُوكُمْ فَاقْتُلُوهُمْ ۗ

**“Wala msipigane nao kwenye Msikiti Mtakatifu mpaka wakupigeni huko. Wakikupigeni huko basi nanyi pia wapigeni”.**  
(2:191)

Kauli ya Allah تعالى:

وَخُذُوهُمْ

**“...na washikeni.”** Wazingireni kwa kuwaua mkitaka au kuwafanya mateka. Kauli ya Allah تعالى,

وَأَحْصُرُوهُمْ وَأَقْعُدُوا لَهُمْ كُلَّ مَرْصِدٍ

**“...na wazungukeni, na wavizieni katika kila njia.”**

Inamaanisha kuwa msingojee, mpaka mkutane nao, bali watafuteni na kuwazuilia katika maeneo na ngome zao na kuwavizia katika njia zao mpaka wasiwe na uhuru na hapo kuchagua ama kufa au kuingia katika Uislamu. Kwa njia hii, Allah تعالى Alisema:

فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَخَلُّوا سَبِيلَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

**“Lakini wakitubu, wakashika Sala na wakatoa Zaka, basi wachilieni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.**

Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه aliitumia Aya hii na mithili yake kuwapiga waliojizuia kutoa Zaka. Kwani imeharamishwa kuwapiga watu, isipokuwa kwa kupatikana matendo haya, ambayo ni kuingia katika Uislamu na kushikamana na utekelezaji wa kila lililo wajibu. Na akatanabahisha kuanza na mambo makuu, kisha ya chini yake. Nguzo kuu kabisa ya Uislamu baada ya Shahada mbili ni Sala, ambayo ndiyo haki ya Allah تعالى. Baada yake ni utekelezaji wa Zakah ambayo ni kwa ajili ya kuwanufaisha mafakiri na wenye haja. Haya ndiyo matendo matukufu ambayo hufanywa na viumbe, na kwa ajili hii mara

nyingi, Zaka hutajwa na Sala kwa pamoja. Imenukuliwa ndani ya *Sahih Mbili* kuwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

دَأْمِرْتُ أَنْ أَقَاتِلَ النَّاسَ حَتَّى يَشْهَدُوا أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا رَسُولُ اللَّهِ  
وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ

*"Nimeamrisha kuwa nipigane na watu mpaka washuhudie hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى na kwamba Muhammad ﷺ ni Mjumbe wa Allah. Wasimamishe Sala na watoe Zaka"*<sup>1</sup>.

Aya hii tukufu iliitwa *Aya As-Sayf* (aya ya upanga) ambayo Adh-Dhahhak bin Muzahim aliizungumzia: "Kwamba ndio iliyovunja makubaliano ya amani baina ya Mtume ﷺ na na washirikina wote, kila mkataba na kila kipindi". Al-'Awfi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alitoa rai kuhusu Ayah hii, "Hapana Mshirikina yeyote aliyewekeana Mkataba au ahadi ya kuachwa salama, baada ya *Surat Al-Bara-ah* kushushwa. Muda uliosalia kabla ya kumalizika kwa Mikataba waliyokuwa nayo Washirikina, kabla haijateremka *Surat Al-Bara-ah* ulikuwa miezi minne, tokea siku ya kutangazwa kwa kujitoa Al-Bara-ah mpaka Tarehe kumi ya mwezi wa *Rabi'ul Aakhir*"<sup>2</sup>.

وَإِنْ أَحَدٌ مِنَ الْمُشْرِكِينَ اسْتَجَارَكَ فَأَجِرْهُ حَتَّى يَسْمَعَ كَلِمَ اللَّهِ ثُمَّ أَبْلِغْهُ مَأْمَنَهُ  
ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦﴾

**6. Na ikiwa mmoja wapo katika Washirikina akikuomba ulinzi, basi mpe ulinzi apate kusikia maneno ya Mwenyezi Mungu. Kisha mfikishie pahala pake pa amani. Haya ni kwa kuwa hao ni watu wasiojua kitu.**

**Mshirikina Akiomba Amani Akubaliwe.**

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ,

وَإِنْ أَحَدٌ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

***"Na ikiwa mmoja wapo katika Washirikina". Wale Niliokuamuru uwapige na***

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 1:95 na Muslim 1:53.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:133.

nilio kuhalalishia nafsi zao na mali zao.

أَسْتَجَارَكَ

“...**akikuomba ulinzi**”. Maana yake: Akikuomba Amani, basi mkubalie ombi lake, mpaka ayasikie Maneno ya Allah تعالى, yaani Qur’an umsomee na umtajje chochote katika mambo ya Dini ambapo utamsimamishia ushahidi wa Allah تعالى dhidi yake,

ثُمَّ أبلغه مَأْمَنَهُ

**“Kisha mfikishie pahala pake pa amani”.**

Maana yake, ilhali akiwa yuko katika amani na aendelee mpaka atakaporejea katika mji, nyumba na mahali pake palipo salama.

ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَعْلَمُونَ

**“Haya ni kwa kuwa hao ni watu wasiojua kitu”.**

Aya inasema: “Tumewawekea amani watu hao ili waijue Dini ya Allah تعالى na ili wito wa Allah تعالى uwafikie waja Wake”.

Ibn Abu Najih alisema kuwa Mujahid katika kuitafsiri Ayah hii alisema: “Ni mtu anayekujia ili asikie unachokisema na ulichoteremshiwa. Huyoyuko salama mpaka akufikie, ayasikie maneno ya Allah تعالى na aendelee kwenda mahali pa salama alipotokea”<sup>1</sup>. Kwa minajili hii, Mtume ﷺ alikuwa akimpa usalama mtu aliyekuja kutafuta uongofu au kufikisha ujumbe. Kama walivyomjia katika siku ya Al-Hudaybiyyah, Wajumbe wa Kikuraishi, miongoni mwao ni ‘Urwah bin Mas’ud, Mirkiz bin Hafis, Suhayl bin Amri na wengine, mmoja baada ya mwengine, wakifanya harakati kwa ajili ya kutatua masuala yaliyokuwepo baina yake na Washirikina. Wakashuhudia heshima kubwa waliyokuwa wakiifanya Waislamu kwa Mtume ﷺ, ambayo iliwashangaza na hawakuwahi kuiona kwa yeyote si wafalme wala Kaizari. Wakarejea kwa kaumu yao na wakawapasha khabari juu ya hilo. Jambo hilo na ya mithili yake, yalikuwa miongoni mwa sababu kubwa za kuongoka kwa wengi wao. Na kwa ajili hii pia aliweza kufika Mwakilishi wa Musaylama muongo mkubwa, kwa Mtume ﷺ na akamuuliza, “Unashuhudia kwamba Musaylama ni mjumbe wa Allah?” Akajibu, “Ndiyo”. Mtume ﷺ akamjibu,

<sup>1</sup> At-Tabari 14:139.

«لَوْلَا أَنَّ الرُّسُلَ لَا تُقْتَلُ لَضَرَبْتُ عُنُقَكَ»

*“Isingelikuwa Wajumbe hawauwawi, ningeliikata shingo yako”<sup>1</sup>.*

Allah تعالی Alimhukumu mtu huyo, Ibn An-Nawahah, akatwe shingo chini ya Ukadhi wa Ibn Mas’ud رضي الله عنه - Kufa (mji wa Iraq). Hayo ni baada ya kuridhika kuwa alikuwa bado akitoa shahada kuwa Musaylamah ni mjumbe wa kweli wa Allah تعالی. Ibn Mas’ud رضي الله عنه alimuita na kumuambia: “Sasa wewe hauko katika kubeba ujumbe (si mjumbe)”. Akaamuru Ibn An-Nawahah akatwe shingo, Allah تعالی asimrehemu na amlaani. Makusudio makubwa ni kwamba, mwenye kuja kutokea katika ardhi iliyo katika vita dhidi ya Waislamu na kuingia katika nchi ya Kiislamu ili kuleta ujumbe, kufanya biashara, kutafuta suluhu, kulipa fidia au sababu nyingine zinazofanana na hizo, na akataka kuhakikishiwa usalama na kiongozi au naibu wake. Inafaa kupewa amani katika kipindi chote cha kuja katika nchi ya Kiislamu, mpaka arejee mahali pake pa salama au nchi yake.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ibn Hisham 4:247.

كَيْفَ يَكُونُ لِلْمُشْرِكِينَ عَهْدٌ عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ رَسُولِهِ  
 إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ فَمَا  
 اسْتَقْتُمُوا لَكُمْ فَاسْتَقِيمُوا هُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ نَجِيبُ الْمُتَّقِينَ  
 ﴿٧﴾ كَيْفَ وَإِن يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ لَا يَرْقُبُوا فِيكُمْ إِلَّا  
 وَلَا ذِمَّةً ۚ يُرْضُونَكُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ وَتَأْبَىٰ قُلُوبُهُمْ وَأَكْثَرُهُمْ  
 فَسِقُونَ ﴿٨﴾ أَشْرَكُوا بِعَايَةِ اللَّهِ تَمَنَّا قَلِيلًا فَصَدُّوا  
 عَنِ سَبِيلِهِ ۚ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩﴾ لَا  
 يَرْقُبُونَ فِي مُؤْمِنٍ إِلَّا ۗ وَلَا ذِمَّةً ۚ وَأُولَٰئِكَ هُمُ  
 الْمُعْتَدُونَ ﴿١٠﴾ فَإِن تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا  
 الزَّكَاةَ فَإِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ ۗ وَتُفْضِلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ  
 يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾ وَإِن نَّكُتُوا أَيْمَنْتُهُمْ مِّنْ بَعْدِ عَهْدِهِمْ  
 وَطَعْنُوا فِي دِينِكُمْ فَفَقِّتُوا أَيْمَةَ الْكُفْرِ ۚ إِنَّهُمْ لَا أَيْمَنَ  
 لَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَنْتَهُوْنَ ﴿١٢﴾

كَيْفَ يَكُونُ لِلْمُشْرِكِينَ عَهْدٌ  
 عِنْدَ اللَّهِ وَعِنْدَ رَسُولِهِ إِلَّا الَّذِينَ  
 عَاهَدْتُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ فَمَا  
 اسْتَقْتُمُوا لَكُمْ فَاسْتَقِيمُوا هُمْ ۚ إِنَّ  
 اللَّهَ نَجِيبُ الْمُتَّقِينَ ﴿٧﴾

**7. Itakuwaje iwepo ahadi na Washirikina mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya Mtume Wake, ila wale mlioahidiana nao kwenye Msikiti Mtakatifu? Basi maadamu wanakwenda nanyi sawa, nanyi pia nendeni sawa nao. Hakika Mwenyezi Mungu Huwampenda wacha-Mungu.**

**Kusisitiza Kujiweka Kando (Baraa) Dhidi ya Washirikina**

Allah تعالی Anabainisha hikima yake katika suala la kujitenga na washirikina na kuwapa wao muda wa miezi minne, na baada ya hapo watakutana na kipigo kikali popote watakapokuwa. Allah تعالی Amesema,

كَيْفَ يَكُونُ لِلْمُشْرِكِينَ عَهْدٌ

**“Itakuwaje iwepo ahadi na Washirikina”.** Ahadi ya wao kuachwa kama walivyo waendeleo na masuala yao ilhali wao wanamshirikisha Allah تعالی na kumkanusha Yeye na Mtume Wake ﷺ.

إِلَّا الَّذِينَ عَاهَدْتُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ۗ

**“...ila wale mlioahidiana nao kwenye Msikiti Mtakatifu?”**

Kwa maana: Mkataba wa siku ya Al-Hudaybiyyah.

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى.

هُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوكُمْ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَأَهِدَىٰ مَعَكُوفًا أَنْ يَبْلُغَ حِجْلَهُ ۗ

**“Hao ndio waliokufuru na wakakuzieni msiingie Msikiti Mtukufu, na wakawazulia dhabihu kufika mahala pake”. (48:25)**

Allah تعالى Akasema tena,

فَمَا اسْتَقَمُوا لَكُمْ فَاسْتَقِيمُوا هُمُ

**“Basi maadamu wanakwenda nanyi sawa, nanyi pia Nendeni sawa nao”.**

Maana: Pindi watakaposhikamana na masharti mliyowawekea, ahadi mlizowapa, ikiwa ni pamoja na kukomesha vita baina yenu na wao kwa miaka ishirini,

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wacha-Mungu”.**

Mtume ﷺ na Waislamu waliyafanya hayo vyema, waliyahifadhi masharti na Mkataba pamoja na watu wa Makkah tangu mwezi wa Dhul-Qaada katika mwaka wa sita, mpaka Makuraishi walipouvunja, kwa kuwasaidia marafiki zao wa Banu Bakr dhidi ya Khuza’ah, waliokuwa na urafiki na Mtume ﷺ, Banu Bakr wakawaua baadhi ya Banu Khuza’ah katika eneo takatifu.

Kwa ajili hiyo, Mtume ﷺ aliwapiga katika Tarehe ishirini ya mwezi wa Ramadhani katika mwaka wa nane. Allah تعالى Akampa ushindi katika eneo takatifu na Akammakinisha kuwatawala, basi sifa na shukrani zinamstahikia Allah تعالى. Mtume ﷺ akawaachilia huru Makuraishi waliosilimu baada ya kuelemeza na kushindwa, wakaitwa waachwa huru *At-Tulaqaa*. Walikuwa watu elfu mbili. Wale walioendelea kumkanusha wakatoroka, Mtume ﷺ aliwapelekea ahadi ya kuwepo amani na uhuru wa kutembea katika ardhi yoyote waliyoitaka, kwa kipindi cha miezi minne. Miongoni mwao ni Swafan bin Umayyah, ‘Ikrimah bn Abu Jahl na wengine. Baada ya hapo, Allah تعالى Aliwaongoza wakaingia katika Uislamu. Allah تعالى Ndiye wa Kusifiwa kwa Kudura na Matendo Yake yote.

كَيْفَ وَإِنْ يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ لَا يَرْقُبُوا فِيكُمْ إِلَّا وَلَا ذِمَّةً يُرْضُونَكُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ وَتَأْبَىٰ  
 قُلُوبُهُمْ وَأَكْفَرُهمَ فَسِقُونَ ﴿٨﴾

**8. Itakuwaje! Nao wakikushindeni hawatazami kwenu udugu wala ahadi. Wanakufurahisheni kwa midomo yao tu, na nyoyo zao zinakataa hayo. Na wengi wao ni wapotovu.**

Allah تعالى Anawahimiza Waumini kudhihirisha uadui dhidi ya Washirikina na kujitenga nao na kuwabainishia kuwa hawastahiki kunufaika na Mkataba wa amani, kwa sababu wanamshirikisha Allah تعالى na humkanusha Mjumbe Wake. Pia kwa sababu lau wangepata fursa ya kuwashinda Waislamu, wasingelimbakisha yeyote katika Waislamu, na wala wasingejali ndugu wala Mkataba. Ali bin Abu Twalhah, 'Ikrimah na Al-'Awfi walisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: "Maana ya "Illa" ni undugu na *Dhimmah* ni mkataba"<sup>1</sup>.

Adh-Dhahhak na As-Suddi walisema sawa na hivyo<sup>2</sup>.

أَشْرَوْا بِبَايَتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِهِمْ إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩﴾ لَا  
 يَرْقُبُونَ فِي مُؤْمِنٍ إِلَّا وَلَا ذِمَّةً وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُعْتَدُونَ ﴿١٠﴾ فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا  
 الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ فَإِخْوَانُكُمْ فِي الدِّينِ وَتُفْصِلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١١﴾

**9. Wamenunua thamani ndogo kwa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakazuilia watu na njia yake. Hakika hayo ni maovu waliyo kuwa wakiyatenda.**

**10. Hawatazami kwa Muumini udugu wala ahadi; basi hao ndio warukao mipaka.**

**11. Basi wakitubu na wakashika Sala na wakatoa Zaka, basi ni Ndugu zenu katika Dini. Na Tunazichambua Ayah kwa watu wajuao.**

Allah تعالى Anawaonya washirikina na Anawahimiza waumini juu ya kuwapiga.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:146.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:147.

أَشْتَرُوا بِقَابَتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا

**“Wamenunua thamani ndogo kwa Ishara za Mwenyezi Mungu.”**

Maana yake: Washirikina wamebadilishana kati ya kufuata Aya za Allah تعالى na mambo waliyoyatamani miongoni mwa mambo dhalili ya kidunia.

فَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِهِ

**“...na wakazuilia watu na njia yake.”** Maana yake: Wamewazuia Waumini dhidi ya kuifuata haki.

إِنَّهُمْ سَاءَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩﴾ لَا يَرْقُبُونَ فِي مُؤْمِنٍ إِلَّا وَّلَا ذِمَّةً

**“Hakika hayo ni maovu waliyokuwa wakiyatenda. Hawatazami kwa Muumini udugu wala ahadi.”**

Tafsiri ya Aya hii na Aya baada yake tayari imeshatangulia,

فَإِنْ تَابُوا وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ

**“Basi wakitubu na wakashika Sala”** Hadi mwisho wa Aya.

وَإِنْ نَكَتُوا أَيْمَانَهُمْ مِنْ بَعْدِ عَهْدِهِمْ وَطَعْنُوا فِي دِينِكُمْ فَقَاتِلُوا أَيْمَةَ الْكُفْرِ إِنَّهُمْ

لَا أَيْمَنَ لَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَنْتَهُونَ ﴿١٠﴾

**12. Na wakivunja viapo vyao baada ya kuahidi kwao, na wakatukana Dini yenu, basi Piganeni na viongozi wa ukafiri. Hakika hao hawana viapo vya kweli. Huenda (kwa hayo) wakaacha.**

**Viongozi wa Kikafiri Hawaheshimu Viapo Vyao.**

Allah تعالى Amesema, ikiwa Washirikina mliowekeana nao Mkataba wa amani wa muda maalumu watauvunja,

أَيْمَانَهُمْ

**“...viapo vyao.”** Maana yake: Masharti ya Mikataba na maagano yao.

وَطَعْنُوا فِي دِينِكُمْ

**“...na wakatukana Dini yenu”.** Wakaidharau na kuitia dosari Dini ya Allah



kwa kuitafutia ila na kasoro. Na kwa Aya hii ilitolewa hukumu ya kifo kwa wenye kumtukana Mtume ﷺ au kuishambulia Dini ya Kiislamu au kuitaja kwa nia ya kuitia ila. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

فَقَتِلُوا أَيْمَةَ الْكُفْرِ إِنَّهُمْ لَا أَيْمَنَ لَهُمْ لَعَلَّهُمْ يَنْتَهُوْنَ

**“...basi Piganeni na viongozi wa ukafiri. Hakika hao hawana viapo vya kweli. Huenda (kwa hayo) wakaacha”.**

Maana: Wakarejea na kutoyafanya hayo waliyomo (wakajirudi) miongoni mwa kufuru, uasi na upotevu. Qatadah na wengine walisema kuwa viongozi wa ukafiri walikuwa kina: Abu Jahl, ‘Utbah, Shaybah, Umayyah bin Khalaf na akataja na wengine kadhaa. A’mash alieleza kutoka kwa Zayd bin Wahb kuwa Hudhaifa رضي الله عنه alisema: “Watu waliozungumziwa katika Aya hii hawakupigwa tena”<sup>1</sup>. Kauli sawa na hii ilisimuliwa kutoka kwa ‘Ali bin Abu Talib رضي الله عنه, lililo sahihi ni kwamba hukumu ya Aya hii inawahusu watu wote, japokuwa sababu za kushushwa kwake iliwahusu Washirikina wa Kikuraish, Allah Aalam. Walid bin Muslim alisema, Swafwan bin Amri alitusimulia kutoka kwa ‘Abdur-Rahman bin Jubary bin Nufayr kuwa, “Tukio hili lilitokea katika zama za Abubakr رضي الله عنه pindi alipolituma jeshi kwenda Ash-Shaam, aliwapa maelekezo kuwa, ‘Huko mtawakuta watu walionyoa nywele vichwani mwao, hivyo waueni, kwani wao waliahidiana na shetani.’ Wallah! Kwangu mimi, kumuua mmoja miongoni mwao ni bora kuliko kuwaua sabiini wasiokuwa wao.”

Hayo ni kwa sababu Allah تعالى Alisema,

فَقَتِلُوا أَيْمَةَ الْكُفْرِ

**“...basi Piganeni na waongozi wa ukafiri”.**

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى aliikusanya.<sup>2</sup>



<sup>1</sup> At-Tabari 14:156.

<sup>2</sup> Ibn Abu Hatim 6:1761.

أَلَا تَقْتُلُونَ قَوْمًا نَكَثُوا أَيْمَانَهُمْ وَهَمُّوا بِإِخْرَاجِ  
 الرَّسُولِ وَهُمْ بَدَءُوكُمْ أُولَئِكَ مَرْءٌ أَنَخَشَوْنَهُمْ ۚ قَالَ اللَّهُ  
 أَحَقُّ أَنْ تَخْشَوْهُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾ قَتَلُوهُمْ  
 يُعَذِّبَهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَتَخْزِيهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ  
 صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ ﴿١٤﴾ وَيُذْهِبَ غَيْظَ قُلُوبِهِمْ ۚ  
 وَيَتُوبُ اللَّهُ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٥﴾ أَمْ  
 حَسِبْتُمْ أَنْ تُتْرَكُوا وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ  
 وَلَمْ يَتَّخِذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَا رَسُولِهِ وَلَا الْمُؤْمِنِينَ  
 وَلِجَاجَةً ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾ مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ  
 أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ بِالْكَفْرِ ۗ  
 أُولَئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ ﴿١٧﴾  
 إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ  
 وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الزَّكَاةَ وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ ۗ فَعَسَىٰ  
 أُولَئِكَ أَنْ يَكُونُوا مِنَ الْمُهْتَدِينَ ﴿١٨﴾

أَلَا تَقْتُلُونَ قَوْمًا نَكَثُوا أَيْمَانَهُمْ  
 وَهَمُّوا بِإِخْرَاجِ الرَّسُولِ وَهُمْ  
 بَدَءُوكُمْ أُولَئِكَ مَرْءٌ أَنَخَشَوْنَهُمْ ۚ  
 قَالَ اللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَوْهُ إِنْ كُنْتُمْ  
 مُؤْمِنِينَ ﴿١٣﴾ قَتَلُوهُمْ يُعَذِّبَهُمُ  
 اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَتَخْزِيهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ  
 عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ  
 مُؤْمِنِينَ ﴿١٤﴾ وَيُذْهِبَ غَيْظَ  
 قُلُوبِهِمْ ۚ وَيَتُوبُ اللَّهُ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ ۗ  
 وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٥﴾

13. Je, hamtapigana na  
 watu waliovunja viapo  
 vyao na wakawa na hamu  
 ya kumfukuza Mtume, nao  
 ndio waliokuanzeni mara  
 ya kwanza? Je, mnawa-  
 gopa? Basi Mwenyezi

*Mungu Anastahiki zaidi mumuogope, ikiwa nyinyi ni Waumini.*

14. Piganeni nao, Mwenyezi Mungu Awaadhibu kwa mikono yenu, na  
 Awahizi na Akunusuruni muwashinde, na Avipoze vifua vya kaumu ya  
 Waumini.

15. Na Aondoe hasira ya nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu Humkubalia toba  
 ya Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima.

**Uhimizaji wa Kupigana na Makafiri na Ubainifu wa Baadhi ya Faida Zake.**

Ayah hizi pia zinahamasisha, zinasisitiza na kupendekeza juu ya kuwapiga Washirikina wanaovunja masharti ya viapo vyao wale ambao Walijaribu kumtoa Mtume ﷺ kutoka Makkah. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٣٠﴾

***“Na walipokupangia mpango waliokufuru wakufunge, au wakuue, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu Akapanga Yake. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa Mipango”.***  
(8:30)

Aidha Allah تعالى Amesema,

يُخْرِجُونَ الرُّسُولَ وَإِيَّاكُمْ أَنْ تُؤْمِنُوا بِاللَّهِ رَبِّكُمْ

***“Wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu”.*** (60:1)

Kauli ya Allah تعالى،

وَإِنْ كَادُوا لَيَسْتَفِزُّوكَ مِنَ الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا

***“Na walitaka kukukera ili uitoke nchi”.*** (17:76)

Na Kauli ya Allah تعالى،

وَهُمْ بَدَأُوكُمْ أَوْلَٰكِ مَرَّةً

***“...nao ndio waliokuanzeni mara ya kwanza?”***

Ilisemwa kuwa makusudio yake ni siku ya Badr ambapo walitoka kwa ajili ya kuunusuru msafara wao, uliponusurika na wakalijua hilo, walisonga mbele kwa kutaka kupigana kwa sababu ya uasi na kiburi chao kama ilivyokwihatangulia kuelezwa kwa kirefu. Pia ilisemwa kuwa: Ni kutokana na kuvunja kwao masharti ya Mkataba na kushirikiana na marafiki zao, Banu Bakr kuwapiga Khuza'ah, waliokuwa marafiki wa Mtume ﷺ. Hii ndio sababu iliyomfanya Mtume ﷺ awaendee katika mwaka wa *Fat-h* na yakatokea yaliyotokea. Sifa njema na shukrani ni za Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى،

أَخْشَوْنَهُمْ ۖ فَاللَّهُ أَحَقُّ أَنْ تَخْشَوْهُ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ۚ

***“Je, mnawaogopa? Basi Mwenyezi Mungu Anastahiki zaidi mumuogope, ikiwa nyinyi ni Waumini”.***

Allah تعالى Anasema: “Msiwaogope makafiri bali Mniogope Mimi kwani Ndiye Ninayestahiki kuogopwa na waja, kwa sababu ya nguvu na adhabu Zangu. Amri iko Mikononi Mwangu, chochote Nikitakacho kiwe huwa, na Ninachokitaka kisiwe hakiwi. Kisha, Allah تعالى Akasema, huku Akiwaamuru Waumini na kubainisha Hikima Yake kwa Kuwajibisha Jihadi, licha ya kudura Yake ya Kuweza Kuwahilikisha maadui kwa amri kutoka Kwake”.

فَتِلْوَهُمْ يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَتُخْزِيهِمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَشْفِ صُدُورَ قَوْمٍ مُؤْمِنِينَ ۚ

***“Piganeni nao, Mwenyezi Mungu Awaadhibu kwa mikono yenu, na Awahizi na Akunusuruni muwashinde, na Avipoze vifua vya kaumu ya Waumini”.***

Aya hii inawaendea waumini wote. Mujahid, ‘Ikrimah na As-Suddi walitoa rai zao juu ya Aya hii: kwamba inawahusu Bani Khuza’ah<sup>1</sup>. Allah تعالى Alirejesha dhamiri katika Kauli Yake,

وَيَذْهَبَ غَيِّظَ قُلُوبِهِمْ ۚ

***“Na Aondoe hasira ya nyoyo zao.”*** Kwao vile vile.

وَيَتُوبُ اللَّهُ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ ۚ

***“Na Mwenyezi Mungu Humkubalia toba ya Amtakaye.”*** Kwa maana: Katika waja Wake.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ ۚ

***“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua.”*** Kwa maana: Juu ya yenye maslahi kwa waja Wake.

حَكِيمٌ ۚ

***“Mwenye Hikima.”*** Katika matendo mazuri na Kauli Zake za mwenendo wa kimaumbile na za kisharia, na kwa hivyo Hufanya Ayatakayo na Anahukumu Atakavyo. Yeye ni Hakimu Muadilifu Ambaye abadani Hapunji chochote wala Hapotezi kheri wala shari yoyote, japo yenye uzito wa mdudu chungu, bali hulipa duniani na Akhera.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:161.

أَمْرٍ حَسِبْتُمْ أَنْ تُتْرَكُوا وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَلَمْ يَتَّخِذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَا رَسُولِهِ وَلَا الْمُؤْمِنِينَ وَلِجَنَّةٍ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

**16. Je, mlidhani kuwa mtaachwa tu, bila ya Mwenyezi Mungu Kuwajuulisha wale waliopigana Jihadi kati yenu, na wala hawakumfanya mwendani wao isipokuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Waumini wenziwe? Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za yote mnayo yatenda.**

**Miongoni mwa Hikima za Jihadi ni Kuwajaribu Waislamu.**

Allah تعالى Anasema,

أَمْرٍ حَسِبْتُمْ

**“Je, mlidhani”** Enyi Waumini kwamba Tutakuacheni hivi hivi na Kukupuuzeni bila ya Kukujaribu kwa mambo ya Kuwadhihirisha wale wenye azma ya kweli na wale waongo? Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema,

وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَلَمْ يَتَّخِذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَا رَسُولِهِ وَلَا الْمُؤْمِنِينَ  
وَلِجَنَّةٍ

**“...bila ya Mwenyezi Mungu Kuwajuulisha wale walio pigana Jihadi kati yenu, na wala hawakumfanya mwendani wao isipo kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Waumini wenziwe?”**

Kwa maana: Mwandani na rafiki wa siri Allah تعالى na Mtume ﷺ kwa dhahiri na kwa ndani na wakatosheka na namna hiyo, si vinginevyo. Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَأَمَّنُوا بِكُمْ أُولَئِكَ الَّذِينَ كَانُوا يُرِيدُونَ الْجَنَّةَ وَلِجَنَّةٍ كَانُوا فِيهَا سَاهِبِينَ ﴿١٧﴾ وَالَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَأَمَّنُوا بِكُمْ أُولَئِكَ الَّذِينَ كَانُوا يُرِيدُونَ الْجَنَّةَ وَلِجَنَّةٍ كَانُوا فِيهَا سَاهِبِينَ ﴿١٨﴾ وَالَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَأَمَّنُوا بِكُمْ أُولَئِكَ الَّذِينَ كَانُوا يُرِيدُونَ الْجَنَّةَ وَلِجَنَّةٍ كَانُوا فِيهَا سَاهِبِينَ ﴿١٩﴾

**“Alif Lam Mim (A.L.M) Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Nao wasijaribiwe? Hakika Tuliwajaribu waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Mwenyezi Mungu Atawatambulisha walio wa kweli na Atawatambulisha walio waongo”. (29:1-3)**

Na Kauli Yake katika Aya nyingine,

﴿١٤﴾ **أَمْرٌ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الصَّابِرِينَ**  
**“Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu Hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana Jihadi, na hajawapambanua waliosubiri?” (3:142)**

Na Allah تعالى Amesema:

﴿١٧﴾ **مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ**  
**“Haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwaacha Waumini katika hali mliyo nayo mpaka Apambanue wabaya na wema”. (3:179)**

Kwa ujumla, Allah تعالى Alipoiwajibisha Jihadi kwa waja Wake alibainisha kuwa kuna hikima katika hilo, nayo ni Kuwajaribu waja Wake na Kuwadhihirisha wale wenye kumtii na wale wenye kumuasi, na Yeye ni Mwenye Kuyajua vyema yaliyotukia, yaliyomo na yatakayotukia, na namna yatakavyotukia. Kwa hivyo, Allah تعالى Anakijua kitu kabla ya kutukia pamoja na namna ya kufanyika kwake. Hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye, wala hapana mola Mlezi ghairi Yake, wala hapana wa kuyarudisha Aliyoyakadiria na Kuyapitisha.

﴿١٨﴾ **مَا كَانَ لِلْمُشْرِكِينَ أَنْ يَعْمُرُوا مَسْجِدَ اللَّهِ شَاهِدِينَ عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ بِالْكَفْرِ أُولَٰئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ** ﴿١٩﴾ **إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَءَاتَى الزَّكَاةَ وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ فَعَسَىٰ أُولَٰئِكَ أَنْ يَكُونُوا مِنَ الْمُهْتَدِينَ** ﴿٢٠﴾

**17. Haiwi kuwa makafiri ndio waimarishe Misikiti ya Mwenyezi Mungu, hali wanajishuhudishia wenyewe ukafiri. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika, na katika Moto watadumu.**

**18. Hakika wanaoimarisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na wakashika Sala na wakatoa Zaka, na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu. Basi huenda hao wakawa katika waongofu.**

**Washirikina Si Waimarishaji Misikiti ya Allah تعالى.**

Allah تعالى Anasema kuwa Washirikina hawawezi kuimarisha Misikiti ambayo imejengwa juu ya Jina Lake Yeye, Peke Yake, Asiyeye na mshirika. Kuna mwenye kusoma Ayah, "*Masjida Allah - Misikiti wa Allah*" badala ya "*Masaajida Allah - Misikiti ya Allah*" na kusema kuwa kinachokusudiwa ni *Al-Masjid Al-Haram*, Misikiti Mtukufu zaidi kuliko yote ardhini, ambao ulijengwa tangu siku ya kwanza, ili kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, Asiyeye na mshirika. Misikiti ambao uliwekwa na *Al-Khalil Ar-Rahman* (Nabii Ibrahim عليه السلام). Washirikina Hufanya hili, huku wakishuhudia kwa nafsi zao kuhusu ukafiri, yaani kwa hali yao na kauli zao. As-Suddi alisema, "Lau kama utamuuliza Mkristo, "Dini yako ni ipi?" Atajibu: "Ukristo". Na kama utamuuliza Yahudi, "Dini yako ni ipi?" Atajibu: "Uyahudi". Kadhalika Sabi-i na mshirikina angelisema ni mshirikina.<sup>1</sup>

أُولَئِكَ حَبِطَتِ أَعْمَلُهُمْ

**"Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika".** Kwa sababu ya ushirikina wao.

وَفِي النَّارِ هُمْ خَالِدُونَ

**"...na katika Moto watadumu".** Allah تعالى Alisema katika Ayah nyingine.

وَمَا لَهُمْ آلَا يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ وَهُمْ يَصُدُّونَ عَنِ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ ۗ إِنَّ

أَوْلِيَاءَهُ ۗ إِلَّا الْمُتَّقُونَ وَلَئِنْ أَكْثَرْتَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨٣﴾

**"Lakini wana jambo gani hata Mwenyezi Mungu Asywaadhibu, na hali ya kuwa wanawazuilia watu Misikiti Mtakatifu? Wala wao hawakuwa ndio walinzi wake, bali walinzi wake hawakuwa ila wacha-Mungu tu. Lakini wengi katika wao hawajui". (8:34)**

**Waumini wa Kiislamu Ndio Waimarishaji wa Misikiti.**

Allah تعالى Alisema:

إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسْجِدَ اللَّهِ مَن ءَامَنَ ۖ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

**"Hakika wanao amirisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanao muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho".**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:165

Kwa hivyo Allah تعالى Anashuhudia imani ya wanaostawisha Misikiti. Ameandika At-Tirmidhi na Ibn Marduwayah na Al-Hakim ndani ya Al-Mustadrak yake<sup>1</sup>. 'Abdur-Razzaq alisimulia kuwa 'Umar bin Maymun Al-Awadi alisema: "Niliwakuta Masahaba wa Mtume ﷺ wakisema, "Misikiti ni nyumba za Allah ardhini, na ni haki ya Allah تعالى kuwakirimu wanaomtembelea katika misikiti hiyo." Kauli ya Allah تعالى,

وَأَقَامَ الصَّلَاةَ

**"...na wakashika Sala".**

Ambayo ndiyo ibada kubwa zaidi inayofanywa na mwili.

وَأَتَى الزَّكَاةَ

**"...na wakatoa Zaka".**

Ambayo ndiyo amali bora zaidi ambayo huwanufaisha viumbe. Na Kauli Yake,

وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ

**"...na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu".**

Maana yake: Hawamuogopi wala kumkhofu yeyote isipokuwa Allah تعالى.

فَعَسَىٰ أَوْلَتْكَ أَن يَكُونُوا مِنَ الْمُهْتَدِينَ

**"Basi huenda hao wakawa katika waongofu".**

'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alitolea rai Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّمَا يَعْمُرُ مَسَاجِدَ اللَّهِ مَنِ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

**"Hakika wanaoimarisha Misikiti ya Mwenyezi Mungu ni wale wanao muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho".**

Anasema, "Maana yule mwenye kumpwekesha Allah تعالى na akaiamini Siku ya Mwisho. Kwa maana ya kwamba anayaamini aliyoyateremsha Allah تعالى ,

وَأَقَامَ الصَّلَاةَ

**"...na wakashika Sala".** Inamaanisha Sala tano.

<sup>1</sup> Tuhfatul - Ahwadhi 7:365 na Al-Hakim 1/212.



وَلَمْ يَخْشَ إِلَّا اللَّهَ<sup>ط</sup>

***"...na wala hawamchi ila Mwenyezi Mungu".***

Maana yake: Hawamuabudu yeyote isipokuwa Allah تعالى. Kisha Akasema,

فَعَسَىٰ ۚ أَوْلَىٰ لَكَ أَنْ يَكُونُوا مِنَ الْمُهْتَدِينَ

***"Basi huenda hao wakawa katika waongofu".***

Allah تعالى Anasema, "Hakika hao ndio waliofaulu". Ni sawa na Kauli nyingine, kumuambia Mtume wake ﷺ,

عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا

***"Huenda Mola wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinacho sifika".***

**(17:79)**

Allah تعالى Anaeleza hapa, "Mola wako Mlezi ewe (Muhammad ﷺ) Atakupa cheo cha sifa, yaani uombezi (katika Siku ya Kiama). Kila neno 'Asaa' linapotumika katika Qur'an lina maana ya lazima 'kitakuwa'.<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 14:167.

\* أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ كَمَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَجَاهِدَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ<sup>٤</sup> وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ أَعْظَمُ دَرَجَةً عِنْدَ اللَّهِ<sup>٥</sup> وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾ يُبَشِّرُهُمْ رَبُّهُمْ بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَرِضْوَانٍ وَجَنَّتْ لَهُمْ فِيهَا نَعِيمٌ مُقِيمٌ ﴿٢١﴾ خَلْدِيذِينَ فِيهَا أَبَدًا<sup>٦</sup> إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٢﴾ يَتَأَيُّمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا ءَابَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ أَوْلِيَاءَ إِنِ اسْتَحَبُّوا الْكُفْرَ عَلَى الْإِيمَانِ<sup>٧</sup> وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنكُمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٢٣﴾ قُلْ إِن كَانَ ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسْكِنٌ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرْتَضُوا حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ<sup>٨</sup> وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٤﴾ لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ<sup>٩</sup> وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُم مُّدْبِرِينَ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا<sup>١٠</sup> وَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿٢٦﴾ ثُمَّ يَتُوبُ اللَّهُ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ عَلَى مَنْ يَشَاءُ<sup>١١</sup> وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٧﴾

\* أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ كَمَنْ ءَامَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَجَاهِدَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ<sup>٤</sup> لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ<sup>٥</sup> وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٩﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَهَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ أَعْظَمُ دَرَجَةً عِنْدَ اللَّهِ<sup>٥</sup> وَأُولَئِكَ هُمُ الْفَائِزُونَ ﴿٢٠﴾ يُبَشِّرُهُمْ رَبُّهُمْ بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَرِضْوَانٍ وَجَنَّتْ لَهُمْ فِيهَا نَعِيمٌ مُقِيمٌ ﴿٢١﴾ خَلْدِيذِينَ فِيهَا أَبَدًا<sup>٦</sup> إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٢﴾

19. "Je, mnafanya kuwanyweshwa maji Mahujaji na kuamirisha Msikiti Mtakatifu ni sawa na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya Mwisho, na akapigana Jihadi kwa njia ya Mwenyezi Mungu? Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Hawa-ongoi watu madhalimu"

20. **“Wale walioamini, na wakahama, na wakapigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao, hao wana cheo kikubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hao ndio wenye Kufuzu”.**

21. **“Mola wao Mlezi Anawabashiria rehema zitokazo Kwake, na radhi, na Bustani ambazo humo watapata neema za kudumu”.**

22. **“Watadumu humo milele. Hakika kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo makubwa”.**

### **Kuwapa Maji Mahujaji na Kuimarisha Msikiti Mtukufu Masjidul-Haraam Havilingani na Imani na Jihadi.**

Al-Awfi alisema katika tafsiri yake kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما katika kuitafsiri Ayah hii kuwa: Washirikina walisema, “Kuistawisha Nyumba ya Allah عزوجل na kuwapatia maji wanaohiji ni bora zaidi kuliko kuwa na imani ya Mungu Mmoja na kupigana Jihadi”. Walikuwa wakijifakharisha na kufanya kiburi kwa watu sababu walikuwa wakidai kuwa wao ndio wahusika na wastawishaji wa Msikiti Mtakatifu “Al-Masjid Al-Haram.” Ndiyo maana Allah تعالى Akazungumzia kuhusu – kiburi chao na kwenda kwao kinyume na imani na Akawaambia wakazi wanaoishi eneo takatifu “Haram” miongoni mwa Washirikina wa Makkah.

فَدَ كَانَتْ ءَايَتِي تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فَكُنْتُمْ عَلَيَّ أَعْقَابِكُمْ تَنَكُّبُونَ ﴿٦٦﴾ مُسْتَكْبِرِينَ بِمِءِ سَنَمِرًا  
تَهْجُرُونَ ﴿٦٧﴾

**“Hakika zilikuwa Ayah Zangu mkisomewa nanyi mkirudi nyuma juu ya visigino vyenu. Na huku mkitakabari na usiku mkiizungumza (Qur’an) kwa dharau”. (23:66-67)**

Maana yake: Walikuwa wakifanya kiburi kwa kuwa ndio wakazi wa eneo takatifu la Al-Haram. Allah تعالى Alisema:

بِمِءِ سَنَمِرًا تَهْجُرُونَ ﴿٦٧﴾

**“...na usiku mkiizungumza (Qur’an) kwa dharau.”** Walikuwa wakiyazungumza haya nyakati za usiku huku wakiihama Qur’an na kumtukana Allah تعالى na Mtume ﷺ. Allah تعالى Akatangaza kwamba Imani na Jihadi pamoja na Mtume ﷺ ni bora zaidi kuliko wanayoyafanya Washirikina ya kuistawisha Nyumba na

kujishughulisha kwao na kuwapatia maji wanaohiji. Mambo yao hayo hayakuwa yakiwanufaisha mbele ya Allah تعالى, kwa sababu walikuwa wakimshirikisha, licha ya kwamba walikuwa wakiimarisha Nyumba Yake na kuihudumia. Allah تعالى Amesema,

لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

**“Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu  
Hawaongoi watu madhalimu”**

Wale waliodai kuwa ni waamirishaji wa Nyumba, Allah تعالى Ameeleza kuwa wana dhuluma kwa sababu ya ushirikina wao na kuimarisha kwao hakutawaepushia lolote.

‘Ali bin Abii Twalha alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuhusu tafsiri ya Aya hii: “Aya hii ilishuka kumhusu Al-‘Abbas bin ‘Abdul-Muttwalib kwani alipokamatwa katika vita vya Badr, alisema, ‘Kama mlitutangulia kusilimu, kufanya Hijrah na Jihadi, sisi tulikuwa tukiimarisha Msikiti Mtakatifu “Al-Masjid Al-Haram” kwa kuwapa maji wanaohiji na kuwasaidia walioelemewa na madeni, Allah تعالى Akashusha Aya,

أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ

**“Je, mnafanya kuwanyweshwa maji Mahujaji”**. Mpaka Kauli Yake Allah تعالى,

وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

**“Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhalimu”**. Maana yake: Wale ambao walidhani kuwa wao ndio wenye kuustawisha Al-Masjid Al-Haram, Allah تعالى Amewaita madhalimu kwa sababu ya shirki yao, kwa hivyo, kustawisha kwao Msikiti hakukuwafaa hata kidogo<sup>1</sup>. ‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliitafsiri aya hii kwa kusema, “Ilishuka kumhusu ‘Abbas bin ‘Abdul-Muttwalib pindi alipotekwa katika vita vya Badr, alisema, “Ikiwa mmetutangulia katika kusilimu, Hijra na Jihadi, basi sisi tulikuwa tukiamirisha msikiti mtakatifu Al-Masjid Al-Haram, tukiwapa maji mahujaji na kumuachilia huru mwenye kuzongwa na madeni. Ndio maana Allah تعالى Amesema,

أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ

**“Je, mnafanya kuwanyweshwa maji Mahujaji”**.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:170.

Kwa maana: “Amali hizi zilifanyika wakiwa bado wako katika ushirikina wala Mimi sipokei amali anayoifanya mtu ilhali angali katika hali ya ushirikina”<sup>1</sup>. Adh-Dhahhak bin Muzahim alisema: “Waislamu walikuja kwa Al-’Abbas na marafiki zake waliotekwa katika vita vya Badr na wakawa wanawasimanga kwa kuwa bado wapo katika ushirikina. Al-’Abbas alisema, “Wallah! Sisi tulikuwa tukiuiimarisha Msikiti Mtakatifu “*Masjid Al-Haram*” tunamkomboa mwenye madeni, tunaihudumia Ka’aba kwa kuifunika vazi lake na tunawapatia maji mahujaji”. Allah تعالى Akateremsha Aya hii,

أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ

**“Je, mnafanya kuwanyweshwa maji Mahujaji”<sup>2</sup>.**

Kuna Hadithi *Marfu’*juu ya tafsiri ya Aya hii na hatuna budi kuitaja hapa. ‘Abdur-Razzaq aliandika kuwa An-Nu’maan bin Bashir alisema, kuna mtu alisema, “Mimi sijali ikiwa sitafanya amali yoyote baada ya kusilimu zaidi ya kuwapatia maji wenye kuhiji”. Mwingine akasema, “Mimi sitajali hata kama sitafanya amali yoyote baada ya kusilimu, isipokuwa kuustawisha Msikiti Mtakatifu “*Al-Masjid Al-Haram*.” Mwingine akasema, “Jihadi katika njia ya Allah تعالى ni bora zaidi kuliko mliyoyasema”. Umar رضي الله عنه akawakemea kwa kuwaambia: “Mspipaze sauti zenu mbele ya mimbari ya Mtume ﷺ”. Ilikuwa siku ya Ijumaa, “Lakini tukishamaliza kusali Ijumaa tutakwenda kwa Mtume ﷺ kumuuliza. Hivyo ikashushwa Aya,

أَجَعَلْتُمْ سِقَايَةَ الْحَاجِّ وَعِمَارَةَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ

**“Je, mnafanya kuwanyweshwa maji Mahujaji na kuamrisha Msikiti Mtakatifu.”** Hadi Kauli Yake Allah تعالى,

لَا يَسْتَوُونَ عِنْدَ اللَّهِ<sup>3</sup>

**“Hawawi sawa mbele ya Mwenyezi Mungu”<sup>3</sup>.**

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا ءَابَاءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ ءَوْلِيَاءَ إِنِ اسْتَحَبُّوا الْكُفْرَ عَلَى الْإِيمَانِ ؕ وَمَنْ يَتَوَلَّهُمْ مِنكُمْ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٩١﴾ قُلْ إِن كَانَ ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا وَتِجَارَةٌ

<sup>1</sup> At-Tabari 14:170.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:172.

<sup>3</sup> Muslim No. 1879 na Abdurazak 2:268.

نَحْشُونَ كَسَادَهَا وَمَسْلِكُنْ تَرْضَوْنَهَا أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنْ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرْتَوُوا حَتَّى يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٢٣﴾

23. *“Enyi mlioamini! Msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanastahabu ukafiri kuliko Imani. Na katika nyinyi atakayewafanya hao ndio vipenzi vyake, basi hao ndio madhalimu”.*

24. *“Sema: Ikiwa baba zenu, na wanenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyoyachuma, na biashra mnazoogopa kuharibika, na majumba mnayoyapenda, ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Jihadi katika njia Yake, basi ngojeni mpaka Mwenyezi Mungu Alete amri Yake. Na Mwenye Mungu Hawaongoi watu wapotovu”.*

**Amri ya Kukataza Kuwafanya Vipenzi na Marafiki Washirikina, Hata Kama ni Ndugu wa Karibu.**

Allah تعالى Ameamuru kujitenga dhidi ya makafiri hata kama ni Wazazi au watoto wako, na Amekataza jambo la kuwafanya marafiki ikiwa watakhitari ukafiri badala ya Imani. Allah تعالى Ameyaonya hayo ndani ya Kauli Yake,

لَا يَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَوْ كَانُوا آبَاءَهُمْ أَوْ أَبْنَاءَهُمْ أَوْ إِخْوَانَهُمْ أَوْ عَشِيرَتَهُمْ أُولَئِكَ كَتَبَ فِي قُلُوبِهِمُ الْإِيمَانَ وَأَيَّدَهُمْ بِرُوحٍ مِنْهُ وَيُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

*“Huwakuti watu wanaoamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hata wakiwa ni baba zao, au watoto wao, au ndugu zao, au jamaa zao. Hao ameandika katika nyoyo zao Imani, na Amewapa nguvu kwa Roho itokayo Kwake. Na Atawaingiza katika bustani zipitazo mito kati yake”. (58:22)*

Hafidh Al-Bayhaqi aliandika kutokana na khabari ya ‘Abdul bin Shawdhab kuwa alisema: “Baba wa Abu ‘Ubaydah bin Al-Jarrah alikuwa akimsifia miungu ya masanamu mwanaye siku ya vita vya Badr, naye Abu ‘Ubaydah akawa

anajiepusha naye. Baada ya Al-Jarrah kukithirisha, Abu 'Ubaydah alimkabili na kisha akamuua. Allah تعالى Akaiteremsha Aya hii,

لَا تَجِدُ قَوْمًا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ يُوَادُّونَ مَنْ حَادَّ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

**“Huwakuti watu wanaoamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho kuwa wanawapenda wanaompinga Mwenyezi Mungu na Mtume Wake”. (58:22)<sup>1</sup>**

Kisha, Allah تعالى Alimuamuru Mtume Wake ﷺ awaonye wale wenye kuziona bora familia, Ndugu na jamaa zao badala ya Allah تعالى, Mjumbe Wake ﷺ na Jihadi katika Njia Yake. Alisema,

قُلْ إِنْ كَانَ آبَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ وَإِخْوَانُكُمْ وَأَزْوَاجُكُمْ وَعَشِيرَتُكُمْ وَأَمْوَالٌ اقْتَرَفْتُمُوهَا

**“Sema: Ikiwa baba zenu, na wanenu, na ndugu zenu, na wake zenu, na jamaa zenu, na mali mliyoyachuma”.**

Maana: Mizozipata na mlizozichuma.

وَتِجَارَةٌ تَخْشَوْنَ كَسَادَهَا وَمَسَاكِينُ تَرْضَوْنَهَا

**“...na biashra mnazoogopa kuharibika, na majumba mnayoyapenda”.**

Mnayoyapenda kwa sababu ya uzuri wake. Kwa maana; ikiwa vitu hivi,

أَحَبَّ إِلَيْكُمْ مِنَ اللَّهِ وَرَسُولِهِ وَجِهَادٍ فِي سَبِيلِهِ فَتَرَبَّصُوا

**“...ni vipenzi zaidi kwenu kuliko Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Jihadi katika Njia Yake, basi ngojeni”.**

Adhabu na majanga yatakayokufikieni. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema:

حَتَّى يَأْتِيَكُمُ اللَّهُ بِأَمْرِهِ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ

**“...mpaka Mwenyezi Mungu Alete Amri Yake. Na Mwenye Mungu Hawaongoi watu wapotovu”.**

Imamu Ahmad aliandika kuwa Zuhrah bin Ma'bad alipokea kutoka kwa babu yake kuwa alisema, “Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ akiwa amemshika mkono 'Umar bin Al-Khattawab رضي الله عنه, naye akasema, “Wallahi! Wewe, ewe

<sup>1</sup> Al-Bayhaqi 9:27.

Mtume! Ni mpendwa kwangu zaidi kuliko kila kitu, isipokuwa nafsi yangu".  
Mtume ﷺ akasema,

«لَا يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتَّىٰ أَكُونَ أَحَبَّ إِلَيْهِ مِنْ نَفْسِهِ»

*"Yeyote miongoni mwenu hawi muumini, mpaka niwe mpendwa wake, kuliko hata nafsi yake".*

'Umar رضي الله عنه akasema, "Sasa, Wallahi! Nakupenda kuliko hata nafsi yangu".

Mtume ﷺ akasema,

«الآنَ يَا عُمَرُ»

*"Sasa umekamilika ewe 'Umar".<sup>1</sup>*

Bukhari ndiye peke yake aliyeikusanya Hadithi hii.<sup>2</sup> Imamu Ahmad na Abu Dawud nao waliinukuu, na lafudhi ni yake, kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa alisema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

إِذَا تَبَايَعْتُمْ بِالْعَيْتَةِ وَأَخَذْتُمْ بِالذَّنَابِ الْبُقَرِ وَرَضَيْتُمْ بِالزَّرْعِ، وَتَرَكْتُمُ الْجِهَادَ سَلَطَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ ذُلًّا لَا يَنْزِعُهُ حَتَّىٰ تَرْجِعُوا إِلَىٰ دِينِكُمْ»

*"Ikiwa mtauziana kwa njia ya 'lynah (namna ya riba), na mkafuata mikia ya ng'ombe, mkawa radhi na kilimo, mkaitelekeza Jihadi, Allah Atakuleteeni udhalili ambao Hatauondoa, mpaka mtakaporejea katika Dini yenu"<sup>3</sup>.*

لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ فِي مَوَاطِنَ كَثِيرَةٍ وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا وَضَاقَتْ عَلَيْكُمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ ثُمَّ وَلَّيْتُم مُّدْبِرِينَ ﴿١٦﴾ ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا وَعَذَّبَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَذَلِكَ جَزَاءُ الْكَافِرِينَ ﴿١٧﴾ ثُمَّ يَتُوبُ اللَّهُ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ عَلَىٰ مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٨﴾

<sup>1</sup> Ahmad 4:336.

<sup>2</sup> Fat'hul Al\_Bari 11:532.

<sup>3</sup> Ahmad 2:42 na Abu Dawud 3462.



**25. "Hakika Mwenyezi Mungu Amekunusuruni katika mapigano mengi, na siku ya Hunayni ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu. Na ardhi ikawa dhiki kwenu juu ya upana wake. Kisha mkageuka na kurudi nyuma".**

**26. "Kisha Mwenyezi Mungu Akateremsha utulivu wake juu ya Mtume Wake na juu ya Waumini. Na Akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona, na Akawaadhibu wale walio kufuru. Na hayo ndiyo malipo ya makafiri".**

**27. "Kisha baada ya hayo Mwenyezi Mungu Atawasamehe Awatakao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu".**

### **Matokeo ya Ushindi ni kwa Msaada wa Allah تعالی.**

Ibn Jurayj alisema kutoka kwa Mujahid: "Hii ndio Aya ya kwanza ya *Al-Baraaah* kuteremshwa, ambapo, Allah تعالی Anawakumbusha Waumini namna Alivyowapa fadhila na ihsani kwa kuwapa ushindi katika vita vingi walivyopigana kwa kushirikiana na Mjumbe Wake ﷺ, na kwamba hayo yanatoka Kwake, na ni kwa Nguvu na Kudura Zake, si kwa idadi na zana zao za kivita. Pia Amewaeleza kwamba ushindi hutoka Kwake bila ya kujali kuwa wapiganaji ni wengi au ni wachache, kwani katika vita vya Hunayn walijifakharisha na wingi wao. Pamoja na hayo, hilo halikuwasaidia hata kidogo, wakageuka na kukimbia, isipokuwa wachache miongoni mwao waliosalia pamoja na Mtume ﷺ, Halafu Allah تعالی Akateremsha nusura na msaada Wake kwa Mjumbe Wake ﷺ na Waumini waliokuwa pamoja naye, kama tutakavyoelezea, Insha Allah, ili Awajulishe kwamba ushindi hutoka Kwake Peke Yake na kwa Msaada Wake hata kama idadi yao ni wachache.

### **Tukio la Vita vya Hunayn.**

Vita vya Hunayn vilitokea baada ya ufunguzi wa Makkah katika mwezi wa Shawwal mwaka wa nane baada ya Hijra. Hayo ni baada ya Mtume ﷺ kukamilisha tukio la ufunguzi wa Makkah na mambo yakatulua na wakazi wake wote wakasilimu na Mtume ﷺ akawaachia huru (*Tulaqaa*). Khabari zikamfikia Mtume ﷺ kwamba kabila la Hawazin wamejikusanya kwa ajili ya kumpiga,

na kwamba kiongozi wao, Malik bin Awf An-Nasri akiwa pamoja na kabila zima la Thaqif, makabila ya Banu Jusham, Banu Sa'd bin Bakr, na kundi kutoka Banu Hilal, na watu wachache kutoka kwa Banu 'Amri bin 'Amir na 'Awfi bin 'Amir. Walikuja pamoja na wanawake, watoto, kondoo, mifugo pamoja na majeshi yao yaliyosheheni silaha. Mtume ﷺ akatoka pamoja na jeshi lake alilokuja nalo kwa ajili ya ufunguzi wa Makka ili awakabili, ambalo ni pamoja na Muhajirina na Ansar elfu kumi, yakiwemo makabila kadhaa ya Waarabu, wakiwemo pia watu wa Makkah waliosilimu na kuachiliwa huru ambao walifikia idadi ya elfu mbili. Mtume ﷺ akaenda nao pamoja, wakakutana na adui mpaka katika bonde baina ya Makkah na Twaif, lililoitwa Hunayn. Vita hivi vilianza mapema asubuhi majeshi ya Waislamu yalipotoremka katika bonde hilo, ilhali hawatambui kuwa Hawazin wamejificha katika bonde hilo. Ghafla Waislamu wakashtukizwa kwa mashambulizi, wakarushiwa mikuki na kukatwa mapanga. Walishambulia ushambulizi wa mara moja, kwa mujibu wa walivyoomrisha na kiongozi wao. Baada ya hapo Waislamu waligeuka na kukimbia, sawa na ilivyosema Kauli ya Allah تعالى. Mtume ﷺ akabaki imara mahali pake huku akiwa amepanda juu ya nyumbu wake, Ash-Shahba-a, akimuelekeza mkabala wa adui. Wakati huo huo ami yake Abbas رضي الله عنه alikuwa ameshikilia hatamu ya upande wa kuumeni mwa nyumbu huyo, na Abu Sufyan bin Al-Harith bin 'Abdul-Muttwalib رضي الله عنه akiwa ameshikilia hatamu ya upande wa kushoto. Walifanya hivyo, ili nyumbu asikimbie mwendo wa haraka kumuelekea adui. Mtume ﷺ alikuwa akilitaja jina lake na kuwataka Waislamu warejee, akisema:

«إِلَيَّ عِبَادَ اللَّهِ إِلَيَّ أَنَا رَسُولُ اللَّهِ»

*“Njoooni kwangu, enyi waja wa Allah! Njoooni kwangu, mimi ni Mjumbe wa Allah”.*

Alikuwa akifuatishia maneno haya,

«أَنَا النَّبِيُّ لَا كَذِبَ. أَنَا ابْنُ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ»

*“Mimi ni Mtume, si uongo. Mimi ni mwana wa 'Abdul-Muttwalib”.*

Pamoja naye, Masahaba wake wapatao mia moja walibaki imara pia. Wapokezi wa Hadithi wengine walisema kuwa walikuwa themanini. Miongoni mwao alikuwepo Abubakr, 'Umar, Al-'Abbas, 'Ali, Al-Fadhl bin 'Abbas, Abu Sufyan bin

Al-Harith, Ayman, Usamah bin Zayd na wengine wengi رضي الله عنهم. Halafu, Mtume ﷺ akamuamuru ami yake Al-'abbas رضي الله عنه, ambaye alikuwa ni mwenye sauti kubwa atangaze kwa sauti yake ya juu kwamba, "Enyi Masahaba wa Mti". Yaani, mti wa *baia* ya *Ar-Ridhwaan* ambapo Waislamu, miongoni mwa Muhajiruna na Ansar walimuambia Mtume ﷺ chini yake kwamba abadani hawatamkimbia. Akawa anawaita, "Enyi Masahaba wa Mti wa Samurah!" Wakati mwingine alikuwa akisema: "Enyi Masahaba wa *Surat Al-Baqarah!*". Waliposikia hivyo wakaitika: "Tunakuja tunakuja!" Waislamu wakawa wanarejea kwa Mtume ﷺ, ilipotokea farasi wa mmoja wao hakumtii (kwa kuwa watu wengi walikuwa wameshughulishwa na muelekeo mmoja wa kukimbia), basi aliweza kuvaa ngao yake na kuteremka na kukimbilia upande alikokuwa Mtume ﷺ kwa miguu. Baada ya kundi kubwa kurejea kwake, Aliwaamuru wapigane, akichota gao la mchanga na akaomba Nusura kutoka kwa Allah تعالى,

«اللَّهُمَّ أَنْجِزْ لِي مَا وَعَدْتَنِي»

"Ewe Allah! Nitimizie uliyoniahidi".

Halafu akawarushia maadui, kila adui aliingiwa na mchanga huo machoni na mdomoni mwake kiasi cha kumshughulisha mbali na kuacha mapigano. Baada ya hapo makafiri wakakimbia, Waislamu wakawawinda huku wakiwaua na kuwateka. Waislamu wengine walirejea (vitani taratibu) na wakawakuta mateka wengi wa kikafiri wakiwa wamefungwa mbele ya Mtume ﷺ.

Ndani ya *Sahih* mbili kuna Hadithi ya Shu'bah kutoka kwa Abu Is-haq kuwa Al-Baraa bin 'Azib alisema kuwa kuna mtu alimuambia: "Ewe Abu Umarah! Siku ya Hunayn mlukimbia na kumuacha Mjumbe wa Allah?" akasema: "Lakini Mtume ﷺ hakukimbia. Kabila la Hawazin walikuwa ni watupa mishale hodari, basi tulipokabiliana nao, tuliwashambulia na wakageuka nyuma kukimbia. Watu wakaanza kuziendea ghanima maadui wakatushambulia kwa mishale, basi Waislamu wakakimbia. Nilimuona Mtume ﷺ huku Abu Sufyan bin Al-Harith رضي الله عنه akishikilia lijamu za nyumbu wake mweupe, huku akisema:

«أَنَا النَّبِيُّ لَا كَذِبَ - أَنَا ابْنُ عَبْدِ الْمُطَّلِبِ»

"Mimi ni Mtume, si uongo. Mimi ni mwana wa 'Abdul-Muttwalib"<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 6:81 na Muslim 3:1401.

Hii inaonesha kiwango cha juu cha ushujaa wake na ukomavu wa Mtume ﷺ katika siku hii, akiwa amezingirwa na mapigano, na wakati huo huo jeshi lake limekimbia na kumuacha yeye bila ulinzi. Licha ya haya yote, bado aliendelea kuwa juu ya nyumbu wake, mnyama mwenye mwendo usio wa kasi, asiyeweza kushambulia wala kukimbia. Pamoja na haya, alikuwa akimhimiza nyumbu wake asonge mbele kuwaendea maadui na wakati huo huo akitaja jina lake ili wale waliokuwa bado kumjua waweze kumjua, Rehema na amani za Allah ﷻ ziwe juu yake hadi siku ya malipo. Na Mtume ﷺ hakufanya hivyo isipokuwa kumtegemea Allah ﷻ na kujua kuwa Allah ﷻ Atamnusuru na kutimiza Ujumbe Aliomtuma aufikishe na kuifanya Dini Yake iwe juu ya nyingine zote. Kwa minajili hii, Allah ﷻ Alisema:

ثُمَّ أَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَى رَسُولِهِ

**“Kisha Mwenyezi Mungu Akateremsha utulivu wake juu ya Mtume Wake”.**

Maana yake: Utulizo Wake juu ya Mjumbe Wake.

وَعَلَى الْمُؤْمِنِينَ

**“...na juu ya Waumini”.** Walio pamoja naye.

وَأَنْزَلَ جُنُودًا لَمْ تَرَوْهَا

**“Na Akateremsha majeshi ambayo hamkuyaona”.**

Nao ni Malaika. Imamu Abu Ja'far bin Jariri رحمه الله تعالى alisema: Al-Qasim alitueleza, Al-Hasan bin 'Arafah aliniambia Al-Mu'tamar bin Sulayman alinisisimulia kutoka kwa 'Awfi, ambaye ni Ibn Abu Jamilah Al-A'rabi kuwa: Nilimsikia 'Abdur-Rahman, mtumwa aliyeachwa huru na Ibn Burthun akisema, “Kuna mtu ambaye alikuwa pamoja na Washirikina katika vita vya Hunayn aliniambia: “Pindi tulipokabilia sisi na Masahaba wa Mtume ﷺ katika vita vya Hunayn, hawakusalia katika vita zaidi ya muda unaotumika kukama maziwa ya kondoo. Tulipowagundua, tulianza kuwafukuza, mpaka tukamfikia mtu aliyekuwa amepanda juu ya nyumbu mweupe, kumbe ni Mtume ﷺ. Tukawakuta watu weupe wenye wajihi mzuri. Wakatuambia, “Nyuso ziangamie! Rudini”. Tukakimbia, wakapanda mabegani mwetu na huo ukawa ndio mwisho wetu”.<sup>1</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 14:186.

Kauli ya Allah تعالی:

ثُمَّ يَتُوبُ اللَّهُ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٧﴾

***“Kisha baada ya hayo Mwenyezi Mungu Atawasamehe Awatakao.  
Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.***

Allah تعالی Aliwasamehe watu waliosalia katika kabila la Hawazin, ambao walisilimu na wakaenda kwa Mtume ﷺ na wakamkuta akiwa amekaribia kufika Makkah katika eneo la Jiranah. Hayo yalitokea siku ishirini baada ya vita hivyo. Mtume ﷺ akawapa khiyari baina ya kuwarudisha watu wao waliokamatwa mateka au warudishiwe mali walizopoteza? Nao wakakhitari hilo la kwanza. Walikuwa mateka elfu sita wakiwemo watoto na wanawake. Na akazigawa ngawira baina ya washindi, kisha mali zingine aliwagawia *Tulaqaa* (walioachwa huru miongoni mwa mateka kwa madhumuni ya kuzizoeshia nyoyo zao katika Uislamu) aliwapa ngamia mia moja. Maalik bin Awfi Al-Nasri ni miongoni mwa waliopewa ngamia mia, kisha Mtume ﷺ alimpa uongozi wa kuwaongoza watu wake, kama alivyokuwa mwanzo. Malik bin Awf akaimba shairi la kumsifia Mtume ﷺ kwa ukarimu na ushujaa wake.

\* \* \*

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَذَا ۖ وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ إِنْ شَاءَ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٢٨﴾ قَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّى يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَنْ يَدٍ وَهُمْ صَاغِرُونَ ﴿٢٩﴾ وَقَالَتِ الْيَهُودُ عُزَيْرُ ابْنُ اللَّهِ ۗ وَقَالَتِ النَّصَارَى الْمَسِيحُ ابْنُ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ قَوْلُهُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ ۗ يُضَاهَوْنَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ ۗ قَتَلْتَهُمُ اللَّهُ ۗ أَنَّى يُؤْفَكُونَ ﴿٣٠﴾ اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا ۗ لَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ سُبْحٰنَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٣١﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَذَا ۖ وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ إِنْ شَاءَ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٢٨﴾ قَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّى يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَنْ يَدٍ وَهُمْ صَاغِرُونَ ﴿٢٩﴾

28. "Enyi mlioamini! Hakika Washirikina ni najsi, kwa

*hivyo wasiukaribie Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka wao huu. Na ikiwa mnakhofia umasikini, basi Mwenyezi Mungu Atakutajirisheni kwa Fadhila Yake Akipenda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima".*

29. "Piganeni na wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, wala hawaharamishi alivyoharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume, wala hawashiki Dini ya Haki, miongoni mwa waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa khiari yao, hali wametii".

### **Kuzuiliwa kwa Washirikina Kuingia Msikiti Mtakatifu *Masjid Al-Haram*.**

Allah تعالى amewaamuru waja Wake Waumini ambao ni wasafi wa Dini na mwili kuwapiga marufuku Washirikina, ambao ni najsi kwa Dini yao, wawe mbali ya *Masjid Al-Haram*, na kwamba wasiukaribie baada ya kushushwa kwa Aya hii. Aya hii, iliteremka katika mwaka wa tisa. Kwa minajili hii, Mtume ﷺ alimtuma ‘Ali رضي الله عنه kuambatana na Abubakr رضي الله عنه katika mwaka huo na akamuamuru awatangazie Washirikina kwamba baada ya mwaka huo asihiji mshirikina yeyote wala asifanye *Tawafu* kuzunguka Al-Kaaba akiwa uchi.

Allah تعالى Akayafanya hayo yatimie na Akaipitisha hukumu na Kuiwezesha kufanya kazi. ‘Abdur-Razzaq aliandika kutoka kwa Jabir bin ‘abdullah ambaye aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَذَا<sup>١</sup>

***“Hakika Washirikina ni najsi, kwa hivyo wasiukaribie Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka wao huu”.***

Alisema, “Isipokuwa mtumishi au mmoja wapo katika watu wa *Dhimmah*”<sup>1</sup>. Imamu Abu Amri Al-Awza’i alisema kuwa ‘Umar bin ‘Abdul-‘Aziz رحمه الله تعالى aliandika (na kuwapelekea magavana wake) kuwa: “Wazuieni Wayahudi na Wakristo dhidi ya kuingia ndani ya Misikiti ya Waislamu”. Onyo lake hilo akalifuatishia na Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّمَا الْمُشْرِكُونَ نَجَسٌ

***“Hakika Washirikina ni najsi”.***

‘Atwaa alisema: “Eneo Takatifu Lote (*Al-Haram*) huchukuliwa (huzingatiwa) kuwa ni Msikiti.”

Ni kwa sababu ya Kauli ya Allah تعالى,

فَلَا يَقْرَبُوا الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ بَعْدَ عَامِهِمْ هَذَا<sup>١</sup>

***“...kwa hivyo wasiukaribie Msikiti Mtakatifu baada ya mwaka wao huu”.***

<sup>1</sup> Abdur-Razzaq 2:271.

Aya hii tukufu inajulisha juu ya unajisi wa Mshirikina, pia imeeleza usafi wa Muumini. Pia ni kutokana na Hadithi iliyoandikwa ndani ya Sahih kuwa;

«الْمُؤْمِنُ لَا يَنْجُسُ»

“Muumini hawi najisi”.<sup>1</sup>

Kauli ya Allah تعالى،

وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

**“Na ikiwa mnakhofia umasikini, basi Mwenyezi Mungu Atakutajirisheni kwa Fadhila Yake Akipenda”.**

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema: “Hayo ni kwa sababu watu walisema, “Masoko yetu yatafungwa, biashara zetu zitavurugika, na kipato tulichokuwa tukikipata kitapotea, ndipo ilipoteremka:

وَإِنْ خِفْتُمْ عَيْلَةً فَسَوْفَ يُغْنِيكُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

**“Na ikiwa mnakhofia umasikini, basi Mwenyezi Mungu Atakutajirisheni kwa Fadhila Yake Akipenda”.**

Atakutajirisheni kwa njia nyingine isiyokuwa hiyo,

إِنْ شَاءَ

“...akipenda”. Mpaka, Kauli Yake:

وَهُمْ صَاعِرُونَ

“...hali wametii”. Ina maana hii ndio badala ya mliyoyakhofia, ya kufungwa kwa masoko. Kwa hivyo, Allah تعالى Aliwapa fidia kwa khasara waliyoipata kwa sababu ya kuyaondosha mambo ya ushirikina kwa kukusanya kodi waliyokuwa wakipata kutoka kwa Watu wa Kitabu”<sup>2</sup>.

Hivi ndivyo pia anavyosimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas, Mujahid, ‘Ikrimah, Sa’id bin Jubayr, Qatadah, Adh-Dhahhak na wengine رضي الله عنهم<sup>3</sup>.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 3:150.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:197.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:193-194.



إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ

**“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua”.**

Mambo ya kuwanufaisha,

حَكِيمٌ

**“Mwenye Hikima”.**

Katika Anayoyaamrisha na Anayoyakataza, kwani Yeye Ndiye Mkamilifu katika Kauli na Matendo Yake, Muadilifu kwa viumbe Wake na Amri Zake. Kwa hivyo, Aliwapa badala ya khasara waliyoipata kwa kulipwa jizia kutoka kwa watu wa Dhimmah.

**Amri ya Kuwapiga Vita Watu wa Kitabu Mpaka Walipe Jizia.**

Allah تعالى Anasema,

فَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ  
وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّى يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَن يَدٍ وَهُمْ

صَغِيرُونَ ﴿٢٨﴾

**“Piganeni na wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, wala hawaharamishi Alivyoharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume, wala hawashiki Dini ya Haki, miongoni mwa waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa khiari yao, hali wametii”.**

Baada ya wao kumkanusha Muhammad ﷺ basi hawakubaki na imani sahihi kwa Mtume yeyote wala Ujumbe waliouleta, bali wanafuata rai na matamanio yao yale waliyo nayo baba zao, si kwamba ni Sharia wala Dini ya Allah تعالى. Lau kama wangelikuwa wana imani sahihi katika yale waliyonayo, basi yangeliwaongoza katika kumuamini Muhammad ﷺ, kwani Mitume wote walitoa khabari zake na wakawaamuru wafuasi wao wamfuata. Lakini alipokuja, walimkataa, ilhali, yeye ndiye mbora wa Mitume waliotangulia. Hapo ikajulikanwa kwamba wao hawafuati sharia ya Mitume waliotangulia, kwa kuwa Mtume Muhammad ﷺ naye ametumwa na Allah تعالى, bali wao walifuata ulaghai na matamanio yao. Kwa ajili hii, imani yao kwa Mitume wengine haitawafaa kitu, kwani wamemkataa mkuu wa Mitume hao na wa

mwisho wao kuletwa na mkamilifu wao zaidi. Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema,

فَقَاتِلُوا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ وَلَا يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ وَرَسُولُهُ  
وَلَا يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ

***“Piganeni na wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho, wala hawaharamishi Alivyoharamisha Mwenyezi Mungu na Mtume, wala hawashiki Dini ya Haki, miongoni mwa waliopewa Kitabu”.***

Aya hii tukufu ilishushwa ikiwa na amri ya kuwapiga Watu wa Kitabu baada ya kumalizika kupigana na Washirikina na baada ya watu wengi kuingia katika Dini ya Allah تعالى. Baada ya Ghuba ya Uarabuni kuwa katika hali ya amani, Allah تعالى Alimuamuru Mtume Wake ﷺ awapige vita Watu wa Kitabu, Mayahudi na Wakristo. Hili lilikuwa katika mwaka wa tisa, na kwa ajili hii, Mtume ﷺ alijiandaa kuwapiga Warumi na akawaita watu wajitayarisha kwa jambo hilo na akawatangazia. Mtume ﷺ alipeleka ujumbe wa nia yake, katika maeneo mbalimbali yaliyozunguka Madinah kuwa pamoja naye na limekusanyika jeshi la Wapiganaji wapatao elfu thelathini walioungana. Baadhi ya watu wa Madinah na pembezoni mwake ambao walikuwa wanafiki hawakujiunga. Hayo yalijiri katika mwaka uliokuwa na ukame na joto kali. Mtume ﷺ akatoka kuelekea Ash-Sham kwa ajili ya kuwapiga Warumi. Mpaka alipofika Tabuk, akapiga kambi hapo kwa kadiri ya siku ishirini, karibu na sehemu iliyokuwa na maji. Halafu akamuomba Allah تعالى *Istikhara* amchagulie la kufanya, na akarejea Madinah kwa sababu mwaka ulikuwa wa dhiki sana na watu walidhoofika, kama tutakavyoeleza, *In sha Allah*.

### **Ulipaji wa Jizia ni Alama ya Ukafiri na Udhalili**

Kauli ya Allah تعالى,

حَتَّىٰ يُعْطُوا الْجِزْيَةَ

***“...mpaka watoe kodi”.*** Ikiwa hawakusilimu,

عَنْ يَدٍ

***“... kwa khiari yao”.*** Kutokana na kushindwa na kutenzwa nguvu.

وَهُمْ صَافِرُونَ

*"...hali wametii".*

Kwa maana: Wamedhalilika, wamenyongeka, na wamenyanyasika. Kwa ajili hii, haijuzu kuwatukuza wala kuwanyanyua juu ya Waislamu, bali wao ni madhalili, wanyonge na wenye kushindwa. Muslim alinukuu Hadithi ya Abu Hurayrah رَضِيَ اللهُ عَنْهُ kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَبْدُؤُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى بِالسَّلَامِ، وَإِذَا لَقَيْتُمْ أَحَدَهُمْ فِي طَرِيقٍ فَاضْطَرُّوهُ إِلَى أَصْبِقِيهِ»

*"Msiwaanze kwa Salaam Mayahudi na Manasara, na mkikutana na mmoja wao njiani, basi m-baneni ili apite katika njia nyembamba zaidi"*<sup>1</sup>.

Kwa sababu hii, Amiri wa Waumini, 'Umar bin Al-Khattwab رَضِيَ اللهُ عَنْهُ aliweka masharti maarufu katika kuwafanya dhalili, wanyonge na kuwanyanyasa. Hayo ni miongoni mwa yaliyohifadhiwa na Hadithi na masimulizi yaliyotolewa na 'Abdur-Rahman bin Ghanm Al-Ash'ari kuwa alisema, "Nilimuandikia 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُ masharti ya mkataba wa amani aliowekeana na Manasara wa Ash-Sham: ulisema, Kwa Jina la Allah تَعَالَى, Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu. Huu ni waraka wa mja wa Allah تَعَالَى, 'Umar رَضِيَ اللهُ عَنْهُ, Amiri wa Waumini kwenda kwa Manasara wa mji kadha. Nyinyi mlipokuja kwetu, tulikuombeni amani kwa ajili yetu sisi, familia zetu na wafuasi wa dini yetu. Pia tulijiwekea masharti kwamba hatutasimamisha katika maeneo yetu nyumba za utawa, kanisa wala mahali patakatifu pa watawa, wala kukarabati kanisa lililoharibika, wala kulumia kanisa lolote kwa ajili ya kuwafanyia uadui Waislamu, wala kuyazuia makanisa yetu dhidi ya kufikiwa kwa mapumziko na Muislamu yeyote, si usiku wala mchana, na kwamba milango yetu itakuwa wazi kwa wapitaji na wasafiri. Muislamu mwenye kufikia kwetu kama mgeni tumfanyie ukarimu kwa muda wa siku tatu. Hatutamruhusu jasusi dhidi ya Waislamu katika makanisa na majumba yetu, wala kumficha msaliti wa Waislamu, wala hatutawafundisha watoto wetu Qur'an, wala hatutadhihirisha ushirikina na wala kumlingania yeyote kuuendea, wala hatutamzuia yeyote katika ndugu zetu kuingia katika Uislamu ikiwa atataka kufanya hivyo. Tutawaheshimu Waislamu, na

<sup>1</sup> Muslim 4:1707.

tutasimama na kuwapisha mahali tulipokaa ikiwa wao watataka wakae. Hatutajishabihisha na wao kwa namna yoyote katika mavazi yao, kama vile kofia, vilemba, viatu wala mitindo ya nywele. Hatutayazungumza maneno yao, wala kuitana kwa majina yao, wala hatutapanda vipando vyao, hatutaiga kuweka mapanga begani, wala kuchukua na kubeba silaha. Hatutapiga mihuri yetu katika lugha ya kiarabu, wala hatutafanya biashara ya pombe. Tutazikata nywele za mbele ya vichwa vyetu, tutavaa nguo za desturi yetu tutakapokuwa, tutavaa mikanda katika viuno vyetu, tutaacha kusimika misalaba juu ya makanisa yetu, wala hatutadhihirisha misalaba yetu wala vitabu vyetu katika njia za Waislamu wala masoko yao. Hatutazipiga kengele za makanisani mwetu isipokuwa sauti khafifu, wala hatutasoma kwa sauti makanisani mwetu mbele ya Waislamu, wala hatutatoka tukiwa tumewasha mienge kwa ajili ya mazishi na kupita kwa kupaza sauti katika njia wala masoko ya Waislamu. Hatutawazika maiti wetu karibu ya Waislamu, wala hatutawanunua mateka waliokamatwa Waislamu. Na tutawaelekeza Waislamu na wala hatutawaingilia faragha za majumbani mwao." Nilipompelekea Umar رضي الله عنه waraka huo, aliongeza kuandika chini yake, "Wala hatutampiga Muislamu yeyote. Masharti haya tumeyaweka kwenu dhidi yetu na wafuasi wa Dini yetu kwa ajili ya amani, kwamba ikiwa tutakhalifu jambo lolote katika masharti hayo tuliyoyaweka, basi hapana *Dhimma* (ahadi ya kutupa sisi hifadhi), *Dhimma* itakuwa imevunjika, na mtaruhusiwa kututendea mnachoruhusiwa kuwafanyia watu mafedhuli na waasi"<sup>1</sup>.

وَقَالَتِ الْيَهُودُ عُزَيْرٌ ابْنُ اللَّهِ وَقَالَتِ النَّصْرَى الْمَسِيحُ ابْنُ اللَّهِ ذَلِكَ قَوْلُهُمْ  
 بِأَفْوَاهِهِمْ يُضَاهِئُونَ قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ فَنَتْلُوهُمُ اللَّهُ أَنْ يُوَفَّقُوا  
 ﴿٣٠﴾ اتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهْبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ  
 وَمَا أُمْرًا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٣١﴾

**30. "Na Mayahudi wanasema: Uzeir ni mwana wa Mungu. Na Wakristo wanasema: Masihi ni mwana wa Mungu. Hiyo ndiyo kauli yao kwa vinywa vyao. Wanayaiga maneno ya walio kufuru kabla yao. Mwenyezi Mungu Awaangamize! Wanageuzwa namna gani hawa!"**

<sup>1</sup> Al-Barhaqi Al-Kubra 4/202 na Al-Muhalla 7:346.

**31. “Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryam. Na wala hawakuamrisha isipokuwa wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mola ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo”.**

**Shirki na Ukafiri wa Mayahudi na Wakristo ndiyo Sababu ya Kupambana nao.**

Hili ni himizo la Allah تعالی kwa Waumini juu ya kupigana na Washirikina wa Makafiri miongoni mwa Mayahudi na Wakristo ambao walitoa kauli ova ya kutisha na ya uzushi dhidi ya Allah تعالی. Ama Wayahudi wao walisema kuhusu ‘Uzayr, “Yeye ni mwana wa mungu”. Allah تعالی Yu mbali kabisa na wanayomnasibisha nayo. Ama upotevu wa Wakristo kuhusu Masihi upo wazi. Ndio maana Allah تعالی Aliyakadhibisha makundi hayo yote mawili kwa kusema,

ذَٰلِكَ قَوْلُهُمْ بِأَفْوَاهِهِمْ

**“Hiyo ndiyo kauli yao kwa vinywa vyao”.** Hawana ushahidi wa kuyathibitisha madai yao, isipokuwa huo ni uongo na uzushi wao.

يُضَاهُونَ

**“Wanayaiga”.** Wanayashabihisha maneno yao na;

قَوْلَ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَبْلُ

**“...maneno ya waliokufuru kabla yao”.** Maana: Wamepotea kama wapotovu wa umma uliopita kabla yao.

فَتَلَّهُمُ اللَّهُ

**“Mwenyezi Mungu Awaangamize!”** Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Maana ya Ayah hii ni Allah تعالی Awalaani”.

أَنِّي يُؤَفِّكُونَ

**“Wanageuzwa namna gani hawa!”**

Vipi wanapotezwa na kuwa mbali na ukweli, ilhali uko dhahiri, na kuukhitari upotevu. Kauli ya Allah تعالی,

أَتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهَيْبَتْهُمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ وَالْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ

***“Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryam”. (9:31)***

Imamu Ahmad, At-Tirmidhi na Ibn Jarir walisimulia kutokana na isnadi tofauti tofauti kutoka kwa 'Adii bin Hatim kuwa pindi zilipomfikia khabari za wito wa Mtume ﷺ alikimbilia Shamu, na alikuwa ameingia katika ukristo. Dada yake na watu wengi wa kaumu yake wakachukuliwa mateka. Mtume ﷺ alimuacha huru dada yake na akampa zawadi, akarejea kwa kaka yake na kumlingania aingie katika Uislamu na aende kwa Mtume ﷺ. 'Adi akaenda Madina na wakati huo alikuwa kiongozi wa jamii yake, kabila la Twa-ii na baba yake, Hatim At-Twa-ii alikuwa mtu maarufu kwa ukarimu. Watu wakaambizana juu ya kuwasili kwake. Akaingia kwa Mtume ﷺ huku akiwa na msalaba wa fedha shingoni mwake. Mtume ﷺ akasoma Aya ifuatayo,

أَتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرُهَيْبَتْهُمْ أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ

***“Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu”.***

Nikamuambia, “Wao hawawaabudu hao”. Akanijibu,

«بَلَىٰ إِنَّهُمْ حَرَّمُوا عَلَيْهِمُ الْحَلَالَ وَأَحَلُّوا لَهُمُ الْحَرَامَ فَاتَّبِعُوهُمْ فَذَلِكَ عِبَادَتُهُمْ  
إِيَّاهُمْ»

*“Ndiyo, wao (makuhani na watawa) waliwaharamishia vya halali na kuwahalalishia vya haramu, na wakawafuata, basi huko ndiko kuwaabudu kwao”.*

Mtume ﷺ akamuambia 'Adi,

«يَا عَدِيُّ مَا تَقُولُ؟ أَيْبُرِّكَ أَنْ يُقَالَ: اللَّهُ أَكْبَرُ؟ فَهَلْ تَعْلَمُ شَيْئًا أَكْبَرَ مِنَ اللَّهِ؟ مَا يُبْرِّكَ؟ أَيْبُرِّكَ أَنْ يُقَالَ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ؟ فَهَلْ تَعْلَمُ مَنْ إِلَهٌ إِلَّا اللَّهُ؟»

*“Ewe 'Adii! Unasemaje? kuhusu kinachokukimbiza (kwenda Sham)? Ni watu kusema Allahu Akbar? Kwa maana Allah ni Mkubwa? Hivi unajua kitu kingine kikubwa zaidi kushinda Allah?, Ni jambo gani linakukimbiza? Linalokukimbiza ni watu kusema (Hapana mola*

*mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah)? Je unamjua mola mwingine wa haki ya kuabudiwa, asiye kuwa Allah?”*

Halafu akamuita katika Uislamu, akasilimu kwa kutoa shahada ya kweli. Uso wake ukawa na bashasha. Kisha Mtume ﷺ akasema:

«إِنَّ الْيَهُودَ مَغْضُوبٌ عَلَيْهِمْ وَالنَّصَارَى ضَالُّونَ»

*“Mayahudi wameghadhikwa, na Wakristo wamepotea”.<sup>1</sup>*

Hivi ndivyo alivyosema Hudhaifah bin Al-Yaman, ‘Abdullah bin ‘Abbas na wengine رضي الله عنهم , katika kuitafsiri Aya hii,

أَتَّخَذُوا أَحْبَارَهُمْ وَرُهَبَانَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ

***“Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu”.***

Wao waliwafuata katika kila walilolihalalisha na waliloliharamisha<sup>2</sup>. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema,

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا إِلَهًا وَاحِدًا

***“Na wala hawakuamrisha isipokuwa wamuabudu Mungu Mmoja”.***

Kwa maana: Ambaye Akikiharamisha kitu basi ni haramu na Akikihalalisha kitu ni halali, Anachokifanya kuwa *Sharia* kinatakiwa kufuatwa, na Anachokihukumu ndicho cha kushikamana nacho.

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ سُبْحَانَهُ عَمَّا يُشْرِكُونَ

***“...hapana mola ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayomshirikisha nayo”.***

Maana yake: Ni Mtukufu Ametakasika na Yu mbali na washirika na Kufanana na wasaidizi, wapinzani na watoto. Hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa, isipokuwa Yeye, wala hapana mola Mlezi isipokuwa Yeye.

<sup>1</sup> Ahmad 4:378, Tufhat Al-Ahwadhi 8:492 na At-Tabari 14:210.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:212.

يُرِيدُونَ أَنْ يُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَيَأْبَى اللَّهُ إِلَا أَنْ يُتِمَّ نُورَهُ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٣٢﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾ \* يَتَأَيَّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْأَخْبَارِ وَالرَّهْبَانِ لَيَأْكُلُونَ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَطْلِ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ وَالَّذِينَ يَكْتُمُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُفْقِئُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٤﴾ يَوْمَ نَحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَتَكْوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ ۗ هَذَا مَا كَتَرْتُمْ لِأَنفُسِكُمْ فَذُوقُوا مَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٥﴾ إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللَّهِ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا فِي كِتَابِ اللَّهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرْمٌ ۗ ذَلِكََ الدِّينُ الْقَيِّمُ ۗ فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنفُسَكُمْ ۗ وَقَتِلُوا الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً كَمَا يُقْتَلُونَكُم كَافَّةً ۗ وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿٣٦﴾

يُرِيدُونَ أَنْ يُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَيَأْبَى اللَّهُ إِلَا أَنْ يُتِمَّ نُورَهُ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٣٢﴾ هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ ﴿٣٣﴾

32. “Wanataka kuizima Nuru ya Mwenyezi Mungu kwa vinywa vyao, na Mwenyezi Mungu Anakataa ila Aitimize Nuru Yake ijapokuwa makafiri watachukia”.

33. “Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa uongofu na Dini ya Haki ipate kushinda dini zote, ijapokuwa Washirikina watachukia”.

**Hila za Watu wa Kitabu za Kuizima Nuru ya Uislamu.**

Allah تعالی Amesema: Makafiri hao wa kishirikina na watu wa Kitabu wanajaribu,

أَنْ يُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ

“...kuizima Nuru ya Mwenyezi Mungu”. Kwa maana: Wanatumia majadiliano na uzushi ili wauzime uongofu na Dini ya kweli aliyotumwa kwayo Mtume ﷺ



kuifikisha. Mfano wao katika kufanya hivyo, ni kama anayepuliza miale ya jua au nuru ya mwezi kwa ajili ya kuizima, kitu ambacho hakiwezekani. Kadhalika yale aliyotumwa nayo Mtume ﷺ kufikisha, yatatimia na kushinda bila ya mashaka. Kwa hilo, Allah تعالى Aliwajibu kutokana na yale waliyoyakusudia na kuyataka,

وَيَأْتِي اللَّهَ إِلَّا أَنْ يُتِمَّ نُورَهُ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ

**“...na Mwenyezi Mungu Anakataa ila Aitimize Nuru Yake ijapokuwa makafiri watachukia”. (9:32)**

*Kafir* katika muktadha wa lugha ya kiarabu ni mtu anayeficha kitu na kukifunika, ndiyo maana, usiku huitwa *Kafiran* (mfuniko), kwa sababu huvistiri vitu, na mkulima huitwa *Kafirin* kwa sababu huzifunika mbegu ardhini. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika aya nyingine,

أَعْجَبَ الْكُفَّارَ بِنَاتِهِ

**“...ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake”. (57:20)**

### Dini ya Uislamu Itazishinda Dini Zingine Zote.

Kisha Allah تعالى Alisema,

هُوَ الَّذِي أَرْسَلَ رَسُولَهُ بِالْهُدَىٰ وَدِينِ الْحَقِّ

**“Yeye Ndiye Aliyemtuma Mtume Wake kwa uongofu na Dini ya Haki”.**

Uongofu, ni khabari za kweli, Imani sahihi na elimu yenye manufaa na maana ya Dini ya Haki ni amali njema, zenye manufaa duniani na Akhera.

لِيُظْهِرَهُ عَلَى الدِّينِ كُلِّهِ

**“...ipate kushinda dini zote, ijapokuwa Washirikina watachukia”.** Maana: Iwe juu ya dini zingine zote. Ni kama ilivyothibiti ndani ya Sahih kwamba Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ اللَّهَ زَوَىٰ لِي الْأَرْضَ مَشَارِقَهَا وَمَغَارِبَهَا، وَسَيَلِّغُ مَلِكُ أُمَّتِي مَا زُوِيَ لِي مِنْهَا»

**“Allah Amenikusanyia pande za Mashariki na Magharibi mwa dunia kwa hiyo Utawala wa umma wangu utafika mpaka katika sehemu zote nilizokusanyiwa”<sup>1</sup>.**

<sup>1</sup> Muslim 4:2215.

Imamu Ahmad aliandika kutoka kwa Tamim Ad-Dari رضي الله عنه kuwa alisema: Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«لَيَبْلُغَنَّ هَذَا الْأَمْرُ مَا بَلَغَ اللَّيْلُ وَالنَّهَارُ، وَلَا يَتْرُكُ اللَّهُ بَيْتَ مَدْيَنَ وَلَا وَبَرَ إِلَّا أَدْخَلَهُ هَذَا الدِّينَ، يُعَزُّ عَزِيْرًا وَيَذِلُّ ذَلِيْلًا، عِزًّا يُعِزُّ اللَّهُ بِهِ الْإِسْلَامَ وَذُلًّا يُذِلُّ اللَّهُ بِهِ الْكُفْرَ»

*“Jambo hili (Uislamu) litafika na kuenea pote panapofikiwa na usiku na mchana. Allah Hataisaza nyumba ya udongo au manyoya, bali Ataiingiza Dini hii ndani yake, na Kumpa nguvu mwenye nguvu (Muislamu) na udhalili kwa dhalili (anayeukataa Uislamu). Nguvu ambayo Allah Huupa Uislamu, na udhalili ambao Allah Huudhalilisha ukafiri”.*

Tamim Ad-Dari رضي الله عنه alikuwa akisema, “Nilikuja kujua maana ya Hadithi hii kwa watu wa nyumbani kwangu. Wale waliosilimu miongoni mwao, walipata kheri, utukufu na nguvu na waliokuwa makafiri miongoni mwao walipatwa na udhalili, kunyanyaswa na kulipa jizya”<sup>1</sup>.

• يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّ كَثِيرًا مِّنَ الْأَحْبَارِ وَالرُّهْبَانِ لِيَأْكُلُونَ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَيُصَدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ وَالَّذِينَ يَكْتُمُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿١٠٤﴾ يَوْمَ نَحْمِيْ عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فُتُكُومًا بِهَا بِنَابُهُمْ وَجُثُوبُهُمْ ۖ وَظُهُورُهُمْ ۗ هُنَا مَا كُتِبْتُمْ لَهَا نُفُسِكُمْ فَذُقُوا مَا كُنتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿١٠٥﴾

**34. “Enyi mlioamini! Hakika wengi katika makuhani na watawa wanakula mali za watu kwa baatili na wanazuilia njia ya Mwenyezi Mungu. Na wanaokusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyochungu”.**

**35. “Siku zitapotiwa katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao”. Wakaambiwa: Haya ndiyo mliojilimbikizia nafsi zenu, basi onjeni mliyokuwa mkilimbika”.**

<sup>1</sup> Ahmad 4:103.

### Onyo Dhidi ya Wanazuoni Waovu na Wafuasi wa Ibada Potofu.

As-Suddi amesema: *Al-Ahbaar* ni katika Wayahudi na *Ruhban* ni watawa wa Kikristo<sup>1</sup>. Naam ni kweli, kwani *Al-Ahbaar* ni makuhani wa Kiyahudi. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى.

لَوْلَا يَنْهَاهُمُ الرَّبَّيُّونَ وَالْأَحْبَارُ عَنْ قَوْلِهِمُ الْإِثْمَ وَأَكْلِهِمُ السُّخْتِ

***“Mbona hao wanazuoni na makohani wao hawawakatazi maneno yao ya dhambi, na ulaji wao vya haramu?” (5:63)***

*Ar-Ruhban* ni watawa wa kikristo na makasisi ni Maulamaa wao, sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى.

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَسَّيْسُوا وَزُهَّبَانَا

***“Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki”.* (5:82)**

Makusudio ya Ayah hii ni kuwaonya wanazuoni waovu na wafanyaji ibada za upotofu. Ni kama alivyosema Sufyan bin ‘Uyaynah, mafisadi katika Maulamaa wetu watakuwa kama Mayahudi na mafisadi na katika wafanya ibada wetu watakuwa kama Wakristo. Pia katika Hadithi *Sahihi*, amesema:

«لَتَرْكَبُنَّ سُنَنَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ حَذَرَ الْقُدَّةِ بِالْقُدَّةِ»

*“Mtafuata nyenendo za waliokuwa kabla yenu, hatua kwa hatua”.*

Wakauliza, “Tutawafuata, Wayahudi na Wakristo?” Akawajibu,

«فَمَنْ؟»

“Ni nani wingine tena?” Katika masimulizi mengine waliuliza: “Tutawafuata, “Waajemi na Warumi?” Akawajibu,

«فَمَنِ النَّاسِ إِلَّا هَؤُلَاءِ؟»<sup>2</sup>

*“Kwani kuna watu wengine tena, kama si hawa?”<sup>2</sup>*

Linalokusudiwa hapa ni onyo dhidi ya kuwaiga wao katika kauli zao na hali zao. Kwa sababu hii, Allah تعالى Alisema:

<sup>1</sup> At-Tabari 14:216.

<sup>2</sup> Ash-Sharia uk. 18.

لَيَأْكُلُونَ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ

**“...wanakula mali za watu kwa baatili na wanazuilia njia ya Mwenyezi Mungu”.**

Wanaiuza dini yao kwa dunia, wanatumia vyeo na ukubwa wao kwa kula mali za watu kwa njia hiyo. Ni sawa na Makuhani wa Kiyahudi walivyokuwa wakiheshimiwa na majahili, wakawa wanapokea kutoka kwao Hidaya, kodi na zawadi wanazowaletea. Baada ya Allah تعالی Kumtuma Mjumbe Wake waliendelea na upotovu, kufuru na ufidhuli wao, kwa matumaini ya kuendeleza hadhi zao. Allah تعالی Akayazima yote hayo kwa nuru ya Utume na Akawapelekea udhalili na unyonge na wakapatwa na ghadhabu ya Allah تعالی. Kauli ya Allah تعالی,

وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ

**“...na wanazuilia njia ya Mwenyezi Mungu”.** Maana yake, licha ya ulaji wao vitu vya haramu, walikuwa wakiwazuia watu dhidi ya kuitafuta haki na kuichanganya haki na batili huku wakijionesha kwa wafuasi wao majahili kwamba wao wanalingania katika kheri, ilhali hawakuwa sawa na madai yao, bali wao ni wenye kulingania Moto na hawatanusurika Siku ya Kiyama.

### **Adhabu kwa Wanaolimbikiza Dhahabu na Fedha.**

Kauli ya Allah تعالی:

وَالَّذِينَ يَكْتُمُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

**“Na wanaokusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu”. (9:34)**

Hawa ni sehemu ya tatu katika viongozi wa jamii ya watu kwani watu kwanza huwategemea wanazuoni wao; pili, wafanya ibada kisha matajiri wao. Pindi hao wanapofisidika basi, jamii nzima nayo huwa imefisidika. Ni sawa na alivyosema Ibn Al-Mubarak:

*“Hakuna walioiharibu Dini ila wafalme.*

*Wanazuoni (waovu) na watawa waovu.”*

Kuhusu *Kanz'* Abdullah bin Diynar alisema kuwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما alisema: "Ni mali ambayo haikutolewa Zaka"<sup>1</sup>. Bukhari aliandika Hadithi ya Az-Zuhri kuwa Khalid bin Aslam alisema, tulitoka pamoja na 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما na akasema: "Hii ilikuwa kabla ya kufaradhishwa Zaka, baada ya kufaradhishwa, Allah تعالى Aliijalia kuwa Zaka ndiyo yenye kuitakasa mali."<sup>2</sup> Hivi ndivyo pia alivyosema 'Umar bin 'Abdul-'Aziz na Irak bin Malik, kwa kusema kuwa Aya hii hukumu yake ilifutwa na Kauli ya Allah تعالى inayosema,

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً

***"Chukua sadaka kutoka katika mali zao".***

Kuna Hadithi nyingi katika kusifia kumiliki uchache wa dhahabu na fedha na kukemea jambo la kujilimbikizia dhahabu na fedha. Hapa tutazitaja baadhi ya Hadithi hizo. 'Abdur-Razzaq aliandika Hadithi kutoka kwa Ali رضي الله عنه juu ya Kauli ya Allah تعالى:

وَالَّذِينَ يَكْتُمُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ

***"Na wanaokusanya dhahabu na fedha".*** Kuwa Mtume ﷺ alisema,

« تَبَا لِلذَّهَبِ تَبَا لِلْفِضَّةِ »

***"Imeangamia dhahabu, imeangamia fedha".***

Alisema hayo mara tatu. Jambo hilo likawatatiza Masahaba wa Mtume ﷺ na wakajiuliza: "Mali ya namna gani tunaweza kuikusany?" 'Umar رضي الله عنه akasema: "Nitakutafutieni majibu juu ya hilo". 'Umar رضي الله عنه akamuambia Mtume ﷺ na kumuuliza: "Ewe Mjumbe wa Allah! Kauli yako imewawia Ugumu Masahaba wako. Wanauliza, "Ni mali ya namna gani tunayoweza kuikusanya?" Akamjibu:

«لِسَانًا ذَاكِرًا وَقَلْبًا شَاكِرًا وَرَوْجَةً تُعِينُ أَحَدَكُمْ عَلَى دِينِهِ»

***"Ulimi wenye kudhukuru, moyo wenye shukurani na mke anayemsaidia mmoja wenu katika Dini yake."<sup>3</sup>***

<sup>1</sup> Al-Muwatta 1:256.

<sup>2</sup> *Fat'hul Al-Bari* 8:175.

<sup>3</sup> Abdur-Razzaq 2:263. Isnadi yake ni dhaifu.

Kauli ya Allah تعالى:

يَوْمَ نَحْمِي عَلَيْهَا فِي نَارِ جَهَنَّمَ فَيُكْوَى بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ وَظُهُورُهُمْ هَذَا مَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿٣٦﴾

**“Siku zitapotiwa katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao. Wakaambiwa: Haya ndiyo mliojilimbikia nafsi zenu, basi onjeni mliyokuwa mkilimbikiza”.**

“Wataambiwa maneno haya kama njia ya kuwakaripia, kuwapinga na kuwadharau. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

ثُمَّ صُبُّوا فَوْقَ رَأْسِهِ مِنْ عَذَابِ الْحَمِيمِ ﴿٤٨﴾ ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٤٩﴾

**“Kisha mmwagieni juu ya kichwa chake adhabu ya maji yanayochemka. Onja! Ati wewe ndiye mwenye nguvu, mtukufu!”**  
(44:48-49)

Makusudio ya neno “Hadha” katika Aya; yaani, “Haya ndiyo mliyojilimbikizia nafsi zenu”, lina maana ya “Ile”. Kwa ajili hii husemwa, “Mwenye kukipenda kitu na akakitanguliza mbele zaidi kuliko kumtii Allah تعالى, basi ataadhibiwa nacho”. Watu hawa nao (matajiri) wameingia katika adhabu ya Allah تعالى kwa sababu jambo la kujilimbikizia mali hizi limekuwa ndilo wanalolipenda zaidi kuliko kutafuta radhi za Allah تعالى”. Ni kama ilivyokuwa kwa Abu Lahabi, Allah تعالى Amlaani, akifanya bidii katika kumfanyia uadui Mtume ﷺ. Halafu mkewe naye akimsaidia katika jambo hilo. Siku ya Kiyama pia atasaidiana na mumewe katika adhabu, shingoni mwake kutakuwa na kamba ya mtende iliyosokotwa, yaani ya kukusanyia kuni Motoni na kumrushia mumewe kiasi kwamba adhabu yake itakuwa kali zaidi kwa kuongozwa na mtu ambaye alikuwa akimpenda zaidi duniani. Ni sawa na mali, pindi inapokuwa ndio kitu azizi zaidi kwa wenye kuwa nayo, kwani itakuwa ndicho kitu kibaya zaidi kwao huko Akhera. Itatiwa joto kali la Moto wa Jahannamu na watachomwa katika paji zao za uso, mbavu na migongo yao.

Imamu Abu Ja'far Ibn Jariri رحمه الله تعالى aliandika kuwa Thawban رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«مَنْ تَرَكَ بَعْدَهُ كَنْزًا مِثْلَ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ شُجَاعًا أَقْرَعَ لَهُ زَيْبَتَانِ يَتَّبِعُهُ وَيَقُولُ: وَبِئْسَ مَا أَنْتَ؟ فَيَقُولُ: أَنَا كَنْزُكَ الَّذِي تَرَكْتَهُ بَعْدَكَ وَلَا يَزَالُ يَتَّبِعُهُ حَتَّى يُلْقِمَهُ يَدَهُ فَيَقْضِمَهَا ثُمَّ يَتَّبِعُهَا سَائِرَ جَسَدِهِ»

*“Mwenye kuacha kanz (hazina) baada ya kufa kwake (ambayo hakuitolea Zaka) basi siku ya kiama mali yake itafananishwa sawa na nondo dume likiwa na madoa mawili meusi juu ya uso wake, litamfuata. Ataliambia, “Ole wako” Ni nani wewe?” Joka litamjibu: “Mimi ni kanz yako uliyoiacha”. Litaendelea kumfuata mpaka mtu huyo atalipa mkono wake, nalo litaumeza na kisha mwili wake wote”.*

Hadithi imeelezwa na Yazid kutoka kwa Sa'id, na asili ya Hadithi hii ipo ndani ya Sahih Mbili kutoka kwa Abu Hurayra رضي الله عنه.

Na Katika Sahih Muslim kuna Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه<sup>1</sup> kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا مِنْ رَجُلٍ لَا يُؤَدِّي زَكَاةَ مَالِهِ إِلَّا جُعِلَ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ صَفَانِجٌ مِنْ نَارٍ، فَيَكْوَى بِهَا جَنْبَهُ وَرَجَبَتَهُ وَظَهْرَهُ فِي يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُ خَمْسِينَ أَلْفَ سَنَةٍ، حَتَّى يُلْقَى بَيْنَ الْعِبَادِ ثُمَّ يُرَى سَبِيلَهُ إِمَّا إِلَى الْجَنَّةِ وَإِمَّا إِلَى النَّارِ»

*“Hapana mtu asiyetekeleza Zakah ya mali yake, isipokuwa mali hizo zitatengenezwa kikaangio cha moto atakaangwa mbavu zake, paji la uso wake na mgongo wake. Katika siku ambayo siku moja inakadiriwa ni sawa na miaka elfu khamsini. Mpaka hukumu baina ya viumbe itakapotolewa. Halafu ataoneshwa njia yake kuwa ni ya kwenda Peponi ama Motoni”<sup>2</sup>.*

Aliitaja Hadithi hii mpaka mwisho wake. Bukhari aliandika tafsiri ya Aya hii kuwa Yazid bin Wahb alisema, “Nilipita kwa Abu Dharr رضي الله عنه huko Rabdhah, na nikamuuliza: “Nini kilichokufanya uishi katika ardhi hii?” Akajibu, “Siku moja tulikuwa Shamu, nikasoma Aya:

<sup>1</sup> At-Tabari 6:363, Ibn Hibban: 803, Ibn Khuzaymah:2255 na Al-Bukhari: 4659.

<sup>2</sup> Muslim 2:682.

وَالَّذِينَ يَكْتُمُونَ الذَّهَبَ وَالْفِضَّةَ وَلَا يُنْفِقُونَهَا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ

**“Na wanaokusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu”.**

Mu’awiya akasema, “Aya hii haituzungumzii sisi. Hii inawasema Watu wa Kitabu tu”. (Abu Dharr رضي الله عنه) Nikasema, “Bali inatuhusu sisi na wao”.<sup>1</sup>

إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللَّهِ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا فِي كِتَابِ اللَّهِ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ ۚ ذَلِكَ الَّذِينَ أَلْقَيْمُ ۚ فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ ۚ وَقَتِلُوا الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً كَمَا يُقْتَلُونَكُمْ كَافَّةً وَعَلِمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿٣٦﴾

**36. “Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni miezi kumi na mbili katika hukumu ya Mwenyezi Mungu tangu Alipoumba Mbingu na ardhi. Katika hiyo iko minne mitakatifu. Hiyo ndiyo Dini iliyo sawa. Basi msidhulumu nafsi zenu humo. Na Piganeni na Washirikina wote kama wao wanavyopigana nanyi nyote. Na Jueni kuwa Mwenyezi Mungu Yu pamoja na Wachamungu”.**

### Mwaka Una Miezi Kumi na Miwili.

Imamu Ahmad alisimulia kutoka kwa Abubakr رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alikhutubu katika Hijjah yake, alisema:

«أَلَا إِنَّ الزَّمَانَ قَدِ اسْتَدَارَ كَهَيْئَتِهِ يَوْمَ خَلَقَ اللَّهُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، السَّنَةُ اثْنَا عَشَرَ شَهْرًا مِنْهَا أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ، ثَلَاثَةٌ مُتَوَالِيَاتٌ: ذُو الْقَعْدَةِ وَذُو الْحِجَّةِ وَالْمَحْرَمُ وَرَجَبٌ مُضَرَ الَّذِي بَيْنَ جُمَادَى وَسَعْيَانَ» ثم قال: «أَيُّ يَوْمٍ هَذَا؟» قلنا: الله ورسوله أعلم، فسكت حتى ظننا أنه سيسميه بغير اسمه قال: «أَلَيْسَ يَوْمَ النَّحْرِ؟» قلنا: بلى ثم قال: «أَيُّ شَهْرٍ هَذَا؟» قلنا: الله ورسوله أعلم، فسكت حتى ظننا أنه سيسميه بغير اسمه قال: «أَلَيْسَ ذَا الْحِجَّةِ؟» قلنا: بلى، ثم قال: «أَيُّ بَلَدٍ هَذَا؟» قلنا: الله ورسوله أعلم فسكت حتى ظننا أنه سيسميه بغير اسمه قال: «أَلَيْسَتِ الْبَلَدَةُ؟» قلنا: بلى»

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:173.



"Tanabahini hakika zama zimezunguka na kurudi kama siku ile ambayo Allah Aliziumba mbingu na ardhi. Mwaka una miezi kumi na miwili, minne kati yake ni mitukufu, kati ya hiyo Mitatu ni yenye kufuatana – Dhul Qadah – Dhul Hijjah na Muharram, na (wa nne ni) Rajab - Mudhwari ambao uko baina ya Jumaadah (Ath-Thaaniya) na Sha'baan". Kisha akasema, "Je mnajua leo ni siku gani?" Tukajibu, "Allah na Mjumbe Wake wanajua zaidi". Akanyamaza, mpaka tukadhani kuwa ataitaja kwa jina lingine. Akauliza, "Kwani si siku ya kuchinja?" Tukajibu: "Ndiyo". Akauliza tena, "Huu ni mwezi gani?" Tukajibu, "Allah na Mjumbe Wake wanajua zaidi". Akanyamaza mpaka tukadhani kuwa atautaja kwa jina lingine. Akauliza, "Kwani si Dhul-Hijjah?" Tukajibu, "Ndiyo". Akaendelea, "Huu ni mji gani?" Tukajibu, "Allah na Mjumbe Wake wanajua zaidi". Akanyamaza, mpaka tukadhani kuwa atautaja kwa jina jingine. Akasaili: "Kwani huu si mji wa (Makkah)?" Tukasema: "Ndiyo". Akasema,

«فَإِنَّ دِمَاءَكُمْ وَأَمْوَالَكُمْ - وَأَحْسِبُهُ قَالَ - وَأَعْرَاضَكُمْ عَلَيْكُمْ حَرَامٌ كَحُرْمَةِ يَوْمِكُمْ هَذَا فِي شَهْرِكُمْ هَذَا، فِي بَلَدِكُمْ هَذَا. وَسَتَلْقَوْنَ رَبَّكُمْ تَسْأَلُكُمْ عَنْ أَعْمَالِكُمْ، أَلَا لَا تَرْجِعُوا بَعْدِي ضَلَالًا يَضْرِبُ بَعْضُكُمْ رِقَابَ بَعْضٍ أَلَا هَلْ بَلَّغْتُ؟ أَلَا لِيُبَلِّغِ الشَّاهِدُ مِنْكُمْ الْغَائِبَ فَلَعَلَّ مَنْ يُلْفَهُ يَكُونُ أَوْعَى لَهُ مِنْ بَعْضٍ مَنْ سَمِعَهُ»

"Kwa hakika! Damu, mali na heshima yenu ni vitu vitukufu, juu yenu kama utukufu wa siku yenu hii, katika mwezi wenu huu na katika mji wenu huu. Na mtakutana na Mola wenu na Kukuhojini kuhusu amali zenu. Angalieni! Msirejee katika upotevu baada yangu kwa baadhi yenu kuzipiga (kuzikata) shingo za baadhi yenu. Nimefikisha ujumbe? Tanabahini! Waliopo wawafikishie (haya) wale ambao hawapo kwani huenda wasiokuwepo wakaelewa vyema zaidi kuliko baadhi ya waliosikia wenyewe (moja kwa moja)".<sup>1</sup>

Bukhari na Muslim waliikusanya Hadithi hii.<sup>2</sup>

<sup>1</sup> Ahmad 5:37.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 8:175, 6:338 na 10;10, Muslim3:1305.

Sheikh Ilimud -Din As-Sakhawi رحمه الله تعالى aliandika katika kitabu kidogo alichokiita “*Al-Mash-hur Fiy Ayyam Wash-Shuhur*” kwamba mwezi wa Muharram uliitwa jina hilo kwa sababu ni mwezi mtukufu (*Muharram*). Kwangu mimi, mwezi huo uliitwa jina hilo kwa ajili ya kusesitiza utukufu wake. Hii ni kwa sababu, Waarabu walikuwa wanabadilisha kwa kuacha kuutukuza mwaka huu na kuutukuza mwaka mwingine. Mwandishi akasema kuwa wingi wa neno hilo ni *Muharamaat*, *Mahaarim* na *Mahaariym*. Mwezi *Swafar* umepewa jina hilo kwa sababu ya kuziacha nyumba zao katika mwezi huo kwa kwenda vitani na safarini. Husemwa “*Swafiral-Makaan*” Maana yake mahali pameachwa peke yake. Wingi wake ni *Aswfaarun*, kama vile *Jamal* na *Ajmaal*. Jina la mwezi wa *Rabiul-Awwal* umeitwa hivyo kwa sababu ya kufanya kwao ukazi *Irtibaa’* ndani yake, maana yake ni kukaa katika kipindi cha Kipupwe. Wingi wake ni *Irbi’a-a* kama vile *Nasib* na *Answiba-a* na *Arbi’ah* kama *Raghif* na *Ar-Ghifah*. Mwezi wa *Rabi’ul-Akhar* ni kama ulivyo *Rabi’ul-Awwal*. Mwezi wa *Jumaada* umeitwa hivyo kutokana na kukauka maji.

Inasemekana kuwa miezi waliyokuwa wakiihesabu ilikuwa haizunguki – kauli hii ina walakini kwani miezi yao ilikuwa ikitegemea miandamo, hivyo haikuwa na budi kuwa inazunguka. Huenda hilo ni jina la kwanza waliloliita wakati wa kukauka maji katika majira ya baridi. Ni sawa na alivyosema mshairi, “*Na usiku kutokana na kukauka kwa vyenye unyenyekevu, ndani ya kiza chake, mtu haoni At-Tunubaa, hakuna mbwa abwekaye humo, isipokuwa mara moja, hadi ajjiviringishe mkia wake juu ya pua yake*”.

Wingi wa neno hilo *Jumaadayat*, sawa na *Hubaaraa* na *Hubaaraat*. Hutumia kiwakilishi cha kiume na cha kike, na kuitwa *Jumadal-Ulaa* au *Jumadal-Awwal*, pia *Jumadal-Aakhir* au *Jumadal-Aakhirah*. Mwezi *Rajab* Unatokana na neno *tarjib*, maana yake kutukuza. Wingi wa neno hilo ni *Arjaab*, *Rijaab* na *Rajabaat*.

Mwezi *Sha’baan* umeitwa hivyo ni kwa sababu ya kutawanyika na kutengana kwa makabila kwa ajili ya kwenda kwenye mashambulizi. Wingi wake ni *Sha’aabiyn* na *Sha’baanaat*. Mwezi wa Ramadhani ni kutokana na kuzidi kwa *Ramdhwa-a*, maana yake joto. Husemwa katika kuachisha ziwa *Ramadhwat Alfiswaal* kunapokuwa na taabu ya kiu. Wingi wake ni *Ramadhwaat*, *Ramaadhwiin* na *Armidthwah*. Mwandishi amesema: Na kauli isemayo kuwa hilo ni mojawapo ya majina ya Allah, ni kosa, kwani hakuna ushahidi wala kinachounga mkono kauli hiyo. Mimi, Ibn Kathir nasema: Kuna Hadithi

iliyosimuliwa juu ya hilo lakini ni dhaifu, na nimeielezea mwanzoni mwa Kitabu cha Saumu.

Maana ya mwezi *Shawwal* ni kutokana na neno *Shaalat*, maana yake kunyanyua au kuinua, kama vile ngamia kuinua mikia yao kutokana na kusikia mlio wa vitu vilivyogongana. Wingi wake ni *Shawaawil*, *Shawaawiyl* na *Shawwaalaat*. Nao *Al-Qa'dah* au *Al-Qi'dah* ni kutokana na kukaa (*Qu'ud*) kwao ndani ya mwezi huo bila ya kupigana wala kusafiri. Wingi wake ni *Dhawaatul Qadah*. Mwezi wa *Al-Hijjah* au *Al-Hajjah* uliitwa jina hilo kwa sababu walikuwa wakifanya Hijja ndani ya mwezi huo. Wingi wake ni *Dhawaatul Hijjah*.

Majina ya siku za wiki: Kwanza ni *Al-Ahad* (Jumapili) na wingi wake ni *Aaahaad*, *Uwhaad* na *Wahuud*. Kisha siku ya *Ithnayn* (Jumatatu) na wingi wake ni *Athaaniyn*. Halafu *Thulathaa* (Jumanne), inayowakilishwa na dhamiri ya kiume au ya kike. Wingi wake ni *Thulaathaawaat* na *Athaalith*. Kisha *Arbi'a-a* (Jumatano) na wingi wake ni *Arbi'aawaat* na *Araabiy'*. Inafuata siku ya Alkhamisi, na wingi wake ni *Akhmisah* na *Akhaamis*. Kisha *Al-Jumu'ah* au *Al-Jum'ah* au *Al-Juma-'ah*. Wingi wake ni *Juma'* au *Juma'aat*. Siku ya *As-Sabt* (Jumamosi) imetokana na neno *Sabt* lenye maana ya kutaka kitu, nako ni kukoma kwa hesabu.

Waarabu siku walikuwa wakiziita kwa majina kwa mfuatano huu: *Awwal*, *Ahwan*, *Jubaar*, *Dubaar*, *Mu-unis*, *Al-'Aruwbah* na *Shiyaar*. Mshairi akasema, "Nataraji kuwa nitaendelea kuwa hai na kwamba siku yangu hii ni *Awwal*. Au *Ahwan*, au *Jubar*. Au inayofuata, *Dubaar*, na iwapo sitazipata, basi ipo siku ya *Mu-unis* au *'Arubah* au *Shiyaar*".

## Miezi Mitukufu

Kauli ya Allah تعالى:

مِنَهَا أَرْبَعَةٌ حُرُمٌ

**"Iko minne mitakatifu".**

Hii ni miezi iliyotukuzwa vilevile na Waarabu wengi katika enzi za ujahili, isipokuwa kikundi kimoja katika wao kilichokuwa kikiitwa *Al-Basl*, chenye msimamo mkali, kilitukuza kwa mwaka miezi minane badala ya minne. Ama Mtume ﷺ kusema kwake:

ثَلَاثَةٌ مُتَوَالِيَاتٌ: ذُو الْقَعْدَةِ وَذُو الْحِجَّةِ وَالْمُحَرَّمِ وَرَجَبٌ مُضَرَ الَّذِي بَيْنَ جُمَادَى  
وَشَعْبَانَ،

*“Mitatu ni yenye kufuatana – Dhul Qa’dah, Dhul-Hijjah na Muharram na (wa nne ni) Rajab wa (kabila la) Mudhwar ambao uko baina ya Jumaadah (Ath-Thaaniyah) na Sha’baan”.*

Mtume ﷺ aliunasibisha mwezi wa *Rajab* kwa *Mudhwar* kwa ajili ya kubainisha usahihi kwa kauli yao kuwa ni mwezi ulio baina ya Jumada na *Sha’baan*, si kama ilivyokuwa dhana ya kabila la *Rabi’ah* kuwa mwezi mtukufu wa *Rajab* uko baina ya *Sha’baan* na *Shawwal*, ambao ni *Ramadhan* kama tunavyouita siku hizi. Mtume ﷺ alifafanua kwamba huo ni mwezi *Rajab* kwa mujibu wa *Mudhwar* na si *Rabi’ah*. Miezi mitukufu kwa hakika ni minne, mitatu yenye kufuatana, na mmoja uko peke yake, ili kuwe na wepesi wa kutekeleza ibada za Hijja na ‘Umrah. Kwa hivyo, mwezi mmoja kabla ya ibada za Hijjah umefanywa mtukufu, nao ni *Dhul Qa’dah*, kwa sababu walikaa na kujiepusha dhidi ya vita. Na ukatukuzwa mwezi wa *Dhul Hijjah* kwa sababu wakati huo wanashughulika na ibada ya Hijjah. Baada yake ukatukuzwa mwezi mwingine, *Muharram*, ili wautumie muda huo kurejea salama katika miji yao ya mbali. Kati kati ya mwaka, mwezi *Rajab*, ukatukuzwa kwa ajili ya kuwapa fursa wanaotoka mbali na rasi ya Uarabuni waweze kuizuru Nyumba na kufanya ‘Umrah, kisha warejee kwa amani katika nchi zao.

Kauli ya Allah تعالى:

ذَٰلِكَ الدِّينُ الْقَيِّمُ ؕ

***“Hiyo ndiyo Dini iliyo sawa”.***

Kwa maana: Hii ndio Shariah iliyonyooka, katika kutekeleza Amri ya Allah تعالى kuhusu miezi Aliyoifanya kuwa mitukufu na hesabu yake sahihi kama ilivyoandikwa tangu hapo awali na Allah تعالى. Allah تعالى Amesema:

فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ ؕ

***“Basi msidhulumu nafsi zenu humo”.***

Kwa maana: Msjidhulumu kwa kufanya madhambi katika Miezi hii Mitukufu, kwani kufanya dhambi ndani yake ni jambo baya zaidi kuliko katika miezi mingine, kama ilivyo dhambi katika Mji Mtakatifu huongezwa mara dufu yake.

Na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine,

وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍ بِظُلْمٍ نُذِقْهُ مِنْ عَذَابٍ أَلِيمٍ

**“Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhulma, basi Tutamuonjesha adhabu chungu.” (22:25)**

Kadhhalika Mwezi Mtukufu, madhambi ndani yake huwa mazito zaidi. Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alitoa rai juu ya Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ عِدَّةَ الشُّهُورِ عِنْدَ اللَّهِ

**“Hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu.”**

Hadi mwisho wa Aya,

فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ

**“Basi msidhulumu nafsi zenu humo.”**

Katika miezi yote hiyo, kisha ikatolewa katika miezi hiyo kumi na mbili, miezi minne ikafanywa kuwa mitukufu, na utukufu wake ukaadhimishwa. Na kutenda dhambi katika miezi minne hiyo ni kosa kubwa sana, kama vile ambavyo kufanya amali bora katika miezi hiyo kuna thawabu na malipo makubwa.<sup>1</sup>

فَلَا تَظْلِمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ

**“Basi msidhulumu nafsi zenu humo.”**

Alisema kuwa, “Hakika dhuluma katika Miezi Mitukufu ni kosa na mzigo mkubwa sana kuliko ndani ya miezi isiyokuwa hiyo. Japokuwa katika hali yoyote, dhuluma ni kosa kubwa, lakini Allah تعالى Hulikuza zaidi Alitakalo”. Akasema tena Qatadah: “Allah تعالى Aliteua kwa baadhi ya viumbe wake kuwa juu ya viumbe wengine. Aliwateua Wajumbe katika Malaika, na katika watu. Na katika maneno, Aliteua dhikri Yake, na katika ardhi Alichagua ardhi za Misikiti. Katika siku Aliteua Ijumaa na katika nyakati za usiku Aliteua *Laylatul Qadr*, yaani, Usiku wa Cheo. Kwa hivyo, tukuzeni Alichokitukuza Allah تعالى, kwani kufanya hivyo, ni katika Desturi za wenye ufahamu na utambuzi”.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:23

**Kupigana Katika Miezi Mitukufu.**

Kauli ya Allah تعالى:

وَقَتِلُوا الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً

**“Na Piganeni na Washirikina wote.”** Maana yake: Wao wote.

كَمَا يُقْتَلُونَكُمْ كَافَّةً

**“...kama wao wanavyopigana nanyi nyote”.** Maana yake: Nyinyi.

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ

**“Na Jueni kuwa Mwenyezi Mungu Yu pamoja na Wachamungu.”**

Jueni kuwa ni haramu kuanzisha mapigano ndani ya Mwezi Mtukufu. Ni kwa sababu ya Kauli ya Allah تعالى,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَحِلُّوا شَعْنِ اللَّهِ وَلَا الشَّهْرَ الْحَرَامَ

**“Enyi mlioamini! Msivunje heshima ya alama ya Dini ya Mwenyezi Mungu wala mwezi Mtakatifu”.** (5:2) Na Kauli Yake تعالى,

الشَّهْرَ الْحَرَامَ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ وَالْحُرُمَتِ قِصَاصٌ ؕ فَمَنِ اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ فَاعْتَدُوا عَلَيْهِ بِمِثْلِ  
مَا اعْتَدَىٰ عَلَيْكُمْ ؕ

**“Mwezi Mtakatifu kwa mwezi Mtakatifu. Na vitu vitakatifu vimewekewa kisasi. Anayekushambulieni nanyi mshambulieni, kwa kadiri alivyokushambulieni.”** (2:194) Na Kauli Yake تعالى;

فَإِذَا أَنسَلَخَ الْأَشْهُرَ الْحُرُمَ فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ

**“Na ikiisha miezi mitukufu basi Wauweni Washirikina.”** (9:5)

Allah تعالى Amesema;

وَقَتِلُوا الْمُشْرِكِينَ كَافَّةً كَمَا يُقْتَلُونَكُمْ كَافَّةً

**“Na Piganeni na Washirikina wote kama wao wanavyo pigana nanyi nyote.”**

Hii ni idhini kwa Waumini kuwapiga Washirikina ndani ya Miezi Mitukufu ikiwa wao wataanzisha vita. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

الشَّهْرُ الْحَرَامُ بِالشَّهْرِ الْحَرَامِ وَالْحُرُمَتُ قِصَاصٌ<sup>ع</sup>

**“Mwezi Mtakatifu kwa mwezi Mtakatifu. Na vitu vitakatifu vimewekewa kisasi”. (2:194)**

Na Allah تعالى،

وَلَا تُقَاتِلُوهُمْ عِنْدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ حَتَّىٰ يُقَاتِلُوكُمْ فِيهِ<sup>ط</sup> فَإِن قَاتَلُوكُمْ فَاقْتُلُوهُمْ<sup>ط</sup>

**“Wala msipigane nao kwenye Msikiti Mtakatifu mpaka wakupigeni huko. Wakikupigeni huko basi nanyi pia wapigeni”. (2:91)**

Kuhusu Mtume ﷺ kuwazingira watu wa Twaif na kuwazuilia huko mpaka ukaingia Mwezi Mtakatifu ilikuwa ni muendelezo wa vita dhidi ya Hawaazin na washirika wao, Thaqiyf, wao ndio walioanzisha mapigano, wakawakusanya wapiganaji na kutangaza vita na mashambulizi. Mtume ﷺ akawaenda katika ngome huko Twaif, akawazingira ili waondoke katika ngome yao, lakini wakawashambulia Waislamu na kuwaua wengi. Kuwazingira kukaendelea kwa siku arubaini, ambazo zilianza katika mwezi ulioruhusiwa (kupigana) na kuingia katika Mwezi Mtukufu na kuendelea kwa siku kadhaa. Mtume ﷺ akawaachilia na kuondoka. Hayo ni mapigano yalipelekea kuingia ndani ya Mwezi Mtukufu na si yanayoanzia ndani yake. Hili ni jambo lenye kukubalika, na kuna mifano mingi iliyotokea ya aina hiyo. *Allah Aalam.*

\* \* \*

إِنَّمَا النَّسِيءُ زِيَادَةٌ فِي الْكُفْرِ يُضَلُّ بِهِ الَّذِينَ كَفَرُوا  
 يُحِلُّونَهُ عَامًا وَيُحَرِّمُونَهُ عَامًا لِيُوَاطِّعُوا عِدَّةَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ  
 فَيُحِلُّوا مَا حَرَّمَ اللَّهُ زَيْنَ لَّهُمْ سُوءَ أَعْمَلِهِمْ<sup>ط</sup> وَاللَّهُ لَا  
 يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٧﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا  
 مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ أَنْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَنَاقَلْتُمْ إِلَى  
 الْأَرْضِ<sup>ع</sup> أَرْضَيْتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ<sup>ع</sup> فَمَا  
 مَتَّعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٣٨﴾ إِلَّا تَنْفِرُوا  
 يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَيَسْتَبْدِلَ قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا  
 تَنْصُرُوهُ شَيْئًا<sup>ط</sup> وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٩﴾ إِلَّا  
 تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ  
 اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ  
 إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا<sup>ط</sup> فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ  
 لَّمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى<sup>ط</sup>  
 وَكَلِمَةَ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا<sup>ط</sup> وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾

إِنَّمَا النَّسِيءُ زِيَادَةٌ فِي الْكُفْرِ<sup>ط</sup>  
 يُضَلُّ بِهِ الَّذِينَ كَفَرُوا يُحِلُّونَهُ  
 عَامًا وَيُحَرِّمُونَهُ عَامًا لِيُوَاطِّعُوا عِدَّةَ  
 مَا حَرَّمَ اللَّهُ فَيُحِلُّوا مَا حَرَّمَ اللَّهُ<sup>ع</sup>  
 زَيْنَ لَّهُمْ سُوءَ أَعْمَلِهِمْ<sup>ط</sup> وَاللَّهُ لَا  
 يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ ﴿٣٧﴾

37. "Bila ya shaka kua-  
 khirisha (miezi) ni kuzidi  
 katika kukufuru; kwa hayo  
 hupotezwa waliokufuru.  
 Wanauhalalisha mwaka  
 mmoja na kuharamisha  
 mwaka mwingine, ili  
 wafanye kuwa sawa idadi  
 ya ile (miezi) Aliyoitukuza  
 Mwenyezi Mungu. Wame-  
 pambiwa ubaya wa  
 vitendo vyao hivi. Na  
 Mwenyezi Mungu Hawa-  
 ongoi watu makafiri".

### Makemeo Dhidi ya Kutumia Rai katika Sheria.

Hili ni mojawapo katika yale ambayo Allah تعالى Amewakemea Washirikina kwa kutanguliza mbele rai zao za kifisadi katika mambo ya kisharia (dini) na kubadilisha kwao hukumu za Allah تعالى kwa utashi wao usio na mwongozo. Pia kuhalalisha kwao haramu na kuharamisha yaliyohalalishwa. Wao walikuwa wamejaa ghadhabu kali, kero na pupa kwa kuona muda wa miezi mitatu mitukufu ni mrefu sana uliowazuia kupigana vita. Hii ndio iliyowapelekea kabla



ya Uislamu wakawa wanabadili muda wa kuanza kwa mwezi *Muharram* na kuuakhirisha mpaka mwezi wa *Swafar*. Wakawa Wanahalalisha mapigano ndani ya Mwezi Mtukufu, na wakawa wanautukuza mwezi usio na haki hiyo ili wautimize muda Aliouweka Allah تعالى, kwa maana miezi minne mitukufu. 'Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alitoa rai kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا أَلْسِيءُ زِيَادَةً فِي الْكُفْرِ<sup>ط</sup>

***“Bila ya shaka kuakhirisha (miezi) ni kuzidi katika kukufuru”.***

Akasema: “Junadah bin 'Awf bin Ummay Al-Kinaani alikuwa akishiriki Hijjah katika kila mwaka, na alikuwa akijulikana kwa jina la Abu Thumaamah, na hunadi, “Jueni kuwa Abu Thumaamah akitangaza jambo hakataliwi wala hatiwi ila”. Na akawa anaufanya mwezi *Swafar* katika mwaka mmoja ni wa kawaida (na kuutukuza *Muharram*), kisha anautukuza katika mwaka mwingine (na kutoutukuza *Muharram* katika mwaka huo). Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Alisema,

إِنَّمَا أَلْسِيءُ زِيَادَةً فِي الْكُفْرِ<sup>ط</sup>

***“Bila ya shaka kuakhirisha (miezi) ni kuzidi katika kukufuru”.***

Allah تعالى Anasema, “Wanauacha *Muharram* kwa mwaka mmoja na kuutukuza katika mwaka mwingine”<sup>1</sup>.

Al-'Awfi alisimulia kauli sawa na ya 'Abbas رضي الله عنه<sup>2</sup>. Layth bin Sulaym alisema kuwa Mujahid alisema, “Kulikuwa na mtu mmoja kutoka kwa Banu Kinana ambaye alikuwa akija kila mwaka wakati wa Hijja, akiwa amempanda Punda wake na kusema, “Enyi watu! Mimi huwa sitiwi kasoro wala kuhojiwa wala kukataliwa kwa lile nilisemalo. Tumeufanya mwezi (ujao wa) *Muharram* kuwa Mtakatifu na sio *Swafar*”. Kisha anakuja katika mwaka unofuata na kusema kama hivyo, Halafu anasema, “Sisi tumeutukuza mwezi wa *Swafar* na kuuakhirisha mwezi *Muharram*”. Hiyo ikawa ni sababu ya Kauli ya Allah تعالى:

لَيُؤَاطِفُوا عِدَّةَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ

***“...ili wafanye kuwa sawa idadi ya ile (miezi) Aliyoitukuza Mwenyezi Mungu”.***

<sup>1</sup> At-Tabari 14:245.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:246.

Maana: Ikamilike miezi minne. Allah تعالیٰ Anasema, “Wanahalalisha alichokiharamisha Allah تعالیٰ kwa kuucheleweshwa Mwezi Mtakatifu”<sup>3</sup>. Na walikuwa hawautukuzi mwezi *Muharram* kwa mwaka mmoja na badala yake wanautukuza *Swafar*. Na baada yake wanaendelea na kuhesabu mwezi *Rabi’u* na miezi mingine kwa nidhamu yake na majina yake mpaka mwisho wa mwaka. Halafu katika mwaka mwingine wanautukuza mwezi *Muharram* na kuendelea na hesabu ya miezi, *Swafar*, *Rabi’u* mpaka mwisho wa mwaka.

تَحِلُّونَهُ عَامًا وَتُحْرَمُونَهُ عَامًا لِيُؤَاطِعُوا عِدَّةَ مَا حَرَّمَ اللَّهُ فَيَحِلُّوا مَا حَرَّمَ اللَّهُ

**“Wanauhalalisha mwaka mmoja na kuharamisha mwaka mwingine, ili wafanye kuwa sawa idadi ya ile (miezi) Aliyotukuza Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo huhalalisha alivyoviharamisha Mwenyezi Mungu.”**

Maana: katika kuitukuza miezi minne katika mwaka, isipokuwa huwa wakati mwingine wanatanguliza kuutukuza mwezi wa tatu katika miezi mitatu yenye kufuatana, ambao ni *Muharram*, na mara nyingine wanaukhairisha hadi *Swafar*. Imamu Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالیٰ suala hili amelizungumza katika Kitabu cha Sira, kwa maneno mazuri yenye kufaidisha vyema. “Mtu wa kwanza katika Waarabu ambaye aliyeahirisha miezi, ambapo hakuitukuza ile miezi iliyotukuzwa na Allah تعالیٰ na akaitukuza miezi ambayo Allah تعالیٰ Hakuifanya mitukufu ni Al-Qalammas”. Yeye jina lake ni Hudhayfah bin ‘Abd Fuqaym bin ‘Adi bin ‘Amir bin Tha’labah bin Al-Harith bin Malik, bin Kinanah bin Khuzaymah bin Mudrikah bin Ilyaas bin Mudhwar bin Nizaar bin Ma’add bin ‘Adnaan. Baada yake mwanaye aliyeitwa ‘Abbad aliendeleza, baada yake mwana wa ‘Abbad, halafu mwanaye Umayyah bin Qala’, halafu mwanaye, ‘Awf bin Umayyah, akafuatiwa na mwanaye, Abu Thumaamah Junaadah bin ‘Awf ambaye alikuwa wa mwisho katika mfuatano huo, kisha Uislamu ukaja. Waarabu walikuwa wanapomaliza Hijjah yao, wakikusanyika na kumzunguka naye husimama na kuwahutubia na kuutukuza mwezi *Rajab*, *Dhul Qa’dah* na *Dhul Hijjah*. Kisha anaacha kuutukuza mwezi *Muharram* kwa mwaka mmoja na kupabadilisha mahala pake kwa mwezi *Swafar* na kuutukuza ili kuikamilisha hesabu ya muda ambao Allah تعالیٰ Aliupanga uwe ndiyo kipindi cha Miezi Mitukufu. Kwa hivyo,

<sup>1</sup> At-Tabari 14:246.

aliyarusu yaliyokatazwa na Allah تعالى. Yaani, na kuharamisha yaliyohalalishwa na Allah تعالى<sup>1</sup>. Allah Ndie Mjuzi zaidi.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ أَنْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَنَا قُلْنَا إِلَى الْأَرْضِ  
أَرْضَيْتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ ۗ فَمَا مَتَّعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلًا  
إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبِكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَيَسْتَبْدِلَ قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّهُ شَيْئًا ۗ وَاللَّهُ  
عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٣٨﴾

**38. Enyi mlioamini! Mna nini mnapoambiwa: Nendeni katika njia ya Mwenyezi Mungu, mnajitia uzito katika ardhi? Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache.**

**39. Kama hamuendi Atakuadhibuni adhabu chungu, na Atawaletea watu wengine, wala nyinyi hamtamdhuru chochote. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila jambo.**

**Lawama na Onyo kwa Wanaojitia Uzito kwenda kwenye Jihad.**

Hili ni onyo kali kwa wale ambao hawakujiunga na Mtume ﷺ katika vita vya Tabuk wakati wa msimu wa matunda kuiva, kukawa na vivuli katika msimu wa joto na kiu kikali. Allah تعالى Alisema:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا مَا لَكُمْ إِذَا قِيلَ لَكُمْ أَنْفِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ

**“Enyi mlio amini! Mna nini mnapo ambiwa: Nendeni katika njia ya Mwenyezi Mungu”.**

Maana: mnapoitwa katika Jihadi katika njia ya Allah تعالى.

أَنَا قُلْنَا إِلَى الْأَرْضِ ۗ

**“...mnajitia uzito katika ardhi?”**

Maana yake: Mmejitia uvivu na mmeamua kubaki, mmekaa katika vivuli na katika matunda yaliyoiva vizuri.

<sup>1</sup> Ibn Hisham 1:45.

أَرْضَيْتُمْ بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ<sup>١</sup>

**“ Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera?”**

Kwanini mmefanya hivyo? Ni kwa kuridhia kwenu dunia badala ya Akhera. Kisha, Allah تعالى Anayaondoa thamani maisha ya duniani na kuhamasisha Akhera kwa Kusema:

فَمَا مَتَعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ

**“ Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache”.**

Ni sawa na alivyonukuu Imamu Ahmad kutoka kwa Al-Mustawrid رضي الله عنه, ndugu wa Banu Fihri, alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا كَمَا يَجْمَلُ أَحَدُكُمْ إِصْبَعَهُ هَذِهِ فِي النَّيْمِ، فَلْيَنْظُرْ بِمَ تَرْجِعُ؟»

*“Dunia si chochote ikilinganishwa na Akhera, bali ni kama mmoja wenu anavyokitumbukiza kidole chake baharini, hebu angalieni kitarejea na nini?”*

Mtume ﷺ alionesha kwa kidole chake cha shahada<sup>1</sup>.

Muslim peke yake alinukuu Hadithi hii<sup>2</sup>. Ath-Thawri alisema kuwa Al-A'mash alitoa rai kuhusu Aya ifuatayo,

فَمَا مَتَعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ

**“Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha na ya Akhera ni chache”.**

Kwamba, “Ni kama masurufu ayachukuayo msafiri”. Naye ‘Abdul-Aziz bin Abu Hazim alisema kuwa baba yake alimuambia: “Wakati mauti yalipomkaribia ‘Abdul-Aziz bin Marwaan, alisema: “Nileteeni sanda yangu nitakayofungiwa, ili niitazame”. Ilipoletwa mbele yake, aliitazama, na akasema; “Ama mimi,

<sup>1</sup> Ahmad 4:228.

<sup>2</sup> Muslim 4:2193.

sina cha kuiagia dunia, isipokuwa hiki". Akageuza mgongo wake huku akilia na kusema; "Ole wako, ewe maisha! Wingi wako ndiyo uchache na uchache wako hudumu kwa muda mfupi, na hakuna tulichokipata kwako isipokuwa udanganyifu". Kisha Allah تعالی Aliwaonya wenye kuiacha Jihadi kwa Kusema,

إِلَّا تَنْفِرُوا يُعَذِّبْكُمْ عَذَابًا أَلِيمًا

***"Kama hamuendi Atakuadhibuni adhabu chungu".***

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, Mtume ﷺ aliwataka baadhi ya Waarabu atoke nao, wao wakafanya uzito wa kujiunga naye, basi, Allah تعالی Alizuia mvua dhidi yao, na hiyo ilikuwa ndiyo adhabu yao waliopewa"<sup>1</sup>.

وَسَتَّيْبِلْنَ قَوْمًا غَيْرَكُمْ

***"...na Atawaleta watu wengine badala yenu".***

Atawaleta kwa ajili ya kumnusuru Mtume ﷺ na kuisimamisha Dini Yake.

Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

وَإِن تَوَلَّوْا يَسْتَبَدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَلَكُمْ ﴿٣٨﴾

***"Na mkigeuka Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi." (47:38)***

وَلَا تَضُرُّهُ شَيْئًا

***"...wala nyinyi hamtamdhuru chochote".***

Kwa kutoshiriki kwenu katika Jihadi, kujiepusha na kujitia kwenu uzito dhidi ya Jihadi.

وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

***"Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila jambo".***

Maana yake, ni Muweza wa Kuwashinda maadui, bila ya nyinyi kuwepo.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:255.

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ ۗ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ

حَكِيمٌ ﴿٤٠﴾

**40. "Ikiwa nyinyi hamtamnusuru Mtume, basi Mwenyezi Mungu Alikwishamnusuru walipokufuru, naye ni wa pili katika wawili walipokuwa katika pango, naye akamuambia sahibu yake: Usihuzunike. Hakika Mwenyezi Mungu Yu pamoja nasi. Mwenyezi Mungu Akamteremshia Utulivu Wake, na Akamuunga Mkono kwa majeshi msiyoyaona, na Akalifanya neno la waliokufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Nguvu Mwenye Hikima."**

Allah تعالى ni Mwenye Kumnusuru Nabii Wake ﷺ

Allah تعالى Anasema,

إِلَّا تَنْصُرُوهُ

**"Ikiwa nyinyi hamtamnusuru".**

Maana yake: Kumnusuru Mjumbe Wake, kwani Allah تعالى Ndiye wa Kumnusuru, Kumsaidia, Kumtosha na Kumhifadhi, kama Alivyofanya.

إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ

**"...walipomtoa waliokufuru, naye ni wa pili katika wawili."**

Maana: Katika mwaka wa *Hijra*, wakati Washirikina walipopanga kumuua, au kumfunga au kumfukuza. Akawatoroka huku akiwa na rafiki na Sahaba wake, Abubakr bin Abu Quhafah رضي الله عنه. Wakakaa siku tatu katika pango la *Thawr* kiasi kuwafanya Washirikina waliotumwa kumfuatilia warejee (Makkah), na wao waendeleo kwenda Madinah. Abubakr رضي الله عنه akawa anakhofia washirikina, kumdhuru Mtume ﷺ. Mtume akawa anamtuliza na kumfariji kwa kusema:

«يَا أَبَا بَكْرٍ، مَا ظَنُّكَ بِإِثْنَيْنِ اللَّهُ تَالِيَهُمَا»

“Ewe Abubakr! Unadhani nini kuhusu wawili, Allah ni wa tatu wao?”<sup>1</sup>

Ni kama alivyoandika Imam Ahmad kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Abubakr رضي الله عنه alimsimulia, “Nilimuambia Mtume ﷺ huku sote tukiwa Pangoni, “Lau kama mmoja wao angelitizama uelekeo wa nyayo miguuni kwake, angelituona chini ya hiyo miguu”. Mtume ﷺ akasema:

«يَا أَبَا بَكْرٍ، مَا ظَنُّكَ بِإِثْنَيْنِ اللَّهُ تَالِيَهُمَا»

“Ewe Abubakr! Unadhani nini kuhusu wawili, Allah ni wa tatu wao?”<sup>2</sup>

Haya yamenukuliwa ndani ya *Sahih Mbili*.<sup>3</sup>

Kwa sababu hii, Allah تعالى Alisema:

فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ

**“Mwenyezi Mungu Akamteremshia Utulivu Wake.”**

Maana: Aliteremsha msaada Wake na ushindi kwa Mjumbe Wake. Ilisemwa pia kwamba inamhusu Abubakr رضي الله عنه. Kisha Allah تعالى Akasema:

وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَّمْ تَرَوْهَا

**“...na Akamuunga mkono kwa majeshi msiyoyaona.”** Nayo ni ya Malaika,

وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَىٰ ۗ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا ۗ

**“...na Akalifanya neno la waliokufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu.”**

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما amesema: Maana ya “Neno la waliokufuru ni ushirikina, na Neno la Allah تعالى ni *Laa ilaaha illallah*, maana, Hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى”<sup>4</sup>. Ndani ya *Sahih Mbili* kuna Hadithi

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:176.

<sup>2</sup> Ahmad 1:4.

<sup>3</sup> Fat’hul Al-Bari 7:11 na Muslim 1854.

<sup>4</sup> At-Tabari 261.

ya Abu Musa Al-Ash'ari رضى الله عنه kuwa alisema, Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu mtu anayepigana kwa sababu ya ushujaa wake na mwingine anapigana kwa ghadhabu na wa tatu kwa riya, katika hao watatu, ni nani aliye katika njia ya Allah?" Akajibu,

«مَنْ قَاتَلَ لِتَكُونَ كَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا فَهُوَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

*"Mwenye kupigana ili Neno la Allah liwe juu, basi atakuwa yuko katika njia ya Allah"*<sup>1</sup>.

Kauli ya Allah تعالى:

وَاللَّهُ عَزِيزٌ

***"Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Nguvu..."***

Katika kulipa kisasi na kunusuru, naye Anaogopwa na hawi katika hatari mwenye kuomba Hifadhi Yake kwa kufuata Amri Zake.

حَكِيمٌ

***"Mwenye hikima"***.

Katika Kauli Zake na Matendo Yake.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 1:268 na Muslim 4:1512.



أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾ لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيبًا وَسَفَرًا قَاصِدًا لَاتَّبَعُوكَ وَلَٰكِن بَعْدَتْ عَنْهُمْ آلُشَّقَّةِ وَسَيِّخِلُفُونَ بِاللَّهِ لَوْ اسْتَطَعْنَا لَخَرَجْنَا مَعَكُمْ يُهْلِكُونَ أَنْفُسَهُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٤٢﴾ عَاثَ اللَّهُ عَنْكَ لِمَ أَذِنَتْ لَهُمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَتَعْلَمَ الْكَاذِبِينَ ﴿٤٣﴾ لَا يَسْتَفْذِلُكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَنْ يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ ﴿٤٤﴾ إِنَّمَا يَسْتَفْذِلُكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَآرْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ فَهُمْ فِي رَيْبِهِمْ يَتَرَدَّدُونَ ﴿٤٥﴾ \* وَلَوْ أَرَادُوا الْخُرُوجَ لَأَعَدُّوا لَهُ عُدَّةً وَلَٰكِن كَرِهَ اللَّهُ انبِعَاثَهُمْ فَثَبَّطَهُمْ وَقِيلَ لَهُمْ قَاعِدُوا مَعَ الَّذِينَ يَتَرَدَّدُونَ ﴿٤٦﴾ لَوْ أَرَادُوا فِئْرًا مَا زَادُوكُمْ إِلَّا حَبَالًا وَلَا أَوْصُعًا حَلَلَكُمْ بِتَعُونِكُمْ الْفِتْنَةَ وَفِيكُمْ سَمَّعُونَ لَهُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤١﴾

**41. “Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito, na Piganeni Jihadi kwa mali yenu na nafsi zenu katika njia ya Mwenyezi Mungu. Haya ni kheri kwenu mkiwa mnajua”.**

**Ulazima wa Kwenda Katika Jihad kwa Hali Yoyote.**

رحمه الله تعالى Sufyan Ath-Thawri alisimulia kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Abu Adh-Dhuha, Muslim bin Swabih, ambaye alisema kuhusu Aya hii,

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا

**“Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito”.**

Ndiyo sehemu ya awali kushushwa katika Surat

Bara-ah.<sup>1</sup> Mu'tamir bin Sulayman alisema kuwa baba yake alisema, “Hadhrami alidai kuwa alitajiwa kwamba watu walikuwa wakitoa sababu ya ugonjwa na utuuzima. Mmoja wao anasema: Mimi siwezi kupata madhambi kama sitotoka kwenda Jihad.” Allah تعالى Akashusha,

<sup>1</sup> At-Tabari 14:270.

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا

***“Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito”.***<sup>1</sup>

Allah تعالى Aliamuru watu wote kutoka pamoja na Mtume ﷺ katika mwaka wa vita vya Tabuk, ili kuwapiga maadui wa Allah تعالى, makafiri wa kirumi ambao ni miongoni mwa watu wa Kitabu. Allah تعالى Aliwajibisha kwa Waumini kujiunga na Mtume ﷺ katika kila hali, iwe katika hali ya raha na karaha, katika hali ya uzito au wepesi. Allah تعالى Alisema,

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا

***“Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito”.***

‘Ali bin Zayd alisema kutoka kwa Anas kutoka kwa Abu Twalhah alisema kuwa Aya hiyo inawahusu: “Wazee na Vijana na Allah تعالى Hakukubali udhuru wa yeyote.” Abu Twalhah Akaenda Shamu akapigana mpaka akauliwa. Katika masimulizi mengine ni kuwa Abu Twalha alisoma *Surat Bara-ah* na alipofikia Aya hii,

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ

***“Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito, na Piganeni Jihadi kwa mali yenu na nafsi zenu katika njia ya Mwenyezi Mungu”.***

Alisema: “Naona Mola wetu Ametutaka tutoke sote wazee kwa Vijana. Wanangu! Niandalieni nitoke”. Wanawe wakamuambia, “Allah تعالى Akurehemu” Umefanya Jihadi pamoja na Mtume ﷺ mpaka akafariki, pia ukapigana ukiwa na Abubakr رضي الله عنه mpaka akafariki, pia na ‘Umar رضي الله عنه mpaka akafariki. Kwa hivyo, sisi tutafanya kazi hiyo badala yako.” Akakataa, akatoka kwa njia ya bahari (chini ya ukamanda wa Mu’awiyah) na akafariki. Wakawa hawakupata kisiwa cha kumzika, isipokuwa baada ya siku tisa bila ya mwili wake kubadilika.<sup>2</sup> Ndipo walipopata kisiwa na wakamzika. As-Suddi alisema kuwa Kauli ya Allah تعالى:

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا

***“Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito”.*** Maana yake ni tajiri au fakiri,

<sup>1</sup> At-Tabari 14:266.

<sup>2</sup> Ibn Abu Hatim 6:1802.

mwenye nguvu na dhaifu. Siku moja akaja mtu mmoja ambaye walidai kuwa ni Miqdad, alikuwa mkubwa na mnene. Akaomba aruhusiwe kutojiunga na Jihadi, lakini Mtume ﷺ alikataa. Siku hiyo ikashuka Ayah,

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا

**“Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito.”** Baada ya hapo, kukawa na ugumu kwa watu. Allah تعالى Akaifuta amri hiyo kwa Kauli Yake,

لَيْسَ عَلَى الصُّعْفَاءِ وَلَا عَلَى الْمَرْضَىٰ وَلَا عَلَى الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ مَا يُنْفِقُونَ  
حَرْجٌ إِذَا نَصَحُوا لِلَّهِ وَرَسُولِهِ

**“Hapana lawama kwa wanyonge, wagonjwa, na wasiopata cha kutumia, maadamu wanamsafia nia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake”. (9:91)**

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema: Hibban bin Zayd Ash-Shar’abi alinisimulia: “Tulihamasisha majeshi yetu pamoja na Swafwan bin ‘Amri ambaye alikuwa kadhi wa Hims yatoke kuelekea upande wa Ephos kwa Wakristo wa Jerajima. Nikamuona mtu mmoja mzee sana lakini mwenye nguvu, ambaye nyusi zake zimeangukia kwenye macho yake, alikuwa miongoni mwa wakazi wa Damaskas akiwa amepanda juu ya mnyama wake. Nikamuendea na kumuambia, “Ewe ami! Allah تعالى Ameshaukubali udhuru wako”. Akanyanyua nyusi zake na kujibu, “Ewe mwana wa Ndugu yangu! Allah تعالى Ametuhamasisha tutoke katika hali ya wepesi na ya uzito. Ujue, yule ambaye Allah تعالى Anampenda, humjaribu. Kisha watarejea kwa Allah تعالى na kuishi milele. Kwa hakika, Allah تعالى Huwafanyia majaribio waja Wake na Kuwaangalia, nani mwenye shukrani, subira, na akamdhukuru, wala siabudu kitu kingine isipokuwa Allah تعالى Peke Yake”.<sup>1</sup> Baada ya hapo, Allah تعالى Anawatia moyo waja juu ya kutoa mali kwa ajili ya njia Yake na mtu kujitolea uhai wake katika kumridhisha Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ. Allah تعالى Alisema:

وَجَاهِدُوا بِأَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ذَلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ

**“...na Piganeni Jihadi kwa mali yenu na nafsi zenu katika njia ya Mwenyezi Mungu. Haya ni kheri kwenu mkiwa mnajua”.**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:264.

Hili ni jema kwenu duniani na Akhera, kwa sababu nyinyi mnatoa kiasi kidogo cha mali, na Allah تعالى Anakupeni Ghanima ya mali za maadui wenu, pamoja na ukarimu Anaokuandalieni huko Akhera. Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ:

«تَكْفَلُ اللَّهُ لِلْمُجَاهِدِ فِي سَبِيلِهِ إِنْ تَوَفَّاهُ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ، أَوْ يَرُدَّهُ إِلَى مَثَرِلِهِ بِمَا نَالَ مِنْ أَجْرٍ أَوْ غَنِيمَةٍ»

*“Allah Amechukua dhamana (badili) kwa anayepigana Jihadi katika Njia Yake kwamba Akimfisha Atamuingiza Peponi, au Atamrudisha nyumbani kwake akiwa amejiipatia malipo ya ghanima”.<sup>1</sup>*

Na kwa ajili hiyo Allah تعالى Alisema:

كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهُ لَكُمْ وَعَسَى أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ وَعَسَى أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا وَهُوَ شَرٌّ لَكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

*“Mmeandikiwa kupigana vita, navyo vinachusha kwenu. Lakini huenda mkachukua kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu Anajua na nyinyi hamjui”. (2:216)*

Pia kwa minajili hii, kuna Hadithi aliyoiandika Imamu Ahmad kuwa Anas رضي الله عنه alisema kwamba Mtume ﷺ alimuambia mtu mmoja,

«أَسْلِمُ»

*“Silimu”*

Akasema: “Najisikia sipendi kufanya hivyo”. Naye akamuambia,

«أَسْلِمُ وَإِنْ كُنْتَ كَارِمًا»

*“Silimu, hata kama hupendi”.<sup>2</sup>*

لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيبًا وَسَفَرًا قَاصِدًا لَاتَّبَعُوكَ وَلَكِنْ بَعُدَتْ عَلَيْهِمُ الشُّقَّةُ وَسَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ لَوِ اسْتَطَعْنَا لَخَرَجْنَا مَعَكُمْ يُلِكونَ أَنفُسَهُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٢١٧﴾

<sup>1</sup> Muslim 4:1496.

<sup>2</sup> Ahmad 3:109.

**42. “Na lau ingelikuwa ipo faida ya papo kwa papo, na safari yenyewe ni fupi, wangelikufuata. Lakini wameona ni mbali na kuna mashaka. Nao wataapa kwa Mwenyezi Mungu: Tungeliweza bila ya shaka tungelitoka pamoja nanyi. Wanaziangamiza nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa hakika hao ni waongo.”**

### Safari ya Wanafiki Kutojiunga Katika Jihadi na Kubainisha Vitimbi Vyao

Allah تعالى Anawashutumumu wale ambao hawakujiunga pamoja na Mtume ﷺ katika vita vya Tabuk na wakabaki nyuma baada ya kumuomba idhini kwa kuonesha kuwa walikuwa na nyudhuru ilhali ukweli haukuwa hivyo. Allah تعالى Alisema,

لَوْ كَانَ عَرَضًا قَرِيبًا

“**Na lau ingelikuwa ipo faida ya papo kwa papo**”. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Ni ngawira zilizokuwa mbele ya macho yao”.

وَسَفَرًا قَاصِدًا

“**...na safari yenyewe ni fupi**”. Kwa maana: Ni ya mwendo mfupi.

لَا تَتَّبِعُوا

“**...wangelikufuata**”. Wangelikuja nawe pamoja.

وَلَيْكِنْ بُعِدَتْ عَنْهُمْ الْأُشُقَّةُ

“**Lakini wameona ni mbali na kuna mashaka**”.

Kwa maana: Masafa ya kwenda Shamu marefu.

وَسَيَخْلِفُونَ بِاللَّهِ

“**Nao wataapa kwa Mwenyezi Mungu**”.

Kwa maana: Kukuapieni pindi mtakaporejea kutoka vitani.

لَوْ أَسْتَطَعْنَا لَخَرَجْنَا مَعَكُمْ

“**Tungeliweza bila ya shaka tungelitoka pamoja nanyi**”.

Inamaanisha, “Kama tusingelikuwa na nyudhuru, tungelitoka pamoja nanyi”. Allah تعالى Anawaambia,

يَلِكُونُ أَنْفُسَهُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ

**“Wanaziangamiza nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu Anajua kuwa hakika hao ni waongo”.**

عَفَا اللَّهُ عَنْكَ لِمَ أَذْنَتْ لَهُمْ حَتَّىٰ يَتَّبِعَنَّ لَكَ الَّذِينَ صَدَقُوا وَتَعْلَمَ الْكَاذِبِينَ ﴿٤٢﴾ لَا يَسْتَفْذِنُكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَنْ يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ ﴿٤٣﴾ إِنَّمَا يَسْتَفْذِنُكَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَرْتَابَتْ قُلُوبُهُمْ فَهُمْ فِي رَبِّهِمْ يَتَرَدَّدُونَ ﴿٤٤﴾

**43. “Mwenyezi Mungu Amekusamehe! Kwa nini ukawapa ruhusa kabla ya kubainikia kwako wanaosema kweli, na ukawajua waongo?”**

**44. “Hawatakuomba ruhusa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, wasiende kupigana Jihadi kwa mali yao na nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuwajua Wachamungu”.**

**45. “Wasiomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na nyoyo zao zikatia shaka, hao tu ndio wanaokutaka ruhusa. Basi hao wanataradadi katika shaka zao”.**

Lawama kwa Mtume ﷺ kwa Kuwapa Idhini ya Kubaki.

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa ‘Awn alisema, “Je mmeshapata kusikia lawama nyepesi zaidi ya hii? Zinaanza kwa kutoa msamaha kabla ya kutajwa lawama,

عَفَا اللَّهُ عَنْكَ لِمَ أَذْنَتْ لَهُمْ

**“Mwenyezi Mungu Amekusamehe! Kwa nini ukawapa ruhusa”.**<sup>1</sup>

Muwarriq Al-‘Ijli na wengine walisema sawa na hivyo.<sup>2</sup> Qatadah alisema, “Ni lawama kama mlivyoisikia, kisha (Mtume ﷺ) aliteremshiwa, katika Surat *An-Nur*, ruhusa ya kuwapa idhini hiyo kama atataka kufanya hivyo,

<sup>1</sup> Ibn Abu Hatim 6:1805.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:273.

فَإِذَا أَسْتَعْدْتُوكَ لِبَعْضِ شَأْنِهِمْ فَأَذِّنْ لِمَنْ شِئْتَ مِنْهُمْ

**“Na wakikuomba ruhusa kwa baadhi ya kazi zao, mruhusu Umtakaye miongoni mwao”. (24:62)<sup>1</sup>**

Ndivyo pia ilivyonukuliwa na ‘Atwaa Al-Khuraasani. Mujahid alisema, “Aya hii ilishuka kuhusu kikundi cha watu ambao walisema, “Muombeni idhini Mtume ﷺ na ikiwa atakukubalieni bakieni, au kama akikataa, bakieni pia!”<sup>2</sup>

Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema:

حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكَ الَّذِينَ صَدَقُوا

**“Kabla ya kubainikia kwako wanaosema kweli”.** Kwa kuzitaja nyudhuru zao,

وَتَعْلَمَ الْكٰذِبِينَ

**“...na ukawajua waongo?”**

Allah تعالى Anasema, “Kwa nini hukukataa kuwakubalia pindi walipokuomba idhini kwa kutokumkubalia yeyote miongoni mwao juu ya kutokujiunga, ili uwajue katika wao, mkweli na muongo katika kukutii, ni akina nani waliokusudia kutokujiunga na vita, hata kama hutawapa idhini ya kufanya hivyo. Kisha, Allah تعالى Alisema kuwa, hapana yeyote anayemuamini Allah تعالى na Mtume ﷺ kisha akataka idhini ya kubakia nyuma. Alisema:

لَا يَسْتَفِذُنَاكَ

**“Hawatakuomba ruhusa”.** Ya kutokujiunga kwenda vitani,

الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَن يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ

**“...wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, wasiende kupigana Jihadi kwa mali yao na nafsi zao”.**

Kwa sababu wanaiona Jihadi kuwa ni kitendo cha kuwaweka karibu na Allah تعالى, na wanapotakiwa kwenda Jihadi, hufanya haraka na kutekeleza amri.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:273.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:273.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ ﴿٤١﴾ إِنَّمَا يَسْتَفْذِنُكَ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwajua Wachamungu. Wanao kutaka ruhusa”.**

Ya kubakia nyuma ni watu wasio na udhuru.

الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

**“...wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho”.**

Ambao hawatarajii malipo ya amali zao huko Akhera.

وَأَرْتَابَتِ قُلُوبُهُمْ

**“...na nyoyo zao zikatia shaka”.** Juu ya usahihi wa yale uliyowaletea.

فَهُمْ فِي رَبِّهِمْ يَتَرَدَّدُونَ

**“Basi hao wanataradadi katika shaka zao”.**

Kwa kupiga hatua moja kwenda mbele na nyingine kurudi nyuma. Hawana msimamo madhubuti katika jambo lolote kwa sababu ni watu wenye shaka na wameangamia. Hawako katika kundi la hawa wala kundi la wale, na aliyedhalilishwa na Allah تعالى, hatapata njia ya kuongoka.

\* وَلَوْ أَرَادُوا الْخُرُوجَ لَأَعَدُّوا لَهُ عُدَّةً وَلَكِنْ كَرِهَ اللَّهُ انْبِعَاثَهُمْ فَثَبَّطَهُمْ وَقِيلَ اقْعُدُوا

مَعَ الْقَاعِدِينَ ﴿٤٢﴾ لَوْ خَرَجُوا فِيكُمْ مَا زَادُوكُمْ إِلَّا خَبَالًا وَلَأَوْضَعُوا خِلَالَكُمْ

يَبْغُونَكُمْ الْأُفْتِنَةَ وَفِيكُمْ سَمْعُونَهُمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ ﴿٤٣﴾

**46. “Na ingelikuwa kweli walitaka kutoka bila ya shaka wangelijandalia maandalio, lakini Mwenyezi Mungu Kachukia kutoka kwao, na kwa hivyo Akawazuia na ikasemwa: Kaeni pamoja na wanaokaa!”**

**47. “Lau wangelitoka nanyi wasingelikuzidishieni ila mchafuko, na wangetangatanga kati yenu kukutilieni fitna. Na miongoni mwenu wapo wanaowasikiliza. Na Mwenyezi Mungu Anawajua madhalimu”.**



**Kufichua Hali za Wanafiki.**

Allah تعالى Anasema:

وَلَوْ أَرَادُوا الْخُرُوجَ

**“Na ingelikuwa kweli walitaka kutoka”.** Pamoja nawe kwenda vitani.

لَأَعَدُّوا لَهُ عُدَّةً

**“...bila ya shaka wangelijiandalia maandalio”.**

Maana yake: Wangelijitayarisha kwa ajili ya kutoka kumkabili adui.

وَلَكِنَّ كَرِهَ اللَّهُ انْبِعَاثَهُمْ

**“...lakini Mwenyezi Mungu Kachukia kutoka kwao”.**

Maana yake Hakupenda, kwa Qudura Yake, kwamba watoke pamoja nawe.

فَتَبَطَّأَهُمْ

**“...na kwa hivyo Akawazuia”.** Inamaanisha, Akawafanya wabakie.

وَقِيلَ أَقْعُدُوا مَعَ الْقَاعِدِينَ

**“...na ikasemwa: Kaeni pamoja na wanao kaa!”**

Kwa Qudura Yake. Kisha Allah تعالى Akabainisha sababu ya Kuchukia Kwake jambo la kutoka kwao pamoja na Waumini. Akasema,

لَوْ خَرَجُوا فِيكُمْ مَا زَادُوكُمْ إِلَّا خَبَالًا

**“Lau wangelitoka nanyi wasingelikuzidishieni ila mchafuko”.**

Kwa sababu wao ni wenye uoga na waliodhalilishwa.

وَلَا وَضَعُوا حِلَّكُمْ يَبْغُونَكُمْ أَلْفِتَةً

**“...na wangetangatanga kati yenu kukutilieni fitna”.**

Kwamba wangeliharakisha kwenda na kueneza utesi, chuki na fitina baina yenu.

وَفِيكُمْ سَمْعُونَ هُمْ

**“Na miongoni mwenu wapo wanaowasikiliza”.**

Maana yake, wanaowatii na wanaoyapenda mazungumzo na kauli zao, na kuwaomba ushauri wao bila ya kuzijua hali zao za kweli za unafiki. Kwa ajili hiyo, shari na ufisadi mkubwa ungeluweza kuwasibu Waumini.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema: “Walioomba idhini (kwa Mtume ﷺ kwamba wabakie nyuma) walikuwa ni pamoja na baadhi ya viongozi. Miongoni mwao ni ‘Abdullah bin Ubayy bin Salul na Jadd bin Qays. Hawa walikuwa viongozi wa kaumu zao. Allah تعالى Aliwafanya wabakie nyuma kwa sababu Alijua kwamba ikiwa Watakwenda pamoja na Mtume ﷺ, wangelipandikiza ufisadi ndani ya jeshi”<sup>1</sup>. Kulikuwa na baadhi ya wapiganaji wa Mtume ﷺ ambao walikuwa wakiwapenda na kuwatii wakuu wao, kwa sababu waliwachukulia kwamba ni waheshimiwa. Allah تعالى Anasema,

وَفِيكُمْ سَمْعُونَ هُمْ

**“Na miongoni mwenu wapo wanaowasiliza”. (9:47)**

Kisha Allah تعالى Akaeleza juu ya Utimilifu wa Ilimu Yake,

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالظَّالِمِينَ

**“Na Mwenyezi Mungu Anawajua madhalimu”.**

Ameeleza kwamba Yeye Anayajua yaliyojiri, na yatakayojiri, na yale ambayo hayajajiri, na kwamba yale ambayo hayakujiri kama yangejiri yangejiri vipi. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Amesema,

لَوْ خَرَجُوا فِيكُمْ مَا زَادُوكُمْ إِلَّا خَبَالًا

**“Lau wangelitoka nanyi wasingelikuzidishieni ila mchafuko”.**

Ameeleza hali yao kuwa lau kama wangelitoka ingelikuwaje. Pamoja na haya hawakutoka. Ni sawa na Kauli Yake nyingine Anasema,

وَلَوْ زِدُوا لَعَادُوا لِمَا بُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ

**“Na kama wangelirudishwa bila ya shaka wangerejea yale yale waliyokatazwa. Na hakika hao ni waongo”. (6:28)**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:277.

Na Kauli Yake nyingine;

﴿٢٣﴾ وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَأَسْمَعَهُمْ ۗ وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوْا وَهُمْ مُعْرِضُونَ ﴿٢٣﴾

**“Na Mwenyezi Mungu Angelijua wema wowote kwao Angewasikilizisha, na lau Angewasikilizisha wangeligeuka wakapuuzi”. (8:23)**

Na Kauli Yake nyingine,

﴿٦٦﴾ وَلَوْ أَنَّا كَتَبْنَا عَلَيْهِمْ أَنْ اقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ أَوْ اخْرَجُوا مِنْ دِيَارِكُمْ مَا فَعَلُوهُ إِلَّا قَلِيلٌ مِّنْهُمْ ۗ ﴿٦٦﴾  
 ﴿٦٧﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ فَعَلُوا مَا يُوعَظُونَ بِهِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ وَأَشَدَّ تَثْبِيثًا ﴿٦٧﴾ وَإِذَا لَأَتَيْنَهُمْ مِّن لَّدُنَّا  
 أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٦٨﴾ وَلَهَدَيْنَهُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا ﴿٦٨﴾

**“Na lau kuwa Tumewaamrisha: Jiueni au tokeni majumbani mwenu, wasingelifanya hayo ila wachache tu miongoni mwao. Na lau kama wangelifanya waliowaidhiwa ingelikuwa bora kwao na uthibitisho wa nguvu zaidi. Na hapo Tungewapa malipo makubwa kutoka Kwetu. Na Tungeliwaongoa njia iliyonyooka”. (4:66-68)**

Zipo Aya nyingi juu ya mada hii. Kisha Anasema,

\* \* \*

لَقَدْ أْتَعَوْا أَلْفِتْنَةً مِّن قَبْلُ وَقَلَّبُوا لَكَ الْأُمُورَ حَتَّى جَاءَ  
 الْحَقُّ وَظَهَرَ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَرِهُونَ ﴿٤٨﴾ وَمِنْهُمْ مَّن  
 يَقُولُ أَئِذْنَ لِي وَلَا تَفْتِنِي ۗ أَلَا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوا ۗ وَإِنَّ  
 جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ ﴿٤٩﴾ إِنْ تُصِيبَكَ  
 حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ ۗ وَإِنْ تُصِيبَكَ مُصِيبَةٌ يَقُولُوا قَدْ أَخَذْنَا  
 أَمْرَنَا مِن قَبْلُ وَيَتَوَلَّوْا وَهُمْ فَرِحُونَ ﴿٥٠﴾ قُلْ لَنْ  
 يُصِيبَنَا إِلَّا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَانَا ۗ وَعَلَى اللَّهِ  
 فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٥١﴾ قُلْ هَلْ تَرَى صُورَ بِنَا  
 إِلَّا إِحْدَى الْحُسَيْنِ ۗ وَنَحْنُ نَرَى صُورَ بِكُمْ أَنْ يُصِيبَكُمُ اللَّهُ  
 بِعَذَابٍ مِّنْ عِنْدِهِ ۗ أَوْ بِأَيْدِينَا ۗ فَتَرَبَّصُوا إِنَّا مَعَكُمْ  
 مُتَرَبِّصُونَ ﴿٥٢﴾ قُلْ أَنْفِقُوا طَوْعًا أَوْ كَرْهًا لَنْ يُتَقَبَلَ  
 مِنْكُمْ ۗ إِنَّكُمْ كُنْتُمْ قَوْمًا فَسِيقِينَ ﴿٥٣﴾ وَمَا مَنَعَهُمْ أَنْ  
 تُقَبَلَ مِنْهُمْ نَفَقَتُهُمْ ۗ إِلَّا أَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَبِرَسُولِهِ وَلَا  
 يَأْتُونَ الصَّلَاةَ إِلَّا وَهُمْ كُسَالَىٰ وَلَا يُعْطُونَ ۗ إِلَّا وَهُمْ  
 كَرِهُونَ ﴿٥٤﴾

لَقَدْ أْتَعَوْا أَلْفِتْنَةً مِّن قَبْلُ وَقَلَّبُوا  
 لَكَ الْأُمُورَ حَتَّى جَاءَ الْحَقُّ وَظَهَرَ  
 أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَرِهُونَ ﴿٤٨﴾

48. "Tangu zamani walitaka kukutilieni fitna, na wakupingulia mambo juu chini, mpaka ikaja Haki na ikadhihirika amri ya Mwenyezi Mungu na wao wamechukia".

Allah تعالیٰ Anamhadharisha Mtume ﷺ juu ya Wanafiki

لَقَدْ أْتَعَوْا أَلْفِتْنَةً مِّن قَبْلُ وَقَلَّبُوا  
 لَكَ الْأُمُورَ

"Tangu zamani walitaka kukutilieni fitna, na wakakupingulia mambo juu chini".

Kwa muda mrefu, wanafiki wamezitumia fikra zao na wameweka wazi mtazamo

wao katika kukufanyia vitimbi dhidi yako na Masahaba wako, kadhalika kuidhalilisha dini yako na kujaribu kuizima. Haya yalitokea muda mrefu na muda mfupi tu baada ya Mtume ﷺ kufika Madinah, Waarabu waliungana na Wayahudi na wanafiki wa Madinah dhidi ya Mtume ﷺ kumpiga vita. Baada ya Allah تعالیٰ kumpa ushindi katika vita vya Badr na Akaliweka juu Neno Lake, 'Abdullah bin Ubayy na marafiki zake walisema: "Jambo hili (Uislamu) limeshinda". Wakasilimu kijuu juu tu na kila wakati ambapo Allah تعالیٰ

Aliunyanyua Uislamu na Waislamu hilo liliwazidisha hasira na kukata tamaa. Allah تعالى Alisema:

حَتَّىٰ جَاءَ الْحَقُّ وَظَهَرَ أَمْرُ اللَّهِ وَهُمْ كَرِهُونَ

**“...mpaka ikaja Haki na ikadhihirika Amri ya Mwenyezi Mungu na wao wamechukia”.**

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَقُولُ أَتَذَّنَ لِي وَلَا تَفْتِنِي ۗ أَلَا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوا ۗ وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ

بِالْكَافِرِينَ ﴿٤٩﴾

**49. “Na miongoni mwao wapo wanao sema: Niruhusu wala usinitie katika fitna. Kwa yakini wao hivyo wamekwisha tumbukia katika fitna. Na hakika Jahannamu imewazunguka”.**

Allah تعالى Anasema: Kuna wanafiki wanaokuambia, Ewe Muhammad,

أَتَذَّنَ لِي

**“Niruhusu”.** Kubaki bila kutoka,

وَلَا تَفْتِنِي ۗ

**“...wala usinitie katika fitna”.** Kwa kutoka pamoja nawe, kwani ikiwa nitatoka pamoja na wewe na kuwaona wanawake wa Kirumi fitna itakuwa kubwa. Allah تعالى Alisema,

أَلَا فِي الْفِتْنَةِ سَقَطُوا ۗ

**“Kwa yakini wao hivyo wamekwisha tumbukia katika fitna”.**

Kwa maana: Wamekwishaingia katika fitna kwa kauli yao hiyo. Ni kama alivyosema Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى kutoka kwa Az-Zuhri, Yazid bin Ruman, ‘Abdullah bin Abu Bakri, ‘Aswim bin Qatadah na wengine walisema kwamba: Siku moja, Mtume ﷺ akiwa katika Maandalizi ya kwenda kwenye Jihadi, alimuambia Jadd bin Qays, aliyetokana na Banu Salimah:

«هَلْ لَكَ يَا جَدُّ الْعَامِ فِي جَلَادِ بَنِي الْأَصْفَرِ؟»

**“Je, ewe Jadd! Utapenda kupigana na wa rangi ya manjano (Warumi-Banu Asfar) mwaka huu?”**

Akasema: “Ewe Mtume ﷺ! Utanipa idhini, na wala hutanitia katika fitna. Wallahi! Kaumu yangu wanajua kwamba hapana mtu anayependa sana wanawake kunishinda mimi. Mimi nachelea kwamba ikiwa nitawaona wanawake na watu hao wa manjano, sitaweza kuvumilia dhidi yao”. Mtume ﷺ akageukia upande mwingine na akamuambia,

«قَدْ أُذِنْتُ لَكَ»

“Nimekupa idhini”.

Ikashuka Aya kumhusu Jadd bin Qays,

وَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ أَئِذْنَ لِي وَلَا تَفْتِنِي<sup>1</sup>

**“Na miongoni mwao wapo wanaosema: Niruhusu wala usinitie katika fitna”.**

Ikiwa anachokihofia ni wanawake wa watu wa Bani Asfar (wakati hayuko hivyo) basi fitna aliyoiingia kwa kubaki bila kutoka na Mtume ﷺ na kujichagulia anavyotaka mwenyewe hiyo ni kubwa zaidi<sup>1</sup>. Hivi ndivyo ilivyosimuliwa na Ibn ‘Abbas, Mujahid na wengine kwamba ilishuka kumhusu Jadd bin Qays, ambaye alikuwa miongoni mwa viongozi wa Banu Salamah<sup>2</sup>. Imeandikwa ndani ya Sahih kuwa Mtume ﷺ aliwauliza,

«مَنْ سَيِّدُكُمْ يَا بَنِي سَلَمَةَ؟»

“Ni nani ndiye mkuu wenu, enyi Banu Salamah?”

Wakajibu: “Ni Al-Jadd bin Qays, ingawa ana tabia ya ubakhili”. Mtume ﷺ akasema,

«وَأَيُّ دَاءٍ أَدْوَأُ مِنَ الْبُخْلِ! وَلَكِنْ سَيِّدُكُمْ الْفَتَى الْجَعْدُ الْأَبْيَضُ بِشْرِ بْنِ الْبَرَاءِ بْنِ مَعْرُورٍ»

“Je, ni maradhi gani mabaya zaidi kuliko ubakhili! Lakini kiongozi wenu anayewafaa ni kijana mweupe mwenye nywele za singa, Bishr bin Al-Bara-I bin Ma’rur”.<sup>3</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 14:287.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:287.

<sup>3</sup> Al-Hakim 3:219.

Kauli ya Allah تعالى،

وَإِنَّ جَهَنَّمَ لَمُحِيطَةٌ بِالْكَافِرِينَ

**“Na hakika Jahannamu imewazunguka”.**

Na kamwe hawataweza kuikwepa, kuizuia wala kuiepuka.

إِنْ تُصِيبَكَ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ ۖ وَإِنْ تُصِيبَكَ مُصِيبَةٌ يَقُولُوا قَدْ أَخَذْنَا أَمْرَنَا مِنْ قَبْلُ  
وَيَتَوَلَّوْا وَهُمْ فَرِحُونَ ﴿٥٠﴾ قُلْ لَنْ يُصِيبَنَا إِلَّا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَنَا هُوَ مَوْلَانَا وَعَلَى  
اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿٥١﴾

**50. “Ukiupata wema unawachukiza, na ukikusibu msiba, wao husema: Sisi tuliangalia mambo yetu vizuri tangu kwanza. Na hugeuka kwenda zao nao wamefurahi”.**

**51. “Sema: Halitusibu ila Alilotuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye Ndiye Mola wetu Mlinzi. Na Waumini Wamtegemee Mwenyezi Mungu tu”.**

Allah تعالى Anamjulisha Mtume ﷺ kuhusu uadui wa wanafiki, kwa sababu, ikiwa anapata jema, yaani ushindi juu ya maadui kiasi cha kumfurahisha yeye na Masahaba wake, basi hilo huwakasirisha wao.

وَإِنْ تُصِيبَكَ مُصِيبَةٌ يَقُولُوا قَدْ أَخَذْنَا أَمْرَنَا مِنْ قَبْلُ

**“...na ukikusibu msiba, wao husema: Sisi tuliangalia mambo yetu vizuri tangu kwanza”.**

Wanasema: Tulichukua tahadhari ya kutofatana naye mapema kabla ya hayo yaliyomtokea.

وَيَتَوَلَّوْا وَهُمْ فَرِحُونَ

**“Na hugeuka kwenda zao nao wamefurahi”.**

Allah تعالى Akamueleza Mtume ﷺ namna ya kuwajibu kutokana na kauli na uadui wao mkubwa kabisa.

Allah تعالى Alisema,

قُلْ

“Sema” Uwaambie.

لَنْ يُصِيبَنَا إِلَّا مَا كَتَبَ اللَّهُ لَنَا

“Halitusibu ila Alilotuandikia Mwenyezi Mungu”.

Maana yake: Sisi tuko chini ya Kutaka Kwake Qudura Yake Allah تعالى.

هُوَ مَوْلَانَا

“Yeye Ndiye Mola wetu Mlinzi”.

Maana: Bwana wetu tunayemtegemea.

وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ

“Na Waumini Wamtegemee Mwenyezi Mungu tu”. (9:51)

Nasi tunatawakali Kwake, Naye Anatutosha na Ndiye Mlezi wetu Mzuri.

قُلْ هَلْ تَرَبُّصُونَ بِنَا إِلَّا إِحْدَى الْحُسَيْنَيْنِ<sup>ط</sup> وَخُنْ نَرَبِّصُ بِكُمْ أَنْ يُصِيبَكُمُ اللَّهُ  
بِعَذَابٍ مِنْ عِنْدِهِ أَوْ بِأَيْدِينَا<sup>ط</sup> فَتَرَبُّصُوا إِنَّا مَعَكُمْ مُتَرَبِّصُونَ ﴿٥١﴾ قُلْ أَنْفِقُوا  
طَوْعًا أَوْ كَرْهًا لَنْ يُتَقَبَلَ مِنْكُمْ<sup>ط</sup> إِنَّكُمْ كُنْتُمْ قَوْمًا فَاسِقِينَ ﴿٥٢﴾ وَمَا مَنَعَهُمْ أَنْ تُقَبَلَ  
مِنْهُمْ نَفَقَتُهُمْ إِلَّا أَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَلَا يَأْتُونَ الصَّلَاةَ إِلَّا وَهُمْ كُسَالَى  
وَلَا يُنْفِقُونَ إِلَّا وَهُمْ كَارِهِونَ ﴿٥٣﴾

52. “Sema: Hivyo mnatutazamia litupate lolote isipokuwa moja katika mema mawili? Na sisi tunakutazameni kuwa Mwenyezi Mungu Akufikishieni adhabu itokayo Kwake, au kutokana na mikono yetu. Basi ngojeni, nasi tunangoja pamoja nanyi”.

53. “Sema: Toeni mkipenda au msipende. Hakitopokelewa kitu kwenu, kwani nyinyi ni watu wapotovu”.

54. “Na hawakuzuliwa kukubaliwa michango yao ila kwa kuwa walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala hawaji



***kwenye Sala ila kwa Uvivu, wala hawatoi michango ila wao wamechukia***”.

Allah تعالیٰ Anasema,

قُلْ

**“Sema”**. Uwaambie, ewe Muhammad!

هَلْ تَرْتَضُونَ بِنَا

**“Hivyo mnatutazamia litupate lolote”**. Kwa maana: Mnatungojea.

إِلَّا أَحَدَى الْحُسَيْنَيْنِ<sup>ط</sup>

**“...isipo kuwa moja katika mema mawili?”**

Na hayo mawili ni: kufa shahidi au ushindi dhidi yenu. Tafsiri hii ni kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas, Mujahid, Qatadah na wengine.<sup>1</sup>

وَنَحْنُ نَرْتَضُ بِكُمْ

**“Na sisi tunakutazameni”**. Maana yake, tunakungojeni.

أَنْ يُصِيبَكُمُ اللَّهُ بِعَذَابٍ مِنْ عِنْدِهِ أَوْ بِأَيْدِينَا<sup>ط</sup>

**“...kuwa Mwenyezi Mungu Akufikishieni adhabu itokayo Kwake, au kutokana na mikono yetu”**.

Tunakungojeni yakufikieni hayo, ama, ni kwa njia ya kutekwa au kuuawa.

فَتَرْتَضُوا إِنَّا مَعَكُمْ مُتَرْتَضُونَ

**“Basi ngojeni, nasi tunangoja pamoja nanyi”**.

Kauli ya Allah تعالیٰ:

قُلْ أَنْفِقُوا طَوْعًا أَوْ كَرْهًا

**“Sema: Toeni mkipenda au msipende”**. Namna yoyote mtakayotoa.

لَنْ يُتَقَبَلَ مِنْكُمْ<sup>ط</sup> إِنْ كُمْ كُنْتُمْ قَوْمًا فَاسِقِينَ

**“Hakitopokelewa kitu kwenu, kwani nyinyi ni watu wapotovu”**.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:292.

Kisha, Allah تعالی Alieleza sababu ya hali hiyo kwamba wao hawatokubaliwa kwa wanachokitoa.

أَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ

**“...kwa kuwa walimkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake”.**

Na amali husihi ikiwa zinafanyika pamoja na usahihi wa Imani.

وَلَا يَأْتُونَ الصَّلَاةَ إِلَّا وَهُمْ كُسَالَىٰ

**“...wala hawaji kwenye Sala ila kwa uvivu”.**

Maana yake hawana nia sahihi wala hima (kujituma) katika kutenda amali (za kiimani).

وَلَا يُنْفِقُونَ

**“Wala hawatoi michango”** Maana yake: Mali.

إِلَّا وَهُمْ كَرِهُونَ

**“ila wao wamechukia.”**

Mkweli wa kusadikiwa, ambaye ukweli ulishushwa kwake, Muhammad ﷺ alisema kuwa Allah تعالی Haachi kutoa malipo isipokuwa mpaka nyinyi (Waumini) muache kufanya amali njema, na kwamba Allah تعالی ni *Twayyib* (Mzuri na Mtakasifu) na Hapokei isipokuwa kilicho *Twayyib* tu. Hivyo, Allah تعالی Hapokei mali au amali za watu waliotajwa katika Aya hizi kwani Hupokea amali za wachamungu.

\* \* \*

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ<sup>٤</sup> إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ  
 بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٥٥﴾  
 وَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنَّهُمْ لَمِنْكُمْ وَمَا هُمْ مِنْكُمْ وَلَكِنَّهُمْ  
 قَوْمٌ يَفْرُقُونَ ﴿٥٦﴾ لَوْ يَخْتَدُونَ مَلَجًا أَوْ مَغْرَاتٍ أَوْ  
 مُدْخَلًا لَوَلَّوْا إِلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَحُونَ ﴿٥٧﴾ وَمِنْهُمْ مَنْ يَلْمِزُكَ  
 فِي الصَّدَقَاتِ فَإِنْ أُعْطُوا مِنْهَا رَضُوا وَإِنْ لَمْ يُعْطَوْا مِنْهَا  
 إِذَا هُمْ يَسْتَخْطُونَ ﴿٥٨﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ رَضُوا مَا آتَاهُمُ  
 اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ سَيُؤْتِينَا اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ  
 وَرَسُولُهُ إِنَّا إِلَى اللَّهِ رَاغِبُونَ ﴿٥٩﴾ \* إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ  
 لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسْكِينِ وَالْعَمِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمَوْلَاةِ قُلُوبِهِمْ  
 وَفِي الرِّقَابِ وَالْغُرَمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ<sup>٥</sup>  
 فَرِيضَةً مِنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾ وَمِنْهُمْ  
 الَّذِينَ يُؤْذُونَ النَّبِيَّ وَيَقُولُونَ هُوَ أُذُنٌ قُلْ أُذُنٌ خَيْرٌ  
 لَكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِينَ وَرَحْمَةٌ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا  
 مِنْكُمْ<sup>٦</sup> وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ رَسُولَ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦١﴾

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ<sup>٤</sup>  
 إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ  
 كَافِرُونَ ﴿٥٥﴾

55. "Yasikughuri mali yao wala wana wao. Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kuwaadhibu kwayo hapa duniani na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri".

Allah تعالى Anamuambia Mtume ﷺ,

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ<sup>٤</sup>

"Yasikughuri mali yao wala wana wao".

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى Aliyosema;

وَلَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ زَهْرَةَ الْحَيَاةِ

الدُّنْيَا لِنَتَفَتَّهِنَّ فِيهِ<sup>٤</sup> وَرَزَقْنَا رِبَّكَ

خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿٦١﴾

"Wala usivikodolee macho Tulivyowastareheshea baadhi ya watu miongoni mwao, kwa ajili ya mapambo ya duniani, ili Tuwajaribu. Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora na inadumu zaidi". (20:131)

Na Allah تعالى Amesema,

أَحْسِبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِ مِنْ مَّالٍ وَبَيْنَ ۞ نَسَارِعُ هُمْ فِي الْخَيْرَاتِ ۗ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ۞

**“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto. Ndio Tunawahimiza kheri? Lakini wenyewe hawatambui”. (23:55-56)**

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

**“Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kuwaadhibu kwayo hapa duniani”.**

Kwa mujibu wa maana iliyotolewa na Al-Hasan Al-Basri, kutokana na Zaka yake na kuitumia katika njia ya Allah تعالى<sup>1</sup>. Kauli ya Allah تعالى:

وَتَزَهَّقَ أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ

**“...na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri”.**

Kwa maana: Na Anataka Kuwafisha wakiwa katika ukafiri, wakati wa kufariki kwao ili hilo liwe jambo gumu kwao na wapate adhabu kali. Allah تعالى Atukinge dhidi ya hayo. Na kufanya hivi kwao wao ni kuwapa muda kidogo kidogo ili wapate kujisahau.

وَيَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِيَّاهُمْ لَمِنْكُمْ وَمَا هُمْ مِنْكُمْ وَلَئِكِنَّهُمْ قَوْمٌ يَفْرُقُونَ ۞ لَوْ

يَجِدُونَ مَلْجَأًا أَوْ مَغْرَبَاتٍ أَوْ مُدْخَلًا لَوْلَا إِلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَعُونَ ۞

**56. “Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba wao ni katika nyinyi, wala wao si katika nyinyi. Lakini ni watu wanaoogopa”.**

**57. “Lau kama wangelipata pa kukimbilia au mapango au pahala pa kuingia basi wangelifyatuka mbio kuelekea huko”.**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:296.

**Kubainisha Woga na Khofu ya Wanafiki.**

Allah تعالى Anampa khabari Mtume Muhammad ﷺ juu ya khofu, uoga na kutishika kwa wanafiki kwamba:

وَيَخْلِفُونَ بِاللَّهِ إِيَّاهُمْ لَمِنكُمْ

***“Na wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kwamba wao ni katika nyinyi”.***

Wanaapa kiapo cha kusisitiza kuwa wapo pamoja nanyi.

وَمَا هُمْ مِّنكُمْ

***“...wala wao si katika nyinyi”.***

Kwa ukweli na kwa uhakika.

وَلَكِنَّهُمْ قَوْمٌ يَفْرُقُونَ

***“Lakini ni watu wanaoogopa”.***

Hilo ndilo lililowapelekea kuapa.

لَوْ يَجِدُونَ مَلَجًا

***“Lau kama wangelipata pa kukimbilia”.***

Wangepata ngome ya kuwakinga au kujihifadhi wakaitumia kujikinga.

أَوْ مَغْرَبٍ

***“...au mapango”.***

Nayo ni yale yaliyo milimani.

أَوْ مُدْخَلًا

***“...au pahala pa kuingia”.***

Kama mferejini au shimo la ardhini. Tafsiri hii ni kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas, Mujahid na Qatadah رضي الله عنهم ,

لَوْلَوْ أَلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَعُونَ

***“...basi wangelifyatuka mbio kuelekea huko”.***

Wangelifanya haraka kuondoka na kwenda kuishi mbali nanyi, kwani wao wanachanganyika nanyi huku wakiona karaha na sio kwa kuwa na mapenzi nanyi, na wanapenda kwamba wasichanganyike na nyinyi, lakini dharura ina kanuni zake. Kwa ajili hii wanaendelea kuwa katika huzuni na majonzi, kwa sababu Uislamu na Waislamu wanaendelea kuwa na nguvu, ushindi na kupanda juu. Kwa hivyo, kila mara Waislamu wanapopata jambo la furaha, wao huhisi vibaya na hiyo ndiyo sababu ya kutokupenda kwao kujishirikisha na Waumini. Kwa mnasaba huu, Allah تعالى Anasema:

لَوْ يَجِدُونَ مَلَجًا أَوْ مَغْرَبًا أَوْ مَدْخَلًا لَوَلَّوْا إِلَيْهِ وَهُمْ يَجْمَحُونَ ﴿٥٨﴾

***“Lau kama wangelipata pa kukimbilia au mapango au pahala pa kuingia basi wangelifyatuka mbio kuelekea huko”.***

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَلْمِزُكَ فِي الصَّدَقَاتِ فَإِنْ أُعْطُوا مِنْهَا رَضُوا وَإِنْ لَمْ يُعْطُوا مِنْهَا إِذَا هُمْ يَسْتَخْطُونَ ﴿٥٩﴾ وَلَوْ أَنَّهُمْ رَضُوا مَا آتَاهُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ سَيُؤْتِينَا

اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَرَسُولُهُ إِنَّا إِلَى اللَّهِ رَاغِبُونَ ﴿٦٠﴾

**58. “Na miongoni mwao wapo wanaokusengenya katika kugawa sadaka. Wanapopewa wao huridhika. Na wasipopewa hukasirika”.**

**59. “Na laiti wao wangeliridhia kile Alichowapa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na wakasema: Mwenyezi Mungu Anatutosheleza, Mwenyezi Mungu Atatupa katika fadhila Yake – na pia Mtume Wake, hakika sisi ni wenye kumtaka Mwenyezi Mungu!”.**

**Usengenyi wa Wanafiki na Tamaa Yao Kuhusu Ugawaji wa Sadaqah.**

Allah تعالى Anasema,

وَمِنْهُمْ

***“Na miongoni mwao”.*** Katika wanafiki.

مَّنْ يَلْمِزُكَ

***“...wapo wanaokusengenya”.*** Kwa kukutafutia kasoro,

فِي

***“...katika”.*** Ugawaji wa,

الْصَّدَقَاتِ

"...*sadaka*". Pindi unapoigawa. Wanahoji uadilifu wako katika hilo ilhali wao ndio wenye kupaswa kuulizwa juu ya jambo hilo. Hawafanyi haya kwa ajili ya kuitetea dini, bali kwa ajili ya nafsi zao. Ndiyo sababu:

أَعْطُوا مِنْهَا

"*Wanapopewa*". Maana yake: Kutoka katika Zakah.

رَضُوا وَإِنْ لَمْ يُعْطُوا مِنْهَا إِذَا هُمْ يَسْتَخْطُونَ

"...*wao huridhika. Na wasipopewa hukasirika*". (9:58)

Maana yake: Huzighadhabikia nafsi zao. Qatadah aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى،

وَمِنْهُمْ مَّنْ يَلْمُكَ فِي الصَّدَقَاتِ

"*Na miongoni mwao wapo wanaokusengeny katika kugawa sadaka*".

Kwamba maana yake ni; "Na miongoni mwao, wapo wanaohoji juu ya uadilifu wako katika kugawa *Sadaqah*". Na tumetajiwa kuwa bedui mmoja ambaye alisilimu karibuni tu, alikuja kwa Mtume ﷺ wakati akiwa katika ugawaji wa dhahabu na fedha, akasema: "Ewe Muhammad! Wallahi, ingawa Allah تعالى Amekuamuru ugawe kwa uadilifu, hukufanya hivyo". Mtume ﷺ akasema:

«وَلَيْكَ فَمَنْ ذَا الَّذِي يَغْدِلُ عَلَيْكَ بَغْدِي؟»

"*Ole wako! Ni nani wa kukufanyia uadilifu baada yangu?*"

Halafu Mtume ﷺ akaendelea kusema:

«اِحْذَرُوا هَذَا وَأَشْبَاهَهُ فَإِنَّ فِي أُمَّتِي أَشْبَاهَ هَذَا يَقْرَأُونَ الْقُرْآنَ لَا يُجَاوِزُ تَرَائِبِهِمْ فَإِذَا خَرَجُوا فَاقْتُلُوهُمْ، ثُمَّ إِذَا خَرَجُوا فَاقْتُلُوهُمْ، ثُمَّ إِذَا خَرَجُوا فَاقْتُلُوهُمْ»

"*Tahadharini dhidi ya mtu huyu na wanaoshabibiana naye, kwani katika ummah wangu kuna watu mfano wa huyu, ambao wanasoma Qur'an, lakini haivuki zaidi ya koo zao. Ikiwa watatoka (dhidi ya Waislamu) basi waueni, kisha wakitoka waueni, kisha wakitoka waueni.*"

Pia, tuliambiwa kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ! مَا أُعْطِيكُمْ شَيْئًا وَلَا أَمْنَعُكُمْوهُ إِنَّمَا أَنَا خَازِنٌ»

*“Naapa kwa Ambaye uhai wangu uko Mkononi Mwake. Sikupeni wala kukunyimeni chochote kwani mimi ni mtunzaji tu”.*<sup>1</sup>

Haya yaliyotajwa na Qatadah yanashabihiana na yaliyoandikwa na mashekhe wawili (Bukhari na Muslim) kutoka kwa Abu Sa'id kuhusu kisa cha Dhul-Khuwaysirah ambaye jina lake ni Khurqus. Pale alipompinga Mtume ﷺ juu ya ugawaji wa ngawira za vita vya Hunayn kwa kumuambia, “Kuwa muadilifu, kwani haujafanya uadilifu!” Mtume ﷺ akasema:

«لَقَدْ جِئْتُ وَخَسِرْتُ إِنْ لَمْ أَكُنْ أَعْدِلُ»

*“Nitakuwa nimekosa na kupata hasara ikiwa sitafanya uadilifu”.*

Kisha Mtume ﷺ alisema baada ya kumuona mtu huyo akiondoka,

«إِنَّهُ يَخْرُجُ مِنْ ضَيْفِيءٍ هَذَا قَوْمٌ يَخْفِرُ أَحَدُكُمْ صَلَاتَهُ مَعَ صَلَاتِهِمْ وَصِيَامَهُ مَعَ صِيَامِهِمْ، يَمْرُقُونَ مِنَ الدِّينِ مُرُوقَ الشَّهْمِ مِنَ الرَّمِيَّةِ، فَأَيْنَمَا لَقِيتُمُوهُمْ فَاقْتُلُوهُمْ؛ فَإِنَّهُمْ شُرٌّ قَتَلَى تَحْتَ أَوْبِيمِ السَّمَاءِ»

*“Miongoni mwa watakaotokana na uzao wa mtu huyu, watakuwepo ambao, mmoja wenu ataidharau Sala yake akilinganisha na yao na Swaumu yake mbele ya Swaumu zao. Wataisaliti Dini kwa wepesi kama vile mshale unaotupwa kwa mnyama (wa kuwindwa). Popote mtakapokutana nao waueni. Kwa hakika! Wao watakufa vifo vibaya zaidi chini ya mfuniko wa mbingu”.*<sup>2</sup>

وَلَوْ أَنَّهُمْ رَضُوا مَا آتَاهُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ سَيُؤْتِينَا اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَرَسُولُهُ إِنَّا إِلَى اللَّهِ رَاغِبُونَ ﴿٥٦﴾

***“Na laiti wao wangeliridhia kile Alichowapa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na wakasema: Mwenyezi Mungu Anatutosheleza,***

<sup>1</sup> At-Tabari 14:302.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 12:302 na Muslim 2:744.



***Mwenyezi Mungu Atatupa katika Fadhila Yake – na pia Mtume Wake, hakika sisi ni wenye kumtaka Mwenyezi Mungu!”***

Aya hii tukufu imebeba adabu kubwa na siri tukufu. Allah تعالى Ameijaalia radhi itokane na kile Alichokitoa Yeye na Mtume ﷺ na kumtegemea Yeye Peke Yake. Amesema,

وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ

***“...na wakasema: Mwenyezi Mungu Anatutosheleza”.***

Na kuwa na matumaini kwa Allah تعالى Peke Yake na Akafanya hizi kuwa ndiyo kanuni za utiifu kwa Mjumbe Wake na ufuasi wa Amri Zake na kuacha Makatazo Yake, kuzisadiki Khabari Zake na kuzifuata Nyayo Zake.

✽ إِنَّمَا الصَّدَقَتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسْكِينِ وَالْعَمِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبِهِمْ وَفِي الرِّقَابِ

وَالْغُرَمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِّنَ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

***60. “Wa kupewa sadaka ni mafakiri na masikini na wanao zitumikia na wa kutiwa nguvu nyoyo zao na katika kukomboa watumwa na wenye Madeni na katika njia ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima”.***

**Ubainifu wa Ugawaji wa Zaka.**

Allah تعالى baada ya kutaja upingaji wa wanafiki na majahili kumpinga Mtume ﷺ na kumkejeli juu ya Ugawaji wake wa Zaka, Allah تعالى Alibainisha kuwa Yeye Ndiye Aliyeigawa na Akaeleza Hukumu Zake, Amelifanya hilo Yeye Mwenyewe, Hakumpa yeyote uwakala wa kulifanya zaidi Yake. Amewapangia mafungu hao waliotajwa. Hapa Amewatanguliza Mafukara mbele ya wengine kwa sababu kama ilivyo mashuhuri, hao ndio wenye haja zaidi kuliko wengine, na kwa sababu kutokana na ufakiri wao na shida yao. Hayo ni kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas, Mujahid, Al-Hasan Al-Basri na Ibn Zayd رضي الله عنهم. Ibn Jariri رحمه الله تعالى na wengine walikhitari rai ya kuwa fakiri ni “Mtu mwenye staha ambaye haombiombi kwa watu, na masikini ni yule ambaye huomba, huwazungukia na huwafuata watu”<sup>1</sup>. Qatadah alisema: “Fakiri ni yule mwenye

<sup>1</sup> At-Tabari 14:305, 306.

ulemavu, na masikini ni mwenye mwili mzima.”<sup>1</sup> Tutabainisha Hadithi za Mtume ﷺ zinazofungamana na anuwai zote nane.

### Mafukara.

Kuhusu Mafukara, Ibn ‘Umar رضي الله عنهما alisema: Mtume ﷺ alieleza;

«لَا تَجْلُ الصَّدَقَةُ لِعَنِي وَلَا لِذِي مِرَّةٍ سِوِي»

*“Zaka si halali kupatiwa matajiri, wala wenye viungo vya mwili vilivyo salama”.*

Ahmad, Abu Dawud na At-Tirmidhi waliikusanya Hadithi hii<sup>2</sup>.

### Masikini.

Ama masikini, Abu Hurayra عنه رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَيْسَ الْمَسْكِينُ بِهَذَا الطَّوَّافِ الَّذِي يَطُوفُ عَلَى النَّاسِ فَرْدُهُ اللَّقْمَةُ وَاللُّقْمَتَانِ،  
وَالتَّمْرَةُ وَالتَّمْرَتَانِ» قالوا: فمن المسكين يا رسول الله؟ قال: «الَّذِي لَا يَجِدُ غِنَى  
يُغْنِيهِ، وَلَا يُفْطِنُ لَهُ فَيُصَدِّقَ عَلَيْهِ، وَلَا يَسْأَلُ النَّاسَ شَيْئًا»

*“Masikini si huyu mzungukaji anayewazungukia watu na kupatiwa tonge moja au tonge mbili na tende moja au mbili sio huyo”*  
Wakauliza: “Basi masikini ni nani, ewe Mtume?” Akajibu: “Ni ambaye hapati cha kumtoshia na hatambuliki hali yake (kama angetambulika) angepatiwa Sadaka, pia haombi kitu kwa watu”.

Mashekhe wawili waliikusanya Hadithi hii<sup>3</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:306.

<sup>2</sup> Ahmad 4:164, Abu Dawud 2:285 na Tufhat Al-Ahwadhi 3:317.

<sup>3</sup> Fat’hul al-Bari 3:399 na Muslim 2:719.

### Wafanyakazi wa *Baitu Zaka*.

Wenye kuzitumikia Zaka ambao ni wakusanyaji na wafatiliaji wake wanastahiki kupata fungu lao kutokana na Zaka. Wala haijuzu (haifai) watokane na Ndugu wa Mtume ﷺ ambao wameharamishwa kupatiwa Sadaka, kutokana na Hadithi iliyoandikwa ndani ya *Sahih* Muslim kutoka kwa Abdul-Muttwalib bin Rabi'ah bin Al-Harith yeye na Al-Fadhl bin Al-'Abbas رضي الله عنهما walikwenda kumuomba Mtume ﷺ awaweke katika orodha ya wahudumu wa Zaka, akawaambia:

«إِنَّ الصَّدَقَةَ لَا تَجُلُّ لِمُحَمَّدٍ وَلَا لِآلِ مُحَمَّدٍ، إِنَّمَا هِيَ أَوْسَاخُ النَّاسِ»

*"Hakika! Zakah si halali kupatiwa Muhammad wala jamaa za Muhammad, kwani hizo ni uchafu wa watu"*<sup>1</sup>.

### Wenye Kuzoeshwa Nyoyo Zao (*Al-Muallafatu Quluubuhum*).

Wenye kuzoeshwa nyoyo zao (*Al-Muallafatu Quluubuhum*) wako wa namna kadha: Wapo wanaopatiwa Zaka ili wasilimu, sawa na Mtume ﷺ alipompatia Swafwaan bin Ummayyah mgao wa Ghanima zilizopatikana Hunayn ambaye alishiriki akiwa angali Mshirikina. Alisema Swafwaan, "Aliendelea kunipa mpaka akawa ni mtu niliyempenda zaidi baada ya kwamba alikuwa ni mwenye kuchukiwa zaidi nami"<sup>2</sup>. Ni sawa na alivyotaarifu Imamu Ahmad kuwa Swafwaan bin Ummayyah alisema: "Mtume ﷺ alinipatia ngawira katika siku ya vita vya Hunayn ilhali akiwa ni mtu niliyekuwa nikimchukia zaidi",<sup>3</sup> Akaendelea kunipa mpaka akawa ndiye mtu niliyempenda zaidi"<sup>4</sup>. Muslim na At-Tirmidhi waliikusanya Hadithi hii pia. Kuna wanaopewa Zaka ili wawe Waislamu wazuri zaidi na kuzifanya nyoyo zao ziwe madhubuti, sawa na ambavyo, Mtume ﷺ alikipatia kikundi cha wakubwa walioachwa huru siku ya kuikomboa Makka *Tulaqaa* pamoja na viongozi wao, kila mmoja ngamia mia moja, katika siku hiyo hiyo ya Hunayn. Kisha Mtume ﷺ alisema,

«إِنِّي لَأَعْطِي الرَّجُلَ وَغَيْرَهُ أَحَبَّ إِلَيَّ مِنْهُ خَشْيَةَ أَنْ يُكَيِّهَ اللَّهُ عَلَى وَجْهِهِ فِي نَارِ جَهَنَّمَ»

*"Mimi humpa mtu (Zaka) ilhali kuna mwingine anapendeza zaidi kwangu, kwa kuchelea kwamba Allah Akamtupa Jahannamu na kuangukia uso wake"*<sup>5</sup>.

<sup>1</sup> Muslim 2:752.

<sup>2</sup> Muslim 4:1806.

<sup>4</sup> Muslim 4:1806 na Tufhat Al-Ahwadhi 3:334.

<sup>3</sup> Ahmad 6:465.

<sup>5</sup> Fat'hul Al-Bari 3:399.

Ndani ya *Sahih* Mbili kuna Hadithi ya Abu Sa'id kuwa 'Ali رضي الله عنه alimpelekea Mtume ﷺ kipande cha dhahabu kikiwa kingali na udongo wake kutoka Yemen, akawagawia watu wanne, Al-Aqra' bin Habis, 'Uyaynah bin Badr, 'Alqamah bin Ulathah na Zayd Al-Khayr. Halafu akasema:

«أَتَأْتُهُمْ»

"Ninazoেশা nyoyo zao"<sup>1</sup>.

Kuna wanaopewa Zaka kwa kutarajiwa kwamba watasilimu watu wa aina yao. Kuna wanaopatiwa Zaka ili wakusanye Zaka kwa Ndugu zao wanaowazunguka, au kwa ajili ya kuwaondoshea madhara Waislamu walio miji ya mbali na ulinzi wa Waislamu. *Allah Aalam*.

### Wenye Kuandikiana na Mabwana Wao Kujikomboa "*Riqaab*"

Kuhusu *Riqaab* imesimuliwa na al-Hasan Al-Basri, Muqatil bin Hayyan, Umar bin Abdul-Aziz, Sa'id bin Jubayr, An-Nakha'i, Az-Zuhri na Ibn Zayd kwamba hao 'Ni watumwa waliowekeana mkataba na bwana wao kwamba walipe fidia ili wapewe uhuru"<sup>2</sup>. Taarifa sawa na hiyo ilisimuliwa na Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه.<sup>3</sup>

Ibn Abbas na Al-Hasan walisema: "Inaruhusiwa kutumia Zaka ili kununua uhuru wa watumwa ili waachiliwe". Na inaonesha kuwa *Riqaab* ina maana ya jumla zaidi kuliko kuwapa mali watumwa ili wanunue uhuru wao, au mtu binafsi wa kumnunua kisha ampe uhuru. Kuna Hadithi nyingi ambazo zimeelezea ubora na thawabu za kuacha huru Mtumwa kwa kila kiungo cha mtumwa aliyeachwa huru, Allah تعالى Naye Huviacha huru viungo vya aliyempa uhuru wake, kiungo kwa kiungo, hata utupu kwa utupu. Hayo ni kwa sababu malipo hulipwa kwa kulinganishwa na kazi liyofanywa.

﴿وَمَا تَجْزُونَ إِلَّا مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

"*Wala hamlipwi ila hayo mliyokuwa mkiyafanya*". (37:39)

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 6:433 na Muslim 2:741.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:317.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:316.

### Fadhila za Kuwapa Uhuru Watumwa.

Katika *Musnad* kuna Hadithi ya Baraa bin 'Azib رضي الله عنه kuwa: Mtu mmoja alikuja na kuuliza: "Ewe Mtume ﷺ! Nijulishe amali itakayonisogeza karibu na Jannah na kuniweka mbali dhidi ya Moto". Akamjibu;

«أُعْتِقِ النَّسَمَةَ وَفُكَّ الرِّقَبَةَ»

"Mpe mtu uhuru wake na ufungue shingo la mtumwa".

Akauliza tena: "Ewe Mtume! Kwani hayo si kitu kimoja?" Akajibu;

«لَا، عِنْتُ النَّسَمَةَ أَنْ تُفْرِدَ بِعَيْتِهَا، وَفُكَّ الرِّقَبَةَ أَنْ تُعَيِّنَ فِي نَمْنِهَا»

"Hapana, mpe mtu uhuru wake, ufanye hivyo wewe mwenyewe, na ufungue shingo (mtumwa), kwa kumsaidia katika thamani ya tatizo lake"<sup>1</sup>.

### Al-Gharimun (Waliozidiwa na Madeni).

Kuhusu *Al-Gharimuna* nao wako wa namna mbalimbali. Miongoni mwao, wapo wanaochukua jukumu au dhamana ya deni kisha linamlazimu kulilipa kwa kutumia mali yake mpaka likaisha na bado deni linaendelea au kaingia deni katika mali yake, au gharama katika kulilipa deni, au wanaoingia katika dhambi kisha wakatubu. Hawa hupatiwa Zaka. Asili ya fungu hili ni Hadithi ya Qabiswah bin Mukhariq Al-Hilaal رضي الله عنه ambaye alisema, "Niliingia katika deni (kwa kufanya usuluhishi baina ya watu), nikamjia Mtume ﷺ kumuuliza juu ya hilo. Akasema:

«أَقِيمْ حَتَّى تَأْتِنَا الصَّدَقَةُ فَتَأْمُرَ لَكَ بِهَا»

"Subiri, mpaka Sadaka itufikie ili tukupatie". Halafu akasema:

«يَا قَيْصُ إِنَّ الْمَسْأَلَةَ لَا تَجُلُّ إِلَّا لِأَحَدٍ ثَلَاثَةً: رَجُلٌ نَحَمَلَ حِمَالَةَ فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ حَتَّى يُصِيبَهَا ثُمَّ يُنْسِكُ، وَرَجُلٌ أَصَابَتْهُ جَائِحَةٌ اجْتَاخَتْ مَالَهُ فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ حَتَّى يُصِيبَ قِرَامًا مِنْ عَيْشٍ - أَوْ قَالَ: سِدَادًا مِنْ عَيْشٍ - وَرَجُلٌ أَصَابَتْهُ فَاقَةٌ حَتَّى يَقُومَ ثَلَاثَةً مِنْ ذَوِي الْحِجَا مِنْ قَرَابَةِ قَوْمِهِ فَيَقُولُونَ: لَقَدْ أَصَابَتْ قُلَانَا فَاقَةٌ فَحَلَّتْ لَهُ الْمَسْأَلَةُ، حَتَّى يُصِيبَ قِرَامًا مِنْ عَيْشٍ - أَوْ قَالَ: سِدَادًا مِنْ عَيْشٍ - فَمَا سِوَاهُنَّ مِنَ الْمَسْأَلَةِ سُحَّتْ بِأَكْلِهَا صَاحِبِهَا سُحْتًا»

<sup>1</sup> Ahmad 4:299.

*“Ewe Qabiswah! Kuomba hakuruhusiwi, isipokuwa kwa ajili ya moja wapo kati ya matatu: Mtu aliyeingia deni katika kusuluhisha ugomvi, anaruhusiwa kuomba mpaka akusanye kiasi kinachotakiwa, kisha aache. Mtu aliyefikwa na majanga yaliyohilikisha mali yake, anaruhusiwa kuomba mpaka apate kiasi cha kujikimu na maisha. Na mtu aliyezidiwa na umasikini, na kufikia hatua ya kusimama jamaa zake Watatu na kusema, “Ama hakika! Fulani amezidiwa na umasikini.” Anaruhusiwa kuomba, mpaka apate cha kujikimu na maisha. Ama uombaji ulio nje ya hali hizi ni kipato kisicho cha halali na mlaji wake anakula moto”. Muslim aliihusiana Hadithi hii.<sup>1</sup>*

Abu Sa'id alisema: Kuna mtu wakati wa uhai wa Mtume ﷺ alipatwa na matatizo ya kuzidiwa na deni kutokana na matunda aliyoyanunua. Mtume ﷺ akasema;

﴿تَصَدَّقُوا عَلَيَّ﴾

*“Mpeni sadaka”.*

Watu wakafanya hivyo, lakini haikutosha kukidhi malipo ya deni, Mtume ﷺ akawaambia wanaomdai mtu huyo:

﴿حُذُّرًا مَّا وَجَدْتُمْ وَلَيْسَ لَكُمْ إِلَّا ذَلِكَ﴾

*“Chukueni mlichokipata, wala hamna kingine zaidi ya hicho”.*

Muslim aliihusiana Hadithi hii<sup>2</sup>.

**Waliotoka katika Njia ya Allah** تعالى.

Wapewa Zaka walio katika kundi hili la njia ya Allah تعالى ni wapiganaji ambao hawapati fidia kupitia katika hazina ya Waislamu.

***Ibnus-Sabil* (Msafiri)**

*Ibnus-Sabil* ni msafiri mwenye kusafiri katika ardhi, na ambaye ameishiwa hana kitu cha kumsaidia safarini kwake. Atapewa Zaka kiasi cha kumtosha mpaka afike katika mji wake hata kama ni mwenye mali katika mji wake. Atapewa kiasi cha kumtosha kwenda na kurudi kwake. Ushahidi wa sheria

<sup>1</sup> Muslim 2:722.

<sup>2</sup> Muslim 3:1161.

hiyo ni Aya na Hadithi ifuatayo. Imamu Abu Dawud, Ibn Majah katika Hadithi ya Ma'amar bin Aslam kutoka kwa Ata bin Yasar, kuwa Abu Sa'd رضي الله عنه alisema: Mtume ﷺ alisema:

«لَا تَجْلُ الصَّدَقَةَ لِنَفْسِي إِلَّا لِحَمْسَةٍ: لِعَامِلٍ عَلَيْهَا، أَوْ رَجُلٍ اشْتَرَاهَا بِمَالِهِ، أَوْ غَارِمٍ، أَوْ غَارٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، أَوْ مَسْكِينٍ تُصَدَّقُ عَلَيْهِ مِنْهَا فَأَهْدَى لِنَفْسِي»

*“Sadaka si halali kwa tajiri isipokuwa kwa ajili ya mambo matano: Aliyepewa kazi ya kukusanya au mtu aliyeinunua kwa mali yake, au aliyezongwa na Madeni au mpiganaji katika njia ya Allah au masikini aliyepatiwa sadaka, kisha akampa tajiri kwa kumzawadia”.*<sup>1</sup>

Kauli ya Allah تعالى:

فَرِيضَةٌ مِّنَ اللَّهِ

**“Huu ni wajibu uliofaridhiwa na Mwenyezi Mungu.”** Kwa maana: Hii ni hukumu iliyokadiriwa kwa Makadirio ya Allah تعالى na ni fungu Lake Aliloligawanya.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua”.** Maana yake: Yeye ni Mwenye Kuyajua mambo yote kwa nje yake na ndani yake na ni Mwenye Kujua maslahi ya waja Wake”.

حَكِيمٌ

**“Mwenye Hikima”.** Katika Kauli Zake na Mambo Ayafanyayo na Sheria Anazozipanga na Hukumu Anazozitoa. Hapana mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye, wala hapana Mola mwingine asiyekuwa Yeye.

وَمِنْهُمْ الَّذِينَ يُؤَدُّونَ النَّبِيَّ وَيَقُولُونَ هُوَ أُذُنٌ قُلْ أُذُنٌ خَيْرٌ لَّكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيُؤْمِنُ  
لِلْمُؤْمِنِينَ وَرَحْمَةً لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَالَّذِينَ يُؤَدُّونَ رَسُولَ اللَّهِ هُمْ عَدَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦١﴾

**61. “Na miongoni mwao wapo wanaomuudhi Nabii na kusema: Yeye ni sikio tu. Sema: Basi ni sikio la kheri kwenu. Anamuamini Mwenyezi Mungu, na ana imani na Waumini, naye ni rehema kwa wanaoamini miongoni mwenu. Na wanaomuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu watapata adhabu chungu”.**

<sup>1</sup> Abu Dawud 2:288 na Ibn Majah 1:590.

**Miongoni mwa Alama za Wanafiki ni Kumuudhi Mtume ﷺ.**

Allah تعالى Anasema: Miongoni mwa wanafiki kuna watu wanaomfanyia udhia Mtume ﷺ katika kauli zao. Na wanasema:

هُوَ أَذُنٌ

**“Yeye ni sikio tu”.**

Kwa maana: Yeyote mwenye kumuambia jambo la kutuhusu, yeye humsadiki. Tukimuendea na kumuapia nasi pia hutusadiki. Masimulizi yenye maana sawa na haya yalitolewa na Ibn ‘Abbas, Mujahid na Qatadah<sup>1</sup> رضي الله عنهم.

Allah تعالى Anasema,

قُلْ أَذُنٌ خَيْرٌ لَّكُمْ

**“Sema: Basi ni sikio la kheri kwenu”.**

Maana yake: Hilo ni sikio jema ambalo humtambua mkweli na muongo.

يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِينَ

**“Anamuamini Mwenyezi Mungu, na ana imani na Waumini”.**

Kwamba anawasadiki walioamini

وَرَحْمَةً لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ

**“...naye ni rehema kwa wanaoamini miongoni mwenu”.**

Ni ushahidi dhidi ya makafiri. Na kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

وَالَّذِينَ يُؤْذُونَ رَسُولَ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

**“Na wanao muudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu watapata adhabu chungu”.**

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 14:226.



تَخْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ لِيُرْضُوكُمْ وَاللَّهُ وَرَسُولُهُ أَحَقُّ أَنْ يُرْضُوهُ إِنْ كَانُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾ أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّهُ مَنِ مُخَادِدِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ فَأَنْ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا ذَلِكَ الْخِزْيُ الْعَظِيمُ ﴿٦٣﴾ تَحَدَّرُ الْمُنَافِقُونَ أَنْ تَنْزَلَ عَلَيْهِمْ سُورَةٌ تُنَبِّئُهُمْ بِمَا فِي قُلُوبِهِمْ قُلِ اسْتَزِرُوا وَإِنَّ اللَّهَ الْخَبِيرُ لِيََقُولُ بِكُمْ إِنْ مَا كُنْتُمْ تُخَذِرُونَ ﴿٦٤﴾ وَإِنْ سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ قُلْ أَبِاللَّهِ وَآيَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ ﴿٦٥﴾ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ إِنْ نَعَفَ عَنْ طَآئِفَةٍ مِنْكُمْ تُعَذِّبْ طَآئِفَةً أُخْرَى إِنْ كَانُوا جَمِيعِينَ ﴿٦٦﴾ أَلَمْ تَنْفِقُوا وَالْمُنَافِقُونَ أَلَمْ يَنْفِقُوا عَنْ بَعْضِهِمْ مِنْ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمَعْرُوفِ وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيَهُمْ نَسُوا اللَّهَ فَنَسِيَهُمْ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٦٧﴾ وَعَدَّ اللَّهُ الْمُنَافِقِينَ وَالْمُنَافِقَاتِ وَالْكُفَّارَ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا هِيَ حَسْبُهُمْ وَلَعْنَةُ اللَّهِ وَاللَّهُ الْعَذَابُ مُقِيمٌ ﴿٦٨﴾

تَخْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ لِيُرْضُوكُمْ وَاللَّهُ وَرَسُولُهُ أَحَقُّ أَنْ يُرْضُوهُ إِنْ كَانُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٦٢﴾ أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّهُ مَنِ مُخَادِدِ اللَّهِ وَرَسُولِهِ فَأَنْ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا ذَلِكَ الْخِزْيُ الْعَظِيمُ ﴿٦٣﴾

62. “Wanakuapieni Mwenyezi Mungu ili kukuridhisheni nyinyi, hali ya kuwa wanaostahiki zaidi kuridhishwa ni Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, lau kama wao ni Waumini.”

63. “Je, hawajui ya kwamba anayeshindana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, basi huyo atapata Moto wa Jahannamu adumu humo? Hiyo ndiyo hizaya kubwa.”

**Katika Alama za Wanafiki ni Kujaribu Kuwahadaa Watu kwa Viapo vya Uongo.**

Qatadah alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

تَخْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ لِيُرْضُوكُمْ

“Wanakuapieni Mwenyezi Mungu ili kukuridhisheni nyinyi”.

Kwa kusema, “Tuliambiwa kwamba Mnafiki mmoja alisema, “Wallahi! Hawa ni wakuu wetu na viongozi wetu. Na kama anayoyasema Muhammad ﷺ ni ya

kweli, basi hao ni wabaya kuliko punda". Muislamu mmoja akayasikia maneno hayo na akamjibu. "Wallahi! Anayoyasema Muhammad ﷺ ni ya kweli kabisa, na wewe ni muovu zaidi kuliko punda". Muislamu akaenda kwa Mtume ﷺ, na kumuelezea. Mtume ﷺ akatuma kwamba yule Mnafiki aitwe, na akamuuliza:

«مَا حَمَلَكَ عَلَى الَّذِي قُلْتَ؟»

*"Ni nini kilichokupelekea kusema hayo?"*

Mtu huyo akaanza kujilaani na kuapa kwa Jina la Allah تعالى kwamba yeye hakuyasema hayo. Muislamu naye akawa anasema: "Ewe Allah تعالى ! Mbainishe mkweli na umdhihirishe muongo". Allah تعالى Akaiteremsha Aya hii.<sup>1</sup>

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّهُ مَنِ مُحَمَّدٍ اللَّهُ وَرَسُولُهُ

***"Je, hawajui ya kwamba anayeshindana na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake".***

Kwa maana: Je hawajapata uhakika na wakajua kwamba mwenye kuvuka mipaka ya Allah تعالى, kwa kwenda kinyume naye na kumpiga vita, kwa hivyo wakawa upande mmoja ilhali Allah تعالى na Mtume ﷺ wako upande mwingine,

فَأَنَّ لَهُ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدًا فِيهَا

***"...basi huyo atapata Moto wa Jahannamu adumu humo?"***

Akiwa katika udhalili na Kuadhibiwa,

ذَلِكَ الْخِزْيُ الْعَظِيمُ

***"Hiyo ndiyo hizaya kubwa."***

Maana yake: Huo ndio udhalili mkubwa na uovu mkubwa.

يَحْذَرُ الْمُتَنَفِقُونَ أَنْ تَنْزَلَ عَلَيْهِمْ سُورَةٌ تُنَبِّئُهُمْ بِمَا فِي قُلُوبِهِمْ ۚ قُلِ اسْتَزِرُوا إِنَّا اللَّهُ مُخْرِجٌ مَا تَحْذَرُونَ ﴿٦٥﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 14:329

**64. “Wanaafiki wanaogopa isije teremshwa Surah itokayofichua yaliyomo katika nyoyo zao. Sema: Fanyeni mzaha! Hakika Mwenyezi Mungu Atayatoa nje hayo mnayoyaogopa”.**

**Katika Alama za Wanafiki ni Kuogopa Siri Zao Kudhihirika.**

Mujahid alisema; Wanafiki huambizana jambo, halafu husema, “Tunatamani Allah تعالى Asiidhihirishe siri yetu hii”<sup>1</sup>. Aya hii inashabihiana na Kauli Yake تعالى nyingine Aliyosema:

وَإِذَا جَاءُوكَ حَيَّوكَ بِمَا لَمْ يُحَيِّكَ بِهِ اللَّهُ وَيَقُولُونَ فِي أَنْفُسِهِمْ لَوْلَا يُعَذِّبُنَا اللَّهُ بِمَا نَقُولُ  
حَسِبُّهُمْ جَهَنَّمَ يَصْلَوْنَهَا فَيَنْسَأَلُ الْمَصِيرُ

**“Na wakikujia hukuamkia sivyo anavyokuamkia Mwenyezi Mungu. Na husema katika nafsi zao: Mbona Mwenyezi Mungu Hatuadhibu kwa haya tuyasemayo? Basi Jahannamu itawatosha; wataingia humo! Na hayo ndiyo marejeo maovu yaliyoje!” (58:8)**

Katika Aya hii, Allah تعالى Amesema:

قُلِ اسْتَهِزُّوْا إِنَّا لِلَّهِ مُخْرِجٌ مَّا تَحْذَرُونَ

**“Sema: Fanyeni mzaha! Hakika Mwenyezi Mungu Atayatoa nje hayo mnayoyaogopa”.**

Kwa maana: Allah تعالى Atamshushia Mtume ﷺ yale ambayo yatakufedhehesheni na atamfunulia jambo lenu. Sawa na Kauli ya Allah تعالى nyingine aliyoisema;

أَمْ حَسِبَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ أَنْ لَنْ نُخْرِجَ اللَّهُ أَضْعَانَهُمْ ﴿٢٩﴾

**“Je! Wenye maradhi nyoyoni mwao wanadhani kwamba Mwenyezi Mungu Hatazidhihirisha chuki zao?” (47:29)**

Inaendelea mpaka,

وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ ؕ

**“...lakini bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemo wao”. (47:30)**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:331.

Kwa mujibu wa Qatadah. Ndiyo maana Surah hii huitwa *Al-Faadhwihah* (yenye kufedhehesha), kwa sababu iliwafeedhehesha wanafiki.<sup>1</sup>

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ۗ قُلْ أِبَاهُ اللَّهِ وَءَايَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ  
تَسْتَهْزِئُونَ ﴿٦٥﴾ لَا تَعْتَذِرُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ ۗ إِنَّ نَعْفَ عَنْ طَائِفَةٍ مِّنْكُمْ  
نُعَذِّبُ طَائِفَةً بِأَنَّهُمْ كَانُوا مُجْرِمِينَ ﴿٦٦﴾

**65. "Na ukiwauliza, wanasema: Sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu. Sema: Mlikuwa mkimfanyia masikhara Mwenyezi Mungu na Ishara Zake na Mtume Wake?"**

**66. "Msitoe udhuru; mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu! Tukilisamehe kundi moja kati yenu, Tutaliadhibu kundi jingine kwa kuwa wao ni wakosefu".**

**Katika Alama za Wanafiki ni Kutoa Nyudhuru kwa Batili Walizofanya.**

'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما alisema: "Katika vita vya Tabuk, mtu mmoja ambaye alikuwa amekaa katika mkusanyiko wa watu alisema, "Sijawahi kuwaona wasomaji Qur'an kama wa kwetu, matumbo yao yana njaa kweli, wenye ndimi zenye kuongopa sana na waoga mno vitani!" Mtu mmoja Msikitini akasema: "Umedanganya, tena wewe ni mnafki nitamuambia Mtume ﷺ. Kauli hii ikafikishwa kwa Mtume ﷺ, na hapo ikashuka Qur'an juu ya jambo hilo. 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما akasema: "Mtu huyo nilimuona katika siku za mbele akiwa ameshikilia nyuma ya ngamia wa Mtume ﷺ huku mawe yakimuangukia, naye akinena, "Ewe Mtume ﷺ! Tulikuwa katika mazungumzo ya porojo na mzaha tu". Na Mtume ﷺ akasema:

أَبَا اللَّهِ وَءَايَاتِهِ وَرَسُولِهِ كُنْتُمْ تَسْتَهْزِئُونَ

**"Mlikuwa mkimfanyia masikhara Mwenyezi Mungu na Ishara Zake na Mtume Wake?" (9:65)<sup>2</sup>**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:332.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:333.

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema: “Kikundi cha wanafiki, akiwemo Wadi’ah bin Thabit, Ndugu wa Banu Umayyah bin Zayd bin ‘Amri bin ‘Awf na mtu mmoja kutoka kwa Ashja’ aliyekuwa na ushirika na Banu Salima, ambaye jina lake alikuwa akiitwa Mukhashin bin Humayyar, walikuwa wakimuashiria Mtume ﷺ akielekea Tabuk. Wakaambizana: “Mnadhani kupigana na (Banu Asfar) mashujaa wa wana wa manjano (Warumi) ni kama Waarabu wanapopigana wenyewe kwa wenyewe?” Wanayasema hayo kuwaogopesha Waislamu. Mukhashin bin Humayyar akasema: Wallahi! Ningelipenda (yaani ni bora) tuhukumiwe kwa kila mmoja katika sisi acharazwe fimbo mia moja, kutokana na hayo mnayoyasema kwani kwa lugha hiyo kuna uwezekano mkubwa wa kuteremka Qur’an ikitaja ubaya wetu”.

Mtume ﷺ akasema kumuambia Ammar bin Yasir رضي الله عنهما; “Waendee watu hao (wanafiki) kwani wameshateketea. Uwaulize juu ya waliyoyasema. Wakikataa, waambie, “Naam mmesema kadhaa wa kadhaa”. ‘Ammar رضي الله عنه akawaenda akawaambia kama alivyotumwa, wakaja kwa Mtume ﷺ wakimuomba udhuru. Wadiy’ah bin Thabit akanena huku Mtume ﷺ akiwa juu ya mnyama wake aliyesimama. Akawa anazungumza huku akiwa ameshika bega la ngamia wa Mtume ﷺ, “Ewe Mtume! Tulikuwa tunafanya utani wa mzaha tu”. Mukhashin bin Humayyar akasema: “Ewe Mtume ﷺ! Jina langu na la baba yangu linikalie”. Matokeo yake ni kuwa mtu aliyesamehewa katika Aya hii ni Mukhashin bin Humayyar, akajiita ‘Abdur-Rahman na akamuomba Allah تعالى kwamba afe shahidi na asijulikane mahali pa kufia kwake. Akauawa huko Al-Yamaamah, wala hakupatikana athari yake.

Kauli ya Allah تعالى;

لَا تَعْتَدُوا قَدْ كَفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

**“Msitoe udhuru; mmekwishakufuru baada ya kuamini kwenu!”**

Kwa maana: Kwa kauli hii mliyoifanyia istihizai,

إِنْ نَعَفُ عَنْ طَآئِفَةٍ مِّنْكُمْ نُعَذِّبْ طَآئِفَةً

**“Tukilisamehe kundi moja kati yenu, Tutaliadhibu kundi jingine”.**

Maana yake: Hamtasamehewa nyinyi nyote, hapana budi baadhi yenu waadhibiwe.

بِأَنَّهُمْ كَانُوا مُجْرِمِينَ

“...kwa kuwa wao ni wakosefu”.

Kwa sababu ya kauli yao hii mbaya iliyowaingiza katika makosa mabaya.

الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَاتُ بَعْضُهُمْ مِّنْ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ  
الْمَعْرُوفِ وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيَهُمْ نَسُوا اللَّهَ فَنَسِيَهُمْ إِنَّ الْمُنْفِقِينَ هُمُ الْفَاسِقُونَ  
﴿٧٧﴾ وَعَدَّ اللَّهُ الْمُنْفِقِينَ وَالْمُنْفِقَاتِ وَالْكُفَّارَ نَارَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا هِيَ حَسْبُهُمْ  
﴿٧٨﴾ وَلَعَنَهُمُ اللَّهُ وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّقِيمٌ ﴿٧٩﴾

67. “Wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, wote ni hali moja. Huamrisha maovu na huyakataza mema, na huifumba mikono yao. Wamemsahau Mwenyezi Mungu, basi na Yeye pia Amewasahau. Hakika wanafiki ndio wapotofu”.

68. “Mwenyezi Mungu Amewaahidi wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na makafiri Moto wa Jahannamu kudumu humo. Hayo yanawatosha, na Mwenyezi Mungu Amewalaani; nao wana adhabu milele”.

### Baadhi ya Sifa Nyingine za Wanafiki.

Allah تعالى Anawakaripia wanafiki ambao wako kinyume na sifa za waumini, baada ya kuwa sifa za waumini ni kuamrisha mema na kukataza maovu. Lakini wanafiki;

يَأْمُرُونَ بِالْمُنْكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمَعْرُوفِ وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيَهُمْ

“Huamrisha maovu na huyakataza mema, na huifumba mikono yao”.

Wanaifumba dhidi ya kutoa katika njia ya Allah تعالى.

نَسُوا اللَّهَ

“Wamemsahau Mwenyezi Mungu”. Maana yake: Hawakumbuki kumdhukuru Allah تعالى.

فَنَسِيئِهِمْ

**“...basi na Yeye pia Amewasahau”.**

Amewafanyia kama walivyomfanyia kwa kuwatelekeza kama aliyewasahau. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَقِيلَ الْيَوْمَ نَنْسِكُمْ كَمَا نَسِيتُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَذَا

**“Na itasemwa: Leo Tunakusahauni kama nyinyi mlivyosahau mkutano wa siku yenu hii.”**

إِنَّ الْمُنْفِقِينَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

**“Hakika wanafiki ndio wapotofu”.** Maana yake: Wenye kutoka katika njia ya haki na kuingia katika njia ya upotevu. Kauli ya Allah تعالى Anasema;

وَعَدَ اللَّهُ الْمُنْفِقِينَ وَالْمُنْفِقَاتِ وَالْكُفَّارَ نَارَ جَهَنَّمَ

**“Mwenyezi Mungu Amewaahidi wanafiki wanaume na wanafiki wanawake na makafiri Moto wa Jahannamu”.**

Kutokana na tendo lao hilo lilotajwa katika Aya hizo.

خَالِدِينَ فِيهَا

**“...kudumu humo”.** Na watakaa humo milele. Wao na makafiri.

هِيَ حَسْبُهُمْ

**“Hayo yanawatosha”.** Kuwa ni adhabu yao. Kwa maana: Ni tosha katika adhabu.

وَلَعَنَهُمُ اللَّهُ

**“...na Mwenyezi Mungu Amewalaani”.**

Kwa Kuwafukuza na Kuwaweka mbali na Rehma Zake.

وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِمٌّ

**“...nao wana adhabu milele”.**

\* \* \*

كَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ كَانُوا أَشَدَّ مِنْكُمْ قُوَّةً وَأَكْثَرَ أَمْوَالًا  
 وَأَوْلَادًا فَاسْتَمْتَعُوا بِخَلْقِهِمْ فَاسْتَمْتَعْتُمْ بِخَلْقِكُمْ كَمَا  
 اسْتَمْتَعَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ بِخَلْقِهِمْ وَخُضْتُمْ كَالَّذِي  
 خَاضُوا<sup>٤</sup> أُولَئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ<sup>٥</sup>  
 وَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٦٩﴾ أَلَمْ يَأْتِهِمْ نَبَأُ الَّذِينَ مِنْ  
 قَبْلِهِمْ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ وَقَوْمِ إِبْرَاهِيمَ وَأَصْحَابِ  
 مَدْيَنَ وَالْمُؤْتَفِكَةَ<sup>٦</sup> أَتَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ<sup>٧</sup> فَمَا  
 كَانُوا اللَّهُ لِيُظْلَمَهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٧٠﴾  
 وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ  
 بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ  
 وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ<sup>٨</sup> أُولَئِكَ  
 سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ<sup>٩</sup> إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾ وَعَدَّ اللَّهُ  
 الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ  
 خَالِدِينَ فِيهَا وَمَسْكَنٌ طَيِّبَةٌ فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ<sup>١٠</sup> وَرِضْوَانٌ  
 مِنَ اللَّهِ أَكْبَرُ ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٧٢﴾

كَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ كَانُوا أَشَدَّ  
 مِنْكُمْ قُوَّةً وَأَكْثَرَ أَمْوَالًا وَأَوْلَادًا  
 فَاسْتَمْتَعُوا بِخَلْقِهِمْ فَاسْتَمْتَعْتُمْ  
 بِخَلْقِكُمْ كَمَا اسْتَمْتَعَ الَّذِينَ  
 مِنْ قَبْلِكُمْ بِخَلْقِهِمْ وَخُضْتُمْ كَالَّذِي  
 خَاضُوا<sup>٤</sup> أُولَئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَالُهُمْ  
 فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ<sup>٥</sup> وَأُولَئِكَ هُمُ  
 الْخَاسِرُونَ ﴿٦٩﴾

69. "Ni kama wale walio kuwa kabla yenu. Walikuwa wana nguvu na mali na watoto zaidi kuliko nyinyi. Basi walistarehea fungu lao, na nyinyi mnastarehea fungu lenu, kama walivyo-starehe kwa fungu lao wale waliokuwa kabla yenu. Na nyinyi mkazama katika maovu kama wao walivyo zama. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika

**katika dunia na Akhera; hao ndio waliokhasiri".**

Allah تعالى Anasema; hao wamepata adhabu ya Allah تعالى duniani na Akhera, sawa na ilivyowapata wa kabla yao.

Allah تعالى Anasema;

بِخَلْقِهِمْ

"...fungu lao". Maana yake: Fungu hapa ni dini yao, hiyo ni kwa mujibu wa Al-



Hasan Al-Basri <sup>1</sup> رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى. Kauli ya Allah تَعَالَى:

وَحُضُّمُ كَالَّذِي حَاضُوا

**“...na nyinyi mnastarehea fungu lenu, kama walivyostarehe kwa fungu lao”.**

Katika uongo na upotevu.

أَوْلَيْكَ حَبِطَتْ أَعْمَلُهُمْ

**“Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika”.** Amali zao zimebatilika, hawatapata malipo kwa kazi zao njema, kwani zimeharibika.

فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَأُولَئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ

**“...katika dunia na Akhera; hao ndio waliokhasiri”.**

Kwa sababu hawakupata thawabu za kazi zao. Ibn ‘Abbas رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا alisema; “Ni kufanana kulioje baina ya jana na leo katika Ayah hii:

كَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ

**“...kama waliokuwa kabla yenu”.** Hao ni Wana wa Israil ambao tumeshabihishwa (tumefananishwa) nao. Mtume ﷺ alisema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَتَتَّبِعُنَّهُمْ حَتَّى لَوْ دَخَلَ الرَّجُلُ مِنْهُمْ جُحْرَ ضَبٍّ لَدَخَلْتُمُوهُ»

**“Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Mtawaiga mpaka lau kama mmoja wao ataingia katika tundu la mburukenge, nanyi mtaingia vile vile”.**<sup>2</sup>

Abu Hurayra رَضِيَ اللهُ عَنْهُ alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَتَتَّبِعُنَّ سَنَنَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ سِيْرًا بِشِيْرٍ وَدِرَاعًا بِدِرَاعٍ، وَبَاعًا بِبَاعٍ حَتَّى لَوْ دَخَلُوا جُحْرَ ضَبٍّ لَدَخَلْتُمُوهُ، قَالُوا: وَمَنْ هُمْ يَا رَسُولَ اللهِ، أَهْلُ الْكِتَابِ؟ قَالَ: «فَمَنْ؟»

**“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake! Mtaiga mwenendo wa waliokuwa kabla yenu, hatua kwa hatua, dhira kwa dhira, kiganja kwa kiganja, mpaka kiasi kwamba, lau kama mmoja wao ataingia katika tundu la mburukenge, nanyi mtaingia**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:343.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:342.

*vile vile.* 'Wakamuuliza: "Ni nani, ewe Mtume? Ni watu wa Kitabu?"<sup>1</sup>  
Akawajibu: "Nani tena mwingine"<sup>1</sup>

Hadithi hii ina ushahidi ndani ya *Sahih*.

أَلَمْ يَأْتِهِمْ نَبَأُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ قَوْمِ نُوحٍ وَعَادٍ وَثَمُودَ وَقَوْمِ إِبْرَاهِيمَ وَأَصْحَابِ مَدْيَنَ  
وَالْمُؤْتَفِكَةَ ۗ أَتَتْهُمْ رُسُلُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ ۖ فَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ وَلَكِنْ كَانُوا أَنْفُسَهُمْ

يَظْلِمُونَ ﴿٧٠﴾

**70. "Je, hazikuwafikia khabari za waliokuwa kabla yao – kaumu ya Nuhu, na A'aad, na Thamud, na kaumu ya Ibrahim, na watu wa Madyana, na miji iliyopinduliwa chini juu? Mitume wao waliwafikia kwa hoja zilizo wazi. Basi Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuwadhulumu, walakini wao walikuwa wakijidhulumu wenyewe".**

**Nasaha kwa Wanafiki Wachukue Mazingatio Kutoka kwa Waliopita Kabla Yao.**

Allah تعالیٰ Anawawaidhi hawa wanafiki wakadhibishao Mitume,

أَلَمْ يَأْتِهِمْ نَبَأُ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ

**"Je, hazikuwafikia khabari za waliokuwa kabla yao".** Kwa maana: "Je hamkupashwa khabari za umma zilizokuwepo kabla yenu ambazo ziliwakadhibisha Mitume.

قَوْمِ نُوحٍ

**"...kaumu ya Nuhu".** Na gharika iliyowafikia na kuwaenea watu wote wa ardhini, isipokuwa waliomuamini mja Wake na Mtume Wake, Nuh عليه السلام.

وَعَادٍ

**"...na A'aad".** Namna walivyohilikishwa kwa upepo tasa usio na kheri yoyote, pindi walipomkanusha Nabii Hud عليه السلام.

وَتَمُودَ

**"...na Thamud".** Jinsi walivyopatwa na ukelele kwa kumkadhibisha Saleh عليه السلام na wakamchinja ngamia.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:342.

وَقَوْمِ إِبْرَاهِيمَ

**“...na kaumu ya Ibrahim”.** Allah تعالى Alivyomnusu na Akampa nguvu kwa kumpa miujiza ya dhahiri juu yao na Akamuangamiza Mfalme wao, Numrudh bin Kan'aan bin Kush Al-Kan'aani, Allah تعالى Amlaani.

وَأَصْحَابِ مَدْيَنَ

**“...na watu wa Madyana”.** Ambao ni kaumu ya Shu'ayb عليه السلام na namna walivyokutwa na zilzala na adhabu ya siku ya kivuli.

وَالْمُرْتَفِكَةَ

**“...na miji iliyopinduliwa chini juu?”** Ya kaumu ya Lut عليه السلام ambao walikuwa wakiishi katika miji kadhaa kama Allah تعالى Alivyosema katika Ayah nyingine.

وَالْمُرْتَفِكَةَ أَهْوَى

**“...na miji iliyopinduliwa”.** (53:53)

Kwa maana: Umma uliopinduliwa. Ilisemwa pia kuwa ni miji yao, nayo ni Sadum (Sodoma). Kwa ujumla, Allah تعالى Aliwaangamiza wote kwa sababu ya kumkana Nabii wao, Lut عليه السلام na kufanya ovu kubwa ambalo halikuwahi kutendwa na yeyote katika walimwengu waliowatangulia.

أَتَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ

**“Mitume wao waliwafikia kwa hoja zilizo wazi”.**

Wote hao Mitume wao waliwaendea kwa ushahidi, hoja na dalili dhahiri ili waamini.

فَمَا كَانَ اللَّهُ لِيَظْلِمَهُمْ

**“Basi Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuwadhulumu”.**

Pale Alipowahilikisha kwa sababu Aliweka ushahidi kwa Kuwapelekea Mitume na Kuondosha mashaka”.

وَلَيْكِن كَانُوا أَنْفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ

**“...walakini wao walikuwa wakijidhulumu wenyewe”.** Kwa kuwakadhibisha Mitume na kuukataa ukweli hivyo yakawapata yaliyowapata na wakawa katika adhabu na kuangamia.

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ  
وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ أُولَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ  
إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿٧١﴾

**71. "Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hao Mwenyezi Mungu Atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima".**

### Sifa Njema za Waumini wa Kweli.

Baada ya Allah تعالى Kutaja sifa mbaya za wanafiki Aliunganisha kwa Kutaja sifa njema za Waumini. Aliposema;

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ

**"Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi".**

Kwamba wanasaidiana na kufaana. Kama ilivyo katika Hadithi *Sahih*. Mtume ﷺ alisema,

«الْمُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِ كَالْبُنْيَانِ يَشُدُّ بَعْضُهُ بَعْضًا»

**"Muumini kwa muumini mwenzake ni sawa na jengo, pande zake zinafungamana".**

Mtume ﷺ akavisokota vidole vyake viwili<sup>1</sup>. Ndani ya *Sahih*, pia kumeandikwa Hadithi isemayo;

«مَثَلُ الْمُؤْمِنِينَ فِي تَوَادُّهِمْ وَتَرَاحِمِهِمْ كَمَثَلِ الْجَسَدِ الْوَاحِدِ، إِذَا اشْتَكَى مِنْهُ عُضْوٌ  
تَدَاعَى لَهُ سَائِرُ الْجَسَدِ بِالْحَمَى وَالسَّهْرِ»

**"Mfano wa Waumini katika kupendana na kuhurumiana kwao ni kama mwili mmoja, kiungo chake kimoja kikiugua, mwili mzima hushiriki maumivu kwa kupata homa na kukesha"<sup>2</sup>.**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 10:464,

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 10:452.

Kauli ya Allah تعالى: يَا مُرُوبَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ

**“Huamrisha mema na hukataza maovu”.** Na Kauli nyingine ya Allah تعالى isemayo;

وَلْتَكُنْ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ

**“Na uwe kutokana na nyinyi umma unaolingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu”.** (3:104)

Kauli ya Allah تعالى: وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ

**“...na hushika Sala, na hutoa Zaka”.** Maana yake: Wanamtii Allah تعالى na wanafanya ihsani kwa viumbe Wake.

وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

**“...na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake”.** Wanamtii kwa kutekeleza Aliyoyaamuru, na kuyaacha Aliyoyakataza.

أُولَئِكَ سَيَرْحَمُهُمُ اللَّهُ

**“Hao Mwenyezi Mungu Atawarehemu”.**

Kwa maana: Allah تعالى Atawarehemu watakaokuwa na sifa hizi.

إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ

**“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye Nguvu”.** Kwamba Anampa nguvu mwenye kumtii, kwani ushindi ni wa Allah تعالى, Mtume ﷺ na waumini.

حَكِيمٌ

**“Mwenye Hikima”.** Katika kuzigawa sifa hizi kwa Waumini, na kwa wakati huo huo kuwapa sifa mbaya wanafiki. Kwa hakika, Allah تعالى ni Mwenye Hikima katika yote Ayafanyayo na Ayasemayo, Sifa Njema na Utukufu ni Wake.

وَعَدَ اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَمَسْكِنٍ

طَيِّبَةٍ فِي جَنَّاتٍ عَدْنٍ وَرِضْوَانٍ مِنَ اللَّهِ أَكْبَرُ ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٧٢﴾

**72. “Mwenyezi Mungu Amewaahidi Waumini wanaume na Waumini wanawake Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu**

**humo. Na makazi mema katika Bustani za kudumu, na Radhi za Mwenyezi Mungu ndio kubwa kuliko yote. Huko ndiko Kufuzu kukubwa”.**

**Habari Njema kwa Waumini ya Kupata Neema za Kudumu Milele.**

Allah تعالى Anaeleza kuhusu kheri na neema ya kudumu Aliyowaandalia Waumini wa kiume na wa kike, kwa Kusema;

جَنَّتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا

**“Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo.”**Kwa maana: Watakaa humo milele.

وَمَسْكَنٍ طَيِّبَةٍ

**“...Na makazi mema”.** Yaliyojengwa vizuri katika mazingira mazuri. Ndani ya Sahih Mbili kumeandikwa Hadithi ya Abu Musa ‘Abdullah bin Qays Al-Ash-ari رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alisema:

«جَنَّاتٍ مِنْ ذَهَبٍ آيْتُهُمَا وَمَا فِيهِمَا، وَجَنَّاتٍ مِنْ فِضَّةٍ آيْتُهُمَا وَمَا فِيهِمَا، وَمَا بَيْنَ الْقَوْمِ وَبَيْنَ أَنْ يَنْظُرُوا إِلَى رَبِّهِمْ إِلَّا رِذَاءَ الْكِبْرِيَاءِ عَلَى وَجْهِهِ فِي جَنَّةٍ عَذِينَ»

*“Pepo mbili ambamo kuna vyombo na vitu vingine vya dhahabu, na pepo mbili ambamo kuna vyombo na vitu vingine vya fedha. Hakuna kinachowazuia watu wake wasimuone Allah Mola wao Mlezi isipokuwa pazia ya kiburi iliyoko usoni Kwake katika pepo ya Adin”<sup>1</sup>.*

Na kutokana na hilo alisema kuwa Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ لِلْمُؤْمِنِينَ فِي الْجَنَّةِ لَخَيْمَةً مِنَ لُؤْلُؤَةٍ وَاجِدَةٍ مُجَوَّفَةٍ، طُولُهَا سِتُونَ مِيلًا فِي السَّمَاءِ! لِلْمُؤْمِنِينَ فِيهَا أَهْلُونَ يَطُوفُ عَلَيْهِمْ لَا يَرَى بَعْضُهُمْ بَعْضًا»

*“Kwa hakika! Katika pepo kuna hema moja la lulu kwa ajili ya Muumini, lenye uwazi. Limeinuka juu kwa umbali wa maili sitini. Muumini atakuwa na familia ya watu wengi ambao atawazuru wote, na wao watakuwa hawaonani”.*

Sahih Mbili ziliikusanya Hadithi hii<sup>2</sup>. Pia ndani ya Sahih Mbili kuna Hadithi nyingine, kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema:

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:491 na Muslim 1:163.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 8:491 na Muslim 4:2182.

«مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَأَقَامَ الصَّلَاةَ وَرَضِمَ رَمَضَانَ، فَإِنَّ حَقًّا عَلَى اللَّهِ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ هَاجِرًا فِي سَبِيلِ اللَّهِ، أَوْ [جَلَسًا] فِي أَرْضِهِ الَّتِي وُلِدَ فِيهَا» قالوا: يا رسول الله أفلا نخبر الناس؟ قال: «إِنَّ فِي الْجَنَّةِ مِائَةَ دَرَجَةٍ أَعَدَّهَا اللَّهُ لِلْمُجَاهِدِينَ فِي سَبِيلِهِ بَيْنَ كُلِّ دَرَجَتَيْنِ كَمَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، فَإِذَا سَأَلْتُمُ اللَّهَ فَاسْأَلُوهُ الْفِرْدَوْسَ فَإِنَّهُ أَعْلَى الْجَنَّةِ وَأَوْسَطُ الْجَنَّةِ، وَمِنْهُ تَفَجَّرُ أَنْهَارُ الْجَنَّةِ، وَفَوْقَهُ عَرْشُ الرَّحْمَنِ»

*"Mwenye kumuamini Allah na Mjumbe Wake, akasimamisha Sala, akafunga Ramadhani, basi atakuwa na haki juu ya Allah kuwa Amuingize Jannah bila ya kujali kuwa alifanya hijira katika njia ya Allah au (aliendelea kubaki) katika ardhi yake aliyozaliwa". Wakamuuliza: "Ewe Mjumbe wa Allah! Tuwajulishe watu kuhusu bishara hii?" Akajibu; Peponi kuna daraja mia moja ambazo, Allah Amewaandalia wanaofanya Jihadi katika njia ya Allah. Masafa baina ya kila daraja mbili ni sawa na umbali wa baina ya mbingu na ardhi. Basi mnapomuomba Allah, Muombeni Akupatieni Firdaus, kwani hiyo ndiyo pepo ya juu zaidi na bora zaidi, na humo ndimo mna vyanzo vya mito yote ya peponi, na juu yake iko Arshi ya Ar-Rahman"<sup>1</sup>.*

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Abu Hurayra رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِذَا صَلَّيْتُمْ عَلَيَّ فَسَلُّوا اللَّهَ لِي الْوَسِيلَةَ، قِيلَ يَا رَسُولَ اللَّهِ وَمَا الْوَسِيلَةُ؟ قَالَ: «أَعْلَى دَرَجَةٍ فِي الْجَنَّةِ لَا يَتَّالِهَا إِلَّا رَجُلٌ وَاحِدٌ وَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَنَا هُوَ»

*"Mtakapomuomba Allah تعالى Anishushie rehema, pia Muombeni Anipatie Al-Wasilah". Akaulizwa, 'Ewe Mjumbe wa Allah "Al-Wasilah ni kitu gani?" Akajibu; "Ni daraja ya juu zaidi Peponi, hataipata yeyote, isipokuwa mtu mmoja tu, na ninataraji kuwa mtu huyo ni mimi"<sup>2</sup>.*

Ndani ya Musnad wa Imamu Ahmad kuna Hadithi ya Sa'd bin Mujahid At-Twaisy kutoka kwa Abu Al-Mudillah kutoka kwa Abu Hurayra رضي الله عنه alisema, "Tulimuuliza Mtume ﷺ, "Tupe sifa za pepo ilivyojengwa". Akasema;

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 6:14.

<sup>2</sup> Ahmad 2:265.

«لَيْتَهُ ذَهَبٌ وَلَيْتَهُ فِضَّةٌ، وَمِلَاطُهَا الْمِسْكُ وَحَضْبَاتُهَا اللَّوْلُؤُ وَالْيَاقُوتُ، وَتُرَابُهَا  
الرَّغَمَرَانُ. مَنْ يَدْخُلُهَا يَنْعَمَ لَا يَتَأَسُّ وَيَخْلُدُ لَا يَمُوتُ، لَا تَبْلَى ثِيَابُهُ وَلَا يَفْنَى  
سَبَابُهُ»

*"Tofali la dhahabu na la fedha. Saruji yake ni ya miski, changarawe zake ni lulu na yakuti na udongo wake ni Zafarani. Mwenye kuingia ameneemeka hakati tamaa, ataishi milele na hatakufa, nguo zake hazichakai wala ujana wake hauishi"*<sup>1</sup>.

Kauli ya Allah تعالى:

وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ

**"...na Radhi za Mwenyezi Mungu". (9:72)** Kwa maana: Radhi ya Allah تعالى kwao ni kubwa, tukufu na adhimu na hiyo ndiyo kubwa na zaidi kuliko neema zingine watakazokuwa nazo. Ni sawa na kauli ya Imamu Malik رحمه الله تعالى kutoka kwa Zayd bin Aslam kutoka kwa 'Atwaa bin Yassar alisema, kuwa Abu Sa'id Al-Khudri عنه رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يَقُولُ لِأَهْلِ الْجَنَّةِ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ فَيَقُولُونَ: لَبَّيْكَ رَبَّنَا وَسَعْدَيْكَ  
وَالْخَيْرُ فِي يَدَيْكَ. فَيَقُولُ: هَلْ رَضِيتُمْ؟ فَيَقُولُونَ: وَمَا لَنَا لَا نَرْضَى يَا رَبُّ وَقَدْ  
أَعْطَيْتَنَا مَا لَمْ نُنْغِظْ أَحَدًا مِنْ خَلْقِكَ، فَيَقُولُ: أَلَا أُعْطِيكُمْ أَفْضَلَ مِنْ ذَلِكَ؟  
فَيَقُولُونَ: يَا رَبُّ وَأَيُّ شَيْءٍ أَفْضَلُ مِنْ ذَلِكَ؟ فَيَقُولُ: أَجَلٌ عَلَيْكُمْ رِضْوَانِي فَلَا  
أَسْخَطُ عَلَيْكُمْ بَعْدَهُ أَبَدًا»

*"Allah تعالى Atawaambia watu wa Peponi: "Enyi watu wa pepo!" Wataitika, "Tumekuitika, ewe Mola wetu, na tunafurahia kukutumikia na kheri yote iko Mkononi Mwako". Atawauliza: "Je mmekuwa radhi?" Watamjibu: "Tuna nini cha kutufanya tusiwe radhi, ilhali Umetupatia vile ambavyo Hukumpatia yeyote katika viumbe wako". Atawauliza tena: "Je Nikupatieni kilicho bora zaidi ya hayo?" Watajibu kwa swali: "Na kuna kitu gani kilicho bora kuliko haya?" Atawaambia: "Nitakupatieni Radhi Zangu na baada ya hapo Sitakughadhikieni".*

Sahih Mbili ziliikusanya Hadithi hii ya Malik<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> Ahmad 2:304.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 11:423 na Muslim 4:2176.



يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ جَبْهَدِ الْكُفَّارَ  
 وَالْمُنْفِقِينَ وَأَعْلَظْ عَلَيْهِمْ<sup>ع</sup>  
 وَمَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ<sup>ط</sup> وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿٧٣﴾  
 خَلْفُونَ بِاللَّهِ مَا  
 قَالُوا وَلَقَدْ قَالُوا كَلِمَةَ الْكُفْرِ  
 وَكَفَرُوا بَعْدَ إِسْلَامِهِمْ  
 وَهُمْ مَا لَمْ يَنَالُوا<sup>ع</sup> وَمَا نَقَمُوا<sup>ع</sup> إِلَّا أَنْ  
 أَغْنَاهُمُ اللَّهُ  
 وَرَسُولُهُ مِنْ فَضْلِهِ<sup>ع</sup> فَإِنْ يَتُوبُوا  
 يَكْ خَيْرًا لَهُمْ<sup>ط</sup> وَإِنْ يَتَوَلَّوْا  
 يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ عَذَابًا أَلِيمًا  
 فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ<sup>ع</sup> وَمَا لَهُمْ فِي  
 الْأَرْضِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٧٤﴾ \*  
 وَبِهِمْ مَن عَاهَدَ اللَّهُ  
 لِيَنْتَظِرَ مِنْ فَضْلِهِ  
 لِنَصِّدَقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ  
 الصَّالِحِينَ ﴿٧٥﴾ فَلَمَّا آتَاهُمُ  
 مِنْ فَضْلِهِ خَلَوْا بِهِ  
 وَتَوَلَّوْا وَهُمْ مُعْرِضُونَ ﴿٧٦﴾  
 فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا فِي قُلُوبِهِمْ  
 إِلَى يَوْمِ يَلْقَوْتَهُ بِمَا  
 أَخْلَفُوا اللَّهَ مَا وَعَدُوهُ  
 وَبِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ ﴿٧٧﴾  
 أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ  
 يَعْلَمُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ  
 وَأَنْ اللَّهَ عَلَّمَ الْغُيُوبَ ﴿٧٨﴾  
 الَّذِينَ يَلْمِزُونَ الْمُطَّوِّعِينَ  
 مِنَ الْمُؤْمِنِينَ فِي الصَّدَقَاتِ  
 وَالَّذِينَ لَا يَجِدُونَ إِلَّا  
 جُهْدَهُمْ فَيَسْخَرُونَ مِنْهُمْ  
 سَخِرَ اللَّهُ مِنْهُمْ وَلَهُمْ  
 عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٩﴾

يَتَأْتِيَا النَّبِيَّ جَبْهَدِ الْكُفَّارَ  
 وَالْمُنْفِقِينَ وَأَعْلَظْ عَلَيْهِمْ<sup>ع</sup> وَمَأْوَاهُمْ  
 جَهَنَّمُ<sup>ط</sup> وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿٧٣﴾  
 خَلْفُونَ بِاللَّهِ مَا قَالُوا  
 وَلَقَدْ قَالُوا كَلِمَةَ الْكُفْرِ  
 وَكَفَرُوا بَعْدَ إِسْلَامِهِمْ  
 وَهُمْ مَا لَمْ يَنَالُوا<sup>ع</sup> وَمَا نَقَمُوا<sup>ع</sup> إِلَّا  
 أَنْ أَغْنَاهُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ  
 مِنْ فَضْلِهِ<sup>ع</sup> فَإِنْ يَتُوبُوا  
 يَكْ خَيْرًا لَهُمْ<sup>ط</sup> وَإِنْ يَتَوَلَّوْا  
 يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ عَذَابًا أَلِيمًا  
 فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ<sup>ع</sup> وَمَا لَهُمْ فِي  
 الْأَرْضِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿٧٤﴾

73. "Ewe Nabii! Pambana na makafiri na wanafiki na wakazanie. Na makazi yao ni Jahannamu, na huo ndio mwisho mbaya".

74. "Wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hawakusema; nao wame

*kwishasema neno la ukafiri, na wakakufuru baada ya kusilimu kwao. Na wakajihimu kufanya ambayo hawakuweza kuyafikia. Na hawakuchukia ila kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake Amewatajirisha kutokana na Fadhila Zake. Wakitubu itakuwa kheri kwao, na wakigeuka Mwenyezi Mungu Atawaadhibu wao duniani na Akhera. Na wala hawana katika ardhi Mlinzi wa kuwanusuru".*

## Amri ya Kufanya Jihadi Dhidi ya Makafiri na Wanafiki na Kuwakomali Wao

Allah تعالی Alimuamuru Mtume ﷺ afanye Jihadi dhidi ya makafiri na wanafiki na awe mgumu kwao. Pia alimuamuru awe mpole kwa Waumini wanaomfuata, na kwamba mwisho wa makafiri na wanafiki huko Akhera ni Motoni.

Ibn Mas'ud رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالی,

جَهَادِ الْكُفَّارِ وَالْمُنَافِقِينَ

**“Pambana na makafiri na wanafiki.”**

“Kwa kutumia mkono kama haikuwezekana basi angalau kuwakazia uso”<sup>1</sup>. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Allah تعالی Alimuamuru afanye Jihadi dhidi ya makafiri kwa upanga na dhidi ya wanafiki kwa ulimi na aondoe upole kwao”<sup>2</sup>. Adh-Dhahhak alisema, “Fanya Jihadi dhidi ya makafiri kwa upanga na uwe mgumu kwa wanafiki kwa njia ya maneno ambapo hiyo ndiyo Jihadi dhidi yao”<sup>3</sup>. Muqatil na Ar-Rabi’ walisimulia mithili ya hayo”<sup>4</sup>. Al-Hasan na Qatadah walisema: “Kufanya Jihadi dhidi yao ni kusimamia mipaka ya ki-Sharia dhidi yao”<sup>5</sup>. Huenda ikasemwa pia kuwa kauli hizi hazipingani, kwani wakati mwingine anaweza kuwaadhibu kwa kutumia njia ya kwanza na mara nyingine vinginevyo, kulingana na mazingira. *Allah Aalam.*

## Sababu za Kushushwa kwa Aya 9:74

Al-Umawi alieleza katika Kitabu chake cha (*Maghazi*) vita: “Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالی alitusimulia kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa Abdur-Rahman Abdillah bin Ka’b bin Malik aliambiwa na ‘Abdur-Rahman bin ‘Abdullah bin Ka’b bin Malik aliambiwa na baba yake kwamba babu yake alisema: “Miongoni mwa wanafiki waliobakia nyuma (bila ya kwenda vitani) na ambao Qur’an ilishuka kuwahu ni Al-Julas bin Suwayd bin Assaamit alikuwa akiishi pamoja na mama wa Umair bin Sa’ad na ulezi wa Umair ukawa chini yake. Baada ya

<sup>1</sup> At-Tabari 14:358.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:359.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:359.

<sup>4</sup> Ibn Abu Hatim 6:1842.

<sup>5</sup> At-Tabari 14:359.

Allah تعالی Kuteremsha Qur'an na Akayaeleza hayo Aliyoyataja kuhusu wanafiki. Al-Julus alisema: "Wallahi! Ikiwa mtu huyu ni mkweli katika anayoyasema, basi sisi ni waovu zaidi kuliko Punda." Umair bin Sa'd aliyasikia maneno hayo na akasema: "Wallahi, ewe Julus! Wewe ni mtu ninayekupenda sana na mwenye ihsani sana kwangu, na ninahofia kukupata madhara. Umezungumza kauli ambazo ikiwa nitazitaja, zitanifedhehesha na kama nitanyamazia, basi zitaniangamiza. Mojawapo kati ya hizi mbili ni ndogo kuliko ya pili". Akaenda kwa Mtume ﷺ na akamtajia aliyoyasema Julus. Khabari hiyo ilipomfikia Julus akamuendea Mtume ﷺ akaapa kwa Jina la Allah تعالی kuwa hakuyasema hayo yaliyoelezwa na Umair bin Sa'd رضي الله عنه, "Na ameongopa juu yangu." Allah تعالی Akashusha Ayah ifuatayo juu ya hayo,

مُخَلَّفُونَ بِاللَّهِ مَا قَالُوا وَلَقَدْ قَالُوا كَلِمَةَ الْكُفْرِ وَكَفَرُوا بَعْدَ إِسْلَامِهِمْ

***"Wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hawakusema; nao wamekwishasema neno la ukafiri, na wakakufuru baada ya kusilimu kwao."***

Mpaka mwisho wa Aya. Mtume ﷺ akaifikisha Aya hii kwa Al-Julus, ambaye walidai kuwa alitubu toba ya ikhlasi, akajitoa katika unafiki. Imamu abu Ja'far bin Jariri رحمه الله aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema: "Mtume ﷺ alikuwa amekaa chini ya kivuli cha mti, akasema:

«إِنَّهُ سَيَأْتِيكُمْ إِنْسَانٌ فَيَنْظُرُ إِلَيْكُمْ بِعَيْنِي الشَّيْطَانِ فَإِذَا جَاءَ فَلَا تُكَلِّمُوهُ»

***"Mtu atakujieni na kukutazameni kwa macho ya Shetani. Atakapokuja, Msiseme naye"***

Punde, akatokea mtu wa rangi ya bluu. Mtume ﷺ akamuita na kumuuliza:

«عَلَامَ تَشْتُمُنِي أَنْتَ وَأَصْحَابُكَ»

***"Ni kwa sababu ya kitu gani wewe na sahibu zako mnanitukana?"***

Mtu huyo akaondoka Halafu akarejea na rafiki zake. Wakaapa kwa Jina la Allah تعالی kwamba hawakufanya jambo kama hilo. Mtume ﷺ akawaacha. Allah تعالی Akashusha Aya;

مُخَلَّفُونَ بِاللَّهِ مَا قَالُوا

***"Wanaapa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hawakusema"***

**Njama za Wanafiki Kutaka Kumuuu Mtume ﷺ.**

Kauli ya Allah تعالى: وَهُمْ أُولَئِكَ لَمْ يَنَالُوا

**“Na wakajihimu kufanya ambayo hawakuweza kuyafikia”.**

Inasemekana Aya hii ilishushwa kumhusu Al-Julas bin Suwayd ambaye alipanga njama za kumuua mwana wa mkewe wakati alipomuambia, “Wallahi! Nitamfahamisha Mtume ﷺ.” Ilisemwa pia, kuwa Aya hii ilimhusu ‘Abdullah bin Ubayy ambaye alikusudia kumuua Mtume ﷺ.<sup>1</sup>

As-Suddi alisema: “Aya hii ilishuka kukihusu kikundi cha watu ambao Walipanga kumtukuza ‘Abdullah bin Ubayy, hata kama Mtume ﷺ hataridhia. Pia ilielezwa kwamba, kuna kikundi cha wanafiki ambacho kilipanga kumuua Mtume ﷺ akiwa katika vita vya Tabuk katika usiku mmoja wapo akiwa katika mazingira ya safari. Walikuwa zaidi ya watu kumi. Adh-Dhahhak alisema, “Aya hii ilishuka kuwahusu wao”. Hii inabainisha yale aliyoyasimulia Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bayhaqi رحمه الله تعالى katika kitabu, *Dalailun-Nubuwwah*, kuwa Hudhayfah bina Al-Yaman رضي الله عنه alisema, “Nilikuwa nimeshika zimamu za ngamia wa Mtume ﷺ nikimuongoza njia huku ‘Ammar رضي الله عنه akimhimiza kwenda au mimi nikimhimiza kwenda na ‘Ammar رضي الله عنه akimuongoza njia. Tulipofika Al-‘Aqabah, watu kumi waliokuwa juu ya wanyama walimzuia Mtume ﷺ. Nikamfahamisha Mtume ﷺ kuhusu watu hao, akawapigia kelele, wakakimbia. Mtume ﷺ akatuuliza;

«هَلْ عَرَفْتُمُ الْقَوْمَ؟»

“Mnatambua walikuwa akina nani?” Tukamjibu: “Hapana ewe Mtume wa Allah! Walikuwa wameziba nyuso zao. Lakini tuliwatambua farasi wao”. Akasema:

«هَؤُلَاءِ الْمُنَافِقُونَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهَلْ تَدْرُونَ مَا أَرَادُوا؟»

“Hao ni wanafiki mpaka Siku ya Kiyama. Je mnakijua walichokikusudia?” Tukajibu: “Hapana”. Akasema;

«أَرَادُوا أَنْ يُرَاجِمُوا رَسُولَ اللَّهِ فِي الْعَقَبَةِ فَيَلْقَوْهُ مِنْهَا»

“Walitaka kumzonga Mtume wa Allah na kumdongosha (bondeni) katika eneo la Al-‘Aqabah”.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:363.

Tukasema: “Ewe Mtume! Kwanini usiwatume wakuu wa makabila yao wakuletee kichwa cha mmoja wao?” Akasema:

«لَا أَكْرَهُ أَنْ تَتَحَدَّثَ الْعَرَبُ بَيْنَهَا أَنَّ مُحَمَّدًا قَاتَلَ بِقَوْمٍ حَتَّى إِذَا أَظْهَرَهُ اللَّهُ إِلَيْهِمْ  
أَقْبَلَ عَلَيْهِمْ بِقَتْلِهِمْ - ثُمَّ قَالَ - اللَّهُمَّ ارْمِهِمْ بِالذَّبَابِ»

“Hapana, kwani naogopa Waarabu wasije kusema Muhammad aliwatumia baadhi ya watu katika mapigano, na baada ya Allah Kumpatia ushindi kwa msaada wao, aliwageuka na kuanza kuwaua”. Kisha akasema: “Ewe Allah! Waangamize kwa kuwatupia Dubaylah”.

Tukamuuliza, “Dubaylah ni nini ewe Mtume wa Allah?” Akajibu:

«شِهَابٌ مِنْ نَارٍ يَقَعُ عَلَى نِطَاطِ قَلْبِ أَحَدِهِمْ فَيَهْلِكُ»

“Ni kimondo cha moto kinachoangukia juu ya moyo wa mmoja wao na kumuua.”<sup>1</sup>

Abu At-ufayl alitusimulia: “Kulikuwa na ugomvi baina ya Hudhayfah na mtu mmoja wa *Al-'Aqabah* ambaye alimuuliza: “Nakuuliza kwa Jina la Allah! Watu wa *Al-'Aqabah* walikuwa wangapi? “Watu wakamuambia: “Mjibu alichokuuliza”. Akajibu: “Tuliambiwa walikuwa kumi na wanne, kama ulikuwemo, basi walikuwa kumi na watano. Nashuhudia kwa Allah تعالی kuwa kumi na wawili kati yao wako vitani dhidi ya Allah تعالی na Mtume ﷺ katika maisha ya duniani na siku Mashahidi wataposimama kutoa ushahidi (siku ya Qiyama). Isipokuwa Watatu kati yao walitoa udhuru kwa kusema: Hatukusikia kabisa mtoa wito wa Mtume ﷺ wala hatukujua kitu walichokipanga watu hao”, kwani Mtume ﷺ alikuwa katika mwendo na joto lilikuwa kali, wakati aliposema:

«إِنَّ الْمَاءَ قَلِيلٌ فَلَا يَسْفِينِي إِلَيْهِ أَحَدٌ»

“Maji ni machache, kwa hivyo kati yenu asinitangulie kufika huko”.

Akawakuta baadhi ya watu wakiwa tayari wamemtangulia, aliwalaani siku hiyo hiyo<sup>2</sup>. Masimulizi mengine aliyaandika Muslim pia, kuwa ‘Ammar bin Yasir alisema, Hudhayfah رضي الله عنه alinipasha khabari kuwa Mtume ﷺ alisema:

<sup>1</sup> *Dalail An-Nubuwwah* 5:260.

<sup>2</sup> Muslim 4:2144.

«فِي أَصْحَابِي اثْنَا عَشَرَ مُتَافِقًا لَا يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يَجِدُونَ رِيحَهَا حَتَّى يَلِجَ  
الْجَمَلُ فِي سَمِّ الْخِيَاطِ: ثَمَانِيَةٌ مِنْهُمْ تَكْفِيكُهُمُ الدُّبَيْلَةُ سِرَاجٌ مِنْ نَارٍ يَظْهَرُ بَيْنَ  
أَكْتَافِهِمْ حَتَّى يَنْجَمَ فِي صُدُورِهِمْ»

*“Miongoni mwa Masahaba wangu kuna wanafiki kumi na wawili. Hawataingia peponi wala hawatapata harufu yake mpaka ngamia aingie katika tundu la sindano. Wanane kati yao watapigwa na Dubaylah, ambalo ni kombora lililofanyizwa kwa moto ambapo litatokezea baina ya mabega yao na kuvipasua vifua vyao.”<sup>1</sup>*

Kwa sababu hii, Hudhayfah رضي الله عنه alikuwa akiitwa *Swahibus-Sirr*, maana yake mtunza siri, ambayo hakuna mwingine yeyote aliyekuwa akijua, na hiyo ni kuhusu kukijua kikundi cha wanafiki. Hao ni wale ambao Mtume ﷺ alimjulisha yeye tu, na si mwingine. *Allah Aalam*. Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا نَقْمُوا إِلَّا أَنْ أَعْتَدْتَهُمُ اللَّهُ وَرَسُولُهُ مِنْ فَضْلِهِ<sup>٢</sup>

***“Na hawakuchukia ila kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake Amewatajirisha kutokana na fadhila Zake”.***

Kwa maana: Mtume ﷺ hakuwafanyia kosa, isipokuwa kosa ni kwamba Allah تعالى Amewatajirisha kwa Fadhila Zake kutokana na baraka na utukufu wa ujumbe wa Mtume wake. Lau Allah تعالى Angeliwaongoa katika yale aliyokuja nayo Mtume ﷺ. Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ alipowaambia Answaar:

«أَلَمْ أَجِدْكُمْ ضَلَّالًا فَهَدَاكُمْ اللَّهُ يٰ، وَرَكُتُمْ مُتَفَرِّقِينَ فَأَلْفَكُمُ اللَّهُ يٰ، وَعَالَةً فَأَغْنَاكُمْ  
اللَّهُ يٰ»

*“Je sijakukuteni mkiwa wapotovu, kisha Allah Akakuongozeni kupitia kwangu, na mlikuwa mmetengana, Allah Akakuunganisheni kupitia kwangu”.*

Kila aliponena hivyo, wao walisema, “Allah تعالى na Mtume ﷺ ni wafadhili mno”.<sup>2</sup> Maneno haya, Hutamkwa pale ambapo hakuna dhambi iliyotendeka. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

<sup>1</sup> Muslim 4:2143.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 7:644.

وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَنْ يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ

**“Nao hawajaona baya lolote kwao (waislamu) ila kumuamini Mwenyezi Mungu”.** (85:8) Kisha Allah تعالى Akawataka wao kuleta Toba, Akasema,

فَإِنْ يَتُوبُوا يَكُ خَيْرًا لَّهُمْ وَإِنْ يَتَوَلَّوْا يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ عَذَابًا أَلِيمًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

**“Wakitubu itakuwa kheri kwao, na wakigeuka Mwenyezi Mungu Atawaadhibu wao Adhabu yenye kutia uchungu duniani na Akhera”.**

Kwa maana: Na kama Wataendelea na njia yao, Allah تعالى Atawapa adhabu iumizayo duniani, kwa mauaji, huzuni na majonzi, na Akhera itakuwepo adhabu, udhalili na unyonge.

وَمَا هُمْ فِي الْأَرْضِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ

**“Na wala hawana katika ardhi Mlinzi wa kuwanusuru”.** Wala hakuna wa kuwasaidia, wala wa kuwanufaisha, wala wa kuwaletea kheri wala wa kuwaondoshea shari.

\* وَمِنْهُمْ مَنْ عَاهَدَ اللَّهُ لَئِنْ آتَيْنَا مِنْ فَضْلِهِ لَنَصَّدَّقَنَّ وَلَنَكُونَنَّ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٦﴾  
 فَلَمَّا آتَاهُمْ مِنْ فَضْلِهِ بَخِلُوا بِهِ وَتَوَلَّوْا وَهُمْ مُعْرِضُونَ ﴿٧٧﴾ فَأَعْقَبَهُمْ نِفَاقًا  
 فِي قُلُوبِهِمْ إِلَى يَوْمِ يَلْقَوْنَهُ بِمَا أَخْلَفُوا اللَّهَ مَا وَعَدُوهُ وَبِمَا كَانُوا يَكْذِبُونَ  
 ﴿٧٨﴾ أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ سِرَّهُمْ وَنَجْوَاهُمْ وَأَنَّ اللَّهَ عَلَّمُ الْغُيُوبِ ﴿٧٩﴾

**75. “Na miongoni mwao wapo waliomuahidi Mwenyezi Mungu kwa kusema: Akitupa katika Fadhila Yake hapana shaka tutatoa sadaka, na tutakuwa katika watendao mema”.**

**76. “Alipowapa katika Fadhila Yake wakaifanyia ubakhili na wakageuka, na huku wakipuuza”.**

**77. “Basi Akawalipa kwa unafiki kuutia nyoyoni mwao mpaka Siku watapokutana Naye, kwa sababu ya kuwa walimkhalifu Mwenyezi Mungu katika yale waliyomuahidi, na kwa sababu ya kusema kwao uongo”.**

**78. “Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu Anajua siri zao na minong’ono yao, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyajua sana ya ghaibu?”**

## Katika Alama za Wanafiki ni Kukusanya Mali na Kuwa Wagumu Katika Kutoa Zaka.

Allah تعالى Anasema; Kuna wanafiki ambao wanampa ahadi Allah تعالى kuwa ikiwa atamtajirisha kutokana na Fadhila Zake, basi atatoa Sadaka kutokana na mali Yake na atakuwa miongoni mwa waja wema, lakini hayatekelezi aliyoyasema wala kuyasadikisha aliyoyadai. Adhabu ya tabia hii ni kuwekwa unafiki nyoyoni mwake mpaka atakapokutana na Allah تعالى, katika Siku ya Kiyama. Kauli ya Allah تعالى:

بِمَا أَخْلَفُوا اللَّهَ مَا وَعَدُوهُ

**“...kwa sababu ya kuwa walimkhalifu Mwenyezi Mungu katika yale waliyomuahidi, na kwa sababu ya kusema kwao uongo”.**

Kwa maana: Amewawekea unafiki nyoyoni mwao kwa sababu ya tabia yao ya kwenda kinyume na ahadi na pia kwa uongo wao. Ni sawa na ilivyoandikwa ndani ya *Sahih* Mbili kuwa Mtume ﷺ alisema;

«آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا اتَّخَذَ خَانَ»

*“Alama za Mnafiki ni tatu, akizungumza hudanganya, akiahidi huvunja ahadi na akiaminiwa Hufanya khiyana (hukhini)”.*<sup>1</sup>

Kauli ya Allah تعالى,

الَّذِينَ يَعْلَمُونَ أَنَّهُ اللَّهُ يَعْلَمُ بِهِمْ وَنَجْوَاهُمْ

**“Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu Anajua siri zao na minong’ono yao”.**

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Anazijua siri na vilivyofichikana na kwamba Anayajua makusudio yao hata kama watadhirisha kuwa ikiwa watapata mali, watatoa Sadaka na watamshukuru. Basi, Allah تعالى Anawajua zaidi kuliko mnavoyojijua, kwani Yeye ni Mjuzi wa ghaibu. Maana, Anajua kila ghaibu na dhahiri, na kila siri na mnong’ono, na Anajua lililo la dhahiri na lililojificha.

الَّذِينَ يَلْمِزُونَ الْمُطَّوِّعِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ فِي الصَّدَقَاتِ وَالَّذِينَ لَا يَجِدُونَ  
إِلَّا جُهْدَهُمْ فَيَسْخَرُونَ مِنْهُمْ سَخِرَ اللَّهُ مِنْهُمْ وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٦﴾

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 1:11 na Muslim 1:78.



**79. "Wale wanaowabeuwa Waumini wanaotoa sadaka nyingi na wasio nacho cha kutoa ila kadri ya juhudi yao, basi huwakejeli. Mwenyezi Mungu Atawakejeli wao! Nao watapata adhabu chungu!"**

### **Katika Alama za Wanafiki ni Kuwabeua Wanaotoa Kingi na Kuwabeza Wanaotoa Kidogo.**

Hii pia ni mojawapo ya sifa za wanafiki, hasalimiki yeyote kutokana na utiaji wao kasoro na kudhihaki katika hali zote, hata watoao Sadaka hawasalimiki nao. Mmoja wao akitoa mali nyingi, wao husema, "Huyu anajionesha tu" na akitoa kichache wao husema, "Allah تعالی Hana haja na Sadaka na mtu huyu". Ni sawa na alivyoandika Bukhari kwamba 'Ubaydullah bin Sa'id alisema, Abu Nu'man Al-Basri, Shu'bah alitusimulia kutoka kwa Sulayman kuwa Abu Wail alimsikia Abu Mas'ud akisema: "Ilipoteremshwa Aya inayozungumzia Sadaka, tulikuwa tukibebeshwa migongoni mwetu. Siku moja mtu mmoja akaja na kutoa Sadaka nyingi, wakasema: "Anafanya ria". Akaja mtu mwingine na kutoa Sadaka ujazo wa pishi moja. Wakasema, "Allah تعالی Hana haja na Sadaka ya huyu". Ikashuka Aya:

الَّذِينَ يَلْمِزُونَ الْمُطَّوِّعِينَ

**"Wale wanao wabeuwa Wanaojitolea"<sup>1</sup>.**

Pia, Muslim alikusanya Hadithi hii ndani ya *Sahih*<sup>2</sup>.

Al-'Awfi alisema kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema kwamba siku moja Mtume ﷺ aliwaendea watu na kuwaambia wazikusanye Sadaka zao. Watu wakakusanya Sadaka zao. Mwishowe akaja mtu na pishi moja ya tende, akasema: "Ewe Mtume ﷺ! Hii ni pishi ya tende, ambapo usiku mzima nilikuwa nabeba maji na malipo yake nimepata pishi mbili za tende. Moja nimeibakisha, na nyingine ni hii nimekuletea". Mtume ﷺ akamuamuru aichanganye na Sadaka (nyingine). Baadhi ya watu wakamkejeli, wakamuambia, "Allah تعالی na Mtume Wake ﷺ hawana haja na Sadaka ya huyu, wala pishi moja hawataifanyia chochote" 'Abdur-Rahman bin 'Awf رضي الله عنه alimuuliza Mtume ﷺ, "Kuna Mtoaji Sadaka mwingine aliyesalia?" Naye akajibu,

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 3:332.

<sup>2</sup> Muslim 2:706.

«لَمْ يَبْقَ أَحَدٌ غَيْرُكَ»

“*Hakubakia yeyote zaidi yako.*” Abdur-rahman bin Awf رضي الله عنه akamuambia: “Hakika mimi nitatoa wakia mia moja za dhahabu.” ‘Umar bin Al-Khattwab رضي الله عنه akamuambia: “Una wazimu?” Akamjibu, “Sina wazimu”. Akamuuliza, “Umeitoa kama ulivyosema?” Akamjibu, “Ndiyo, kwani mali yangu yote ni (Dirham) elfu nane, ambapo elfu nne kati ya hizo ninamkopesha Mola wangu na nyingine elfu nne ninabakia nazo”. Mtume ﷺ akamuomba dua kwa kusema:”

«بَارَكَ اللهُ لَكَ فِيمَا أَمْسَكْتَ وَفِيمَا أُعْطَيْتَ»

“*Allah Akubariki katika ulichokibakisha na ulichokitoa.*”

Wanafiki wakambeua kwa kumuambia, “Wallahi! ‘Abdur-Rahman hakutoa mali yake kwa ajili ya jingine isipokuwa ni ria”. Waliongopa kwani alifanya hivyo kwa dhati. Allah تعالى Akashusha Aya kuhusu kusafika kwake yeye na nasibu yake masikini, ambaye alileta pishi moja ya tende, Allah تعالى Alisema katika Kitabu Chake,

الَّذِينَ يَلْمُزُونَ الْمُطَّوِّعِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ فِي الصَّدَقَاتِ

“*Wale wanao wabeua Waumini wanao toa sadaka.*” (9:79)<sup>1</sup>

Hivi ndivyo ilivyosimuliwa kutoka kwa Mujahid na wengine. Ibn Is-haqi رحمه الله تعالى alisema: “Miongoni mwa Waumini waliotoa Sadaka ni ‘Abdur-Rahman bin ‘Awf رضي الله عنه ambaye alitoa (Dinari) elfu nne, na Asim bin Adiy رضي الله عنه ndugu wa Banu Ajlani, walifanya hivyo, kwa sababu Mtume ﷺ aliwahimiza na kuwashajiisha kutoa sadaka. Akasimama Abdur- Rahman bin ‘Awf رضي الله عنه akatoa Dirhamu elfu nne, akasimama ‘Aswim bin ‘Adi رضي الله عنه akatoa *Wasaq* mia moja za tende Wanafiki wakawakejeli hawa wawili na wakasema: “Hiyo ni ria tu”. Sahaba aliyetoa Sadaka ndogo alikuwa Abu ‘Aqil رضي الله عنه ndugu wa Banu Unaif Al-Araashi, rafiki wa Banu ‘Amri bin ‘Awf. Alileta pishi ya tende na kuichanganya katika Sadaka zingine. Wakamcheka na kusema, “Allah تعالى Hana haja na pishi ya Abu ‘Aqil.” Kauli ya Allah تعالى,

فَيَسْخَرُونَ مِنْهُمْ سَخِرَ اللَّهُ مِنْهُمْ

“*...basi huwakejeli. Mwenyezi Mungu Atawakejeli wao!*”

<sup>1</sup> At-Tabari 14:383

Allah تعالى Anasema, "Huwakejeli" wanafiki ili lugha yake ifanane na tendo lao la kejeli na shere kwa Waumini. Hii inaitwa *Muqaabala* kwani malipo yanatakiwa yafanane na kazi, Amewalipa shere kutokana na tendo lao la kuwafanyia shere Waumini; ili Kuwapa ushindi Waumini hapa duniani na Akhera Amewaandalia Wanafiki adhabu kali sana, kwani malipo yanayofanana na kazi husika.



اَسْتَغْفِرُ هُمْ اَوْ لَا تَسْتَغْفِرُ هُمْ اِنْ تَسْتَغْفِرُ هُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً  
 فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ هُمْ ؕ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ؕ  
 وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْفَاسِقِينَ ﴿٨٠﴾ فَرِحَ الْمُخَلَّفُونَ  
 بِمَقْعَدِهِمْ خِلَافَ رَسُولِ اللَّهِ وَكَرِهُوا أَنْ يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ  
 وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُوا لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ قُلْ نَارُ  
 جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا ؕ لَوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ ﴿٨١﴾ فَلْيَضْحَكُوا  
 قَلِيلًا وَلْيَبْكُوا كَثِيرًا جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨٢﴾ فَإِنْ  
 رَجَعَكَ اللَّهُ إِلَى طَائِفَةٍ مِنْهُمْ فَاسْتَأْذَنُوكَ لِلْخُرُوجِ فَقُلْ  
 لَنْ نَخْرُجُوا مَعَكُمْ أَبَدًا وَلَنْ تُقَاتِلُوا مَعِيَ عَدُوًّا إِنَّكُمْ رَضِيتُمْ  
 بِالْقُعُودِ أَوَّلَ مَرَّةٍ فَاقْعُدُوا مَعَ الْخَالِفِينَ ﴿٨٣﴾ وَلَا تَصَلِّ  
 عَلَى أَحَدٍ مِنْهُمْ مَاتَ أَبَدًا وَلَا تَقُمْ عَلَى قَبْرِهِ ؕ إِنَّهُمْ كَفَرُوا  
 بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَأَمَانُوا وَهُمْ فَاسِقُونَ ﴿٨٤﴾ وَلَا تُعْجِبَكَ  
 أَمْوَالُهُمْ وَأَوْلَادُهُمْ ؕ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الدُّنْيَا  
 وَتَزْهَقَ أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٨٥﴾

اَسْتَغْفِرُ هُمْ اَوْ لَا تَسْتَغْفِرُ هُمْ اِنْ  
 تَسْتَغْفِرُ هُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ  
 هُمْ ؕ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ  
 وَرَسُولِهِ ؕ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ  
 الْفَاسِقِينَ ﴿٨٠﴾

**80. "Waombe msamaha au usiwaombe. Hata ukiwao mbea msamaha mara sabini, Mwenyezi Mungu Hata wasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wame-mkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu Hawa-ongoi watu wapotofu".**

**Makatazo Juu ya Kuwaombea Msamaha Wanafiki.**

Allah تعالى Anamjulisha Mtume ﷺ kwamba hawa

Wanafiki Hawastahiki kuombewa maghufira, na kwamba hata kama atawaombea msamaha mpaka mara sabini, Allah تعالى Hatawaghufiria. Inasemekana kuwa ilitajwa idadi ya sabini ili kufunga kabisa jambo la kuwaghufiria, kwani Waarabu huitumia namba hiyo katika maneno yao kwa njia ya kutilia mkazo jambo, wala si kuikusudia namba hiyo au zaidi yake. Ilisemwa pia kuwa idadi hiyo ina maana nyingi na ni kama alivyosema Ash-Sha'bi, wakati 'Abdullah bin Ubayy alipokuwa katika hatua za kutaka kufariki dunia, mwanaye alikwenda kwa Mtume ﷺ na kumuambia; "Baba yangu amefariki, napenda ukamuone na umsalie". Mtume ﷺ akamuuliza:

«مَا اسْمُكَ»

“Jina lako nani?”

Akajibu: “Al-Hubab bin ‘Abdullah”. Mtume ﷺ akasema:

«بَلْ أَنْتَ عَبْدُ اللَّهِ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ إِنَّ الْحُبَّابَ اسْمَ شَيْطَانٍ»

“Bali wewe ni ‘Abdullah bin ‘Abdullah, kwani Al-Hubab ni jina la shetani”.

Akaondoka naye, akamuona na akamvalisha kanzu yake (kama sanda) na akamsalia. Mtume ﷺ akaambiwa: “Unamsalia ilhali yeye ni Mnafiki?” Akajibu:

«إِنَّ اللَّهَ قَالَ: ﴿إِنْ تَسْتَغْفِرَ لِنَفْسِكَ مِائَةَ مَرَّةٍ﴾ وَلَا تَسْتَغْفِرُونَ لَهُمْ سَبْعِينَ وَسَبْعِينَ»

“Allah Amesema: “Hata mkiwaombea msamaha mara sabini.” Hakika nitawaombea maghufira mara sabini na sabini na sabini”<sup>1</sup>.

Masimulizi sawa na haya yalikusanywa kutoka kwa ‘Urwah bin Az-Zubayr, Mujahid, Qatadah bin Di‘amah na Ibn Jariri رحمه الله تعالى kwa isnadi zake<sup>2</sup>.

فَرِحَ الْمُخَلَّفُونَ بِمَقْعَدِهِمْ خَلِيفَ رَسُولِ اللَّهِ وَكَرِهُوا أَنْ يُجَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُوا لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا لَوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ ﴿٨١﴾  
فَلْيَضْحَكُوا قَلِيلًا وَلْيَبْكُوا كَثِيرًا جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨٢﴾

**81. “Walifurahi walioachwa nyuma kwa kule kubakia kwao nyuma na kumuacha Mtume na Mwenyezi Mungu. Na walichukia kupigana Jihadi kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya Allah, na wakasema: Msitoke nje katika joto! Sema: Moto wa Jahannamu una joto zaidi, laiti wangelifahamu!”**

**82. “Basi na wacheke kidogo; watalia sana. Hayo ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyachuma”.**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:396.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:396-397. Ingawa Hadithi hii ni *Mursal*, ina ushahidi mwingi na isnadi ambazo zina nguvu. Msingi wake pia umetajwa ndani ya Al-Bukhari (46704 na 4671). Pia rejea katika Tafsir ya Ibn Kathir chini ya maelezo ya Aya (9:84).

## Furaha ya Wanafiki kwa Kubaki Nyuma Wakati wa Vita vya Tabuk.

Allah تعالى Anawashutumu Wanafiki ambao hawakujiunga na Mtume ﷺ katika vita vya Tabuk, na wakafurahia kubakia kwao nyuma baada ya Mtume ﷺ kutoka,

وَكْرَهُوا أَنْ يُجَاهِدُوا

“*Na walichukia kupigana Jihadi*”. Na kushirikiana naye,

بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَقَالُوا

“*...kwa mali zao na nafsi zao katika njia ya Allah, na wakasema*”.

Kuambizana wao kwa wao.

لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ

“*Msitoke nje katika joto!*” Hayo ni kwa sababu uendaji katika vita vya Tabuk ulikuwa katika wakati wa joto kali na kipindi cha vivuli na wingi wa matunda.

Kwa ajili hii, walisema:

لَا تَنْفِرُوا فِي الْحَرِّ

“*Msitoke nje katika joto!*” Allah تعالى Alimuambia Mtume Wake ﷺ:

قُلْ

“*Sema*”. Uwaambie.

نَارُ جَهَنَّمَ

“*Moto wa Jahannamu*”. Ambao mtaungia kutokana na kutokujiunga kwenu.

أَشَدُّ حَرًّا

“*...una joto zaidi*”. Kuliko joto mlilolikimbia, bali ni kali zaidi kuliko hata moto. Ni sawa na alivyosema Imamu Malik رحمه الله تعالى, kutoka kwa Abu Az-Zinaad kutoka kwa Al-A'raj aliyesema kuwa Abu Hurayra رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«نَارُ بَنِي آدَمَ الَّتِي تُوقَدُونَهَا جُزْءٌ مِنْ سَبْعِينَ جُزْءًا مِنْ نَارِ جَهَنَّمَ»

“*Moto wa wanadamu mnaouwasha ni sehemu moja kati ya sabini za moto wa Jahannamu*”

Wakauliza: “Ewe Mtume! Moto huo si ulikuwa unatosha?”

«فُضِّلَتْ عَلَيْهَا بِتِسْعَةِ وَبِئْسَيْنِ جُزْءًا»

*“Joto la Jahannamu limefanywa kali zaidi kuliko joto la Moto duniani kwa sehemu sitini na moja”<sup>1</sup>. Sahih Mbili zilinukuu Hadithi hii<sup>2</sup>.*

Al-A'mash alisema kutoka kwa Abu Is-haq رحمه الله تعالى kutoka kwa Nu'man bin Bishr رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّ أَهْوَنَ أَهْلِ النَّارِ عَذَابًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ لِمَنْ نَهَ نَعْلَانٍ وَشِرَاكَيْنِ مِنْ نَارِ جَهَنَّمَ يَغْلِي مِنْهُمَا دِمَاغُهُ كَمَا يَغْلِي الْمِرْجَلُ، لَا يَرَى أَنَّ أَحَدًا مِنْ أَهْلِ النَّارِ أَشَدَّ عَذَابًا مِنْهُ وَإِنَّ أَهْوَنَهُمْ عَذَابًا»

*“Mtu wa motoni atakayepata adhabu ndogo zaidi kuliko wote katika Siku ya Kiyama ni yule ambaye atakuwa amevaa makubadhi mawili yaliyotengenezwa kwa moto wa Jahannamu yatakasababisha ubongo wake uchemke sawa na namna kinavyochemka chungu. Na atadhani kuwa hapana mtu wa Motoni mwenye adhabu kali zaidi yake, ilhali yeye ndiye mwenye adhabu ndogo zaidi”<sup>3</sup>.*

Sahih Mbili zimeandika Hadithi hii.<sup>4</sup> Kuna athari na Hadithi nyingi juu ya mada hii. Allah تعالى Amesema ndani ya Kitabu Chake Kitukufu;

كَلَّا إِنَّهَا لَأَطْلَى ﴿٧٠﴾ نَزَّاعَةً لِّلشَّوَى ﴿٧١﴾

***“La, hashu! Kwa hakika huo ni Moto mkali kabisa, unao babua ngozi ya kichwa!” (70:15-16)*** Na Kauli Yake Allah تعالى ,

يُصَبُّ مِنْ فَوْقِ رُءُوسِهِمُ الْحَمِيمُ ﴿٧٢﴾ يُصْهَرُ بِهِ مَا فِي بُطُونِهِمْ وَالْجُلُودُ ﴿٧٣﴾ وَهُمْ مَقْمُوعٌ مِنْ حَدِيدٍ ﴿٧٤﴾ كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا وَذُوقُوا عَذَابَ الْخَرْيِقِ ﴿٧٥﴾

***“...yataminiwa juu ya vichwa vyao maji yanayochemka. Kwa maji hayo vitayayushwa viliomo matumboni mwao, na ngozi zao pia. Na kwa ajili yao yatakuwapo marungu ya chuma. Kila***

<sup>1</sup> Al-Muwatta 2:994.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 6:380 na Muslim 4:2184.

<sup>3</sup> Al-Hakim 4:580.

<sup>4</sup> Fat'hul Al-Bari 11:425 Muslim 1:196.

**wakitaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo, na wataambiwa: Onjeni adhabu ya kuungua!"**

(22:19-22) Na Allah تعالى Amesema

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِنَا سَوْفَ نُصَلِّبُهُمْ نَارًا كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُمْ بَدَّلْنَاهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا لِيَذُوقُوا الْعَذَابَ

**"Hakika wale waliozikataa Ishara Zetu Tutawaingiza Motoni. Kila zitapowiva ngozi zao Tutawabadilishia ngozi nyengine ili waionje hiyo adhabu". (4:56)**

Katika Aya hii Tukufu, Allah تعالى Amesema:

قُلْ نَارُ جَهَنَّمَ أَشَدُّ حَرًّا لَوْ كَانُوا يَفْقَهُونَ

**"Sema: Moto wa Jahannamu una joto zaidi, laiti wangelifahamu!"**

Kwa maana: Lau kama wangelikuwa wana ufahamu na uelewa wangelijiunga na Mtume ﷺ katika njia ya Allah تعالى katika joto, ili wajikinge dhidi ya joto la Jahannamu, ambalo ni kali mno kuliko hilo waliloliogopa, baada ya hapo, Allah تعالى Anawaonya wanafiki kutokana na kitendo chao hiki, kwa Kusema:

فَلْيَضْحَكُوا قَلِيلًا

**"Basi na wacheke kidogo".**

Ibn Abu Twalha alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alitoa rai: "Maisha ya duniani ni mafupi, basi waache wacheke humo kadiri watakavyo. Uhai utakapotatika na wakaenda kwa Allah تعالى, wataanza kilio ambacho hakitakatika daima".

فَإِنْ رَجَعَلَ اللَّهُ إِلَىٰ طَائِفَةٍ مِّنْهُمْ فَاسْتَدْنُوكَ لِلْخُرُوجِ فَقُلْ لَّنْ نَّخْرُجُوا مَعِيَ أَبَدًا  
وَلَن نُّقَاتِلُوا مَعِيَ عَدُوًّا إِنَّكُمْ رَضِيتُمْ بِالْقُعُودِ أَوَّلَ مَرَّةٍ فَاقْعُدُوا مَعَ الْخَالِفِينَ ﴿٨٥﴾

**83. "Basi Mwenyezi Mungu Akikurudisha kwenye kikundi kimoja miongoni mwao – na wakakutaka idhini ya kutoka – sema: Nyinyi hamtatoka pamoja nami kabisa, wala hamtapigana na adui pamoja nami. Nyinyi mliridhia kukaa nyuma mara ya kwanza, basi kaeni pamoja na hao watakaobakia nyuma".**



**Wanafiki Hawaruhusiwi Kutoka na Waumini Katika Jihadi.**

Allah تعالی Alimuamuru Mtume ﷺ;

فَإِنْ رَجَعَكَ اللَّهُ

**“Basi Mwenyezi Mungu Akikurudisha”.**

Allah تعالی Akikurudisha kutoka katika vita vyako hivi,

إِلَى طَائِفَةٍ مِّنْهُمْ

**“...kwenye kikundi kimoja miongoni mwao”.**

Qatadah alisema, “Tuliambiwa kuwa walikuwa watu kumi na wawili.”<sup>1</sup>

فَأَسْتَدْنُوكَ لِالْخُرُوجِ

**“...na wakakutaka idhini ya kutoka”.**

Wakataka watoke pamoja nawe katika vita nyingine,

فَقُلْ لَنْ تَخْرُجُوا مَعِيَ أَبَدًا وَلَنْ تُقَاتِلُوا مَعِيَ عَدُوًّا

**“...sema: Nyinyi hamtatoka pamoja nami kabisa, wala hamtapigana na adui pamoja nami”.**

Haya ni majibu ya fedheha kwao na kuwaadhibu kwa kutoshiriki na Mtume ﷺ katika vita. Allah تعالی Anataja sababu ya Uamuzi huo kwa Kusema;

إِنْكُمْ رَضِيتُمْ بِالْقُعُودِ أَوْلَ مَرَّةٍ

**“Nyinyi mliridhia kukaa nyuma mara ya kwanza”.**

Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی;

وَوُتِّقِلْبَ أَفِيدَتِهِمْ وَأَبْصَرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا بِهِمْ أَوْلَ مَرَّةٍ

**“Nasi Tunazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyo kuwa hawakuamini mara ya kwanza.” (6:110)**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:404.

Kwani malipo ya ubaya baada yake ni kujitokeza baya la mfano wake, kama vile yalivyo malipo ya jambo jema hupelekea jema jingine. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى kuhusu 'Umrah ya Al-Hudaybiyyah,

سَيَقُولُ الْمُخَلَّفُونَ إِذَا انطَلَقْتُمْ إِلَىٰ مَغَائِمٍ لِّتَأْخُذُوا

**“Walio baki nyuma watasema: Mtapokwenda kuchukua ngawira.”**  
(48:15)

Kauli ya Allah تعالى:

فَأَقْعُدُوا مَعَ الْخَلِيفِينَ

**“...basi kaeni pamoja na hao watakaobakia nyuma”.**

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: “Wanaokusudiwa ni watu waliobakia nyuma badala ya kwenda vitani.”<sup>1</sup>

وَلَا تُصَلِّ عَلَىٰ أَحَدٍ مِّنْهُمْ مَّا تَأْتِي قَبْرَهُ وَلَا تَقُمْ عَلَيْهِ قَبْرَهُ ۚ إِنَّهُمْ كَفَرُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَمَاتُوا وَهُمْ فَسِقُونَ ﴿٨٤﴾

**84. “Wala usimsalie kabisa yeyote katika wao akifa, wala usisimame kaburini kwake. Hakika hao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na wakafa na hali ni wapotofu”.**

### Makatazo Juu ya Kusalia Jeneza za Wanafiki.

Allah تعالى Alimuamuru Mtume Muhammad ﷺ ajibari na wanafiki na asimsalie yeyote katika wao anapofariki, wala asisimame kaburini kwake kumuomba maghufira, au dua, kwa sababu hao wamemkufuru Allah تعالى na Mtume ﷺ, na wakafariki wakiwa katika hali hiyo.

Hukumu hii inamuenea kila ambaye unafiki wake unajulikana wazi, japokuwa sababu ya kushuka kwa Ayah hii ni 'Abdullah bin Ubayy bin Salul, kiongozi wa Wanafiki. Ni sawa na alivyonukuu Bukhari kutoka kwa Ibn 'Umar ambaye alisema, wakati alipofariki 'Abdullah bin Ubayy, alikuja mwanaye, 'Abdullah bin 'abdullah kwa Mtume ﷺ na akamuomba ampe kanzu yake ili aviringishiwe

<sup>1</sup> At-Tabari 14:404.

baba yake - iwe sanda yake, akampa. Halafu akamuomba amsalie, Mtume ﷺ akasimama ili amsalie. 'Umar رضي الله عنه akasimama na kushika nguo ya Mtume ﷺ na kumuambia: "Ewe Mtume! Unamsalia ilhali Mola Wako Amekukataza kumsalia?" Mtume ﷺ akasema:

«إِنَّمَا خَيْرِنِي اللَّهُ فَقَالَ:

*"Bali Allah Alinikhiyarisha kwa Kuniambia:*

أَسْتَغْفِرُ هُمْ أَوْ لَا تَسْتَغْفِرُ هُمْ إِنْ تَسْتَغْفِرَ لَهُمْ سَبْعِينَ مَرَّةً فَلَنْ يَغْفِرَ اللَّهُ لَهُمْ

***"Waombee msamaha au usiwaombee. Hata ukiwa ombea msamaha mara sabini, Mwenyezi Mungu Hatawa samehe."***

وَسَأَزِيدُهُ عَلَى السَّبْعِينَ

*"Nami Nitafanya zaidi ya mara sabini".*

'Umar رضي الله عنه akasema: "Huyu ni Mnafiki". Mtume ﷺ akamsalia, Allah تعالى Akashusha Aya:

وَلَا تُصَلِّ عَلَى أَحَدٍ مِّنْهُمْ مَّتَّ أَبَدًا وَلَا تَقُمْ عَلَى قَبْرِهِ

***"Wala usimsalie kabisa yeyote katika wao akifa, wala usisimame kaburini kwake".<sup>1</sup>***

'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه naye alisimulia sawa na hivyo<sup>2</sup>. Ndani ya masimulizi yake alisema: "Kisha akamsalia halafu akasindikiza jeneza lake, akasimama kaburini kwake, mpaka akamaliza maziko yake. Nikastaajabu namna nilivyothubutu kuzungumza na Mtume ﷺ." Akaendelea: "Wallahi! Hakikupita kitambo, zikashuka Aya hizi mbili;

وَلَا تُصَلِّ عَلَى أَحَدٍ مِّنْهُمْ مَّتَّ أَبَدًا

***"Wala usimsalie kabisa yeyote katika wao akifa".***

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:184.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 8:185.

Baada ya hapo, Mtume ﷺ hakumsalia Mnafiki abadani, wala hakusimama kaburini kwake, mpaka Allah تعالى Alipomfisha<sup>1</sup>. Hivi ndivyo pia alivyoandika At-Tirmidhi katika tafsir na akasema: “Ni *Hasan Sahih*”<sup>2</sup>. Na pia Imam Bukhari ameinukuu.

وَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَأَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ أَنْفُسُهُمْ  
وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٨٥﴾

**85. “Wala zisikutishe mali zao na watoto wao. Mwenyezi Mungu Anataka Kuwaadhibu kwa hayo katika dunia; na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri”.**

Tulishaeleza tafsiri ya Aya inayolingana na hiyo, kila Sifa Njema Anastahiki Allah تعالى na Shukrani ni Zake Yeye.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ahmad 1:16.

<sup>2</sup> Tuhfatul Ahwadhi 8:495.

وَإِذَا أَنْزَلْتَ سُورَةَ أَنْ ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَجَاهِدُوا مَعَ رَسُولِهِ  
 اسْتَعِذْنَاكَ أَوْلُوا الطَّوْلِ مِنْهُمْ وَقَالُوا ذَرْنَا نَكُنْ مَعَ  
 الْقَاعِدِينَ ﴿٨٦﴾ رَضُوا بِأَنْ يَكُونُوا مَعَ الْخَوَالِفِ وَطَبَعَ  
 عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ ﴿٨٧﴾ لَكِنِ الرَّسُولُ  
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ جَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ  
 وَأُولَئِكَ لَهُمُ الْخَيْرَاتُ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٨٨﴾  
 أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا  
 ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٨٩﴾ وَجَاءَ الْمُعَذِّرُونَ مِنَ  
 الْأَعْرَابِ لِيُؤْذَنَ لَهُمْ وَقَعَدَ الَّذِينَ كَذَبُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ  
 سَيُصِيبُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٩٠﴾ لَيْسَ  
 عَلَى الضُّعَفَاءِ وَلَا عَلَى الْمَرْضَى وَلَا عَلَى الَّذِينَ لَا  
 يَجِدُونَ مَا يُنْفِقُونَ حَرَجٌ إِذَا نَصَحُوا لِلَّهِ وَرَسُولِهِ  
 مَا عَلَى الْمُحْسِنِينَ مِنْ سَبِيلٍ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩١﴾  
 وَلَا عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا أَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ قُلْتَ لَا أَجِدُ مَا  
 أَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ تَوَلَّوْا وَأَعْيُنُهُمْ تَفِيضُ مِنَ الدَّمْعِ حَزَنًا أَلَّا  
 يَجِدُوا مَا يُنْفِقُونَ ﴿٩٢﴾ \* إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ  
 يَسْتَعِذُّونَكَ وَهُمْ أَغْنِيَاءُ رَضُوا بِأَنْ يَكُونُوا مَعَ  
 الْخَوَالِفِ وَطَبَعَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٩٣﴾

وَإِذَا أَنْزَلْتَ سُورَةَ أَنْ ءَامِنُوا بِاللَّهِ  
 وَجَاهِدُوا مَعَ رَسُولِهِ اسْتَعِذْنَاكَ أَوْلُوا  
 الطَّوْلِ مِنْهُمْ وَقَالُوا ذَرْنَا نَكُنْ مَعَ  
 الْقَاعِدِينَ ﴿٨٦﴾ رَضُوا بِأَنْ يَكُونُوا  
 مَعَ الْخَوَالِفِ وَطَبَعَ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ  
 لَا يَفْقَهُونَ ﴿٨٧﴾

86. "Na inapoteremshwa Surah isemayo: Muaminini Mwenyezi Mungu na Piganeni Jihadi pamoja na Mtume Wake, wale wenye nguvu miongoni mwao hukutaka ruhusa na husema: Tuache tuwe pamoja na wanao kaa nyuma!".

87. "Wameridhia kuwa pamoja na wabakiao nyuma, na nyoyo zao zikapigwa muhuri; kwa hivyo hawafahamu".

Shutuma kwa Wanao-kataa Kushiriki Jihadi.

Allah تعالیٰ Anawakaripia na Kuwakemea kwa ubaya wa tendo lao wale walioacha kujiunga katika Jihadi na

wanaojiepusha nayo, pamoja na kuwa na uwezo wa kiafya, kinafasi na kimali, badala yake wakamuomba Mtume ﷺ kubaki. Wakasema:

ذَرْنَا نَكُنْ مَعَ الْفَاعِلِينَ

**“Tuache tuwe pamoja na wanaokaa nyuma!”**

Nafsi zao zikaridhia aibu ya kubaki pamoja na wanawake mjini. Kwani wanawake ndio wanaotakiwa kubaki baada ya jeshi kuondoka. Vita vinapoanza, wanakuwa waoga mno na kunapokuwa na amani, basi wanakuwa na maneno mengi (ya majisifu). Kama Allah تعالى Alivyowataja katika Aya nyingine,

فَإِذَا جَاءَ الْخَوْفُ رَأَيْتَهُمْ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ تَدُورُ أَعْيُنُهُمْ كَالَّذِي يُغْتَبَىٰ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۗ  
فَإِذَا ذَهَبَ الْخَوْفُ سَلَقُوكُمْ بِأَلْسِنَةٍ حِدَادٍ

**“Ikifika khofu utawaona wanakutazama na macho yao yanazunguka, kama yule ambaye aliyezimia kwa kukaribia mauti. Na khofu ikiondoka wanakuudhini kwa ndimi kali”. (33:19)**

Maana yake: Hupaza sauti zao kwa maneno makali na ya nguvu, wakati wa amani, lakini vikifika vita wao huwa waoga zaidi. Allah تعالى Alisema katika Aya nyingine;

وَيَقُولُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَوْلَا نُزِّلَتْ سُورَةٌ ۚ فَإِذَا أُنزِلَتْ سُورَةٌ مُحْكَمَةٌ وَذُكِرَ فِيهَا الْقِتَالُ ۗ رَأَيْتَ الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يَنْظُرُونَ إِلَيْكَ نَظَرَ الْمَغْشَىٰ عَلَيْهِ مِنَ الْمَوْتِ ۗ فَأُولَٰئِكَ لَهُمْ طَاعَةٌ وَقَوْلٌ مَّعْرُوفٌ ۚ فَإِذَا عَزَمَ الْأَمْرُ فَلَوْ صَدَقُوا اللَّهَ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُمْ ﴿٢١﴾

**“Na waumini wanasema: Kwa nini haiteremshwi Surah? Na inapoteremshwa Sura madhubuti na ikatajwa ndani yake khabari ya vita, utawaona wenye maradhi katika nyoyo zao wanakutazama mtazamo wa anayezimia kwa mauti. Basi ni bora kwao. Utiifu na kauli njema. Na jambo likiishaazimiwa, basi wakiwa ni wa kweli kwa Mwenyezi Mungu, bila ya shaka itakuwa ni kheri kwao”. (47:20-21) Kauli ya Allah تعالى:**

وَطُوعٌ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ

**“...na nyoyo zao zikapigwa muhuri”.** Kwa sababu ya kutokujiunga kwao na Jihadi na kutoka pamoja na Mtume ﷺ katika njia ya Allah تعالى.

فَهُمْ لَا يَفْقَهُونَ

“...*kwa hivyo hawafahamu*”. Yenye kuwanufaisha ili wayafanye, wala yenye kuwadhuru ili wayaepuke.

لَكِنِ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ جَاهِدُوا بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ ۖ وَأُولَٰئِكَ لَهُمُ  
الْخَيْرَاتُ ۗ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٨٨﴾ أَعَدَّ اللَّهُ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ  
خَالِدِينَ فِيهَا ۚ ذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٨٩﴾

**88. “Lakini Mtume na wale walioamini pamoja naye waliwania Jihadi kwa mali zao na nafsi zao. Hao ndio watakaopata kheri nyingi, na hao ndio wenye kufanikiwa”.**

**89. “Mwenyezi Mungu Amewatengenezea Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Huko ndiko kufuzu kukubwa”.**

Baada ya Allah تعالى Kutaja dhambi za wanafiki Alielezea Sifa Zake juu ya Waumini na malipo yao huko Akhera, Alisema:

لَكِنِ الرَّسُولُ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا مَعَهُ جَاهِدُوا

**“Lakini Mtume na wale walioamini pamoja naye waliwania Jihadi..”.**

Mpaka mwishoni mwa Ayah mbili hizi (9:88-89). Hizi zinabainisha sifa na malipo yao. Kauli ya Allah تعالى:

وَأُولَٰئِكَ لَهُمُ الْخَيْرَاتُ

**“Hao ndio watakao pata kheri nyingi”.** Huko Akhera, katika Pepo za Firdaus na daraja za juu.

وَجَاءَ الْمُعَذِّرُونَ مِنَ الْأَعْرَابِ لِيُؤْذَنَ لَهُمْ وَقَعَدَ الَّذِينَ كَذَبُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۖ سَيُصِيبُ  
الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٩٠﴾

**90. “Na walikuja wenye kutoa udhuru katika Mabedui ili wapewe ruhusa, na wakakaa wale waliomuambia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake uongo. Itawafika waliokufuru katika wao adhabu chungu”.**

Baada ya hapo, Allah تعالى Alieleza hali za waliokuwa na nyudhuru za kweli za kutoshiriki Jihadi, ambao walikuja kwa Mtume ﷺ kumuomba ruhusa na

kumueleza matatizo yao, kama vile kudhoofika na kushindwa kujiunga vitani. Wao walikuwa ni watu waliotokana na makabila ya Waarabu waliokuwa wakiishi katika vitongoji vinavyouzunguka mji wa Madina. Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alikuwa akisoma, "*Wajaa-al-Mu'dhiruwn*", bila kutia shada kwenye "*dha*" na kusema kuwa hawa ni watu waliokuwa na nyudhuru za kweli, kwani baada ya hapo, Allah تعالى Alisema;

وَقَعَدَ الَّذِينَ كَذَبُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ

***"...na wakakaa wale waliomuambia Mwenyezi Mungu na Mtume Wake uongo".***

Maana yake: Hawakuja kuomba ruhusu. Kisha Allah تعالى Akawaonya dhidi ya adhabu iumizayo. Alisema:

سَيُصِيبُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

***"...Itawafika waliokufuru katika wao adhabu chungu".***

لَيْسَ عَلَى الضُّعَفَاءِ وَلَا عَلَى الْمَرْضَى وَلَا عَلَى الَّذِينَ لَا يَجِدُونَ مَا يُنْفِقُونَ حَرَجٌ إِذَا نَصَحُوا لِلَّهِ وَرَسُولِهِ مَا عَلَى الْمُحْسِنِينَ مِنْ سَبِيلٍ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩١﴾  
وَلَا عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا اتَّوَكَّلُوا لِيَتَحْمِلَهُمْ قُلْتُمْ لَا أُجِدُّ مَا أَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ تَوَلَّوْا وَأَعْيُنُهُمْ تَفِيضٌ مِنَ الدَّمْعِ حَزَنًا أَلَّا يَجِدُوا مَا يُنْفِقُونَ ﴿٩٢﴾ \* إِنَّمَا السَّبِيلُ عَلَى الَّذِينَ يَسْتَعِذُّونَكَ وَهُمْ أَغْيَاءٌ رَضُوا بَأَن يُكُونُوا مَعَ الْخَوَالِفِ وَطَبَعَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٩٣﴾

91. ***"Hapana lawama kwa wanyonge, wagonjwa na wasiopata cha kutumia, maadamu wanamsafia niya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hapana njia ya kuwalaumu wanaofanya wema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu".***

92. ***"Wala wale waliokujia ili uwachukue ukasema: Sina kipando cha kukuchukueni. Tena wakarudi na macho yao yanamiminika machozi kwa huzuni ya kukosa cha kutoa".***

93. ***"Ipo njia ya kuwalaumu wale wanaokuomba ruhusa wasiende vitani na hali wao ni matajiri. Wameridhia kuwa pamoja na wanao bakia nyuma. Na Mwenyezi Mungu Amewapiga muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawajui".***



### Nyudhuru Halali za Kisheria Zinazoruhusu Kutokushiriki Jihadi.

Allah تعالی Anabainisha nyudhuru ambazo hakuna ubaya kwa mwenye kuwa nazo kukaa na kutokujiunga na mapigano. Amezitaja kuwa ziko zile ambazo zimeambatana na mtu na hawezi kuepukana nazo, ambazo ni udhaifu wa kimwili unaomzuia kupambana katika Jihadi. Hizo ni pamoja na upofu, ulemavu wa viungo na mfano wake. Baada ya hizo, Anataja sababu zinazojitokeza kwa sababu ya maradhi yaliyompata mwilini mwake, hawezi kujiandaa kwa ajili ya vita. Hakuna ubaya kwa hawa wote kutojiunga na wakawa wanaendelea kutoa nasaha kwa watu wakati wa kukaa kwao, wala hawafanyi uovu kwa kuwatia hofu watu au kujaribu kuwavunja moyo, bali wakawa wanafanya mema katika hali yao hii. Kwa ajili hii, Allah تعالی Amesema:

مَا عَلَى الْمُحْسِنِينَ مِنْ سَبِيلٍ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

***“Hapana njia ya kuwalaumu wanao fanya wema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.***

Al-Awzaa'y رحمه الله تعالی alisema, “Watu walitoka kwenda kuomba mvua *“Istisqaa”* Bilal bi Sa'd akasimama, akamhimidi Allah تعالی na kumsifu, Halafu akasema: “Enyi mliohudhuria hivi hamkubali kuwa ovu limetendeka?” Wakasema: “Ni kweli, Wallahi!” Akasema: “Ewe Allah! Sisi tunakusikilizisha Kauli Yako isemayo;

مَا عَلَى الْمُحْسِنِينَ مِنْ سَبِيلٍ

***“Hapana njia ya kuwalaumu wanaofanya wema”.***

“Ewe Allah تعالی! Tumekiri makosa yetu, Utusamehe, Uturehemu na Utupatie mvua”. Akainua mikono yake, na watu nao wakainua mikono yao, na wakanyeshelezwa mvua”<sup>1</sup>.

Al-Awfi alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Ayah hii, kwamba Mtume ﷺ aliwaamuru watu wamletee watu watakaojiunga naye katika vita. Likamjia kundi katika Masahaba wake, akiwemo 'Abdullah bin Ma'a'qil bin Mukarrin Al-Muzani رضي الله عنه. Wakasema: “Ewe Mtume ﷺ! Tupatie kipando”. Akawaambia: *“Wallahi! Sina kipando cha kukubebeni juu yake.”* Wakaondoka huku wakiwa wanalia na likawawia zito jambo la kutoshiriki katika Jihadi.

<sup>1</sup> Ibn abu Hatim 6:1862.

Kwa kuwa hawana mali ya kutoa wala hawana kipando. Allah تعالى Akaiona juhudi yao katika kumpenda Yeye na Mtume ﷺ. Aliteremsha udhuru wao katika Kitabu Chake kwa Kusema: “*Hapana lawama kwa wanyonge.*” Inaendelea mpaka, “*Kwa hivyo hawajui*”<sup>1</sup>.

Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَلَا عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا أَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ

**“Wala wale waliokujia ili uwachukue”.**

Kwamba Aya hii, “Ilishushwa juu ya Banu Muqarrin kutoka katika kabila la Muzaynah”.<sup>2</sup> Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alimnukuu Al-Hasan رضي الله عنه kuwa alisema: Mtume ﷺ alisema:

وَلَقَدْ خَلَقْتُمْ بِالْمَدِينَةِ أَقْوَامًا مَا أَنْفَقْتُمْ مِنْ نَفَقَةٍ وَلَا قَطَعْتُمْ وَايًّا وَلَا تَلُتُمْ مِنْ عَدُوِّ  
نَيْلًا إِلَّا وَقَدْ سَرَّكُمْ فِي الْأَجْرِ

*“Kuna baadhi ya watu Mmewaacha nyuma yenu mjini Madina, nyinyi hamkutumia mali yoyote, wala hamkuvuka bonde, wala hamkupata matatizo yoyote kutoka kwa adui, ila nao wamekuwa wameshirikiana nanyi katika malipo.”*

وَلَا عَلَى الَّذِينَ إِذَا مَا أَتَوْكَ لِتَحْمِلَهُمْ قُلْتَ لَا أَجِدُ مَا أَحْمِلُكُمْ عَلَيْهِ

**“Wala wale waliokujia ili uwachukue ukasema: Sina kipando cha kukuchukueni”<sup>3</sup>.**

Asili ya Hadithi hii ni katika *Sahih* Mbili kutokana na Hadith hiyo Anas رضي الله عنه alisema, kwamba Mtume ﷺ alisema:

إِنَّ بِالْمَدِينَةِ أَقْوَامًا مَا قَطَعْتُمْ وَايًّا وَلَا سِرْتُمْ سَيْرًا إِلَّا وَهُمْ مَعَكُمْ

*“Hakika Madinah kuna watu, wala nyinyi hamjavuka bonde, wala hamjakwenda mbali, isipokuwa na wao wako pamoja nanyi”.*

<sup>1</sup> At-Tabari 14:420.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:421. Sanadi yake ni dhaifu.

<sup>3</sup> Ibn abu Hatim 6:1863.

Wakauliza: "Tuko nao huku wakiwa Madina?" Akawajibu,

«نَعَمْ حَبَسَهُمُ الْعُدَّةُ»

*"Ndiyo, udhuru umewazuia"<sup>1</sup>.*

Allah تعالی Akawatupia lawama wanaoomba idhini ya kutoshiriki vitani huku ni matajiri, Akawakaripia kwa kuridhika kwao kubakia nyumbani na wanawake walioachwa wakichunga nyumba,

وَطَعَّ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ

***"Na Mwenyezi Mungu Amewapiga muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawajui".***

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 7:732 na Muslim 1911.

يَعْتَذِرُونَ إِلَيْكُمْ إِذَا رَجَعْتُمْ إِلَيْهِمْ<sup>ع</sup> قُلْ لَا تَعْتَذِرُوا لَنْ  
 نُؤْمِنَ لَكُمْ قَدْ نَبَأْنَا اللَّهُ مِنْ أَحْبَابِكُمْ<sup>ع</sup> وَسَيَرَى اللَّهُ  
 عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ ثُمَّ تُرَدُّونَ إِلَىٰ عِلْمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ  
 فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٤﴾ سَيَخْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ  
 إِذَا أَنْقَلَبْتُمْ إِلَيْهِمْ لِتُعْرِضُوا عَنْهُمْ<sup>ط</sup> فَأَعْرِضُوا عَنْهُمْ<sup>ط</sup> إِنَّهُمْ  
 رِجْسٌ<sup>ط</sup> وَمَأْوَهُمْ جَهَنَّمُ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ  
 ﴿٩٥﴾ تَخْلِفُونَ لَكُمْ لِتَرْضَوْا عَنْهُمْ<sup>ط</sup> فَإِنْ تَرْضَوْا عَنْهُمْ  
 فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَىٰ عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٦﴾  
 الْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا حُدُودَ  
 مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ<sup>ط</sup> وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٩٧﴾ وَمِنَ  
 الْأَعْرَابِ مَنْ يَتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ مَغْرَمًا وَيَتَرَبَّصُّ بِكُمِ الدَّوَابِرَ<sup>ع</sup>  
 عَلَيْهِمْ دَائِرَةُ السَّوْءِ<sup>ط</sup> وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٩٨﴾ وَمِنَ  
 الْأَعْرَابِ مَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَيَتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ  
 قُرْبَةً عِنْدَ اللَّهِ وَصَلَوَاتِ الرَّسُولِ<sup>ع</sup> أَلَّا يَأْتِيَ قُرْبَةً هُمْ  
 سَيُدْخِلُهُمُ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ<sup>ط</sup> إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٩﴾

يَعْتَذِرُونَ إِلَيْكُمْ إِذَا رَجَعْتُمْ إِلَيْهِمْ<sup>ع</sup>  
 قُلْ لَا تَعْتَذِرُوا لَنْ نُؤْمِنَ لَكُمْ<sup>ع</sup>  
 قَدْ نَبَأْنَا اللَّهُ مِنْ أَحْبَابِكُمْ<sup>ع</sup>  
 وَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ ثُمَّ  
 تُرَدُّونَ إِلَىٰ عِلْمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ  
 فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٩٤﴾  
 سَيَخْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ إِذَا أَنْقَلَبْتُمْ  
 إِلَيْهِمْ لِتُعْرِضُوا عَنْهُمْ<sup>ط</sup> فَأَعْرِضُوا عَنْهُمْ<sup>ط</sup>  
 إِنَّهُمْ رِجْسٌ<sup>ط</sup> وَمَأْوَهُمْ جَهَنَّمُ جَزَاءً  
 بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٥﴾  
 تَخْلِفُونَ لَكُمْ لِتَرْضَوْا عَنْهُمْ<sup>ط</sup> فَإِنْ  
 تَرْضَوْا عَنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَىٰ  
 عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿٩٦﴾

94. "Watakutoleeni udhuru mtapowarudia. Sema: Msitoe udhuru; hatuku-aminini. Mwenyezi Mungu

*Amekwisha tueleza khabari zenu. Na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wataviona vitendo vyenu. Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; naye Atakuambieni mliyokuwa mkiyatenda".*

95. "Watakuapieni kwa Mwenyezi Mungu mtakaporudi kwao ili muwachilie mbali. Basi wachilieni mbali. Hakika hao ni najisi na makazi yao ni Jahannamu, kuwa ni malipo kwa waliyokuwa wakiyachuma".

**96. “Wanakuapieni ili muwe radhi nao. Basi hata mkiwa radhi nao nyie, Mwenyezi Mungu Hawi radhi na watu wapotofu”.**

**Ubainifu wa Vitimbi vya Wanafiki.**

Allah تعالى Alieleza habari za Wanafiki kwamba pindi wakisharudi Madinah, wataanza kutoa nyudhuru,

قُلْ لَا تَعْتَذِرُوا لَنْ نُؤْمِنَ لَكُمْ

**“Sema: Msitoe udhuru; hatukuaminini”.**

Maana yake: Hatutakusadikini.

قَدْ نَبَأْنَا اللَّهُ مِنْ أَحْبَابِكُمْ

**“Mwenyezi Mungu Amekwishatueleza khabari zenu”.**

Kwa maana: Hali zenu.

وَسِيرَى اللَّهِ عَمَلِكُمْ وَرَسُولِهِ

**“Na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wataviona vitendo vyenu”.**

Kwamba Atavidhihirisha vitendo vyenu kwa watu humu duniani.

ثُمَّ تَرُدُّونَ إِلَىٰ عِلْمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ

**“Kisha mtarudishwa kwa Mjuzi wa siri na dhahiri; Naye Atakuambieni mliyokuwa mkiyatenda”.**

Atakujulisheni amali zenu, za kheri na za shari na Kukulipeni. Kisha Akasema watakuapieni na kutoa Nyudhuru zao ili muache kuwalaumu. Waacheni kwa kuwadharau kwani wao ni,

رَجَسٌ

**“...najisi”.** Kutokana na itikadi yao na batini yao ya unafiki. Na makazi yao ni motoni.

جَزَاءٌ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ

**“...kuwa ni malipo kwa waliyokuwa wakiyachuma”.** Maana: Katika madhambi na makosa waliyochuma, na kwamba ikiwa wataridhia kutokana na viapo vyao.

فَاتَّ اللَّهُ لَا يَرْضَىٰ عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ

**“Mwenyezi Mungu Hawi radhi na watu wapotofu”.**

Wanaotoka nje ya utii wa Allah تعالى na Mtume ﷺ, kwani maana ya *Ufasiki* ni kutoka, ndio maana, panya ameitwa *Fuwaysiqah*, maana yake mwenye kutoka nje ya shimo lake, kwa ajili ya kufanya uharibifu. Pia husemwa, tende *Fasaqat*, yaani zimeharibika pindi zinapochomoka kutoka katika mikungu yake.

الْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا حُدُودَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٩٧﴾  
 وَمِنَ الْأَعْرَابِ مَنْ يَتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ مَغْرَمًا وَيَتَرَبَّصُّ بِكُمُ الدَّوَائِرَ ۗ عَلَيْهِمُ  
 دَائِرَةُ السَّوْءِ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٩٨﴾ وَمِنَ الْأَعْرَابِ مَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ  
 وَيَتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ قُرْبَتٍ عِنْدَ اللَّهِ وَصَلَوَاتِ الرَّسُولِ ۗ أَلَّا يَأْتِيَ قَرْبَةً هُمْ سَيُدْخِلُهُمُ اللَّهُ فِي  
 رَحْمَتِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٩﴾

97. **“Mabedui Wamezidi sana katika ukafiri na unafiki, na wameelekea zaidi kutojua mipaka ya Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume Wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Hikima”.**

98. **“Na katika Mabedui hao wapo wanaofikiri kuwa wanayo yatoa ni gharama ya bure, na wanakungojeleeni mambo yakugeukieni. Mageuko maovu yatakuwa juu yao! Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua”.**

99. **“Na katika Mabedui wapo wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wanaitakidi kuwa wanayoyatoa ndiyo ya kuwasogeza kwa Mwenyezi Mungu na ya kuwapatia dua za Mtume. Naam! Hayo ni kweli mambo ya kuwasogeza. Mwenyezi Mungu Atawaingiza katika Rehema Yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghufira Mwenye Kurehemu”.**

### Mabedui Wamezidi Katika Ukafiri na Unafiki.

Allah تعالى Anaeleza kwamba katika mabedui wapo makafiri, wanafiki na Waumini, na kuwa ukafiri na unafiki wao ni mkubwa zaidi kuliko ulivyo kwa wengine. Wao ni miongoni mwa watu wasiojua kabisa mipaka aliyoishusha Allah تعالى kwa Mtume ﷺ. Ni kama alivyosema Al-A'mash kutoka kwa Ibrahim kuwa: "Kuna bedui mmoja alikaa mkabala na Zayd bin Swuhan ambaye alikuwa akizungumza na marafiki zake, na alikuwa amepoteza mkono wake katika vita vya Nahaawand. Bedui akamuambia: "Wallahi! Nayapenda mazungumzo yako, lakini mkono wako unanitia shaka". Zayd akamuuliza: "Mkono wangu unakupa shaka gani, mbona ni wa kushoto?" Bedui akajibu: "Wallahi! Mimi Sijui (mwizi anapoiba) hukatwa mkono wa kulia ama kushoto?" Zayd bin Sawhan akasema: Allah تعالى Amesema kweli katika Kauli Yake;

الْأَعْرَابُ أَشَدُّ كُفْرًا وَنِفَاقًا وَأَجْدَرُ أَلَّا يَعْلَمُوا حُدُودَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ ۗ

***"Mabedui Wamezidi sana katika ukafiri na unafiki, na wameelekea zaidi kutojua mipaka ya Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu juu ya Mtume Wake"***<sup>1</sup>.

Imamu Ahmad alimnukuu Ibn 'Abbas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَنْ سَكَنَ الْبَادِيَةَ جَفَا، وَمَنْ اتَّبَعَ الصَّيْدَ غَفَلَ، وَمَنْ أَتَى السُّلْطَانَ افْتِنَ»

*"Mwenye kuishi jangwani huwa na moyo mgumu, wenye kufuata mnyama wa kuwinda hughafilika na mwenye kujishirikisha na Mtawala huangukia katika Fitnah"*<sup>2</sup>.

Pia Abu Dawud, At-Tirmidhi na An-Nasai waliikusanya Hadithi hii. At-Tirmidhi alisema: "Ni *Hasan Gharib*"<sup>3</sup> Kuna wakati, Bedui alimpa Mtume ﷺ zawadi, baada ya Bedui huyo kumzawadia Mtume ﷺ; naye alimpa zawadi maradufu ya zile alizopokea mpaka akaridhika. Kisha akasema,

«لَقَدْ هَمَمْتُ أَنْ لَا أَقْبَلَ هَدِيَّةَ إِلَّا مِنْ قُرْبِيِّ أَوْ نَفَقِي أَوْ أَنْصَارِي أَوْ دَوْسِي»

*"Nilitaka kuamua nisipokee zawadi isipokuwa kutoka kwa makabila ya Makuraishi, Thaqafi, Answare au Daws."*<sup>4</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 14:429. Sanadi yake ni dhaifu. <sup>2</sup> Ahmad 1:357.

<sup>3</sup> Abu Dawud 3:278, Tuhfat Al-Ahwadhi 6:532 na An-Nasai 7:195.

<sup>4</sup> Annasaai 6:280.

Kwa sababu hao walikuwa wakiishi katika Miji ya Makkah, Twaif, Madinah na Yemen. Hao ni wenye tabia njema zaidi kuliko mabedui waliokuwa na mioyo migumu. Kauli ya Allah تعالى:

وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Hikima”.**

Kwamba Anawajua wanaostahiki kufundishwa Imani na ilimu, ni Mwenye Hikima kwa namna Alivyoigawa baina ya waja wake katika mambo ya ilimu, ujahili, Imani, ukafiri na unafiki. Allah تعالى Haulizwi kuhusu Ayafanyayo kutokana na Ilimu na Hikima Zake. Allah تعالى Alieleza pia kuwa;

مَنْ يَتَّخِذْ مَا يُنْفِقُ

**“...wapo wanaofikiri kuwa wanayoyatoa”.**

Katika Njia ya Allah تعالى.

مَغْرَمًا

**“...ni gharama ya bure”.** Kwamba ni khasara.

وَيَتَرَىٰ صُكْرًا مُّذَوِّبًا

**“...na wanakungojeleeni mambo yakugeukieni”.**

Maana yake: Wanaosubiri mabalaa na majanga yakufikeni.

عَلَيْهِمْ ذَايِرَةٌ أَلْسُوٓءٌ

**“Mageuko maovu yatakuwa juu yao!”**

Kuwa, badala yake yatawasibu wao kinyume cha matarajio yao.

وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua”.**

Ni Mwenye Kuzisikia dua za waja Wake, ni Mwenye Kuwajua wanaostahiki Kupewa Nusura dhidi ya wenye kustahiki kufedheheshwa. Kauli Yake;

وَمِنَ الْأَعْرَابِ مَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَيَتَّخِذُ مَا يُنْفِقُ قُرْبًا عِنْدَ اللَّهِ  
وَصَلَوَاتِ الرَّسُولِ ﷺ



***“Na katika Mabedui wapo wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wanaitakidi kuwa wanayoyatoa ndiyo ya kuwasogeza kwa Mwenyezi Mungu na ya kuwapatia dua za Mtume”.***

Hawa ni aina ya mabedui wenye kusifika kwa sifa njema. Hawa ni wale wanaochukulia kwamba mali wanayoitoa katika njia ya Allah تعالى ni kujikurubisha Kwake na wakitaraji kuombewa dua na Mtume ﷺ, kutokana na walivyovitoa.

أَلَا إِنَّا قُرْبَةُ هُمْ

***“Naam! Hayo ni kweli mambo ya kuwasogeza”.***

Na watayapata waliyo yataka.

سَيُدْخِلُهُمُ اللَّهُ فِي رَحْمَتِهِ إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٩٤﴾

***“Mwenyezi Mungu Atawaingiza katika Rehema Yake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Maghufira Mwenye Kurehemu.”***

\* \* \*

وَالسَّابِقُونَ<sup>١٠٠</sup> الْأُولُونَ<sup>١٠١</sup> مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ  
 اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ  
 لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ  
 الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٠٠﴾ وَمِمَّنْ حَوْلَكُم مِّنَ الْأَعْرَابِ  
 مُنَافِقُونَ<sup>١٠٢</sup> وَمِنَ أَهْلِ الْمَدِينَةِ<sup>١٠٣</sup> مَرَدُوا عَلَى الْإِنْفَاقِ لَا  
 نَعْلَمُهُمْ<sup>١٠٤</sup> نَحْنُ نَعْلَمُهُمْ<sup>١٠٥</sup> سَنُعَذِّبُهُمْ<sup>١٠٦</sup> مَرَّتَيْنِ ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَى  
 عَذَابٍ عَظِيمٍ ﴿١٠١﴾ وَأَخْرُوجُوا<sup>١٠٧</sup> أَعْرَفُوا بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُوا  
 عَمَلًا صَالِحًا<sup>١٠٨</sup> وَأَخْرَسَيْنَا<sup>١٠٩</sup> عَيْ أَلَّهِ أَنْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ<sup>١١٠</sup> إِنَّ  
 اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠٢﴾ خُذْ<sup>١١١</sup> مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ  
 وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا<sup>١١٢</sup> وَصَلِّ عَلَيْهِمْ<sup>١١٣</sup> إِنَّ صَلَاتَكَ سَكَنٌ لَهُمْ<sup>١١٤</sup> وَاللَّهُ  
 سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٣﴾ أَلَمْ يَعْلَمُوا<sup>١١٥</sup> أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ  
 عِبَادِهِ وَيَأْخُذُ<sup>١١٦</sup> الصَّدَقَاتِ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ الرَّحِيمُ  
 ﴿١٠٤﴾ وَقُلْ<sup>١١٧</sup> أَعْمَلُوا<sup>١١٨</sup> فَسَيَرَى<sup>١١٩</sup> اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ  
<sup>١٢٠</sup> وَسَتُرَدُّونَ<sup>١٢١</sup> إِلَى<sup>١٢٢</sup> عِلْمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنشِرُكُمْ<sup>١٢٣</sup> بِمَا كُنتُمْ  
 تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾ وَأَخْرُوجُوا<sup>١٢٤</sup> مُرْجُونَ<sup>١٢٥</sup> لِأَمْرِ اللَّهِ<sup>١٢٦</sup> إِمَّا يُعَذِّبُهُمْ  
 وَإِمَّا يَتُوبُ عَلَيْهِمْ<sup>١٢٧</sup> وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٠٦﴾

وَالسَّابِقُونَ<sup>١٠٠</sup> الْأُولُونَ<sup>١٠١</sup> مِنَ  
 الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ  
 اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ  
 وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ  
 تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا  
 أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٠٠﴾

100. "Na wale walio-  
 tangulia, wa kwanza,  
 katika Wahajiri na Ansari,  
 na waliowafuata kwa  
 wema. Mwenyezi Mungu  
 Ameridhika nao, na wao  
 wameridhika Naye; na  
 Amewaandalia Bustani  
 zipitazo mito kati yake,  
 wadumu humo milele.  
 Huko ndiko Kufuzu  
 kukubwa".

Fadhila za Muhajiruna,  
 Answar na Waliowafuta  
 kwa Wema.

Allah تعالى Anatoa habari ya  
 Kuwaridhia Kwake Muha-

jiruna na Answari na wanaowafuata wao kwa wema, na Radhi Zake kwao ni  
 yale Aliyowaandalia Kuwapa miongoni mwa pepo zenye neema ya kudumu.  
 Ash-Sha'bi alisema,

وَالسَّابِقُونَ<sup>١٠٠</sup> الْأُولُونَ<sup>١٠١</sup> مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ

"Na wale waliotangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari".

Na wale ambao walidiriki kiapo cha maridhiano *Bay'atu ya Ar-Ridhwaan* katika mwaka wa mkataba wa Hudaybiyyah<sup>1</sup>. Abu Musa Al-Ash-'Ari, Sa'id bin Al-Musayyab, Muhammad bin Seeren, Al-Hasan na Qatadah رضي الله عنهم walisema: Watu hao ni wale ambao walisali kuelekea kibla mbili pamoja na Mtume ﷺ [kwanza kuelekea Jerusalem na baadaye Al-Ka'bah].<sup>2</sup>

Allah تعالى Alieleza kuwa Yeye Ameshawaridhia waliotangulia wa mwanzo katika Muhajiruna na Ansvar na waliowafuata kwa ihsani, basi ole wao wanaowachukia au kuwalaani, khasa mbora wa Masahaba baada ya Mtume ﷺ, mwenye fadhila zaidi kuliko Masahaba wote, msadikishaji mkubwa na Khalifa Mkuu, Abubakr bin Abu Quhafah رضي الله عنه. Kikundi cha wenye kufedheheshwa, *Ar-Rafidhah* (Mashia) wanawafanyia uadui – walio wabora – Masahaba wenye fadhila nyingi, na huwatukana na kuwalaani. Allah تعالى Atukinge dhidi yao. Hii inaonesha kwamba akili zao zimegeuzwa na nyoyo zao zimepinduliwa juu chini, basi imani yao kuhusu Qur'an ipo wapi? Wanawalaani wale ambao Allah تعالى Yuko radhi nao. Ama watu wa Sunna huwaridhia wale ambao Allah تعالى Yuko radhi nao, na huwalaani wale ambao wamelaaniwa na Allah تعالى na Mtume ﷺ. Wao ni waaminifu kwa wapenzi wa Allah تعالى na huwapiga vita maadui wa Allah تعالى. Wao ni wafuasi, wala si wenye kuanzisha (bida'a), hufuata Sunnah, na siyo wazushi. Hawa ndio kundi la Allah تعالى lililofaulu na wao ndio waja Wake Waumini.

وَمِمَّنْ حَوْلَكُم مِّنَ الْأَعْرَابِ مُنْفِقُونَ<sup>ط</sup> وَمِنَ أَهْلِ الْمَدِينَةِ<sup>ط</sup> مَرُدُّوْا عَلَى الْيَفَاقِ لَا تَعْلَمُهُمْ<sup>ط</sup> حَتَّىٰ تَعْلَمَهُمْ<sup>ط</sup> سَنُعَذِّبُهُمْ مَّرَّتَيْنِ ثُمَّ يُرَدُّوْنَ إِلَىٰ عَذَابٍ عَظِيمٍ ﴿١٠١﴾

**101. “Na katika mabedui walio jirani zenu wamo wanafiki; na katika wenyeji wa Madinah pia wapo waliobobeza katika unafiki. Wewe huwajui. Sisi Tunawajua. Tutawaadhibu mara mbili, kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa”.**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:435.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:436, 437, 439.

## Wanafiki Mabedui wa Madinah

Allah تعالیٰ Anamuambia Mtume ﷺ kwamba miongoni mwa mabedui wanaoishi vitongoji vyenye kuzunguka Madinah kuna wanafiki. Pia kuna watu wa Madinah ambao nao ni wanafiki,

مَرَدُوا عَلَىٰ الْبِفَاقِ

“...**waliobobea katika unafiki**”. Maana yake: Wameshikamana na unafiki na wakaendelea nao. Mfano wa neno *Maradu* (waliobobea) lililotumika katika Aya, husemwa *Shaytwaan Mariyd* na *Shaytwaan Maarid*. Pia husemwa, fulani ame-*tamarad* kwa Allah تعالیٰ, kwa maana ya kwamba ameeasi na kufanya kiburi. Kauli ya Allah تعالیٰ;

لَا تَعْلَمُهُمْ حَتَّىٰ تَعْلَمَهُمْ

“**Wewe huwajui. Sisi Tunawajua**”.

Aya hii haikinzani na Kauli Yake nyingine,

وَلَوْ نَشَاءُ لَأَرَيْنَاكَهُمْ فَلَعَرَفْتَهُمْ بِسِيمَاهُمْ ۗ وَلَتَعْرِفَنَّهُمْ فِي لَحْنِ الْقَوْلِ

“**Na Tungelipenda kukuonesha hao na ungeliwatambua kwa alama zao; lakini bila ya shaka utawajua kwa namna ya msemo wao**”.

(47:30)

Kwa sababu Aya hii ya pili inawataja kwa alama na sifa wanazojulikana kwazo, si kwamba anawajua wote walioko kwake katika wale wenye unafiki na wenye shaka kuwajua mmoja mmoja. Mtume ﷺ alikuwa akijua kwamba baadhi ya watu wa Madina anaochanganyika nao ni wanafiki, japokuwa walikuwa akionana nao asubuhi na jioni (hakuwajua kwamba ni akina nani hasa). Imekwisha tangulia tafsir ya Kauli ya Allah تعالیٰ:

وَهُمُومَا لَمْ يَنَالُوا

“**Na wakajihimu kufanya ambayo hawakuweza kuyafikia**”. (9:74)

Kwamba Mtume ﷺ alimjulisha Hudhaifah رضي الله عنه majina ya wanafiki kumi na wanne au kumi na watano. Hii ni makhsusi, haimaanishi kwamba alimtajia majina ya wanafiki wote. *Allah Aalam*.

‘Abdur-Razzaq alisema: Ma‘mar alitufahamisha kuwa Qatadah alitolea rai Ayah hii (9:101) kuwa: “Wengine wamepatwa na nini kwa kudai wanawajua wenzao,

kuwa, “Fulani ni wa Peponi na fulani wa Motoni”. Ukimuuliza juu ya nafsi yake, atasema, “Sijui (kama nitaishi Peponi ama Motoni)!” Hakika, unaijua vyema nafsi yako kuliko wengine. Umejikalifisha kufanya kazi ambayo hata Mitume kabla yako hawakujilazimisha kuifanya. Nabii wa Allah ﷺ, Nuh عليه السلام alisema:

وَمَا عَلَّمِي بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٦﴾

**“Nayajuaje waliyokuwa wakiyafanya?” (26:112)**

Nabii Shu’ayb عليه السلام naye alisema,

بَقِيَّتُ اللَّهِ خَيْرٌ لَّكُمْ إِن كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ۗ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِحَفِيظٍ ﴿١١٨﴾

**“Alivyokubakishieni Mwenyezi Mungu ndiyo bora kwa ajili yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini. Wala mimi siye Mlinzi wenu.” (11:86)**

Na Allah ﷻ Alimuambia Mtume Muhammad ﷺ.

لَا تَعْلَمُهُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَهُمْ ۗ

**“Wewe huwajui. Sisi Tunawajua”<sup>1</sup>**. Mujahid alizungumzia Kauli ya Allah ﷻ;

سَتَعْلَمُهُمْ مَرَّتَيْنِ

**“Tutawaadhibu mara mbili”<sup>2</sup>**. Maana yake: Kuwaua na kuwateka. Katika masimulizi mengine, alisema, mara mbili hizo ni njaa na adhabu ya kaburini.

ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَىٰ عَذَابٍ عَظِيمٍ

**“...kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa”<sup>2</sup>**. ‘Abdur-Rahman bin Zayd alisema: “Adhabu ya duniani ni mali na watoto”. Kisha akasoma Kauli ya Allah ﷻ:

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ ۗ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

**“Yasikufurahishe mali zao wala wana wao. Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kuwaadhibu kwayo hapa duniani”. (9:55)**

Masaibu haya kwao ni adhabu, lakini kwa waumini ni malipo. Na adhabu ya Akhera ni kuingizwa Motoni.

<sup>1</sup> ‘Abdur-Razzaq 2:285.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:442.

ثُمَّ يُرَدُّونَ إِلَىٰ عَذَابٍ عَظِيمٍ

**“Kisha watarudishwa kwenye adhabu kubwa”.**

Alisema kuwa maana yake ni Motoni.<sup>1</sup>

وَأَخْرُونَ أَعْتَرَفُوا بِذُنُوبِهِمْ خَلَطُوا عَمَلًا صَالِحًا وَآخَرَ سَيِّئًا عَسَىٰ اللَّهُ أَن يَتُوبَ عَلَيْهِمْ  
 إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٠٢﴾

**102. “Na wengine walikiri dhambi zao, wakachanganya vitendo vyema na vingine viovu. Asaa Mwenyezi Akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu”.**

**Waumini Ambao Hawakujiunga na Jihadi kwa Sababu ya Uvivu.**

Baada ya Allah تعالى Kubainisha hali za wanafiki wenye kujibakisha nyuma dhidi ya vita kwa njia ya kuvichukia, kukadhibisha na kuwa na shaka, Aliingia katika Kueleza hali za wakosefu ambao hawakujiunga na Jihadi kwa sababu ya Uvivu na kupenda raha, japo wana imani na kusadiki ukweli. Alisema:

وَأَخْرُونَ أَعْتَرَفُوا بِذُنُوبِهِمْ

**“Na wengine walikiri dhambi zao”.**

Maana yake: Walikiri na kukubali yaliyo baina yao na Mola wao, na wao wana amali nyingine njema, wamezichanganya na dhambi. Hawa wako chini ya msamaha na maghufira ya Allah تعالى. Ingawa Ayah hii ilishushwa kuwahu watu makhsusi, lakini inawaenea kila watenda dhambi na wakosefu wenye kuchanganya mema na maovu, wenye kuchafuka kwa maovu. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema:

وَأَخْرُونَ

**“Na wengine”.** Aya hii ilishuka kumhusu Abu Lubabah na kikundi cha Masahaba ambao hawakujiunga na Mtume ﷺ katika vita vya Tabuk. Baadhi yao wakasema: “Ni Abu Lubabah na watu wengine watano pamoja naye”. Pia ilisemwa: “Na wengine saba pamoja naye”. Tena ilisemwa, “Na wengine tisa pamoja naye”. Baada ya Mtume ﷺ kurejea kutoka vitani, walijifunga katika

<sup>1</sup> At-Tabari 14:444.

nguzo za Msikitini na wakaapa kwamba Mtume ﷺ ndiye atakayewafungua kutoka kwenye nguzo hizo. Baada ya Allah تعالى Kuishusha Ayah hii:

وَأَخْرُونَ أَعْرَفُوا بِدُنُوبِهِمْ

**“Na wengine walikiri dhambi zao”.**

Mtume ﷺ aliwafungua na kuwasamehe”.<sup>1</sup> Al-Bukhari alipokea kutoka kwa Samura bin Jundubi رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema:

«أَنَا فِي اللَّيْلَةِ آتِيَانِ فَابْتَعَنَانِي، فَانْتَهَبَا بِي إِلَى مَدِينَةِ مَنِيَّةَ بَلَيْنِ ذَهَبٍ وَلَبِنِ فِضَّةٍ فَتَلَقَانَا رَجَالٌ شَطْرُ مِنْ خَلْفِهِمْ كَأَحْسَنِ مَا أَنْتَ رَأَيْتَ، وَشَطْرُ كَأَفْبَحِ مَا أَنْتَ رَأَيْتَ، قَالَا لَهُمْ: اذْهَبُوا فَعَمُوا فِي ذَلِكَ النَّهْرِ فَوَقَعُوا فِيهِ ثُمَّ رَجَعُوا إِلَيْنَا قَدْ ذَهَبَ ذَلِكَ الشُّؤْءُ عَنْهُمْ فَصَارُوا فِي أَحْسَنِ صُورَةٍ، قَالَا لِي: هَذِهِ جَنَّةٌ عَذْبٌ وَهَذَا مَثْرَلُكَ، قَالَا: وَأَمَّا الْقَوْمُ الَّذِينَ كَانُوا شَطْرُ مِنْهُمْ حَسَنٌ وَشَطْرُ مِنْهُمْ قَبِيحٌ، فَإِنَّهُمْ خَلَطُوا عَمَلًا صَالِحًا وَآخَرَ سَيِّئًا تَجَاوَزَ اللَّهُ عَنْهُمْ»

*“Usiku wa leo wamenijia Malaika Wawili (ndotoni) na kunipeleka katika mji uliojengwa kwa matofali ya dhahabu na fedha. Tukakutana na watu wakiwa na upande mmoja uliokuwa mzuri sana ambao hujapata kuuona, na upande mwingine mbaya sana, hujapata kuuona. Malaika hao wawili wakawaambia: “Nendeni mkajitumbukize katika mto ule”. Wakajitumbukiza, kisha wakarudi kwetu huku ule ubaya umewatoka na wakawa katika hali nzuri sana. Malaika wawili wakaniambia: “Hii ni Pepo ya ‘Adn, na haya ndio makazi yako. Watu hao ambao walikuwa upande mmoja mzuri na mwingine mbaya, ni waliochanganya matendo mema na mengine mabaya, Allah Akawasamehe”.*<sup>2</sup>

Al-Bukhari aliinukuu Hadithi hii kwa mukhtasari katika kuitafsiri Ayah hii.

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِمْ بِهَا وَصَلِّ عَلَيْهِمْ إِنَّ صَلَاتَكَ سَكَنٌ لَهُمْ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٩١﴾ أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ وَيَأْخُذُ الصَّدَقَاتِ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ أَتَوْابٌ الرَّحِيمُ ﴿٩٢﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 14:437 Masimulizi haya si *Sahih*. Kuna masimulizi *Mursal* yanayolingana na haya, kutoka kwa Sa'id bin Al-Musayyab katika *Dalail An-Nubuwwah*.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 8:193.

**103. “Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua”.**

**104. “Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Amepokea toba ya waja wake, na Anazikubali sadaka na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kupokea toba na Mwenye Kurehemu?”**

### **Amri ya Kukusanya Zaka na Kubainisha Faida Zake.**

Allah تعالی Alimuamuru Mtume ﷺ achukue Zaka kutoka katika mali zao ambayo itawatwaharisha na kuwatakasa. Amri hii ni yenye kuenea kwa wote, hata kama wengine wanakirejesha kiwakilishi kilichopo “katika mali zao”, kwamba ni wale waliokiri madhambi yao na wakachanganya amali njema na nyingine mbaya. Kwa ajili hii, baadhi ya mabedui waliokuwa wakizuia Zaka walidhani kwamba jambo la kumpa kiongozi Zaka halipo, kwani hii ilikuwa makhsusi kwa Mtume tu na wanatumia Kauli ya Allah تعالی ifuatayo kama ushahidi,

خُذْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ صَدَقَةً

**“Chukua sadaka katika mali zao”.** Abubakr As-siddiq رضي الله عنه na Masahaba wengine رضي الله عنهم waliwakatalia tafsiri yao hiyo na ufahamu wao mbaya, kisha alipigana nao mpaka wakakubali kutoa Zaka kwa Khalifah, sawa na walivyokuwa wakitoa kwa Mtume ﷺ. Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه akasema: “Wallahi! Kama wangelijizua kuikusanya kwangu japo mbuzi mdogo, na katika masimulizi mengine japo kamba ya kumfungia mbuzi ningewapiga kwa sababu ya kukataa kwao kuikusanya Zaka”<sup>1</sup>. Kauli ya Allah تعالی:

وَصَلِّ عَلَيْهِمْ

**“...na uwaombee rehema.”** Maana: Waombee dua na maghufira. Ushahidi wa tafsiri hii ni kama alivyoandika Muslim ndani ya *Sahih* yake kwamba ‘Abdullah bin Abu Awfa رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alipokuwa akiletewa Zaka na watu alikuwa akiwaombea, siku moja Baba yangu akampelekea Zaka yake, Mtume akaomba dua akisema;

«اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى آلِ أَبِي أَوْفَى»

**“Ewe Allah! Nakuomba Uwape rehema familia ya Abu Awfa”<sup>1</sup>.**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 13:264.

<sup>2</sup> Muslim 2:756.



Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ صَلَاتَكَ سَكَنٌ لَهُمْ

**“Hakika maombi yako ni utulivu kwao”.**

Aya hii ina aina mbili za usomaji, neno “Sala” limesomwa kwa umoja na wingi. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Maana yake ni rehema kwao”<sup>1</sup>. Kauli ya Allah

تعالى:

وَاللَّهُ سَمِيعٌ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia”.** Kuzisikia dua zako.

عَلِيمٌ

**“Mwenye Kujua”.** Anajua juu ya wenye kuistahiki dua hiyo na ambao ndio watu wa kuombewa. Kauli ya Allah تعالى:

الَّذِينَ يَعْلَمُونَ أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ وَيَأْخُذُ الصَّدَقَاتِ

**“Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Amepokea toba ya waja wake, na Anazikubali sadaka”.**

Aya hii inamaanisha jambo la kuleta toba na kutoa Sadaka. Haya ni mambo mawili ambayo kila moja linafuta na kuyaondosha madhambi. Allah تعالى Ameeleza tena kuwa: Kila mwenye kufanya toba, Yeye Atamkubalia, na mwenye kutoa Sadaka kutoka katika pato la halali, basi Yeye Ataipokea kwa Mkono Wake wa Kuume na Kumtunzia Mtoaji na Kuikuza kama itakuwa ni sadaka ya tende itafikia mithili ya mlima Uhud. Kwa ushahidi wa Hadithi inayoelezea hili kuwa Abu Hurayra رضي الله عنه alieleza kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alisema:

«إِنَّ اللَّهَ يَقْبَلُ الصَّدَقَةَ وَيَأْخُذُهَا بِيَمِينِهِ فَيُرِيهَا لِأَحَدِكُمْ كَمَا يُرِي أَحَدَكُمْ مَهْرَهُ، حَتَّى  
إِنَّ اللَّفْظَةَ لَتَكُونُ مِثْلَ أَحَدٍ»

**“Hakika Allah Hupokea Sadaka na kuichukua kwa Mkono Wake wa Kuume na Kuitunza kwa ajili ya mmoja wenu kama ambavyo mmoja wenu humtunza mwana farasi wake, mpaka tonge moja la chakula linakuwa mpaka kufikia mithili ya mlima Uhud”.**

Haya yanasadikishwa na Kitabu cha Allah تعالى Aliposema:

<sup>1</sup> At-Tabari 14:457.

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ وَيَأْخُذُ الصَّدَقَاتِ

**“Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anakubali toba ya waja wake, na Anazikubali sadaka”.**

Kauli ya Allah تعالى;

يَمْحَقُ اللَّهُ الرِّبَا وَيُرِي الصَّدَقَاتِ

**“Mwenyezi Mungu Huiondolea baraka riba, na Huzibariki sadaka”.**  
(2:276)<sup>1</sup>

‘Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema: “Sadaka huingia Mkononi mwa Allah تعالى kabla ya kufikia Mkononi mwa muombaji”. Kisha akaisoma Aya ifuatayo:

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ وَيَأْخُذُ الصَّدَقَاتِ

**“Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anakubali toba ya waja wake, na Anazikubali sadaka”.**<sup>2</sup> (9:104)

وَقُلْ أَعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ عِلِّيِّمِ  
وَالشَّهَادَةِ فَيُنبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

**105. “Na sema: Tendeni vitendo. Na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Waumini wataviona vitendo vyenu. Na mtarudishwa kwa Mwenye Kujua siri na dhahiri; Naye Atakuambieni mliyokuwa mkiyatenda”.**

**Onyo kwa Waasi.**

Mujahid alisema kwamba hili ni onyo<sup>3</sup> kutoka kwa Allah تعالى kwenda kwa wenye kuzikhalifu Amri Zake, kwamba amali zao zitadhihirishwa kwa Allah تعالى, kwa Mtume ﷺ na kwa Waumini. Hili litatukia katika Siku ya Kiyama bila ya shaka yoyote. Kwa ushahidi wa Kauli nyingine ya Allah تعالى;

يَوْمَئِذٍ تُعْرَضُونَ لَا تَخْفَىٰ مِنْكُمْ خَافِيَةٌ ﴿١٠٦﴾

**“Siku hiyo mtahudhurishwa – haitafichika siri yoyote yenu”.** (69:18)

<sup>1</sup> At-Tabari 14:461.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:460.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:463.

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ﴿٩١﴾

**“Siku zitakapo dhihirishwa siri”. (86:9) Aidha Amesema,**

وَحُصِّلَ مَا فِي الصُّدُورِ ﴿١٠٠﴾

**“Na yakakusanywa yaliyomo vifuani?” (100:10)**

Yaweze kana Allah تعالى Akadhihirisha baadhi ya amali za watu humuhumu duniani. Bukhari alisema, ‘Aisha رضي الله عنها alisema: “Zikikupendeza amali njema za Muislam, basi sema;

أَعْمَلُوا فَسَيَرَى اللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ

**“Tendeni vitendo. Na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake na Waumini wataviona vitendo vyenu”<sup>1</sup>.**

Kuna Hadithi iliyonukuliwa ambayo inashabihiana na hayo,

«لَا عَلَيْكُمْ أَنْ تُعْجَبُوا بِأَحَدٍ حَتَّى تَنْظُرُوا بِمِ بَخْتَمِ لَهُ، فَإِنَّ الْعَامِلَ يَعْمَلُ زَمَانًا مِنْ عُمْرِهِ - أَوْ بَرَهَةً مِنْ دَهْرِهِ - . يَعْمَلُ صَالِحٍ لَوْ مَاتَ عَلَيْهِ دَخَلَ الْجَنَّةَ ثُمَّ يَنْتَحَوِلُ فَيَعْمَلُ عَمَلًا سَيِّئًا، وَإِنَّ الْعَبْدَ لَيَعْمَلُ الْبَرَهَةَ مِنْ دَهْرِهِ بِعَمَلٍ سَيِّئٍ، لَوْ مَاتَ عَلَيْهِ دَخَلَ النَّارَ ثُمَّ يَنْتَحَوِلُ فَيَعْمَلُ عَمَلًا صَالِحًا، وَإِذَا أَرَادَ اللَّهُ بِعَبْدِهِ خَيْرًا اسْتَعْمَلَهُ قَلِيلَ مَوْتِهِ»

*“Msifurahishwe na amali za mmoja wenu mpaka muone mwisho wa matendo yake unakuwaje. Kwani, mmoja wenu anaweza kufanya amali njema kwa kipindi au muda fulani katika umri wake kiasi kwamba akifa akiwa katika hali hiyo ataingia Peponi. Kisha anabadilika na kufanya amali mbaya. Mja mwingine anaweza kufanya amali mbaya katika kipindi fulani katika umri wake kiasi akifa akiwa katika hali hiyo ataingia Motoni, kisha anabadilika na kufanya amali njema. Allah Anapomtakia kheri mja wake, humtumikisha kabla ya umauti wake”*

Wakauliza: “Ewe Mtume! Humtumikisha vipi?” Naye alijibu,

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 13:512.

«يُوقَفُهُ لِعَمَلٍ صَالِحٍ ثُمَّ يَبْرِئُهُ عَلَيْهِ»

*"Anamuwafikisha kufanya amali njema, halafu Anamfisha angali katika hali hiyo"*<sup>1</sup>.

Imamu Ahmad peke yake ndiye aliyenukuu.

وَأَخْرُوتُ مُرَجُونَ لِأَمْرِ اللَّهِ إِمَّا يُعَذِّبُهُمْ وَإِمَّا يَتُوبُ عَلَيْهِمْ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١٠٦﴾

**106. "Na wapo wengine wanangojea Amri ya Mwenyezi Mungu – ama Atawaadhibu au Atawasamehe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima".**

**Kucheleweshwa Uamuzi kwa Masahaba Watatu Ambao Hawakushiriki Katika Vita vya Tabuk.**

Ibn 'Abbas, Mujahid, 'Ikrimah, Adh-Dhahhak na wengine رضي الله عنهم walisema, "Hao ni masahaba Watatu ambao walisubirishwa ili ijulikane kama toba yao imekubaliwa. Hao ni Murarah bin Ar-Rabi', Ka'b bin Malik na Hilaal bin Umayyah رضي الله عنهم wao ni miongoni mwa wale ambao hawakushiriki vita vya Tabuk kwa sababu ya uvivu, kukhitari raha, wepesi, matunda yaliyoiva na kivuli, si kwa sababu ya kuwa na mashaka na unafiki. Miongoni mwao, walikuwepo waliojifunga katika nguzo za Masjid, kama alivyofanya Abu Lubabah na marafiki zake رضي الله عنهم. Wengine hawakufanya hivyo, nao ni hao Watatu waliotajwa. Msamaha kwa ajili ya akina Lubabah رضي الله عنه ulishuka kabla ya hao Watatu. Mpaka ikashuka Ayah ifuatayo:

لَقَدْ تَابَ اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ

**"Mwenyezi Mungu Amekwishapokea toba ya Nabii na Wahajiri na Ansari". (9:17)**

وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خَلَفُوا حَتَّىٰ إِذَا صَافَتْ عَلَيْهِمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ

**"Na pia wale Watatu walioachwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjufu wake..." (9:18)<sup>2</sup>**

<sup>1</sup> Ahmad 3:120.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:465-466.

Ufafanuzi wake utaelezwa baadaye, katika Hadithi ya Ka'b bin Malik رضي الله عنه.  
Kauli ya Allah تعالى:

إِمَّا يُعَذِّبُهُمْ وَإِمَّا يَتُوبُ عَلَيْهِمْ

***“Ama Atawaadhibu na Atawasamehe”.***

Maana: Wao katika kupata msamaha wa Allah تعالى, ama Akitaka Atawahukumu hivi au Awahukumu vinginevyo, lakini Rehema Zake Huzishinda Ghadhabu Zake.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

***“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima”.***

Maana yake: Anawajua wanaostahiki adhabu na wenye kustahiki msamaha, ni Mwenye Hikima katika Matendo Yake na Kauli Zake, hapana Mola mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye, wala hapana Mola Mlezi asiyekuwa Yeye.

\* \* \*

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مَسْجِدًا ضِرَارًا  
وَكُفْرًا وَتَفْرِيقًا بَيْنَ  
الْمُؤْمِنِينَ وَإِرْصَادًا لِمَنْ حَارَبَ  
اللَّهُ وَرَسُولَهُ مِنْ قَبْلُ<sup>٤</sup> وَلِيُخْلِفَنَّ  
إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا الْحُسْنَى<sup>٥</sup> وَاللَّهُ يَشْهَدُ  
لَهُمْ لَكُذِبُونَ ﴿١٠٧﴾ لَا تَقُمْ فِيهِ  
أَبْدًا<sup>٦</sup> لِمَسْجِدٍ أُسِّسَ عَلَى  
التَّقْوَى مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَنْ  
تَقُومَ فِيهِ<sup>٧</sup> فِيهِ رِجَالٌ  
مُحِبُّونَ أَنْ يَتَطَهَّرُوا<sup>٨</sup> وَاللَّهُ  
يُحِبُّ الْمُطَهَّرِينَ ﴿١٠٨﴾ أَفَمَنْ  
أَسَّسَ بُنْيَانَهُ عَلَى تَقْوَى مِنْ  
اللَّهِ وَرِضْوَانٍ خَيْرٌ أَمْ مَنْ  
أَسَّسَ بُنْيَانَهُ عَلَى شَفَا جُرُفٍ  
هَارٍ فَاتَّخَذَ بِهِ فِي نَارِ جَهَنَّمَ<sup>٩</sup>  
وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٩﴾ لَا  
يُرَالُ بُنْيَانُهُمُ الَّذِي بَنَوْا رِيبَةً  
فِي قُلُوبِهِمْ إِلَّا أَنْ تَقَطَّعَ  
قُلُوبُهُمْ<sup>١٠</sup> وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١١٠﴾ \*  
إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنْ الْمُؤْمِنِينَ  
أَنْفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَنْ لَهُمُ  
الْجَنَّةُ<sup>١١</sup> يُقْبَلُونَ فِيهَا بِغَيْرِ  
حَقٍّ فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْفُرْآنِ<sup>١٢</sup>  
وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنْ اللَّهِ<sup>١٣</sup>  
فَأَسْتَبِشِرُوا بِبَيْعِكُمْ الَّذِي بَايَعْتُمْ  
بِهِ<sup>١٤</sup> وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١١١﴾

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مَسْجِدًا ضِرَارًا  
وَكُفْرًا وَتَفْرِيقًا بَيْنَ  
الْمُؤْمِنِينَ وَإِرْصَادًا لِمَنْ حَارَبَ  
اللَّهُ وَرَسُولَهُ مِنْ قَبْلُ<sup>٤</sup> وَلِيُخْلِفَنَّ  
إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا الْحُسْنَى<sup>٥</sup> وَاللَّهُ يَشْهَدُ  
لَهُمْ لَكُذِبُونَ ﴿١٠٧﴾ لَا تَقُمْ فِيهِ  
أَبْدًا<sup>٦</sup> لِمَسْجِدٍ أُسِّسَ عَلَى  
التَّقْوَى مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَنْ  
تَقُومَ فِيهِ<sup>٧</sup> فِيهِ رِجَالٌ  
مُحِبُّونَ أَنْ يَتَطَهَّرُوا<sup>٨</sup> وَاللَّهُ  
يُحِبُّ الْمُطَهَّرِينَ ﴿١٠٨﴾

107. "Na wapo waliojenga Msikiti kwa ajili ya madhara na ukafiri na kuwafarakisha Waumini, na pa kuvizia kwa walio mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hapo kabla. Na bila ya shaka wataapa kwamba: Hatukukusudia ila wema tu. Na Mwenyezi Mungu

Anashuhudia kuwa wao ni waongo".

108. "Usisimame kwenye Msikiti huo kabisa. Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa ucha Mungu tangu siku ya mwanzo unastahiki zaidi wewe usimame ndani yake. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaojitakasa".

## Msikiti Uliojengwa kwa Lengo la Kuwagawa Watu, na Uliojengwa kwa lengo la Uchaji Mungu

Sababu za kushushwa kwa Ayah hizi tukufu, ni kuwa, kabla ya kufika kwa Mtume ﷺ Madinah, alikuwepo mtu mmoja wa Kikhazraji aliyekuwa akiitwa Abu 'Amir Ar-Rahib ambaye katika wakati wa ujahili aliingia katika Ukristo na akasoma elimu ya Ahlu-Kitabu. Katika ujahili, Abu 'Amir alikuwa anajulikana sana kwa ibada na alikuwa na hadhi ya juu katika kabila la Khazraj. Baada ya Mtume ﷺ kufika Madinah, Waislamu wakamkusanyikia, Uislamu ukawa ndio neno la juu na Allah ﷻ Akawapa ushindi Waislamu katika vita vya Badr, Abu Amir mlaaniwa alisongwa kooni mwake na mate yake mwenyewe, akadhihirisha na kutangaza uadui wake dhidi ya Uislamu. Akakimbilia kwa makafiri wa Makkah, washirikina wa Kikuraishi, kwa ajili ya kuwaunga mkono katika vita vyao dhidi ya Mtume ﷺ, wakaungana na makabila ya Kiarabu yaliyokuwa yakiwafikiana nao, na wakaja katika mwaka wa vita vya Uhud. Waislamu yakawatokea yaliyowatokea ambapo, Allah ﷻ Aliwapa mtihamu, lakini mwisho mwema ukawa kwa Wachamungu. Muovu huyu (Abu 'Amir) alichimba mashimo baina ya safu (kambi) mbili. Mtume ﷺ akaangukia katika moja wapo, akapata madhara siku hiyo, akajeruhiwa uso wake, akavunjika mojawapo ya meno yake ya kulia kwa chini. Kichwa chake pia kilipata majeraha. Kabla ya mapigano kuanza, Abu 'Amir aliwaendea watu wake miongoni mwa Answar akawahutubia na akawashawishi wamsaidie yeye na kumuafiki. Baada ya kuyaelewa maneno yake walimuambia; "Allah ﷻ Asilineemeshe jicho lako kwa kukupa ushindi, ewe Fasik adui wa Allah ﷻ". Wakamshutumu na kumlaani, akarejea na kusema, "Wallahi! Kaumu yangu wamepatwa na shari baada yangu". Wakati huo huo Mtume ﷺ alimlingania kuja kwa Allah ﷻ kabla hajakimbia, na alimsomea Qur'an. Akakataa kusilimu na akaasi. Mtume ﷺ akamuomba Allah ﷻ kwamba Abu Amir afariki mbali akiwa ametengwa. Dua hii ikampata. Hayo yalitokea wakati watu walipomaliza mapigano ya vita vya Uhud, na akauona wito wa Mtume ﷺ ukizidi kuwa juu na kushinda. Akaenda kwa Heraclius, Mfalme wa Rumi kumtaka Amsaidie dhidi ya Mtume ﷺ. Heraclius akamuahidi msaada, akakaa kwake kwa muda mrefu. Akawaandikia jamaa zake katika Answar ambao walikuwa wanafiki na wenye shaka ambao aliwaahidi na kuwadokezea atakuja na jeshi na atalitumia kumpiga Mtume ﷺ na kwamba atamshinda na kuuzuia ujumbe alionao usizidi kuenea.

Akawaamuru wamuandalie ngome ambayo atawapeleka Wajumbe wake na kufanya Maandalizi ya kuja kwake. Wakaanza kujenga Msikiti jirani na Msikiti wa *Quba*, ambao waliukamilisha kuujenga kabla Mtume ﷺ hajatoka kwenda Tabuk. Wakaja kumuomba aende na akasali katika Msikiti huo ili watumie ushahidi huo wa kusali kwake kuwa ni kuukubali na kuuthibitisha. Wakamuambia wao waliujenga kwa ajili ya watu dhaifu na wagonjwa katika nyakati za usiku wenye mvua. Allah تعالى Akamzuia Mjumbe Wake dhidi ya kusali katika Msikiti huo. Mtume ﷺ akasema;

«إِنَّا عَلَى سَفَرٍ وَلَكِنَّ إِذَا رَجَعْنَا إِلَىٰ شَاءَ اللَّهُ»

*“Sisi tuko safarini, lakini tutakaporejea, In sha Allah”.*

Baada ya Mtume ﷺ kuanza msafara wa kurejea Madinah kutokea Tabuk, na kukaribia kufika, kwa kiasi cha siku moja na nusu yake, Jibril عليه السلام alimshukia Mtume ﷺ kumletea khabari za Msikiti uliojengwa kwa msingi wa kuwagawa waumini *“Masjidu Dhawraar”* na walioujenga wana malengo yao ya ukafiri na kuleta mfarakano katika umoja wa Waumini wa *“Masjid Quba”* ambao tangu siku ya kwanza uliasisiwa katika misingi ya kumchamungu. Mtume ﷺ akawatuma watu kuuvunja Msikiti huo kabla yeye hajafika Madinah.

Kama alivyosema ‘Ali bin Abu Twalhah kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Ayah hii kwamba, “Hao ni baadhi ya Answar ambao walijenga *Msikiti*, kisha Abu ‘Amir akawaambia, “Jengeni *Msikiti* na muandae nguvu na silaha kadiri mtakavyoweza. Mimi nakwenda kwa *Kaisari*, Mfalme wa Roma, na kuwaleta wanajeshi kutoka katika nchi hiyo. Halafu nitamfukuza Muhammad na Masahaba wake.” Walipomaliza kuujenga Msikiti wao, walimjia Mtume ﷺ na kumuambia, “Tumekamilisha kuujenga Msikiti wetu, tunapenda usali ndani yake na utuombe baraka”. Allah تعالى Akashusha Aya ifuatayo:

لَا تَقُمْ فِيهِ أَبَدًا

*“Usisimame kwenye Msikiti huo kabisa.”* Mpaka,

الظَّالِمِينَ

*“...madhalimu...”*<sup>1</sup>. Kauli ya Allah تعالى:

<sup>1</sup> At-Tabari 14:470.



وَلِيَخْلِفَنَّ

**“Na bila ya shaka wataapa”.** Wale walioujenga.

إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا الْحُسْنَىٰ

**“...kwamba: Hatukukusudia ila wema tu”.**

Maana yake: Hatukukusudia jingine katika kuujenga Msikiti huu isipokuwa kheri na huruma kwa watu. Allah تعالیٰ Anasema;

وَاللَّهُ يَشْهَدُ إِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ

**“Na Mwenyezi Mungu Anashuhudia kuwa wao ni waongo”.**

Ni waongo katika makusudio na nia zao, na kwamba waliujenga kwa ajili ya kuudhuru Msikiti wa Quba, kumkufuru Allah تعالیٰ, na kuwafarakanisha Waumini.

وإِرْصَادًا لِمَنْ حَارَبَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ مِنْ قَبْلُ

**“...na pa kuvizia kwa walio mpiga vita Mwenyezi Mungu na Mtume wake hapo kabla...”.**

Kama vile Abu Amir, fasiki, ambaye alikuwa akiitwa Ar-Rahib, laana ya Allah imshukie. Kauli ya Allah تعالیٰ;

لَا تَقُمْ فِيهِ أَبَدًا

**“Usisimame kwenye Msikiti huo kabisa”.**

Ni makatazo kwa Mtume ﷺ, na umma wake nao unamfuata yeye katika kuhusishwa na katazo hilo, kwamba wasisimame ndani yake kwa ajili ya Sala.

### **Fadhila za Msikiti wa Qubaa na Hukumu ya Kusali Ndani Yake.**

Kisha Allah تعالیٰ Alimtia moyo Mtume ﷺ asali katika Msikiti wa Quba ambao aliuasisi, tangu siku ya kwanza – ulijengwa juu ya misingi ya kumcha Allah تعالیٰ, ambayo ni kufanya utii kwa Allah تعالیٰ na kwa Mtume ﷺ, kwa kuunganisha umoja wa Waumini na kituo na ngome kwa ajili ya Uislamu na Waislamu.

Kwa ajili hii Allah تعالیٰ Alisema;

لَمَسْجِدٍ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَىٰ مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَنْ تَقُومَ فِيهِ ۗ

**“Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa ucha Mungu tangu siku ya mwanzo unastahiki zaidi wewe usimame ndani yake”.**

Mtiririko wa Aya unaonesha unaokusudiwa hapa ni Msikiti wa Quba, kwa kuzingatia hilo, kuna Hadithi katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema:

«صَلَاةٌ فِي مَسْجِدِ قُبَاءٍ كَعُمْرَةٍ»

*“Sala moja ndani ya Msikiti wa Qubaa ni kama ‘Umrah’”<sup>1</sup>.*

Kumeandikwa ndani ya Sahih kuwa Mtume ﷺ alikuwa akizuru Msikiti wa Quba huku akiwa amepanda juu ya mnyama na mara nyingine kwa kutembea kwa mguu<sup>2</sup>. Pia ipo Hadithi inayosema kuwa wakati Mtume ﷺ alipoujenga na kuuasisi Msikiti wa Quba baada tu ya kuwasili na kufikia kwa Banu Amr bin Awf, Malaika Jibril عليه السلام ndiye aliyemuelekeza upande wa Qiblah kilipo<sup>3</sup>. Allah Aalam.

Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa ‘Uwaym bin Sa’idah Al-Answari رضي الله عنه, kwamba alimsimulia kuwa Mtume ﷺ aliwajia katika Masjid Quba na kuwaambia:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى قَدْ أَحْسَنَ عَلَيْكُمُ الشَّاءَ فِي الطُّهُورِ فِي بَصَةِ مَسْجِدِكُمْ، فَمَا مَدَا الطُّهُورُ الَّذِي تَطَهَّرُونَ بِهِ؟»

*“Allah تعالى Amekusifuni vyema kuhusu twahara mnayoifanya katika khabari ya msikiti wenu, basi ni twahara gani hii mnayojitakasa kwayo?”*

Wakasema: “Wallahi! Ewe Mtume ﷺ, sisi hatujui, isipokuwa tulikuwa na jirani wa Kiyahudi ambao walikuwa wakitumia maji kwa kustanji nasi tukawa tunajiosha sawa na walivyokuwa wakijiosha”<sup>4</sup>. Ibn Khuzaymah aliikusanya Hadithi hii ndani ya Sahih yake<sup>5</sup>. Kauli ya Allah تعالى:

<sup>1</sup> Ibn Majah 1:452 na At-Tirmidhi 324.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 3:82 na Muslim 1399.

<sup>3</sup> Abu Dawud 44 na At-Tirmidhi 3100 na Ibn Majah 357.

<sup>4</sup> Ahmad 3:422.

<sup>5</sup> Ibn Khuzaymah 1:45.

لَمَسْجِدٍ أُسِّسَ عَلَى التَّقْوَىٰ مِن أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَن تَقُومَ فِيهِ ۚ فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَن يَتَطَهَّرُوا ۗ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُطَهَّرِينَ

***“Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa uchamungu tangu siku ya mwanzo unastahiki zaidi wewe usimame ndani yake. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu Anawapenda wanaojitakasa”.***

Ni ushahidi wa kutia moyo kuwa watu wasali katika Misikiti ya zamani ambayo tangu mwanzo wa kujengwa kwake iliasisiwa kwa ajili ya kumuabudu Allah تعالى Peke Yake, Asiyeye na mshirika. Pia inasisitiza Sunnah ya kuswali sala ya Jama'ah ya waja wema wenye kufanya ibada zao kwa vitendo, ambao huchukua udhu wao vyema na hujiepusha dhidi ya mavazi machafu.

Imamu Ahmad aliandika kuwa mtu mmoja katika Masahaba wa Mtume ﷺ alipokea kwamba Mtume ﷺ aliwasalisha Sala ya As-Subhi. Akasoma Surat Ar-Rum humo na akafanya makosa katika usomaji. Alipomaliza Sala alisema;

«إِنَّهُ يَلْبِسُ عَلَيْنَا الْقُرْآنَ أَنَّ أَقْوَامًا مِنْكُمْ يُصَلُّونَ مَعَنَا لَا يُحْسِنُونَ الرُّضُوءَ، فَمَنْ شَهِدَ الصَّلَاةَ مَعَنَا فَلْيُحْسِنِ الرُّضُوءَ»

*“Wakati mwingine sisi hukosea katika usomaji Qur'an, kwa kuwa kuna watu miongoni mwenu wanaosali pamoja na sisi lakini hawauchukui udhu vyema. Atakayeshiriki Sala pamoja na sisi, basi achukue udhu vyema”.*

Inajulisha kwamba ukamilishaji wa twahara huleta wepesi wa kudumisha ibada na husaidia katika kuitimiza na kuikamilisha na kusimamisha sheria zake.

أَقَمْنَ أُسُسَ بُنْيَانِهِ عَلَى تَقْوَىٰ مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانٍ خَيْرٌ أَمْ مَنَ أُسُسَ بُنْيَانِهِ عَلَىٰ شَفَا جُرُفٍ هَارٍ فَانَهَارٍ بِهِ فِي نَارِ جَهَنَّمَ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٩﴾ لَا يَزَالُ بُنْيَانُهُمُ الَّذِي بَنَوْا رِيبَةً إِلَّا أَن تَقَطَّعَ قُلُوبُهُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿١١٠﴾

***109. “Je! Mwenye kuweka msingi wa jengo lake juu ya kumcha Mwenyezi Mungu na Radhi Zake ni bora au Mwenye kuweka msingi***

<sup>1</sup> Ahmad 3:471-472.

***wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo likabiringika, naye katika Moto wa Jahannamu? Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhalimu”.***

***110. “Na jengo lao hilo walilolijenga litakuwa sababu ya kutia wasiwasi nyoyoni mwao mpaka nyoyo zao hizo zikatike vipande vipande. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua Mwenye Hikima”.***

**Tofauti kati ya Misikiti Miwili hiyo, Masjidut Taqwaa na Masjidu Adh-Dhwiraar.**

Allah تعالى Anasema: “Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa kumcha Allah تعالى na kutaka radhi Zake haulingani na uliojengwa kwa ajili ya madhara, ukafiri na kuwafarakanisha Waumini, na kuufanya kuwa ni kituo cha wale wanaompiga vita Allah تعالى na Mtume ﷺ. Hawa wa mara ya pili wameujenga Msikiti wao. Mfano wake ni,

عَلَىٰ شَفَا

***“Juu ya ukingo wa shimo...”*** Maana: Pembezoni mwa ncha ya shimo.

فِي نَارِ جَهَنَّمَ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

***“...katika Moto wa Jahannamu? Na Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhalimu”***

Maana yake: Amali za wafisadi hazitengemai. Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنه alisema: “Niliuona Msikiti uliojengwa kwa ajili ya kuleta madhara ambao ulikuwa ukifuka moshi, katika wakati wa uhai wa Mtume ﷺ”.<sup>1</sup> Kauli ya Allah تعالى:

لَا يَزَالُ بُنِيْنُهُمُ الَّذِي بَنَوْا رِيبَةَ فِي قُلُوبِهِمُ

***“Na jengo lao hilo walilo lijenga litakuwa sababu ya kutia wasiwasi nyoyoni mwao”.***

Maana: Litawatia mashaka na unafiki, kwa sababu ya kukifanya kitendo hiki kibaya. Na kimewarithisha unafiki nyoyoni mwao, kama walivyoshawishiwa watu walioabudu ndama wa ng’ombe na kumpenda. Kauli ya Allah تعالى:

إِلَّا أَنْ تَقَطَّعَ قُلُوبُهُمْ

***“...mpaka nyoyo zao hizo zikatike vipande vipande”.*** Maana: Kwa kufa. Hayo

<sup>1</sup> At-Tabari 14:49

ni kwa mujibu wa Ibn ‘Abbas, Mujahid, Qatadah, Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam na wengine رضي الله عنهم<sup>1</sup>, katika wanazuoni wa *Salaf*. Allah تعالى anasema;

وَاللَّهُ عَلِيمٌ

**“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua”.** Anajua matendo ya viumbe Wake.

حَكِيمٌ

**“Mwenye Hikima”.** Katika Kuwalipa kheri au shari.

﴿ إِنَّ اللَّهَ اشْتَرَى مِنَ الْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَالَهُمْ بِأَرْبَ لَهُمُ الْجَنَّةَ يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ وَعَدَا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنَ اللَّهِ فَاسْتَبْشِرُوا بِالَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ ۚ وَذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿۱۱۱﴾

**111. “Hakika Mwenyezi Mungu Amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa watapata Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu – wanaua na wanauwawa. Hii ni ahadi Aliyojilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur’ani. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya Naye. Na huko ndiko Kufuzu kukubwa”.**

**Allah Amezidhamini Roho na Mali za Wanaopigana Jihadi kwa Kuwapa Pepo.**

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Amewapatia Waumini m-badala wa roho na mali zao, pale walipozitoa katika njia Yake – badala hiyo ni Pepo. Hii ni miongoni mwa Fadhila, Ukarimu na ihsani Zake, kwani Yeye Amekubali kuchukua badala kwa nafsi zao kitu ambacho ni miliki Yake ambacho aliwatunuku nacho waja Wake Watiifu. Kwa minajili hii, Al-Hasan Al-Basri na Qatadah walisema: “Wallahi! Allah تعالى Ameliahidi hilo kwao wao na kuzipandisha thamani zao.”<sup>2</sup> Shimar bin ‘Atwiyah alisema; “Hapana Muislamu yeyote isipokuwa shingoni mwake kuna ahadi baina yake na Allah تعالى, ima awe ameitekeleza au afe bila kuitekeleza”. Kisha akasoma Aya hiyo<sup>3</sup>. Kwa ajili hiyo, husemwa mwenye kutoka katika Jihadi ya Allah تعالى Atakuwa amefanya *baia*, yaani ameukubali mkataba huo na kuutekeleza. Kauli ya Allah تعالى;

<sup>1</sup> At-Tabari 14:495-497.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:495-499.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:499.

يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيَقْتُلُونَ وَيُقْتَلُونَ<sup>ط</sup>

**“Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu – wanaua na wanauwawa”.**

Maana yake: Ni sawa sawa tu, ama waue au wauawe, au yote kwa pamoja, Pepo itakuwa ni yao. Kwa ajili hii, ilikusanywa Hadithi ndani ya *Sahihi* Mbili ikisemwa kuwa;

«وَتَكْفَلُ اللَّهُ لِمَنْ خَرَجَ فِي سَبِيلِهِ لَا يُخْرِجُهُ إِلَّا جِهَادًا فِي سَبِيلِي وَتَصْدِيقًا بِرُسُلِي  
بِأَنْ تَوَفَّاهُ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ، أَوْ يَرْجِعَهُ إِلَى مَثَرِهِ الَّذِي خَرَجَ مِنْهُ، نَائِلًا مَا نَالَ مِنْ  
أَجْرٍ أَوْ غَنِيمَةٍ»

“Allah تعالى Amempa ahadi mtu aliyetoka katika njia Yake: “Ambaye hakikumtoa kingine zaidi ya Jihadi katika Njia Yangu na kuwasadiki Mitume Wangu”. Huyo, kama Atamfisha ni kumingiza Peponi au Amrejeshe katika makazi yake alikotokea huku akiwa amepata malipo ya mali au Ngawira”<sup>1</sup>.

Kauli ya Allah تعالى:

وَعَدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِي التَّوْرَةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالْقُرْآنِ<sup>ع</sup>

**“Hii ni ahadi Aliyojilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur’ani”.**

Ayah hii inasisitiza ahadi hiyo na kujulisha kwamba Amejilazimisha Kuitekeleza, na Aliishusha kwa Mitume Wake ndani ya Vitabu Vyake Vitukufu ambavyo ni, Taurati iliyoshuka kwa Musa عليه السلام, Injili kwa Isa عليه السلام na Qur’an kwa Muhammad ﷺ, rehema na amani za Allah تعالى ziwafikie wote hawa. Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ أَوْفَى بِعَهْدِهِ مِنْ اللَّهِ<sup>ع</sup>

**“Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu?”**

Kwani Yeye Huwa Hakiuki miadi. Hii inalingana na Kauli Yake nyingine;

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا

**“Na nani msema kweli kuliko Mwenyezi Mungu?” (4:87)**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 6:254 na Muslim 3:1496.

Na Kauli Yake;

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ قِيلًا

**“Na nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Mwenyezi Mungu?”  
(4:122)**

Ndipo Allah تعالى Aliposema;

فَاسْتَبْشِرُوا بِبَيْعِكُمُ الَّذِي بَايَعْتُمْ بِهِ ۚ وَذَٰلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٠٣﴾

**“Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye. Na huko ndiko  
Kufuzu kukubwa”.**

Basi na wafurahi wale ambao wenye kutenda kwa muktadha wa mkataba huu na kuitimiza ahadi hii, kwamba watapata Kufuzu kukubwa na neema za kudumu milele.

\* \* \*

اَلتَّائِبُونَ اَلْعَبِيدُونَ اَلْحَمِيدُونَ اَلسَّائِحُونَ  
 اَلرَّاكِعُونَ اَلسَّجِدُونَ اَلْأَمْرُونَ بِالْمَعْرُوفِ  
 وَالنَّاهُونَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَالْحَافِظُونَ لِحُدُودِ اللَّهِ وَبَشِّرِ  
 اَلْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾ مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ  
 يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أَوْلَىٰ قُرْبَىٰ مِنْ بَعْدِ  
 مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١١٣﴾ وَمَا كَانَ  
 اسْتِغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَن مَّوْعِدَةٍ وَعَدَهَا إِيَّاهُ فَلَمَّا  
 تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ ۖ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ  
 ﴿١١٤﴾ وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِلَّ قَوْمًا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَهُمْ حَتَّىٰ  
 يُبَيِّنَ لَهُمْ مَا يَتَّقُونَ ۚ إِنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١٥﴾  
 إِنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ مُخْتَصِمٌ ۖ وَمَا  
 لَكُمْ مِّنْ ذُنُوبٍ اللَّهُ مِّنْ وَلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١١٦﴾ لَقَدْ  
 تَابَ اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالأَنْصَارِ الَّذِينَ  
 اتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ الْعُسْرَةِ مِن بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيغُ قُلُوبَ  
 فَرِيقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ ۚ إِنَّهُ بِهِمْ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٧﴾

اَلتَّائِبُونَ اَلْعَبِيدُونَ  
 اَلْحَمِيدُونَ اَلسَّائِحُونَ  
 اَلرَّاكِعُونَ اَلسَّجِدُونَ  
 اَلْأَمْرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَالنَّاهُونَ عَنِ  
 الْمُنْكَرِ وَالْحَافِظُونَ لِحُدُودِ اللَّهِ  
 وَبَشِّرِ اَلْمُؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾

112. "(Kwa) wanaotubia,  
 wanaoabudu, wanahimidi,  
 wanaokimbilia kheri,  
 wanaorukuu, wanaosujudu,  
 wanaoamrisha mema na  
 wanaokataza maovu, na  
 wanaolinda mipaka ya  
 Mwenyezi Mungu. Na  
 wabashirie Waumini".

Hii ni sifa ya Waumini  
 ambao Allah تعالى Amezi-  
 nunua roho zao na mali zao.  
 Wana sifa hizi nzuri na za  
 utukufu,

اَلتَّائِبُونَ

"(Kwa) wanaotubia". Madhambi yote na kuyaacha maovu.

اَلْعَبِيدُونَ

"...wanaoabudu".

Wanachunga ibada ya Mola wao, kwa kauli na matendo yao. Miongoni mwa  
 kauli hizo njema ni kumsifu. Ndiyo maana, Allah تعالى Alisema;



الْحَمْدُونَ

“...wanaohimidi”.

Miongoni mwa amali njema ni Saumu, nayo ni kuacha vitamu katika vyakula, vinywaji na jimai. Hii ndiyo maana iliyokusudiwa hapa. Kwa hiyo, Allah تعالى Alisema;

السَّاجِدُونَ

“...wanaokimbilia kheri”. (9:122)

Ni sawa na Alivyowasifu wake wa Mtume ﷺ, Allah تعالى Alisema;

سَائِحَاتٍ

“Saaihaat”. (66:5)

Maana yake: Wenye kufunga. Kadhalika kurukuu na kusujudu, ambayo ni miongoni mwa matendo ya kiibada. Kwa hivyo, Alisema:

الرَّكُوعِ السَّاجِدُونَ

“...wanao rukuu, wanao sujudu”.

Pamoja na hayo, wao wanawanufaisha viumbe wa Allah تعالى na wanawa-ongoza katika kumtii Allah تعالى kwa sababu ya tabia yao ya kuamrisha mema na kukataza maovu, pamoja na kuyajua wanayotakiwa kuyafanya na wanayotakiwa kuyaacha, nayo ni kuchunga mipaka ya Allah تعالى juu ya mambo Aliyoyahalalisha na Aliyoyaharamisha. Wayajue na kuyafanyia kazi. Wakadumisha kumuabudu Allah تعالى na kuwaasa viumbe. Ndipo, Allah تعالى Alisema;

وَنَشِيرِ الْمُؤْمِنِينَ

“Na wabashirie Waumini”.

Kwa sababu Imani hujumuisha haya yote, na mafanikio makubwa ni kwa mwenye kuwa nayo (Imani).

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولَىٰ قُرْبَىٰ مِنْ  
بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١١٧﴾ وَمَا كَانَ أَسْتِغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا  
عَنْ مَّوْعِدَةٍ وَعَدَهَا إِيَّاهُ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ ۚ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ ﴿١١٨﴾

**113. “Haimpasii Nabii na wale walioamini kuwatakia msamaha Washirikina, ijapokuwa ni jamaa zao, baada ya kwisha bainika kuwa hao ni watu wa Motoni”.**

**114. “Wala haikuwa kwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye. Lakini ilipombainikia kwamba yeye ni adui wa Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye. Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekevu, mvumilivu”.**

### Makatazo Juu ya Kuwaombea Dua Washirikina.

Imamu Ahmad aliandika kutoka kwa Ibn Al-Musayyab kuwa baba yake alisema, Abu Twalib alipofikwa na mauti, Mtume ﷺ alimuendea na kumkuta Abu Jahl na ‘Abdullah bin Abu Umayyah wakiwa kwake. Mtume ﷺ alisema:

«أَيُّ عَمٍّ، قُلْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ كَلِمَةً أَحَاجُّ لَكَ بِهَا عِنْدَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Ewe ami! Sema Laa ilaaha illallah”. Kalima ambayo itaniwezesha nikuombe mbele ya Allah Mtukufu”.

Abu Jahl na ‘Abdullah bin Abu Umayyah wakamuuliza, “Ewe Abu Twalib! Utaicha mila (dini) ya ‘Abdul Muttwalib?” Akajibu: “Nitaendelea na mila (dini) ya ‘Abdul Muttwalib”. Mtume ﷺ akasema;

«لَا سْتُغْفِرَنَّ لَكَ مَا لَمْ أَنَا عَنْكَ»

“Nitakuombea maghufira maadam sijakatazwa kufanya hivyo”.

Ikashuka Aya nyingine;

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ وَلَوْ كَانُوا أُولَىٰ قُرْبَىٰ مِنْ  
بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُمْ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿١١٦﴾

**“Haimpasii Nabii na wale walioamini kuwatakia msamaha Washirikina, ijapokuwa ni jamaa zao, baada ya kuishabainika kuwa hao ni watu wa Motoni”.**

Na ikashuka;

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

**“Kwa hakika wewe humuongoi umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye”. (28:56)<sup>1</sup>**

Hadithi hii imeandikwa ndani ya *Sahih Mbili*.<sup>2</sup> Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kwamba Sulayman bin Buraydah alisema kuwa baba yake alieleza kwamba Mtume ﷺ alipofika Makkah, alikwenda kwenye alama ya kaburi, akaketi karibu yake, ikawa kama anasema jambo, kisha akasimama huku akilengwa lengwa na machozi machoni mwake. Tukamuambia: “Ewe Mtume ﷺ, sisi tumeona ulichokifanya”. Akasema;

«إِنِّي اسْتَأْذَنْتُ رَبِّي فِي زِيَارَةِ قَبْرِ أُمِّي فَأَذِنَ لِي، وَاسْتَأْذَنْتُهُ فِي الْاسْتِغْفَارِ لَهَا فَلَمْ يَأْذَنْ لِي»

*“Mimi nilimuomba idhini Mola wangu kuhusu kulizuru kaburi la mama yangu na Akaniruhusu. Pia nikamuomba juu ya kumuomba maghufira, lakini hakuniruhusu”.*

Hajapata kuonekana akilia sana (kwa machozi mengi) kama siku hiyo<sup>3</sup>. Al-‘Awfi alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ

**“Haimpasii Nabii na wale walioamini kuwatakia msamaha Washirikina”.**

Kwa maana yake ni kwamba Mtume ﷺ alitaka kumuomba mama yake maghufira, Allah تعالى Akamkataza kufanya hivyo. Mtume ﷺ akasema;

«إِنَّ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلَ اللَّهِ ﷺ قَدِ اسْتَغْفَرَ لِأَبِيهِ»

*“Ibrahim Al-Khalil alimuomba Allah Amghufirie baba yake”.*

Allah تعالى Akashusha Aya;

وَمَا كَانَ اسْتَغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَن مَّوْعِدَةٍ وَعَدَهَا إِيَّاهُ

**“Wala haikuwa kwa Ibrahim kumtakia msamaha baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye”<sup>4</sup>.**

<sup>1</sup> Ahmad 5:433.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 8:192 na Muslim 1:54.

<sup>3</sup> At-Tabari 6:489.

<sup>4</sup> At-Tabari 14:512.

'Ali ibn Abu Twalhah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliongelea Ayah hii kwa kusema: "Walikuwa wakiwaombea maghufira, mpaka ikashuka Ayah hii, wakaacha kuwaombea msamaha maiti wao, wala hawakuzuliwa kuwaombea jamaa zao walio hai mpaka wanapofariki. Kisha Allah تعالى Akateremsha ayah:

وَمَا كَانَ اسْتِغْفَارُ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ

**"Wala haikuwa Ibrahim kumtokia msamaha baba yake". (9:114)<sup>1</sup>**

Kauli ya Allah تعالى;

فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ

**"Lakini ilipombainikia kwamba yeye ni adui wa Mwenyezi Mungu, alijiepusha naye". (9:114)**

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema: "Ibrahim عليه السلام aliendelea kumuomba maghufira baba yake mpaka akafariki, na alipogundua kuwa ni adui wa Allah تعالى alijitenga naye". Na katika masimulizi mengine, "...alipofariki ilimbainikia kuwa alikuwa adui wa Allah تعالى"<sup>2</sup> Hivi ndivyo pia walivyosema Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah na wengine. Allah تعالى Awarehemu.<sup>3</sup> 'Ubayd bin 'Umar na Sa'id bin Jubayr walisema: "Ibrahim عليه السلام atajitenga na baba yake Siku ya Kiyama, mpaka atamkuta akiwa na vumbi na uchovu katika wajihi wake, na atasema, "Ewe Ibrahim! Mimi nilikuwa nakuasi, lakini leo sitakuasi". Ibrahim عليه السلام atasema: "Ewe Mola wangu! Uliniahidi kuwa Hutanifedhehesha Siku ya Kufufuliwa, basi kuna fedheha gani kubwa kama kumuona baba yangu akidhalilika?" Ataambiwa, "Angalia kilicho nyuma yako". Atamuona fisi aliyetapaka damu, kisha atavutwa kwa miguu yake na kutupwa motoni.<sup>4</sup> Ama Kauli ya Allah تعالى;

إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ

**"Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba, mnyenyekevu, mvumilivu".**

'Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema, "Maana ya neno *Al-Awwah* ni dua"<sup>5</sup>. Masimulizi mengine kadha sawa na hayo kwa isnadi nyingine yanaelezwa

<sup>1</sup> At-Tabari 14:513.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:519.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:518-519.

<sup>4</sup> At-Tabari 14:521.

<sup>5</sup> At-Tabari 14:523-524.

kutoka kwa Ibn Mas'ud رضى الله عنه<sup>1</sup>. Pia imesemwa kuwa ina maana ya 'mnyenyekevu', mwenye huruma, mwenye Imani ya yakini, mwenye kumsabihi Allah تعالى na zimetolewa maana nyingine zisizokuwa hizo.

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِلَّ قَوْمًا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَهُمْ حَتَّىٰ يُبَيِّنَ لَهُمَ مَا يَتَّقُونَ ۚ إِنَّ اللَّهَ  
بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١١٥﴾ إِنَّ اللَّهَ لَهُ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ يُخَيِّرُ وَيُمِيتُ ۚ وَمَا لَكُمْ  
مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِن وَّلِيٍّ وَلَا نَصِيرٍ ﴿١١٦﴾

**115. "Na haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwahesabu watu kuwa wamepotea baada ya kwisha waongoza mpaka Awabainishie ya kujiepusha nayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua kila kitu".**

**116. "Hakika Mwenyezi Mungu Anao Ufalme wa mbingu na ardhi; Huhuisha na Hufisha. Nanyi hamna Mlinzi wala Msaidizi isipokuwa Mwenyezi Mungu"**

**Allah تعالى Hawaadhibu Wafanyao Maasi ila Baada ya Kusimamisha Hoja.**

Allah تعالى Anaeleza kuhusu Nafsi Yake Tukufu na Hukumu Yake ya kiuadilifu, kwamba Hawaachi watu wapotee ila baada ya Kuwapelekea Ujumbe, ili kwamba hoja dhidi yao iwe imesimama. Kama alivyosema katika Kauli Yake nyingine;

وَأَمَّا ثَمُودُ فَهَدَيْنَاهُمْ

**"Na ama Thamudi Tuliwaongoza". (41:17) Mujahid aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى;**

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُضِلَّ قَوْمًا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَهُمْ

**"Na haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwahesabu watu kuwa wamepotea baada ya kuisha waongoza".**

Kwamba, "Allah تعالى Aliwabainishia Waumini kuhusu kuacha kuwaombea maghufira Washirikina kama hukumu mahususi, na kwa ujumla, ni onyo kwao dhidi ya kumuasi Yeye na Kuwataka wawe watiifu Kwake, kwa hivyo ni hiyari yenu kufanya au kuacha"<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:524.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:537.

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema: "Allah تعالى Anasema, "Hatakuachilieni mpotee kwa kuwaombea maghufira Washirikina waliofariki, baada ya kukupeni uongofu na Akakuwafikisheni kumuamini Yeye na Mjumbe Wake. Kwanza, Anakufahamisheni ambacho mnatakiwa kukiacha, hivyo mnakiacha. Ama kabla ya Kukufahamisheni ubaya wa hayo kwa Kukukatazeni dhidi ya hayo, msingeliruka mpaka na kuyafanya yale Aliyokukatazeni. Kwa hivyo, Hatakuachilieni mpotee, kwani utii na uasi hutukia baada ya kutangulizwa maamrisha na makatazo, ama wale ambao hawakuamrisha wala kukatazwa hawawi Watiifu wala wenye kuasi katika yale ambayo hawakuamrisha wala hawakukatazwa kuyafanya"<sup>1</sup>.

Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّ اللَّهَ لَهُ مَلِكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ تَحِيَّءٌ وَيُحْيِي وَمَا لَكُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ مِن وَّلِيٍّ  
وَلَا نَصِيرٍ

***"Hakika Mwenyezi Mungu Anao Ufalme wa mbingu na ardhi; Huhuisha na Hufisha. Nanyi hamna Mlinzi wala Msaidizi isipo kuwa Mwenyezi Mungu".***

Ibn Jariri رحمه الله تعالى alisema: "Huu ni Msisitizo wa Allah تعالى kwa waja Wake wa kupigana na washirikina na wakuu wa ukafiri, na Kuwataka wawe na matumaini ya kupata nusra ya Allah تعالى, Mmiliki wa mbingu na ardhi, wala wasiwaogope maadui zake, kwani Waumini hawana Mlinzi wala Msaidizi mwingine asiyekuwa Yeye"<sup>2</sup>.

لَقَدْ تَابَ اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ الْعُسْرَةِ  
مِنْ بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيغُ قُلُوبَ فَرِيقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ إِنَّهُ بِهِمْ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٧﴾

***117. "Mwenyezi Mungu Amekwishapokea toba ya Nabii na Wahajiri na Ansari waliomfuata katika saa ya dhiki, pale baada ya kukaribia nyoyo za baadhi yao kugeuka. Basi Akapokea toba yao, kwani hakika Yeye kwao wao ni Mpole na ni Mwenye Kuwarehemu".***

<sup>1</sup> At-Tabari 14:536.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:538.

## Vita vya Tabuk.

Mujahid na wengine walisema: Aya hii ilishuka juu ya vita vya Tabuk, kwamba walikwenda huko wakati wa taabu. Ni mwaka uliokuwa na uhaba wa mvua, joto kali na ukosefu wa chakula na maji<sup>1</sup>. Qatadah alisema: “Walielekea Ash-Sham katika mwaka wa vita vya Tabuk wakati wa joto kali. Allah تعالی Alikuwa Anajua mambo yalivyokuwa magumu na watu walipata tabu kubwa, na tuliambiwa kwamba ilifika kiasi cha watu wawili kukatiana tende moja kisha anakunywa maji, halafu anaifyonza tende mwingine na anakunywa maji. Allah تعالی Akawasamehe na Akawapa ruhusa ya kurejea kutoka katika vita hivyo”<sup>2</sup>. Ibn Jariri رحمه الله تعالی alinukuu kutoka kwa ‘Abdullah bin ‘Abbas رضي الله عنه kuwa ‘Umar bin Al-Khattwab رضي الله عنه alikumbushwa juu ya suala la vita vigumu (Tabuk). ‘Umar رضي الله عنه akasema; “Tulitoka pamoja na Mtume ﷺ katika joto kali kuelekea Tabuk. Tukapiga kambi mahali ambapo tulipatwa na kiu kali kiasi kwamba tukadhani shingo zetu zitakatika. Kisha mmoja wetu aliweza kwenda kusaka maji bila ya kurejea, mpaka ikadhaniwa kuwa shingo yake inataka kukatika. Mwingine aliweza kumchinja ngamia wake na kumkamua matumbo yake na kunywa maji yaliyomo na yanayosalia kuyaweka katika mafigo yake. Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه akasema: “Ewe Mtume ﷺ! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuzoesha Kukupa kheri kila Unapomuomba, basi tuombe”. Akasema;

«تُجِبُّ ذَلِكَ؟»

“Unalipenda hilo?”

Abubakar رضي الله عنه akajibu: “Ndiyo”. Naye akainua mikono yake akaomba na hakuirudisha (chini) tayari mvua nyingi zikawa zinanyesha kutoka angani. Ilinyesha, halafu ikakatika, wakajaza maji katika vyombo walivyokuwa navyo. Kisha tukaenda kuangalia ilivyonyesha, na tukakuta kwamba haikunyeshwa nje ya kambi yetu”<sup>3</sup>. Ibn Jariri رحمه الله تعالی alisema juu ya Kauli ya Allah تعالی:

لَقَدْ تَابَ اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ الْعُسْرَةِ

**“Mwenyezi Mungu Amekwishapokea toba ya Nabii na Wahajiri na Ansari waliomfuata katika saa ya dhiki”.**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:540.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:541.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:539.

Ilikuwa dhiki kutokana na Matumizi, usafiri, masurufu na maji.

مِنْ بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيغُ قُلُوبُ فَرِيقٍ مِّنْهُمْ

**“...pale baada ya kukaribia nyoyo za baadhi yao kugeuka”.**

Zilikaribia kugeuka na kuwa mbali na ukweli, kisha zikaanza kuwa na mashaka na Dini ya Mtume ﷺ kutokana na taabu na ugumu walioupata katika safari na vita vyao.

ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ

**“Basi Akapokea toba yao”.**

Anasema: “Kisha Akawajaalia kufanya toba kwa Mola wao na kurudi kuwa imara katika Dini Yake.”

إِنَّهُمْ بِهِمْ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

**“...kwani hakika Yeye kwao wao ni Mpole na ni Mwenye Kuwarehemu”.**<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 14:539.



وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خُلِفُوا حَتَّىٰ إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ  
 الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ أَنْفُسُهُمْ وَظَنُّوا أَن لَّا  
 مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ هُوَ  
 التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١١٨﴾ يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ  
 وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ ﴿١١٩﴾ مَا كَانَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ  
 وَمَنْ حَوْلَهُمْ مِنَ الْأَعْرَابِ أَن يَتَخَلَّفُوا عَن رَّسُولِ اللَّهِ وَلَا  
 يَرْغَبُوا بِأَنْفُسِهِمْ عَن نَّفْسِهِ ۗ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ لَا يُصِيبُهُمْ  
 ظَمَأٌ وَلَا نَصَبٌ وَلَا مَخْمَصَةٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَطْئُونَ  
 مَوْطِئًا يَغِيظُ الْكُفَّارَ وَلَا يَنَالُونَ مِنَ عَدُوِّ نِيْلًا إِلَّا  
 كُتِبَ لَهُم بِهِ عَمَلٌ صَالِحٌ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ  
 الْمُحْسِنِينَ ﴿١٢٠﴾ وَلَا يُنْفِقُونَ نَفَقَةً صَغِيرَةً وَلَا  
 كَبِيرَةً وَلَا يَقْطَعُونَ وَادِيًا إِلَّا كُتِبَ لَهُمْ لِيَجْزِيَهُمُ  
 اللَّهُ أَحْسَنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢١﴾ \* وَمَا كَانَ  
 الْمُؤْمِنُونَ لِيَنْفِرُوا كَافَّةً ۗ فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ  
 طَائِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوا فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا  
 إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خُلِفُوا حَتَّىٰ  
 إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الْأَرْضُ بِمَا  
 رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ أَنْفُسُهُمْ  
 وَظَنُّوا أَن لَّا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ  
 ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ هُوَ  
 التَّوَّابُ الرَّحِيمُ ﴿١١٨﴾ يَتَأْتِيهِمُ  
 الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ  
 الصَّادِقِينَ ﴿١١٩﴾

118. "Na pia wale watatu walioachwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjufu wake, na nafsi zao zikanyongeka, na waka-yakinika kuwa hapana pa kumkimbia Mwenyezi Mungu isipokuwa Kwake Yeye. Kisha Akawaelekea kwa Rehema Yake ili nao waendeleo kutubu. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kupokea toba na Mwenye Kurehemu".

119. "Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli".

## Kisa cha Masahaba Watatu Ambao Shauri Lao Lilisubiri Wahyi Kutoka kwa Allah

Imamu Ahmad aliandika kuwa ‘Abdullah bin Ka’b bin Malik رضي الله عنه ambaye alikuwa akimkongoja Ka’b رضي الله عنه baada ya kupatwa na upofu, alisema: Nilimsikia Ka’b bin Malik akisimulia kisa chake wakati alipokosa kujiunga na Mtume ﷺ katika vita vya Tabuk. Alisema, “Haijatokea kuacha kushiriki pamoja na Mtume ﷺ katika vita vyovyote alivyowahi kupigana isipokuwa vya Tabuk, ukiacha kwamba sikujiunga naye katika vita vya Badr, lakini hapana yeyote aliyekemewa kwa kutoshiriki katika vita hivyo. Ambavyo kwa hakika, Mtume ﷺ alitoka kwa ajili ya kuuendea msafara wa Makuraishi mpaka Allah تعالى Akawakutanisha wao na maadui wao pasi na miadi. Pia nilishuhudia pamoja na Mtume ﷺ katika usiku wa Al-‘Aqabah, wakati ambao Mtume ﷺ alipochukua ahadi zetu juu ya Uislamu. Na kwa kuwa nimeshuhudia Aqabah sikupenda kushuhudia Badri ingawa Badr ndiyo yenye kukumbukwa zaidi na watu na ndio mashuhuri kuliko *baiat* ya ‘Aqabah. Ama kuhusu khabari zangu kuhusu vita vya Tabuk ambapo sikujiunga pamoja na Mtume ﷺ ni kwamba, mimi sikuwahi kamwe kuwa na nguvu au mali zaidi ya wakati huo, ambapo sikujiunga naye katika vita hivyo. Wallahi! Kabla yake, sikupata kumiliki ngamia wawili lakini katika kipindi cha vita hivyo niliweza kuwamiliki”. Kila wakati Mtume ﷺ alipotaka kwenda vitani, alikuwa akificha kusudio lake kwa kutaja vita vingine, mpaka ulipowadia wakati wa vita hivyo, Mtume ﷺ akapigana katika majira ya joto kali na akaikabili safari ya mbali na akapambana na askari wengi wa adui. Kwa hivyo, Mtume ﷺ akawawekea bayana Waislamu kuhusu vita anayoikusudia ili waweze kujiandaa, na akawafahamisha alikokusudia kwenda. Mtume ﷺ alikuwa na idadi kubwa ya Waislamu kiasi cha kushindikana kuorodheshwa majina yao katika kitabu kimoja, yaani *Al-Diwan* (Jalada la kusajili)”.

Ka’b akaendelea kunisimulia: “Kila ambaye aliyekusudia kutoshiriki katika vita hiyo angelidhani kwamba nia yake haingefahamika, isipokuwa kama Allah تعالى Atateremsha Wahyi kulibainisha. Mtume ﷺ alipigana vita hivyo katika msimu ambao matunda yalikuwa yameiva na kuna vivuli vizuri, nami nikajikuta nimevutiwa navyo. Mtume ﷺ akajitayarisha kwa ajili ya vita hivyo, pamoja na Waumini. Nami nikatoka ili niweze kujiandaa kutoka pamoja nao, lakini nikarejea huku nikiwa sijajiandaa kitu. Nikawa najiambia, “Mimi naweza

kufanya hivyo muda wote pindi nitakapotaka". Nikaendelea kujichelewesha kila mara mpaka watu wakawa tayari wameshajitayarisha. Mtume ﷺ akaondoka pamoja na Waislamu. Mimi nilikuwa bado sijajiandaa chochote, na nikawa najiambia, "Nitajiandaa baada ya siku moja au mbili, halafu nitajiunga nao". Asubuhi ya siku ya pili baada ya kuondoka kwao nitatoka kwa ajili ya kufanya Maandalizi, lakini nikarejea bila ya kufanya chochote. Hali hiyo ikaendelea kunitokea, mpaka nikavikosa vita. Wakati huo, niliamua khasa kuondoka na kuungana nao. Natamani ingekuwa hivyo, lakini haikuwezekana. Nikatoka na kuwaendea watu baada ya Mtume ﷺ kuondoka, ikanihuzunisha kwamba kila niliyekutana naye alikuwa katika wale waliotuhumiwa unafiki au watu dhaifu ambao Allah تعالی Amewanusuru. Mtume ﷺ hakukumbuka mpaka akafika Tabuk, akauliza huku akiwa ameketi pamoja na watu huko Tabuk,

«مَا فَعَلَ كَعْبُ بْنُ مَالِكٍ؟»

*"Ka'b bin Malik amefanya nini?"*

Mtu mmoja katika Banu Salamah akajibu: "Ewe Mtume ﷺ, amezuiliwa na Burdah (nguo) zake mbili, kiburi na kujiona". Mu'adh bin Jabal رضي الله عنه akasema: "Ni kibaya sana ulichokisema. Wallah! Ewe Mtume ﷺ! Hatujui kumhusu yeye isipokuwa mazuri yake tu". Mtume ﷺ akanyamaza. Ka'b bin Malik رضي الله عنه akaendelea: "Khabari ziliponifikia kuwa Mtume ﷺ alikuwa akirejea Madinah, hali yangu ilinielemea, na nikawa nabuni namna ya kuongopa. Nikawa najiambia, "Kesho nitaiepuka vipi ghadhabu yake?" Nikawa natafuta msaada kutoka kwa jamaa zangu mwenye rai juu ya hili. Iliposemwa kwamba Mtume ﷺ amekaribia kuwasili (Madinah), basi kila lililokuwa batilifu lilinitoka akilini mwangu, na nikatambua kwamba abadani nisingeliweza kujinasua dhidi ya tatizo hili kwa kutunga uongo. Nikaazimia kusema ukweli. Mtume ﷺ akafika asubuhi, na kawaida yake alikuwa akishawasili kutoka safarini, alikuwa akianzia Msikitini kwanza, husali rakaa mbili, halafu huketi kwa ajili ya kusalimiana na watu. Baada ya kuyafanya hayo, wale ambao hawakujiunga naye vitani walikuja kwake na wakaanza kumtaja nyudhuru zao na kutoa viapo. Walikuwa watu zaidi ya themanini. Mtume ﷺ alizikubali nyudhuru zao kwa dhamiri yao na kuwaombea maghufira na siri zao alimuachia Allah تعالی ili Awahukumu. Mpaka mimi nilipomjia, na nilipomtotea *Salaam* alitabasamu kama anavyofanya mtu mwenye ghadhabu. Halafu akaniambia:

«تَعَالَى»

“Njoo.” Nikatembea mpaka mbele yake, na nikakaa. Akaniambia:

«مَا خَلَقَكَ أَنْتُمْ تَكُنُّنَ قَدْ اشْتَرَيْتَ ظَهْرًا»

“Ni nini kilichokukalisha nyuma, haukununua myama wa kukubeba?”

“Nikajibu: “Ewe Mtume! Kama ningelikuwa nimekaa mbele ya yeyote ghairi yako katika wakazi wa duniani, ningeamua kuondosha hasira zake kwa kumtajaia udhuru. Mimi nina kipaji cha kuzungumza kwa ufasaha, lakini, “Wallahi! Nimejua kwamba, lau kama nitakueleza leo maneno ya uongo ili kutaka radhi zako, basi, Allah تعالى Atakufanya unighadhibikie baada ya muda mfupi. Na kama nitakueleza ukweli, utanikasirikia, lakini nina matumaini ya kupata Msamaha wa Allah تعالى. Wallahi! Sikuwa na udhuru. Wallahi! Kamwe sijapata kuwa na nguvu na mali nyingi kuliko kipindi hiki ambacho sijajiunga nawe”. Mtume ﷺ akasema:

«أَمَّا هَذَا فَقَدْ صَدَقَ قَوْلُ حَتَّى يَقْضِيَ اللَّهُ فِيكَ»

“Ama huyu, amesema ukweli, kwa hiyo, simama mpaka Allah Atakapotoa hukumu inayomuhusu”.

Nikasimama, na akanifata mtu mmoja wa Bani Salama na wakasimama watu wengine na wakanifuata, wakaniambia: “Wallahi! Hatujapata kujua kuwa ulipata kufanya dhambi yoyote kabla ya hii, na umeshindwa kutaja udhuru wako kwa Mtume ﷺ kama walivyofanya hivyo wenzako ambao hawakujiunga. Dua ya Mtume ﷺ kukuombea maghufira inakutosha kusamehewa dhambi yako”. Wallahi! Waliendelea kunilaumu sana mpaka nikatamani nirejee kwa Mtume ﷺ na kujiongopea nafsi yangu. Kisha nikauliza: “Kuna mwingine yeyote aliyefikwa sawa na haya yangu?” Wakajibu: “Ndiyo kuna watu wawili ambao yamewasibu kama ya kwako, wao walisema sawa na ulivyosema wewe, na wakaambiwa mithili ya uliyoambiwa”. Nikauliza: “Ni akina nani hao?” Wakajibu: “Ni Murarah bin Ar-Rabi’ Al-‘Amiri na Hilal bin Umayyah Al-Waaqifi رضي الله عنهما”. Kwa hivyo, walinitajia watu wawili watenda mema ambao walishiriki katika vita vya Badr na wakawa ndio kiliwazo kwangu. Baada ya kutajiwa majina yao nikaondoka. Mtume ﷺ akawakataza Waislamu kuzungumza nasi. Sisi Watatu ambao hatukwenda vitani. Tukatengwa na watu

na wakatubadilikia mpaka ardhi (niliyokuwa nikiishi) ilionekana ngeni kwangu, haikuwa ile ardhi niliyokuwa nikijua. Tulibaki katika hali hiyo kwa muda wa siku Hamsini. Ama wenzangu wawili, walikaa katika nyumba zao wakilia. Ama mimi, nilikuwa mdogo zaidi na madhubuti kuliko wao. Nilikuwa nikishiriki Sala pamoja na Waislamu na kwenda sokoni, lakini hakuna aliyenisemesha. Nikawa namuendea Mtume ﷺ akiwa ameketi baada ya Sala, namtolea Salaam na najiambia katika nafsi yangu: “Ametikisa midomo yake kuitikia Salaam yangu au laa? Halafu nasali karibu yake na kumtazama kwa namna ya kuvizia. Nilipokuwa nikishughulika na Sala yangu alikuwa akiniangalia. Nilipokuwa nikigeuka kumtazama alikuwa akigeuza uso wake na kuelekeza kwingine. Baada ya kutengwa kwa muda mrefu na watu kunigomea, nilitembea mpaka nikafika katika ukuta wa Abu Qatadah ambaye ni mtoto wa ami yangu na nilimpenda sana, nikaruka, nikafika pale alipokuwa. Nikamsalimia lakini Wallahi! Hakuniitikia Salaam yangu. Nikamuuliza: “Ewe Abu Qatadah! Nakusihi kwa Allah! Je Unajua kwamba mimi ninampenda Allah ﷻ na Mtume?” Akanyamaza. Nikarudia kumueleza na kumsihi, akanyamaza, nikafanya tena hivyo, lakini hakunijibu. Halafu akasema: “Allah ﷻ na Mtume ﷺ ni wenye ujuzi zaidi.”

Macho yangu yakabubujikwa na machozi, nikageuka na kuondoka, nikaruka uzio. Nikiwa natembea katika soko la Madinah, nilikutana na Mkulima mmoja kutoka Sham aliyekuja kuuza chakula Madina. Akauliza, “Ni nani atakayenielekeza kwa Ka'b bin Malik”. Watu wakamuashiria kwangu. Akaja kunipa barua kutoka kwa Mfalme wa Ghassan (wa Syria chini ya Kaisar), kwa sababu nilikuwa najua kusoma na kuandika. Iliandikwa hivi: “Baada ya hayo, imetufikia khabari kuwa rafiki yako (Mtume ﷺ amekususa) ilhali Allah Hakukufanya uwe katika hali ya udhalili wala katika hali ya kupoteza haki. Kwa hivyo, ungana nasi, tukufariji”. Baada ya kuisoma, nikajiambia tena: “Huu ni mtihani mwingine”. Nikaipeleka barua hiyo katika tanuri, nikaiwasha moto na kuichoma. Baada ya kupita siku arubaini kati ya khamsini, akanijia mjumbe kutoka kwa Mtume ﷺ na kusema; “Mtume ﷺ anakuamuru ujitenge na mkeo”. Nikauliza: “Nimpe talaka au nifanyeje?” Akasema: “Bali ujiweke mbali naye, wala usimkaribie”. Wale wenzangu wawili, nao wakapelekewa ujumbe huo huo. Nikamuambia mke wangu: “Nenda kwenu na ukae na nduguzo, mpaka Allah ﷻ Atakapolihukumu jambo hili vile Atakavyo Yeye”. Mke wa Hilal bin

Umayyah akamuwendea Mtume ﷺ, akasema: “Ewe Mtume! Hilal ni mzee aliyedhoofika na hana mtumishi. Je hupendi nimtumikie?” Akamjibu,

«لَا وَلَكِنْ [لَا يَفْرَبُكَ]»

*“Hapana (unaweza kumhudumia), lakini asikukaribie”.*

Akasema mkewe: “Wallahi! Yeye hana hamu na chochote. Wallahi! Yeye hajaacha kulia tangu tatizo lake lilipoanza, mpaka siku yake hii ya leo”. Kisha akasema, baadhi ya Ndugu zangu wakaniambia: “Ungelimuomba idhini Mtume ﷺ kuhusu mkeo, kwani amemruhusu mke wa Hilal bin Umayyah kumhudumia”. Mimi nikasema: “Wallahi! Sitamuomba idhini Mtume ﷺ juu ya mke wangu kubaki kunihudumia, wala sijui atakachonijibu iwapo nitamuomba ruhusa, kwani mimi bado ni kijana”.

Tukakaa siku kumi zaidi, zikakamilika siku khamsini tangu watu wakatazwe kuzungumza nasi. Nikasali Alfajir asubuhi ya siku ya khamsini juu ya paa la mojawapo ya nyumba zetu. Nikiwa ningali niko katika hali yetu ambayo Allah تعالی Aliitaja (katika Qur’an), nafsi yangu ikadhikika na ardhi ikawa ndogo pamoja na upana wake, nikasikia sauti ya mtu aliyepanda mlimani akisema kwa sauti ya juu: “Pokea bishara ewe Ka’b bin Malik.” Nikaporomoka kwa kusujudu, nikajua faraji imeshakuja kutoka kwa Allah تعالی kwamba Ametusamehe. Mtume ﷺ akatangaza kukubaliwa kwa toba yetu wakati wa kipindi cha Sala ya Alfajir. Watu wakaja kunipa khabari njema, na wakaenda pia kuwajulisha wenzangu wawili. Akanijia upesi mtu akiwa juu ya farasi na wakati huo huo, mtu mmoja kutoka Banu Aslam naye akakwea juu ya mlima na sauti yake ikawa inakwenda kwa haraka zaidi kuliko farasi. Baada ya kunifikia yule ambaye nilikuwa naisikia sauti yake kunipa bishara, nikavua nguo zangu na kumvalisha yeye kwa kuniletea bishara hiyo. Wallahi! Siku hiyo, sikuwa na nguo nyingine isipokuwa hizo. Nikaazima nguo mbili, nikazivaa halafu nikaondoka kumfuata Mtume ﷺ, watu katika vikundi vikundi walinipokea kwa kunipongeza kutokana na Allah تعالی Kukubali toba yangu, wakisema: “Tunakupongeza kwa Allah تعالی Kuikubali toba yako”. Nikaingia Msikitini, nikamkuta Mtume ﷺ akiwa amekaa huku watu wamemzunguka. Twalhah bin ‘Ubaydullah akasimama kunikimbilia, tukashikana mikono na akanipongeza. Wallahi! Hapana yeyote katika Muhajirin ambaye alisimama kunilaki isipokuwa huyo. Kwa ajili hiyo, sitamsahahu Twalhah kwa kitendo hiki. Baada ya kumtolea *Salaam* Mtume ﷺ akaniambia huku uso wake ukiwa unang’aa kwa furaha:

«أَبْشِرْ بِخَيْرِ يَوْمٍ مَرَّ عَلَيْكَ مُنْذُ وَلَدْتِكَ أُمَّكَ»

*"Furahia siku njema ambayo hujapata kuiona tangu alipokuzaa mama yako".*

Nikauliza: "Ni kutoka kwako ewe Mtume ﷺ au kutoka kwa Allah تعالى?" Akajibu,

«لَا بَلَّ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ»

*"Hapana, bali ni kutoka kwa Allah".*

Uso wa Mtume ﷺ kipindi alichokuwa na furaha ulinururika mithili ya kipande cha mwezi, na hilo lilikuwa likijulikana na watu wanaomjua. Baada ya kuketi mbele yake, nilisema: "Ewe Mjumbe wa Allah تعالى! Kutokana na kupokelewa toba yangu, mali yangu yote nitaitoa Sadaka kwa Allah تعالى na kwa Mtume ﷺ". Akasema;

«أَمْسِكَ عَلَيْكَ بَعْضَ مَالِكَ فَهُوَ خَيْرٌ لَكَ»

*"Tunza baadhi ya mali zako, kwani hilo ni bora kwako"*

Nikasema: "Basi nitabakisha fungu langu nililolipata kutoka Khaybar". Nikasema: "Ewe Mtume! Allah تعالى Ameniokoa kwa sababu ya kusema ukweli, kwa hivyo, katika sehemu ya toba yangu nakuahidi kuwa nitasema kweli katika kipindi cha muda wangu wote niliosalia kuwa hai. Wallahi! Sikupata kumjua yeyote katika Waislamu, ambaye, Allah تعالى Alimjaalia kuwa msema kweli katika mazungumzo tangu nimtajie hayo Mtume ﷺ zaidi yangu mimi, tangu nimuahidi mpaka leo hii. Pia ninatumai kuwa Allah تعالى Atanihifadhi katika muda uliosalia."

Kwa hivyo, Allah تعالى Akateremsha Aya:

لَقَدْ تَابَ اللَّهُ عَلَى النَّبِيِّ وَالْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ فِي سَاعَةِ الْعُسْرَةِ  
 مِنْ بَعْدِ مَا كَادَ يَزِيغُ قُلُوبَ فَرِيقٍ مِّنْهُمْ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ إِنَّهُ بِهِمْ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١١٨﴾  
 وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خُلِفُوا حَتَّىٰ إِذَا ضَاقَتْ عَلَيْهِمُ الْأَرْضُ بِمَا رَحُبَتْ وَضَاقَتْ عَلَيْهِمْ  
 أَنْفُسُهُمْ وَظَنُّوْا أَنْ لَا مَلْجَأَ مِنَ اللَّهِ إِلَّا إِلَيْهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيْهِمْ لِيَتُوبُوا إِنَّ اللَّهَ هُوَ التَّوَّابُ  
 الرَّحِيمُ ﴿١١٩﴾ يَتَّيِبُهُمُ اللَّهُ وَأَمْنُوا بِآيَاتِهِ وَأَكْفَرُوا بِاللَّهِ وَرَكِبُوا فِي الْكُفْرِ الْكَبِيرِ ﴿١٢٠﴾

***“Mwenyezi Mungu Amekwishapokea toba ya Nabii na Wahajiri na Ansari waliomfuata katika saa ya dhiki, pale baada ya kukaribia nyoyo za baadhi yao kugeuka. Basi Akapokea toba yao, kwani hakika Yeye kwao wao ni Mpole na ni Mwenye Kuwarehemu. Na pia wale Watatu walioachwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjuvu wake, na nafsi zao zikanyongeka, na wakayakinika kuwa hapana pa kumkimbia Mwenyezi Mungu isipokuwa Kwake Yeye. Kisha Akawaelekea kwa Rehema Yake ili nao waendeleo kutubu. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kupokea toba na Mwenye Kurehemu. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na Kuweni pamoja na wakweli”. (9:117-119)***

Mpaka mwisho wa Aya hizo. Basi, Wallahi! Allah تعالى Hajanipa neema kubwa zaidi katika nafsi yangu baada ya kuniongoa kwa neema ya Uislamu kuliko kule kumuambia ukweli Mtume ﷺ katika siku hiyo, kwamba nisiwe muongo kama wale waliomuongopa ili nisije angamia kama walivyoangamia hao waliomdanganya. Kwani Allah تعالى Aliwataja kwa maneno mabaya wale waliomdanganya Mtume ﷺ. Pale Aliposhusha Wahyi Aliwataja kwa ubaya zaidi kuliko Alivyowahi kutajwa mtu mwingine yeyote. Allah تعالى Alisema:

سَيَخْلِفُونَ بِاللَّهِ لَكُمْ إِذَا أَنْقَلَبْتُمْ إِلَيْهِمْ لَتُعَرِّضُوا عَنْهُمْ ط فَأَعْرِضُوا عَنْهُمْ ط إِنَّهُمْ رِجْسٌ ط  
وَمَا وَنَهُمْ جَهَنَّمَ جَزَاءُ بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿١١٧﴾ سَخِلْفُونَ لَكُمْ لَتَرْضَوْنَ عَنْهُمْ ط فَإِنْ  
تَرْضَوْنَ عَنْهُمْ فَإِنَّ اللَّهَ لَا يَرْضَىٰ عَنِ الْقَوْمِ الْفَاسِقِينَ ﴿١١٨﴾

***“Watakuapieni kwa Mwenyezi Mungu mtakaporudi kwao ili muwaachilie mbali. Basi waachilieni mbali. Hakika hao ni najisi, na makazi yao ni Jahannamu, kuwa ni malipo kwa waliyokuwa wakiyachuma. Wanakuapieni ili muwa radhi nao. Basi hata mkiwa radhi nao nyie. Mwenyezi Mungu Hawi radhi na watu wapotofu.” (9:95-96)***

Ka'b رضي الله عنه akaendelea kusimulia: “Tulikuwa watu Watatu, tuliotofautiana na wale ambao Mtume ﷺ aliwakubalia nyudhuru zao pindi walipoapa. Alikubali kiapo chao na akawaombea maghufira kwa Allah تعالى, na akaliacha tatizo



letu lisubiri mpaka hapo Allah تعالى Atakapolitolea Uamuzi. Kwa hilo, Allah تعالى Alisema:

وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خَلَفُوا

**“Na pia wale watatu walioachwa nyuma...”.**

Alilolisema Allah تعالى hapa si suala la kutokujiunga kwetu na vita hivyo na kusubirishwa kwa tatizo letu bali ni kuhusu waliomuapia Mtume ﷺ na kumtajaia udhuru na akawakubalia”<sup>1</sup>. Hii ni Hadithi Sahih iliyothibiti na ambayo *Mut-tafaq* (imewafikiwa) juu ya usahihi wake. Hadithi kama hii imenukuliwa na wakusanyaji wa *Sahih* Mbili, Al-Bukhari na Muslim<sup>2</sup>. Hadithi hii imebeba maana ya Aya hii tukufu kwa njia nzuri na ndefu. Kadhalika, imesimuliwa na zaidi ya mwanazuoni mmoja wa *Salaf* katika kuitafsiri. Ni sawa na alivyosimulia Al-A'mash kutoka kwa Abu Sufyan, kutoka kwa Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَعَلَى الثَّلَاثَةِ الَّذِينَ خَلَفُوا

**“Na pia wale watatu walio achwa nyuma...”.**

Maana yake: Ni kuwa, “Hao ni Ka'b bin Malik, Hilaal bin Umayyah na Murarah bin Ar-Rabi' رضي الله عنهم na wote hao ni Ansvar”<sup>3</sup>.

### **Amri Juu ya Kusema Ukweli.**

Baada ya Allah تعالى Kutaja Faraja Zake kwa Kuwaondolea dhiki hao watu Watatu kutokana na Waislamu kuwatenga kwa siku khamsini, na kuwatia dhiki katika nafsi zao na ardhi – licha ya ukubwa wake, lakini njia zilifungwa dhidi yao, na hawakuongoka juu ya jambo la kufanya. Wakasubiri wakawa na unyenyekevu kwa Amri ya Allah تعالى, na wakawa imara mpaka Allah تعالى Alipowaletea ukunjufu kwa sababu ya kumuambia ukweli Mtume ﷺ kuhusu kutokujiunga kwao na kwamba hilo lilitokea pasi na udhuru, wakapewa adhabu kwa jambo hilo kwa muda, halafu Allah تعالى Akawasamehe. Matokea ya ukweli wao yakawa ni kupata kheri na kukubaliwa toba yao. Allah تعالى Alisema:

<sup>1</sup> Ahmad 3:457.

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Bari 8:193 na Muslim 4:2121.

<sup>3</sup> At-Tabari 14:544.

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ ﴿١١٨﴾

**“Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu na kuweni pamoja na wakweli”.**

Maana yake: Semeni ukweli na mshikamane na ukweli mtakuwa ni katika watu wakweli na mtanusurika na maangamizo. Pia, Allah تعالى Atakujaalieni kupata faraji na ufumbuzi katika mambo yenu. Imamu Ahmad aliandika kutoka kwa ‘Abdullah, na jina lake ni Ibn Mas’ud رضي الله عنه kuwa alisema: Mtume ﷺ alisema:

«عَلَيْكُمْ بِالصُّدْقِ فَإِنَّ الصُّدْقَ يَهْدِي إِلَى الْبِرِّ، وَإِنَّ الْبِرَّ يَهْدِي إِلَى الْجَنَّةِ، وَلَا يَزَالُ الرَّجُلُ يَصْدُقُ وَيَتَحَرَّى الصُّدْقَ حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ صِدْقًا، وَإِيَّاكُمْ وَالْكَذِبَ فَإِنَّ الْكُذِبَ يَهْدِي إِلَى الْفُجُورِ وَإِنَّ الْفُجُورَ يَهْدِي إِلَى النَّارِ، وَلَا يَزَالُ الرَّجُلُ يَكْذِبُ وَيَتَحَرَّى الْكُذِبَ حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ كَذَابًا»

*“Shikamaneni na ukweli, kwani ukweli huelekeza kwenye uchamungu, ambao huongoza kwenda Peponi. Na mtu hataacha kuwa mkweli na kujitahidi kuwa hivyo mpaka anaandikiwa kwa Allah kuwa ni mkweli. Nakutahadharisheni dhidi ya uongo kwani huongoza kuyaendea maovu, ambayo huongoza kwenda Motoni. Mtu hataacha kuwa mwongo na kushikamana nao mpaka huandikwa mbele ya Allah kuwa ni mwongo”<sup>1</sup>.*

Sahih Bukhari na Muslim zilionukuu Hadithi hiyo<sup>2</sup>.

مَا كَانَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ وَمَنْ حَوْلَهُمْ مِنَ الْأَعْرَابِ أَنْ يَتَخَلَّفُوا عَنِ رَسُولِ اللَّهِ وَلَا يُرْغَبُوا بِأَنْفُسِهِمْ عَنِ نَفْسِهِمْ<sup>١</sup> ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ لَا يُصِيبُهُمْ ظَمَأٌ وَلَا نَصَبٌ وَلَا مَخْمَصَةٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَلَا يَطْئُونَ مَوْطِئًا يَغِيظُ الْكُفَّارَ وَلَا يَنَالُونَ مِنْ عَدُوِّ نَيْلًا إِلَّا كُتِبَ لَهُمْ بِهِ عَمَلٌ صَالِحٌ<sup>٢</sup> إِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٢٠﴾

**120. “Haiwafalii watu wa Madina na Mabedui walio jirani zao kubakia nyuma wasitoke na Mtume, wala kujipendelea nafsi zao**

<sup>1</sup> Ahmad 1:384.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 10:523 na Muslim 4:2012.

***kuliko yeye. Hayo ni kwa kuwa hakiwapati kiu, wala machafu, wala njaa, kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawaendi mahali panapowaghadhibisha makafiri, wala hakiwapati chochote kutokana na maadui, ila huandikwa kuwa ni kitendo chema. Hakika Mwenyezi Mungu Haupotezi ujira wa wanaofanya mema”.***

### **Malipo ya Kutoka Kwenda Kupigana Jihadi.**

Allah تعالى Anawalaumu watu wa Madinah na mabedui waliokuwa wakiishi kuuzunguka mji huo waliobaki nyuma badala ya kushirikiana na Mtume ﷺ katika vita vya Tabuk. Walipendelea kujibakisha nyuma, badala ya kumfariji Mtume ﷺ katika taabu. Wamezikhasiri nafsi zao katika fungu lao la malipo, kwa sababu,

لَا يُصِيبُهُمْ ظَمَأٌ

“...***hakiwapati dhamaun***”. Maana yake: Kiu.

وَلَا نَصَبٌ

“...***wala machafu***”. Ambayo ni kutaabika.

وَلَا مَخْمَصَةٌ

“...***wala njaa***”. Inamaanisha, haja ya chakula.

وَلَا يَطُورُ مَوَاطِنًا يَغِيظُ الْكُفَّارَ

“...***wala hawaendi mahali panapowaghadhibisha makafiri.***”

Kwa mbinu za kivita zenye kuwaogofya maadui zao.

وَلَا يَتَأَلَوْنَ

“...***wala hakiwapati chochote kutokana na maadui.***”

Katika kushindwa kwa jeshi.

إِلَّا كُتِبَ لَهُم

“...***ila huandikwa kuwa ni kitendo chema.***”

Kutokana na amali hizi ambazo haziko chini ya uwezo wao, bali ni matokeo ya amali njema na malipo mazuri.

إِنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُحْسِنِينَ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Haupotezi ujira wa wanaofanya mema”.**

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا

**“...hakika Sisi Hatupotezi ujira wa anayetenda mema”. (18:20)**

وَلَا يُنْفِقُونَ نَفَقَةً صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً وَلَا يَقْطَعُونَ وَادِيًا إِلَّا كُتِبَ لَهُمْ لِيَجْزِيَهُمْ

اللَّهُ أَحْسَنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٦﴾

**121. “Wala hawatoi cha kutoa kidogo wala kikubwa, wala hawalivuki bonde, ila huandikiwa, ili Mwenyezi Mungu Awalipe bora ya waliyo kuwa wakiyatenda”.** Allah تعالى Anasema:

وَلَا يُنْفِقُونَ

**“Wala hawatoi”.** Hao wapiganaji katika njia ya Allah تعالى.

نَفَقَةً صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً

**“...cha kutoa kidogo wala kikubwa”.** Maana yake kichache wala kingi.

وَلَا يَقْطَعُونَ وَادِيًا

**“...wala hawalivuki bonde”.** Katika kuwaendea maadui.

إِلَّا كُتِبَ لَهُمْ

**“...ila huandikiwa”.** Hapa, Allah تعالى hakusema “Bihī” bali Ametumia neno “Lahum”, kwa sababu matendo yanafanywa na wao. Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema:

لِيَجْزِيَهُمُ اللَّهُ أَحْسَنَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**“...ili Mwenyezi Mungu Awalipe bora ya waliyokuwa wakiyatenda”.**

Amiri wa waumini, ‘Uthman bin ‘Affan رضي الله عنه alipata hadhi na fungu kubwa la fadhila, kwa kutoa mali nyingi sana katika vita hivyo (Tabuk). Abdullah, mtoto wa Imam Ahmad alinukuu kuwa ‘Abdallah bin Khabbab As-Sulami رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alihutubu na kuhimiza kutoa mali kwa ajili ya jeshi gumu (la Tabuk).

'Uthman bin 'Affan رضي الله عنه alisema, 'Nitatoa ngamia mia moja pamoja na matandiko yao.' Halafu akawahimiza zaidi. 'Uthman رضي الله عنه akasema tena, 'Nitaongeza ngamia wengine mia moja pamoja na matandiko yao.' Mtume ﷺ akashuka kidato kimoja cha mimbari na akawahimiza tena. 'Uthman bin 'Affan رضي الله عنه akasema, 'Nitaongeza ngamia wengine mia moja pamoja na matandiko yao.' Nikamuona Mtume ﷺ akionesha mkono wake kama hivi huku mkono wa 'Abdus-Swamad (mmojawapo katika wasimulizi) ukiashiria jinsi ilivyokuwa kwa kumaanisha kustaajabu - huku akisema:

«مَا ضَرَّ ابْنَ عُمَانَ مَا عَجَلَ بَعْدَ التَّيْمِ»

"Mwana wa 'Affan hakitamdhuru chochote alichokifanya baada ya leo"<sup>1</sup>.

'Abdullah رضي الله عنه alisimulia tena kutoka kwa 'Abdur-Rahman bin Samurah رضي الله عنه kuwa alisema: "Uthman رضي الله عنه alikuja kwa Mtume ﷺ akiwa na dinari elfu moja nguoni mwake ambazo Mtume ﷺ alizitumia kuliandaa jeshi lake gumu. Akazimimina mapajani mwa Mtume ﷺ, naye akawa anazigeuzageuza kwa mkono wake na kusema:

«مَا عَلَى عُثْمَانَ مَا عَجَلَ بَعْدَ هَذَا»

"Mwana wa 'Affan (yaani 'Uthman) hatadhurika baada ya haya aliyoyafanya leo." Ikawa Mtume ﷺ anakariri kauli hiyo,<sup>1</sup>

Qatadah alitoa rai juu ya Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا يَقْطَعُونَ وَاذِيًّا إِلَّا كُتِبَ لَهُمْ

"...wala hawalivuki bonde, ila huandikiwa...". Qatadah alisema, "Kadiri kaumu inavyozidisha kuwa katika njia ya Allah تعالى، ndivyo watakavyokuwa karibu zaidi na Allah تعالى"<sup>2</sup>.

\* وَمَا كَانَ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنْفِرُوا كَافَّةً ۚ فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ لِّيَتَفَقَّهُوا

فِي الدِّينِ وَلِيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ ﴿١٢٢﴾

**122. "Wala haiwafalii Waumini kutoka wote. Ni vyema katika kila kundi miongoni mwao, wangelitoka kujifunza baadhi yao**

<sup>1</sup> Ahmad 5:63.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:565.

***vyema Dini, na kisha waje kuwaonya wenzao watakapowarejea, ili wapate kujihadharisha”.***

Hapa, Allah تعالى Anaeleza Amri Yake ya Kuwataka Waislamu kwenda pamoja na Mtume ﷺ katika vita vya Tabuk. Kwanza vizuri tueleze kuwa kikundi cha *Salaf* kinasema kuwa jambo la kujiunga na Mtume ﷺ pindi anapotoka kwenda vitani, lilikuwa ni wajibu kwa kila Muislamu. Kwa minajili hii, Allah تعالى Alisema:

أَنْفِرُوا خِفَافًا وَثِقَالًا

***“Nendeni mtoke, mkiwa wepesi na wazito.” (9:41)***

Na Amesema,

مَا كَانَ لِأَهْلِ الْمَدِينَةِ وَمَنْ حَوْلَهُمْ مِنَ الْأَعْرَابِ

***“Haiwafalii watu wa Madinah na Mabedui walio jirani zao...” (9:120)***

Inasemekana Allah تعالى Alifuta hukumu ya Aya hiyo (9:41) kwa hii (9:120). Huenda kukasemwa pia kuwa ayah hii inafafanua maana ambayo Allah تعالى Aliikusudia pale Alipowataka Waarabu wote walio majirani washiriki vitani na kwamba angalau kuwepo kikundi kutoka katika kila kabila kijiunge katika kupigana Jihadi, ili wale watakaojiunga na Mtume ﷺ wapate kufahamu Wahyi unaoteremshwa kwake, na wawaonye kaumu zao kuhusu vita walivyopigana pindi warejeapo. Kwa hiyo yanawajumuikia mambo mawili kutokana na utokaji huu maalumu, na baada yake kundi linaloungana na Mtume ﷺ kwa ajili ya vita linakuwa, ama limepata uelewa (wa mambo ya dini) au limejifunza kupigana Jihadi, kwani ni Faradhi inayohitajika kufanywa na angalau sehemu ya umma wa Kiislamu. ‘Ali bin Abu Twalhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Aya ifuatayo:

• وَمَا كَانَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ لِيَنْفِرُوا كَافَّةً

***“Wala haiwafalii Waumini kutoka wote”.***

Haiwafalii Waumini watoke wote na kumuacha Mtume ﷺ peke yake.

فَلَوْلَا نَفَرَ مِنْ كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ

***“Ni vyema katika kila kundi miongoni mwao, walingelitoka baadhi yao.”***

Maana yake: Kundi au kikosi, wala wasiende isipokuwa kwa idhini yake. Kundi likisharejea na Aya za Qur'an zimeshashuka baada yao, basi kundi lililobakia litajifunza kwa Mtume ﷺ. Wakisharejea watasema: "Allah تعالى Amemte-remshia Mtume wenu ﷺ Aya za Qur'an, nasi tumefundishwa kadha wa kadha, kundi hilo nalo litajifundisha kutoka kwao yale yaliyoshushwa kwa Mtume ﷺ katika wakati ambapo hawakuwepo. Hao nao wanalifikishia kundi jingine. Hii ndiyo maana ya Kauli ya Allah تعالى;

لَيَتَفَقَّهُوْا فِي الدِّينِ

**"...wakajifunze vyema Dini".**

Anasema, ili wakajifunze juu ya yale Aliyoyateremsha Allah تعالى kwa Mtume wao, pia ili wapiganaji wajifunze mbinu za kivita na pindi wakisharejea kwa wenzao wawape mafunzo waliyoyapata.

لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ

**"...ili wapate kujihadharisha".<sup>1</sup>**

Mujahid alisema: Ayah hii ilishuka kuhusu kikundi cha Masahaba wa Mtume ﷺ ambao walitoka kwenda majangwani na wakapata msaada wa watu na mwaka mzuri wa mvua. Walimlingania katika uongofu kila mtu waliyekutana naye. Watu wakawaambia, "Tunakuoneni kuwa mmewaacha jamaa zenu na mmekuja kwetu". Wakajisikia vibaya kwa sababu hiyo, na wote wakaondoka majangwani na kurejea kwa Mtume ﷺ. Allah تعالى Akasema;

فَلَوْلَا نَفَرَ مِن كُلِّ فِرْقَةٍ مِّنْهُمْ طَائِفَةٌ

**"Ni vyema katika kila kundi miongoni mwao, walingelitoka baadhi yao."**

Wanaotafuta kheri.

لَيَتَفَقَّهُوْا فِي الدِّينِ

**"...wakajifunze vyema Dini".**

Kwa kuyasikia waliyo nayo watu, na tena wajifunze Aliyoyateremsha Allah تعالى.

<sup>1</sup> At-Tabari 14:567.

وَلْيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ

**“...na kisha waje kuwaonya wenzao”.**

Wote pindi watakaporejea.

لَعَلَّهُمْ يَحْذَرُونَ

**“...ili wapate kujihadharisha”<sup>2</sup>.**

Qatadah alisema: kuhusu Aya hiyo: “Inahusu kipindi ambacho Mtume ﷺ anapo yaagiza majeshi, Allah تعالی Aliwaamuru waingie vitani huku kundi jingine likibaki pamoja na Mtume ﷺ likifundishwa Dini. Kundi jingine linarejea kwa watu wao kwa ajili ya kuwalingania na kuwatahadharisha juu ya adhabu ya Allah تعالی iliyowapata waliokuwepo kabla yao”<sup>1</sup>. Ibn Abuu Twalha vilevile amesema kutoka kwa Ibn Abbasi رضي الله عنهما: Kauli Yake Allah تعالی,

\* وَمَا كَانِ الْمُؤْمِنُونَ لِيَنْفِرُوا كَافَّةً

**“Wala haiwafalii Waumini kutoka wote”.**

Aya hii haihusu kujiunga na Jihadi, lakini ni kwamba Mtume ﷺ alipomuomba Allah تعالی dhidi ya Mudhwar, kwamba Awape mtihani wa kupatwa na njaa kwa miaka kadhaa walipatwa na baa hilo. Baadhi ya makabila miongoni mwao yakaanza kuja, mpaka kipindi fulani likaja kabila lote Madinah, na kwa sababu ya njaa iliyowapata, wakadai wamesilimu ilhali wanaongopa. Wakawadhikisha Masahaba wa Mtume ﷺ. Allah تعالی Akateremsha Aya Kumjulisha Mtume ﷺ kwamba hao si waumini. Mtume ﷺ akawarejesha katika makabila yao na akawaonya watu wao wasirudie tena kitendo chao. Kwa hivyo, Allah تعالی Akasema;

وَلْيُنذِرُوا قَوْمَهُمْ إِذَا رَجَعُوا إِلَيْهِمْ

**“...na kisha waje kuwaonya wenzao watakapowarejea”.**

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 14:566.

<sup>2</sup> At-Tabari 14:568.



يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَتَلُوا الَّذِينَ يُلُونَكُمْ مِنَ الْكُفَّارِ  
 وَلَيَجِدُوا فِيكُمْ غِلْظَةً ۗ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ ﴿١٢٣﴾  
 وَإِذَا مَا أَنْزَلَتْ سُورَةٌ فَمِنْهُمْ مَن يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ  
 هَذِهِ ءِيمَنًا ۗ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا فَزَادَتْهُمْ إِيمَنًا وَهُمْ  
 يَسْتَبْشِرُونَ ﴿١٢٤﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ  
 فَزَادَتْهُمْ رِجْسًا إِلَىٰ رِجْسِهِمْ وَمَاتُوا وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿١٢٥﴾  
 أَوْلَا يَرَوْنَ أَنَّهُمْ يُفْتَنُونَ فِي كُلِّ عَامٍ مَّرَّةً أَوْ مَرَّتَيْنِ  
 ثُمَّ لَا يَتُوبُونَ وَلَا هُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿١٢٦﴾ وَإِذَا مَا  
 أَنْزَلَتْ سُورَةٌ نَّظَرَ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ هَلْ يَرَيْنَاكُمْ مِنْ  
 أَحَدٍ ثُمَّ انصَرَفُوا ۗ صَرَفَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا  
 يَفْقَهُونَ ﴿١٢٧﴾ لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ  
 عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ  
 رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢٨﴾ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ لَا إِلَهَ  
 إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ ۗ وَهُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿١٢٩﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَتَلُوا الَّذِينَ  
 يُلُونَكُمْ مِنَ الْكُفَّارِ وَلَيَجِدُوا  
 فِيكُمْ غِلْظَةً ۗ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ  
 الْمُتَّقِينَ ﴿١٢٣﴾

**123. "Enyi mlio amini!  
 Piganeni na wale makafiri  
 walio karibu yenu, na  
 wakute Ugumu kwenu. Na  
 Jueni ya kwamba Mwe-  
 nyezi Mungu Yu pamoja na  
 wacha-Mungu".**

**Amri ya Jihadi Dhidi ya  
 Makafiri, wa Karibu, Zaidi  
 Kisha Wanaowafuatia.**

Allah تعالی Amewaamuru  
 Waumini wapigane dhidi ya  
 makafiri kwa mfuatano,  
 walio karibu kabisa na Dola

ya Kiislamu, kisha wanao- fuatia kwa ukaribu na kwa ajili hiyo, Mtume ﷺ alianza kwa kuwapiga Washirikina katika Bara la Uarabuni. Baada ya kumaliza na kupata ushindi wa Makkah, Madina, Twaif, Yemen, Yamamah, Hajr, Khaybar, Hadhramawt na sehemu nyingine katika maeneo ya Bara la Uarabuni, watu wengine wakaingia katika Dini ya Allah تعالی makundi kwa makundi, baada ya hapo alianza mapigano na Watu wa Kitabu. Akajiandaa kwa ajili ya kuwapiga Warumi ambao ndio watu wa karibu zaidi na Eneo la Arabuni, na ndio watu waliofaa zaidi kulinganiwa katika Uislamu kwani wao ni Watu wa Kitabu. Akafika mpaka Tabuk, Halafu akarejea kwa sababu ya taabu waliyoipata watu ya kudhoofika na kupatwa na dhiki. Huo ulikuwa mwaka wa tisa baada ya Hijra yake.

Katika mwaka wa kumi alijishughulisha na Hijjah ya Kuaga kisha umauti ukamuwahi. Akafariki baada ya siku Themanini na moja tangu atoke Hijjah. Allah تعالى Akamkhitari kulingana na Alivyomuandalia. Baada yake, uongozi ukashikwa na waziri wake, rafiki yake na Khalifa wake, Abubakr As-Siddiq رضي الله عنه. Wakati huo, Dini ilipita kipindi kigumu na kukaribia kushindwa. Allah تعالى Akaipa Dini Yake umadhubuti kupitia kwa Abubakr رضي الله عنه, ambaye Aliifanya iwe madhubuti na akaiimarisha misingi yake. Akawarudisha waliokuwa wakitatizika na walioritadi akawarejesha katika Uislamu. Aliikusanya Zaka kutoka kwa watu waovu walioizuia. Akaubainisha ukweli kwa ambao hawakuujua. Kwa niaba ya Mtume ﷺ, Abubakr رضي الله عنه alirudisha kila amana aliyopewa. Halafu akaanza kuyaandaa majeshi ya Waislamu kwa ajili ya kwenda kwa Warumi walioabudu msalaba, na kwa Waajemi walio abudu moto. Allah تعالى Akamfungulia miji na nchi mbalimbali, akamuangusha Kisra na Kaisari waliokuwa chini ya utii wao. Abubakr رضي الله عنه akazitumia hazina zao alizoziteka katika njia ya Allah تعالى, sawa na Mtume ﷺ alivyoelekeza. Mpango huu uliendelea baada ya Abubakr رضي الله عنه, chini ya mtu ambaye alimchagua kushika mahali pake, Al-Faruq na Shahidi wa *Mihrab*<sup>1</sup>, Abu Hafsw 'Umar bin Al-Khattwab رضي الله عنه. Allah تعالى kupitia kwake yeye akaziteka Himaya za wafalme, aliwaangamiza makafiri, akawakandamiza waasi na wanafiki na akayafungua maeneo ya Mashariki na Magharibi mwa dunia. Khazina za mali katika maeneo mengine ya mbali na ya karibu zilipelekwa kwake. Akazigawa kwa kufuata Sharia na njia iliyoridhiwa. Kisha baada ya kufariki akiwa shahidi baada ya kuishi maisha ya kusifika, Masahaba miongoni mwa Muhajirina na Answaar walijumuika chini ya Ukhalifa wa Amiri wa Waumini, 'Uthmaan bin 'Affan رضي الله عنه, shahidi wa ndani ya Nyumba. Uislamu ukavaa vazi lake pana la uongozi na ushahidi usiopingika. Dini ya Allah تعالى ikaenezwa katika maeneo mengi ya dunia. Uislamu ukaenea mpaka Mashariki na Magharibi. Kalima ya Allah تعالى ikawa juu na Dini Yake ikashinda. Dini sahihi ikafikia malengo yake dhidi ya maadui wa Allah تعالى. Na kila umma wa Kiislamu ulipopata ushindi ulisonga mbele dhidi ya wanaofuata miongoni mwa madhalimu waovu. Walifanya hivi kwa kufuata Kauli ya Allah تعالى,

---

<sup>1</sup> Mahali ambapo 'Umar رضي الله عنه aliuwawa wakati akiwasalisha Waislamu.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا فَنِتْلُوا الَّذِينَ يُلُونَكُمْ مِنَ الْكُفَّارِ

**“Enyi mliaoamini! Piganeni na wale makafiri walio karibu yenu”.**

Kauli ya Allah تعالى:

وَلِيَجِدُوا فِيكُمْ غِلْظَةً

**“...na wakute Ugumu kwenu”.**

Maana yake: Makafiri wapate ugumu kutoka kwenu kutokana na nyinyi kuwapiga, kwani Muumini kamili ni yule aliye mpole kwa nduguye na mgumu kwa adui yake, kafiri.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَسَوْفَ يَأْتِي اللَّهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ

**“...basi Mwenyezi Mungu Atakujaleta watu Anaowapenda nao wanampenda, wanyenyekevu kwa Waumini na wenye nguvu juu ya makafiri”. (5:54)**

Na Kauli Yake Allah تعالى:

مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ ؓ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ ؓ

**“Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao”. (48:29)**

Na Kauli Yake Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا النَّبِيُّ جَاهِدِ الْكُفَّارَ وَالْمُنَافِقِينَ وَأَغْلُظْ عَلَيْهِمْ ؓ

**“Ewe Nabii! Pambana na makafiri na wanafiki, na wakazanie”. (9:73)**

Kauli ya Allah تعالى:

وَأَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُتَّقِينَ

**“Na Jueni ya kwamba Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wacha-Mungu”.**

Maana yake: Wapigeni makafiri na mumtegemee Allah تعالى, na mjue kwamba Allah تعالى Yu pamoja nanyi pindi mtakapomcha na mtakapomtii. Hivi ndivyo ilivyokuwa kwa vizazi vitatu ambavyo ndio bora katika ummah huu kwa kufikia kiwango cha juu cha imani na uimara katika kumtii Allah تعالى, na waliendelea kuwashinda maadui zao. Ushindi ukawa mwingi na maadui wakaendelea kushuka chini na kuingia katika khasara”.

Kisha baada ya kutokea kwa Fitnah, utashi na ikhtilafu zikajitokeza baina ya wafalme na viongozi wa Kiislamu wenye tamaa, maadui wakapata tamaa ya kushambulia vituo vya Waislamu na wakafanya hivyo, wala hawakupata upinzani, kwa sababu wafalme wa Kiislamu walikuwa wakijishughulisha na uadui baina yao wenyewe. Wakaenda na kuiteka miji mikuu ya Waislamu, na hawakukomea hapo mpaka wakaiteka miji mingi ya Waislamu, (na jambo lote kuanzia mwanzo mpaka mwisho liko kwa Allah تعالى).

Kila ataposimama Mtawala mmojawapo wa Kiislamu, akatii Amri za Allah تعالى na akamtegemea Allah تعالى, basi Allah تعالى Atamfungulia ushindi katika nchi mbalimbali, katika nchi za maadui na kuzirejesha kwa Waislamu kwa kiwango kinacholingana na utiifu wa kumtii Allah تعالى. Tunamuomba Allah تعالى Awamakinishe Waislamu wawadhibiti maadui zao, makafiri, na Alinyanyue neno lao katika maeneo mengine, kwa hakika, Yeye ni Mkarimu na Mpaji sana.

وَإِذَا مَا أَنْزَلَتْ سُورَةً فَمِنْهُمْ مَن يَقُولُ أَيْكُمُ زَادَتْهُ هِذِهِ إِيمَانًا فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا  
فَزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿١٢٤﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَّرَضٌ فَزَادَتْهُمْ رِجْسًا  
إِلَىٰ رِجْسِهِمْ وَمَاتُوا وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿١٢٥﴾

**124. “Na inapoteremshwa Surah wapo miongoni mwao wasemao: Ni nani miongoni mwenu Surah hii imemzidishia Imani? Ama wale walioamini inawazidishia Imani, nao wanafurahi”.**

**125. “Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao, basi inawazidishia uovu juu ya uovu wao; na wanakufa hali ni makafiri”.**

## Imani ya Waumini Huongezeka na Hupungua Wakati Wanafiki Huzidi Shaka na Wasiwasi.

Allah تعالی Anasema;

وَإِذَا مَا أَنْزَلَتْ سُورَةٌ

**“Na inapoteremshwa Surah”.**

Basi wapo katika wanafiki.

مَنْ يَقُولُ أَيْكُمْ زَادَتْهُ هَذِهِ إِيمَانًا

**“...wasemao: Ni nani miongoni mwenu Surah hii imemzidishia Imani?”**

Wao huambizana, ni nani katika nyinyi ambaye Surah hii inamzidishia Imani?

Allah تعالی Anasema;

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا فَزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ

**“Ama wale walioamini inawazidishia Imani, nao wanafurahi”.**

Aya hii ni moja wapo ya ushahidi mkubwa kwamba Imani ya Muislamu huongezeka na kupungua. Ni sawa na zilivyo rai za Maulamaa wengi miongoni mwa *Salaf* na *Khalaf*. Maulamaa wanasema kuwa wengi wanaiunga mkono hoja hiyo. Maelezo juu ya mada hii yameelezwa kwa kirefu mwanzoni mwa sherehe ya Kitabu cha Bukhari, Allah تعالی Amrehemu.

وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ فَزَادَتْهُمْ رِجْسًا إِلَىٰ رِجْسِهِمْ

**“Ama wale wenye maradhi katika nyoyo zao, basi inawazidishia uovu juu ya uovu wao”.**

Maana yake: Huwaongezea mashaka na wasiwasi kwa Mola wao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی Aliyosema:

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ

**“Na Tutateremsha katika Qur’an yaliyo ni matibabu.” (17:83)**

Na Kauli Yake Allah تعالی ,

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً ۗ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَاذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى ۗ اُولٰٓئِكَ يُنَادَوْنَ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٤٤﴾

**“Sema: Qur’an hii ni uwongofu na pozo kwa wenye kuamini. Na wasioamini umo uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni. Hao wanaitwa nao wako pahala mbali”. (41:44)**

Hii inaonesha uovu wa wanafiki kwamba yanayoziongoza nyoyo za Waumini ndiyo sababu ya kupotea na kuangamia kwa nyoyo zao. Ni kama mfano wa mtu kujisikia vizuri baada ya kula chakula kizuri lakini akajisikia vibaya.

اَوَّلًا يَرَوْنَ اَنَّهُمْ يُفْتَنُونَ فِي كُلِّ عَامٍ مَّرَّةً اَوْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ لَا يَتُوبُونَ وَلَا هُمْ يَذَكَّرُونَ ﴿١٢٦﴾ وَاِذَا مَا اُنزِلَتْ سُورَةٌ نَّظَرَ بَعْضُهُمْ اِلَىٰ بَعْضٍ هَلْ يَرٰنَكُمْ مِّنْ اَحَدٍ ثُمَّ اَنْصَرَفُوْا صِرَفَ اللّٰهِ قُلُوْبُهُمْ بِاٰيٰتِهِمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُوْنَ ﴿١٢٧﴾

**126. “Je, huwaoni ya kwamba wanaitwa mtihanini kila mwaka mara moja au mara mbili? Kisha hawatubu, wala hawakumbuki”.**

**127. “Na ikiteremka Surah hutazamana wao kwa wao, (kama kwamba wanasema) Je! Yuko mtu anakuoneni? Kisha hugeukilia mbali. Mwenyezi Mungu Amezigeuza nyoyo zao kwa kuwa hao ni watu wasio fahamu”.**

**Kutahiniwa kwa Wanafiki.**

Allah تعالیٰ Anasema: Kwani hawa wanafiki hawaoni,

اَنَّهُمْ يُفْتَنُونَ

**“...kwamba wanaitwa mtihanini”.**

Maana yake: Wanajaribiwa.

فِي كُلِّ عَامٍ مَّرَّةً اَوْ مَرَّتَيْنِ ثُمَّ لَا يَتُوبُونَ وَلَا هُمْ يَذَكَّرُونَ

**“kila mwaka mara moja au mara mbili? Kisha hawatubu, wala hawakumbuki”.**

Maana yake: Hawatubu kutokana na madhambi yao yaliyopita, wala hawakumbuki hali zao katika mustakabali wao. Mujahid alisema, “Wanatahaniwa kwa Ukame na njaa.”<sup>1</sup> Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَإِذَا مَا أَنْزَلَتْ سُورَةً نَّظَرَ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ هَلْ يَرَيْنَا مِنْ أَحَدٍ ثُمَّ أَنْصَرَفُوا  
صَرَفَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ ﴿١٢٣﴾

**“Na ikiteremka Surah hutazamana wao kwa wao, (kama kwamba wanasema) Je! Yuko mtu anakuoneni? Kisha hugeukilia mbali. Mwenyezi Mungu Amezigeuza nyoyo zao kwa kuwa hao ni watu wasio fahamu”.**

Hizi pia khabari za wanafiki, kwamba pindi ikiteremshwa Surah mojawapo kwa Mtume ﷺ،

نَّظَرَ بَعْضُهُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ

**“...hutazamana wao kwa wao”.** Kwa maana: Huangaliana.

هَلْ يَرَيْنَا مِنْ أَحَدٍ ثُمَّ أَنْصَرَفُوا

**“...(kama kwamba wanasema) Je! Yuko mtu anakuoneni? Kisha hugeukilia mbali”.**

Maana yake: Wao ukweli huupa mgongo na wakiondoka huacha na hii ndiyo hali yao duniani, hawawi imara katika ukweli wala hawakubali wala hawaufahamu. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى؛

فَمَا لَهُمْ عَنِ التَّذْكَرَةِ مُعْرِضِينَ ﴿٧٤﴾ كَأَنَّهُمْ حُمُرٌ مُّسْتَنْفِرَةٌ ﴿٧٥﴾ فَرَّتْ مِنْ قَسْوَرَةٍ ﴿٧٦﴾

**“Basi wana nini hata wanapuuza onyo hili? Kama kwamba wao ni mapunda milia waliotimuliwa, wanaomkimbia simba!” (74:49-51)**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

فَمَالِ الَّذِينَ كَفَرُوا قَبْلَكَ مُهْطِعِينَ ﴿٧٠﴾ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ عِزِينَ ﴿٧١﴾

**“Wana nini wale waliokufuru wanakutumbulia macho tu? Makundi kwa makundi upande wa kulia na upande wa kushoto!” (70:36-37)**

<sup>1</sup> At-Tabari 14:580.

Watu hao wana nini kwani wanakukodolea macho kutokea upande wa kuumeni na kushoto, huku wakiukimbia ukweli na wakiuendea upotevu.

Kauli ya Allah تعالى:

ثُمَّ أَنْصَرَفُوا ۖ صَرَفَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ

**“Kisha hugeukilia mbali. Mwenyezi Mungu Amezigeuza nyoyo zao”.**

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاغَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ

**“Walipopotoka, Mwenyezi Mungu Aliziachia nyoyo zao zipotoke”.**  
(61:5)

Kauli ya Allah تعالى,

بِأَنَّهُمْ قَوْمٌ لَا يَفْقَهُونَ

**“...kwa kuwa hao ni watu wasiofahamu”.**

Maana yake: Hawayafahamu maneno ya Allah تعالى, wala hawajaribu kuyaelewa wala hawataki. Bali wao wanashughulishwa mbali nayo, na wenye kuyakimbia. Kwa ajili hii, wameishia katika hali hiyo.

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ  
بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢٨﴾ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلَيْهِ  
تَوَكَّلْتُ وَهُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿١٢٩﴾

**128. “Hakika amekwishakujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayokutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma”.**

**129. “Basi wakigeuka, wewe sema: Mwenyezi Mungu Ananitoshleza. Hapana mola isipokuwa Yeye tu. Mimi namtegemea Yeye, na Yeye Ndiye Mola Mlezi wa Kiti Kikuu cha Enzi”.**



**Kuletwa Mtume ﷺ ni Neema Kubwa Kutoka kwa Allah تعالى**

Allah تعالى Anawakumbusha Waumini kuwa Amewapelekea Mtume ﷺ kutokana na wao wenyewe, maana, kutokana na jinsi ya lugha yao. Kama alivyosema Ibrahim عليه السلام:

رَبَّنَا وَأَبْعَثْ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْهُمْ

**“Ewe Mola Mlezi wetu! Walettee Mtume anayetokana na wao”.**

(2:129)

Na Allah تعالى Amesema,

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Amewafanyia wema mkubwa Waumini vile Alivyowaletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe”.**

(3:164)

Kauli ya Allah تعالى;

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ

**“Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe”.**

Maana yake: Kutokana na nyinyi na anazungumza kwa lugha yenu. Ni sawa na alivyosema Ja'far bin Abu Talib رضي الله عنه, alimuambia An-Najjash, naye Mughira bin Shu'bah رضي الله عنه alimuambia mjumbe wa Kisra: “Hakika, Allah تعالى Ametuletea Mtume ﷺ kutoka miongoni mwetu, ambaye tunaijua nasaba yake, sifa zake, kuingia na kutoka kwake, tunaujua ukweli na uaminifu wake”<sup>1</sup>.

Kauli ya Allah تعالى;

عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ

**“...yanamhuzunisha yanayokutaabisheni”.**

Maana yake: Kinamhuzunisha kitu kinachosumbua umma wake na kuwatatiza. Ndani ya *Sahih* kuna Hadithi, ambayo Mtume ﷺ anasema;

«بُعِثْتُ بِالْخَيْفَةِ السَّمْحَةِ»

**“Nimetumwa na imani nyepesi ya kumpwekesha Mwenyezi Mungu”.**<sup>2</sup>

Hadithi nyingine *Sahih* inasema;

<sup>1</sup> Ahmad 1:202 na 5:291.

<sup>2</sup> Ahmad 5:266. Hadithi hii ni Dhaifu.

«إِنَّ هَذَا الدِّينَ يُسْرٌ»

“*Hakika! Dini hii ni nyepesi*”.

Na sharia zake zote ni sahali zenye upole zilizo kamili kabisa. Ni rahisi kwa mwenye kurahisishiwa na Allah تعالیٰ<sup>1</sup>.

حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ

“*...anakuhangaikieni sana*”.

Ili muweze kupata Hidaya na mpate manufaa ya kidunia na ya Akhera. Imamu Ahmad alinukuu kutokana na Hadith ya ‘Abdullah bin Mas’ud رضى الله عنه kuwa alisema: Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ لَمْ يُحَرِّمْ حُرْمَةً إِلَّا وَقَدْ عَلِمَ أَنَّهُ سَيَطْلُعُهَا مِنْكُمْ مُطْلَعًا، أَلَا وَإِنِّي آخِذٌ بِحُجْرِكُمْ أَنْ تَهَافُتُوا فِي النَّارِ كَتَهَافَتِ الْفَرَاسِ أَوْ الدُّبَابِ»

“*Hakika Allah Hakuliharamisha jambo, bali Anajua kabisa kwamba atalichungulia miongoni mwenu mwenye kulichungulia (baadhi yenu mtazivunja). Nami nitakushikeni vifuani mwenu ili msiangukie Motoni kama vipepeo na nzi*”<sup>2</sup>.

Kauli ya Allah تعالیٰ;

بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ

“*Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma*”. (9:128)

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ;

وَإِخْفِضْ جَنَاحَكَ لِمَنِ اتَّبَعَكَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٢٦﴾ فَإِنْ عَصَوْكَ فَقُلْ إِنَّي بِرَبِّي مِمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾ وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٢٨﴾

“*Na watwae kwa upole wanaokufuata miongoni mwa Waumini. Na ikiwa watakuasi basi sema: Mimi najitenga mbali na hayo mnayoyatenda. Na umtegemee Mtukufu Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu*”. (26:215-217)

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 1:116.

<sup>2</sup> Ahmad 1:390.

Hivi ndivyo Allah تعالى Alivyomuamuru Mtume ﷺ katika Aya hii tukufu. Alisema;

فَإِنْ تَوَلَّوْا

**“Basi wakigeuka”.**

Kwa maana: Wakaipa mgongo Sharia hii tukufu, safi, kamilifu na iliyofafanua kila jambo niliyowaletea.

فَقُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

**“...wewe sema: Mwenyezi Mungu Ananitosheleza. Hapana mola isipokuwa Yeye tu”.**

Maana yake: Allah تعالى Peke Yake Ananitosha, hapana Mola Mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye, ninamtegemea Yeye tu.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

رَبُّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا ﴿٩﴾

**“Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi, hapana mola isipokuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako”.** (73:9)

Allah تعالى Amesema;

وَهُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ

**“Na yeye ni Mola Mlezi wa Kiti Kikuu cha Enzi”.**

Inamaanisha kuwa Yeye Allah تعالى Ndiye Mmiliki na Muumba wa kila kitu, kwa sababu Yeye Ndiye Mola wa Arshi Tukufu ambayo iko juu ya viumbe wote wa mbinguni na wa ardhini na vilivyomo humo na vilivyo juu ya hivyo.

Vyote viko chini ya Arshi, vikiwa vimetiishwa kwa Qudura ya Allah تعالى, na Ilimu Yake imekizunguka kila kitu na Hukumu Yake ni yenye kukipitia kila kitu, na Yeye ni Mtegemewa wa kila kitu.

Imamu Ahmad alimnukuu Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما ambaye alisema kuwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه alisema: “Aya ya mwisho katika Qur’an kushushwa ni hii ifuatayo;

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ

*“Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe”<sup>1</sup>.*

Mpaka mwisho wa Surah. Ndani ya *Sahih* kuna masimulizi kwamba Zayd alisema: “Niliikuta Aya ya mwisho katika Surat *Al-Bara-ah* kwa Khuzaymah bin Thabit au Abu Khuzaymah”. Tulikwishatanguliza maelezo kwamba kikundi cha Masahaba walilitaja neno hilo mbele ya Mtume ﷺ, kama alivyosema Khuzaymah bin Thabit wakati alipowaanzishia jambo hilo. *Allah Aalam*<sup>2</sup>.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ahmad 5:117.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Bari 8:195.



## Tafsiri ya Suratu Yunus

### Sura ya 10

#### Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu

سُوْرَةُ يُوْنُسَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الرَّ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ ﴿١﴾ أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا  
 أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ الَّذِينَ  
 ءَامَنُوا أَنَّ لَهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ قَالَ الْكٰفِرُونَ إِنَّ  
 هَذَا لَسِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٢﴾ إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ  
 السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوٰى عَلَى الْعَرْشِ  
 يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ۗ مَا مِنْ شَفِيعٍ إِلَّا مِنْ بَعْدِ إِذْ يَبْعَثُ إِلَٰهَ  
 رَبِّكُمْ فَاَعْبُدُوهُ ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٣﴾ إِلَٰهِيهِ مَرْجِعُكُمْ  
 جَمِيعًا ۗ وَعَدَّ اللَّهُ حَقًّا إِنَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ لِيَجْزِيَ  
 الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّٰلِحٰتِ بِالْقِسْطِ ۗ وَالَّذِينَ كَفَرُوا  
 لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٤﴾  
 هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا  
 وَقَدَرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ اللَّيْلِ وَالنَّجْمِ ۗ مَا  
 خَلَقَ اللَّهُ ذَلِكَ إِلَّا بِالْحَقِّ ۗ يُفَصِّلُ الْآيٰتِ لِقَوْمٍ  
 يَعْلَمُونَ ﴿٥﴾ إِنَّ فِي آخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا خَلَقَ  
 اللَّهُ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ لَآيٰتٍ لِّقَوْمٍ يَتَّقُونَ ﴿٦﴾

الرَّ تِلْكَ ءَايَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ ﴿١﴾  
 أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ  
 الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنَّ لَهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ قَالَ الْكٰفِرُونَ إِنَّ  
 هَذَا لَسِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿٢﴾

1. "Alif Lam Ra. Hizo ni aya za Kitabu chenye Hikima".

2. "Je! Imekuwa ajabu kwa watu kwamba Tumem funulia mmoja wao kuwa: Waonye watu, na wabashirie wale walio amini ya kuwa watakuwa na cheo cha juu kwa Mola wao Mlezi? Wakasema makafiri: Hakika huyu ni mchawi dhahiri!"

Maelezo juu ya herufi moja moja mwanzoni mwa Surah, yamekwisha tangulia katika Surat Al-Baqarah.

تِلْكَ آيَاتُ الْكِتَابِ الْحَكِيمِ

**“Hizo ni aya za Kitabu chenye Hikima”.** Maana yake: Hizi ni Aya za Qur’an zenye hikima pamoja na kubainisha.

**Mtume ﷺ ni Mwanadamu.**

Kauli ya Allah تعالى:

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا

**“Je! Imekuwa ajabu kwa watu”.**<sup>1</sup>

Allah تعالى Anawaambia makafiri wanaostaajabu kwamba Mitume ni miongoni mwa wanadamu. Kama Allah تعالى Alivyojulisha kuhusu kaumu za karne zilizopita, kutokana na kauli yao:

أَبَشَرٌ مِّثْلُ وَنَا

**“Hivyo binadamu ndio atuongoe?” (64:6)**

Hud عليه السلام na Saleh<sup>2</sup> عليه السلام waliwaambia kaumu zao,

أَوْعَجِبْتُمْ أَنْ جَاءَكُمْ ذِكْرٌ مِنْ رَبِّكُمْ عَلَى رَجُلٍ مِّنْكُمْ

**“Je, mnastaajabu kukujieni mawaidha yanayotoka kwa Mola Mlezi wenu kwa njia ya mtu aliye ni mmoja katika nyinyi”.** (7:63)

Allah تعالى Alizungumzia juu ya makafiri wa kikuraishi, pindi waliposema:

أَجْعَلِ آلَآهَةً إِلَهًا وَحِدًا إِنَّ هَذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ ﴿٣٨﴾

**“Amewafanya miungu wote kuwa ni Mungu Mmoja tu? Hakika hili ni jambo la ajabu”.** (38:5)

Adh-Dhahhak alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Allah تعالى Alipomtuma Muhammad ﷺ kuwa Mtume, Waarabu walilikataa hilo. Wakasema, Allah تعالى ni Mtukufu zaidi kuliko kuwa na Mtume wa kibinadamu kama Muhammad ﷺ. Allah تعالى Akateremsha:

<sup>1</sup> Zingatia: Katika Aya 7:63 kauli hiyo ilitamkwa na Nuh (sio Saleh, kama Ibn Kathir alivyotaja kimakosa), na Hud aliwaambia watu wake maneno sawa na hayo, katika Aya 7:69).

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا

**“Je imekuwa ajabu kwa watu”.<sup>1</sup>**

Kauli ya Allah تعالى: أَنَّهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ

**“...ya kuwa watakuwa na cheo cha juu kwa Mola wao Mlezi?”**

Maulamaa wametofautiana kwa kuleta rai mbali mbali katika hili. ‘Ali bin Abu Twalhah alisema, kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliizungumzia Kauli ya Allah تعالى:

وَبَشِّرِ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنَّ لَهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ

**“...na wabashirie wale walioamini ya kuwa watakuwa na cheo cha juu”.**

Kwa maana: “Wameandikiwa furaha ya milele”<sup>2</sup>. Al-‘Awfi alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “...kuwa watakuwa na cheo cha juu”. “Ni malipo mema kwa waliyoyatanguliza”. Mujahid alisema, “...kuwa watakuwa na cheo cha juu” ni, “Amali njema kama vile Sala, Saumu, Sadaka na Tasbihi zao.” Na amesema: kwamba, “Muhammad ﷺ atawashufaia wao”<sup>3</sup>. Kauli ya Allah تعالى:

قَالَ الْكَافِرُونَ إِنَّا هَذَا لَسِحْرٌ مُّبِينٌ

**“Wakasema makafiri: Hakika huyu ni mchawi dhahiri!”**

Maana yake: Makafiri wanasema haya pamoja na kwamba Allah تعالى Aliwapelekea Mtume ﷺ kutokana nao, mtu wa jinsi yao akiwa Mbashiri na Muonyaji. Lakini wao wanakadhibisha katika hilo.

إِنَّ رَبَّكُمْ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُدَبِّرُ الْأُمْرَ ۗ مَا مِنْ شَيْعٍ إِلَّا مِنْ بَعْدِ إِذْنِهِ ۗ ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ ۗ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٣١﴾

**3. “Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenyezi Mungu Ambaye Ameziumba mbingu na ardhi kwa siku sita na kisha Akakaa juu ya Kiti cha Enzi, Anaendesha mambo yote. Hapana muombezi ila baada ya Idhini Yake. Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi Basi muabuduni Yeye. Je! Hamkumbuki?”**

<sup>1</sup> At-Tabari 15:13. Sanadi yake ni dhaifu.

<sup>2</sup> At-Tabari 15:15.

<sup>3</sup> At-Tabari 15:14. Sanadi yake ni dhaifu.



**Allah تعالى Ndiye Muumbaji Ulimwengu, ni Mola Wake Mlezi na Mpangaji wa Mambo Yote.**

Allah تعالى Anaeleza kwamba Yeye Ndiye Mola Mlezi wa Ulimwengu wote na kwamba Aliziumba Mbingu na Ardhi katika siku sita. Ilisemwa: “Kama siku hizi za kawaida”. Pia ilisemwa: “Ni sawa na miaka elfu kwa jinsi mnavyohesabu”. Kama itakavyobainishwa baadaye.

ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ ط

**“...kisha Akakaa juu ya Kiti cha Enzi (al-'Arsh)”.**

Al-'Arsh na sakafu yake ndicho kiumbe kikubwa zaidi. Kauli ya Allah تعالى،

يُدَبِّرُ الْأَمْرَ ط

**“Anaendesha mambo yote”.** Maana yake: Anayadabiri mambo ya viumbe.

لَا يَعْزُبُ عَنْهُ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ ط

**“Hapana kinachofichikana Kwake hata chenye uzito wa chembe tu, si katika mbingu wala ardhi”. (34:3)**

Na hapana jambo la Kumshughulisha na Kumfanya Aghafilike na jingine, wala masuala hayamfanyi Akosee, wala kudumu kwa muombaji hakumsumbui, wala halifanyii mchezo jambo dogo wala kubwa, likiwepo milimani, baharini, kwenye makazi au katika ardhi isiyotumika.

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا ط

**“Na hakuna kiumbe yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu”. (11:6)**

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي

كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾

**“Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinachobainisha”. (6:59)**

Ad-Darawardi alisema kuwa Sa'd bin Is-haq bin Ka'b bin 'Ujrah alisema baada ya kushuka Aya hii:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ

**“Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenyezi Mungu Ambaye Ameziumba mbingu na ardhi”.**

Kwamba walikutana na msafara mkubwa ambao waliudhania kwamba ni wa Waarabu. Wakawaambia: “Nyinyi ni akina nani?” Wakasema: “Sisi ni miongoni mwa majini. Tumetoka Madinah. Kilichotutoa ni Aya hii”. Aliyasimulia hayo Ibn Abu Hatim. Kauli ya Allah تعالى:

مِن شَفِيعٍ إِلَّا مِنْ بَعْدِ إِذْنِهِ

**“Hapana muombezi ila baada ya Idhini Yake”.** Sawa na Kauli ya Allah تعالى,

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ

**“Ni nani huyo Awezaye kuomba mbele Yake bila ya Idhini Yake?”**

(2:255) Na Kauli Yake Allah تعالى,

\* وَكَمْ مِنْ مَلَكٍ فِي السَّمَوَاتِ لَا تُغْنِي شَفَعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ بَعْدِ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ

وَيَرْضَى

**“Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipo kuwa baada ya Mwenyezi Mungu Kutoa Idhini kwa Amtakaye na Kumridhia”.** (53:26) Na Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ

**“Wala uombezi mbele Yake hautawapa faida, isipokuwa kwa Aliye mpa Idhini”.** (34:23)

Kauli ya Allah تعالى:

ذَٰلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ

**“Huyo Ndiye Mwenyezi Mungu, Mola wenu Mlezi. Basi muabuduni Yeye. Je! Hamkumbuki?”**

Maana yake: Wampwekeshe katika ibada, Yeye Peke Yake, wala hana mshirika.

أَفَلَا تَذَكَّرُونَ

**“Je! Hamkumbuki?”** Maana yake: “Enyi mshirikishao katika ibada ilhali mnajua

fika kwamba Yeye Peke Yake Ndiye Muumbaji". Ni sawa na Kauli Yake;

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَن خَلَقَهُمْ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

**“Na ukiwauliza ni nani aliye waumba? Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu”. (43:87)**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٤٧﴾ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٤٨﴾

**“Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa A'rshi Kuu? Watasema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Sema: Basi je, hamuogopi?” (23:86-87)**

Kadhalika, Aya kabla yake na baada yake.

إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا وَعَدَّ اللَّهُ حَقًّا إِنَّهُ يَبْدُوهُمُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُمْ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ بِالْقِسْطِ ﴿٤٩﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٥٠﴾

**4. “Kwake Yeye tu ndio marejeo yenu nyote. Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo ya kweli. Hakika Yeye Ndiye Aliyeanzisha Uumbaji, na kisha Ataurejesha ili Awape kwa Uadilifu wale walioamini na wakatenda mema. Na waliokufuru, wao watapata vinywaji vinavyochemka, na adhabu chungu kwa sababu ya walivyokuwa wakikufuru”.**

**Kila Kitu Kitarejea kwa Allah تعالى.**

Allah تعالى Anaeleza kwamba marejeo ya viumbe wote katika Siku ya Kiyama ni Kwake, Hatamuacha yeyote bali atarudi kama alivyoanza. Kisha, Allah تعالى Alitaja kwamba, kama Alivyoanzisha Kuumba, kadhalika Atavirudisha viumbe.

وَهُوَ الَّذِي يَبْدُوهُمُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُمْ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

**“Na Yeye Ndiye Anayanzisha uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyingine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake”. (30:27)**

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ بِالْقِسْطِ ۚ

**“..ili Awape kwa uadilifu wale walioamini na wakatenda mema”.**

Maana yake: Kwa uadilifu na jaza kamilifu.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِّنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ۚ

**“Na waliokufuru, wao watapata vinywaji vinavyochemka, na adhabu chungu kwa sababu ya walivyokuwa wakikufuru”.**

Kwa sababu ya kufuru yao, wataadhibiwa Siku ya Kiyama kwa namna nyingi za adhabu, kama vile upepo mkali wa moto, maji ya moto na kivuli cha moshi mweusi.

هَذَا فَلْيَذُقُوهُ حَمِيمٌ وَعَسَاقٌ ۖ وَءَاخِرُ مِنْ شَكْلِهِمْ أَزْوَاجٌ ۖ

**“Ndio hivi! Basi wayaonaje maji ya moto na ya usaha! Na adhabu nyenginezo za namna hii”. (38:57-58)**

هَذِهِ جَهَنَّمُ الَّتِي يُكَذِّبُ بِهَا الْمُجْرِمُونَ ۖ يَطُوفُونَ فِيهَا بَيْنَ أُبُيَّاتٍ حَمِيمٍ ؕ إِنَّ فِي

**“Hii ndiyo Jahannamu ambayo wakosefu walikanusha. Watakauwa wakiizunguka baina ya hiyo na maji ya moto yanayochemka”. (55:43-44)**

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسُ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَّرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ ۚ مَا خَلَقَ اللَّهُ ذَلِكَ إِلَّا بِالْحَقِّ ۚ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ۖ إِنَّ فِي

أَخْتَلَفِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا خَلَقَ اللَّهُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَتَّقُونَ ۖ

**5. “Yeye Ndiye Aliyelijaalia jua kuwa na mwangaza, na mwezi kuwa nuru, na Akaupimia vituo ili mjue idadi ya miaka na hesabu. Mwenyezi Mungu Hakuviumba hivyo ila kwa Haki. Anazipambanua Ishara kwa watu wanaojua”.**

**6. “Hakika katika kukhitilafiana usiku na mchana, na hakika Alivyumba Mwenyezi Mungu katika mbingu na ardhi, zipo Ishara kwa watu wanao mcha-Mungu”.**

### Kila Kitu ni Shahidi wa Qudura ya Allah تعالى.

Allah تعالى Anaeleza ishara Alizoziumba zinazojulisha ukamilifu wa Kudura Yake na Mamlaka makubwa. Na Amejaalia miale inayotoka katika jua kuwa mwangaza. Na angalia mionzi itokayo katika mwezi kuwa ni nuru. Kila kimoja kinafanya kazi kwa namna yake. Akavitofautisha ili visilete utata. Akajaalia mamlaka ya jua kuwa mchana na ya mwezi kuwa usiku. Akauwekea mwezi vituo. Kwanza huanza ukiwa mdogo, kisha nuru na gimba lake unaongezeka mpaka unakamilisha duara yake. Kisha, unapungua mpaka unarejea hali yake ya awali katika kutimia mwezi. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى;

وَالْقَمَرَ قَدَرْتَهُ مَنَازِلَ حَتَّىٰ عَادَ كَالْعُرْجُونِ الْقَدِيمِ ﴿٣٦﴾ لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِيٰ هَآءَ أَنْ  
تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ ۗ وَكُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٣٧﴾

**“Na mwezi Tumeupimia vituo, mpaka unakuwa kama karara kongwe. Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao.” (36:39-40)**

Na Kauli Yake تعالى,

وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا

**“...na jua na mwezi kwenda kwa hisabu”. (6:96)**

Kauli ya Allah تعالى katika Aya hii takatifu,

وَقَدَرَهُ

**“...na Akaupimia.”** Maana yake: Mwezi.

مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ

**“...vituo ili mjue idadi ya miaka na hesabu.”**

Kwa kutumia jua, masiku hujulikana na kwa mwendo wa mwezi, hujulikana miezi na miaka.

مَا خَلَقَ اللَّهُ ذَٰلِكَ إِلَّا بِالْحَقِّ

**“Mwenyezi Mungu Hakuviumba hivyo ila kwa Haki.”**

Maana yake: Hakuviumba kwa upuuzi, bali Ana Hekima kubwa katika hilo na hoja yenye kufika (yenye kukata). Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بِنِبْلَةٍ ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۖ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا

مِنَ النَّارِ ﴿٧﴾

**“Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya waliokufuru. Ole wao waliokufuru kwa Moto utaowapata.” (38:27)**

Aidha Allah تعالى Amesema,

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ ﴿١١٥﴾ فَتَعَلَىٰ اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ ﴿١١٦﴾

**“Je! Mlidhani ya kwamba Tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi Kwetu hamtarudishwa? Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mola ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi Tukufu.” (23:115-116)**

Kauli ya Allah تعالى:

يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

**“Anazipambanua Ishara kwa watu wanao jua.”**

Kwa maana: Tunazibainisha hoja na dalili, kwa watu wanaojua. Na Kauli Yake Allah تعالى,

إِنَّ فِي آخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ

**“Hakika katika kukhitilafiana usiku na mchana”.**

Maana yake: Alivifuatisha, kikiondoka hiki basi kingine kinaingia au kinapoingia hiki kingine kinatoka. Hakuna kitu kinachotaakhari. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

يُعْثِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا

**“Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi.” (7:54)**

Na Amesema,

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي لَهَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ

**“Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kupitia mchana.” (36:40)**

Na Allah تعالى Amesema,

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا

**“Ndiye Anayepambazua mwangaza wa asubuhi na Ameufanya usiku kwa mapumziko na utulivu.” (6:96)**

Kauli ya Allah تعالى:

وَمَا خَلَقَ اللَّهُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

**“...na katika Alivyounda Mwenyezi Mungu katika mbingu na ardhi.”**

Ni miongoni mwa Aya zinazojulisha juu ya Utukufu wa Allah تعالى. Ni sawa na Kauli Yake nyingine;

وَكَايْنٍ مِّنْ آيَاتِهِ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

**“Ni ishara ngapi katika mbingu na ardhi.” (12:105)**

Na Kauli Yake Allah تعالى,

فَلْيَنْظُرُوا مَاذَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَنْ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠١﴾

**“Sema: Angalieni yaliyomo mbinguni na kwenye ardhi! Na ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini”. (10:101)**

Na Amesema,

أَفَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

**“Kwani hawaoni yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao ya mbingu na ardhi.” (34:9)**

Na Amesema tena,

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٩٠﴾

**“Hakika katika Kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko ishara kwa wenye akili.” (3:190) Maana: Utambuzi.**

Allah تعالى Alisema hapa;

لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ

**“...zipo Ishara kwa watu wanaomcha Mungu”.** Kwa maana: wanaogopa mateso ya Allah تعالى, Ghadhabu Zake na Adhabu Yake.

إِنَّ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا  
 وَرَضُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا  
 وَأَطْمَأَنُّوا بِهَا وَالَّذِينَ هُمْ  
 عَنْ آيَاتِنَا غَافِلُونَ ﴿٧﴾  
 أُولَئِكَ مَا لَهُمْ النَّارُ بِمَا  
 كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨﴾ إِنَّ  
 الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا  
 الصَّالِحَاتِ يَدْبِرُهُمْ رَبُّهُمْ  
 بَرِيْمِينَ ﴿٩﴾ تَجْرِي مِنْ  
 تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ فِي جَنَّاتِ  
 النَّعِيمِ ﴿١٠﴾ دَعَوْهُمْ فِيهَا  
 سُبْحٰنَكَ اللَّهُمَّ وَنَحْمِيْكُمْ  
 فِيهَا سَلَمٌ ۗ وَآخِرُ دَعْوَتِهِمْ  
 أَنْ اَلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١١﴾ \* وَلَوْ  
 يُعَجِّلُ اللَّهُ لِلنَّاسِ  
 الشَّرَّ اسْتَعْجَلَهُمْ بِالْآخِرِ لَفُضِي  
 إِلَيْهِمْ أَجَلُهُمْ ۗ فَنَذَرَ  
 الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا فِي  
 طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١٢﴾ وَإِذَا  
 مَسَّ الْإِنْسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا  
 لِجَنبِهِ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَائِمًا  
 فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهُ مَرَّ  
 كَأَن لَّمْ يَدْعُنَا إِلَىٰ ضُرِّ  
 مَسَّهُ ۗ كَذٰلِكَ زَيْنٌ لِّلْمُسْرِفِينَ  
 مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣﴾ وَلَقَدْ  
 أَهْلَكْنَا الْقُرُونََ مِنْ قَبْلِكُمْ  
 لَمَّا ظَلَمُوا ۗ وَجَاءَهُمْ رُسُلُهُمْ  
 بِالْبَيِّنَاتِ وَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا ۗ  
 كَذٰلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٤﴾ ثُمَّ  
 جَعَلْنَاكُمْ خَلَائِفَ فِي الْأَرْضِ  
 مِنْ بَعْدِهِمْ لِنَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

إِنَّ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ لِقَاءَنَا  
 وَرَضُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَأَطْمَأَنُّوا بِهَا  
 وَالَّذِينَ هُمْ عَنْ آيَاتِنَا غَافِلُونَ  
 ﴿٧﴾ أُولَئِكَ مَا لَهُمْ النَّارُ بِمَا  
 كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٨﴾

**7. "Hakika wasiotaraji kukutana Nasi, na wakaridhia maisha ya dunia na wakatua nayo, na walio-ghafilika na ishara Zetu".**

**8. Hao makazi yao ni Motoni kwa sababu ya waliyokuwa wakiyachuma".**

**Makazi ya Wanaoikanusha Siku ya Kiyama ni Motoni.**

Allah تعالی Anaeleza juu ya hali za waovu (watu wenye mwisho mbaya) ambao walikufuru kukutana na Allah تعالی katika Siku ya Kiyama, wala hawakutarajia chochote katika kukutana Naye, waka-

yaridhia maisha haya ya duniani na nafsi zao zikatulia kwenye hii dunia. Al-Hasan alisema: "Wallahi! Dunia Waliipamba na kuinyanyua mpaka wakaridhika humo, ilhali wakiwa wameghafilika na ishara za Allah تعالی ulimwenguni, hawazitafakari, wala hawakuifuata Sharia. Makazi yao katika siku ya marejeo ni Motoni, kama jaza ya yale waliyokuwa wakiyachuma duniani. Nayo ni



madhambi, makosa na uhalifu, pamoja na kufuru waliyonayo kwa Allah تعالى Mtume ﷺ na Siku ya Mwisho”.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ يَدْرِهَمَ رُبُّهُمْ بِإِيمَانِهِمْ ۖ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهِمُ  
الْأَنْهَارُ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٩﴾ دَعَوْنَهُمْ فِيهَا سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَتَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ۖ وَءَاخِرُ  
دَعْوَانَهُمْ أَنِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾

**9. “Hakika walioamini na wakatenda mema, Mola wao Mlezi Atawaongoa kwa sababu ya Imani yao. Itakuwa inapita mito kati yao katika bustani yenye neema”.**

**10. “Wito wao humo utakuwa: Subhanaka LLahumma “Umetakasika Ee Mwenyezi Mungu”. Na maamkio yao humo ni “Salama”. Na mwisho wa wito wao ni: Alhamdulillah Rabbi A’lamiin, “Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa ulimwengu wote”.**

### Malipo Mema ni kwa Watu wa Imani na Amali Njema.

Hizi ni habari kuhusu hali za watu wema waliomuamini Allah تعالى na kuwasadiki Mitume, wakayafuata waliyoamrisha na wakatenda mema, kwamba Yeye Atawaongoa kwa Imani yao. Hapa inawezekana kukawa kuna Tafsiri mbili Tafsiri ya kwanza kwa sababu ya Imani yao duniani, Allah تعالى Atawaongoa katika Siku ya Kiyama juu ya njia iliyonyooka, mpaka waipite na kuingia peponi. Tafsiri nyingine, kwa msaada wa Imani yao. Kama alivyosema Mujahid katika Kauli ya Allah تعالى:

يَدْرِهَمَ رُبُّهُمْ بِإِيمَانِهِمْ ۖ

**“Mola wao Mlezi Atawaongoa kwa sababu ya Imani yao”.**

Kwamba, “Imani yao itakuwa nuru watakayotembea kwayo.”<sup>1</sup>

Kauli ya Allah تعالى:

دَعَوْنَهُمْ فِيهَا سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَتَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَامٌ ۖ وَءَاخِرُ دَعْوَانَهُمْ أَنِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ  
الْعَالَمِينَ ﴿١٠﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 15:28.

**“Wito wao humo utakuwa: Subhanaka Llahumma “Umetakasika Ee Mwenyezi Mungu”. Na maamkio yao humo ni “Salama”. Na mwisho wa wito wao ni: Alhamdulillah Rabbi A’lamiin, “Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa ulimwengu wote.”**

Kwa maana: Hii ndiyo hali ya watu wa peponi. Ayah hii inashabihiana na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

فَجِيئْتُهُمْ يَوْمَ يَلْقَوْنَهُ سَلَامًا

**“Maamkiano yao siku ya kukutana Naye yatakuwa: Salama!” (33:44)**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْتِيْمًا ﴿٢٥﴾ إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿٢٦﴾

**“Humo hawatasikia porojo wala maneno ya dhambi, isipokuwa maneno ya Salama, Salama.” (56:25-26)**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

سَلَامٌ قَوْلًا مِّن رَّبِّ رَحِيمٍ ﴿٥٨﴾

**“Salama!” Hiyo ndiyo Kauli itokayo kwa Mola Mlezi Mwenye Kurehemu.” (36:58)**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَأَلْمَلَيْكَةُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِم مِّن كُلِّ بَابٍ ﴿٢٣﴾ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ

**“Na malaika wanawaingilia katika kila mlango. (Wakiwaambia) Asalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu”. (13:23-24)**

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَجْرُ دَعْوَتِهِمْ أَنِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**“Na mwisho wa wito wao ni: Alhamdulillah Rabbi A’lamiin, “Kuhimidiwa kote ni kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa ulimwengu wote.”**

Katika Aya hii kuna dalili kuwa Yeye Ndiye Msifiwa wa milele, wa kuabudiwa kipindi chote. Ndiyo maana, Alianza kujisifu Mwenyewe wakati wa Kuumba Kwake na kuendelea, na katika Kukianza Kitabu Chake na wakati wa Kuanza kukiteremsha. Ni pale Allah تعالى Aliposema:

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيَّ عَبْدِهِ الْكِتَابَ

**“Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu, Ambaye Amemteremshia mja wake Kitabu.” (18:1)**

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ

**“Sifa Njema zote ni za Mwenyezi Mungu Aliyeumba mbingu na ardhi.” (6:1)**

Na zingine ambazo ni ndefu sana kuzieleza. Pia, Yeye ni Msifiwa mwanzoni na mwishoni, duniani na Akhera na katika hali zote. Ndipo ilipokuja katika Hadithi;

«إِنَّ أَهْلَ الْجَنَّةِ يُلْهَمُونَ التَّسْبِيحَ وَالتَّحْمِيدَ كَمَا يُلْهَمُونَ التَّنَسُّهَ»

**“Watu wa Jannah watafanyiwa ilhamu ya Kumtukuzia Allah na Kumsifu kama wanavyofanyiwa ilhamu ya kuvuta pumzi”.<sup>1</sup>**

Kwa hakika, hali itakuwa hivyo, kwa sababu ya kuongezeka kwa neema za Allah تعالى juu yao. Zinajikariri, zinarudi tena, na kuongezeka, hazimaliziki wala hazina ukomo. Basi, hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye, wala hapana mola Mlezi ila Yeye.

﴿ وَلَوْ يُعَجِّلُ اللَّهُ لِلنَّاسِ الشَّرَّ اسْتَعْجَالَهُمْ بِالْخَيْرِ لَقُضِيَ إِلَيْهِمْ أَجْلُهُمْ فَبَدَّرَ الَّذِينَ لَا

يَرْجُونَ لِقَاءَنَا فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١﴾

**11. “Na lau kama Mwenyezi Mungu Angeliwafanyia watu haraka Kuwaletea shari kama wanavyojihimiza kuletewa kheri, bila ya shaka wangelishatimiziwa ajali yao. Lakini Tunawaacha wale wasiotumainiwa kukutana Nasi wakihangaika katika upotovu wao”.**

<sup>1</sup> Muslim 4:2181.

**Allah تعالی Hazijibu Dua za Shari Kama Anavyozijibu za Kheri.**

Allah تعالی Anaeleza kuhusu ustahamilivu na ulatifu kwa waja Wake kwamba Yeye Hawajibu dua zao dhidi ya nafsi zao, mali zao au watoto wao wanapoomba shari katika hali zao za udhia na ghadhabu. Pia, Anajua ukosefu wao wa kukusudia shari katika kutaka kwao hivyo, kwa ajili hiyo, hawajibu. Hali hii inatokana na ulatifu na rehema. Ni kama Anavyowajibu wanapojiomba kheri, baraka na nyongeza katika mali na watoto. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

وَلَوْ يُعَجِّلُ اللَّهُ لِلنَّاسِ الشَّرَّ أَتَّعَجَبَ لَهُمْ بِالْخَيْرِ لَقَضَىٰ إِلَيْهِمْ أَجْلَهُمْ ۗ

***“Na lau kama Mwenyezi Mungu Angeliwafanyia watu haraka Kuwaletea shari kama wanavyojihimiza kuletewa kheri, bila ya shaka wangelishatimiziwa ajali yao”.***

Maana: Lau Angeliwajibu kila wanapomuomba hivyo angeliwaangamiza. Hata hivyo haitakikani kukithirisha hayo. Ni kama ilivyokuja katika Hadithi ambayo aliipokea Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bazzar رحمه الله تعالی katika Musnad wake kuwa Jabir رضي الله عنه alisema: Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَدْعُوا عَلَىٰ أَنْفُسِكُمْ، لَا تَدْعُوا عَلَىٰ أَوْلَادِكُمْ، لَا تَدْعُوا عَلَىٰ أَمْوَالِكُمْ، لَا تُؤَافِقُوا مِنْ اللَّهِ سَاعَةً فِيهَا إِجَابَةٌ فَيَسْتَجِيبَ لَكُمْ»

*“Msiombe dhidi ya nafsi zenu. Msiombe dhidi ya watoto wenu. Msiombe dhidi ya mali zenu. Isije dua hiyo ikawafikiana na saa ambayo dua hujibiwa na Allah تعالی Akaijibu”.*

Hadithi hii ilinukuliwa na Abu na Dawud<sup>1</sup>.

Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَيَدْعُ الْإِنْسَانُ بِالشَّرِّ دُعَاءَهُ بِالْخَيْرِ ۗ

***“Na mwanadamu huomba shari kama vile aombavyo kheri”.* (17:11)**

Mujahid alisema, katika tafsiri ya Aya hii;

<sup>1</sup> Abu Dawud 2:185.

وَلَوْ يُعَجِّلُ اللَّهُ لِلنَّاسِ الشَّرَّ اسْتَعَجَّلَهُمْ بِالْخَيْرِ

**“Na lau kama Mwenyezi Mungu Angeliwafanyia watu haraka Kuwaletea shari kama wanavyojihimiza kuletewa kheri, bila ya shaka wangelishatimiziwa ajali yao”.**

Ni mtu anayesema juu ya mwanaye au mali yake huku akiwa ameighadhabikia, “Ewe Allah! Usiibariki na Uilaani”. Lau Angeliwaharakishia Kuwajibu hayo kama Anavyowajibu kwa la kheri, basi Angeliwahiliki.

وَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنبَيْهِ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَائِمًا فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ ضُرَّهُ مَرَّ كَأَنْ لَمْ يَدْعُنَا إِلَىٰ ضُرِّ مَسَّهُ ۗ كَذَٰلِكَ زُيِّنَ لِلْمُسْرِفِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٢﴾

**12. “Na mtu akiguswa na shida hutuomba naye kaegesha ubavu, au kaka, au kasimama. Lakini Tukimuondoshea shida yake huendelea kama kwamba hakupata kutuomba Tumuondoshee shida iliyompata. Ndio namna hiyo wamepambiwa warukao mipaka yale waliyokuwa wakiyatenda”.**

**Mwanadamu Humkumbuka Allah تعالی Wakati wa Shida na Kumsahau Wakati wa Neema.**

Allah تعالی Anaeleza juu ya udhia na mashaka ya mwanadamu anapopatwa na madhara. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

وَإِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ فَذُوْ دُعَاءٍ عَرِيضٍ

**“...na inapomgusa shari, huwa na madua marefu marefu”.** (41:51)

Maana: Nyingi, hayo maneno mawili yana maana moja. Hayo ni kwa sababu, akishapatwa na shida, hupatwa na mashaka, na kukithirisha dua kuhusu hilo. Atamuomba Allah تعالی Aiondoshe kwa khofu. Anamuomba akiwa mja huyo katika hali zake za kulala, kukaa na kusimama kwake, kugeuka na kujitenga kando. Allah تعالی Huiondosha kama kwamba hakukuwa na jambo lolote.

مَرَّ كَأَنْ لَمْ يَدْعُنَا إِلَىٰ ضُرِّ مَسَّهُ ۗ

**“...huendelea kama kwamba hakupata kutuomba Tumuondoshee shida iliyompata”.**

Kisha, Allah تعالى Aliwakosoa wenye sifa na njia hii.

كَذَلِكَ زَيْنَ لِلْمُسْرِفِينَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

**“Ndio namna hiyo wamepambiwa warukao mipaka yale waliyokuwa wakiyatenda”.**

Ama mtu ambaye Allah تعالى Amemruzuku Hidaya, Taufiki na Mwongozo, basi Hamhusishi na hayo.

Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

**“...Ila wale waliosubiri wakatenda mema”. (11:11)**

Ni sawa na kauli ya Mtume ﷺ:

«عَجَبًا [لِأَمْرِ] الْمُؤْمِنِ لَا يَقْضِي اللَّهُ لَهُ قَضَاءَ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ، إِنْ أَصَابَتْهُ ضَرَاءٌ فَصَبَرَ كَانَ خَيْرًا لَهُ، وَإِنْ أَصَابَتْهُ سَرَاءٌ فَشَكَرَ كَانَ خَيْرًا لَهُ، وَلَيْسَ ذَلِكَ لِأَحَدٍ إِلَّا لِلْمُؤْمِنِ»

*“Jambo la Muumini ni la ajabu. Allah Hapatishi jambo bali huwa ni la kheri kwake. Jambo baya likimsibu, na akasubiri, hilo huwa la kheri kwake. Akipatwa na kheri, na akashukuru, nayo huwa kheri kwake. Hayo si kwa yeyote, isipokuwa Muumini tu”<sup>1</sup>.*

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا الْقُرُونََ مِنْ قَبْلِكُمْ لَمَّا ظَلَمُوا وَجَاءَهُمْ رَسُولُهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ وَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا  
كَذَلِكَ نَجْزِي الْقَوْمَ الْمُجْرِمِينَ ﴿١٣﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاكُمْ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ مِنْ بَعْدِهِمْ لِنَنْظُرَ  
كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

**13. “Na kwa yakini Tumekwisha ziangamiza kaumu za kabla yenu walipodhulumu, na waliwajia Mitume wao kwa Ishara zilizo wazi; lakini hawakuwa wenye kuamini. Ndio kama hivyo Tunavyowalipa watu wakosefu”.**

<sup>1</sup> Muslim 4:2295.

**14. “Kisha Tukakufanyeni nyie ndio wenye kushika mahala pa baada yao katika ardhi ili Tuone jinsi mtakavyotenda”.**

**Mazingatio Yanayopatikana Katika Hilaki za Umma Zilizotangulia.**

Allah تعالى Anatufahamisha juu ya kilichowatokea vizazi vilivyotangulia kwa kuwakadhibisha Mitume na yale waliyokuja nayo, miongoni mwa Ufafanuzi na hoja zilizo wazi wazi. Kisha, Allah تعالى Aliwaleta wengine baada yao, na Akawapelekea Mtume ﷺ ili Aangalie utiifu wao na kumfuata kwao Mtume ﷺ. Katika *Sahih* Muslim, katika Hadithi ya Abu Nadhrah kutoka kwa Abu Sa'id رضي الله عنه alisema: Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ الدُّنْيَا حُلْوَةٌ خَضِرَةٌ، وَإِنَّ اللَّهَ مُسْتَخْلِفُكُمْ فِيهَا، فَنَظَرْتُ كَيْفَ تَعْمَلُونَ، فَاتَّقُوا الدُّنْيَا وَاتَّقُوا النَّسَاءَ، فَإِنَّ أَوَّلَ فِتْنَةٍ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَانَتْ فِي النَّسَاءِ»

*“Hakika! Dunia ni tamu na kijani. Na kwa hakika! Allah Atakuwekeni humo na Atayaangalia mnayoyafanya. Na muepuke mtihani unaosababishwa na wanawake. Kwani mtihani wa kwanza kwa Wana wa Israil ulitokana na wanawake”<sup>1</sup>.*

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa 'Abdur-Rahman bin Abu Layla kwamba 'Awf bin Malik alimuambia Abubakr رضي الله عنه, “Nimeota kama waotavyo waliolala. Nimeona kama vile kuna kamba iliyoning'inizwa kutokea mbinguni, ikamnyanyua Mtume ﷺ, kisha ikarudi, ikamnyanyua Abubakr رضي الله عنه. Halafu watu wakapewa vipimo mbalimbali kuzunguka mimbari. 'Umar رضي الله عنه alifadhiliwa kupata dhiraatatu kuzunguka mimbari”. 'Umar رضي الله عنه akasema: “Tuondokee na ndoto zako. Hatuna haja nayo”. 'Umar رضي الله عنه alipokuwa Khalifa wa Waislamu, alisema: “Ewe 'Awf! nisimulie ile ndoto yako”. Akasema: “Kwa sasa unataka kuisikia ndoto yangu? Ama kwa nini ulinikaripia?” Akasema: “Ole wao! Sikupenda uitaje kwa Khalifa wa Mtume ﷺ.” Akamsimulia kisa hicho, mpaka alipofikia kupimiwa watu katika mimbari na zile dhiraatatu. Umar رضي الله عنه alisema: “Ama mojawapo ni kwa kuwa Khalifa. Ya pili, ni kwa kutokukhofia kwake kwa ajili ya Allah تعالى, lawama ya mwenye Kulaumu na ya tatu ni kwa kufa shahidi”. Kisha akasema: “Allah تعالى Anasema;

<sup>1</sup> Muslim 4:2098.

ثُمَّ جَعَلْنَاكُمْ خَلَائِفَ فِي الْأَرْضِ مِنْ بَعْدِهِمْ لِنَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿١٤﴾

***“Kisha Tukakufanyieni nyie ndio wenye kushika mahala pa baada yao katika ardhi ili Tuone jinsi mtakavyo tenda”.***

Basi, ewe mwana wa mama wa ‘Umar رضي الله عنه, umeteuliwa kuwa Khalifa, basi, angalia utakacho kifanya!”. Kuhusu kauli ya kwamba mimi sikhofii kwa ajili ya Allah تعالى lawama za mwenye kulaumu, huo ni utashi wa Allah تعالى. Kuhusu kufa shahidi, ‘Umar رضي الله عنه atafikiaje hilo ilhali Waislamu wanamzunguka?<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 15:39. Isnadi yake ni dhaifu sana.



وَإِذَا تَتَلَوُا عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا يَبْسُتُونَ ۚ قَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ  
 لِقَاءَنَا آتَيْتَ بِقُرْآنٍ غَيْرِ هَذَا أَوْ بَدَّلَهُ ۗ قُلْ مَا يَكُونُ لِي  
 أَنْ أُبَدِّلَهُ مِنْ تِلْقَائِي نَفْسِي ۗ إِنِّي أَخَافُ إِلَّا مَا يُوْحَىٰ إِلَيَّ ۗ  
 إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٥﴾ قُلْ لَوْ  
 شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُ عَلَيْكُمْ وَلَا أَدْرَاكُمْ بِهِ ۗ فَقَدْ لَبِثْتُ  
 فِيكُمْ عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦﴾ فَمَنْ أَظْلَمُ  
 مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ إِنَّهُ  
 لَا يُفْلِحُ الْمُجْرِمُونَ ﴿١٧﴾ وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ  
 مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا  
 عِنْدَ اللَّهِ ۗ قُلْ أَتَعْبُدُونَ اللَّهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمَوَاتِ  
 وَلَا فِي الْأَرْضِ ۗ سُبْحٰنَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٨﴾  
 وَمَا كَانَ النَّاسُ إِلَّا أُمَّةً وَاحِدَةً فَاخْتَلَفُوا ۗ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ  
 سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ فِيمَا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٩﴾  
 وَيَقُولُونَ لَوْلَا أَنْزَلَ عَلَيْهِ آيَةٌ مِّن رَّبِّهِ ۗ فَقُلْ إِنَّمَا  
 الْغَيْبُ لِلَّهِ فَانْتَظِرُوا إِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُنْتَظِرِينَ ﴿٢٠﴾

وَإِذَا تَتَلَوُا عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا يَبْسُتُونَ ۚ قَالَ الَّذِينَ لَا يَرْجُونَ  
 لِقَاءَنَا آتَيْتَ بِقُرْآنٍ غَيْرِ هَذَا أَوْ بَدَّلَهُ ۗ قُلْ مَا  
 يَكُونُ لِي أَنْ أُبَدِّلَهُ مِنْ تِلْقَائِي نَفْسِي ۗ إِنِّي  
 أَخَافُ إِلَّا مَا يُوْحَىٰ إِلَيَّ ۗ إِنِّي أَخَافُ إِنْ  
 عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٥﴾ قُلْ  
 لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُ عَلَيْكُمْ وَلَا أَدْرَاكُمْ  
 بِهِ ۗ فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۗ  
 أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٦﴾

15. "Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi, wale wasiotaraji kukutana na Sisi husema: Lete Qur'an isiyokuwa hii, au ibadilishe. Sema: Hainifalii mimi kuibadilisha kwa nitakavyo nafsi yangu. Mimi sifuati ila ninayofunuliwa kwa Wahyi.

**Hakika mimi naogopa, nikimuasi Mola wangu Mlezi, adhabu ya Siku iliyo kuu".**

16. "Sema: Mwenyezi Mungu Angelitaka nisingelikusomeeni, wala nisingeli kujuyeni. Kwani nilikwishakaa nanyi umri mzima kabla yake! Basi, je! Hamzingatii?"

**Ubainifu wa Ukaidi wa Wakuu wa Makuraishi.**

Allah تعالى Anaeleza juu ya ukaidi wa makafiri wa Kikuraishi waliompinga Yeye na kumkataa. Mtume ﷺ alipokuwa akiwasomea Kitabu cha Allah تعالى na hoja zake za wazi wazi, walisema: “Lete Qur’an isiyokuwa hii”. Yaani, irudishe hii na utuletee nyingine, yenye namna tofauti au uibadilishe katika mtindo mwingine. Allah تعالى Akamuambia Mtume ﷺ,

قُلْ مَا يَكُونُ لِي أَنْ أُبَدِّلَهُ مِنْ تَلْقَائِي نَفْسِي ۗ

**“Sema: Hainifalii mimi kuibadilisha kwa nitakavyo nafsi yangu.”**

Kwa maana: Hii si juu yangu, mimi ni mwenye kuamriwa, ni Mtume mfikishaji kutoka kwa Allah تعالى.

إِنْ أَتَيْتُ إِلَّا مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ ۗ إِنِّي أَخَافُ إِنْ عَصَيْتُ رَبِّي عَذَابٌ يَوْمٍ عَظِيمٍ

**“Mimi sifuati ila ninayofunuliwa kwa Wahyi. Hakika mimi naogopa, nikimuasi Mola wangu Mlezi, adhabu ya Siku iliyo kuu.”**

Kisha Mtume ﷺ akawapa hoja juu ya usahihi wa aliyowaletea wao.

**Uthibitisho wa Ukweli wa Qur’an**

قُلْ لَوْ شَاءَ اللَّهُ مَا تَلَوْتُهُمْ عَلَيْهِمْ وَلَا أَدْرَأَكُمْ بِهِ ۗ

**“Sema: Mwenyezi Mungu Angelitaka nisingelikusomeeni, wala nisingelikujuvyeni.”**

Sema, kwa hakika! Haya nimekuleteeni kwa idhini ya Allah تعالى katika hilo na utashi Wake. Dalili kwamba mimi siyasemi kutokana nami mwenyewe wala kuyazua, ni kule kushindwa kwenu kuikataa. Nyinyi mnajua kuwa mimi ni mkweli na mwaminifu, tangu kukulia kwangu hapa kwenu mpaka sasa anaponituma Allah تعالى. Mtume ﷺ hakuwahi kupingwa au kubezwa kwa jambo lolote. Kwa hiyo, alisema;

فَقَدْ لَبِثْتُ فِيكُمْ عُمُرًا مِّن قَبْلِهِ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ

**“Kwani nilikwishakaa nanyi umri mzima kabla yake! Basi, je! Hamzingatii?”**

Nyinyi inamaanisha hamna akili kubainisha ukweli na uongo? Pindi Heraclius, Mfalme wa Roma alipomuuliza Abu Sufyan na waliokuwa pamoja naye. Miongoni mwa aliyomuuliza ni sifa za Mtume ﷺ. Heraclius alimuuliza Abu Sufyan, "Je! Mlikuwa mkimtumumu kuongopa kabla hajayasema aliyoyasema?" Abu Sufyan alisema: "Nikajibu, 'Hapana'". Kwa wakati huo, Abu Sufyan alikuwa kiongozi wa makafiri na Washirikina. Pamoja na haya aliukubali ukweli. Ushahidi unapotolewa na maadui huwa bora. Heraclius akamuambia: "Nilishangaa baada ya kujua kwamba yeye hakuwa akiwaongopea watu, vipi aanze kuongopa juu ya Allah?"<sup>1</sup> Ja'far bin Abu Talib رضي الله عنه alimuambia An-Najashi, Mfalme wa Ethiopia: "Allah تعالى Ametuletea Mtume ambaye sisi tunaujua ukweli wake na uaminifu. Alikaa pamoja na sisi kwa miaka arubaini kabla ya Utume"<sup>2</sup>.

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ  
 الْمُجْرِمُونَ

**17. "Basi ni nani aliye dhalimu zaidi kuliko yule anayemzulia uongo Mwenyezi Mungu na akazikanusha Ishara Zake? Hakika hawafanikiwi wakosefu".**

Allah تعالى Anasema, hapana dhalimu zaidi, jeuri na mkosefu sana, "...kuliko yule anayemzulia uongo Mwenyezi Mungu". Akasema ya uongo juu ya Allah تعالى na kudai kuwa Alimtuma, ilhali sivyo. Basi hapana aliye na udhalimu au kosa kubwa zaidi ya huyu. Kama ambavyo jambo la mtu kama huyu halifichikani kwa wapumbavu, basi ni kwa vipi hali ya mtu wa namna hii ashabihiane na Manabii? Mwenye kuyasema maneno haya kwa ukweli au uongo, hapana budi kwamba Allah تعالى Atampatia dalili dhahiri kabisa juu ya usahihi au ubatili wake. Kwa hivyo, tofauti baina ya Muhammad ﷺ na Musaylimah Al-Kaddhab (Mwongo) kwa waliowashuhudia, ziko wazi kama vile kutofautiana kwa wakati wa dhuha na usiku wa manane katika kiza kinene. Sifa za kila mmoja kati ya hao wawili, matendo yake na maneno yanajulisha, kwa mwenye uoni mzuri, ukweli wa Muhammad ﷺ na uchuku wa Musaylimah Mwongo, Saajah na Al-

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:82.

<sup>2</sup> Ahmad 1:202.

As'wad Al-'Ansi. 'Abdullah bin Salam alisema: "Mtume ﷺ alipowasili Madina, watu walishikwa na khofu. Mimi pia nilikuwa miongoni mwa hao waliopatwa na faza. Nilipomuona tu, nilitambua kwamba uso wake haukuwa wa mtu mwongo. Basi maneno ya kwanza niliyomsikia, ni pale aliposema kauli hii:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! أَفْتَسُوا السَّلَامَ، وَأَطْعِمُوا الطَّعَامَ، وَصَلُّوا الْأَرْحَامَ، وَصَلُّوا بِاللَّيْلِ  
وَالنَّاسُ نِيَامٌ، تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ بِسَلَامٍ»

*"Enyi watu! Enezeni maamkizi ya amani, walisheni wengine chakula, tekelezeni wajibu wa undugu na msali nyakati za usiku ilhali watu wamelala, mtaingia jannah kwa amani"<sup>1</sup>.*

Ujumbe wa Dhimmam bin Tha'labah ulipokuja kwa Mtume ﷺ akiwa na kaumu yake ya Banu Sa'd bin Bakr, alimuambia Mtume ﷺ juu ya aliyoyasema, 'Ni nani aliyenyanyua mbingu hii?' Mtume ﷺ akamjibu "Ni Allah تعالی" "Ni nani aliyesimamisha milima hii?" Alisema: "Allah تعالی". Akasema: "Ni nani aliyelitandaza dunia hii?" Akasema: "Allah تعالی". Akasema, basi nakuuliza kwa Jina la Aliyenanyua mbingu, Akaisimamisha milima na Akaitandaza ardhi hii, ni Allah تعالی Ndiye Aliyekutuma kwa watu wote?" Mtume ﷺ Akasema;

«اللَّهُمَّ نَعَمْ»

*"Naapa kwa Allah! Ndiyo".*

Halafu akamuuliza juu ya Sala, Zaka, Hijja na Saumu. Kwa kila swali aliapa kwa Jina la Allah تعالی, na Mtume ﷺ pia aliapa hivyo kwa kila jibu alilotoa. Kisha Dhimmam akamuambia: "Umesema kweli. Naapa kwa Jina la Aliyekutuma kwa haki! Sitapunguza wala kuongeza katika haya". Mtu huyu akatosheka na haya, akiwa ameyakinisha ukweli wa Mtume kwa dalili alizoziona na kuzishuhudia<sup>2</sup>. Na ilielezwa kwamba 'Amri bin Al-'As alikwenda kwa Musaylimah ambaye alikuwa rafiki yake katika zama za ujahili, na wakati huo 'Amri alikuwa hajasilimu bado. Musaylimah akamuambia: "Ole wako ewe 'Amri! Ni nini kilichoteremka kwa sahibu yenu, akimaanisha, Mtume ﷺ, katika muda huu?" Akasema: "Niliwasikia Masahaba wake wakisoma Sura fupi lakini kubwa". Akauliza: "Ni ipi?" Akasema;

<sup>1</sup> Ahmad 5:451.

<sup>2</sup> Angalia Zad Al-Ma'ad 3:647 na chanzo chake ni Al-Bukhari na. 63 na Muslim na. 12

وَالْعَصْرِ ﴿١٠٠﴾ إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُفٍ ﴿١٠١﴾

***“Naapa kwa Zama! Hakika wanadamu wote wamo katika khasara”. (103:1-2)***

Mpaka mwisho wake. Musaylimah akafikiri kwa muda kisha akasema: “Hata mimi niliteremshiwa mfano wa hivyo”. Akamuuliza: “Ni ipi hiyo?” Akamjibu, “Ewe Wabr! Ewe Wabr!” (aina ya sungura wanaoishi majabalini) Kwa hakika! Wewe una masikio mawili na kifua. Sehemu zako zilizosalia ni wazi.” Unaanaje wewe ‘Amri?. ‘Amri akamuambia: “Naapa kwa Allah! Unajua kwamba mimi nakujua kuwa wewe unaongopa”<sup>1</sup>.

Ikiwa hii ndio hali ya mtu mshirikina katika ushirikina wake, ambaye hakutatizika na hali ya Muhammad ﷺ na ukweli wake, pia kwa hali ya Musaylimah (Laana ya Allah iwe juu yake) na uongo wake, basi Itakuwaje kwa watu wenye uoni na utambuzi bora? Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ شَيْءٌ وَمَنْ قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ

***“Nani dhalimu mkubwa kuliko yule anayemzulia uongo Mwenyezi Mungu, au anayesema: Mimi nimeletewa wahyi; na hali hakuletewa wahyi wowote. Na yule anayesema: nitateremsha kama Alivyoteremsha Mwenyezi Mungu”. (6:93).***

Na Alisema;

فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِآيَاتِهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْمُجْرِمُونَ ﴿١٠٠﴾

***“Basi ni nani aliye dhalimu zaidi kuliko yule anayemzulia uongo Mwenyezi Mungu na akazikanusha Ishara Zake? Hakika hawafanikiwi wakosefu”. (10:17)***

Kadhalika atakayeupinga ukweli waliokuja nao Wajumbe wa Allah تعالی wakasaidiwa na hoja nyingi. Hapana aliye dhalimu zaidi yake.

<sup>1</sup> Al-Bidayah wan-Ni hayah 6:326.

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنْفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَتُّؤُلَاءِ شُفَعَتُونَا  
عِنْدَ اللَّهِ قُلْ أَتُنَبِّئُونَ اللَّهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ سُبْحٰنَهُ وَتَعَالَى  
عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٥﴾ وَمَا كَانَ النَّاسُ إِلَّا أُمَّةً وَاحِدَةً فَاخْتَلَفُوا وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ  
مِن رَّبِّكَ لَفُضِيَ بَيْنَهُمْ فِيمَا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿١٦﴾

18. "Nao, badala ya Mwenyezi Mungu, wanaabudu wasiowadhuru wala kuwanufaisha, na wanasema: Hawa ndio waombezi wetu kwa Mwenyezi Mungu! Sema" Je! Mnamuambia Mwenyezi Mungu Asiyoyajua ya katika mbingu wala katika ardhi? Subhanahu wa Taa'la Ametakasika na Ametukuka na hao wanaomshirikisha naye."

19. "Wala watu hawakuwa ila Umma mmoja tu. Kisha wakakhitalifiana. Na lau kuwa si neno lililokwisha tangulia kutokana na Mola wako Mlezi, hapana shaka hukumu ingelikwishakatwa baina yao katika hayo wanayokhitalifiana."

### Wanachokiamini Washirikina Juu ya Miungu Yao.

Allah تعالی Anawasuta Washirikina wanaomuabudu Allah تعالی pamoja na ghairi yake, huku wakidhani kwamba shufaa ya miungu hiyo italeta manufaa kwa Allah تعالی. Allah تعالی Akajulisha kwamba hiyo miungu haidhuru wala kunufaisha, wala haimiliki jambo lolote, wala lolote katika wanayoyadai halipo na halitakuwepo abadani. Ndio sababu Allah تعالی Alisema,

قُلْ أَتُنَبِّئُونَ اللَّهَ بِمَا لَا يَعْلَمُ فِي السَّمَوَاتِ وَلَا فِي الْأَرْضِ

**"Sema Je! Mnamuambia Mwenyezi Mungu Asiyoyajua ya katika mbingu wala katika ardhi?"**

Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisema: "Maana yake, "Je mnamuambia Allah تعالی juu ya ambacho hakitakua mbinguni wala ardhini?"<sup>1</sup> Kisha, Allah تعالی Aliiepusha Nafsi Yake Tukufu dhidi ya ushirikina na kufuru zao. Alisema;

<sup>1</sup> At-Tabari 15:46.

سُبْحٰنَهُ وَتَعَالٰى عَمَّا يُشْرِكُوۡنَ

***“Subhanahu wa Taa’la Ametakasika na Ametukuka na hao wanao mshirikisha naye.”***

### **Ushirikina ni Jambo Geni.**

Kisha Allah تعالى Alijulisha kwamba ushirikina ni jambo lililozuka kwa Mwanadamu. Limetokea tu, halikuwepo na kwamba watu walikuwa katika Dini moja tu, ambayo ni Uislamu. Ibn Kathir رحمه الله تعالى alisema: “Kulikuwa na karne kumi baada ya Adam عليه السلام na Nuh عليه السلام. Zote zilikuwa katika Uislamu.”<sup>1</sup> Kisha ikatoka tofauti baina ya watu, wakaabudu masanamu na washindani. Allah تعالى Akapeleka Mitume wakiwa na ishara Zake, hoja zisizopingika na ushahidi wa wazi.

لِيَهْلِكَ مِّنْ هٰلِكَ عَنۢ بَيْنِنَا وَيَحْيٰى مَنۢ حَيٍّ عَنۢ بَيْنِنَا

***“Kwa sababu aangamie wa kuangamia kwa dalili zilizo dhahiri na asalimike wa kusalimika kwa dalili zilizo dhahiri”. (8:42).***

Kauli ya Allah تعالى: وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ

***“...Na lau kuwa si neno lililo kwisha tangulia kutokana na Mola wako Mlezi...” (20:129)***

Maana: Kama Allah تعالى Asingepitisha Uamuzi kwamba Yeye Hatamuadhibu yeyote isipokuwa baada ya kumpa hoja, na kwamba Amewawekea viumbe muda wao makhsusi, Angelikuwa tayari Ameshahukumu baina yao juu ya waliyo khitilafiana, na Kuwafanya Waumini wafurahi na Makafiri wawe katika tabu.

وَيَقُولُوۡنَ لَوْلَاۤ اُنۡزِلَ عَلَیْهِ ءَایَةٌۭ مِّنۡ رَّبِّهِۦ فَقُلۡ اِنَّمَا الۡغَیۡبُ لِلّٰهِ فَانۡتَظِرُوۡۤا اِنِّیۡ مَعَكُمۡ مِّنَ الۡمُنۡتَظِرِیۡنَ ﴿۲۰﴾

***20. “Na wanasema: Kwa nini hakuteremshiwa Ishara kutoka kwa Mola wake Mlezi? Sema: Mambo ya ghaibu ni ya Mwenyezi Mungu. Basi nyinyi ngojeni, na mimi ni pamoja nanyi katika wanao ngojea”.***

<sup>1</sup> Al-Badiyah wan-Nihayah 1:101 na alisema: “Al-Bukhari aliinukuu”.

### Washirikina Wataka Muujiza.

Makafiri hawa wakadhibishaji na wakaidi wanasema: “Kwa nini ishara isiteremshwe kwa Muhammad ﷺ kutoka kwa Mola Wake?” Wakimaanisha kama Allah تعالى Alivyowapatia kaumu ya Thamud, ngamia, ama Awahawilishie kilima cha Swafa kiwe dhahabu, au Awaondoshee milima ya Makkah na mahali pake aweke bustani na mito, au mengine. Allah تعالى Ana uwezo wa hayo, lakini Yeye ni Mwenye Hekima katika Matendo na Kauli Zake. Ni sawa na Alivyosema katika,

تَبَارَكَ الَّذِي إِنْ شَاءَ جَعَلَ لَكَ خَيْرًا مِّنْ ذَلِكَ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَيَجْعَلُ لَكَ فُضُوزًا ﴿١٠﴾ بَلْ كَذَّبُوا بِالسَّاعَةِ وَأَعْتَدْنَا لِمَنْ كَذَّبَ بِالسَّاعَةِ سَعِيرًا ﴿١١﴾

**“Ametukuka Ambaye Akitaka Atakujaalia yaliyo bora kuliko hayo, nayo ni bustani zipitazo mito kati yao, na Atakujaalia majumba ya fakhari. Bali wanaikanusha Saa (ya Kiyama). Na Sisi Tumemuandalia Moto mkali kabisa huyo mwenye kuikanusha Saa” (25:10-11) Na Kauli Yake Allah تعالى:**

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأُولُونَ

**“Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani walikanusha, ...” (17:59)**

Allah تعالى Anasema: “Nilivyo kwa viumbe Wangu, ni kwamba pindi Nikiwapatia walichokiomba, kisha wakaamini ni vyema, la sivyo huwaharakishia adhabu. Pindi Mtume ﷺ alipopewa fursa ya kukhitari baina ya kupatiwa walichokiomba ikiwa wataamini ama vinginevyo waadhibiwe na baina ya kuwacheleweshea adhabu. Alichagua kucheleweshe. Ni kama Mtume ﷺ alivyowafanyia wao upole zaidi ya mara moja. Kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Alimuongoza Mtume ﷺ katika kuyajibu waliyomuuliza. Allah تعالى Alisema;

فَقُلْ إِنَّمَا الْغَيْبُ لِلَّهِ

**“Sema: Mambo ya ghaibu ni ya Mwenyezi Mungu”.**

Kwa maana: Jambo lenyewe lote lipo kwa Allah تعالى, na Yeye Anajua matokeo yote ya mambo.



فَانْتَظِرُوا إِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُنتَظِرِينَ

***“Basi nyinyi ngojeni, na mimi ni pamoja nanyi katika wanao ngojea”.***

Kwa maana: Ikiwa nyinyi hamuamini, mpaka myashuhudie mliyoyaomba, basi ngojeeni hukumu ya Allah تعالى juu yangu na juu yenu. Haya ni baada ya wao kuzishuhudia ishara kubwa kubwa kuliko walizoziomba pindi alipoashiria mbele yao katika mwezi, katika usiku wa mwezi kamili, ukapasuka vipande viwili, kimoja kikawa nyuma ya mlima na kingine mbele yao. Hii ni ishara kubwa zaidi ardhini kuliko walizoziomba na ambazo bado hawajaziomba. Kama wangelikuwa wameyaomba hayo kwa ajili ya kutaka uongofu na ujuzi thabiti, Allah تعالى Angelilijua hilo na Angeliwajibu (maombi yao). Lakini alijua kwamba wao walikuwa wakiomba hayo kwa ujeuri, basi Akawaacha katika mashaka yao. Pia alijua kwamba hapakuwa na yeyote kati yao ambaye aliamini. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٩٦﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ

***“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini. Ijapokuwa itawajia kila Ishara”.*** (10:96-97)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَى وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ قُبُلًا مَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ

***“Na lau kuwa Tungeliwateremshia Malaika na Maiti wakazungumza nao na Tukawakusanyia kila kitu mbele yao, bado wasingeliamini, ila Mwenyezi Mungu Atake.”*** (6:111)

Hii ni pamoja na kiburi walichokuwa nacho. Allah تعالى Alisema katika Aya nyingine;

وَلَوْ فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا مِّنَ السَّمَاءِ

***“Na lau Tungeliwafungulia mlango wa mbingu....”*** (15:14)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَإِنْ يَرَوْا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ سَاقِطًا

**“Na hata wangeona pande linatoka mbinguni linaanguka...” (52:44)**

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ،

وَلَوْ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ كِتَابًا فِي قِرْطَاسٍ فَلَمَسُوهُ بِأَيْدِيهِمْ لَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ هَذَا إِلَّا سِحْرٌ

مُتَّبِعٌ

**“Na hata Tungelikuteremshia kitabu cha karatasi wakakigusa kwa mikono yao, wangelisema waliokufuru: Haya si chochote ila ni uchawi dhahiri”. (6:7)**

Mfano wa watu hawa hawastahiki kujibiwa waliyo yaomba, kwa sababu hakuna faida katika kuwajibu. Hii ni kwa kuwa, wao ni wenye kuzunguka katika ukaidi na ujeuri wao kutokana na kukithiri kwa makosa na ufisadi wao.

Allah تعالیٰ Alisema;

فَأَنْتَظِرُونَا إِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُنْتَظِرِينَ

**“Basi nyinyi ngojeni, na mimi ni pamoja nanyi katika wanao ngojea”.**

\* \* \*

وَإِذَا أَدَقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً مِنْ بَعْدِ  
 صَرَاءَ مَسْئَلِهِمْ إِذَا لَهُمْ مَكْرٌ فِي آيَاتِنَا  
 قُلِ اللَّهُ أَسْرَعُ مَكْرًا ۚ إِنَّ رُسُلَنَا  
 تَمَكَّرُونَ ﴿٢١﴾ هُوَ الَّذِي يُسِيرُكُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ حَتَّى  
 إِذَا كُنْتُمْ فِي الْفُلِكِ وَجَرَيْنَ بِهِم بِرِيحٍ طَيِّبَةٍ وَفَرِحُوا بِهَا  
 جَاءَتْهَا رِيحٌ عَاصِفٌ وَجَاءَهُمُ الْمَوْجُ مِنْ كُلِّ مَكَانٍ وَظَنُوا  
 أَنَّهُمْ أُحِيطَ بِهِمْ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ لَئِنِ أَجَبْنَا  
 مِنْ هُنْدِهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٢٢﴾ فَلَمَّا أَجَبْتَهُمْ  
 إِذَا هُمْ يَبْغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ يَتَأَيَّبُوا النَّاسُ إِنَّمَا  
 بَغْيُكُمْ عَلَى أَنْفُسِكُمْ ۗ مَتَّعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا  
 مَرْجِعُكُمْ فَنُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٣﴾ إِنَّمَا مَثَلُ  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَاءٍ أَنْزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ  
 نَبَاتُ الْأَرْضِ مِمَّا يَأْكُلُ النَّاسُ وَالْأَنْعَامُ حَتَّى إِذَا أَخَذَتِ  
 الْأَرْضُ زُخْرُفَهَا وَازَّيَّنَتْ وَظَنَّ أَهْلُهَا أَنَّهُمْ قَدِرُونَ  
 عَلَيَّهَا أَتْنَاهَا لَيْلًا أَوْ نَهَارًا فَجَعَلْنَاهَا حَصِيدًا كَأَن لَّمْ  
 تَغْنَ بِالْأَمْسِ ۚ كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ  
 ﴿٢٤﴾ وَاللَّهُ يَدْعُوا إِلَى دَارِ السَّلَامِ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى  
 صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٢٥﴾

وَإِذَا أَدَقْنَا النَّاسَ رَحْمَةً مِنْ بَعْدِ  
 صَرَاءَ مَسْئَلِهِمْ إِذَا لَهُمْ مَكْرٌ فِي آيَاتِنَا  
 قُلِ اللَّهُ أَسْرَعُ مَكْرًا ۚ إِنَّ رُسُلَنَا  
 يَكْتُمُونَ مَا تَمَكَّرُونَ ﴿٢١﴾ هُوَ  
 الَّذِي يُسِيرُكُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ حَتَّى  
 إِذَا كُنْتُمْ فِي الْفُلِكِ وَجَرَيْنَ بِهِم  
 بِرِيحٍ طَيِّبَةٍ وَفَرِحُوا بِهَا جَاءَتْهَا رِيحٌ  
 عَاصِفٌ وَجَاءَهُمُ الْمَوْجُ مِنْ كُلِّ  
 مَكَانٍ وَظَنُوا أَنَّهُمْ أُحِيطَ بِهِمْ دَعَوُا  
 اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ لَئِنِ أَجَبْنَا  
 مِنْ هُنْدِهِ لَنَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿٢٢﴾  
 فَلَمَّا أَجَبْتَهُمْ إِذَا هُمْ يَبْغُونَ فِي  
 الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ يَتَأَيَّبُوا النَّاسُ  
 إِنَّمَا بَغْيُكُمْ عَلَى أَنْفُسِكُمْ ۗ مَتَّعَ  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُكُمْ  
 فَنُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٢٣﴾

21. "Na Tunapowaonjesha  
 watu rehema baada ya

shida waliyoipata, utawaona wana vitimbi kuzipangia Ishara Zetu. Sema:  
 Mwenyezi Mungu ni Mwepesi zaidi wa kupanga. Hakika Wajumbe wetu  
 wanayaandika mnayoyapanga".

22. *“Yeye Ndiye Anayekuendesheni bara na baharini. Hata mnapo kuwa majahazini na yanakuwa yanakwenda kwa upepo mzuri wakaufurahia, upepo mkali ukawazukia na yakawajia mawimbi kutoka kila upande na wakaona wameshazongwa, basi hapo humuomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia niya. Ukituokoa na haya bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru”.*

23. *“Lakini Akishawaokoa, mara wanafanya jeuri tena katika nchi bila ya haki. Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe. Hii ni starehe ya maisha ya dunia. Kisha marejeo yenu ni Kwetu, na hapo Tutakuambieni mliyokuwa mkiyatenda”.*

### **Kubadilika kwa Mwanadamu Akishapata Rehema Baada ya Madhara.**

Allah تعالی Anaeleza kwamba, Akishawaonjesha watu rehema baada ya madhara yaliyowagusa, kama vile kuwa na raha baada ya shida, na mavuno baada ya njaa na mvua baada ya ukame na kama hivyo.

إِذَا لَهُمْ مَكْرُفِي آيَاتِنَا<sup>٥</sup>

*“...utawaona wana vitimbi kuzipangia Ishara Zetu”.*

Mujahid alisema: “Tabia hiyo ya binadamu ni stihizai na kukadhibisha”<sup>1</sup>. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالی,

وَإِذَا مَسَّ الْإِنْسَانَ الضُّرُّ دَعَانَا لِجَنبِهِ أَوْ قَاعِدًا أَوْ قَائِمًا

*“Na mtu akiguswa na shida hutuomba naye kaegesha ubavu, au kaka, au kasimama”. (10:12)*

Katika *Sahih* kuna Hadithi kwamba Mtume ﷺ aliwasalisha Masahaba Sala ya Al-Fajiri baada ya usiku uliokuwa na mvua, halafu akasema;

«هَلْ تَذُرُونَ مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ اللَّيْلَةَ؟»

*“Je mnakijua alichokisema Mola wenu usiku (wa leo)?”*

Walisema: “Allah تعالی na Mtume ﷺ wanajua zaidi”. Akasema,

<sup>1</sup> At-Tabari 15:49.

«قَالَ: أَصْبَحَ مِنْ عِبَادِي مُؤْمِنٌ بِي وَكَافِرٌ، فَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِفَضْلِ اللَّهِ  
وَرَحْمَتِهِ فَذَلِكَ مُؤْمِنٌ بِي كَافِرٌ بِالْكَوْكَبِ، وَأَمَّا مَنْ قَالَ: مُطِرْنَا بِنَوْءِ كَذَا  
وَكَذَا فَذَلِكَ كَافِرٌ بِي مُؤْمِنٌ بِالْكَوْكَبِ،»

“Allah تعالى Alisema: ‘Katika asubuhi hii ya leo, baadhi ya waja Wangu wamekuwa Waumini na wengine Makafiri. Ama aliyesema, ‘Tumepata mvua kutokana na Fadhila na Rehema za Allah تعالى. ‘Huyo ndiye anayeniamini Mimi na anazikataa nyota. Na aliyesema: “Tumepata mvua kwa sababu ya nyota kadha na kadha, basi huyo ndiye amenikufuru na muumini wa nyota”<sup>1</sup>.

Kauli ya Allah تعالى: قُلْ اللَّهُ أَسْرَعُ مَكْرًا

**“Sema: Mwenyezi Mungu ni Mwepesi zaidi wa Kupanga...”**

Maana yake: Ni Muweza zaidi wa Kuwavuta taratibu mpaka mkosefu anaweza kudhani kwamba Allah تعالى Hatamuadhibu. Lakini kwa hakika! Huko ni kusogezwa mbele kwa muda tu, kisha Ataadhibu kwa ghafla. Wakati huo huo, waandishi watukufu (yaani, Malaika) wanaandika kila alitendalo na kuyahifadhi. Kisha wanayafikisha kwa Mwenye Kuyajua ya ghaibu na ya Kuonekana, na Atawajazi kwa amali tukufu na za kudharaulika, na zenye udogo hata kama wa tundu dogo la kokwa na ugozi mwembamba wa katika kokwa. Kisha, Allah تعالى Alieleza kwamba;

هُوَ الَّذِي يُسِيرُكُمْ فِي الْأَبْرَارِ وَالْبَحْرِ ط

**“Yeye Ndiye Anayekuendesheni bara na baharini”.**

Kwa maana: Anakuhifadhini na Kukutunzeni kwa Uangalizi Wake na Usimamizi.

حَتَّىٰ إِذَا كُنْتُمْ فِي الْفُلِكِ وَجَرَبَ بِكُمْ بَرِيحٌ طَيِّبَةٌ وَفَرِحُوا بِهَا

**“Hata mnapokuwa majahazini na yanakuwa yanakwenda nao kwa upepo mzuri wakaufurahia”.**

Maana yake: Kwa wepesi na utulivu. Wakati wakiwa katika hali hiyo, ghafla.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 2:607.

جَاءَتْهَا

“...*ukawazukia*”. Kwa maana: Safina hizo.

رِيحٌ عَاصِفٌ

“...*upepo mkali*”. Kwa maana: Wa kasi.

وَجَاءَهُمُ الْمَوْجُ مِنْ كُلِّ مَكَانٍ

“...*na yakawajia mawimbi kutoka kila upande*”. Maana: Bahari ikawafunika.

وَوَطَّنُوا أُنثَمَ أَحْيَطَ بِهَمِّ

“...*na wakaona wameshazongwa...*”. Kwa maana wameangamia.

دَعَاؤُا اللَّهِ مُخْلِصِينَ لَهُ الَّذِينَ

“...*basi hapo humuomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia niya*”.

Maana yake: Hawamshirikishi na sanamu katika kumuomba, bali wanampwekesha katika Kumuabudu na Kumnyenyekea. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَاهُ فَلَمَّا نَجَّكُم إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ وَكَانَ

الْإِنْسَانُ كَفُورًا ﴿٦٧﴾

“*Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu. Na Anapokuvueni mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanadamu ni mwingi wa kukanusha*”.  
(17:67)

Na katika Aya inayoelezwa hapa, Allah تعالى Alisema;

دَعَاؤُا اللَّهِ مُخْلِصِينَ لَهُ الَّذِينَ لَئِنْ أُجِبْتُمْ مِنْ هُنْدِهِ

“...*basi hapo humuomba Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia niya: ukituokoa na haya...*”.

Maana yake: Hali hii.

لَتَكُونَنَّ مِنَ الشَّاكِرِينَ

“...*bila ya shaka tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru*”.

Kwa maana: Katu hatutakushirikisha na chochote na kabisa tutakupwekesha kwa Ibada huko tuendako, kama tunavyokuomba Wewe Peke Yako katika dua hapa ulimwenguni. Allah تعالى Alisema;

فَلَمَّا أَنْجَبَهُمْ

“**Lakini Akishawaokoa.**” Kutoka katika shida hiyo.

إِذَا هُمْ يَبْتَغُونَ فِي الْأَرْضِ بِغَيْرِ الْحَقِّ<sup>ط</sup>

“...**mara wanafanya jeuri tena katika nchi bila ya haki.**” Kwa maana: Kama hawakuwa na lolote katika dua na ahadi zao.

كَأَن لَّمْ يَدْعُنَا إِلَىٰ ضُرٍّ مِّنْهُ<sup>ط</sup>

“...**kama kwamba hakupata kutuomba Tumuondoshee shida iliyompata.**” (10:12) Na Allah تعالى Akasema:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنَّمَا بِغَيْرِكُمْ عَلَىٰ أَنْفُسِكُمْ<sup>ط</sup>

“**Enyi watu! Jeuri zenu zitakudhuruni wenyewe.**” Kwa maana: Kwa hakika, mtakaonja athari ya uasi ni nyinyi wenyewe, wala hamtamdhuru yeyote isipokuwa nyinyi wenyewe. Kama ilivyo katika Hadithi;

«مَا مِنْ ذَنْبٍ أَجْدَرَ أَنْ يُعَجِّلَ اللَّهُ عُقُوبَتَهُ فِي الدُّنْيَا مَعَ مَا يَدَّخِرُ اللَّهُ لِصَاحِبِهِ فِي  
الْآخِرَةِ مِنَ الْبَغْيِ وَقَطِيعَةِ الرَّجْمِ»

“**Hapana dhambi yenye haki zaidi ya kuharakisha adhabu ya Allah تعالى, duniani pamoja na kuyaweka hifadhini kwa ajili ya Mtendaji huko Akhera, kuliko uasi na kukata mahusiano ya kindugu.**”<sup>1</sup>

Na Kauli Yake Allah تعالى:

مَتَنَعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا<sup>ط</sup>

“**Hii ni starehe ya maisha ya dunia.**” Maana yake: Hiyo ni starehe dhaifu na hakiri kabisa ya duniani.

ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُكُمْ

“**Kisha marejeo yenu ni Kwetu.**” Kwa maana: Mwisho wenu na wa malengo yenu.

<sup>1</sup> Abu Dawud 5: 208.

## فُنُنِيكُمْ

“...*na hapo Tutakuambieni*”. Maana: Tutakupasheni khabari juu ya amali zenu, na kukulipeni kwazo. Atakayekuta kheri, basi amhimidi Allah تعالى na mwenye kukuta kinyume cha hivyo, basi asimlaumu yeyote isipokuwa nafsi yake.

إِنَّمَا مَثَلُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَاءٍ أَنْزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ مِمَّا يَأْكُلُ  
النَّاسُ وَالْأَنْعَامُ حَتَّى إِذَا أَخَذَتِ الْأَرْضُ زُخْرُفَهَا وَازَّيَّنَتْ وَظَنَّ أَهْلُهَا أَنَّهُمْ قَدِرُوا  
عَلَيْهَا أَتَتْهَا أَمْرًا لَيْلًا أَوْ نَهَارًا فَجَعَلْنَاهَا حَصِيدًا كَأَن لَّمْ تَغِبْ بِالْأَمْسِ ۚ كَذَلِكَ  
نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ ﴿٢٤﴾ وَاللَّهُ يَدْعُوا إِلَىٰ دَارِ السَّلَامِ وَيَهْدِي مَن يَشَاءُ إِلَىٰ  
صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٢٥﴾

24. *“Hakika mfano wa maisha ya dunia ni kama maji Tuliyoateremsha kutoka mbinguni, kisha yakachanganyika na mimea ya ardhi wanayoila watu na wanyama. Mpaka ardhi ilipokamilika uzuri wake, na ikapambika, na wenyewe wakadhani wameshaiweza, iliifikia Amri Yetu usiku na mchana, Tukaifanya kama iliyofekwa – kama kwamba haikuwapo jana. Namna hivi Tunazipambanua Ishara Zetu kwa watu wanaofikiri”.*

25. *“Na Mwenyezi Mungu Anaita kwenda Nyumba ya Amani, na Anamuongoa Amtakaye kwenye njia iliyonyooka”*

## Mfano wa Maisha ya Duniani.

Allah تعالى Amepiga mfano wa uzuri wa dunia na uharaka wa kumalizika na kuondoka kwake kuwa ni kama mimea Aliyoiotesha ardhini kwa maji Aliyoyateremsha kutoka mbinguni. Mimea hiyo ni pamoja na mazao na matunda ya namna mbalimbali; na inayoliwa na wanyama, kama vile klova (jamii ya mimea yenye majani ya pande tatu, hupendwa sana na mifugo), majani mateke na mengine.

حَتَّى إِذَا أَخَذَتِ الْأَرْضُ زُخْرُفَهَا

*“Mpaka ardhi ilipo kamilika uzuri wake,...”* Kwa maana: Kupendeza kwake kusikodumu.



وَأَزَيَّنْتَ

"...*na ikapambika*". Maana yake: Ikawa nzuri kwa kinachoota katika milima kama vile maua yenye kuchanua yenye maumbo na rangi tofauti.

وَوَظَّنَّ أَهْلَهَا

"...*na wenyewe wakadhani*...". Waliolima na kupanda.

أَنَّهُمْ قَدِيرُونَ عَلَيْهَا

"...*wameshaiweza*..." Kwa maana: Katika kulima na kuvuna, mara wakiwa katika hali hiyo, wakafikwa na radi au upepo mkali wa baridi. Ukayakausha majani yake na kuyatilifu matunda yake. Allah تعالى Alisema;

أَتَيْتَهَا أَمْرًا لَيْلًا أَوْ نَهَارًا فَجَعَلْنَاهَا حَصِيدًا

"...*iliifikia Amri Yetu usiku na mchana, Tukaifanya kama iliyofekwa*". Kwa maana: Kavu, baada ya ukijani na kupapatuka.

كَأَن لَّمْ تَغْنَبْ بِالْأَمْسِ

"...*kama kwamba haikuwapo jana*". Maana yake: Kama kwamba hakuna kilichokuwepo pale kabla ya hayo. Qatadah alisema, "Kama vile haikustawi. Na hivyo ndivyo mambo yatakavyokuwa baada ya kuondoka, ni kama kwamba hayakuwepo." Kwa ajili hii, ilikuja katika Hadithi;

«يُؤْتَى بِأَنْعَمِ أَهْلِ الدُّنْيَا، فَيُعْمَسُ فِي النَّارِ غَمَسَةً، فَيُقَالُ لَهُ: هَلْ رَأَيْتَ خَيْرًا قَطُّ؟ هَلْ مَرَّ بِكَ نَعِيمٌ قَطُّ؟ فَيَقُولُ: لَا، وَيُؤْتَى بِأَشَدِّ النَّاسِ عَذَابًا فِي الدُّنْيَا، فَيُعْمَسُ فِي النَّعِيمِ غَمَسَةً، ثُمَّ يُقَالُ لَهُ: هَلْ رَأَيْتَ بُرْسًا قَطُّ؟ فَيَقُولُ لَا»

"Ataletwa mtu aliyeshi maisha ya anasa sana duniani na kuchowwa Motoni. Kisha ataambiwa: "Je uliwahi kupata kheri yoyote? Je umewahi kupata neema yoyote?" Atasema; "Hapana". Na ataletwa mtu aliyekuwa na dhiki sana duniani, na kuchowwa katika neema, na ataambiwa: "Uliwahi kukumbana na Tatizo lolote?" Atasema; "Hapana"<sup>1</sup>.

Katika kupasha khabari juu ya waliohiliki, Allah تعالى Alisema;

<sup>1</sup> Muslim 4:2162.

فَأَصْبَحُوا فِي دَيْرِهِمْ جَثِيمِينَ ﴿٦٧﴾ كَأَن لَّمْ يَغْنَوْا فِيهَا

**“...wakapambazukiwa nao ni maiti majumbani mwao. Kama kwamba hawakuwako huko”. (11:67-68)**

Kisha Allah تعالى Alisema;

كَذَلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ

**“Namna hivi Tunazipambanua Ishara Zetu”**. Kwa maana: Tunazibainisha hoja na dalili.

لِقَوْمٍ يَتَفَكَّرُونَ

**“...kwa watu wanaofikiri”** Kisha wanaozingatia mifano hii kwa dunia kuondoka haraka licha watu wake wameghurika nayo, kutegemea na kushikilia ahadi zake, mara inawakimbia kwa ghafla. Miongoni mwa tabia zake ni kuwatoroka wenye kuihitaji. Allah تعالى Amekuisha piga mfano wa dunia kwa mimea ya ardhini katika Aya nyingi katika Kitabu Chake. Alisema katika *Surat Al-Kahf*,

وَأَضْرَبَ لَهُم مَّثَلًا الْحَيَاةَ الدُّنْيَا كَمَا أَنزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ فَأَصْبَحَ هَشِيمًا تَذْرُوهُ الرِّيحُ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾

**“Na uwapigie mfano wa maisha ya dunia. Hayo ni kama maji Tunayoyateremsha kutoka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi, kisha hiyo mimea ikawa vibuwa vinavyopeperushwa na upepo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu”**. (18:45)

Kadhalika, katika *Surat Az-Zumar* Aya ya (21) na *Al-Hadid* Aya ya (20). Allah تعالى Anapiga mfano wa maisha ya duniani.

**Kuhamasishwa Kwenye Neema za Milele Ambazo Haziondoki.**

Kauli ya Allah تعالى;

وَاللَّهُ يَدْعُوًا إِلَىٰ دَارِ السَّلَامِ

**“Na Mwenyezi Mungu Anaita kwenye Nyumba ya Amani”**.

Baada ya kuitaja dunia na kuondoka kwake haraka, Aliwaita watu kwenda Jannah na Akawahimiza kuiomba. Ameiita Nyumba ya Amani, yaani isiyoyosha na dosari, nuksani na tabu. Allah تعالى Alisema;

وَاللَّهُ يَدْعُوا إِلَى دَارِ السَّلَامِ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ

**“Na Mwenyezi Mungu Anaita kwenye Nyumba ya Amani na Anamuongoa Amtakaye kwenye njia iliyo nyooka.”**

Jabir bin ‘Abdullah رضي الله عنهما alisema, siku moja Mtume ﷺ alitoka na kusema;

«إِنِّي رَأَيْتُ فِي الْمَنَامِ كَأَنَّ جِبْرِيْلَ عِنْدَ رَأْسِي، وَمِيكَائِيلَ عِنْدَ رِجْلَيْ، يَقُولُ أَحَدُهُمَا لِيصَاحِبِي: اضْرِبْ لَهُ مَثَلًا، فَقَالَ: اسْمَعْ، سَمِعْتُ أَدْنُكَ، وَاعْقِلْ، عَقَلَ قَلْبُكَ، إِنَّمَا مَثَلُكَ وَمَثَلُ أُمَّتِكَ كَمَثَلِ مَلِكٍ اتَّخَذَ دَارًا، ثُمَّ بَنَى فِيهَا بَيْتًا، ثُمَّ جَعَلَ فِيهَا مَادَبَةً، ثُمَّ بَعَثَ رَسُولًا يَدْعُو النَّاسَ إِلَى طَعَامِهِ، فَمِنْهُمْ مَنْ أَجَابَ الرَّسُولَ، وَمِنْهُمْ مَنْ تَرَكَهُ، فَاللَّهُ الْمَلِكُ، وَالِدَارُ الْإِسْلَامُ، وَالْبَيْتُ الْجَنَّةُ، وَأَنْتَ يَا مُحَمَّدُ رَسُولُ، فَمَنْ أَجَابَكَ دَخَلَ الْإِسْلَامَ، وَمَنْ دَخَلَ الْإِسْلَامَ دَخَلَ الْجَنَّةَ، وَمَنْ دَخَلَ الْجَنَّةَ أَكَلَ مِنْهَا»

*“Mimi nimeona ndotoni, kama vile Jibril yuko kichwani kwangu, na Mikail akiwa miguuni kwangu. Mmoja wao anamuambia mwenzake: “Mpigie mfano”. Akasema: “Fungua sikio lako na ufungue moyo wako upate kufahamu vizuri. Mfano wako na wa umma wako, ni kama Mfalme aliyechukua ardhi, kisha akajenga nyumba humo. Halafu akaandaa dhifa. Akamtuma mjumbe kuwaalika watu katika chakula chake. Miongoni mwao, wapo waliomuitika mjumbe, na wengine walikataa. Allah تعالی Ndiye Mfalme, ardhi ni Uislamu, nyumba ni Jannah, na wewe ewe Muhammad ni Mjumbe. Basi atakayekuitika ataingia katika Uislamu, na atakayeingia katika Uislamu, ataingia Peponi na atakula humo”.*

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu Hadithi hii<sup>1</sup>.

Pia ilielezwa kwamba Abud-Dardai رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema;

«مَا مِنْ يَوْمٍ طَلَعَتْ فِيهِ الشَّمْسُ إِلَّا وَبِجَنِّيْهَا مَلَكَانِ يُتَادِيَانِ يَسْمَعُهُ خَلْقُ اللَّهِ كُلُّهُمْ إِلَّا الثَّقَلَيْنِ: يَا أَيُّهَا النَّاسُ! هَلُمُّوا إِلَى رَبِّكُمْ، إِنَّ مَا قَلَّ وَكَفَى خَيْرٌ مِمَّا كَثُرَ وَالنَّهْيُ»

*“Hapana siku inayochomozewa na jua bali hushuka Malaika wawili*

<sup>1</sup> At-Tabari 15:61. Isnadi yake si unganifu.

wakinadi na kusikiwa na viumbe wote wa Allah تعالى, isipokuwa *Thaqalain* (vizito viwili – majini na wanadamu): “Enyi watu! Njooni kwa Mola wenu. Kwa hakika, kilicho kichache na kikatoshenzeza ni bora kuliko kilichokithiri lakini cha pumbao tu”.

Na alisema kwamba Allah تعالى Aliyateremsha hayo ndani ya Qur’an, katika Kauli Yake;

وَاللَّهُ يَدْعُوْا إِلَىٰ دَارِ السَّلَامِ

**“Na Mwenyezi Mungu Anaita kwenda Nyumba ya Amani”.**

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى walilinukuu hili<sup>1</sup>.

\* \* \*

\* الَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۗ وَلَا يَرْهَقُ وُجُوهَهُمْ قَتَرٌ  
 وَلَا ذِلَّةٌ ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٥٦﴾  
 وَالَّذِينَ كَسَبُوا السَّيِّئَاتِ جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا وَتَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ۗ  
 مَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ ۗ كَانَمَا أُغْشِيَتْ وُجُوهُهُمْ قِطْعًا  
 مِنَ اللَّيْلِ مُظْلِمًا ۗ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٥٧﴾  
 وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا  
 مَكَانَكُمْ أَنْتُمْ وَشُرَكَائِكُمْ ۗ فزِيلْنَا بَيْنَهُمْ ۗ وَقَالَ شُرَكَائِهِمْ مَا  
 كُنْتُمْ إِلَّا بَنَاتُنَا عَبَدُودٌ ﴿٥٨﴾ فَكَلَّمْنَا بِلَاغٍ شَهِيدًا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ  
 ۗ إِنَّ كُنَّا عَنْ عِبَادَتِكُمْ لَغَافِلِينَ ﴿٥٩﴾ هُنَالِكَ تَبْلَأُونَ كُلُّ  
 نَفْسٍ مِمَّا أَسْلَفَتْ ۗ وَرُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقُّ ۗ وَضَلَّ  
 عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٦٠﴾ قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِّنْ  
 السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَمَنْ يُخْرِجُ  
 الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَنْ يُدْبِرُ  
 الْأُمُورَ ۗ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۗ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٦١﴾ فَذَلِكُمُ اللَّهُ  
 رَبُّكُمْ الْحَقُّ ۗ فَمَاذَا بَعَدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ ۗ فَأَنَّى  
 تُصْرَفُونَ ﴿٦٢﴾ كَذَٰلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى  
 الَّذِينَ فَسَقُوا أَنَّهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٣﴾

\* الَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ ۗ  
 وَلَا يَرْهَقُ وُجُوهَهُمْ قَتَرٌ وَلَا ذِلَّةٌ ۗ  
 أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَنَّةِ ۗ هُمْ فِيهَا  
 خَالِدُونَ ﴿٥٦﴾

26. "Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi. Wala vumbi halitawafunika nyuso zao, wala madhila. Hao ndio watu wa Peponi. Humo watadumu".

**Malipo ya Waja Wema.**

Allah تعالى Anaeleza kwamba mwenye kufanya vizuri duniani kwa imani na amali njema, basi atapata mema katika Akhera. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى,

هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَنِ إِلَّا الْإِحْسَانُ ﴿٦١﴾

"Hakuna malipo ya ihsani ila kulipa ihsani (vile vile)?" (55:60)

Kauli ya Allah تعالى,

وَزِيَادَةٌ ۗ

"...na zaidi". Huko ni kuongezewa thawabu kwa mara kumi ya mifano wake, mpaka mara mia saba, hata zaidi ya hapo. Hii inakusanya yale ambayo

1 At-Tabari 15:60 na Ahmad 5:197.

Allah تعالی Atawapa Peponi, kama vile makasri, mahurulaini na Allah تعالی kuwa radhi nao. Atawapa Alichokificha kwa ajili yao kitakachotuliza jicho, na lililo bora na la juu zaidi katika hayo ni kuutazama Wajih Wake Mtukufu. Hiyo ni ziada kubwa kuliko yote Aliyowapa. Si amali zao ndizo zinazowafanya wastahiki hilo, bali ni kwa Fadhila na Rehema Zake.

Kuna tafsiri iliyosimuliwa juu ya ziada ya kuuangalia Wajih wa Allah تعالی, kutoka kwa Abubakr As-siddiq, Hudhaifah bin Al-Yaman, 'Abdullah bin 'Abbas, Sa'id bin Al-Musayyab, 'Abdur-Rahman bin Abu Layla, 'Abdur-Rahman bin Sabit, Mujahid, 'Ikrimah, 'Amir bin Sa'd, 'Ata, Adh-Dhahhak, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi, Muhammad bin Is-haq na wengine رضي الله عنهم<sup>1</sup> katika wanazuoni wa hapo mwanzo na wa baada yao. Kuna Hadithi nyingi zilizosimuliwa kutoka kwa Mtume ﷺ miongoni mwazo ni aliyoinukuu Ahmad kuwa Suhayb رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ alisoma Aya hii,

لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ

**"Kwa wafanyao wema ni wema na zaidi".** Halafu akasema;

«إِذَا دَخَلَ أَهْلُ الْجَنَّةِ الْجَنَّةَ وَأَهْلُ النَّارِ النَّارَ نَادَىٰ مُنَادٍ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ إِنَّ لَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ مَوْعِدًا يُرِيدُ أَنْ يُنَجِّزَكُمُوهُ فَيَقُولُونَ: وَمَا هُوَ؟ أَلَمْ يُنْقَلْ مَوَازِينَنَا؟ أَلَمْ يَبْتِئَضْ وَجُوهَنَا وَيُدْخِلْنَا الْجَنَّةَ وَيُجْرِنَا مِنَ النَّارِ؟ - قَالَ - فَيَكْشِفُ لَهُمُ الْحِجَابَ، فَيَنْظُرُونَ إِلَيْهِ، فَوَاللَّهِ مَا أَعْطَاهُمُ اللَّهُ شَيْئًا أَحَبَّ إِلَيْهِمْ مِنَ النَّظَرِ إِلَيْهِ، وَلَا أَقَرَّ لِأَعْيُنِهِمْ»

*"Watu wa Peponi wakishaingia katika pepo na wale wa Motoni wakishaingia katika moto, mtangazaji atanadi: "Enyi watu wa Peponi! Mna miadi kutoka kwa Allah تعالی mnayotaka Akutekelezeeni". Nao Watauliza: "Ni ipi hiyo? Hakuifanya Mizani Yake kuwa nzito zaidi? Hakuzifanya nyuso zetu kuwa nyeupe na Kutuingiza Peponi na Kutuepusha na Moto?" Kisha, Allah تعالی Atakiondoa kizuizi kwao, na watamuona Yeye. Wallahi! Itakuwa, hakuna kitu Alichowapa watakachokipenda sana na kuyatuliza macho zaidi ya kumuangalia Yeye."<sup>2</sup>*

<sup>1</sup> At-Tabari 15:63-68.

<sup>2</sup> Ahmad 4:333.

Hivi ndivyo Muslim na kundi la Maimamu walivyonyuka Hadithi hii<sup>1</sup>. Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَلَا يَرَهُقُ وُجُوهُهُمْ قَتْرٌ

**“Wala vumbi halitawafunika nyuso zao”**. Maana yake: Si utusitusi wala kiza kitakachowapata katika Siku ya Mkusanyiko, ambapo nyuso za makafiri zitatiwa weusi na vumbi.

وَلَا ذَلَّةٌ

**“Wala madhila”**. Kwa maana: Unyonge na udhalili. Inamaanisha kuwa hawatafikiwa na udhalili wa ndani wala wa dhahiri. Bali ni sawa na Kauli ya Allah تعالى juu yao;

فَوَقْنَهُمُ اللَّهُ شَرَّ ذَلِكَ الْيَوْمِ وَلَقَلْهُمْ نَضْرَةٌ وَسُرُورًا ﴿٦١﴾

**“Basi Mwenyezi Mungu Atawalinda na shari ya siku hiyo, na Atawakutanisha na raha na furaha”**. (76:11)

Kwa maana: Nuru katika nyuso zao na furaha nyoyoni mwao. Kwa Fadhila na Rehema Zake, Allah تعالى Atujaalie tuwe miongoni mwao – Amin.

وَالَّذِينَ كَسَبُوا السَّيِّئَاتِ جَزَاءُ سَيِّئَةٍ بِمِثْلِهَا وَتَرَهُفُهُمْ ذَلَّةٌ مَّا هُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ طَّ كَانَمَا  
أَغْشَيْتِ وُجُوهُهُمْ قِطْعًا مِنَ اللَّيْلِ مُظْلِمًا أُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٦٢﴾

**27. “Na wale waliochuma maovu, malipo yao ni mfano wake vile vile, na yatawafika madhila. Hawatakuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu. Nyuso zao kama kwamba zimefunikwa na vipande vya usiku wa giza. Hao ndio watu wa Motoni, wao humo watadumu”**.

### Malipo ya Waovu.

Baada ya Allah تعالى Kueleza hali za watu wema ambao wataongezewa zaidi malipo yao mema. Allah تعالى Aliendelea kwa Kutaja hali za waovu. Alieleza Uadilifu Wake kwao, na kwamba Atawajazi sawa na uovu wao, Hatawazidishia chochote katika hayo;

وَتَرَهُفُهُمْ

**“...na yatawafika...”**. Maana: Watafunikwa na kugubikwa na madhila. Kutokana

<sup>1</sup> Muslim 1:163, Tufhat Ahwadh 8:522, An-Nasai katika Al-Kubra 6:361 na Ibn Majah 1:67.

na maasi yao na khofu yao ndani yake. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَتَرَاهُمْ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا خَشِيعِينَ مِنَ الْذَّلِّ

**“Na utawaona wanapelekwa kwenye Moto, nao wamenyenyekea kwa unyonge”.** (42:45) Na Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفِيلاً عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ  
الْأَبْصَارُ ﴿٤٢﴾ مُهْطِعِينَ مُقْنِعِي رُءُوسِهِمْ

**“Wala usidhani Mwenyezi Mungu Ameghafilika na wanayo yafanya madhalimu. Hakika Yeye Anawaakhirisha tu mpaka siku yatapokodoka macho yao. Nao wako mbioni, vichwa juu”.**  
(14:42-43)

Kauli ya Allah تعالى;

مَا هُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ عَاصِمٍ ط

**“Hawatakuwa na wa Kuwalinda na Mwenyezi Mungu”.**

Maana yake: Wa kuzuia wala wa kuwakinga dhidi ya adhabu.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

يَقُولُ الْإِنْسَانُ يَوْمَئِذٍ أَيْنَ الْمَفْرُغُ ﴿١٠﴾ كَلَّا لَا وَزَرَ ﴿١١﴾ إِلَىٰ رَبِّكَ يَوْمَئِذٍ الْمُسْتَقَرُّ ﴿١٢﴾

**“Siku hiyo mtu atasema: Yako wapi makimbilio? La! Hapana pa kukimbilia! Siku hiyo pa kutua ni kwa Mola wako Mlezi tu”.**  
(75:10-12)

Kauli ya Allah تعالى;

كَأَنَّمَا أَغْشَيْتَ وُجُوهُهُمْ

**“Nyuso zao kama kwamba zimefunikwa na vipande vya usiku wa giza”.**

Nyuso zao zitakuwa nyeusi huko Akhera. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌُ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌُ فَأَمَّا الَّذِينَ آسَوْدَتْ وُجُوهُهُمْ أَكْفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ  
فَذُقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿١٣﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ أَبْيَضتْ وُجُوهُهُمْ ففِي رَحْمَةِ اللَّهِ هُمْ

فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٤﴾



**“Siku ambayo nyuso zitanawiri na nyuso zitasawijika. Ama hao ambao nyuso zao zitasawijika wataambiwa: Je! Mlikufuru baada ya kuamini kwenu? Basi onjeni adhabu kwa vile mliyokuwa mnakufuru. Ama wale ambao nyuso zao zitanawiri watakuwa katika Rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao humo watadumu”.**  
(3:106-107)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ ﴿٢٨﴾ صَاحِكَةٌ مُّسْتَبْشِرَةٌ ﴿٢٩﴾ وَوُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ عَلَيَّهَا غَبْرَةٌ ﴿٣٠﴾

**“Siku hiyo ziko nyuso zitazonawiri, zitacheka, zitachangamka zikifurahia habari njema za Peponi. Na nyuso zingine siku hiyo zitakuwa zimenata na mavumbi”.** (80:38-40)

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ جَمِيعًا ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا مَكَانَكُمْ أَنْتُمْ وَشُرَكَائِكُمْ فَزَيْلَنَا بَيْنَهُمُ ۗ وَقَالَ شُرَكَائُهُمْ مَا كُنْتُمْ إِلَّا نَا تَعْبُدُونَ ﴿٢٨﴾ فَكَفَى بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ إِنْ كُنَّا عَنْ عِبَادَتِكُمْ لَغَافِلِينَ ﴿٢٩﴾ هُنَالِكَ تَبْلُوا كُلُّ نَفْسٍ مَّا أَسْلَفَتْ ۗ وَرُدُّوْنَا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمْ ۗ الْحَقِّي ۗ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٣٠﴾

**28. “Na siku Tutakapowakusanya wote, kisha Tutawaambia walio shirikisha: Simameni mahali penu nyinyi na wale mliowafanya washirika. Kisha Tutawatenga baina yao. Na hao walio washirikisha watasema: Nyinyi hamkuwa mkituabudu sisi”.**

**29. “Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni Shahidi baina yetu na nyinyi. Hakika sisi tulikuwa hatuna khabari ya ibada yenu”.**

**30. “Huko kila mtu atayajua aliyoyatangeliza. Na watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki, na yote waliyokuwa wakiyazua yatawapotea”.**

**Waungu wa Washirikina Watawakana Wafuasi Wao Siku ya Kiama**

Allah تعالی Anasema;

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ

**“Na siku Tutakapowakusanya wote”.**

Maana yake: Wakazi wote wa ardhini, majini, watu, wema na waovu.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی,

وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾

**“...na Tukawafufua – wala hatutamuacha hata mmoja kati yao”.**

(18:47)

ثُمَّ نَقُولُ لِلَّذِينَ أَشْرَكُوا مَكَانَكُمْ أَنْتُمْ وَشُرَكَائِكُمْ

**“...kisha Tutawaambia walioshirikisha: Simameni mahali penu nyinyi na wale mliowafanya washirika.”**

Maana yake: Kuweni nyinyi na wao katika mahali maalumu ambapo mtakuwa mmejitenga na mahali pa Waumini. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی;

وَأَمْتَنُوا الْيَوْمَ أَيُّهَا الْمَجْرُمُونَ ﴿٥١﴾

**“Na enyi wakosefu! Jitengeni leo!” (36:59)**

Na Kauli Yake Allah تعالی,

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُومِئِدُ يَتَفَرَّقُونَ ﴿٥٢﴾

**“Na siku itaposimama Saa, siku hiyo watagawanyika”. (30:14)**

Na katika Aya nyingine;

يَوْمِئِذٍ يَصَّدَّعُونَ

**“Siku hiyo watu watatengana”. (30:43)**

Kwa maana: Watagawanyika katika makundi mawili.

Haya ni pindi Atakapokuja Allah تعالی kwa ajili ya Hukumu ya Mwisho. Kwa ajili hii, hayo jamesemwa. Waumini watamuomba sana Allah تعالی: “Ewe Allah! (Tunaomba) Hukumu ya Mwisho ifanyike ili tupate kupumzika kutokana na hali yetu hii”. Katika Hadithi nyingine;

اِنْحَرُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ كَوْمٍ فَوْقَ النَّاسِ<sup>1</sup>

*“Katika Siku ya Kiyama, sisi tutakuwa mahali pa juu pa kuonekana na watu (wengine).”<sup>1</sup>*

Katika Aya hii tukufu, Allah تعالیٰ Ameeleza Atakachowaamuru katika Siku ya Kiyama, Washirikina na wale waliowafanya Washirika na masanamu yao;

مَكَانَكُمْ اَنْتُمْ وَاَشْرَاؤُكُمْ<sup>ط</sup> فَزَيَّلْنَا بَيْنَهُمْ

***“...mahali penu nyinyi na wale mliowafanya washirika. Kisha Tutawatenga baina yao.”***

Kwamba wao watazikana ibada zao na kudai kujitenga nao. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ;

كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ

***“Sivyo kabisa! Watakataa hiyo ibada yao.” (19:82)***

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ,

اِذْ تَبَرَّأَ الَّذِينَ اتُّبِعُوا مِنَ الَّذِينَ اتَّبَعُوا

***“Waliofuatwa watakapowakataa wale waliowafuata”. (2:166)***

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ,

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِن دُونِ اللَّهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَن دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ﴿٥٦﴾ وَإِذَا حُشِرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً

***“Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Mwenyezi Mungu, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao. Na ambao watu watakapo kusanywa watakuwa maadui zao”. (46:5-6)***

Kauli ya Allah تعالیٰ katika Aya hii inarejea habari juu ya kauli ya Washirikina kuwajibu wanaowaabudu wao pindi watakapokana kwamba waliwaabudu”.

<sup>1</sup> Muslim 1:177.

فَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ

**“Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni Shahidi baina yetu na nyinyi”.**

Maana: Hatukuwa tukitambua wala tukijua, bali nyinyi mlikuwa mkituabudu kwa namna ambayo tulikuwa hatuna ujuzi nanyi. Allah تعالى ni Shahidi baina yetu na nyinyi, sisi hatukukuiteni katika kutuabudu, wala hatukukuamrisheni wala sisi hatukuwa radhi nanyi katika hilo. Kauli ya Allah تعالى:

هُنَالِكَ تَبْلُوا كُلُّ نَفْسٍ مَّا أَسْلَفَتْ

**“Huko kila mtu atayajua aliyo yatanguliza”.**

Maana yake: Kisimamo cha hesabu katika Siku ya Kiyama, kila nafsi itayajua yote yaliyopita katika amali zake, ikiwa ni kheri au shari. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine;

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ

**“Siku itakapodhihirishwa siri” (86:9)**

Na Kauli Yake Allah تعالى,

يُنَبِّئُوا الْإِنْسَانَ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ

**“Siku hiyo mwanadamu ataambiwa aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha”. (75:13)** Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَنُخْرِجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا ﴿١٣﴾  
أَقْرَأْ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ  
عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٤﴾

**“Na Siku ya Kiyama Tutamtolea Kitabu atakachokikuta kiwazi kimekunjuliwa. Ataambiwa: Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu”. (17:13-14)**

Kauli ya Allah تعالى,

وَرُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمْ الْحَقِّ

**“Na watarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, Mola wao wa Haki”.**

Kwa maana: Na mambo yote yatarejea kwa Allah تعالى, Mwenye Kuhukumu kwa Uadilifu. Atahukumu na Kuwaingiza Jannah wakazi wa Peponi, na Motoni kwa watu wa motoni.

وَضَلَّ عَنْهُمْ

"...na yatawapotea". Maana yake: Yatawaondoka.

مَا كَانُوا يَفْتُرُونَ

"...yote waliyokuwa wakiyazua". Kwa maana: Waliyokuwa wakiyaabudu badala ya Allah تعالى kwa uzushi.

قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمْ مَنْ يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَمَنْ يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيتِ وَيُخْرِجُ الْمَمِيتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَنْ يُدْبِرُ الْأَمْرَ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٣١﴾ فَذَلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمْ الْحَقُّ ۖ فَمَاذَا بَعَدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ ۗ فَأَنْتُمْ تُصِرُّونَ ﴿٣٢﴾ كَذَلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ فَسَقُوا أَنَّهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٣﴾

31. "Sema: Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Au ni nani anayemiliki kusikia na kuona? Na nani amtoaye hai kutoka maiti, na akamtoa maiti katika aliye hai? Na nani anayeyadabiri mambo yote? Watasema: Allah, Mwenyezi Mungu. Basi sema: Je! Hamchi?"

32. "Basi huyo Ndiye Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu wa haki. Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu? Basi huwaje mkageuzwa?"

33. "Ndio kama hivyo Kauli ya Mola wako Mlezi itakavyo wathibitikia wale waliopotoka, ya kwamba hawataamini".

Washirikina Wanaitambua Tawhidi ya Allah تعالى Kwamba Yeye ni Mola, Hivyo Husimamishiwa Hoja Kutokana na Kulitambua Kwao Hilo.

Allah تعالى Anawahoji Washirikina kwa kutambua kwao Uumoja wa Allah تعالى katika Uungu. Ni ushahidi dhidi yao ambao lazima waukubali na wautambue Uungu Mmoja Uliyotakasika na Uwabudiwe. Allah تعالى Alisema:

قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

"Sema: Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi?" Kwa maana: Ni nani Anayeteremsha maji toka mbinguni na yakaipasua ardhi kwa Uweza wa Nguvu Zake na Kudura na Utashi Wake na Kuotesha humo,

حَبًّا ۝ وَعَيْبًا وَقَضْبًا ۝ وَزَيْتُونًا وَنَخْلًا ۝ وَحَدَاقٍ غُلْبًا ۝ وَفَيْكِهَةً وَأُبًّا ۝

**“(Kuotesha humo) nafaka. Na zabibu, na mimea ya majani. Na mizaituni, na mitende, na Bustani zenye miti iliyosongana barabara, na matunda, na malisho ya wanyama”. (80:27-31)**

أَأَلَّهُ مَعَ اللَّهِ ۝

**“Je! Yupo Mola mwengine zaidi ya Mwenyezi Mungu (ambaye huwezesha)?” (27:62)**

فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۝

**“Watasema: Allah, Mwenyezi Mungu”**

أَمَّنْ هَذَا الَّذِي يَرْزُقُكُمْ إِنْ أَمْسَكَ رِزْقَهُ ۝

**“Au ni nani huyo ambaye Atakupeni riziki kama Yeye Akizuia riziki Yake?” (67:21)**

Kauli ya Allah تعالى: أَمَّنْ يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ ۝

**“Au ni nani anayemiliki kusikia na kuona?”**

Kwa kumaanisha kuwa Allah تعالى Ndiye, Aliyekupeni nguvu hii ya kusikia na ya kuona. Angelitaka, Angelikuondoleeni na Kukupokonyeni hayo. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قُلْ هُوَ الَّذِي أَنْشَأَكُمْ وَجَعَلَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ ۝

**“Sema: Yeye Ndiye Aliyekuumbeni tangu mwanzo, na Akakupeni masikio na macho...” (67:23)**

Allah تعالى Amesema tena,

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَخَذَ اللَّهُ سَمْعَكُمْ وَأَبْصَرَكُمْ ۝

**“Sema: Mwaonaje Mwenyezi Mungu Akanyakua kusikia kwenu, na kuona kwenu...”. (6:46)**

Kauli ya Allah تعالى:

وَمَنْ يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيتِ وَيُخْرِجُ الْمَمِيتَ مِنَ الْحَيِّ

**“Na nani amtoaye hai kutoka maiti, na akamtoa maiti katika aliye hai?”**

Maana: Kwa Kudura Yake Tukufu na Neema Zake zenye kuenea. Kauli ya Allah تعالى:

وَمَنْ يُدْبِرُ الْأَمْرَ

**“Na nani anayeyadabiri mambo yote?”**

Kwa maana: ni nani Ambaye Mkononi Mwake kuna Umiliki wa kila kitu, na Ambaye Hulinda yote wala Halindwi. Ambaye Anahukumu. Hakuna wa kuipinga Hukumu Yake, wala kuigeuza, wala Haulizwi kuhusu Ayafanyayo, ilhali wao ni wenye kuulizwa?.

يَسْأَلُهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلَّ يَوْمٍ هُوَ فِي شَأْنٍ ﴿٢٩﴾

**“Vinamuomba Yeye vilivyomo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye Yumo katika mambo”. (55:29)**

Basi, Ufalme wote wa juu na wa chini na vilivyomo humo, kama vile Malaika, wanadamu na majini ni wenye haja Kwake, ni waja Wake, na wako katika kudhibitiwa na Yeye.

فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ

**“Watasema: Allah, Mwenyezi Mungu”.**

Kwa maana: Ilhali wanayajua na kuyatambua hayo.

فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ

**“Basi sema: Je! Hamchi?”**

Maana: Hamumkhofu kiasi kwamba mnamuabudu Yeye pamoja na wasiokuwa Yeye, kwa rai na ujahili wenu? Kauli ya Allah تعالى:

فَذَلِكُمْ اللَّهُ رَبُّكُمُ الْحَقُّ ط

**“Basi huyo Ndiye Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wenu wa haki”.**

Maana: Haya ndiyo mliyoyajua kwamba mwenye kuyafanya yote haya Ndiye Mola na Mungu wangu wa kweli Anayestahiki kupwekeshwa katika ibada.

فَمَاذَا بَعْدَ الْحَقِّ إِلَّا الضَّلَالُ<sup>ط</sup>

**“Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu?”**

Maana: Kila kinachoabudiwa, kisichokuwa Yeye ni batili. Hapana Mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye, Mmoja tu, wala hana mshirika.

فَأَنِّي تُصْرَفُونَ

**“Basi huwaje mkageuzwa?”**

Kwa maana: Vipi mnageuzwa dhidi ya kumuabudu mkaelekea katika kuabudu asiyekuwa Yeye, ilhali mnajua kuwa Yeye Ndiye Mola Aliyeumba na Ndiye Mtawala wa kila kitu? Kauli ya Allah تعالی:

كَذَلِكَ حَقَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى الَّذِينَ فَسَقُوا

**“Ndio kama hivyo Kauli ya Mola wako Mlezi itakavyowathibitikia wale waliopotoka,”**

Maana yake: Kama ambavyo hao Washirikina walikufuru na wakaendelea na ushirikina wao na kumuabudu Allah تعالی pamoja na visivyokuwa Yeye, pamoja na kuwa, wao wanatambua kwamba Yeye Ndiye Muumbaji, Mwenye Kuruzuku, Mtawala Pekee, Ambaye Aliwatuma Mitume kwa Tawhidi Yake. Ndiyo sababu ya Kauli ya Allah تعالی kwamba wao ni wenye kupata tabu zaidi katika wakazi wa Motoni;

قَالُوا بَلَىٰ وَلَٰئِكَ حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَى الْكَافِرِينَ ﴿٧١﴾

**“Watasema: Kwanini! Lakini limekwisha thibiti neno la adhabu juu ya makafiri”. (39:71)**

\* \* \*



قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَبْدُوا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ۚ قُلِ اللَّهُ  
 يَبْدُوا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ۚ فَأَنْتُمْ تُؤْفَكُونَ ﴿٣٤﴾ قُلْ هَلْ مِنْ  
 شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ ۚ قُلِ اللَّهُ يَهْدِي لِلْحَقِّ ۚ  
 أَفَمَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ أَحَقُّ أَنْ يُتَّبَعَ أَمْ لَا يَهْدِي  
 إِلَّا أَنْ يَهْدِي ۚ فَمَا لَكُمُ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٣٥﴾ وَمَا يَتَّبِعُ  
 أَكْثَرُهُمْ إِلَّا ظَنًّا ۚ إِنَّ الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ۚ إِنَّ اللَّهَ  
 عَلِيمٌ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾ وَمَا كَانَ هَذَا الْقُرْآنُ أَنْ يُفْتَرَى  
 مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ  
 الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٣٧﴾ أَمْ يَقُولُونَ  
 افْتَرَاهُ ۚ قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِثْلِهِ وَادْعُوا مَنْ اسْتَطَعْتُمْ مِنْ  
 دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾ بَلْ كَذَّبُوا بِمَا لَمْ  
 يُحِيطُوا بِعِلْمِهِ وَلَمَّا يَأْتِهِمْ تَأْوِيلُهُ ۚ كَذَلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ  
 مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَنِيبَةُ الظَّالِمِينَ ﴿٣٩﴾  
 وَمِنْهُمْ مَنْ يُؤْمِنُ بِهِ وَمِنْهُمْ مَنْ لَا يُؤْمِنُ بِهِ ۚ وَرَبُّكَ  
 أَعْلَمُ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿٤٠﴾ وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلٍ  
 وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ ۚ أَنْتُمْ بَرِيءُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِمَّا  
 تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾

قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَبْدُوا  
 الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ۚ قُلِ اللَّهُ  
 يَبْدُوا الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ ۚ فَأَنْتُمْ تُؤْفَكُونَ ﴿٣٤﴾  
 قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَهْدِي إِلَى  
 الْحَقِّ ۚ قُلِ اللَّهُ يَهْدِي لِلْحَقِّ ۚ  
 أَفَمَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ أَحَقُّ أَنْ يُتَّبَعَ  
 أَمْ لَا يَهْدِي إِلَّا أَنْ يَهْدِي ۚ فَمَا  
 لَكُمُ كَيْفَ تَحْكُمُونَ ﴿٣٥﴾ وَمَا  
 يَتَّبِعُ أَكْثَرُهُمْ إِلَّا ظَنًّا ۚ إِنَّ  
 الظَّنَّ لَا يُغْنِي مِنَ الْحَقِّ شَيْئًا ۚ إِنَّ  
 اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾

34. "Sema: Je! Yupo katika miungu yenu ya ushirikina aliyeanzisha kuumba viumbe, na kisha akavi rejesha? Huwaje, basi mkadanganywa?"

35. "Sema: Je! Yupo katika miungu yenu ya ushirikina anaongoa kuendea Haki?

Sema: Mwenyezi Mungu Anaongoa kuendea haki. Basi, je anayestahiki kufuatwa ni yule Mwenye Kuongoa kwendea Haki au asiyeongoa ila aongozwe yeye? Basi nyinyi mna nini? Mnahukumu namna gani?"

36. "Na wengi wao hawaifuati ila dhana tu. Na dhana haifai kitu mbele ya haki. Hakika Mwenyezi Mungu Anajua yote wanayoyatenda".

Hii ni kuwakosoa madai yao katika waliyomshirikisha Allah تعالى na vingine na wakayaabudu masanamu na washindani.

قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَبْدُوا أَلْحَقَ نُمْ يُعِيدُهُ<sup>٤</sup>

**“Sema: Je! Yupo katika miungu yenu ya ushirikina aliyeanzisha kuumba viumbe, na kisha akavirejesha?”**

Kwamba, ni nani aliyeanzisha uumbaji wa mbingu hizi na ardhi, kisha na viumbe walio ndani yake? Na akafarakisha vilivyomo mbinguni na ardhini na kuzibadilisha mahali zilipo? Kisha (ni nani wa) kurudia hatua mbalimbali za kuumba?

قُلِ اللَّهُ

**“Sema: Mwenyezi Mungu”.** Yeye Ndiye Ayafanyaye haya.

فَأَنِّي تَوَفُّكُونَ

**“Huwaje, basi mkadanganywa?”** Maana yake: Namna gani tena mnageuzwa kutoka katika njia ya uongofu mkaelekea njia ya batili?

قُلْ هَلْ مِنْ شُرَكَائِكُمْ مَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ<sup>٥</sup>

**“Sema: Je! Yupo katika miungu yenu ya ushirikina anayeongoa kuendea Haki? Sema: Mwenyezi Mungu Anaongoa Kuendea haki”.**

Kwamba, nyinyi mnajua kwamba mnaowashirikisha hawawezi kumuongoza mpotevu. Allah تعالى Peke Yake Ndiye wa Kumuongoza aliyetatanika na mpotevu, pia Huzibadili nyoyo, kutoka katika njia ya batili kwenda katika njia ya kuongoka. Allah تعالى Ndiye ambaye hapana Mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye.

أَفَمَنْ يَهْدِي إِلَى الْحَقِّ أَحَقُّ أَنْ يُتَّبَعَ أَمْ لَا يَهْدِي إِلَّا أَنْ يَهْدِي<sup>٥</sup>

**“Basi, je anaye stahiki kufuatwa ni yule Mwenye Kuongoa kuendea Haki au asiyeongoa ila aongozwe yeye?...”**

Maana yake: Je, mtu amfuata yule anayeongoza kuuendea ukweli na akaweza kuona baada ya kuwa kipofu au ambaye haongozi kwenye chochote bali aongozwe yeye kwa sababu ya upofu na ububu wake.

Ni sawa na Allah تعالى Anavyotoa habari juu ya Ibrahim عليه السلام, Aliposema;

يَتَأْتِي لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا

**“Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyo sikia, na visivyo ona na visivyo kufaa chochote?” (19:42)**

Na kama Allah تعالى Alivyosema kuhusiana na Nabii Ibrahim عليه السلام pale Aliposema,

أَتَعْبُدُونَ مَا تَنْحِتُونَ ﴿٩٦﴾ وَاللَّهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ ﴿٩٧﴾

**“Hivyo mnaviabudu ni vitu mnavyovichonga wenyewe? Na hali Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyekuumbeni nyinyi na hivyo mnavyo vifanya!” (37:95-96)**

Pamoja na Ayah nyingine. Kauli ya Allah تعالى:

فَمَا لَكُمْ كَيْفَ تَحْكُمُونَ

**“Basi nyinyi mna nini? Mnahukumu namna gani?”**

Kipi, nini kilichokusibuni kiasi cha kuondosha akili zenu? Vipi mmeweka usawa baina ya Allah تعالى na viumbe Wake, mkawalinganisha, na mkawaweka pamoja katika ibada? Kwa nini hamkumpwekesha Allah تعالى, Mfalme, Mwenye Kuhukumu, Muongozaji kutoka katika upotevu, kwa kumuabudu Yeye Peke Yake na kumtakasia dua na kurejea Kwake tu. Kisha Allah تعالى Alibainisha kwamba, wao katika dini yao wanayoifuata hawana dalili wala ushahidi. Na hayo hayatawafaa chochote.

إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِمَا يَفْعَلُونَ

**“Hakika Mwenyezi Mungu Anajua yote wanayoyatenda”.**

Hili ni tishio na ahadi ya adhabu kali, kwani Allah تعالى Alishaeleza Atawalipa malipo timilifu.

وَمَا كَانَ هَذَا الْقُرْآنُ أَنْ يُفْتَرَىٰ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَٰكِن تَصَدِّقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ  
الَّذِينَ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠١﴾ أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ ۗ قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّثْلِهِ  
وَأَدْعُوا مَنِ اسْتَطَعْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٠٢﴾ بَلْ كَذَّبُوا بِمَا لَمْ يُحِيطُوا بِعِلْمِهِ  
وَلَمَّا يَأْتِهِمْ تَأْوِيلُهُ ۗ كَذَٰلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ ۗ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظَّالِمِينَ  
﴿١٠٣﴾ وَمِنْهُمْ مَنْ يُؤْمِنُ بِهِ ۖ وَمِنْهُمْ مَنْ لَا يُؤْمِنُ بِهِ ۗ وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿١٠٤﴾

**37. “Na haiwezekani Qur’an hii kuwa imetungwa na haitokei kwa Mwenyezi Mungu. Lakini hii inasadikisha yaliyotangulia, na ni mfafanuo wa Kitabu kisicho na shaka ndani yake, kutoka kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote”.**

**38. “Je! Ndiyo wanasema amezua? Sema: Hebu leteni surah moja mfano wake na muwaite (kukusaidideni) muwawezao, isipo kuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnasema kweli”.**

**39. “Bali wameyakanusha wasioyaelewa ilimu yake kabla hayajawajia maelezo yake. Kadhalika walio kabla yao walikanusha vile vile. Basi angalia jinsi ilivyokuwa mwisho wa madhalimu hao”.**

**40. “Na miongoni mwao wapo wanaoiamini, na miongoni mwao wapo wasioiamini. Na Mola wako Mlezi Anawajua vyema mafisadi”.**

### **Qur’an Kweli ni Maneno ya Allah تعالی na Kubainisha Muujiza Wake.**

Haya ni maelezo ya muujiza wa Qur’an na kwamba kiumbe hawezi kuleta mithili yake japo kwa Surah kumi za mfano wake, kwa sababu, ufasaha wake, umbuji, usahihi, utamu na ukusanyaji wake pamoja na maana nyingi zenye manufaa duniani na Akhera, haiwi, bali kutoka kwa Allah تعالی Ambaye hapana cha kushabihiana Naye katika Dhati Yake, Sifa, Matendo wala Kauli. Mazungumzo Yake Hayafanani na ya viumbe. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

وَمَا كَانَ هَذَا الْقُرْآنُ أَنْ يُفْتَرَىٰ مِنْ دُونِ اللَّهِ

**“Na haiwezekani Qur’an hii kuwa imetungwa na haitoki kwa Mwenyezi Mungu”.**

Maana yake: Qur’an ya namna hii haiwi bali ni kutoka kwa Allah تعالی, wala maneno yake hayalandani na maneno ya viumbe.

وَلَيْكِن تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ

**“Lakini hii inasadikisha yaliyotangulia”.**

Katika vitabu vilivyotangulia, kinavithibitisha na kuyabainisha yaliyogeuzwa, kupotoshwa na kubadilishwa. Kauli ya Allah تعالی;

وَتَفْصِيلَ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**“...na ni mfafanuo wa Kitabu kisicho na shaka ndani yake, kutoka kwa Mola Mlezi wa viumbe vyote”.**

Kwa maana: Na ubainishaji wa hukumu mbali mbali, uhalali na uharamu. Ubainifu kamilifu, wa kutosha, wa kweli, na usio na mashaka ndani yake, utokao kwa Allah تعالى, Mola wa viumbe wote. Kauli ya Allah تعالى;

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِثْلِهِ وَادْعُوا مَنِ اسْتَلَطَعْتُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ كُنْتُمْ

صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾

**“Je! Ndiyo wanasema amezua? Sema: Hebu leteni surah moja mfano wake na muwaite (kukusaidieni) muwawezao, isipokuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnasema kweli”.**

Ikiwa mnadai, mnabisha na mnakuwa na mashaka kwamba hii Qur'an inatoka kwa Allah تعالى. Pia mliongopa na mkatukana kwamba inatoka kwa Muhammad ﷺ, ambaye ni kiumbe sawa na nyinyi, na madhali ameileta (kama mnavyodai) hii Qur'an, basi nyinyi mlete Surah moja mfano wake, yaani katika jinsi ya Qur'an hii. Na kwa hilo, mumuombe yeyote msaada, iwe ni katika watu au majini. Hii ni hatua ya tatu katika kuwapa hoja. Allah تعالى Aliwapa swali na kuwataka ikiwa walikuwa wakweli katika madai yao kwamba ilitoka kwa Muhammad ﷺ basi walete ya kifanani cha hicho alichokileta Yeye Peke Yake. Pia wamuombe yeyote awasaidie. Allah تعالى Alieleza kuwa wao hawaliwezi hilo, wala hawana njia ya kulifanya hilo. Allah تعالى Alisema katika Aya nyingine;

قُلْ لِيْنِ اجْتَمَعَتِ الْاِنْسُ وَالْجِنُّ عَلٰى اَنْ يَأْتُوْا بِمِثْلِ هٰذَا الْقُرْاٰنِ لَا يَأْتُوْنَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ

كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظٰهِيْرًا ﴿٣٩﴾

**“Sema: Wangelikusanyika watu na majini ili walete mfano wa hii Qur'ani basi hawaleti mfano wake, hata wakisaidiana wao kwa wao”. (17:88)**

Kisha Akawapunguzia hadi Surah kumi, akasema katika Surat Hud.

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَاهُ قُلْ فَأْتُوا بِعَشْرِ سُوْرٍ مِثْلِهِ مُفْتَرِيْنَ وَادْعُوا مَنِ اسْتَلَطَعْتُمْ مِنْ دُونِ

اللّٰهِ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِيْنَ ﴿٤٠﴾

**“Au wanasema: Ameizua? Sema: Basi leteni Surah kumi zilizo zuliwa mfano wa hii, na waiteni muwawezao badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli”. (11:13)**

Halafu Alishuka zaidi hadi Surah moja mfano wake, Akasema katika Surah hii;

أَمْ يَقُولُونَ افْتَرَيْنَاهُ قُلْ فَأْتُوا بِسُورَةٍ مِّثْلِهِ وَادْعُوا مَنِ اسْتَشْتَعْتُمْ مِّن دُونِ اللَّهِ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٧﴾

**“Je! Ndiyo wanasema ameizua? Sema: Hebu leteni surah moja mfano wake na muwaite (kukusaidieni) muwawezao, isipokuwa Mwenyezi Mungu, ikiwa nyinyi mnasema kweli”. (10:38)**

Kadhhalika katika *Surat Al-Baqarah*, nayo iliteremshwa Madinah, Aliwapa changamoto na Akaeleza kuwa wao hawataweza hilo abadani.

فَإِن لَّمْ تَفْعَلُوا وَلَٰن تَفْعَلُوا فَاتَّقُوا النَّارَ

**“Na mkitofanya – na wala hamtofanya kamwe – basi uogopeni moto...”. (2:24)**

Hapa ieleweke kuwa umbuji ulikuwa ni katika sifa za Waarabu. Mashairi yao na *Al-Mu’allaqat* zao– mkusanyiko wa mashairi ya zamani ya kiarabu yaliyokuwa na umbuji zaidi – yalichukulika ndio yaliyokuwa bora zaidi katika sanaa ya uandishi ambao waliyatundika katika Ka’aba. Hata hivyo, Allah تعالی Aliwapelekea kitu ambacho walishindwa kukikabili (kwa kukipinga). Kwa sababu hii, wale walioamini miongoni mwao ilitokana na kile kilichofikishwa na maneno hayo, utamu, usanifu, ufaidishaji na ufundi. Wakaweza kuijua na kuifahamu, kuifuata na wenye kuinyenyekea.

Ni kama wachawi walivyotambua katika fani zao kuwa alichokifanya Musa عليه السلام hakitokei isipokuwa kwa kufanywa na mwenye kusaidiwa na kutumwa na Allah تعالی, na kwamba mwanadamu haliwezi, isipokuwa kwa idhini toka kwa Allah تعالی. Kadhhalika, ‘Isa عليه السلام alitumwa katika zama za Maulamaa wa tiba na waponyaji maradhi. Akawa Anaponyesha wenye ukoma na mbalanga na kuwahuisha wafu kwa ruhusa ya Allah تعالی. Mambo kama haya, hayakuwezekana kuponywa kwa tiba na dawa. Wakatambua baadhi yao kwamba yeye alikuwa mja wa Allah تعالی na Mtume Wake. Kwa mnasaba huu, ilikuja Hadithi katika *Sahih* Mbili kwamba Mtume ﷺ alisema,

«مَا مِنْ نَبِيٍّ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ إِلَّا وَقَدْ أُوْتِيَ مِنَ الْآيَاتِ مَا آمَنَ عَلَىٰ مِنْهُ الْبَشَرُ، وَإِنَّمَا كَانَ الَّذِي أُوتِيَهُ وَحْيًا أَوْحَاهُ اللَّهُ إِلَيْهِ فَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَكْثَرَهُمْ تَابِعًا»

*“Hakukuwepo Nabii yeyote katika Manabii, bali alipatiwa ishara ambazo watu walimuamini kupitia hizo, na miongoni mwa nilizopatiwa mimi ni Wahyi Alionifunulia Allah, hivyo nataraji kwamba nitakuwa na wafuasi wengi kuliko wao”.<sup>1</sup>*

Kauli ya Allah تعالى:

بَلْ كَذَّبُوا بِمَا لَمْ يُحِيطُوا بِعِلْمِهِ وَلَمَّا يَأْتِهِمْ تَأْوِيلُهُ<sup>ع</sup>

***“Bali wameyakanusha wasioyaelewa ilimu yake kabla hayajawajia maelezo yake”.***

Anasema, bali hao waliikadhibisha Qur’an, hawakuifahamu wala kuitambua.

وَلَمَّا يَأْتِهِمْ تَأْوِيلُهُ<sup>ع</sup>

***“...kabla hayajawajia maelezo yake”.***

Kwa maana: Hawakuupata uongofu na dini iliyomo ndani yake, wakati wa kuikadhibisha kwao, kwa ujahili na usafihi.

كَذَلِكَ كَذَّبَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ<sup>ط</sup>

***“Kadhalika walio kabla yao walikanusha vile vile”.*** Yaani umma zilizopita.

فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الظَّالِمِينَ

***“Basi angalia jinsi ilivyokuwa mwisho wa madhalimu hao”.***

Kwa maana: Angalia namna Tulivyowahilikisha kutokana na wao kuwakadhibisha Mitume Wetu kwa dhuluma, ujeuri, kufuru, ukaidi na ujahili. Basi, enyi wakadhibishaji! Tahadharini kukupateni yaliyowasibu wao. Kauli Yake;

وَمِنْهُمْ مَّنْ يُؤْمِنُ بِهِ

***“Na miongoni mwao wapo wanaoiamini”.***

Kwa maana: Na katika hao ambao umetumwa kwao, ewe Muhammad ﷺ, wapo watakaoiamini Qur’an hii, watakaofuata na kunufaika na uliyotumwa nayo.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 8:619.

وَمِنْهُمْ مَّنْ لَا يُؤْمِنُ بِهِمْ

*“...na miongoni mwao wapo wasioiamini”.*

Na wanakufa katika hali hiyo na kufufuliwa hivyo.

وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِالْمُفْسِدِينَ

*“Na Mola wako Mlezi Anawajua vyema mafisadi”.*

Maana yake: Na Yeye (Allah تعالى) ni Mjuzi zaidi juu ya Anayestahiki Hidaya, basi Humhidi na Anayestahiki kuachwa apotee, basi humuacha hivyo. Na Yeye ni Muadilifu Asiyedhulumu, bali Humpa kila mmoja anachostahiki. Ni Mtukuka, Mkuu, hapana mola wa haki kuabudiwa isipokuwa Yeye.





وَمِنْهُمْ مَّن يَنْظُرُ إِلَيْكَ ۚ أَفَأَنْتَ هَدَىٰ الْعَمَىٰ وَلَوْ كَانُوا  
 لَا يُبْصِرُونَ ﴿٤١﴾ إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْئًا وَلَكِنَّ  
 النَّاسَ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤٢﴾ وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ كَأَن لَّمْ  
 يَلْبَثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّنَ النَّهَارِ يَتَعَارَفُونَ بَيْنَهُمْ ۗ قَدْ خَسِرَ  
 الَّذِينَ كَذَّبُوا بِلِقَاءِ اللَّهِ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿٤٣﴾ وَإِنَّمَا  
 نُرِيدُكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَقَّعُكَ فَإِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ  
 ثُمَّ اللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا يَفْعَلُونَ ﴿٤٤﴾ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولٌ  
 ۗ فَإِذَا جَاءَ رَسُولُهُمْ قُضِيَ بَيْنَهُمْ بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ  
 ﴿٤٥﴾ وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٦﴾  
 قُلْ لَا أَمْلِكُ لِنَفْسِي ضَرًّا وَلَا نَفْعًا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ ۗ لِكُلِّ  
 أُمَّةٍ أَجَلٌ ۗ إِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ فَلَا يَسْتَعْجِرُونَ سَاعَةً ۗ وَلَا  
 يَسْتَفْتِمُونَ ﴿٤٧﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِن آتَاكُمْ عَذَابُهُ بَيِّنَاتًا أَوْ  
 هَارًا مَّاذَا يَسْتَعْجِلُ مِنْهُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٤٨﴾ أَتُمْ إِذَا مَا وَقَعَ  
 ءَامَنْتُمْ بِهِ ۗ ءَأَلْعَنَ وَقَدْ كُنْتُمْ بِهِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٤٩﴾ ثُمَّ قِيلَ  
 لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ ۗ هَلْ تُحْزَنُونَ إِلَّا بِمَا كُنْتُمْ  
 تَكْسِبُونَ ﴿٥٠﴾

وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ  
 عَمَلُكُمْ ۗ أَنتُمْ بَرِيءُونَ مِمَّا أَعْمَلُ  
 وَأَنَا بَرِيءٌ مِّمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾ وَمِنْهُمْ  
 مَّن يَسْتَمِعُونَ إِلَيْكَ ۚ أَفَأَنْتَ تُسْمِعُ  
 الْأَصْمُمَ وَلَوْ كَانُوا لَا يَعْقِلُونَ ﴿٤٢﴾  
 وَمِنْهُمْ مَّن يَنْظُرُ إِلَيْكَ ۚ أَفَأَنْتَ  
 تَهْدِي الْعَمَىٰ وَلَوْ كَانُوا لَا  
 يُبْصِرُونَ ﴿٤٣﴾ إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ  
 النَّاسَ شَيْئًا وَلَكِنَّ النَّاسَ أَنفُسَهُمْ  
 يَظْلِمُونَ ﴿٤٤﴾

41. "Na wakikukanusha wewe sema: Mimi nina a'mali yangu, na nyinyi mna a'mali yenu. Nyinyi hamna jukumu kwa niyatendayo, wala mimi sina jukumu kwa myatendayo".

42. "Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza. Je,

wewe unaweza kuwafanya viziwi wasikae ijapokuwa hawafahamu?"

43. "Na wapo miongoni mwao wanaokutazama. Je, wewe utawaongo vipofu ingawa hawaoni".

44. "Hakika Mwenyezi Mungu Hawadhulumu watu kitu chochote; lakini watu wenyewe wanajidhulumu nafsi zao".

**Amri ya Kujitenga Dhidi ya Washirikina.**

Allah تعالى Anamuambia Mtume ﷺ: Na hao Washirikina wakikukadhibisha, basi jitenge mbali nao na amali zao;

فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ

**“...sema: Mimi nina amali yangu, na nyinyi mna amali yenu”.**

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قُلْ يَا أَيُّهَا الْكَافِرُونَ ﴿١﴾ لَا أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٢﴾

**“Sema: Enyi makafiri! Siabudu mnacho abudu”. (109:1-2)**

Mpaka mwisho wake. Ibrahim Al-Khalil عليه السلام na wafuasi wake waliwaambia Washirikina katika kaumu yake;

إِنَّا بَرَاءُؤُا مِنْكُمْ وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ

**“Hakika sisi tumejitenga nanyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Mwenyezi Mungu”. (60:4)**

Kauli ya Allah تعالى:

وَمِنْهُمْ مَّن يَسْتَمِعُونَ إِلَيْكَ

**“Na wapo miongoni mwao wanaokusikiliza”.**

Maana: Wanasikiliza mazungumzo yako mazuri na Qur'an tukufu na Hadithi zilizo sahihi na fasaha, zenye kunufaisha nyoyo, dini na viwiliwili. Katika haya kuna manufaa makubwa ya kutosha. Lakini hilo la kuhidi haliko juu yako wala kwao, kwani wewe huna uwezo wa kumsikilizisha kiziwi, pia huwezi kuwaongoa hao isipokuwa Allah تعالى Akipenda.

وَمِنْهُمْ مَّن يَنْظُرُ إِلَيْكَ

**“Na wapo miongoni mwao wanaokutazama”.**

Wao, wanakutazama wewe na katika Aliyokupa Allah تعالى, kama vile heshima, hadhi na tabia njema, ni dalili dhahiri juu ya Utume wake kwa wenye uoni na uerevu. Hao wanaangalia kama waangaliavyo wengine, wala hakuna chochote katika Hiday ambacho kinamfikia kama inavyokuwa kwa wengine. Waumini

ndio wanaokutazama kwa jicho la taadhima, ilhali hao makafiri wanakuangalia kwa jicho la dharau.

وَإِذَا رَأَوْكَ إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُؤًا

**“Na wanapokuona hawakuchukulii ila ni mzaha tu”. (25:41)**

Kisha Allah تعالى Anaeleza kwamba Hadhulumu chochote kwa yeyote. Humhidi wa Kumhidi, Kumpa uoni kipofu, Kuyafumbua macho ya aliyekosa, pia masikio ya kiziwi na nyoyo zilizoghafilika. Pia Huwapoteza wengine mbali na Imani. Yeye ni Hakimu Mwenye mamlaka yote kadiri Atakavyo katika Miliki Yake. Haulizwi juu ya Akifanyacho, bali wao ni wenye kuulizwa. Hayo ni kwa sababu ya Elimu Yake, Hekima na Uadilifu. Na kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Alisema;

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ النَّاسَ شَيْئًا وَلَكِنَّ النَّاسَ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿٤١﴾

**“Hakika Mwenyezi Mungu Hawadhulumu watu chochote; lakini watu wenyewe wanajidhulumu nafsi zao”.**

Kuna Hadithi ya Abu Dharr رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ anayoisimulia kutoka kwa Mola Wake;

«يَا عِبَادِي! إِنِّي حَرَمْتُ الظُّلْمَ عَلَى نَفْسِي وَجَعَلْتُهُ بَيْنَكُمْ مُحَرَّمًا فَلَا تَظَالَمُوا»

**“Enyi waja Wangu! Nimejiharamishia dhuluma Mwenyewe na Nimeiharamisha baina yenu, basi msidhulumiane.”**

Mpaka aliposema mwishoni mwa Hadithi:

يَا عِبَادِي! إِنَّمَا هِيَ أَغْمَالُكُمْ أُحْصِيهَا لَكُمْ، ثُمَّ أُوَفِّيكُمْ بِآثَارِهَا، فَمَنْ وَجَدَ خَيْرًا فَلْيُحْمَدِ اللَّهَ، وَمَنْ وَجَدَ غَيْرَ ذَلِكَ فَلَا يَلُومَنَّ إِلَّا نَفْسَهُ»

**“Enyi waja Wangu! Kwa hakika! Amali zenu huwa Nazihesabu, kisha Nakulipeni kwazo. Atakayepata kheri (huko Akhera) basi amshukuru Allah, na atakayepata kilicho ghairi ya hivyo, basi asimlaumu yeyote, isipokuwa nafsi yake”.**

Ukamilifu wake umenukuliwa na Muslim<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Muslim 4:1994.

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ كَأَن لَّمْ يَلْبَثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّنَ النَّهَارِ يَتَعَارَفُونَ بَيْنَهُمْ قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا  
بِلِقَاءِ اللَّهِ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ ﴿٤١﴾

**45. “Na siku Atakapowakusanya, itakuwa kama kwamba hawakukaa ila saa moja tu ya mchana! Watatambuana. Hakika wamekhasirika waliokanusha kukutana na Mwenyezi Mungu, wala hawakuwa wenye kuongoka”.**

**Hisia Juu ya Ufupi wa Maisha ya Kidunia Katika Siku ya Kufufuliwa.**

Allah تعالی Anawakumbusha watu juu ya kusimama kwa kiyama na kufufuliwa kwao kutoka makaburini mwao kwenda katika mkusanyiko wa Siku ya Hukumu. Allah تعالی Anasema;

وَيَوْمَ نَحْشُرُهُمْ

**“Na siku Atakapowakusanya”.**

Ni sawa na Kauli Yake nyingine;

كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَ مَا يُوعَدُونَ لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا سَاعَةً مِّنَ نَّهَارٍ

**“Siku watakayoyaona waliyoahidiwa itakuwa kama kwamba hawakukaa ulimwenguni ila saa moja ya mchana...” (46:35) Na Kauli Yake Allah تعالی,**

كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحًى ﴿٤٢﴾

**“Ni kama kwamba wao siku watapoiona (hiyo Saa) hawakuwa ila jioni moja tu, au mchana wake.” (79:46) Na Kauli Yake Allah تعالی,**

يَوْمَ يَنْفَخُ فِي الصُّورِ وَنَحْشُرُ الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ زُرْقًا ﴿٤٣﴾ يَتَخَفَتُونَ بَيْنَهُمْ إِنْ لَبِثْتُمْ إِلَّا عَشْرًا ﴿٤٤﴾ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ إِذْ يَقُولُ أَمْثَلُهُمْ طَرِيقَةً إِنْ لَبِثْتُمْ إِلَّا يَوْمًا ﴿٤٥﴾

**“Siku litakapopolizwa baragumu, na Tutawakusanya wakhalifu Siku hiyo, hali macho yao ya kibuluu. Watanong’onezana wao kwa wao: Hamkukaa ila siku kumi tu. Sisi Tunajua zaidi watakayoyasema, atakaposema mbora wao katika mwendo: Nyinyi hamkukaa ila siku moja tu.” (20:102-104) Na Allah تعالی Amesema,**

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُقْسِمُ الْمُجْرِمُونَ مَا لَبِثُوا غَيْرَ سَاعَةٍ ۗ

**“Na siku itaposimama Saa wakosefu wataapa kwamba hawakukaa duniani ila saa moja tu”. (30:55)**

Na hii ni dalili juu ya ufupi wa maisha ya duniani huko Akhera. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

قَالَ كَمْ لَبِثْتُمْ فِي الْأَرْضِ عَدَدَ سِنِينَ ﴿٣٠﴾  
 قَالُوا لَبِثْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ فَسَلِّ الْعَادِينَ ﴿٣١﴾  
 قُلْ إِنْ لَبِثْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ۗ لَوْ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٣٢﴾

**“Atasema: Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hesabu ya miaka? Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wanaoweka hesabu. Atasema: Nyinyi hamkukaa huko duniani ila kidogo, laiti ingelikuwa mnajua”. (23:112-114)**

Kauli ya Allah تعالى: يَتَعَارَفُونَ بَيْنَهُمْ ۗ

**“Watatambuana”**. Kwa maana: Na watoto watawajua mababa, na ndugu watajuana wao kwa wao, kama walivyokuwa duniani, lakini kila mmoja atajishughulisha na nafsi yake tu.

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ

**“Basi litapopulizwa baragumu hapo hautakuwepo ujamaa baina yao siku hiyo...”. (23:101)**

Allah تعالى Alisema pia: وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ﴿٧٠﴾

**“Wala jamaa hatamuuliza jamaa yake”. (70:10)**

Kauli ya Allah تعالى:

قَدْ خَسِرَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِلِقَاءِ اللَّهِ وَمَا كَانُوا مُهْتَدِينَ

**“Hakika wamekhasirika waliokanusha kukutana na Mwenyezi Mungu, wala hawakuwa wenye kuongoka...”**

Sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَيَلَّ يَوْمَئِذٍ لِلْمُكَذِّبِينَ ﴿٧٧﴾

**“Ole wao, siku hiyo hao wanaokanusha!” (77:15)**

Kwa sababu wao wamejitia khasara wao wenyewe na ahali zao Siku ya Kiyama. Kwa kweli, hiyo ni khasara bayana, wala hakuna hasara kubwa zaidi aipatayo mtu kuliko kule kufarakana na wapenzi wake katika Siku ya Majuto.

وَأَمَّا نُرْيِكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ أَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ فَإِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ اللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا  
يَفْعَلُونَ ﴿٤١﴾ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولٌ ۖ فَإِذَا جَاءَ رَسُولُهُمْ قُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا  
يُظْلَمُونَ ﴿٤٢﴾

**46. “Na vyovyote vile, Tukikuonesha baadhi ya Tunayowaahidi, au Tukakufisha kabla yake, marejeo yao ni Kwetu. Kisha Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa wanayo yafanya”.**

**47. “Na kila umma una Mtume. Alipowajia Mtume wao walihukumiwa baina yao kwa uadilifu, wala hawakudhulumiwa”.**

**Wahalifu Watalipizwa Kisasi, Ima Humu Duniani Ama Huko Akhera.**

Allah تعالیٰ Anamuambia Mtume ﷻ:

وَأَمَّا نُرْيِكَ بَعْضَ الَّذِي نَعِدُهُمْ

**“Na vyovyote vile, Tukikuonesha baadhi ya Tunayowaahidi”.** Maana: Tutawalipiza kisasi katika kipindi cha uhai wako ili jicho lako litulie.

أَوْ نَتَوَفَّيَنَّكَ فَإِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ

**“...au Tukakufisha kabla yake, marejeo yao ni Kwetu”.** Maana: Muelekeo na mwisho wao. Allah تعالیٰ ni Shahidi juu ya vitendo vyao baada yako. Kauli ya Allah تعالیٰ:

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولٌ ۖ فَإِذَا جَاءَ رَسُولُهُمْ

**“Na kila umma una Mtume. Alipowajia Mtume wao”.**

Mujahid alisema: “Hii itakuwa ni katika Siku ya Kiyama”<sup>1</sup>.

قُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ

**“...walihukumiwa baina yao kwa uadilifu”.**

<sup>1</sup> At-Tabari 15:99.

Na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا

**“Na ardhi itang’ara kwa Nuru ya Mola wake Mlezi”. (39:69)**

Kila ummah utaletwa mbele ya Allah تعالى pamoja na Kitabu cha Amali zao, ambapo Mitume wao nao watakuwemo. Kheri na shari zitakuwa zimeandikwa kama ushahidi juu yao. Malaika walenzi pia, nao watakuwa mashahidi. Ni umma mmoja baada ya mwingine. Umma huu mtukufu nao pia, ingawa umekuwa ni wa mwisho humu duniani, utakuwa wa awali kuhojiwa na kuhukumiwa Siku ya Kiyama. Ni sawa na ilivyokuja katika *Sahih* Mbili kuwa Mtume ﷺ alisema;

«نَحْنُ الْأَخِرُونَ السَّابِقُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، الْمُنْضِيُّ لَهُمْ قَبْلَ الْخَلَائِقِ»

*“Sisi ni umma wa mwisho, ni wa kwanza katika Siku ya Kiyama. Tutahukumiwa kabla ya viumbe wengine”<sup>1</sup>.*

Kwa hivyo, umma wake umepata heshima ya kutangulia kwa sababu ya hadhi ya Mtume ﷺ, daima mpaka katika Siku ya Kiyama.

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٤٨﴾ قُلْ لَا أَمْلِكُ لِنَفْسِي ضَرْبًا وَلَا نَفْعًا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ لِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ ۖ إِذَا جَاءَ أَجْلُهُمْ فَلَا يَسْتَفْخِرُونَ سَاعَةً ۖ وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ ﴿٤٩﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَاكُمْ عَذَابُهُ بَيْنًا أَوْ نَهَارًا مَّاذَا يَسْتَعْجِلُ مِنْهُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٥٠﴾ أُنزِلَ إِذَا مَا وَقَعَ ءَامَنُكُمْ بِمِءِءِ الْفَنِّ وَقَدْ كُنْتُمْ بِمِءِءِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٥١﴾ ثُمَّ قِيلَ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ هَلْ تُجْزَوْنَ إِلَّا بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٥٢﴾

**48. “Na wanasema: Lini ahadi hii, ikiwa mnasema kweli?”**

**49. “Sema: Sijimiliki nafsi yangu shari wala kheri ila Apendavyo Mwenyezi Mungu. Kila umma una muda wao waliowekewa. Ukifika muda wao hawakawii hata saa moja wala hawatangulii”.**

**50. Sema: Mwaonaje ikikufikieni hiyo adhabu Yake usiku au mchana, sehemu gani ya adhabu wanahimiza wakosefu?”**

<sup>1</sup> Fat’h Al-Bari 6:595 na Muslim 2:585.

**51. "Tena je! Ikishatokea mtaiamini? Je! Ndio sasa tena? Na nyinyi mlikuwa mkiihimiza."**

**52. "Kisha waliodhulumu wataambiwa: Onjeni adhabu ya kudumu. Kwani hamtalipwa isipokuwa yale mliyokuwa mkiyachuma?"**

**Juu ya Waikanushao Siku ya Kiyama Ambao Hutaka Iharakishwe na Jawabu walilopewa.**

Allah تعالی Anaeleza juu ya kufuru ya Washirikina hawa katika kutaka kwao adhabu iharakishwe, pia na kuulizia kwao wakati wake. Ufafanuzi wa hayo, ni katika yasiyo na faida yoyote. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا وَالَّذِينَ آمَنُوا مُشْفِقُونَ مِنْهَا وَيَعْلَمُونَ أَنَّهَا الْحَقُّ

**"...huhimiza hiyo Saa ifike upesi; lakini wanaoamini wanaiogopa, na wanajua kwamba hakika hiyo ni kweli." (42:18)**

Kwa maana: Ni yenye kutuka, hakuna vinginevyo. Kitatokea tu, hata kama hawajui wakati wake khasa. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alimueleza Mtume ﷺ kuwajibu, Alisema;

قُلْ لَّا أَمْلِكُ لِنَفْسِي ضَرًّا وَلَا نَفْعًا

**"Sema: Siimilikii nafsi yangu madhara wala manufaa." (10:49, 7:188)**

Sisemi, isipokuwa Alichonielimisha Yeye, wala siwezi lolote isipokuwa Alichonionesha Allah تعالی. Mimi ni mja tu, pia ni Mtume kwenu. Nimekujulisheni habari ya kuja Kiyama, wala Allah تعالی Hakunijulisha wakati wake, lakini;

لِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ

**"Kila umma una muda wao waliowekewa".**

Kwa maana: Kila kizazi kina umri uliokadiriwa. Muda wake utakapomalizika,

فَلَا يَسْتَفْخِرُونَ سَاعَةً وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ

**"Ukifika muda wao hawakawii hata saa moja wala hawatangulii."**

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:



وَلَنْ يُؤَخِّرَ اللَّهُ نَفْسًا إِذَا جَاءَ أَجْلُهَا

**“Wala Mwenyezi Mungu Hataiakhirisha nafsi yoyote inapofika ajali yake.” (63:11)**

Halafu alijulisha kwamba adhabu ya Allah تعالى itawafikia kwa ghafla. Alisema;

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَتَيْتُمْ عَذَابُهُ بَيْنًا أَوْ نَهَارًا مَاذَا يَسْتَعْجِلُ مِنْهُ الْمُجْرِمُونَ ﴿٦٣﴾ أَتُمْ إِذَا مَا وَقَعَ ءَامَنْتُمْ بِهِ ءَالْقِنَ وَقَدْ كُنْتُمْ بِهِ تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٦٤﴾

**“Sema: Mwaonaje ikikufikieni hiyo adhabu yake usiku au mchana, sehemu gani ya adhabu wanahimiza wakosefu? Tena je! Ikisha tokea mtaiamini? Je! Ndio sasa tena? Na nyinyi mlikuwa mkiihimiza.”**

Maana: Itakapowajia adhabu, watasema;

رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا

**“Mola wetu Mlezi! Tumeshiona, na tumeshasikia.” (32:12)**

Na Kauli yake Allah تعالى,

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدُّهُ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿٦٥﴾ فَلَمَّ يَكُ يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا ۗ سُنَّتَ اللَّهُ الَّتِي قَدْ خَلَتْ فِي عِبَادِهِ ۗ وَخَسِرَ هُنَالِكَ الْكَافِرُونَ ﴿٦٦﴾

**“Walipoiona Adhabu Yetu walisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa Pekee, na tunaikataa miungu tuliyokuwa tukiishirikisha Naye. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa kitu wakati ambao wamekwishaiona Adhabu Yetu. Huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu uliokuwa kwa waja Wake. Na hapo walio kufuru walikhasiri.” (40:84-85)**

ثُمَّ قِيلَ لِلَّذِينَ ظَلَمُوا ذُوقُوا عَذَابَ الْخُلْدِ

**“Kisha waliodhulumu wataambiwa: Onjeni adhabu ya kudumu.”**

Maana: Katika Siku ya Kiyama wataambiwa kwa Kuwalaumu na Kuwakaripia.

يَوْمَ يُدْعُونَ إِلَى نَارِ جَهَنَّمَ دَعَاً ﴿٣١﴾ هَذِهِ النَّارُ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿٣٢﴾ أَفَسِحْرٌ  
 هَذَا أَمْ أَنْتُمْ لَا تُبْصِرُونَ ﴿٣٣﴾ أَصَلَوْهَا فَاصْبِرُوا أَوْ لَا تَصْبِرُوا سَوَاءٌ عَلَيْكُمْ إِنَّمَا  
 تُحْزَنُونَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣٤﴾

*“Siku wataposukumwa kwenye Moto kwa msukumo wa nguvu,  
 (Waambiwe): Huu ndio ule Moto mliokuwa mkiukanusha! Je! Huu ni  
 uchawi, au hamuoni tu? Uingieni mkistahamili au msistahamili – ni  
 mamoja kwenu. Hakika mnalipwa kwa mliyo kuwa mkiyatenda”.*  
 (52:13-16)

\* \* \*

\* وَيَسْتَدْعُونَكَ أَحَقُّ هُوَ قُلْ إِي وَرَبِّي إِنَّهُ لَحَقُّ وَمَا  
 أَنتُمْ بِمُعْجِزِينَ ﴿٥٣﴾ وَلَوْ أَنَّ لِكُلِّ نَفْسٍ ظَلَمَتْ مَا فِي  
 الْأَرْضِ لَافْتَدَتْ بِهِ ۗ وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ ۗ  
 وَفُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ ۗ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٥٤﴾ أَلَا إِنَّ  
 لِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ أَلَا إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَلٰكِنَّ  
 أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٥﴾ هُوَ نُحِّي- وَيُحْيِي وَيُمِيتُ وَإِلَيْهِ  
 تُرْجَعُونَ ﴿٥٦﴾ يٰٓأَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَ تَكْمٌ مَّوْعِظَةٌ مِّن  
 رَبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِّمَا فِي الصُّدُورِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ  
 ﴿٥٧﴾ قُلْ بِفَضْلِ اللَّهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُوا هُوَ خَيْرٌ  
 مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٥٨﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ مَا أَنزَلَ اللَّهُ لَكُمْ مِّن  
 رِّزْقٍ فَجَعَلْتُمْ مِّنْهُ حَرَامًا وَحَلٰلًا قُلْ ۗ إِنَّ اللَّهَ أُذِنَ لَكُمْ أَمْرًا  
 عَلَى اللَّهِ تَفْتَرُونَ ﴿٥٩﴾ وَمَا ظَنُّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ  
 عَلَى اللَّهِ الْكَذِبِ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى  
 النَّاسِ وَلٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٦٠﴾ وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ  
 وَمَا تَتَلَوٰنَا مِنْهُ مِن قُرْءَانٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا  
 عَلَيْكُمْ شُهَدَآءَ ۗ إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ ۗ وَمَا يَعْزُبُ عَن رَّبِّكَ مِن  
 مِّثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَآءِ وَلَا أَصْغَرَ مِن  
 ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٦١﴾

\* وَيَسْتَدْعُونَكَ أَحَقُّ هُوَ قُلْ إِي  
 وَرَبِّي إِنَّهُ لَحَقُّ وَمَا أَنتُمْ  
 بِمُعْجِزِينَ ﴿٥٣﴾ وَلَوْ أَنَّ لِكُلِّ  
 نَفْسٍ ظَلَمَتْ مَا فِي الْأَرْضِ لَافْتَدَتْ  
 بِهِ ۗ وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوُا  
 الْعَذَابَ ۗ وَفُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ ۗ  
 وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٥٤﴾

53. "Na wanakuuliza: Je! Ni kweli hayo? Sema: Ehe! Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hakika hayo ni kweli, na wala nyinyi hamshindi!"

54. "Na lau kuwa kila nafsi iliyodhulumu inamiliki kila kiliomo duniani, bila ya shaka ingelitoa vyote kujikombolea. Na watakapoiona adhabu wataficha Majuto. Na patahukumiwa baina yao kwa uadilifu, nao hawatadhulumiwa".

**Kiyama ni Kweli.**

Allah تعالى Anasema; wanakutaka uwape habari.

أَحَقُّ هُوَ

**“Hakika hayo ni kweli”.** Kwa maana: Marejeo na kusimamishwa siku ya Kiyama kutoka makaburini baada ya miili kugeuka kuwa mchanga.

قُلْ إِي وَرَبِّي إِنَّهُ لَحَقٌّ وَمَا أَنْتُمْ بِمُعْجِزِينَ

**“Sema: Ehe! Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hakika hayo ni kweli, na wala nyinyi hamshindi!”**

Kwa maana: Kugeuka kwenu udongo hakumshindi Allah تعالى Kukurejesheni kama Alivyokuumbeni kutoka katika kutokuwepo, kwani;

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

**“Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kinakuwa”.** (36:82)

Ayah hii haina nyingine katika Qur’an zilizo katika mfano wake isipokuwa mbili, moja imo katika Surat Sabaa ambapo Allah تعالى Anamuamuru Mtume ﷺ aape Kwake kwa mwenye kulikanusha suala la marejeo.

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَأْتِينَا السَّاعَةُ قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتَأْتِيَنَّكُمْ

**“Na walisema waliokufuru: Haitatufikia Saa (ya Kiyama). Sema: Kwani? Hapana shaka itakufikieni”.** (34:3) Katika Surat Taghaabun:

رَعَمَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ لَنْ يُبْعَثُوا قُلْ بَلَىٰ وَرَبِّي لَتُبْعَثُنَّ ثُمَّ لَتُنَبَّؤُنَّ بِمَا عَمِلْتُمْ وَذَلِكَ عَلَىٰ

اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧﴾

**“Waliokufuru wanadai kuwa hawatafufuliwa. Sema: Kwani? Naapa kwa Mola wangu Mlezi! Hapana shaka mtafufuliwa, na kisha hapana shaka mtaambiwa mliyoyatenda. Na hayo ni mepesi kwa Mwenyezi Mungu”.** (64:7)

Kisha Allah تعالى Alitoa habari kwamba, Kiyama kitakaposimama, kafiri atatamani ajikomboe dhidi ya adhabu hiyo kwa dhahabu sawa na ujazo wa ardhi.

وَأَسْرُوا النَّدَامَةَ لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ وَقُضِيَ بَيْنَهُم بِالْقِسْطِ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٥٣﴾

**“...wataficha Majuto. Na patahukumwiwa baina yao kwa uadilifu, nao hawatadhulumiwa.”**

أَلَا إِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ أَلَا إِنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَلَكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٥٤﴾  
هُوَ يُحْيِي - وَيُمِيتُ وَإِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٥٥﴾

**55. “Hapana shaka, Jueni kuwa hakika vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi ni vya Mwenyezi Mungu. Jueni kuwa hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya haki. Lakini wengi wao hawajui”.**

**56. “Yeye Ndiye Anayefufua na Anayefisha. Na Kwake mtare-jeshwa.”**

Allah تعالى Yeye Ndiye Mmiliki wa mbingu na ardhi na kwamba Ahadi Yake ni ya kweli, bila shaka itatimia! Pia Yeye Ndiye Anayehuisa na Kufisha na Kwake Yeye ndio marejeo yenu, na kwamba Yeye ni Mwenye Nguvu na Muweza wa hayo, Mwenye Ujuzi wa kila kitu kuhusu Viumbe, kuhusu kilichoharibika katika kiwiliwili na kilichopotea katika maeneo ya ardhini, baharini na majangwani.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُمْ مَوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِّمَا فِي الصُّدُورِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾ قُلْ بِفَضْلِ اللَّهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُوا هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿٥٨﴾

**57. “Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na poza kuponyesha yaliyomo vifuani, na uwongofu na rehema kwa Waumini.”**

**58. “Sema: Kwa Fadhila ya Mwenyezi Mungu na Rehema Yake! Basi na wafurahi kwa hayo. Haya ni bora kuliko hayo wanayo-yakusanya.”**

**Qur’an ni Mawaidha, Ponyo, Rehema na Mwongozo**

Katika kuipa nguvu Qur’an Tukufu Aliyoiteremsha kwa Mtume ﷺ, Allah تعالى Anawaambia viumbe Wake:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُمْ مَوْعِظَةٌ مِّن رَّبِّكُمْ

**“Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi.”**

Ni yenye kuyakemea maovu.

وَشِفَاءٍ لِّمَا فِي الصُّدُورِ

“...na poza kuponyesha yaliyomo vifuani”. Dhidi ya utata na mashaka, nako ni kuondoa uchafu, na shirki zilizomo ndani ya nyoyo.

وَهُدًى وَرَحْمَةً

“...na uwongofu na rehema”. Kwa maana: Hidaya na Rehema kutoka kwa Allah تعالى. Kwa hakika! Hilo ni kwa Waumini, wasadikishaji wenye yakini na yaliyomo ndani yake. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَنَزَّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿١٧﴾

“Na Tunateremsha katika Qur’an yaliyo ni matibabu na Rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaliamu ila khasara.” (17:82) Na Kauli Yake Allah تعالى,

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً

“Sema: Qur’an hii ni uwongofu na poza”. (41:44) Kauli ya Allah تعالى;

قُلْ بِفَضْلِ اللَّهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُوا

“Sema: Kwa fadhila ya Mwenyezi Mungu na Rehema Yake! Basi na wafurahi kwa hayo.”

Kwa maana: Waifurahie Hidaya na Dini ya kweli iliyowajia kutoka kwa Allah تعالى, kwani hayo ndio mazuri zaidi katika vyenye kufurahiwa.

هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ

“Haya ni bora kuliko hayo wanayoyakusanya”. Kwa maana: Starehe ya dunia na vilivyomo na anasa zake ni zenye kuisha na kuondoka, bila shaka.

قُلْ أَرَأَيْتُمْ مَا أَنزَلَ اللَّهُ لَكُمْ مِنَ الرَّزْقِ فَجَعَلْتُمْ مِنْهُ حَرَامًا وَحَلَلًا قُلْ إِنَّ اللَّهَ  
أَذِنَ لَكُمْ ۗ أَمَّا عَلَى اللَّهِ تَفَتَّرُونَ ﴿٥٩﴾ وَمَا ظَنُّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ  
الْكُذِبَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٦٠﴾

59. “Sema: Je! Mwaonaje zile riziki Alizokuteremshieni Mwenyezi

***Mungu nanyi mkafanya katika hizo nyingine haramu na nyingine halali. Sema: Je! Mwenyezi Mungu Amekuruhusuni au mnamzulia Mwenyezi Mungu tu?"***

***60. "Na nini dhana ya wanaomzulia Mwenyezi Mungu kwa Siku ya Kiyama? Hakika Mwenyezi Mungu Ana fadhila juu ya watu, lakini wengi wao hawashukuru".***

**Allah تعالیٰ Pekee Ndiye Mwenye Mamlaka ya Kuhalalisha Kitu au Kuharamisha Kitu na Wale Aliowapa Uwezo Kufanya Hivyo.**

Ibn 'Abbas, Mujahid, Adh-Dhahhak, Qatadah, 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam na wengine رضي الله عنهم walisema, "Ayah hii iliteremshwa kuwakanushia Washirikina kwa tabia yao ya kujihalalishia na kujiharamishia. Kama vile Bahira<sup>1</sup>, Saibah<sup>2</sup> na Wasilah<sup>3</sup>".

Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ:

وَجَعَلُوا لِلَّهِ مِمَّا ذَرَأَ مِنَ الْحَرْثِ وَالْأَنْعَامِ نَصِيبًا

***"Na wamemuwekea sehemu Mwenyezi Mungu katika mimea na wanyama Alioumba". (6:136)***

Imamu Ahmad alisimulia kuwa Malik bin An-Nadhwilah alisema: "Nilimjia Mtume ﷺ nikiwa nimevaa nguo chafu. Akaniuliza;

«مَلَّ لَكَ مَالٌ؟»

"Una mali?" Nikasema, "Ndiyo" Akaniuliza;

«مِنْ أَيِّ الْمَالِ؟»

"Mali ya aina gani?" Nikajibu:

"Kila aina ya mali; ngamia, watumwa, farasi na kondoo". Akasema;

<sup>1</sup> Ngamia jike ambaye maziwa yake yaliachwa kwa ajili ya masanamu na hapana aliyeruhusiwa kumkamua.

<sup>2</sup> Ngamia jike aliyeachwa huru kuchunga kwa ajili ya miungu yao batili, na hakuruhusiwa kubebeshwa kitu.

<sup>3</sup> Ngamia jike aliyeachiliwa kwa ajili ya miungu kwa sababu amezaa ngamia jike katika uzao wake wa awali na akafanya hivyo katika uzao wake wa pili. (At-Tabari 15:112-113)

«إِذَا آتَاكَ اللَّهُ مَالًا فَلْيَرَّ عَلَيْكَ»

“Allah Akikupatia mali basi ionekane kwako”. Kisha Akasema;

«هَلْ تَنْتَجُ إِلَيْكَ صِحَاحًا آذَانُهَا، فَتَعْمِدَ إِلَى مُوسَى فَتَقْطَعَ آذَانَهَا، فَتَقُولَ: هَذِهِ بُحْرٌ. وَتَشُقُّ جُلُودَهَا وَتَقُولَ: هَذِهِ صُرْمٌ. وَتَحْرِمَهَا عَلَيْكَ وَعَلَى أَهْلِكَ؟»

“Je, ngamia wako Hakuzaliwa na masikio mazima? Unachukua kijembe na kuyakata masikio, Halafu unasema: “Hii ni Buhur”. Unaichana ngozi yake na kusema: “Hii ni Swaum” Na unaiharamisha kwako na kwa familia yako?” Nikasema; “Ndiyo”. Akasema;

«فَإِنَّ مَا آتَاكَ اللَّهُ لَكَ جَلٌّ، سَاعِدُ اللَّهِ أَشَدُّ مِنْ سَاعِدِكَ، وَمُوسَى اللَّهُ أَحَدٌ مِنْ مُوسَاكَ»

“Alichokupa Allah, ni halali kwako. Mkono wa Allah Una nguvu kuliko wa kwako. Na wembe wa Allah ni mkali kuliko wako”<sup>1</sup>.

Akaitaja hadithi nzima. Hadithi hii ni *Jayyid*, na ina isnadi yenye nguvu.

Allah تعالی Aliwakanusha wenye kuharamisha Alichokihalalisha Yeye au Alichokiharamisha Yeye kwa kutegemea rai na matamanio yasiyo na isnadi yoyote wala dalili. Kisha Allah تعالی Aliwaonya dhidi ya ahadi ya Siku ya Kiyama, Alisema;

وَمَا ظَنُّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ<sup>2</sup>

“Na nini dhana ya wanaomzulia Mwenyezi Mungu kwa Siku ya Kiyama?”

Kwa maana: Nini dhana yao juu ya watakachofanyiwa Siku ya Marejeo yao Kwetu, Siku ya Kiyama. Kauli ya Allah تعالی;

إِنَّ اللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى النَّاسِ

“Hakika Mwenyezi Mungu Ana Fadhila juu ya watu”.

Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisema: Ni juu ya kuacha Kwake Kuwaharakishia adhabu duniani<sup>2</sup>. Mimi (Ibn Kathir) nasema: Maana yake yaweza kuwa, “Ana fadhila juu ya watu”, ni katika Aliyoyaruhusu kwao wanufaike duniani, kutokana na

<sup>1</sup> Ahmad 3:473, 4:136.

<sup>2</sup> At-Tabari 15:113.



Alivyoviumba, wala hawakuhamisha bali vyenye madhara kwa dunia au dini yao.

وَلَيْكِنَّا أَكْثَرَهُمْ لَا يَشْكُرُونَ

“...lakini wengi wao hawashukuru...” Bali wao huviharamisha walivyo-neemeshwa na Allah تعالى na kuzidhiki nafsi zao, kisha huvifanya baadhi yake halali na vingine haramu. Hili limekwishawatokea Washirikina kwa sheria walizojiweka wenyewe na Watu wa Kitabu katika bidaa waliyoizusha katika dini yao.

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦١﴾

**61. “Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’an, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi Huwa ni Mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi.”**

**Kitu Chochote, Kikubwa na Kidogo Kimo Katika Elimu ya Allah تعالى**

Allah تعالى Anampa khabari Nabii Wake kwamba Yeye Anazijua hali zake zote na za umma Wake na viumbe wote, katika kila saa na sekunde (muda na kitambo kidogo). Hakuna cha kuutoroka Ujuzi Wake na Kuona Kwake hata kama ni cha uzito wa chembe ndogo katika kudharaulika na udogo wake. Si mbinguni wala ardhini, wala kilicho kidogo au kikubwa zaidi kuliko hicho, bali kiko katika Kitabu kilicho bayana. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَعِنْدَهُ مَفَاتِحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبُرِّ وَالْبَحْرِ وَمَا تَسْقُطُ مِنَ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظِلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٦٢﴾

**“Na ziko Kwake funguo za ghaibu; hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye Anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani ila Analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinachobainisha.” (6:59)**

Allah تعالى Ameeleza kwamba Yeye Anaijua mitikisiko ya miti na vingine katika vitu visivyo na uhai na wanyama wanapokula. Katika Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا طَيْرٍ يَطِيرُ بِجَنَاحَيْهِ إِلَّا أُمَمٌ أَمْثَالُكُمْ<sup>٤</sup>

**“Hakuna kiumbe chochote kinachotambaa ardhini, wala ndege anayeruka kwa mbawa zake mbili, ila ni umma kama nyinyi”.**

(6:38) Na Allah تعالى Amesema,

وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا

**“Na hakuna kiumbe yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu.” (11:6)**

Ikiwa huku ndiko Kujua Kwake juu ya mienendo ya vitu hivi, basi ni vipi kuhusu Kujua Kwake mishughuliko ya viumbe waliokalifishwa na kuamriwa juu ya ibada. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ ﴿٦٧﴾ الَّذِي يَرِنُكَ حِينَ تَقُومُ ﴿٦٨﴾ وَتَقْبَلُكَ فِي السُّجُودِ ﴿٦٩﴾

**“Na umtegemee Mtukufu Mwenye Nguvu Mwenye Kurehemu. Ambaye Anakuona unaposimama. Na mageuko yako kati ya wanaosujudu”.** (26:217-219) Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

وَمَا تَكُونُ فِي شَأْنٍ وَمَا تَتْلُوا مِنْهُ مِنْ قُرْآنٍ وَلَا تَعْمَلُونَ مِنْ عَمَلٍ إِلَّا كُنَّا عَلَيْكُمْ شُهُودًا إِذْ تُفِيضُونَ فِيهِ<sup>٥</sup>

**“Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur’an, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni Mashahidi juu yenu mnaposhughulika nayo.”**

Maana: Pindi mkijiingiza kufanya chochote katika hilo, basi Sisi huwa Tunawashuhudieni, Tukiwa katika hali ya Kusikia vyema na Kuona. Na kwa kuzingatia hilo Mtume ﷺ alisema pindi Jibril عليه السلام alipomuuliza kuhusu Ihsan;

«أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ»

**“Ni kwamba, unamuabudu Allah kama kwamba unamuona, lakini, kama haumuoni, hakika Yeye Anakuona.”<sup>1</sup>**

<sup>1</sup> Muslim 1:37.

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفَ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ  
 ٦٢ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ ﴿٦٢﴾ لَهُمْ  
 الْبُشْرَىٰ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۗ لَا تَبْدِيلَ  
 لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٣﴾ وَلَا  
 يَحْزَنُونَ قَوْلُهُمْ إِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا ۗ هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ  
 ٦٤ أَلَا إِنَّ لِلَّهِ مَنْ فِي السَّمٰوٰتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ  
 وَمَا يَتَّبِعُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ شُرَكَاءَ  
 إِنَّ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿٦٥﴾ هُوَ  
 الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا ۗ إِنَّ  
 فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٦٦﴾ قَالُوا اتَّخَذَ  
 اللَّهُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ الْغَنِيُّ ۗ لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا  
 فِي الْأَرْضِ ۗ إِنْ عِنْدَكُمْ مِنْ سُلْطٰنٍ بِهٰذَا ۗ اتَّقُوا اللَّهَ  
 عَلَىٰ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾ قُلْ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتُرُونَ  
 عَلَىٰ اللَّهِ الْكُذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿٦٨﴾ مَتَّعَ فِي الدُّنْيَا ثَمَّرَ  
 إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُنذِقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا  
 يَكْفُرُونَ ﴿٦٩﴾

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفَ  
 عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٢﴾  
 الَّذِينَ ءَامَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ  
 لَهُمُ الْبُشْرَىٰ فِي الْحَيَاةِ  
 الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۗ لَا تَبْدِيلَ  
 لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۗ ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ  
 الْعَظِيمُ ﴿٦٣﴾

62. "Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika".

63. "Hao ni ambao wameamini na wakawa wana-mcha Mungu".

64. "Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera. Hapana mabadiliko katika Maneno ya Mwenyezi Mungu. Huko ndiko Kufuzu kukubwa".

**Kuwatambuwa Mawalii wa Allah تعالی**

Allah تعالی Anaeleza kuwa, mawalii wake (marafiki Wake) ni wale walioamini na wakawa na Taqwa, kama Alivyowaelezea. Basi, kila mwenye Taqwa, ni Walii wa Allah تعالی, kwa hivyo;

لَا خَوْفَ عَلَيْهِمْ

"...hawatakuwa na khofu...". Juu ya hali za Akhera zinazowakabili.

وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ

**“...wala hawatahuzunika”.** Juu ya waliyoyaacha nyuma yao, duniani. Ibn Jarir رضي الله عنه alisimulia kutoka kwa Abu Hurayra رحمه الله تعالى alisema: Mtume ﷺ alisema;

«إِنَّ مِنْ عِبَادِ اللَّهِ عِبَادًا يَغِطُّهُمْ الْأَنْبِيَاءُ وَالشُّهَدَاءُ»

*“Miongoni mwa waja wa Allah, kuna ambao Mitume na Mashahidi watakaowachukulia kwamba ni wenye bahati”.*

Palisemwa: “Ni akina nani hao, ewe Mtume ﷺ, ili nasi tuwapende?” Akasema:

«هُمْ قَوْمٌ تَحَابُّوا فِي اللَّهِ مِنْ غَيْرِ أَمْوَالٍ وَلَا أَنْسَابٍ، وَجُوهُهُمْ نُورٌ عَلَى مَتَابِرٍ مِنْ نُورٍ، لَا يَخَافُونَ إِذَا خَافَ النَّاسُ، وَلَا يَحْزَنُونَ إِذَا حَزَنَ النَّاسُ»

*“Hao ni watu waliopendana kwa ajili ya Allah na si kwa ajili ya mali wala nasaba. Nyuso zao zitakuwa ni zenye nuru juu ya mimbari za nuru. Hawatakuwa na khofu, pindi watu wengine watakaposhikwa na khofu, wala hawatafikwa na huzuni, pindi watu watakapohuzunika”.*

Kisha akasoma;

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفَ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٦٦﴾

**“Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika”<sup>1</sup>.**

**Ndoto ya Kweli ni Utaratibu wa Uzuri wa Bishara (Habari).**

Ibn Jariri رضي الله عنه alisimulia kuwa ‘Ubadah bin As-Swamit رحمه الله تعالى alimuambia Mtume ﷺ:

لَهُمُ الْبُشْرَىٰ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ ۗ

**“Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera”.**

Tumekwisha fahamu kwamba bishara ya Akhera ni Jannah. Basi ni nini bishara ya duniani?” Akasema;

<sup>1</sup> At-Tabari 15:120.

«الرُّؤْيَا الصَّالِحَةُ يَرَاهَا الْعَبْدُ أَوْ تُرَى لَهُ . وَهِيَ جُزْءٌ مِنْ أَرْبَعَةٍ وَأَرْبَعِينَ جُزْءًا أَوْ سَبْعِينَ جُزْءًا مِنَ النَّبْوَةِ»

*"Ndoto njema huiona mja mwema au huonekanwa kwa ajili yake. Nayo ni sehemu moja kati ya arubaini au sabini ya Utume"<sup>1</sup>.*

Imamu Ahmad alimnukuu Abu Dharr رضي الله عنه, kuwa alisema: "Ewe Mtume! Ni vipi juu ya mja anayefanya amali na watu humsifia kwayo?" Mtume ﷺ akasema:

«تِلْكَ عَاجِلُ بُشْرَى الْمُؤْمِنِ»

*"Huko ni kuiharakisha bishara kwa ajili ya Muumini"<sup>2</sup>.*

Muslim ameinukuu<sup>3</sup>. Ahmad alinukuu pia kwamba, 'Abdullah bin 'Amri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema;

لَهُمْ الْبُشْرَى فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ

***"Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera".***

Akasema;

«الرُّؤْيَا الصَّالِحَةُ يُبَشِّرُهَا الْمُؤْمِنُ، جُزْءٌ مِنْ تِسْعَةٍ وَأَرْبَعِينَ جُزْءًا مِنَ النَّبْوَةِ، فَمَنْ رَأَى ذَلِكَ فَلْيُخَبِرْ بِهَا، وَمَنْ رَأَى سِوَى ذَلِكَ فَإِنَّمَا هُوَ مِنَ الشَّيْطَانِ لِيُخْرِتَهُ، فَلْيَنْتَفِ عَنْ بَسَارِهِ ثَلَاثًا، وَلْيُكَبِّرْ، وَلَا يُخَبِرْ بِهَا أَحَدًا»

*"Ndoto njema hubashiriwa Muumini, ikiwa ni fungu moja kati ya arubaini na tisa katika Utume. Basi mwenye kuiota ya namna hiyo, awaambie wengine. Na atakayeota kinyume cha hivyo, basi hiyo ni ya shetani ili amhuzunishe. Kwa hivyo apulize upande wa kushotoni kwake mara tatu na aseme: "Allahu Akbar", na asimueleze mtu mwingine kuihusu"<sup>4</sup>.*

<sup>1</sup> At-Tabari 5:132. Sanadi yake ni dhaifu. Kwa njia hii ya Musa bin Ubaida Tz. "Attakrib" imekuja kwa njia nyingine ambayo ni sahihi. Tazama "Assahiha" cha Albani (1716).

<sup>2</sup> Ahmad 5:156.

<sup>3</sup> Muslim 4:2034.

<sup>4</sup> Ahmad 5:219. Isnadi yake ni dhaifu.

Hawakuiweka (katika nukuu zao). Ilisemwa pia kwamba makusudio yake ni bishara ya Malaika kwa ajili ya Waumini zama za kufika kwao Jannah na katika kupewa maghufira. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى،

إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللَّهُ ثُمَّ اسْتَقَمُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلَائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلَا تَحْزَنُوا  
وَأُبَشِّرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٤١﴾ نَحْنُ أَوْلِيَاؤُكُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ  
وَلَكُمْ فِيهَا مَا نَشْتَهُ أَنْفُسُكُمْ وَلَكُمْ فِيهَا مَا تَدَّعُونَ ﴿٤٢﴾ تُوَلَّوْا مِنْ غَفُورٍ رَحِيمٍ ﴿٤٣﴾

**“Hakika waliosema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Kisha wakanyooka sawa, hao huwateremkia Malaika wakawaambia: Msiogope, wala msihuzunike; nanyi furahini kwa Pepo mliyokuwa mkiahidiwa. Sisi ni vipenzi vyenu katika maisha ya dunia na katika Akhera, na humo mtapata kinachotamaniwa na nafsi zenu, na humo mtapata mtakavyovitaka. Ni takrima itokayo kwa Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”. (41:30-32)**

Pia ipo Hadithi ya Al-Baraa رضي الله عنه؛

إِنَّ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا حَضَرَهُ الْمَوْتُ جَاءَهُ مَلَائِكَةٌ بِيضُ الْوُجُوهِ بِيضُ الثِّيَابِ فَقَالُوا:  
اخْرُجِي أَتَيْتِهَا الرُّوحَ الطَّيِّبَةَ إِلَى رُوحٍ وَرِيحَانٍ وَرَبٌّ غَيْرِ غَضَبَانَ، فَتَخْرُجُ مِنْ فِيهِ  
كَمَا تَسِيلُ الْقَطْرَةُ مِنْ قَمِ السَّمَاءِ

**“Kifo kinapomkaribia Muumini, hujiwa na Malaika wakiwa na nyuso na nguo nyeupe na kusema: “Ewe roho nzuri! Toka uelekee katika raha na manukato, na Mola Akiwa katika hali ya Kutokuwa na ghadhabu nawe. Basi, Roho itatoka kupitia kinywani mwake, kama vile tone la maji linavyodondoka kutoka katika kiriba.”<sup>1</sup>**

Ama juu ya bishara yao huko Akhera, Allah تعالى Alisema;

لَا يَحْزَنُهُمُ الْفَزَعُ الْأَكْبَرُ وَتَتَلَقَّيْنَهُمُ الْمَلَائِكَةُ هُنَا يَوْمَئِذٍ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٤٤﴾

**“Hicho kitisho kikubwa hakitowahuzunisha. Na Malaika watawapokea (kwa kuwaambia): Hii ndiyo siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa!” (21:103) Na Allah تعالى Amesema,**

<sup>1</sup> Ahmad 4:287.

يَوْمَ تَرَى الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ يَسْعَى نُورُهُمْ بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَبِأَيْمَانِهِمْ بُشْرَانُكُمْ الْيَوْمَ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿٦٢﴾

**“Siku utakapowaona Waumini wanaume na Waumini wanawake, nuru yao iko mbele yao, na kuliani kwao: Furaha yenu leo – Bustani zipitazo mito kati yake mtakaa humo milele. Huko ndiko Kufuzu kukubwa”. (57:12)**

Kauli ya Allah تعالى:

لَا تَبْدِيلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ

**“Hapana mabadiliko katika Maneno ya Mwenyezi Mungu.”**

Maana yake: Ahadi hii haibadilishi, wala haiendewi kinyume chake, wala haighairishwi, bali imeamuliwa, imethibitishwa, ni yenye kutokea haswa.

ذَلِكَ هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

**“Huko ndiko Kufuzu kukubwa”.**

وَلَا يَخْرُجُ قَوْلُهُمْ إِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٦٥﴾ أَلَا إِنَّ لِلَّهِ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ وَمَا يَتَّبِعُ الَّذِينَ يَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ شُرَكَاءَ إِنْ يَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿٦٦﴾ هُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ اللَّيْلَ لَتَسْكُنُوا فِيهِ وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَسْمَعُونَ ﴿٦٧﴾

**65. “Wala yasikuhuzunishe maneno yao. Hakika Utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu. Yeye Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kujua.”**

**66. “Jueni kuwa ni vya Mwenyezi Mungu vyote viliomo mbinguni na ardhini. Na wala hawawafuati hao wanaowaomba badala ya Mwenyezi Mungu kuwa ni washirika wake. Wao hawafuati ila dhana tu, na hawasemi ila uwongo.”**

**67. “Yeye Ndiye Aliyekujaalieni usiku mpate kutulia humo, na mchana wa kuonea. Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanaosikia.”**

## Nguvu Zote, Uwezo na Utukufu Wote ni wa Allah تعالی, Yeye Pekee Ndiye Mwenye Mamlaka Ulimwenguni

Allah تعالی Anamuambia Mjumbe Wake;

وَلَا تَحْزُنْكَ

**“Wala yasikuhuzunisha”**. Yasemwayo na Washirikina hao, bali mumuombe Allah تعالی msaada dhidi yao na mumtegemee Yeye tu. Kwani kwa;

إِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا

**“Hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu”**. Kwa maana: Wote kabisa, ni wake Yeye, Mtume ﷺ na Waumini.

هُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

**“Yeye Ndiye Mwenye Kusikia Mwenye Kujua”**. Maana: Ni Mwenye Kuzisikia kauli za waja Wake, Mwenye kuzijua hali zao. Kisha, Allah تعالی Alieleza kwamba ni Wake Yeye Ufalme wa mbingu na ardhi na kwamba, Washirikina huabudu masanamu, na kwamba hayo hayamiliki chochote, si madhara wala manufaa, wala wao hawana dalili juu ya ibada yao, bali katika hilo hufuata dhana, uongo na uzushi tu. Tena Alieleza kuwa Ameujaalia usiku kwa waja Wake ili wapate kutulia. Maana yake, wapumzike katika wakati huo kutokana na uchovu, mavuno na shughuli zao.

وَالنَّهَارَ مُبْصِرًا

**“...na mchana wa kuonea”**. Kwa maana: Unatoa mwangaza kwa ajili ya kuwanufaisha kimaisha, kwenda kwao, safari na maslahi yao mengine.

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَسْمَعُونَ

**“Hakika katika haya zipo ishara kwa watu wanaosikia”**. Maana: Wanaozisikia hoja na dalili hizi, basi wazizingatie na kuwajulisha juu ya Ukuu wa Muumbaji, Mwenye Kukadiria na Mwendeshaji Wake.

قَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ هُوَ الْعَزِيزُ ۗ لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۗ اِنَّ عِنْدَكُمْ مِّنْ سُلْطٰنٍ بِهٰذَا ۗ اَتَقُولُوْنَ عَلٰى اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ ﴿٦٤﴾ قُلْ اِنَّ الَّذِيْنَ يَفْتَرُوْنَ عَلٰى اللّٰهِ الْكٰذِبُ لَا يُفْلِحُوْنَ ﴿٦٥﴾ مَتَّعْ فِي الدُّنْيَا نٰمِرًا لِّئِنَّا مَرْجِعُهُمْ نَمُرُّ بِذٰلِكُمْ اَلْعَذٰبِ الشَّدِيدِ بِمَا كَانُوْا يَكْفُرُوْنَ ﴿٦٦﴾



**68. “Wamesema: Mwenyezi Mungu ana mwana. Subhanahu, Aliye takasika! Yeye ni Mkwasi, Mwenye Kujitosheleza. Vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi ni Vyake Peke Yake. Nyinyi hamna uthibitisho wowote wa haya! Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua?”**

**69. “Sema: Hao wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa.”**

**70. “Hivyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejea yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.”**

**Allah تعالیٰ Yu Mbali na Jambo la Kujifanyia Mke au Mtoto**

Allah تعالیٰ Anawakanusha wale waliodai kwamba Yeye;

وَلَدًا سُبْحٰنَهُ هُوَ الْغَفِيُّ

**“...ana mwana. Subhanahu, Aliyetakasika! Yeye ni Mkwasi.”**

Maana: Ametakasika dhidi ya hayo. Yeye Hamhitajii asiyekuwa Yeye, ilhali kila kitu kina haja Kwake.

لَهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ

**“Vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi ni Vyake Peke Yake.”**

Maana: Vipi awe na mwana katika Alivyoviumba, ilhali kila kitu Amekimiliki Yeye, na pia ni mja Wake.

اِنَّ عِنْدَكُمْ مِّنْ سُلْطٰنٍ بِهٰذَا

**“Nyinyi hamna uthibitisho wowote wa haya!”**

Maana: Nyinyi hamna dalili juu ya uongo na uzushi mnaousema.

اَتَقُولُوْنَ عَلٰى اللّٰهِ مَا لَا تَعْلَمُوْنَ

**“Mnamzulia Mwenyezi Mungu msiyoyajua?”**

Hili ni tishio kali na onyo kali. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالیٰ;

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ۝ تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ  
 مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ۝ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ وَلَدًا ۗ وَمَا يُكْنِي  
 لِلرَّحْمَنِ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا ۗ إِنَّ كُلَّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَى الرَّحْمَنِ  
 عَبْدًا ۗ لَقَدْ أَحْصَاهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ۗ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ۗ

***“Na wao ati husema kuwa Arrahmani Mwingi wa Rehema Ana mwana! Hakika mmeleta jambo la kuchusha mno! Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kuanguka vipande vipande. Kwa kudai kwao kuwa Arrahmani Mwingi wa Rehema Ana mwana. Wala hahitajii Arrahman Mwingi wa Rehema kuwa na mwana. Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Arrahman Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa Wake. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahisabu sawa sawa. Na kila mmoja katika wao Atamfikia Siku ya Kiyama peke Yake!” (19:88-95)***

Halafu, Allah تعالى Aliwaonya waongo, wazushi waliodai kwamba Yeye Ana mwana, kuwa wao hawatafaulu duniani wala Akhera. Ama duniani, Yeye Atawavuta taratibu katika maangamizi na Atawapa muda kidogo kwa starehe kidogo.

ثُمَّ نَضَّطَّرَّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ

***“Kisha Tutawasukuma kwenye adhabu ngumu.” (31:24)***

Kama Allah تعالى Alivyosema hapa;

مَتَّعٌ فِي الدُّنْيَا

***“...ni starehe ya katika dunia tu...”***. Maana yake: Muda wa karibu tu;

ثُمَّ إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ

***“...kisha marejea yao ni Kwetu”***. Maana yake: Katika Siku ya Kiyama.

ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ

***“Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.”***Maana yake: Marejeo machungu, kwa sababu ya ukafiri wao na uzushi wao kwa Allah تعالى.

\* وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ نُوحٍ إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ يَنْقُومِ إِنْ كَانَ كَبُرَ  
 عَلَيْكُمْ مَقَامِي وَتَذَكِيرِي بِمَا يَتِ اللَّهُ فَعَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْتُ  
 فَأَجْمِعُوا أَمْرَكُمْ وَشُرَكَاءَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُنْ أَمْرُكُمْ عَلَيْكُمْ غُمَّةً  
 ثُمَّ أَقْضُوا إِلَيَّ وَلَا تُنظِرُونِ ﴿٧١﴾ فَإِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَمَا سَأَلْتُمْ  
 مِنْ أَجْرٍ إِنْ أَجْرِي إِلَّا عَلَى اللَّهِ وَأَمِرتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ  
 الْمُسْلِمِينَ ﴿٧٢﴾ فَكَذَّبُوهُ فَتَجِيتُهُ وَمَنْ مَعَهُ فِي الْفَلَكِ  
 وَجَعَلْنَاهُمْ خَلِيفَ وَأَعْرَفْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَانظُرْ  
 كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٣﴾ ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْ بَعْدِهِ رُسُلًا  
 إِلَى قَوْمِهِمْ فَجَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا  
 كَذَّبُوا بِهِ مِنْ قَبْلُ كَذَلِكَ نَطْبَعُ عَلَى قُلُوبِ الْمُعْتَدِينَ  
 ﴿٧٤﴾ ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْ بَعْدِهِم مُوسَى وَهَارُونَ إِلَى فِرْعَوْنَ  
 وَمَلَائِمِهِ بِآيَاتِنَا فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُجْرِمِينَ ﴿٧٥﴾  
 فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوا إِنَّ هَذَا لَسِحْرٌ مُبِينٌ  
 ﴿٧٦﴾ قَالَ مُوسَى أَتَقُولُونَ لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَكُمْ أَسِحْرٌ  
 هَذَا وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُونَ ﴿٧٧﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَلْفِتْنَا عَمَا  
 وَجَدْنَا عَلَيْهِ ءَابَاءَنَا وَتَكُونُ لَكُمْ أَلِكِبْرِيَاءُ فِي الْأَرْضِ وَمَا  
 نَحْنُ لَكُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٧٨﴾

\* وَأَتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَأَ نُوحٍ إِذْ قَالَ  
 لِقَوْمِهِ يَنْقُومِ إِنْ كَانَ كَبُرَ عَلَيْكُمْ  
 مَقَامِي وَتَذَكِيرِي بِمَا يَتِ اللَّهُ فَعَلَى  
 اللَّهِ تَوَكَّلْتُ فَأَجْمِعُوا أَمْرَكُمْ  
 وَشُرَكَاءَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُنْ أَمْرُكُمْ عَلَيْكُمْ  
 غُمَّةً ثُمَّ أَقْضُوا إِلَيَّ وَلَا تُنظِرُونِ ﴿٧١﴾  
 فَإِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَمَا سَأَلْتُمْ مِنْ أَجْرٍ إِنْ  
 أَجْرِي إِلَّا عَلَى اللَّهِ وَأَمِرتُ أَنْ أَكُونَ  
 مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٧٢﴾ فَكَذَّبُوهُ  
 فَتَجِيتُهُ وَمَنْ مَعَهُ فِي الْفَلَكِ  
 وَجَعَلْنَاهُمْ خَلِيفَ وَأَعْرَفْنَا الَّذِينَ  
 كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ  
 عَاقِبَةُ الْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٣﴾

71. "Na Wasomee habari za  
 Nuhu alipowaambia watu  
 wake: Enyi watu wangu!  
 Ikiwa kukaa kwangu nanyi  
 na kukumbusha kwangu  
 kwa Ishara za Mwenyezi  
 Mungu kinakutieni

mashaka basi mimi namtegemea Mwenyezi Mungu. Nanyi tengezeni mambo  
 yenu pamoja na washirika wenu, na wala mambo yenu yasifichikane kwenu.  
 Kisha nihukumuni, wala msinipe muhula."

**72. "Lakini mkigeuka, basi mimi sikukuombeni ujira. Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu."**

**73. "Wakamkanusha. Basi Tukamuokoa, pamoja na waliokuwa naye, katika jahazi. Na Tukawafanya wao ndio waliobakia, na Tukawazamisha waliozikanusha Ishara Zetu. Basi angalia vipi ulikuwa mwisho wa walioonywa."**

### Kisa cha Nuh عليه السلام Pamoja na Kaumu Yake

Allah تعالى Anamuambia Nabii Wake;

وَأْتَلُ عَلَيْهِمْ

**"Wasomee".** Maana yake: Wape habari na uwasimulie makafiri wa Makkah wanaokukadhibisha na kukukhalifu.

نَبَأُ نُوحٍ

**"...habari za Nuhu".** Maana yake: Toa habari zake pamoja na kaumu yake waliomkadhibisha. Eleza jinsi Allah تعالى Alivyowahilikisha na Kuwaangamiza wote mpaka wa mwisho wao kwa gharika. Ili nao wajihadharishe na hivyo Hilaki na kuangamia kusiwasibu kama ilivyotokea kwa hao.

إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِ يَنْقُومِ إِنْ كَانَ كَبُرَ عَلَيْكُمْ مَقَامِي

**"Alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Ikiwa kukaa kwangu nanyi."**

Maana yake: Ikiwa kukaa pamoja nanyi limekuwa jambo kubwa kwenu.

وَتَذَكِّرِي بِآيَاتِ اللَّهِ

**"Na kukumbusha kwangu kwa Ishara za Mwenyezi Mungu."**

Maana yake: kukukumbusheni nyinyi hoja na ishara Zake.

فَعَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْتُ

**"Kinakutieni mashaka basi mimi namtegemea Mwenyezi Mungu."**

Maana yake: Sijali, wala siliachi jambo hilo, ikiwa limekuwa kubwa kwenu au vinginevyo.

فَأَجْمِعُوا أَمْرَكُمْ وَشُرَكَاءَكُمْ

**“Nanyi tengezeni mambo yenu pamoja na washirika wenu.”**

Kwa maana: Tengezeni nyinyi pamoja na washirika wenu, miongoni mwa masanamu, mnavyodai badala ya Allah تعالى.

ثُمَّ لَا يَكُنْ أَمْرُكُمْ عَلَيْكُمْ غُمَّةً ثُمَّ اقْضُوا إِلَيَّ

**“...na wala mambo yenu yasifichikane kwenu. Kisha nihukumuni...”**

Kwa maana: Msilifanye kuwa siri, bali hali yangu muiweke wazi pamoja nami, na mkiwa mnadai kwamba mko katika ukweli, basi pitisheni hukumu juu yangu;

وَلَا تُنظِرُونَ

**“...wala msinipe muhula.”**

Maana yake: Wala msiikawize hata kwa saa moja, vyovyote muwezavyo, fanyeni mimi sijali kuhusu nyinyi wala sina khofu kwenu kwani nyinyi si chochote.

Ni sawa na alivyosema Hud عليه السلام kuwaambia watu wake;

إِنِّي أَشْهَدُ اللَّهَ وَأَشْهَدُوا أَنِّي بَرِيءٌ مِمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٥٤﴾ مِنْ دُونِهِ ۖ فَكَيْدُونِي جَمِيعًا ثُمَّ لَا

تُنظِرُونَ ﴿٥٥﴾ إِنِّي تَوَكَّلْتُ عَلَى اللَّهِ رَبِّي وَرَبِّكُمْ

**“Hakika mimi namshuhudia Mwenyezi Mungu, na nyinyi shuhudieni, ya kwamba mimi najitenga mbali na hao mnao wafanya washirika. Mkamuacha Yeye. Basi nyote nyinyi nipangieni vitimbi, na kisha msinipe muhula! Hakika mimi nimemtegemea Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wangu na Mola Mlezi wenu.” (11:54-56)**

## Uislamu ni Dini ya Manabii Wote

Kauli ya Allah تعالى;

فَإِنْ تَوَلَّيْتُمْ

**“Lakini mkigeuka.”**

Maana yake: Mmekadhibisha na mkaipa mgongo twaa.

فَمَا سَأَلْتُمْ مِّنْ أَجْرٍ

**“...basi mimi sikukuombeni ujira.”**

Kwa maana: Mimi sihitaji chochote kwa kutoa kwangu nasaha kwenu.

إِنْ أُجْرِيَ إِلَّا عَلَى اللَّهِ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ

**“Ujira wangu hauko ila kwa Mwenyezi Mungu. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu.”**

Maana yake: Mimi pia nafuata ninayoamrisha kwayo katika Uislamu kwa ajili ya Allah تعالى, na kwamba, Uislamu ndiyo Dini ya Manabii wote tangu wa mwanzo mpaka wa mwisho wao, japokuwa Sharia zao zilikuwa za namna mbali mbali na kanuni zao zikapishana kwa idadi.

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَا جَا

**“Kila mmoja katika nyinyi Tumemuwekea Sharia yake na njia yake.” (5:48)**

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema; “Ni njia na Sunnah zake”<sup>1</sup>. Nuhu عليه السلام anasema hapa,

وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُسْلِمِينَ

**“Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waislamu.”**

Pia Allah تعالى Alisema kuhusu Ibrahim Al-Khalil عليه السلام.

<sup>1</sup> At-Tabari 10:388.

إِذْ قَالَ لَهُ رَبُّهُ أَسْلِمِ ۗ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿٧١﴾ وَوَصَّىٰ بِهَا إِبْرَاهِيمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبَ يَبْنِيَّ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ لَكُمْ الدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٧٢﴾

**“Na Mola wake Mlezi Alipowaambia: Silimu, nyenyenyekea! Alinena: Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote. Na Ibrahim akawausia Wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu Amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyenyekevu.” (2:131:132)**

Nabii Yusuf عليه السلام naye alisema;

رَبِّ قَدْ ءَاتَيْتَنِي مِنَ الْمَلِكِ وَعَلَّمْتَنِي مِنْ تَأْوِيلِ الْأَحَادِيثِ ۗ فَاطِرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ أَنْتَ وَليُّي فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ تَوَفَّيْ مُسْلِمًا وَآلِحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ ﴿١٢١﴾

**“Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika Umenipa Utawala na Umenifunza tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe Ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni Muislam na nichanganyishe na watendao mema.” (12:101)**

Nabii Musa عليه السلام alisema;

يَنْقُومَ إِنْ كُنْتُمْ ءَامِنْتُمْ بِاللَّهِ فَعَلَيْهِ تَوَكَّلُوا إِنْ كُنْتُمْ مُسْلِمِينَ

**“Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu.” (10:84)**

Wachawi walisema;

رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَتَوَفَّنَا مُسْلِمِينَ

**“Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu na Utufishe hali ni Waislamu.” (7:126)**

Baliqis alisema;

رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي وَأَسْلَمْتُ مَعَ سُلَيْمَانَ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

**“Mola wangu Mlezi! Mimi nimejidhulumu nafsi yangu, na sasa nanyenyenyekea pamoja na Sulaiman kwa Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.” (27:44)**

Na Allah تعالی Amesema:

إِنَّا أَنْزَلْنَا التَّوْرَةَ فِيهَا هُدًى وَنُورٌ نَحْكُمُ بِهَا النَّبِيِّينَ الَّذِينَ أَسْلَمُوا

**“Hakika Sisi Tuliteremsha Taurati yenye uwongofu na nuru, ambayo kwayo wanahukumu Manabii walio nyenyekea ...” (5:44)**

Na Allah تعالی Amesema tena:

وَإِذْ أَوْحَيْتُ إِلَى الْحَوَارِيِّينَ أَنْ ءَامِنُوا بِي وَبِرَسُولِي قَالُوا ءَامَنَّا وَأَشْهَدُ بِأَنَّنا مُسْلِمُونَ ﴿١١١﴾

**“Na Nilipowafunulia Wanafunzi kwamba waniamini Mimi na Mtume Wangu, wakasema: Tumeamini na shuhudia kuwa sisi ni Waislamu.” (5:111)**

Na Mtume wa mwisho na Mtume wa mitume wote amesema,

إِنْ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٦٢﴾ لَا شَرِيكَ لَهُ ۗ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

**“Hakika Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.” (6:162-163)**

Maana: Katika ummah huu, na alisema katika Hadithi iliyothibiti kutoka kwake;

«نَحْنُ مَعْشَرَ الْأَنْبِيَاءِ أَوْلَادُ عَالَمٍ. وَدِينُنَا وَاحِدٌ»

**“Sisi, Mitume ni Ndugu wa (baba mmoja lakini wa) mama mbalimbali. Dini yetu ni moja.”<sup>1</sup>**

Maana yake: Nayo ni kufanya ibada kwa Allah تعالی Peke Yake, Asiye na mshirika, japokuwa sharia zetu zilikuwa za namna mbalimbali.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 6:550.



**Lengo la Uovu na Mwisho wa Madhalimu (Khatma Yao)**

Kauli ya Allah تعالى:

فَكَذَّبُوهُ فَتَجِيبْنَاهُ وَمَنْ مَعَهُ

**“Wakamkanusha. Basi Tukamuokoa, pamoja na waliokuwa naye”.**

Kwa maana: Katika dini yake.

فِي الْفَلَكِ

**“...katika jahazi...”. Ambayo ni Safina.**

وَجَعَلْنَاهُمْ حَلِيفَ

**“Na Tukawafanya wao ndio waliobakia...”. Katika ardhi.**

وَأَعْرَفْنَا الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۖ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكذِبِينَ

**“...na Tukawazamisha waliozikanusha Ishara Zetu. Basi angalia vipi ulikuwa mwisho wa walioonywa”.**

Kwa maana: Ewe Muhammad! Angalia namna Tulivyowaokoa Waumini na Tukawahiliki wakadhibishaji.

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْ بَعْدِهِ رَسُولًا إِلَىٰ قَوْمِهِمْ فَجَاءَهُمْ بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا  
بِهِ مِنْ قَبْلُ ۚ كَذَٰلِكَ نَطْبَعُ عَلَىٰ قُلُوبِ الْمُعْتَدِينَ ﴿٧٦﴾**74. “Kisha baada yake Tukawatuma Mitume kwa watu wao. Nao wakawajia kwa Ishara zilizo wazi. Lakini hawakuwa wenye kuyaamini waliyoyakanusha kabla yake. Ndio kama hivyo Tunapiga muhuri juu ya nyoyo za warukao mipaka”.**

Allah تعالى Anasema: Kisha baada ya Nuh عليه السلام, Tuliwapeleka Mitume wengine kwa kaumu zao na wakawaendea wakiwa pamoja na vyenye kuwabainishia. Yaani hoja mbalimbali, dalili na ushahidi wa kuyasadikisha waliyokuja nayo.

فَمَا كَانُوا لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا بِهِ مِنْ قَبْلُ

**“Lakini hawakuwa wenye kuyaamini waliyoyakanusha kabla yake”.**

Kwa maana: Umma hazikuyaamini waliyoletewa na Mitume wao kwa sababu walishayakataa tangu mwanzo. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

وَنُقَلِّبُ أَفْئِدَتَهُمْ وَأَبْصَرَ لَهُمْ

**“Nasi Tunazigeuza nyoyo zao na macho yao”. (6:110)**

Kauli ya Allah تعالى: كَذَلِكَ نَطْبَعُ عَلَى قُلُوبِ الْمُعْتَدِينَ

**“Ndio kama hivyo Tunapiga muhuri juu ya nyoyo za warukao mipaka”.**

Hii ina maana, kama Allah تعالى Alivyopiga muhuri juu ya nyoyo zao, basi hawatoamini kwa sababu ya kukadhibisha kwao kulikotangulia. Hivi ndivyo Allah تعالى Anavyotia muhuri juu ya nyoyo za watu wa baada yao walioshabihiana nao. Kwa hivyo Anatia chapa katika nyoyo zao, hivyo hawataamini, mpaka waione adhabu iumizayo. Maana yake ni kwamba, Allah Aliwahiliki umma zilizowakadhibisha Mitume, na Aliwaokoa waliowaamini. Hayo ni baada ya Nuh عليه السلام, kwani tangu kipindi cha Adam عليه السلام watu walikuwa katika Uislamu, mpaka walipozusha ibada ya masanamu. Allah تعالى Akamtuma Nuh عليه السلام kwao. Kwa ajili hiyo, Waumini watamuambia Siku ya Kiyama: “Wewe ndiye Mtume wa kwanza uliyetumwa na Allah تعالى kwa wakazi wa ardhi”. Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema: “Kulikuwa na vizazi kumi baina ya Adam عليه السلام na Nuh عليه السلام, na vyote vilikuwa vikifuata Uislamu”<sup>1</sup>. Allah تعالى Alisema;

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنَ الْقُرُونِ مِنْ بَعْدِ نُوحٍ

**“Na kaumu ngapi Tumeziangamiza baada ya Nuhu”. (17:17)** Katika haya, kuna maonyo makubwa kwa Washirikina wa kiarabu waliomkadhibisha Mkuu wa Mitume, Nabii na Mtume wa mwisho ﷺ kuletwa, kwani, ikiwa adhabu na Hilaki kutoka kwa Allah تعالى iliwasibu waliowakadhibisha Mitume hao. Ni ipi basi dhana ya hawa, ilhali wamelimbikiza madhambi makubwa zaidi ya hao (wa kabla yao)?

ثُمَّ بَعَثْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ مُوسَىٰ وَهَارُونَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ بِآيَاتِنَا فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُجْرِمِينَ ﴿١٧٠﴾ فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوا إِنَّ هَذَا لَسِحْرٌ مُّبِينٌ ﴿١٧١﴾ قَالَ مُوسَىٰ أَتَقُولُونَ لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَكُمْ أَسِحْرٌ هَذَا وَلَا يُفْلِحُ السَّاجِرُونَ ﴿١٧٢﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَلْفِتَنَّا عَمَّا وَجَدْنَا عَلَيْهِ ءِآبَاءَنَا وَتَكُونَ لَكُمْ ءَالِكِبْرِيَاءَ فِي الْأَرْضِ وَمَا خُنُّ لَكُمْ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٧٣﴾

<sup>1</sup> Al-Bidayah wan-Nihayah 1:101 na alisema, Al-Bukhari aliinukuu”

75. *“Kisha baada yao Tukamtuma Musa na Haruni kwa Firauni na waheshimiwa wake, kwa Ishara Zetu. Wakajivuna, na wakawa watu wakosefu”.*

76. *“Basi ilipowajia Haki kutoka Kwetu walisema: Hakika huu ni uchawi dhahiri”.*

77. *“Akasema Musa: Mnasema hivi juu ya Haki ilipokujieni? Huu ni uchawi? Na wachawi hawafanikiwi!”*

78. *“Wakasema: Je! Umetujia ili utuachishe tuliyowakuta nayo baba zetu, na mpate nyinyi wawili ukubwa katika nchi? Wala sisi hatukuaminini nyinyi”.*

Kisa cha Nabii Musa عليه السلام na Firauni.

Allah تعالى Anasema;

نُمَّرَ بَعَثْنَا

*“Kisha Tukamtuma”.*

Baada ya Mitume hao.

مُوسَىٰ وَهَارُونَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ

*“Musa na Haruni kwa Firauni na waheshimiwa wake”.*

Maana: Kaumu yake.

بِقَائِنَا

*“...kwa Ishara Zetu”.* Maana yake: Hoja na dalili Zetu.

فَأَسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُّجْرِمِينَ

*“Wakajivuna, na wakawa watu wakosefu”.*

Maana yake: Walifanya kiburi dhidi ya kufuta ukweli na kumfuata, wakawa kaumu ya wakosefu.

فَلَمَّا جَاءَهُمُ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِنَا قَالُوا إِنَّ هَذَا لِسِحْرٌ مُّبِينٌ

*“Basi ilipowajia Haki kutoka Kwetu walisema: Hakika huu ni uchawi dhahiri”.*

Kana kwamba wao – Allah تعالى Awaangamize – waliapa kwa hilo, na huku wakiwa wanajua kuwa walichosema kilikuwa cha uongo na uzushi.

Kama Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine;

وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا

**“Na wakazikataa kwa dhulma na kujivuna, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo”. (27:14)**

قَالَ مُوسَىٰ

**“Musa akasema”.**

Kuwaambia wao, na kuwakanusha.

أَتَقُولُونَ لِلْحَقِّ لَمَّا جَاءَكُمْ ۗ أَسِحْرٌ هَذَا وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُونَ ﴿٧١﴾ قَالُوا أَجِئْنَا لِنَتَلَفَّتْنَا

**“Mnasema hivi juu ya Haki ilipokujieni? Huu ni uchawi? Na wachawi hawafanikiwi Wakasema: Je! Umetuja ili utuachishe...”.**

Maana yake: Sisi wawili.

عَمَّا وَجَدْنَا عَلَيْهِ ءَابَاءَنَا

**“...tuliyowakuta nayo baba zetu”.** Maana yake: Dini yao.

وَتَكُونُ لَكُمْ

**“...na mpate nyinyi wawili...”.**

Maana yake, kwa ajili yako na Harun عليه السلام.

الْكِبْرِيَاءِ

**“...ukubwa...”.** Inamaanisha ukuu na uongozi.

فِي الْأَرْضِ وَمَا نَحْنُ لَكُمْ بِمُؤْمِنِينَ

**“...katika nchi? Wala sisi hatukuaminini nyinyi”.**

\* \* \*

وَقَالَ فِرْعَوْنُ أَتُنُونِي بِكُلِّ سَجْرٍ عَلِيمٍ ﴿٧٩﴾ فَلَمَّا جَاءَ  
 السَّحْرَةَ قَالَ لَهُمْ مُوسَىٰ أَلْقُوا مَا أَنْتُمْ مُلقُونَ ﴿٨٠﴾  
 فَلَمَّا أَلْقَوْا قَالَ مُوسَىٰ مَا جِئْتُمْ بِهِ السَّحْرُ إِنَّ اللَّهَ  
 سَيُبْطِلُهُ إِنَّ اللَّهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٨١﴾ وَيُحِقُّ  
 اللَّهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴿٨٢﴾ فَمَا  
 ءَامَنَ لِمُوسَىٰ إِلَّا ذُرِّيَّةٌ مِّن قَوْمِهِ عَلَىٰ خَوْفٍ مِّن  
 فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِمْ أَن يَفْتِنَهُمْ وَإِنَّ فِرْعَوْنَ لَعَالٍ فِي  
 الْأَرْضِ وَإِنَّهُ لَمِنَ الْمُسْرِفِينَ ﴿٨٣﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ يَنْقُومُ إِن  
 كُنْتُمْ ءَامِنُمْ بِاللَّهِ فَعَلَيْهِ تَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُسْلِمِينَ ﴿٨٤﴾  
 فَقَالُوا عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ  
 الظَّالِمِينَ ﴿٨٥﴾ وَجَنَّا بِرَحْمَتِكَ مِنَ الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿٨٦﴾  
 وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ وَأَخِيهِ أَن تَبَوَّءَا لِقَوْمِكُمَا  
 بِمِصْرَ بَيْوتًا وَاجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قِبْلَةً وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَبِئْسَ  
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٧﴾ وَقَالَ مُوسَىٰ رَبَّنَا إِنَّكَ ءَاتَيْتَ  
 فِرْعَوْنَ وَمَلَئَهُ زِينَةً وَأَمْوَالًا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا رَبَّنَا  
 لِيُضِلُّوا عَن سَبِيلِكَ رَبَّنَا اطْمِسْ عَلَيَّ أَمْوَالَهُمْ وَاشْدُدْ  
 عَلَيَّ قُلُوبَهُمْ فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّىٰ يَرُوا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٨٨﴾  
 قَالَ قَدْ أُجِيبَت دَعْوَتُكُمَا فَاسْتَقِيمَا وَلَا تَتَّبِعَان سَبِيلَ  
 الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨٩﴾

وَقَالَ فِرْعَوْنُ أَتُنُونِي بِكُلِّ سَجْرٍ  
 عَلِيمٍ ﴿٧٩﴾ فَلَمَّا جَاءَ السَّحْرَةَ قَالَ  
 لَهُمْ مُوسَىٰ أَلْقُوا مَا أَنْتُمْ مُلقُونَ  
 ﴿٨٠﴾ فَلَمَّا أَلْقَوْا قَالَ مُوسَىٰ مَا  
 جِئْتُمْ بِهِ السَّحْرُ إِنَّ اللَّهَ سَيُبْطِلُهُ  
 إِنَّ اللَّهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ  
 ﴿٨١﴾ وَيُحِقُّ اللَّهُ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ  
 كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴿٨٢﴾

79. "Na Firauni akasema: Nileteeni kila mchawi Mjuzi!"

80. "Basi walipo kuja wachawi, Musa aliwa-ambia: Tupeni mnavyo tupa"

81. "Walipotupa, Musa alisema: Mliyoleta ni uchawi. Hakika Mwenyezi Mungu Haitengenezi kazi ya waharibifu."

82. "Na Mwenyezi Mungu Huthibitisha Haki kwa Maneno Yake, hata wanga lichukia wakosefu."

**Baina ya Nabii Musa عليه السلام na Wachawi.**

Allah تعالى Alitaja kisa cha wachawi pamoja na Musa عليه السلام katika *Surat Al-Araaf* na maelezo yake yalikwishatangulia katika Surah hiyo, pia yapo katika Surah hii, *Twaha* na *Ash-Shu'araa*. Nayo ni kwamba, Firauni, Allah تعالى Amlaani, alitaka kuwahadaa watu na kuipinga haki bayana aliyokuja nayo Musa عليه السلام kwa kiini macho cha wachawi na wana mazingaombwe. Matokeo yakawa kinyume kabisa, na hivyo hakulifikia lengo lake, ushahidi wa Mola Ukadhihiri katika mahafali hayo.

وَأَلْقَى السَّحْرَةَ سَاجِدِينَ ﴿١٢٠﴾ قَالُوا ءَأَمَّنَّا بِرَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٢١﴾ رَبِّ مُوسَى وَهَارُونَ ﴿١٢٢﴾

***“Na wachawi wakapomoka wakisujudu. Wakasema: Tume muamini Mola Mlezi wa viumbe vyote. Mola Mlezi wa Musa na Harun”. (7:120-122)***

Firauni Alidhani kwamba atapata ushindi kwa kuwatumia wachawi dhidi ya Mjumbe aliyetumwa na Allah تعالى Ambaye ni Mjuzi wa siri zote. Akashindwa, akaipoteza Jannah na akawajibikiwa na Moto.

وَقَالَ فِرْعَوْنُ أَتُنْتُونِي بِكُلِّ سَاحِرٍ عَلِيمٍ ﴿١٢٣﴾ فَلَمَّا جَاءَ السَّحْرَةَ قَالَ لَهُمْ مُوسَى أَلْقُوا مَا أَنْتُمْ مُلْقُونَ ﴿١٢٤﴾

***“Na Firauni akasema: Nileteeni kila mchawi Mjuzi! Basi walipo kuja wachawi, Musa aliwaambia: Tupeni mnavyotupa!”***

Kwa hakika! Aliyasema hayo kwa sababu walijipanga safu wakiwa wameahidiwa kuwa karibu na Firauni na kupewa zawadi maridhawa.

قَالُوا يَمْوَسَىٰ ءِإِمَّا أَنْ تُتْلَىٰ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَلْقَىٰ ﴿١٢٥﴾ قَالَ بَلْ أَلْقُوا ﴿١٢٦﴾

***“Wakasema: Ewe Musa! Je! Utatupa wewe, au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa? Akasema: Bali tupeni nyinyi!” (20:65-66)***

Musa عليه السلام alitaka wao ndio waanze ili watu wayaone waliyoyafanya, kisha ukweli uje baada yake ili aishinde batili yao. Kwa hivyo, walipotupa, waliyaroga macho ya watu na kuwatia hofu, na walikuja na sihiri kubwa.

فَأَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُوسَى ﴿٧٧﴾ قُلْنَا لَا تَخَفْ إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعْلَى ﴿٧٨﴾ وَأَلْقَى مَا  
فِي يَمِينِكَ تَلْقَفَ مَا صَنَعُوا إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سِحْرٍ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَى ﴿٧٩﴾

**“Basi Musa ikaingia khofu nafsi yake. Tukasema: Usikhofu! Hakika wewe ndiye utakayeshinda. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyoviunda. Hakika walivyoviunda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo.”** (20:67-69)

Wakati huo, Musa عليه السلام alisema baada ya wao kutupa.

مَا جِئْتُمْ بِهِ السِّحْرَ إِنَّ اللَّهَ سَبَّطِلُكُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٨٠﴾ وَيُحِقُّ اللَّهُ  
الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴿٨١﴾

**“Mliyoleta ni uchawi. Hakika Mwenyezi Mungu Haitenganezi kazi ya waharibifu. Na Mwenyezi Mungu Huithibitisha Haki kwa Maneno yake, hata wangalichukia wakosefu.”**

فَمَا ءَامَنَ لِمُوسَىٰ إِلَّا ذُرِّيَّةٌ مِّن قَوْمِهِ عَلَىٰ خَوْفٍ مِّن فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِمْ أَن يَفْتِنَهُمْ  
وَإِنَّ فِرْعَوْنَ لَعَالٍ فِي الْأَرْضِ وَإِنَّهُ لَمِنَ الْمُسْرِفِينَ ﴿٨٢﴾

**83. “Basi hawakumuamini Musa isipokuwa baadhi ya Vijana wa kaumu yake, kwa kumuogopa Firauni na wakuu wao wasiwatese. Kwani hakika Firauni alikuwa jeuri katika nchi. Na kwa yakini alikuwa miongoni mwa waliopita kiasi.”**

**Vijana Wachache tu Katika Kaumu ya Firauni Ndio Waliomuamini Musa عليه السلام.**

Allah تعالى Anaeleza kwamba hawakumuamini Musa عليه السلام pamoja na Ishara bayana, hoja zisizopingika na ushahidi dhahiri, isipokuwa vijana wachache kutoka katika kaumu ya Firauni.

Hata hivyo, walikuwa wakimkhofu Firaun na wakuu wake kuwarudisha katika ukafiri waliokuwemo hapo kabla, kwani Firauni - Allah Amlaani - alikuwa muovu mkorofi, aliyezidi sana kwa kiburi na ufidhuli.

فَمَا ءَامَنَ لِمُوسَىٰ إِلَّا ذُرِّيَّةٌ مِّن قَوْمِهِ عَلَىٰ خَوْفٍ مِّن فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِمْ أَن يَفْتِنَهُمْ<sup>٤</sup>

**“Basi hawakumuamini Musa isipokuwa baadhi ya Vijana wa kaumu yake, kwa kumwogopa Firauni na wakuu wao wasiwatese.”**

Akasema: “Ni watu wachache tu katika kizazi cha kaumu ya Wana wa Israil, waliomuamini Musa عليه السلام. Miongoni mwao alikuwemo mke wa Firauni, Muumini aliyekuwa akiificha imani yake, mweka hazina wa Firauni na mkewe”<sup>1</sup>. Ama kuhusu Wana wa Israili, lililo mashuhuri ni kwamba wote walimuamini Musa عليه السلام. Walifurahia kuja kwake na walikuwa wakizijua sifa zake na bishara zake kutoka katika Vitabu vilivyotangulia. Walijua kuwa Allah تعالى Atawaokoa kutokana na kutekwa na Firauni na kuwapa ushindi dhidi yake. Kwa hivyo, baada ya habari hii kumfikia Firauni, akachukua kila namna ya tahadhari, lakini haikumsaidia kitu. Musa عليه السلام alipowajia, basi Firauni aliwasumbua kwa kiasi kikubwa sana.

قَالُوا أَوَإِذِينَا مِن قَبْلِ أَن تَأْتِيَنَا وَمِن بَعْدِ مَا جِئْتَنَا قَالَ عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ  
وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿٧٩﴾

**“Wakasema: Tumeudhiwa kabla hujatufikia, na baada ya wewe kutujia! Musa akasema: Huenda Mola wenu Mlezi Akamhiliki adui wenu, na Akakufanyeni nyinyi ndio wa kufuatia kushika nchi, ili Atazame mtakavyokuja tenda nyinyi.” (7:129)**

Miongoni mwa yanayojulisha kwamba Wana wa Israil kulikuwa na Muumini mmoja tu, ni Kauli ya Allah تعالى:

وَقَالَ مُوسَىٰ يَنْقُومِ إِن كُنتُمْ ءَامَنتم بِاللّهِ فَعَلَيْهِ تَوَكَّلُوا إِن كُنتُمْ مُّسْلِمِينَ ﴿٨٠﴾ فَقَالُوا عَلَىٰ  
اللّهِ تَوَكَّلْنَا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ الظّٰلِمِينَ ﴿٨١﴾ وَجِئْنَا بِرَحْمَتِكَ مِنَ الْقَوْمِ  
الْكٰفِرِينَ ﴿٨٢﴾

**84. “Na Musa alisema: Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 15:164



**85. "Wakasema: Tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Ewe Mola wetu Mlezi! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhalimu."**

**86. "Na Utuokoe kwa Rehema Yako na watu makafiri."**

**Musa عليه السلام Aliwatumainisha Kaumu Yake Wamtegemee Allah تعالى.**

Allah تعالى Anatoa habari za Musa عليه السلام kwamba aliwaambia Wana wa Israili;

يَنْقُومُ إِن كُنْتُمْ ءَامِنْتُمْ بِاللَّهِ فَعَلَيْهِ تَوَكَّلُوا إِن كُنْتُمْ مُسْلِمِينَ

**"Enyi watu wangu! Ikiwa nyinyi mmemuamini Mwenyezi Mungu, basi mtegemeeni Yeye, ikiwa nyinyi ni Waislamu."**

Kwa maana: Allah تعالى Anatosha kwa wanaomtegemea.

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ

**"Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtoshela mja wake?" (39:36)**

وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ

**"Na anayemtegemea Mwenyezi Mungu, Yeye Humtoshia." (65:3)**

Mara nyingi Allah تعالى Hutaja ibada na kumtegemea pamoja, kama katika Kauli Yake nyingine.

فَاعْبُدْهُ وَتَوَكَّلْ عَلَيْهِ

**"Basi muabudu Yeye na umtegemee Yeye." (11:123)**

قُلْ هُوَ الرَّحْمَنُ ءَامَنَّا بِهِ وَعَلَيْهِ تَوَكَّلْنَا

**"Sema: Yeye Ndiye Mwingi wa Rehema; tunamuamini Yeye, na juu Yake tunategemea." (67:29)**

رَبِّ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاتَّخِذْهُ وَكِيلًا

**'Mola Mlezi wa Mashariki na Magharibi, hapana mola isipokuwa Yeye, basi mfanye kuwa Mtegemewa wako.' (73:9)**

Allah تعالى Amewaamuru Waumini waseme mara nyingi katika kila Sala zao;

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴿٥﴾

**“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada.” (1:5)**

Wana wa Israil walilifuata hilo, kwani walisema;

عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٦﴾

**“Tunamtegemea Mwenyezi Mungu. Ewe Mola wetu Mlezi!  
Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na hao watu madhalimu.”**

Na hii ina maana, Usiwape ushindi juu yetu wakatutawala, na wakadhani kwamba imekuwa hivyo kwa kuwa katika ukweli, na si katika batili. Huu utakuwa ni mtihani (wa Kuwahadaa) wao. Maana hii ilielezwa kutoka kwa Abu Mijlaz na Abu Adh-Dhuha,<sup>1</sup> Abdur-Razzaq alimnukuu Mujahid kuwa, alisema;

رَبَّنَا لَا تَجْعَلْنَا فِتْنَةً لِّلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٦﴾

**“Ewe Mola wetu Mlezi! Usitufanye wenye kutiwa misukosuko na  
hao watu madhalimu.”**

Maana yake: Usiwaachilie juu yetu, kiasi kwamba wakatufanyia mtihani.<sup>2</sup>

Kauli ya Allah تعالى;

وَجِئْنَا بِرَحْمَتِكَ

**“Na Utuokoe kwa rehema Yako.”**

Maana yake: Tupe nusura kwa rehema na ihsani Yako.

مِنَ الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ

**“...na watu makafiri.”**

Maana yake: Walioukataa ukweli na kuuficha, nasi tumekuamini Wewe na tunatawakali Kwako.

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ وَأَخِيهِ أَنْ تَبَوَّءَا لِقَوْمِكُمَا بِمِصْرَ بَيْوتًا وَأَجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قِبْلَةً

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآذِنُوا الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٧﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 15:169.

<sup>2</sup> Abdur-Razzaq 2:297.

**87. “Na Tukampelekea Musa na Ndugu yake wahyi huu: Watengenezeeni majumba watu wenu katika Misri na zifanyeni nyumba zenu ndio mahali mwa ibada, na mshike Sala na wabashirie Waumini”.**

### **Waliamriwa Wasali Majumbani Mwao.**

Allah تعالی Anataja sababu na namna Alivyowaokoa na kuwanusuru Wana wa Israili dhidi ya Firauni na kaumu yake. Hayo ni kwamba, Allah تعالی Alimuamuru Musa عليه السلام na nduguye, Harun عليه السلام achukue nyumba kadha kwa ajili ya kaumu yao. Kauli ya Allah تعالی:

وَأَجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قِبْلَةً

**“...na zifanyeni nyumba zenu ndio mahali mwa ibada”.**

Al-‘Awfi alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما aliitafsiri Aya hii. Alisema: “Wana wa Israil walimuambia Musa عليه السلام: “Sisi Hatuwezi kudhihirisha Sala zetu kwa watu wa Firaun”. Allah تعالی Akawapa idhini wasali majumbani mwao. Wakaamriwa wajenge nyumba zao kuelekea Qibla”<sup>1</sup>. Mujahid Alisema;

وَأَجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قِبْلَةً

**“...na zifanyeni nyumba zenu ndio mahali mwa ibada”.**

“Wana wa Israil walipomkhofu Firauni kuwaua katika mikusanyiko ya kwenye mahekalu yao, waliamriwa wazifanye nyumba zao kuwa mahala pa kusalia kwa kuzielekeza Qibla na kusali humo kisirisiri”<sup>2</sup>. Hili lilielezwa na Qatada na Adh-Dhahak”<sup>3</sup>.

وَقَالَ مُوسَى رَبَّنَا إِنَّكَ آتَيْتَ فِرْعَوْنَ وَمَلَأَهُ زِينَةً وَأَمْوَالًا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا رَبَّنَا لِيُضِلُّوهُ عَنِ سَبِيلِكَ رَبَّنَا اطْمِسْ عَلَيَّ أَمْوَالَهُمْ وَاشْدُدْ عَلَيَّ قُلُوبَهُمْ فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّى يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٧٩﴾ قَالَ قَدْ أُجِيبَت دَعْوَتُكُمْ مَا فَاسْتَقِيمَا وَلَا تَتَّبِعَانِ سَبِيلَ الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٨٠﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 15:174.

<sup>2</sup> At-Tabari 15:174.

<sup>3</sup> At-Tabari 15:173.

**88. “Na Musa akasema: Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe Umempa Firauni na wakuu wake mapambo na mali katika maisha ya dunia. Hivyo wanapoteza watu na njia yako. Mola wetu Mlezi! Yafutilie mbali mali yao na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu.”**

**89. “Mwenyezi Mungu Akasema: Maombi yenu yamekubaliwa. Basi simameni sawa sawa, wala msifuate njia za wale wasiojua.”**

### Dua ya Nabii Musa عليه السلام Dhidi ya Firauni na Wakuu Wake.

Haya ni maelezo toka kwa Allah تعالى juu ya aliyoyaomba Musa عليه السلام dhidi ya Firauni na wakuu wake baada ya kukataa kwao kuukubali ukweli na kuendelea na upotevu, kufuru, majivuno, inadi, udhalimu na uasi, na kiburi. Musa عليه السلام alisema;

رَبَّنَا إِنَّا أِتَيْنَاكَ أَتَيْنًا فِرْعَوْنَ وَمَلَأَهُ زِينَةً

**“Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe mmempa Firauni na wakuu wake mapambo”.**

Kwa maana: Katika samani za kidunia.

وَأَمْوَالًا

**“...na mali...”.** Nyingi sana.

فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا رَبَّنَا لِيُضِلُّوا عَن سَبِيلِكَ

**“...katika maisha ya dunia. Hivyo wanapoteza watu na njia yako”.**

Baadhi yao, husoma, “Liyadhwillu”, Maana: Umewapatia, na Wewe Unajua kuwa hawayaamini uliyonituma kwayo. Umefanya hivyo kwa ajili ya kuwavuta taratibu. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

لَتَفْتَنَّهُمْ فِيهِ

**“...ili Tuwajaribu...” (20:131) na (72:17)**

Wengine husoma, “Liyadillu na Liyudillu”, Maana: ili wapewe mtihani kwa kile Ulichowapa viumbe wako Uliowataka. Wale Uliowaacha wapotee,

watadhani kwamba Wewe Umewapa haya kwa sababu ya Kuwapenda na Kuwajali.

رَبَّنَا أَطْمَسْنَا عَلَىٰ أَمْوَالِنَا

**“Mola wetu Mlezi! Yafutilie mbali mali yao.”**

Alisema Ibn ‘Abbas na Mujahid: “Maana yake: Azihiliki mali zao”<sup>1</sup>. Allah تعالى Alizifanya mali zao kuwa mawe yaliyonakishiwa kama hapo awali”<sup>2</sup>. Kauli ya Allah تعالى;

وَأَشَدُّ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ

**“...na zifunge nyoyo zao.”**

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Maana yake: Zitie muhuri juu yake”<sup>3</sup>.

فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ

**“...wasiamini mpaka waione adhabu chungu.”**

Dua hii ya Musa عليه السلام ilitokana na ghadhabu kwa ajili ya Allah تعالى na kwa dini Yake, dhidi ya Firauni na wakuu wake alipobaini kwamba hakuna kheri kwao. Ni kama alivyoomba dua Nuh عليه السلام. Aliposema;

رَبِّ لَا تَذَرْ عَلَى الْأَرْضِ مِنَ الْكَافِرِينَ دَيَّارًا ﴿٦٦﴾ إِنَّكَ إِن تَذَرَهُمْ يُضِلُّوْا عِبَادَكَ وَلَا يَلِدُوْا إِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا ﴿٦٧﴾

**“Mola wangu Mlezi! Usimuache juu ya ardhi mkazi wake yeyote katika makafiri! Hakika Ukiwaacha watawapoteza waja wako, wala wao hawatazaa ila waovu makafiri.” (71:26-27)**

Kwa ajili hii Allah تعالى Alimjibu Musa عليه السلام dua hii ambayo nduguye, Harun عليه السلام aliitikia Amin. Allah تعالى Alisema;

قَدْ أُجِيبَت دَعْوَتُكُمْ

**“Maombi yenu yamekubaliwa.”** Maana: Tumekwisha kujibuni (nyinyi wawili) mlichokiomba kuhusu kuiangamiza jamaa ya Firauni. Allah تعالى Alisema;

<sup>1</sup> At-Tabari 15:180.

<sup>2</sup> At-Tabari 15:181.

<sup>3</sup> At-Tabari 15:181.

قَدْ أُجِيبَت دَعْوَتُكُمْ فَاَسْتَقِيمَا

***“Maombi yenu yamekubaliwa. Basi simameni sawa sawa”.***

Maana yake: Kama mlivyojibiwa dua zenu, basi msimame imara katika Amri Yangu. Ibn Jurayj alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Muwe imara na muifuate amri yangu.”<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> At-Tabari 15:187.

\* وَجَنُوزَنَا بِنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ  
 فَاتَّبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجَنُودُهُ بَغِيًّا  
 وَعَدْوًا ۗ حَتَّىٰ إِذَا أَدْرَكَهُ الْغَرَقُ قَالَ  
 ءَامَنْتُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا الَّذِي ءَامَنْتُ  
 بِهِ بَنُو إِسْرَائِيلَ وَأَنَا مِنَ  
 الْمُسْلِمِينَ ﴿٩٠﴾ ءَأَلْفَنُ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ  
 وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾ فَالْيَوْمَ  
 نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِيَتَكُونَ لِمَنْ  
 خَلَفَكَ ءَايَةً ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ  
 النَّاسِ عَنْ ءَايَاتِنَا لَغَافِلُونَ ﴿٩٢﴾  
 وَلَقَدْ بَوَّأْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ مَبُوءًا  
 صَدَقِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِّنَ  
 الطَّيِّبَاتِ فَمَا اخْتَلَفُوا حَتَّىٰ جَاءَهُمُ  
 الْعِلْمُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ  
 يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
 فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٩٣﴾  
 فَإِنْ كُنْتَ فِي شَكٍّ مِّمَّا أَنْزَلْنَا  
 إِلَيْكَ فَسْئَلِ الَّذِينَ  
 يَقْرَأُونَ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكَ ۗ  
 لَقَدْ جَاءَكَ الْحَقُّ مِنْ  
 رَبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ  
 الْمُمْتَرِينَ ﴿٩٤﴾ وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ  
 الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ  
 فَتَكُونَ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٥﴾  
 إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ  
 كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٩٦﴾  
 وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ ءَايَةٍ حَتَّىٰ  
 يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٩٧﴾

\* وَجَنُوزَنَا بِنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ  
 فَاتَّبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ وَجَنُودُهُ بَغِيًّا  
 وَعَدْوًا ۗ حَتَّىٰ إِذَا أَدْرَكَهُ الْغَرَقُ قَالَ  
 ءَامَنْتُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا الَّذِي ءَامَنْتُ  
 بِهِ بَنُو إِسْرَائِيلَ وَأَنَا مِنَ  
 الْمُسْلِمِينَ ﴿٩٠﴾ ءَأَلْفَنُ وَقَدْ عَصَيْتَ  
 قَبْلُ وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾  
 فَالْيَوْمَ نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِيَتَكُونَ  
 لِمَنْ خَلَفَكَ ءَايَةً ۗ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ  
 النَّاسِ عَنْ ءَايَاتِنَا لَغَافِلُونَ ﴿٩٢﴾

90. "Tukawavusha bahari Wana wa Israili, na Firauni na askari wake waka-wafuata kwa dhulma na uadui. Hata Firauni alipo-kuwa anataka kuzama akasema: Naamini kuwa hapana mola ila yule waliyemuamini Wana wa

*Israili, na mimi ni miongoni mwa walio nyenyekea!"*

91. "Ala! Sasa? Na hali uliasi kabla yake na ukawa miongoni mwa mafisadi!"

92. "Leo, basi, Tutauokoa mwili wako, ili uwe ishara kwa ajili ya walio nyuma yako. Na hakika watu wengi wameghafilika na Ishara Zetu."

### Wana wa Israili Waliokolewa na Watu wa Firauni Wakagharikishwa.

Allah تعالى Anataja namna Alivyomgharikisha Firauni na majeshi yake. Baada ya Wana wa Israili kutoka Misri pamoja na Musa عليه السلام. Inasemekana kwamba walikuwa laki sita, pamoja na vizazi vyao. Walikuwa wamekopa mapambo mengi kutoka kwa Wamisri. Wakatoka pamoja nayo. Firauni akawaghadhibikia sana. Kwa hivyo akatuma ujumbe katika kila mji kumkusanyia askari wake kutoka katika majimbo yake. Akapanda kipando na kuwafuata nyuma yao akiwa amejazwa majivuno mengi na majeshi makubwa. Allah تعالى Alilitaka hili kwao, wala hapana hata mmoja aliyesalia nyuma ambaye alikuwa na mamlaka na Utawala katika mamlaka ya Firauni. Wakawakuta Wana wa Israili wakati wa mawio.

﴿قَلَّمَا تَرَاءَا أَلْجَمْعَانَ قَالَ أَصْحَبُ مُوسَى إِنَّا لَمُدْرِكُونَ﴾

**“Na yalipoonana majeshi mawili haya, watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana!” (26:61)**

Waliyasema hayo kwa sababu walipofika pwani ya bahari, huku Firauni akiwa nyuma yao, na hakukubakia kingine, isipokuwa majeshi mawili yapigane. Watu wa Musa عليه السلام wakauliza kwa shauku, “Leo tutaokolewa vipi?” Akawajibu: “Mimi nimeamrisha nipite hapa”.

﴿قَالَ كَلَّا إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهْدِينِ﴾

**“Hasha! Hakika Yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye Ataniongoa!” (26:62)**

Jambo lilipozidi kuwa la dhiki sana, mara likawa jepesi. Allah تعالى Akamuamuru apige bahari kwa fimbo yake. Akaipiga, nayo bahari ikaachia mwanya na kila fungu likawa kama mlima mkubwa, zikatokea njia kumi na mbili, kila moja kwa kabila moja wapo la Wana wa Israili. Allah تعالى Akauamuru upepo ukaikausha ardhi Yake.

﴿فَأَضْرَبَ لَهُمْ طَرِيقًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا لَا تَخَفُ دَرَكًا وَلَا تَخْشَى﴾

**“...na uwapigie njia kavu baharini. Usikhofu kukamatwa, wala Usiogope”. (20:77)**



Maji yalikuwa yakitoka baina ya njia hizo kama vile madirisha ili kila kaumu iwaone wengine na wasidhani kwamba ni wenye kuhiliki. Wa mwisho wao alipotoka, Firauni na majeshi yake wakafika katika ukingo wa Pwani ya upande mwingine. Alikuwa pamoja na Wapanda farasi weusi mia moja pamoja na farasi wa rangi nyingine. Alipoyaona hayo alishikwa na khofu kubwa, akaduwa na kuogopa, akataka kurudi nyuma, lakini wapi! Umewadia wakati usio-kwepeka. Kudura imepenya na dua imejibiwa.

Jibril عليه السلام akaja juu ya farasi aliyekuwa akipiga kelele. Akapita kando ya farasi wa Firauni. Farasi wa Jibril عليه السلام akamtotea mlio yule wa Firauni, Jibril عليه السلام akakimbilia baharini na Firauni akamfuata humo. Firauni hakujimudu tena, akataka kuwatotea sauti kubwa wakuu wake. Akasema: "Wana wa Israili hawana haki na bahari zaidi yetu". Wote wakakimbilia baharini. Mikaili عليه السلام alikuwa nyuma yao akiwaswaga. Hakumuacha hata mmoja kati yao, bali alimkutanisha nao. Walipoingia wote katika maji kwa ukamilifu, na wa kwanza wao alipokusudia kutoka humo (upande wa pili), Allah تعالى, Mwenye Nguvu, Aliiamuru bahari kuwakwamisha. Ikawakwamisha, na hakunusurika hata mmoja, na mawimbi yakawa yanawainua na kuwashusha chini. Mawimbi yakajilimbikiza juu ya Firauni. Akaelemewa na bumbuazi la mauti. Huku akiwa katika hali hiyo, alisema;

أَنْتُمْ لَا إِلَهَ إِلَّا الَّذِي ءَامَنْتُمْ بِهِ بَنُو إِسْرَائِيلَ وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ

***"Naamini kuwa hapana mola ila Yule waliyemuamini Wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa walionyenyekaa!"***

Akaamini katika wakati ambapo imani hainufaishi.

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدَّهُ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿٨٤﴾ فَلَمَّ يَكُ يَنْفَعُهُمْ إِيمَانُهُمْ لَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا ۗ سُنَّتَ اللَّهُ الَّتِي قَدْ خَلَتْ فِي عِبَادِهِ ۗ وَخَسِرَ هُنَالِكَ الْكَافِرُونَ ﴿٨٥﴾

***"Walipoiona adhabu Yetu walisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa Pekee, na tunaikataa miungu tuliyo kuwa tukiishirikisha Naye. Lakini imani yao haikuwa yenye kuwafaa kitu wakati ambao wamekwishaiona adhabu Yetu. Huu ndio mwendo wa Mwenyezi Mungu uliokuwa kwa waja wake. Na hapo waliokufuru walikhasiri". (40:84-85)***

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema katika Kumjibu Firauni aliyoyasema;

ءَأَلْتَنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ

**“Ala! Sasa? Na hali uliasi kabla yake”.**

Maana yake: Sasa ndio unasema hivyo, ilhali umeasi yaliyokuwa baina yako na Yeye kabla ya haya.

وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ

**“...na ukawa miongoni mwa mafisadi!”**

Maana yake: Wanaowapoteza watu ardhini.

وَجَعَلْنَاهُمْ أُمَّةً يَدْعُونَ إِلَى النَّارِ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يُنصَرُونَ ﴿٤١﴾

**“Na Tuliwafanya ni waongozi waitao kwenye Moto. Na Siku ya Kiyama hawatanusuriwa.” (28:41)**

Haya ndiyo Aliyosimulia Allah تعالى kumhusu Firauni kwa sababu ya kauli na hali yake hiyo. Hizi ni miongoni mwa siri za ghaibu ambazo Allah تعالى Alimjulisha Mjumbe Wake. Kwa ajili hii, Abu Dawud At-Twayalisi رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما, alisema kwamba Mtume ﷺ alisema;

«قَالَ لِي جِبْرِيلُ: لَوْ رَأَيْتَنِي وَأَنَا آخِذٌ مِنْ حَالِ الْبَحْرِ فَأَدُّشُهُ فِي فَمٍ فِرْعَوْنَ مَخَافَةَ أَنْ تُذْرِكَهُ الرَّحْمَةُ»

*“Jibril aliniambia: “Lau ungeliniona Nilipokuwa nikiuchukua mchanga mweusi wa baharini na kuutia kinywani kwa Firauni kwa kuchelea kwamba asipatwe na rehema”<sup>1</sup>.*

Abu ‘Isa At-Tirmidhi رحمه الله تعالى<sup>2</sup> na Ibn Jarir رحمه الله تعالى<sup>3</sup> pia waliinukuu. At-Tirmidhi alisema, *“Hasan Gharib Sahih”*. Kauli ya Allah تعالى;

<sup>1</sup> Musnad At-Tayalis na. 341.

<sup>2</sup> Tufhat Al-Ahwadhi 8:526.

<sup>3</sup> At-Tabari 15:190-191.

فَالْيَوْمَ نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِتَكُونَ لِمَنْ خَلَقَكَ آيَةً

**“Leo, basi, Tutakuokoa kwa mwili wako, ili uwe ishara kwa ajili ya walio nyuma yako. Na hakika watu wengi wameghafilika na ishara Zetu.”**

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما na wengineo katika *Salaf* walisema: “Baadhi ya Wana wa Israili walitia shaka juu ya mauti ya Firauni, Allah تعالى Akaiamrisha bahari itupe mwili wake mzima pasi na roho, akiwa na dirizi yake mashuhuri. Mwili huo ulitupwa mahali pa juu nchi kavu ili Wana wa Israili wakithibitisha kifo chake na Hilaki yake”<sup>1</sup>. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

فَالْيَوْمَ نُنَجِّيكَ

**“Leo, basi, Tutakuokoa”.**

Maana yake: Tunakuweka mahali pa juu ardhini.

بِبَدَنِكَ

**“...kwa mwili wako”.**

Mujahid alisema maana ya *Badanik* ni “Mwili wako halisi.”<sup>2</sup> Kauli ya Allah تعالى:

لِتَكُونَ لِمَنْ خَلَقَكَ آيَةً

**“...ili uwe ishara kwa ajili ya walio nyuma yako.”**

Maana: Ili iwe dalili kwa Wana wa Israili juu ya mauti na Hilaki yako.

Na kwamba, Allah تعالى Ndiye Muweza Ambaye Anavidhibiti viumbe vyote, na kwamba hapana chochote cha kuweza kuhimili ghadhabu Yake.

وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ النَّاسِ عَنَّا لَعَفِيلُونَ ﴿١٧﴾

**“Na hakika watu wengi wameghafilika na ishara Zetu.”**

Maana yake: Hawawaidhiki nazo wala kuzingatia.

<sup>1</sup> At-Tabari 15:196.

<sup>2</sup> At-Tabari 15:197.

Kuangamizwa kwao kulitokea katika siku ya *Ashuraa*. Ni sawa na alivyonukuu Bukhari kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, alisema: Mtume ﷺ aliwasili Madina, na kukuta Mayahudi wakifunga katika siku ya *Ashuraa*. Akasema;

«مَا هَذَا الْيَوْمِ الَّذِي تَصُومُونَهُ؟»

“Hii ni siku gani mnayofunga.”

Wakasema: “Hii ndio siku ambayo Musa عليه السلام alimshinda Firauni”. Mtume ﷺ akasema;

«أَنْتُمْ أَحَقُّ بِمُوسَى مِنْهُمْ فَصُومُوهُ»

“Nyinyi mnastahiki zaidi kwa Musa kuliko wao, basi fungeni.”<sup>1</sup>

وَلَقَدْ بَوَّأْنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ مُبَوَّأً صِدْقٍ وَرَزَقْنَاهُمْ مِّنَ الطَّيِّبَاتِ فَمَا اخْتَلَفُوا حَتَّىٰ  
جَاءَهُمُ الْعِلْمُ إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ﴿٩٣﴾

**93. “Na hakika Tuliwaweka Wana wa Israili kikao chema, na Tukawaruzuku vitu vizuri. Nao hawakukhitalifiana mpaka ilipowafikia ilimu. Hakika Mola wako Mlezi Atahukumu baina yao Siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakikhitalifiana.”**

**Kuwekwa kwa Wana wa Israili Katika Ardhi na Kuruzukiwa Vitu Vizuri.**

Katika Aya zifuatazo Allah تعالى Anazungumzia juu ya neema za kidini na kidunia Alizowafadhili Wana wa Israili. Kauli ya Allah تعالى;

مُبَوَّأً صِدْقٍ

“...**kikao chema**”. Ilisemwa: Ni nchi ya Misri na Sham kuzunguka *Baytul-Muqaddas*, kwani Allah تعالى Alipowahiliki Firauni na askari wake, Dola ya Musawiyyah ilichukua nafasi katika nchi ya Misri yote. Sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى;

وَأَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضَعُونَ مَشْرِقَ الْأَرْضِ وَمَغْرِبَهَا الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا  
وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ بِمَا صَبَرُوا ۖ وَدَمَّرْنَا مَا كَانَ يَصْنَعُ  
فِرْعَوْنُ وَقَوْمُهُ وَمَا كَانُوا يَعْرِشُونَ ﴿٩٤﴾

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 8:198

**“Na Tukawarithisha watu waliokuwa wanadharauliwa Mashariki na Magharibi ya ardhi Tuliyoibariki. Na likatimia neno jema la Mola Mlezi wako juu ya Wana wa Israili, kwa vile walivyosubiri. Na Tukayaangamiza aliyokuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake, na waliyokuwa wakiyajenga.” (7:137)**

Allah تعالی Akasema katika Aya nyingine;

فَأَخْرَجْنَاهُمْ مِّن جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٥٧﴾ وَكُنُوزٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ ﴿٥٨﴾ كَذَلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٩﴾

**“Basi Tukawatoa katika bustani na chemchem. Na khazina na vyote vya heshima. Kadhaalika; na tukawarithisha hayo Wana wa Israili.” (26:57-59)** Na Allah تعالی Amesema:

كَمْ تَرَكُوا مِّن جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٥٧﴾

**“Bustani ngapi na chemchem ngapi waliziacha!” (44:25-27)**

Hata hivyo, waliendelea pamoja na Musa عليه السلام kuelekea Baytul-Muqaddas (Jerusalem), nchi ya Al-Khalil Ibrahim عليه السلام. Musa عليه السلام na aliokuwa nao waliendelea kwenda Baytul-Muqaddas, mji ambao ulikuwa na majitu makubwa. Wana wa Israil wakakataa kupigana nao. Allah تعالی Akawafukuza kwenda katika jangwa kwa miaka arubaini. Katika muda huo alifariki Harun عليه السلام kisha Musa عليه السلام. Wana wa Israil wakatoka baada yao, pamoja na Yusha bin Nun. Allah تعالی Akawapa ushindi wa kuikomboa ardhi Takatifu “Baytul-Muqaddas” na wakatawala kwa muda fulani. Kauli ya Allah تعالی;

وَرَزَقْنَاهُمْ مِّنَ الطَّيِّبَاتِ

**“...na Tukawaruzuku vitu vizuri...”** Maana yake: Riziki nzuri za halali zenye manufaa ambazo ni nzuri kitabia na kwa Sharia. Kauli ya Allah تعالی,

فَمَا اخْتَلَفُوا حَتَّىٰ جَاءَهُمُ الْعِلْمُ ﴿٥٩﴾

**“Nao hawakukhitalifiana mpaka ilipowafikia ilimu”**. Maana yake: Hawakutofautiana katika masuala yoyote isipokuwa baada ya kujiwa na elimu. Maana yake, wala haikutakikana kwamba wakhitalifiane ilhali, Allah تعالی Alikwishabainisha na Akawaondolea utata. Na imekuja katika Hadithi ya Mtume

«إِنَّ الْيَهُودَ اخْتَلَفُوا عَلَىٰ إِحْدَىٰ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، وَإِنَّ النَّصَارَىٰ اخْتَلَفُوا عَلَىٰ اثْنَتَيْنِ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، وَسَتَفْتَرُونَ هَذِهِ الْأُمَّةَ عَلَىٰ ثَلَاثٍ وَسَبْعِينَ فِرْقَةً، مِنْهَا وَاحِدَةٌ فِي الْجَنَّةِ، وَاثْنَتَانِ وَسَبْعُونَ فِي النَّارِ»

*“Kwa hakika! Mayahudi walikhitilafiana katika makundi sabini na moja. Manaswara walitofautiana katika makundi sabini na mbili. Na umma huu utagawanyika katika makundi sabini na matatu. Kati ya hayo, moja ndilo la Janna, na mengine sabini na mbili ni ya Motoni”.*

Palisemwa: “Ni akina nani hao ewe Mtume ﷺ?” Akasema;

«مَا أَنَا عَلَيْهِ وَأَصْحَابِي»

*“Lile ambalo nimo Mimi na Masahaba wangu”<sup>1</sup>.*

Aliinukuu Al-Hakim katika kitabu chake, *Al-Mustadrak* kwa maneno haya. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

إِنَّ رَبَّكَ يَقْضِي بَيْنَهُمْ

*“Hakika Mola wako Mlezi Atahukumu baina yao”.*

Maana yake: Atapambanua baina yao.

يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كَانُوا فِيهِ يَخْتَلِفُونَ

*“Siku ya Kiyama katika yale waliyokuwa wakikhitalifiana”.*

فَإِنْ كُنْتَ فِي شَكٍّ مِّمَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ فَسْأَلِ الَّذِينَ يَفْرَهُونَ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكَ لَقَدْ جَاءَكَ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٩٦﴾ وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِ اللَّهِ فَتَكُونُوا مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٩٨﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٩٩﴾

<sup>1</sup> Al-Hakim 1:129.

94. *“Na ikiwa unayo shaka katika Tuliyo kuteremshia, basi waulize wasomao Kitabu kabla yako. Kwa yakini imekwishakujia Haki kutoka kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wenye shaka.”*

95. *“Na kabisa usiwe miongoni mwa wale wanaozikanusha ishara za Mwenyezi Mungu, usije kuwa katika waliokhasiri.”*

96. *“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini.”*

97. *“Ijapokuwa itawajia kila ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.”*

### Vitabu Vilivyotangulia Vinathibitisha Ujio wa Qur'an

Allah تعالى Alisema;

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَةِ  
وَالْإِنْجِيلِ

*“Ambao kwamba wanamfuata Mtume, Nabii asiyesoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurati na Injili.”*  
(7:157)

Kisha, pamoja na elimu hii wanayoitambua katika Vitabu vyao kama wanavyowatambua watoto wao wanayachanganya hayo, wanayageuza na kuyabadili, wala hawayaamini, pamoja na hoja kusimama dhidi yao.

Allah تعالى Alisema;

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٦﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى  
يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٦٧﴾

*“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwi shathibitika juu yao, hawa taamini. Ijapo kuwa itawajia kila ishara, mpaka waione adhabu iliyo chungu.”*

Maana yake: Hawataamini kwa kunufaika. Hayo ni pindi watakapoamini bila kunufaika na imani. Mfano ni dua ya Musa عليه السلام dhidi ya Firauni na wakuu wake, alisema;

رَبَّنَا أَطْمَسْنَا عَلَىٰ أَمْوَالِهِمْ وَأَشَدُّدَ عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُوا حَتَّىٰ يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٨٨﴾

***“Mola wetu Mlezi! Yafutilie mbali mali yao na zifunge nyoyo zao, wasiamini mpaka waione adhabu chungu.” (10:88)***

Na Allah تعالى Alivyosema,

﴿ وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَيْهِمُ الْمَلٰٓئِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَىٰ وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ قُبُلًا مَا كَانُوا

لِيُؤْمِنُوا إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ يَجْهَلُونَ ﴿١١١﴾

***“Na lau Tungeliwateremshia Malaika, na maiti wakazungumza nao, na Tukawakusanyia kila kitu mbele yao, bado wasingeliamini, ila Mwenyezi Mungu Atake. Lakini wengi wao wamo ujingani.” (6:111)***

Kisha Allah تعالى Alisema;

\* \* \*



فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ ءَامَنَتْ فَفَنَعَمَهَا إِيمَانَهَا إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ  
 لَمَّا ءَامَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ عَذَابَ الْخِزْيِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا  
 وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٩٨﴾ وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي  
 الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا ۖ أَفَأَنْتَ تَكْرَهُ النَّاسَ حَتَّىٰ يَكُونُوا  
 مُؤْمِنِينَ ﴿٩٩﴾ وَمَا كَانَتْ لِنَفْسٍ أَنْ تُؤْمِنَ إِلَّا بِإِذْنِ  
 اللَّهِ ۗ وَيَجْعَلُ الرِّجْسَ عَلَى الَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٠٠﴾ قُلِ  
 أَنْظِرُوا مَاذَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ  
 وَالنُّذُرُ عَنْ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٠١﴾ فَهَلْ يَنْتَظِرُونَ إِلَّا  
 مِثْلَ أَيَّامِ الَّذِينَ خَلَوْا مِن قَبْلِهِمْ ۗ قُلْ فَانْتَظِرُوا إِنِّي  
 مَعَكُمْ مِنَ الْمُنْتَظِرِينَ ﴿١٠٢﴾ ثُمَّ نُنَجِّي رُسُلَنَا  
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ كَذَٰلِكَ حَقًّا عَلَيْنَا نَجِ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةٌ ءَامَنَتْ فَفَنَعَمَهَا  
 إِيمَانَهَا إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ لَمَّا ءَامَنُوا  
 كَشَفْنَا عَنْهُمْ عَذَابَ الْخِزْيِ فِي  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿٩٨﴾

**98. "Kwa nini usiwepo mji  
 mmoja ukaamini na Imani  
 yake ikawafaa – isipokuwa  
 kaumu Yunus? Waliamini  
 na Sisi Tukawaondolea  
 adhabu ya hizaya katika  
 maisha ya dunia, na  
 Tukawastarehesha kwa  
 muda".**

**Imani Wakati wa Adhabu  
 Haikufaa kwa Yeyote  
 Isipokuwa kwa Watu wa  
 Yunus عليه السلام.**

Allah تعالى Anasema; Je, kuna mji wowote uliamini kikamilifu katika umma zilizopita ambazo Tuliwapelekea Mitume? Bali hatukumpeleka Mtume yeyote kabla yako ewe Muhammad ﷺ isipokuwa kaumu yake au wengi wao walimkadhibisha. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى:

يَنْحَسِرُونَ عَلَىٰ آلْعِبَادِ ۖ مَا يَأْتِيهِمْ مِّن رَّسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٣٠﴾

**"Nawasikitikia waja wangu. Hawajii Mtume ila wao humkejeli".  
 (36:30)**

كَذَٰلِكَ مَا آتَىٰ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِم مِّن رَّسُولٍ إِلَّا قَالُوا سَاحِرٌ أَوْ مُجْتَوٍ ﴿٥٢﴾

**"Basi ndio hivyo hivyo, hawakuwajia kabla yao Mitume ila  
 walisema: Huyu ni mchawi au mwendawazimu". (51:52)**

وَكَذَلِكَ مَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ فِي قَرْيَةٍ مِنْ نَذِيرٍ إِلَّا قَالَ مُتْرَفُوهَا إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ  
 أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُّقْتَدُونَ ﴿٤٣﴾

**“Na kadhalika hatukumtuma Muonyaji kwenye mji wowote ila watu wake waliodeka kwa starehe walisema: Hakika sisi tuliwakuta baba zetu wanashika dini makhsusi, na sisi tunafuata nyayo zao”. (43:23) Katika Hadithi Sahih:**

«عَرَضَ عَلَيَّ الْأَنْبِيَاءُ فَجَعَلَ النَّبِيُّ يَمُرُّ وَمَعَهُ الْغَنَامُ مِنَ النَّاسِ، وَالنَّبِيُّ يَمُرُّ مَعَهُ الرَّجُلُ، وَالنَّبِيُّ مَعَهُ الرَّجُلَانِ، وَالنَّبِيُّ لَيْسَ مَعَهُ أَحَدٌ»

**“Manabii walidhihirishwa kwangu. Na kulikuwa na Nabii mmoja aliyekuwa akipita huku akiwa na kundi la watu, Nabii mwingine alikuwa na watu wawili na mwingine ambaye hakuwa hata na mtu mmoja”<sup>1</sup>.**

Kisha Alitaja wingi wa wafuasi wa Musa عليه السلام, kisha kukithiri kwa umma wake Mtume ﷺ, ambao umeenea kutoka Mashariki mpaka Magharibi. Nukta muhimu ni kwamba, hakuna mji hata mmoja baina ya Musa عليه السلام na Yunus عليه السلام katika iliyopita ambao uliomuamini Nabii wao kwa ukamilifu isipokuwa kaumu ya Yunus عليه السلام. Wao ni watu wa Ninawa. Imani yao haikuwa isipokuwa ni kwa kuchelea adhabu ambayo aliwaonya Mtume wao baada ya kuziona dalili zake na Mtume wao akiwa tayari amekwishatoka baina ya maeneo yao. Wakalia kwa Allah تعالى na wakamuomba msaada, wakamnyenyekea na wakawaleta pia watoto wao na mifugo yao. Wakamuomba Allah تعالى Awaondolee adhabu ambayo Nabii wao Aliwaonya kwayo. Allah تعالى Akawarehemu, Akawaondolea adhabu na Akawaakhirishia. Ni sawa na Kauli nyengine ya Allah تعالى:

إِلَّا قَوْمٌ يُونُسَ لَمَّا ءَامَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ ءَعْدَابَ الْخِزْيِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ

حِينٍ ﴿١٠٣﴾

**“Isipokuwa kaumu Yunus? Waliamini na Sisi Tukawaondolea adhabu ya hizaya katika maisha ya dunia, na Tukawastarehesha kwa muda”.**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 10:224.

Katika kuitafsiri Aya hii, Qatadah alisema: Hakuna Mji wowote uliokufuru kisha ukaamini wakati adhabu ilipoanza kuufikia hivyo ukaachwa Kuadhibiwa isipokuwa kaumu ya Yunus عليه السلام. Walipomkosa Nabii wao na wakadhani kwamba adhabu imewasogelea, Allah تعالى Alipeleka utayari wa kufanya toba nyoyoni mwao. Wakavaa nguo za sufu na wakamtenga kila mnyama mbali na mwanaye. Wamkalilia Allah تعالى kwa siku (usiku) arubaini. Allah تعالى Alipoona ukweli katika nyoyo zao, toba na majuto juu ya yaliyopita kwao, Aliwaondolea adhabu baada ya kuwanging'inizia juu yao. Qatadah alisema: "Ilielezwa kwamba kaumu ya Yunus عليه السلام walikuwa wakiishi sehemu za Ninawa, katika ardhi ya Mosul"<sup>1</sup>. Hili lिलielezwa pia na Ibn Mas'ud, Mujahid, Sa'id bin Jubayr na wengineo katika *Sala*<sup>2</sup>.

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَأَمَنَّ مِنَ فِي الْأَرْضِ كُلُّهُمْ جَمِيعًا أَفَأَنْتَ تُكْرِهُ النَّاسَ حَتَّىٰ يَكُونُوا  
 مُؤْمِنِينَ ﴿٩٩﴾ وَمَا كَانَتْ لِنَفْسٍ أَنْ تُؤْمِنَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَجَعَلَ الزَّجْسَ عَلَى  
 الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ﴿١٠٠﴾

**99. "Angelitaka Mola wako Mlezi wangeliamini wote waliomo katika ardhi. Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu mpaka wawe Waumini?"**

**100. "Na hawezi mtu kuamini ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Naye Hujaalia adhabu iwafikie wasiotumia akili zao".**

**Sio Katika Hekima ya Allah تعالى Kuwalazimisha Watu katika Imani.**

Allah تعالى Anasema;

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ

**"Angelitaka Mola wako Mlezi...".**

Ewe Muhammad ﷺ Angeliwapa idhini wakazi wa duniani wote katika kuyaamini uliyowaletea wao. Kisha wote wakaamini. Lakini Allah تعالى Ana Hekima sana katika Ayafanyayo. Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى ;

<sup>1</sup> At-Tabari 15:208.

<sup>2</sup> At-Tabari 15:208 -210.

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً ۗ وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ﴿١١٨﴾ إِلَّا مَنْ رَحِمَ رَبُّكَ ۗ وَلِذَلِكَ خَلَقَهُمْ ۗ وَتَمَّتْ كَلِمَةُ رَبِّكَ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿١١٩﴾

**“Na Mola wako Mlezi Angelipenda Angewafanya watu wote wakawa umma mmoja. Lakini hawaachi kukhitalifiana. Isipokuwa wale ambao Mola wako Mlezi Amewarehemu; na kwa hiyo ndio Mwenyezi Mungu Amewaumba. Na litatimia neno la Mola wako Mlezi: Kweli kweli Nitajaza Jahannam kwa majini na watu pamoja” (11:118-119)**

Na Allah تعالى Amesema,

أَفَلَمْ يَأْيَسِ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ لَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَهْدَىٰ النَّاسَ جَمِيعًا

**“Je. Hawajajua walioamini kwamba lau kuwa Mwenyezi Mungu Angependa bila ya shaka Angeliwaongoa watu wote?” (13:31)**

Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

أَفَأَنْتَ تُكْرَهُ النَّاسَ

**“Je, wewe utawalazimisha watu kwa nguvu”.** Maana yake: Unawashurutisha na kuwakandamiza.

حَتَّىٰ يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ

**“...mpaka wawe Waumini?”** Maana yake: Hilo si juu yako, bali ni la Allah تعالى.

يُضِلُّ مَنْ يَشَاءُ وَيَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

**“...Humuacha akapotea Amtakaye, na Humuongoa Amtakaye.”**

فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسْرَتٍ

**“Basi nafsi yako isijihiliki kwa kuwasikitikia.” (35:8) na,**

لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

**“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye.” (2:272) Na,**

لَعَلَّكَ بِنِعْمَةِ رَبِّكَ أَكْبَرُ ۝۳۰

**"Huenda labda ukajikera nafsi yako kwa kuwa hawawi Waumini."**

(26:3) na,

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ

**"Kwa hakika wewe humuongoi umpendaye." (28:56) na,**

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ۝۳۱

**"...juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu Yetu ni hesabu."**

(13:40) na,

فَذَكِّرْ إِنَّمَا أَنْتَ مُذَكِّرٌ ۝۳۲ لَسْتَ عَلَيْهِمْ بِمُصَيِّرٍ ۝۳۳

**"Basi kumbusha! Hakika wewe ni Mkumbushaji. Wewe si mwenye kuwatawalia." (88:21-22)**

Na Aya nyingine zenye kujulisha kwamba Allah تعالى ni Mwenye Kuyafanya Ayatakayo, Humuongoza Amtakaye, Humuacha apotee Amtakaye. Hayo ni kwa Elimu, Hekima na Uadilifu Wake. Kwa ajili hii, Allah تعالى Alisema;

وَمَا كَانَتْ لِنَفْسٍ أَنْ تُؤْمِنَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ ۚ وَيَجْعَلُ الرِّجْسَ

**"Na hawezi mtu kuamini ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Naye Hujaalia adhabu".**

Nazo ni dhana mbaya na upotevu.

عَلَى الَّذِينَ لَا يَعْقِلُونَ ۝۳۴

**"..kwa wasiotumia akili zao." Maana yake: Hoja na dalili za Allah تعالى. Yeye ni Muadilifu katika yote hayo, katika Kumuongoza Amtakaye na Kumuacha apotee Amtakaye.**

قُلْ أَنْظَرُوا مَاذَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۚ وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَنْ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ

۝۳۵ فَهَلْ يَنْتَظِرُونَ إِلَّا مِثْلَ أَيَّامِ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِهِمْ ۚ قُلْ فَانْتَظِرُوا إِنِّي مَعَكُمْ

مِنَ الْمُنْتَظِرِينَ ۝۳۶ ثُمَّ نُتِجِي رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا ۚ كَذَلِكَ حَقًّا عَلَيْنَا نُنَاجِ

الْمُؤْمِنِينَ ۝۳۷

**101. "Sema: Angalieni yaliyomo mbinguni na kwenye ardhi! Na ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini."**

**102. "Basi, je! Wanangojea jingine ila kama yaliyotokea siku za watu waliopita kabla yao? Ngojeni Nami ni pamoja nanyi katika wanaongoja."**

**103. "Kisha Sisi Huwaokoa Mitume wetu na walioamini. Ndio kama hivyo, inatustahiki kuwaokoa Waumini."**

### **Amri ya Kutafakari Juu ya Kuumbwa kwa Mbingu na Ardhi.**

Allah تعالی Anawaelekeza Waja Wake watafakari katika Alivyoviumba Allah تعالی mbinguni na ardhini, miongoni mwa ishara dhahiri kwa wenye akili. Kati ya hivyo ni nyota zenye kutoa nuru, ziko zilizotulia na zenye kwenda, jua na mwezi, usiku na mchana, na kupishana kwao, kimoja wapo kuingia kwa kingine mpaka kinakuwa kirefu, na wakati huo huo kupungua kingine na kinyume chake. Kunyanyuka kwa mbingu, ukunjufu, uzuri na kupambika kwake. Mvua Aiteremshayo Allah تعالی kutokea huko angani, ikahuisha ardhi baada ya kufa kwake, na Akatoa humo namna mbalimbali za mimea, na wanyama Aliowaweka humo wenye maumbo, rangi na manufaa tofauti tofauti, na milima, tambarare, majangwa, majengo na mahame. Na katika yaliyo baharini, miongoni mwa maajabu, mawimbi, lakini pamoja na hayo imetiishwa kwa wanaosafiri, meli zao zinawachukua na kwenda nao kwa urahisi. Haya yako chini ya usimamizi wa Mwenye uwezo wote, hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye, wala hakuna mola zaidi Yake. Kauli ya Allah تعالی;

وَمَا تُغْنِي الْآيَاتُ وَالنُّذُرُ عَنْ قَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ

**"Na ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasioamini."**

Maana yake: Kitu gani kitakachowafaa makafiri zaidi ya ishara za kimbinguni na ardhini pamoja na Mitume wenye miujiza, hoja, ushahidi wenye kujulisha ukweli wao?

Ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالی:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١١٦﴾

**“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha thibitika juu yao, hawataamini.” (10:96)**

Kauli ya Allah تعالى:

فَهَلْ يَنْتَظِرُونَ إِلَّا مِثْلَ أَيَّامِ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِهِمْ

**“Basi, je! Wanangojea jingine ila kama yaliyotokea siku za watu waliopita kabla yao?”**

Maana yake: Je hao wakadhibishaji wanangoja adhabu na nakama kwa sababu yako, kama vile siku Allah تعالى Alipowaadhibu waliowakadhibisha Mitume katika umma zilizopita kabla yao.

قُلْ فَانْتَظِرُوا إِنِّي مَعَكُمْ مِنَ الْمُنْتَظِرِينَ ﴿١١٧﴾ ثُمَّ نُتَجَّى رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا

**“Ngojeni Nami ni pamoja nanyi katika wanaongoja. Kisha Sisi Huwaokoa Mitume wetu na walioamini...”**

Kwa maana: Naam, Tunawahiliki wanaowakadhibisha Mitume.

كَذَلِكَ حَقًّا عَلَيْنَا نُنَجِّ الْمُؤْمِنِينَ

**“Ndio kama hivyo, inatustahiki Kuwaokoa Waumini.”**

Ni haki Aliyojiwekea Allah تعالى katika Nafsi Yake Tukufu. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

كَتَبَ رَبُّكُمْ عَلَى نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ

**“Mola wenu Mlezi Amejilazimisha Rehema katika Nafsi Yake”. (6:54)**

\* \* \*

قُلْ يَتَّيِبُهَا النَّاسُ إِنْ كُنْتُمْ فِي شَكٍّ مِنْ دِينِي فَلَا أَعْبُدُ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ أَعْبُدُ اللَّهَ الَّذِي يَتَوَفَّنَكُمْ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٤﴾ وَأَنْ أَقِمَّ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٥﴾ وَلَا تَدْعُ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ فَإِنْ فَعَلْتَ فَإِنَّكَ إِذَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٦﴾ وَإِنْ يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ وَإِنْ يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَادَّ لِفَضْلِهِ ۗ يُصِيبُ بِهِ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٠٧﴾ قُلْ يَتَّيِبُهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكُمْ ۗ فَمَنْ آهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيَّ ۗ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِوَكِيلٍ ﴿١٠٨﴾ وَاتَّبِعْ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَأَصْبِرْ حَتَّىٰ يَحْكُمَ اللَّهُ ۗ وَهُوَ خَيْرُ الْحَاكِمِينَ ﴿١٠٩﴾

قُلْ يَتَّيِبُهَا النَّاسُ إِنْ كُنْتُمْ فِي شَكٍّ مِنْ دِينِي فَلَا أَعْبُدُ الَّذِينَ تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ أَعْبُدُ اللَّهَ الَّذِي يَتَوَفَّنَكُمْ ۗ وَأُمِرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٤﴾ وَأَنْ أَقِمَّ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٠٥﴾ وَلَا تَدْعُ مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَ ۗ فَإِنْ فَعَلْتَ فَإِنَّكَ إِذَا مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿١٠٦﴾ وَإِنْ يَمْسَسْكَ اللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُ إِلَّا هُوَ ۗ وَإِنْ يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَادَّ لِفَضْلِهِ ۗ يُصِيبُ بِهِ مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ ﴿١٠٧﴾

104. "Sema: Enyi watu! Ikiwa nyinyi mnayo shaka katika Dini yangu, basi mimi siwaabudu mnao waabudu nyinyi badala ya Mwenyezi Mungu. Lakini mimi namuabudu Mwenyezi Mungu Anayekufisheni. Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waumini".

105. "Na uelekeze uso wako kwenye Dini ya kweli, wala usiwe katika Washirikina".

106. "Na wala usiwaombe wasiokuwa Mwenyezi Mungu ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo, basi utakuwa miongoni mwa walio dhulumu".



**107. “Na Mwenyezi Mungu Akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na Akikutia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila Yake. Huifikisha kwa Amtakaye katika waja Wake, na Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.**

**Amri ya Kumuabudu Allah تعالی Peke Yake na Kutawakali Kwake.**

Allah تعالی Anamuambia Mtume Muhammad ﷺ: “Sema, Enyi watu! Iwapo mtakuwa na mashaka juu ya kusihi kwa niliyokuleteeni, kuhusu Dini *Hanif* (ya kumpwekesha Allah تعالی) ambayo Allah تعالی Amenifunulia, basi siabudu mnavyoviabudu kinyume na Allah تعالی. Lakini ninamuabudu Allah تعالی Peke Yake, Hana mshirika, na Yeye Ndiye Anayekufisheni, sawa na Anavyokuhui - sheni, kisha Kwake Yeye ndio marejeo. Ikiwa miungu yenu mnayoilingania ni ya kweli, basi mimi siabudu, na iombeni inidhuru, kwani haidhuru wala kunufaisha. Mwenye Kumiliki madhara na manufaa ni Allah تعالی Peke Yake, na Hana mshirika.”

وَأْمُرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

**“Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waumini”. (10:104)**

Kauli ya Allah تعالی;

وَأَنْ أَقْرَ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا

**“Na uelekeze uso wako kwenye Dini ya kweli”.**

Maana yake: Fanya ibada kwa ikhlasi, kwa ajili ya Allah تعالی Peke Yake, hali ya kuwa *Hanif*, yaani katika hali ya kujiepusha na ushirikina. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alisema;

وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ الْمُشْرِكِينَ

**“...wala usiwe katika Washirikina”.**

Kauli hii inaunganishwa moja kwa moja na Kauli Yake nyingine;

وَأْمُرْتُ أَنْ أَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

**“Na nimeamrisha niwe miongoni mwa Waumini”.**

Kauli ya Allah تعالی;

وَإِنْ يَمَسَّكَ اللَّهُ بِضُرٍّ

**“Na Mwenyezi Mungu Akikugusisha madhara...”.**

Hapa pana ubainifu, kwani kheri na shari na manufaa na madhara hurejea kwa Allah تعالى Peke Yake, hamshirikishi yeyote katika hayo. Kwa hivyo, Yeye Peke Yake Ndiye Anayestahiki kuabudiwa, Hana mshirika.

Kauli ya Allah تعالى:

وَهُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

**“...na Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu”.**

Maana yake: Kwa anayetubu Kwake, kutokana na dhambi yoyote, hata ya kumshirikisha, Yeye Husamehe.

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكُمْ ۖ فَمَنِ اهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۖ  
وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۖ وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِوَكِيلٍ ﴿١٠٤﴾ وَأَتَّبِعْ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَأَصْبِرْ  
حَتَّىٰ تَخْرُجَ مِنَ اللَّهِ ۚ وَهُوَ خَيْرُ الْخَارِعِينَ ﴿١٠٥﴾

**108. “Sema: Enyi watu! Haki imekwishakukujieni kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Basi anaye ongoka anaongoka kwa faida ya nafsi yake, na anayepotea anapotea kwa khasara ya nafsi yake. Na mimi si mwakilishi juu yenu.”**

**109. “Na wewe fuata yanayofunuliwa kwako kwa wahyi. Na vumilia mpaka Mwenyezi Mungu Ahukumu, na Yeye Ndiye Mbora wa mahakimu.”**

Allah تعالى Anamuamuru Mtume ﷺ awajulisha watu kwamba aliyowaletea kutoka kwa Allah تعالى ni ya kweli na hayana wasiwasi wala shaka. Mwenye kuridhika nayo na akamfuata, basi manufaa ya ufuasi huo yanarejea kwake, na mwenye kupotezwa nayo, hakika si vingine balaa litamrudia mwenyewe.

وَمَا أَنَا عَلَيْكُمْ بِوَكِيلٍ

**“Na mimi si mwakilishi juu yenu.”**

Maana yake: Wala mimi sikufanywa kuwa muwakilishi kwenu mpaka muwe Waumini, bali mimi ni Muonyaji wenu. Hidayah ni juu ya Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى:

وَأَتَّبِعْ مَا يُوحَىٰ إِلَيْكَ وَأَصْبِرْ

**“...na uyafuate unayofunuliwa na usubiri...”**

Maana yake: Shikamana na Aliyoyateremsha Allah تعالى juu yako na Kukufunulia, na usubiri juu ya watu wanaokukhalifu.

حَتَّىٰ تَحْكُمَ ٱللَّهُ

*"...mpaka Allah Ahukumu".*

Maana yake: Apitisha Uamuzi baina yako na wao.

وَهُوَ خَيْرُ ٱلْحَكَمِينَ

*"Naye ni Hakimu M-bora".*

Maana yake: Mbora kati ya wapitishaji hukumu, kwa namna ya Uadilifu na Hekima Yake.

\* \* \*